# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

FEBUARI, 2024.

# YALIYOM0

*UTANGULIZI* ........ *1*

*WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAC* ........ *4*

Waheshimiwa Wajumbe: ........ 4

Sekretarieti: ........ 5

*MGONGANO WA MASLAHI* ........ *5*

*UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI* ........ *6*

*UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022* ........ *7*

4.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA WIZARA YA ELIMU NAMAFUNZO YA AMALI (WEMA) ........ 7

5.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA TUME YA MIPANGOZANZIBAR (ZPC) ........ 28

6.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA ........ 36

9.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR 56

ZIARA YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSIANA NA UFUATILIAJI WA HOJA NAMBARI 9.4.1.1 JIJINI DAR ES SALAAM ........ 78

*UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA TAWALA ZA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022* ........ *84*

6.0 TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ ........ 84

6.1 TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) ........ 84

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - PEMBA ........ 106

6.1.2 FUNGU D02: JESHI LA KUJENGA UCHUMI ........ 115

SKULI YA MTONI YA JESHI LA KUJENGA UCHUMI ........ 120

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) PEMBA ........ 124

*UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022 ... 131*

4.0 UKAGUZI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA FEDHA ZA MKOPO WA AHUENI YA UVIKO-19 ZANZIBAR ... 131

4.3 MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA YA AFYA ... 131

4.5 MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI 154

6.0 MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA KWA FEDHA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR NA WAHISANI WA MAENDELEO - PEMBA ... 174

6.3 MIRADI YA UJENZI WA MADARASA NA MASOKO MKOA WA KASKAZINI PEMBA ... 174

6.6 MRADI WA UJENZI WA TUTA LA KUZUIA MAJI CHUMVI KATIKA BONDE LA TOVUNI KIUNGONI UNAOTEKELEZWA NA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO - PEMBA ... 195

*UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022 ... 208*

4.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 208

4.1 UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA ... 208

4.1.3 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC) ... 208

SHIRIKA LA BANDARI - PEMBA ... 220

ZIARA YA MAFUNZO YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KATIKA MAMLAKA YA BANDARI TANZANIA (TPA) ... 227

4.1.4 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC) ... 230

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)- PEMBA ... 247

ZIARA YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KATIKA NYUMBA NA DUKA LA SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) - JIJINI DAR ES SALAAM 252

5.0 MAMLAKA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR ... 255

5.1.4 MAMLAKA YA MAJI (ZAWA) - UNGUJA ... 255

MAMLAKA YA ZAWA PEMBA ... 276

5.1.6 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA - ZANZIBAR ... 282

MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA - PEMBA ... 296

5.1.9 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI 300

MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI - PEMBA. 308

6.0 UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR 311

6.1.4 WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO ZANZIBAR 311

WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO - PEMBA 320

6.1.6: WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR (ZBA) 328

WAKALA WA MAJENGO - PEMBA 359

7.0 UKAGUZI WA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR 366

7.1.2 MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA) 366

ZIARA YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KATIKA KITUO CHA TAIFA CHA KUHIFADHIA TAARIFA CHA SERIKALI (NATIONAL INTERNET DATA CENTRE) NA IDARA YA UKAGUZI NA UPELELEZI WA WALIPAKODI - JIJINI DAR ES SALAAM 437

*UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA SERIKALI KUU KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022 441*

7.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 441

7.2 WIZARA YA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI 441

7.2.4 TUME YA UKIMWI 441

TUME YA UKIMWI - PEMBA 449

7.4 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO 459

7.4.4 AFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR 459

*HITIMISHO 486*

RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI
HESABU ZA SERIKALI (PAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI - ZANZIBAR,
KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## UTANGULIZI

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ni Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia masuala ya fedha ambayo imeundwa chini ya Kanuni ya 107(1) ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 na kuainishwa majukumu yake katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hiyo ambapo pamoja na mambo mengine inajukumu kuu la kufuatilia na kuchunguza Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara tu baada ya kuwasilishwa kwa Ripoti hizo kwa Mheshimiwa Spika. Kiujumla, Kamati hufuatilia Ripoti hiyo kwa niaba ya Baraza na hatimae kuwasilisha Ripoti yake hususan katika mwezi wa Febuari au muda mwengine wowote ambao Kamati ya Uongozi ya Baraza itaamua kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 109(15) ya Baraza.

Ikumbukwe kwamba, tarehe 11 Mei 2023, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman aliwasilisha Vitabu Sita vya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali vya ukaguzi unaoishia tarehe 30 Juni, 2022 mbele ya Baraza la Tisa la Wawakililshi ambavyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliviwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 03 Mei 2023 Ikulu Zanzibar.

Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Baraza, Kamati ya PAC imefanikiwa kuvifanyia uchunguzi vitabu vitano vya Ripoti za Mdhibiti ambazo ni:-

1. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHEMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022 iliyojumuisha Ripoti zifuatazo:-
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Tume ya Mipango Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022; na
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni,

2022.

2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022.

    - Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU)

3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022 iliyojumuisha Ripoti zifuatazo:-

    - Ripoti ya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Fedha za Mfuko wa Ahueni ya UVIKO - 19 Zanzibar katika Sekta ya Afya kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Fedha za Mfuko wa Ahueni ya UVIKO - 19 Zanzibar katika Sekta ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Madarasa na Masoko - Mkoa wa Kaskazini Pemba katika Sekta ya Elimu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kuhusu Ujenzi wa wa Vyumba vya Kusomea kwa Chuo cha Kiislamu Micheweni Pemba kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022; na
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo wa Tuta la Kuzuia Maji Chumvi katika Bonde la Tovuni - Kiungoni kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022.

4. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022 iliyojumuisha Ripoti zifuatazo:-

- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma kwa Shirika la Bandari kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma kwa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mamlaka ya ZAWA kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Wakala za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022;
- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Wakala za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Wakala wa Majengo Zanzibar kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022; na
- Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kwa kipindi cha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022.

5. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022.
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa Tume ya Ukimwi kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022; na
    - Ripoti ya Ukaguzi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022.

## WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAC

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati hii imeundwa na Wajumbe Wanane (8) wafuatao:-

### Waheshimiwa Wajumbe:

| Na. | Jina Kamili | | Cheo/Wadhifa |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma Ali Khatib | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | - | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Jamal Kassim Ali | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraj Khamis Mussa | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Shadya Mohammed Suleiman | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Kombo Mwinyi Shehe | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Mjumbe |

Aidha, Katika kutekeleza masharti ya Kanuni za Baraza, Wajumbe hao walisaidiana na Sekretarieti iliyoundwa na Maafisa Wanne (4) ambao ni Makatibu wa Kamati na Maofisa Tisa (9) kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sekritariet yenyewe ni:-

### Sekretarieti:

| Na. | Jina Kamili | | Cheo/Wadhifa |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Maryam Haji Ali | - | Katibu wa Kamati |
| 2. | Ndg. Said Khamis Ramadhan | - | Katibu wa Kamati |
| 3. | Ndg. Fatma Omar Ali | | Katibu wa Kamati |
| 4. | Ndg. Adam Maulid Simai | - | Katibu wa Kamati |
| 5. | Ndg. Robert Laurian Mweiro | - | Mkurugenzi TEHAMA-Ofisi ya Mdhibiti |
| 6. | Ndg. Ramadhan Iddi Hassan | - | Mkurugenzi wa Ukaguzi-Ofisi ya Mdhibiti |
| 7. | Ndg. Nassor Mdachi Mwinyi | - | Mkaguzi-Ofisi ya Mdhibiti (Unguja) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | Ndg. Juma Mohammed Juma | - | Mkaguzi-Ofisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 9. | Ndg. Mussa Kadir Mussa | - | Mkaguzi-Ofisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 10. | Ndg. Shehe Abdallah Ali | - | Mkaguzi- fisi ya Mdhibiti |
| 11. | Ndg. Maryam Ali Khamis | - | Mkaguzi-Ofisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 12. | Ndg. Mariyam Alhaji Juma | - | Mkaguzi-Ofisi ya Mdhibiti |
| 13. | Ndg. Moh'd Suleiman Amour | - | Mkaguzi-Ofisi ya Mdhibiti (Pemba |

## MGONGANO WA MASLAHI

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya PAC ilifuata matakwa ya Kanuni na Sheria za nchi zilizoelekeza uwekaji wazi Mgongano wa Maslahi kwa Wajumbe dhidi ya jambo linalojadiliwa ili kuepusha kujitokeza kwa upendeleo hususan wakati wa kufanya maamuzi na kusababisha uonevu au ubatilishaji wa haki. Kwa bahati nzuri, Katika majadiliano ambayo Kamati imeyafanya, hakujajitokeza aina yoyote ya mgongano wa maslahi kwa Wajumbe dhidi ya maamuzi waliyoyatoa.

## UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Kamati ya PAC imezingatia matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020). Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo hutumika kuwa ni Hadudi Rejea pamoja na Sheria ya Kinga, Uwezo na Fursa za Wajumbe, Nambari 6 ya 2022.

Kadhalika, Kamati kwa mara kadhaa ilikuwa ikifanya rejea ya Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nambari 11 ya mwaka 2016, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nambari 12 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria nyengine za Zanzibar.

Sambamba na hilo, Kamati ilikutana na Watendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali zilizohusika na hoja zilizoibuliwa katika Ripoti ya Mdhibiti kwa kufanya mahojiano, kupitia vielelezo na hatimae kufanya ziara katika maeneo mbali mbali ili kuthibitisha uhalisia wa majibu yaliyotolewa na Wizara au Taasisi husika.

Kwa kipindi hiki cha ukaguzi, kazi za Kamati zilitekelezwa ndani ya mizunguko mitatu ifuatayo:-

1. **Mzunguko wa Kwanza:** Ulianzia tarehe 07/08/2023 hadi 18/08/2023 - Unguja na kumalizia tarehe 28/08/2023 hadi 01/09/2023 - Pemba.
2. **Mzunguko wa Pili:** Ulianzia tarehe 30/11/2023 hadi 03/11/2023 - Pemba na

kumalizia tarehe 06/11/2023 hadi 17/11/2023.

3. **Mzunguko wa Tatu:** Ulianzia tarehe 15/01/2024 hadi tarehe 19/01/2024 - Pemba na kumalizia tarehe 22/01/2024 hadi tarehe 02/02/2024 – Unguja

# UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022

## 4.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI (WEMA)

### Hoja nambari 4.8.1.1: Udhaifu katika udhibiti wa akaunti za watumiaji wa Mifumo

Viwango bora kubalifu vya TEHAMA kwenye usimamizi wa akaunti za watumiaji wa mifumo vinaelekeza kufanyika kwa mapitio ya mara kwa mara kwenye akauntiza watumiaji wa mifumo (Periodic Access Reviews) ili kuhakikisha kwamba watumiaji wa mifumo wanaruhusa ya kufikia maeneo yale wanayotakiwa kufikiapekee na sio vinginevyo. Aidha, mapitio ya akaunti hizi pia husaidia kubaini watumiaji ambao sio hai na wale wasio fanya kazi na taasisi husika tena kwa sababu mbali mbali na kuwaondolea ufikiaji wa mifumo husika.

Ukaguzi umebaini kwamba akaunti za watumiaji wa mifumo ya Wizara ya Elimu hazifanyiwi mapitio ya mara kwa mara jambo ambalo limepelekea uwepo wa baadhi ya akaunti za watumiaji ambao walishahama Wizara lakini kuendelea kuwa hai kwenye mifumo mbali mbali. Akaunti hizi zinaweza kuwa chanzo cha kudukuliwa na kutumiwa vibaya kwa mifumo husika. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa akaunti zenye majina ya jumla kama vile "Administrator" ambazo zinatumika kwa namna mbali mbali kwenye mifumo ya Wizara.

Kutumia akaunti zisizo na utambulisho wa moja kwa moja ni hatari (risk) hususani inapotokea akaunti hizi kutumika vibaya kama vile kwenye ubadhirifu/wizi au kuharibu taarifa za Serikali vyombo vinavyohusika na kutoa haki hutumia muda mrefu kufanya hivyo kwani ushahidi huwa hauko wazi kwa watuhumiwa hali inayochelewesha utendaji haki na utatuzi wa kesi husika.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaandaa Sera za TEHAMA zinazojumuisha usimamizi sahihi wa akaunti za watumiaji wa mifumo yote ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya mara kwa mara ili

kubaini usahihi wa haki za ufikiaji wa mifumo husika na kuchukuwa hatua stahiki.

Aidha, Sera hizo ziweke utaratibu maalumu wa kufanya mawasiliano baina ya Idara ya Rasilimali Watu na Idara ya TEHAMA kuhusiana na mabadiliko mbali mbali kwa wafanyakazi kama vile kustaafu, kuhama Taasisi/Idara, kwenda likizo, kubadilishiwa majukumu, n.k ili kuyafanyia kazi mabadiliko hayo mara moja kwenye mifumo kulingana na hali halisi ya wakati husika.

Pia, Wizara inashauriwa kuweka usimamizi wa mifumo na watumiaji wa mifumoyote ya TEHAMA chini ya Idara ya TEHAMA ili kufanya kazi za usimamizi na uendeshaji wa mifumo kwa kuzingatia matakwa ya viwango bora kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA kama ilivyoelezewa hapo juu.

Kwa upande wa akaunti zenye majina ya ujumla ukaguzi unashauri akaunti hizozisitishwe ufikiaji wa mifumo mara moja na wahusika wapewe akaunti zenye majina yao halisi na zenye uwezo wa kufanya majukumu yao kwenye mifumo kwa mujibu wa kazi zao.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Wizara iko katika mchakato wa ukamilishaji wa sera ya TEHAMA pamoja na miongozo mengine yenye lengo la kuelekeza utumiaji wa mifumo ya TEHAMA na udhibiti wake.

Pia, usimamizi wa mifumo yote ya TEHAMA na watumiaji umewekwa chini ya Idara ya TEHAMA.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa bado Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haijakamilisha sera ya TEHAMA ambayo itakuja kuwa suluhisho la uwepo wa viwango vya udhibiti wa akaunti za watumiaji wa Mifumo kwa vile Wizara bado imo katika mchakato ambao haujulikani utakamilika muda gani. Kwa msingi huo, Kamati haijaridhika na majibu ya uongozi wa Wizara na inamtaka Mkaguzi kuendelea kuifuatilia kwa karibu hoja hii ili iweze kutekelezwa.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao ihakikishe inaandaa sera ya TEHAMA ili iweze kuondoa changamoto za matumizi na watumiaji wa mifumo.

## Hoja nambari 4.8.1.2: Udhaifu wa mfumo wa Zanzibar Advance Student Allocation System (ZASAS) kwenye kusajili wanafunzi waliorudia mtihani wa kidato cha nne

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa Zanzibar Advance School Allocation System(ZASAS) hauna uwezo wa kusajili wanafunzi walio "re-seat" mitihani ya kidato cha nne na badala yake wanafunzi hao hupangiwa kuendelea na kidatu cha tano kwa njia ya kawaida (manually). Hali hii inaashiria kushindwa kutambua mahitaji kamili ya watumiaji wa mfumo kwani wanafunzi kurudia mitihani ya kidatu cha nne ni sehemu ya mchakato (business process) wa kusoma na hivyobasi ilitarajiwa kuwa sehemu ya mfumo husika.

Uhafifu wa tija na kupunguza ufanisi ni miongoni mwa athari za udhaifu uliobainika kwenye mfumo huo, aidha, matumizi endelevu ya mfumo huo yako mashakani ikiwa changamoto hii haitafanyiwa kazi kwa wakati.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Elimu kufanya tathmini ya udhaifu wa mfumo huo haraka iwezekanavyo na kuchukua hatua za kuutatua kwa kuwashirikisha watumiaji wote kwa upande wa Unguja na Pemba.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Mfumo wa ZASAS umeboreshwa kwa kuondosha mapungufu yaliyoonekana katika usajili wa wanafunzi wa kidato cha nne ambao wanarudia mitihani.

Kwa sasa mfumo unasajili wanafunzi wote wa kidato cha nne wanaostahiki.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa wanafunzi wote ambao wanarudia mitihani kwa sasa wanasajiliwa kwenye mfumo. Katika kulithibitisha hilo, Kamati iliomba ipatiwe ripoti ambayo inaonesha wanafunzi ambao wana "reseat" wamesajiliwa vizuri, na kujiridhisha utendaji kazi wa mfumo huo.

Halkadhalika, Kamati imebaini kwamba Wizara imekiuka miongozo ambayo ipo e-Gaz inayotaka marekebisho yoyote ya mfumo bila kujali ukubwa wake lazima yapate kibali kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao ambapo Wizara iliamua kufanya marekebisho ya mfumo wao bila ya kupata ruhusa kutoka kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati inaushauri uongozi wa Wizara wakiamua kufanya marekebisho katika mifumo

yao ya TEHAMA ipeleke maombi Mamlaka ya Serikali Mtandao ili kuwapa taarifa na kupata approval kutoka kwao

## Hoja nambari 4.8.1.3: Udhaifu uliopo kwenye Vituo vya Sayansi na Ubunifu (HUBs)

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilitengeneza Vituo vya Sayansi na Ubunifu kwa ajili ya kujifunzia lugha, TEHAMA na Sayansi kupitia mradi wa Zanzibar Improvement Students Prospects (ZISP) ambapo kwa upande wa Pemba Vituo hivi vipo 9 wakati Unguja ikiwa na Vituo 13,"HUBs" ya lugha na ile ya TEHAMA zimefungiwa Kompyuta kwa ajili ya wanafunzikujifunzia.

Ukaguzi ulibaini kwamba Kompyuta zilizowekwa kwenye vituo hivyo ziliwekewa programu za majaribio na Mzabuni kinyume na matakwa ya Mkataba wa kutoa huduma hiyo uliomtaka kuweka programu halisi zilizolipiwa leseni. Hali hii inaweza kuisababishia Serikali hasara kwani fedha hizo tayari zilishalipwa kwa mzabuni aliyepewa zabuni husika.

Aidha, "HUBs" nyingi zinakabiliwa na changamoto mbali mbali kama vile Wataalamu wa TEHAMA, Lugha na Sayansi. Pia, "HUBs" zinakabiliwa na changamoto ya mtandao (Internet) hali inayokwamisha matumizi yenye kuleta tija na kuongeza ufanisi kwa wanafunzi katika kujifunza TEHAMA, Lugha na Sayansi maarifa yanayopatikana kwenye mifumo kama vile ZLMS/ mtandao (online) unaoweza kufikiwa na wanafunzi ikiwa kuna huduma ya mtandao (Internet services).

Uwepo wa Kompyuta zisizo na "Internet" kwenye "HUBs" unarudisha nyuma manufaa yaliyotarajiwa kupatikana kwa uwepo wa mifumo mbali mbali ya kujifunzia na kusoma mtandaoni kwa wanafunzi kama vile ZLMS. Aidha, kukosekana kwa wataalamu wa kufundisha masomo mbali mbali kunaikwamishanchi katika kunufaika na uwepo wa "HUBs" hizo.

Wizara inashauriwa kutafuta ufumbuzi wa changamoto na udhaifu uliobainika haraka iwezekanvyo kwani mpaka sasa ni zaidi ya miaka 2 tangu "HUBs" hizo zikamilike lakini bado haijaleta tija inayotarajiwa.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Wizara imepanga kuziunganisha HUBs zote na mkonga wa taifa wa mawasiliano kupitia mradi wa ZIQUE ambao utaimarisha matumizi ya TEHAMA kwa walimu na wanafunzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa bado Watendaji wa Wizara hawajafanikiwa kuunganisha mfumo wao na Mkonga wa Taifa. Lakushangaza zaidi kamati imegundua kuwa Wizara inatumia kompyuta zilizowekwa program za majaribio badala ya program halisi za kutumia wanafunzi na walimu ambazo zinapatiwa leseni ya matumizi. Aidha, vituo vya sayansi na ubunifu (Hubs) hazina mtandao (internet) jambo ambalo linapelekea kutofikia lengo la matumizi yake.

Kwa vile Wizara bado haijakamilisha uondoshaji wa kasoro ambazo Mkaguzi amezibaini. Kamati ya PAC haijaridhika na majibu ya uongozi wa Wizara na hoja hii inabakia ili kwa hatua za utekelezaji na uondoshaji wa kasoro zilizoibuliwa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati inaishauri Wizara kutafuta wataalamu wabobezi ili vituo vya sayansi na ubunifu zifanye kazi na kuleta matokeo chanya kwa Walimu na Wanafunzi wetu.
2. Wizara itafute ufumbuzi wa changamoto na udhaifu uliobainika na Mkaguzi haraka iwezekanvyo kwani mpaka sasa ni zaidi ya miaka 2 tangu “HUBs” hizo zikamilike lakini bado hazijaleta tija inayotarajiwa.

## Hoja nambari 4.8.1.4: Ukosefu wa maudhui kwenye mfumo wa Zanzibar LearningManagement System (ZLMS)

Ukaguzi umebaini ya kwamba mfumo wa ZLMS uliotengenezwa kwa lengo la kuweka maudhui ili wanafunzi kuanzia Skuli za Awali mpaka Sekondari kuweza kujisomea na kuleta tija kwenye elimu, hata hivyo mfumo huo umebainika kuwa hauna sehemu kubwa ya maudhui yaliyotarajiwa kuwemo jambo ambalo limewanyima wanafunzi fursa ya kujisomea kwa kutumia mfumo huo na kupelekea mfumo husika kushindwa kufikia lengo la utengenezwaji wake na kukosa tija katika uwekezaji uliofanyika.

Aidha, hali hii ya matumizi madogo ya mfumo huo yamechangiwa na kutokushirikishwa kikamilifu watumiaji wa mfumo huu, yaani watengeneza maudhui na wanafunzi kwani mpaka sasa mfumo huu umetimiza miaka zaidi ya2 lakini bado hauna zaidi ya asilimia 90 za maudhui yaliyotakiwa kuwemo.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Elimu kusimamia na kufuatilia kwa karibu taasisi iliyopewa jukumu la kuandaa na kuweka maudhui kwenye mfumo kwa ajili ya wanafunzi kujisomea ili itimize wajibu wake kwa haraka iwezekanavyo kwa kuzingatia miongozo mbali mbali ya Elimu iliyopo.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Taasisi ya Elimu Zanzibar inaendelea na taratibu wa kukusanya maudhui katika njia ya “Soft copy” kwa vitabu vya kiada na vitabu vya ziada na kuviingiza katika kwa ajili ya matumizi ya walimu na wanafunzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa mfumo wa Zanzibar Learning Management System (ZLMS) umewekwa zaidi ya miaka miwili ambapo bado Wizara inaendelea na mchakato wa kukusanya maudhui katika njia ya nakala laini (Soft copy). Hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake maudhui hayo hayajawekwa.

Kamati pia imegundua kuwa “speed” ya Wizara ni ndogo katika kuweka maudhui ya kujifunza katika mfumo licha ya juhudi wanazozichukua katika kuukamilisha mfumo huu.

Kwa vile Wizara haijakamilisha utekelezaji wa hoja hii, Kamati imeamua kuibakisha hadi Mkaguzi atakapokuja kujiridhisha.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali uhakikishe unakamilisha hatua zilizosalia za kuingizwa taarifa za nakala laini katika mfumo Zanzibar Learning Management System (ZLMS).

## Hoja nambari 4.8.1.5: Udhaifu wa usimamizi wa Vishkwambi “Tablet PC” walivyopewa walimu wakuu kwenye Skuli za msingi na Sekondari kukusanyia takwimu

Ukaguzi ulibaini kwamba Wizara ya Elimu ilinunua Vishkwambi 210 vya aina ya Touchmate na kuvigawa kwenye Skuli mbali mbali nchini kwa lengo la kukusanyatakwimu za elimu. Hata hivyo, imebainika kwamba baadhi ya Vishkwambi hivyo viligawiwa bila kufanyiwa usajili na vile vilivyofanyiwa usajili havijawahi kuhuishwataarifa zake kwa muda mrefu na kupelekea taarifa zilizopo kama vile majina ya watumiaji/msimamizi, nambari ya simu, na mahali alipo, kwa kuwa kuna walimuwengi ambao walishahama kutoka Skuli moja kwenda nyengine na wengine kustaafu kazi lakini daftari la taarifa “register” la Wizara kuendelea kuwatambuakama watumiaji/wasimamizi wa Vishkwambi vilivyo vingi kinyume na uhalisia.

Hali hii imesababishwa na uwepo wa udhaifu katika usimamizi wa Idara ya TEHAMA kwenye vifaa na mifumo iliyopo Wizarani ambapo ilibainika kwamba baadhi ya Idara

zisizo za TEHAMA zinafanya majukumu ya Idara ya TEHAMA kama ilivyofanyika kwenye ununuzi na usimamizi wa Vishkwambi hivo ulio kuwa ukifanywa na Idara ya Sera, Mipango na Takwimu huku watumishi wa Idara hio kukosa maarifa na weledi wa uhitaji wa namna sahihi ya usimamizi wa vifaa husika vya TEHAMA. Athari nyengine ni pamoja na uwezekano wa kupotea na kuharibika, kutofanyiwa matengenezo stahiki kwa wakati kwa vifaa hivyo.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Elimu kutatua changamoto ya udhibiti na usimamiziwa vifaa vya TEHAMA Wizarani kwa kuviweka chini ya Idara ya TEHAMA na kuunda daftari la kusajili rasilimali za TEHAMA (ICT Asset Register) ambalo lingefaa zaidi kama likiwa la kielektroniki na kuvisajili vifaa vyote na kuendelea kufanya uboreshaji wa taarifa hizo mara kwa mara ili ziendane na hali halisi.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Udhibiti na Usimamizi wa Vifaa vya TEHAMA umewekwa chini ya Idara ya TEHAMA kwa vifaa kusajiliwa katika daftari la kusajili rasilimali za TEHAMA (ICT Asset Register) na Idara ipo katika mpango wa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa uwekaji wa kumbukumbu wa vifaa vyote vya TEHAMA.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya juhudi ambazo uongozi wa Wizara umezichukua za kuanzisha Idara ya TEHAMA. Hata hivyo, Kamati imegundua mfumo wa kielektroniki bado haujaanzishwa na kupelekea vifaa hivyo (tablets) kutokusajili katika daftari la kusajili rasilimali za TEHAMA.

Aidha, Kamati imebaini kuwa vifaa vilivyogaiwa (tablets) kwa baadhi ya Walimu kutojulikana wamiliki wake na kushindwa kurejeshwa katika Wizara. Kwa mnasaba huo, Kamati imeamua kuibakisha hoja hii ili Mkaguzi aweze kuifuatilia na kukamilishwa utekelezaji wake.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inaushauri uongozi wa Wizara ya Elimu kuvitafuta na kuwatambua wahusika wote waliokabidhiwa vifaa hivyo na kuviweka katika udhibiti wa Wizara.
2. Uongozi wa Wizara uhakikishe unaandaa mfumo utakaohakikisha kunakuwa na udhibiti na usalama wa kutosha wa vifaa vya Wizara chini ya usimamizi wa Idara ya TEHAMA.

## Hoja nambari 4.8.1.6: Udhaifu wa ulinzi na Kutumika kwa programu za burekwenye vifaa vya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kuwa Kompyuta nyingi za Wizara zimewekewa Programu za bure ambazo sio rasmi kama vile programu za kuzuia virusi (anti-viruses) na programu za “Microsoft Office”.

Aidha, kwa upande wa ulinzi wa vifaa vya TEHAMA ukaguzi ulibaini kwamba vifaa vingi vya Wizara Unguja na Pemba havina ulinzi dhidi ya athari za umeme (UPS) hali ambayo inaweza kupelekea kujitokeza kwa uharibifu mkubwa kwa vifaa vya TEHAMA vyenye thamani kubwa na kusababisha hasara kwa Serikali.

Kuhatarisha usalama wa taarifa za taasisi kwa kutumia Programu za bure zenye udhaifu wa kiusalama na zinazoweza kuwa na madhara na kuleta athari kwenye mifumo ikiwa ni pamoja na kuvujisha au kuharibu taarifa.

Aidha, hali hii inaashiria uwepo wa udhaifu katika usimamizi na ufuatiliaji wa Idara ya TEHAMA katika vitendea kazi vya Afisi kwa ujumla.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara kutatua changamoto hizi mara moja kwani zinahatarisha usalama wa vifaa vya TEHAMA na taarifa zilizomo kwenye vifaa husika.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Wizara imechukuwa hatua ya kutumia “specifications’ kutoka Idara ya TEHAMA kwa ununuzi wa vifaa vyote vya Wizara vinavyohusiana na teknolojia ya habari na mawasiliano, pamoja na ukaguzi wa vifaa husika baada ya ununuzi.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya kiukaguzi, kasoro hizo zilikuwepo. Hata hivyo, bado Wizara haijakamilisha hatua za uwekaji wa ulinzi dhidi ya athari za umeme (UPS) pamoja uwekaji wa programu halisi za ‘computer’. Hali hiyo inaweza kupelekea kujitokeza kwa uharibifu mkubwa kwa vifaa vya TEHAMA vyenye thamani kubwa na kusababisha hasara kwa Serikali.

Kwa msingi huo, Kamati ya PAC haiukuridhika na majibu ya hoja hii na kuibakisha kwa hatua za utekelezaji

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Wizara uhakikishe unaweka ulinzi na kutumia programu halisi (Original

Computers Program) ambazo zitatumika kihifadhi vifaa vya Wizara vilivyonunuliwa kwa gharama kubwa.

## Hoja nambari 4.8.1.7: Kukosekana kwa usimamizi imara wa mifumo, miundombinu na rasilimali nyengine za TEHAMA

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina changamoto ya usimamizi wa mifumo, miundombinu na rasilimali nyengine za TEHAMA, ambapo ilibainika kwamba kuna baadhi ya kazi za TEHAMA zinatekelezwa na Idara au Vitengo visivyo vya TEHAMA na kuleta mgongano ndani ya Wizara hususani pale ambapo kuna mapungufu kwenye usimamizi na utawala wa kazi hizo, kama vile ununuzi wa vifaa visivyokidhi vigezo stahiki vya TEHAMA.

Aidha, imebainika uwepo wa ufadhili kupitia Wahisani wa Maendeleo kwenye Miradi ya **Tusome Pamoja na ZISP** ulionunua vifaa na kutengeneza mifumo ya TEHAMA ambayo iliratibiwa na kusimamiwa na Idara ya Mipango Sera kitengo chaTakwimu nje ya utaratibu rasmi ambao ulitakiwa kufanywa na Idara ya TEHAMA yenye wataalamu na weledi wa masuala yote ya TEHAMA.

Katika mradi huu vilinunuliwa Vishkwambi takribani 210 vya aina ya Touchmate vyenye thamani ya shilingi 126,600,000 ambavyo vilikuwa na viwango vya chini(low specifications) ukilinganisha na mahitaji halisi yaliyopo. Hali hii imepelekeavifaa hivyo kushindwa kukidhi haja ya matumizi kwani ndani ya kipindi cha mudamfupi vilishindwa kufanya kazi na vingi kuharibika hali inayopelekea Serikali kutakiwa kufanya uwekezaji mwingine kwenye eneo hilo na kukosa tija kwenye matumizi ya fedha za Umma.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuzingatia muundo waTEHAMA uliopo na kuhakikisha kwamba kazi zote zinazohusiana na TEHAMAbila kujali Idara au Kitengo kinachonufaika zitekelezwe na Idara ya TEHAMA na kwamba watumishi wa Wizara walioajiriwa kama wataalamu wa TEHAMA kwenye maeneo mbali mbali watekeleze majukumu yao chini ya Idara ya TEHAMA ili kutengeneza utaratibu mzuri wa uwajibikaji kwenye utekelezaji wa majukumu yaTEHAMA ndani ya Wizara.

Aidha, miradi yote ya TEHAMA ikijumuisha vifaa, mifumo na Teknolojia mbali mbali iliyoko chini ya usimamizi na uendeshaji wa Idara au Vitengo vyengine ihamishiwe na kukabidhiwa kwenye Idara ya TEHAMA kwenye masuala ya utawala(system administration - Technical) wakati kwenye masuala ya usimamizi (system management - application) yawekwe chini ya Idara/Kitengo kinachonufaika.

Kwa upande wa ununuzi/utengenezaji wa vifaa, mifumo na Teknolojia ya TEHAMA ukaguzi unashauri Sheria, Kanuni na Miongozo ya manunuzi ya Ummakuzingatiwa wakati

Idara ya TEHAMA ikishiriki ipasavyo kwenye kutengeneza vigezo (specifications) zitakazotokana na mapitio ya mahitaji kutoka kwa watumiaji. Aidha, wakati wa kupokelewa kwa vitu hivyo Idara ya TEHAMA ndiyo yenye dhamana ya kuhakikisha kwamba vipimo vilivyotolewa vimezingatiwa na mtoa Huduma.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imezingatia muundo wa Idara ya TEHAMA kwa kazi zote za TEHAMA kuelekezwa katika Idara husika.

Idara ya TEHAMA inashiriki katika utayarishaji wa specifications pamoja na kuwa na dhamana ya kuhakikisha kuwa vigezo (specifications) zilizotolewa zimezingatiwa na mtoa huduma.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati imebaini kuwa ni kweli vifaa vilinunuliwa bila ya kuwepo kwa 'specifications' zinazoendana na mahitaji halisi ya matumizi ya Wizara. Hali hiyo ilitokana na kutokushirikisha ipasavyo Kitengo cha TEHAMA ambacho ndio chenye utaalamu wa kutambua 'specifications' bora kulingana na matumizi husika.

Hata hivyo, kwasasa Wizara imeshaandaa Idara ya TEHAMA na inawashirikisha ipasavyo katika uandaaji wa 'specifications' za ununuzi wa vifaa vya Wizara.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unawashirikiasha ipasavyo katika kila manunuzi ya vifaa vya TEHAMA wataalamu kutoka Idara ya TEHAMA ili kupatikane vifaabora vitakavyotumika kwa muda mrefu.

## Hoja nambari 4.8.1.8: Uhaba wa Seva kwa ajili ya kuweka mifumo pamoja na kuhifadhi nakala za mifumo hiyo

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara haina Seva za kutosha kwa ajili ya kuweka mifumo mbali mbali inayotengenezwa/kununuliwa na Wizara hali iliyopelekea Wizara kufanya uamuzi wa kuweka mifumo hiyo kwenye Seva za kukodi zilizoko nje ya mipaka ya Zanzibar kinyume na miongozo ya Serikali kwenye uhifadhi wataarifa za Serikali.

Mifumo kama vile Zanzibar Learning Management System umewekwa kwenye Seva za Blue Host zilizoko kwenye "cloud" kwa gharama za dola za Kimarekanikumi na nane ($18) kila mwezi wakati mfumo wa Zanzibar Education AssesmentSystem (ZEAS) umewekwa

kwenye Seva za Just Host zilizoko kwenye “cloud” kwa gharama ya dola za Kimarekani Thelathini na Nne (USD. 34) kila mwezi.

Aidha, uhaba huu wa Seva umesababisha Wizara kukosa Seva kwa ajili ya kuhifadhia nakala (backups) za mifumo yake yote kinyume na matakwa ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA vinavyoelekeza kwamba taasisi inapaswa kuwa na angalau Seva mbili zenye uwezo stahiki ambapo moja kwa ajili ya kazi za kila siku (Primary Server) na nyengine kwa ajili ya kuhifadhia nakala za taarifaza mifumo.

Hali hii imechangia udhaifu wa Wizara kwenye kuchukua na kuhifadhi nakala za mifumo iliyopo jambo ambalo ni hatari kubwa kwakuwa ikitokea matatizo yatakayopelekea kupoteza taarifa zilizomo kwenye Seva ya Msingi (Primary Server) Wizara itakuwa imepoteza taarifa hizo moja kwa moja na haitaweza kuzirejesha. Hii itarejesha nyuma jitihada za Serikali kuifanya TEHAMA kusaidia kuleta tija na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma Serikalini.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutatua changamoto hii kwa uharaka unaostahili kwa kupeleka maombi rasmi ZICTIA ili kupatiwa nafasi kulingana na mahitaji ya Wizara kwa lengo la kuepusha kufanyika kwa matumizi mabaya ya taarifa za Serikali pamoja na kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipia gharama za kuweka mifumo kwenye Seva za kukodi ambazo hazipo nchinikinyume na miongozo ya Serikali.

Aidha, ikiwa ZICTIA kwa sababu moja au nyengine haina nafasi za kutosha Wizara itenge bajeti itakayoiwezesha kufanya manunuzi ya Seva husika ili kutatua changamoto hii na kuepusha hatari ya kupoteza taarifa kwa kukosa nakala.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Wizara imechukuwa juhudi ya kupeleka maombi ZICTIA kwa ajli ya kupatiwa nafasi ya kuweka mifumo yake katika seva za ZICTIA.

Pia, Wizara imepanga kununua seva 4 kupitia Mradi wa ZIQUE baada ya kupata ruhusa kutoka Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (EGAZ) juu ya vigezo vya seva zinazohitajika na Wizara.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa Wizara imechukua juhudi ya kufanya mawasiliano na Mamlaka ya Serikali Mtandao (ZICTIA) kwa ajili ya kuomba kuhifadhiwa taarifa zao kwenye “server” za ZICTIA. Halkadhalika, Kamati imegundua kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao kupitia Barua nambari CBA.164/289/01-C/76 ya tarehe 19/08/2023 kuiruhusu Wizara kununua “servers” nne (4) kupitia mradi wa ZIQUE kwa ajili ya kuhifadhia taarifa za Wizara ya

Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwa msingi huo, Kamati inamtaka Mkaguzi kufuatilia utekelezaji wa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wizara uhakikishe unafuatilia kwa karibu ununuzi wa seva zao ili taarifa zake ziweze kuhifadhiwa katika sehemu salama na kudhibitiwa ipasavyo.

## Hoja nambari 4.8.1.9: Kukosekana kwa mpango wa matumizi endelevu ya mifumo inayofadhiliwa kupitia miradi ya maendeleo

Kwa zaidi ya miaka 10 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekuwa ikipata ufadhili wa fedha na utaalamu kupitia miradi mbali mbali kutoka kwa wahisani wa maendeleo kwenye eneo la TEHAMA katika kujenga uwezo, kununua/kutengeneza mifumo na vifaa mbali mbali vya TEHAMA.

Ukaguzi umebaini kwamba ufadhili huo haujaleta tija kama ilivyostahili kwenye eneo la mifumo ya TEHAMA kwa sababu ya kukosekana kwa mpango wa matumizi endelevu ya mifumo hiyo. Mipango inayokuwepo Wizarani inaishia kwenye utengenezaji/ ununuzi wa mifumo husika bila kufanyika tathmini inayo onesha baada ya mfumo kukamilika na kukabidhiwa Wizarani utaendelezwa kwa utaratibu gani, gharama za maboresho na matengenezo ya mfumo zitalipwa kutoka vyanzo gani, mafunzo ya mara kwa mara ya watumiaji na wasimamizi yatafanywa kwa utaratibu gani n.k, hali hii imepelekea uwepo wa mifumo mbali mbali iliyofadhiliwa na wahisani wa maendeleo lakini haina tija kwa Taifa, mfanoni mfumo wa Zanzibar Learning Management System (ZLMS) ambao tangu kutengenezwa kwake zaidi ya miaka miwili (2) iliyopita mpaka leo haujatumika ipasavyo kwa kuwekewa programu na vipindi husika kwa ajili ya wanafunzi na watu wengine kujifunza. Mfumo wa School Information System (SIS) ambao umekuwa ukifadhiliwa na miradi zaidi ya miwili na kila mradi mmoja unapoishia panakuwa hakuna muendelezo mpaka uje tena mradi mwengine.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba kabla ya kuanza utengenezaji/ununuzi wa mifumo na vifaa vya TEHAMA, wakati wa kuandaa mpango/andiko uandaliwe mpango wa matumizi endelevu (sustainability plan) ya mfumo na vifaa husika ili kuhakikisha kwamba mahitaji yote yanazingatiwa na kwamba mifumo na vifaa husika vinatumika kama ilivyokusudiwa kwa muda uliopangwa bila kukwamia njiani.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara kupitia Idara ya TEHAMA imechukuwa hatua ya kutayarisha "Business Continuity Plan (BCP)" na "Sustainability Plan" kwa lengo la kuhakikisha kwamba mifumo yote na vifaa vya TEHAMA vinatumika kama ilivyokusudiwa bila kukwama.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati imebaini kuwa hadi inakamilisha uchunguzi wake tarehe 25/08/2023, bado Wizara haijakamilisha uandaaji wa Mpango wa Matumizi Endelevu (Sustainability Plan). Hali hiyo inaifanya Kamati kushindwa kuridhika na majibu ya Wizara na kukubaliana na hoja ya CAG.

Kuwepo kwa Mpango huo ni muhimu sana kwa vile utaisaidia mifumo hiyo kuweza kuendelea kufanyakazi hata baada ya mradi kuisha kutokana na mipango ambayo Wizara itakayopanga ili kuhakikisha uendelevu wa mifumo ya Serikali.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wizara uweke kipaumbele kuandaa Mpango wa Matumizi Endelevu (Sustainability Plan) ya mifumo ya TEHAMA.

## Hoja nambari 4.8.1.10: Uwepo wa mifumo zaidi ya mmoja inayofanya kazi za aina moja

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Elimu imekosa usimamizi mzuri wa utengenezaji wa mifumo, ambapo mifumo inatengenezwa bila ya kuratibiwa na kusimamiwa katika ngazi ya Wizara na badala yake wanaotengeneza mifumo husika wanafanya hivyo kwa kuangalia mahitaji ya Idara au Kitengo pekee hali ambayo inapelekea uwepo wa baadhi ya mifumo ambayo inafanya kazi zinazoendana na kuongeza gharama za usimamizi na uendeshaji.

Mfano, mfumo wa ZLMS unaotumika kwa ajili ya wanafunzi kujisomea na mfumo wa ZEAS unaotumika kwa ajili ya wanafunzi kujifanyia tathmini (assessment), mifumo hii ingeweza kuunganishwa na kuwa mfumo mmoja unaoruhusu wanafunzi kujisomea na kujifanyia tathmini kulingana na maarifa waliyopata.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Elimu kuunganisha mifumo yote yenye matumizi yanayoendana ili kuwepo na mifumo michache ambayo Wizara itaweza kuisimamia kwa karibu na kuhakikisha kwamba inaleta tija na ufanisi kwenye utendaji kazi za Wizara. Moja wapo ya mifumo ya kuunganishwa ni pamoja na mfumo wa ZLMS na mfumo wa

ZEAS.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara kupitia Idara ya TEHAMA imechukuwa hatua za kuiunganisha mifumo ya ZLMS na ZEAS ili Wizara iweze kuisimamia kwa ukaribu na kutoa tija kwa watumiaji wa mfumo husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Wizara imefanikiwa kuiunganisha Mifumo ya ZLMS na ZEAS ambapo kwasasa mfumo wa ZLMS umefutwa kabisa na kubakishwa mfumo wa ZEAS tu ambao umeongezewa baadhi ya 'module' zilizokuwepo katika mfumo wa ZLMS ili kuweza kuiunganisha mifumo hiyo kwa ukamilifu. Hali hiyo itaisaidia Wizara katika kufanikisha kwa urahisi uwezo wa wanafunzi kujisomea na kujifanyia tathmini kulingana na maarifa waliyoyapata.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wizara uhakikishe unausimamia Mfumo wa ZEAS ulioanzishwa ili uweze kutumika ipasavyo na kuleta tija kwa wanafunzi wetu.

## Hoja nambari 4.8.1.11: Ushirikishwaji hafifu wa watumishi katika utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kwamba mifumo yote ya TEHAMA inayotengenezwa/kununuliwa na Wizara ya Elimu haina ushirikishwaji wa kutosha kwa watumishi wa Wizara hiyo walioko Pemba ingawa inapokamilika hutumika Unguja na Pemba.

Hali hii inapelekea uwepo wa ugumu mkubwa katika utumiaji na upatikanaji wa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa Pemba kwa sababu ni lazima msaada wowote unaohitajika utolewe na watumishi walioko Unguja ambao hawapatikani muda wote wanapohitajika kutoa msaada unaotakiwa na kusababisha matumizi hafifu ya mifumo hiyo kwa upande wa Pemba.

Aidha, inapotokezea changamoto za kiufundi katika mifumo hiyo kwa upande wa Pemba wasimamizi wa Wizara kutoka Unguja hulazimika kusafiri kwenda Pemba kwa ajili ya kutatua changamoto hizo jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwagharama zisizokuwa za lazima kwa Wizara ya Elimu.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba inaongeza ushiriki wa

watumishi wa Pemba kuanzia kwenye wazo na mahitaji ya mifumo mbali mbali, utengenezaji/ununuzi, mafunzo, utumiaji na utoaji wa msaada kwa watumiaji n.k ili kuhakikisha kwamba watumishi wa Pemba wanakuwa na uelewa mpana na umiliki wa mifumo hiyo sawa sawa na wale wa Unguja ili kuweza kupata tija na ufanisi uliokusudiwa.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Uanzishwaji wa mifumo yote ya TEHAMA, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA mafunzo na shughuli zozote zinazohusiana na masuala ya TEHAMA hutekelezwa kwa mashirikiano baina ya wafanyakazi wa Idara ya TEHAMA katika Elimu kutoka Makao Makuu Unguja na Ofisi ya Pemba. 0713234550

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kutokuwepo kwa ushirikiano kati ya Watendaji wa Idara ya TEHAMA kwa upande wa Unguja na Pemba. Hali inayopelekea watumishi wa Pemba kukosa elimu ya kutosha ya kuiendesha mifumo hiyo na hatimae huiongezea gharama Wizara kwa Watendaji wa kusafiri kwenda Pemba iwapo kutajitokeza kasoro yoyote ili kutatua changamoto hiyo.

Kuwepo kwa kasoro hiyo kunapelekea kukosekana kwa ufanisi wa utekelezaji wa kazi zinazopangwa na Wizara.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara ihakikishe inawashirikisha kiukamilifu watendaji wote wa Idara ya TEHAMA bila kujali maeneo yao ya kazi.

## Hoja nambari 4.8.1.12: Kutokufanyiwa matengenezo kamera za ulinzi zilizopo Wizarani

Ukaguzi umebaini kuwa kamera za ulinzi (CCTV Camera) zilizofungwa Wizarani (Unguja na Pemba) hazifanyiwi matengenezo ya mara kwa mara hali iliyopelekea ubovu kwenye kamera na mfumo wa kamera hizo na kusababisha kukosa ulinziuliokusudiwa Wizarani.

Kutokufanyiwa matengenezo kwa kamera za ulinzi zilizopo Wizarani kunaweza kupelekea kukosekana kwa usalama wa watumishi na rasilimali za Wizara.

Ukaguzi unashauri kwamba Kamera zote ziwekewe mpango wa matengenezo kwa kila mwaka wa fedha na zifanyiwe matengenezo husika kulingana na mpango huo ili kuiwezesha Wizara kukusanya matukio mbali mbali kwa sababu za kiusalama na kuzuia

au kutambua vitendo vya kihalifu mapema.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Kwa sasa, Wizara ina mpango wa kubadilisha CCTV kamera zote na kufunga CCTV kamera za kisasa kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa ofisi. Mpango huu umepangwa kutekelezwa kwa kupitia miradi ya maendeleo ya Wizara.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati katika kufanya uchunguzi wake, imebaini kwamba CCTV kamera kwa upande wa Unguja na Pemba zina kasoro inayotokana na kutofanyiwa matengenezo kwa muda mrefu. Hali inayopelekea kukosekana kwa ulinzi katika maeneo ya Wizara.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inashauri Wizara kuhakikisha mpango wao wa kuzifunga CCTV kamera mpya unatekelezwa kwa uharaka ili kuimarisha usalama na udhibiti katika maeneo yao ya Ofisi na kazi.

## Hoja nambari 4.8.1.13: Ufinyu wa Bajeti ya Idara ya TEHAMA

Sera ya TEHAMA ya Zanzibar ya mwaka 2013 sehemu ya 4.8.1.2. (a) inaelekeza kwamba, kila taasisi ya umma itatenga fedha za kutosha kwenye bajeti zake za kila mwaka kwa ajili manunuzi ya TEHAMA, matengenezo ya vifaa vya TEHAMA, mifumo na mitandao kwa ajili ya mabadiliko ya haraka ya Teknolojia.

Ukaguzi ulibaini kwamba Wizara ya Elimu ilitenga takribani asilimia 0.07 ya bajeti yake kwa ajili ya Idara ya TEHAMA kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 ambayo haikuzingatia ubunifu, uvumbuzi na kujenga uwezo kwenye TEHAMA kwa watumishi wa Wizara. Aidha, bajeti hii imejumuishwa na bajeti za Idara nyengine kiasi cha ukaguzi kushindwa kuitambua pasipo msaada wa muhasibu hali inayodhoofisha ufanyaji wa tathmini ya utekelezaji wa bajeti husika.

Ufinyu huo wa bajeti ya TEHAMA unakinzana na maelekezo ya Sera ya TEHAMA ya taifa ambayo inapelekea kuzorotesha ubunifu na uvumbuzi kwenye TEHAMA hapa nchini.

Ukaguzi unashauri Wizara kuzingatia maelekezo yaliyowekwa kwenye Sera ya TEHAMA ya Taifa ya mwaka 2013 kwenye kutenga fedha za kutosha kupitia bajeti za kila mwaka.

Aidha, ukaguzi unashauri Wizara kuweka Programu ya TEHAMA kwenye bajeti zake huku ikionesha mchanganuo wa Pemba na Unguja (Sub Programs) ili kuongeza uwazi na

uwajibikaji wa Idara ya TEHAMA kwa kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti husika kirahisi ukilinganisha na hali ilivyo kwa sasa.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imehakikisha kuwa bajeti ya TEHAMA inajitegemea na pia Idara hiyo imepangiwa kutekeleza baadhi ya shughuli zake kupitia miradi mbalimbali ya WEMA.

Aidha, kuhusu mchanganuo wa programu kwa bajeti ya Pemba, umeainishwa katika mfumo wa IFMS.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haijaridhika na utekelezaji wa hoja iliyobainishwa na Mkaguzi kwamba Wizara ilitenga Bajeti finyu kwa ajili ya Idara ya TEHAMA, hali inayopelekea kupungua kwa ubunifu ndani ya Idara hiyo na kupunguza hamasa ya kuendelea kujituma na kuleta mabadiliko ndani ya Idara ya TEHAMA na maendeleo ya Wizara kwa ujumla.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha wanatoa kipaumbele wakati wa kuandaa Bajeti ya Wizara kwa Idara ya TEHAMA ili kuongeza hamasa na ubunifu kwa Watendaji wa Idara hiyo ambayo ndio msingi wa maendeleo kwa ustawi wa Wizara na Serikali kwa ujumla.

## Hoja nambari 4.8.1.14: Udhaifu wa udhibiti na mazingira duni kwenye chumba cha Seva (Server Room)

Chumba cha Seva ni chumba muhimu sana kwa kuwa kinahifadhi Kompyutana Seva zinazoendesha mifumo na kuhifadhi taarifa za mifumo ya taasisi na vifaa mbali mbali vya TEHAMA. Kwa kuzingatia umuhumu wa usiri, uadilifu, na upatikanaji wa taarifa zinazohifadhiwa kwenye chumba cha Seva, Viwango bora kubalifu vya kimataifa vimeweka vigezo vinavyotakiwa kuzingatiwa kwenye chumba cha Seva, miongoni mwa vigezo hivyo ni pamoja na joto, hali ya unyevunyevu, udhibiti wa moto, udhibiti wa watu kwenye kuingia, uwepo wa kamera za ulinzi n.k.

Ukaguzi umebaini uwepo wa mazingira duni kwenye chumba cha Seva kilichopo Wizara ya Elimu Pemba, chumba hiki hakina udhibiti wa moto wa moja kwa moja (automatic fire suppresion system) kama inavyotarajiwa, udhaifu kwenye udhibiti wa mlango ambapo hakuna mashine ya kurikodi taarifa za watu wanaoingia ndani, hakuna Kiyoyozi (AC), udhaifu wa usafi wa mazingira, kutokuwepo kamera za ulinzi.

Miongoni mwa athari za udhaifu wa udhibiti na mazingira duni ya chumba cha Seva ni pamoja na kuhatarisha usiri, uadilifu, kupunguza utegemezi wa taarifa zinazochakatwa na kuhifadhiwa kwenye chumba cha Seva. Aidha, uwepo wa mazingira duni kama vile mavumbi kwenye chumba cha Seva unatishia matumizi endelevu ya vifaa vya TEHAMA vilivyomo kwenye chumba cha Seva vilivyoigharimu Serikali fedha nyingi, kukosekana kwa mifumo sahihi ya kuzima moto kunaziweka taarifa na vifaa vyote vya TEHAMA vilivyomo ndani ya chumba cha Seva hatarini kuteketea kama ikitokea janga la moto.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara kuyafanyia kazi mapungufu yote yaliyobainika kwenye ukaguzi kwa muda muafaka ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokea ambayo ni pamoja na hasara, upotevu wa taarifa za Serikali na Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Wizara imepanga kufanya ukarabati wa chumba cha seva pamoja na kuweka vifaa vya kisasa vya usalama kama vile CCTV kamera na Mfumo wa kudhibiti majanga ya moto (Automatic Suppression System)

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati katika kufanya uchunguzi wake imebaini kuwepo kwa dosari ya kutozingatia usalama na udhibiti wa chumba ambacho kinahifadhiwa Kompyuta na Seva za Wizara kwa upande wa pemba, jambo linalodoorofisha usalama wa taarifa nyeti na vifaa vya Wizara kutokana na kukosekana na udhibiti wa mlangoni, kutokuwepo kwa CCTV Kamera, kukosekana kwa kipoza hewa ambacho kimsingi kinasaidia kushusha “temperature” za Seva na kusaidia katika maisha marefu ya Seva hizo n.k.

Kamati imepokea majibu ya Wizara ambayo kimsingi yanakiri kuwepo kwa Dosari hizo. Hivyo, Kamati imeridhia kuibakisha hoja hiyo kwa ajili ya ufuatiliaji.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha vyumba ambavyo vinavyo hifadhiwa Seva za Wizara zinawekewa mifumo bora ya usalama na udhibiti ili kulinda taarifa na vifaa vya Wizara ambavyo kimsingi kina gharama kubwa sana.

## Hoja nambari 4.8.1.15: Kukosekana kwa vifaa vya TEHAMA na tija ya matumizi ya Mfumo wa ZLMS

Ukaguzi ulibaini kwamba ni Skuli nne (4) za msingi pekee kati ya Skuli mia moja na arobaini na mbili (142) za Pemba sawa na asilimia 3 ndio zilizopatiwa mafunzoya namna ya kuutumia mfumo wa ZLMS na kwa upande wa Unguja ni Skuli nne (4) za msingi pekee kati ya mia tatu na kumi (310) ndio zilizopatiwa mafunzo yakutumia mfumo wa ZLMS.

Kwa upande wa Skuli za Sekondari Pemba hakuna Skuli iliyopatiwa mafunzo katiya Skuli tisini na sita (96) na Unguja hakuna Skuli iliyopatiwa mafunzo kati ya Skulimia mbili na kumi na tisa (219) sawa na asilimia 0 ya utoaji mafunzo ya kutumia mifumo husika jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa yamatumizi ya mfumo wa ZLMS.

Aidha, imebainika kuwa wanafunzi walio wengi kutokuwa na vifaa vya TEHAMA kama vile Vishkwambi, Kompyuta Mpakato au Kompyuta ambavyo ndivyo vinavyohitajika ili kuweza kunufaika na mifumo ya Zanzibar Learning Management System (ZLMS) na mfumo wa Zanzibar Education Assesment System (ZEAS) ambayo wanafunzi wangeweza kujisomea kwa muda wao wakiwa majumbani mwao. Hali hii inapunguza upatikanaji wa tija na ufanisi kwenye elimu kwa kutumia mifumo hii.

Ukaguzi unashauri Wizara kufanya mapitio ya mpango wa mafunzo kwa wanafunzi wote wa Skuli za Msingi na Sekondari na kuhakikisha kwamba unajumuisha wanafunzi wote ili kupatiwa elimu ya namna sahihi ya kuitumia mifumo ya ZLMS na ZEAS kwa wakati.

Aidha, kwa upande wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kujisomea ukaguzi unashauri Wizara kuandaa mpango mbadala wa kuwawezesha wanafunzi kupata vifaa hivyo kwa kupitia "School Hubs" au kwa kila mwanafunzi mwenye uhitaji.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Kwa kuwa Wizara imepanga kuanzisha mfumo wa LMS kwa mwaka huu wa fedha, mpango huo unaendana na mpango wa mafunzo kwa walimu wa masingi na sekondari pamoja na walimu wa ICT waliomo kwenye hubs ambapo walimu wote hawa watahusika katika kutoa mafunzo kwa wanafunzi kupitia skuli zao na kwenye hubs.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haijaridhishwa na majibu ya Wizara kwa hoja hii ya Mkaguzi ambapo hoja hii imejibiwa kwa ufupi sana bila kuleta muelekeo unaokusudiwa katika kuonesha mabadiliko na muelekeo wa Wizara katika mnasaba mzima wa maendeleo ya wanafunzi wetu na ubora wa mifumo yetu katika kurahisisha na kuwasaidia wanafunzi wetu,

ukizingatia wanafunzi hawa ndo nguvu kazi inayotegemewa na Taifa letu miaka kadhaa mbeleni.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha wanaanda mpango kabambe wa kutoa mfunzo ya jinsi ya kutumia mfumo wa ZEAS kwa skuli za Msingi na Sekondari pamoja na kutoa vifaa vya TEHAMA kwa wanafunzi kupitia "Hubs" zilizopo kwenye skuli hizo ili kutoa fursa kwa wanafunzi kuweza kutumia mifumo hii kama ilivyokusudiwa, ma hatime kuengeza uelewa na maarifa kwa wanafunzi.

## 5.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA TUME YA MIPANGO ZANZIBAR (ZPC)

### Hoja nambari 5.12.1.1: Mfumo kutengenezwa kwa muda mrefu tofauti na makubaliano ya mkataba

Kwa mujibu wa mkataba wa Julai, 2020 uliofungwa baina ya Tume ya Mipango Zanzibar na Kampuni ya Techno Solution kuhusiana na utengenezwaji wa Mfumo wa Electronic M&E System kwa gharama ya shilingi 27,801,144 kipengele cha 7 cha mkataba huo kimeeleza kwamba mfumo unatakiwa kuchukuwa siku 30 za kazi na si zaidi ya miezi mitatu baada ya kusainiwa kwa mkataba huo. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa mfumo huo umekua ukiendelea kutengenezwa kwa zaidi ya miezi kumi na tisa (19) kutokana na hadidu rejea zilizotolewa na Tume kubainika kuwa na udhaifu katika kukusanya mahitaji ya matumizi ya Mfumo kwa upande wa Tume ya Mipango ambapo hadi ukaguzi unakamilika fedha zote zenye thamani ya shilingi 27,801,144 zimelipwa na mfumo huo bado haujamaliza na unaendelea kutengenezwa.

Hali hii inaonesha udhaifu kwa Tume ya Mipango Zanzibar kutokana na kutofanya upembuzi yakinifu wa mahitaji ya watumiaji wa mifumo (user requirements) kabla ya kuanza kutengeneza mfumo huo jambo ambalo limepelekea kuchelewa kukamilika na kuingizia hasara Serikali kutokana na kuongezeka.

Ukaguzi unashauri Tume ya Mipango Zanzibar (ZPC) kufanya upembuzi yakinifu wa kukusanya mahitaji ya watumiaji wa mifumo (business process and user requirements) kabla ya kuanza kutengenezesha mifumo yake kwa lengo la kupatikana kwa mifumo iliyoimara na kamilifu na kuepuka kuingia gharama za ziada zisizokuwa za lazima zitakazosababisha kuingiza hasara Serikali.

**Majibu ya uongozi wa Tume**

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E System), umechukuwa muda mrefu kukamilika kutokana na mapungufu yaliyojitokeza katika hatua za awali za ukusanyaji wa taarifa kutoka katika Wizara/Taasisi za Serikali kwa kuweka mahitaji ya watumiaji. Hali hii ilipelekea mfumo kutofanya kazi kama ilivyotarajiwa.

Tume ya Mipango imekusanya tena taarifa kwa mujibu wa mahitaji yawatumiaji wa mfumo na tayari imesharekebisha kasoro zilizojitokeza. Marekebisho yalifanyika nje ya Mkataba kwa maridhiano na Kampuni ya Techo Solution ambayo hayakuwa na gharama za ziada. Ushauri wa Mkaguzi umezingatiwa kwa utengenezaji wa Mifumo mengine ndani ya Tume ya Mipango.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imefanya uchunguzi wake na kubaini kwamba moja ya vikwazo vya mfumo huu kuchukua muda mrefu kukamilika ni ukweli kwamba ulikosa kufanywa upembuzi yakinifu ambapo ilipelekea kubadilishwa kwa mahitaji kwa mara kadhaa. Licha ya kuwepo kwa dosari hiyo katika kipindi cha ukaguzi, Kamati pia imebaini kwamba mfumo huo kwa sasa umekamilika na baadhi ya Maafisa Mipango wa Taasisi za Serikali wameshaanza kupatiwa mafunzo.

Kwa mnasaba huo, baada ya mahojiano, Kamati imeridhika na jitihada zilizochukuliwa na Tume ya Mipango, na kuridhika kuiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 5.12.1.2: Mzabuni wa mfumo wa M&E kufanya kazi bila ya mkataba

Kutokana na mabadiliko ya mahitaji yaliyofanyika baada ya mfumo kukamilika ilitakiwa mzabuni apewe mkataba wa ziada (addendum) ili aendelee kufanya kazi hiyo akiwa ndani ya mkataba. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa baada ya mkataba huo kumaliza muda wake mzabuni huyo aliendelea kufanya mabadiliko ya mfumo huo nje ya mkataba na nje ya hadidu rejea nyengine wala muongozorasmi wa mabadiliko hayo.

Kukosekana kwa mkataba huo kunauweka mfumo huo hatarini kutokana na kushindwa kumwajibisha mzabuni huyo kisheria ikiwa ataamua kuharibu mfumo au kukataa kuendelea kuutengeneza.

Ukaguzi unashauri Tume ya mipango Zanzibar (ZPC) kuhakikisha kuwa inafungamkataba mwengine na mzabuni au ifunge nae mkataba wa nyongeza (addendum) ili mfumo huo ufanyiwe matengenezo katika utaratibu wa kisheria zaidi.

**Majibu ya uongozi wa Tume**

Wakati wa majaribio ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E System) Tume ya Mipango ilibaini changamoto za kwa kukosekana matokeo yaliyotarajiwa ambazo zilisababishwa na kasoro katika ukusanyaji wa mahitaji ya watumiaji (User Requirement). Ni kweli umetumika muda mwingi kuendelea kurekebisha kasoro nje ya Mkataba wa awali. Ushauri wa Mkaguzi unachukuliwa kuhakikisha mapungufu yaliyojitokeza hayajitokezi tena.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwepo kwa dosari ya kuongezewa mahitaji na muda mfumo nje ya mkataba bila kuwepo kwa mkataba wa nyongeza (Addendum), jambo ambalo ni kinyume na miongozo ya Sheria. Hata hivyo, nyongeza hiyo ya mahitaji na muda haikupelekea kuongezeka na gharama za mfumo na badala yake mfumo huo ilikamilika kwa gharama za makubaliano ya awali ya mkataba. Hivyo, Kamati imeridhia na kuiondoa hoja hii kwa kuzingatia kwamba hakuna fedha ya Serikali iliyopotea.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Tume kuhakikisha inafunga mkataba wa nyongeza ili makubaliano mapya ya mfumo yaweze kuonekana katika mkataba yatakayoisaidia Tume kuwepo katika usalama wa kisheria.

## Hoja nambari 5.12.1.3: Kukosekana kwa umakini wa kutosha wakati wa ukusanywaji wa mahitaji ya watumiaji wa mfumo (User requirements)

Moja kati ya vitu muhimu na vya msingi sana katika mchakato wa utengenezaji wamfumo ni kujua jinsi taasisi inavyofanya kazi (business Processes) na kipengele cha ukusanyaji wa mahitaji ya watumiaji wa mfumo (user requirements). Vipengele hivi ndio vinaweza kuufanya mfumo uweze kufanya kazi sawa na utendaji kazi wa taasisi husika.

Ukaguzi umebaini kuwa hayo yote hayakufanyika kwa umakini wa kutosha na ushirikishwaji wa wadau haukuwa mzuri kiasi ambacho baada ya mfumo kutengenezwa kwa mujibu wa hadidu za rejea za ZPC, mfumo huo ulionekana hauendani sawa na mahitaji husika ya Tume.

Kukosekana kwa umakini katika ukusanyaji wa mahitaji ya watumiaji wa mfumo kumepelekea kuletwa kwa mfumo usiokidhi mahitaji ya Tume na kusababisha mfumo huo kuchukuwa muda mrefu usiojulikana kikomo chake kutokana na kuendelea kutolewa

kwa mahitaji mengine baada ya mfumo huo kukamilika.

Ukaguzi unashauri Tume ya Mipango Zanzibar (ZPC) kuhakikisha inakusanya mahitaji ya watumiaji wa mfumo kwa umakini mkubwa sambamba na kushirikisha kikamilifu idara na vitengo vyote vinavyotarajiwa kuutumia mfumo huo.

**Majibu ya uongozi wa Tume**

Ni kweli kulikua na kasoro katika ukusanyaji wa mahitaji ya watumiaji wa mfumo kilichopelekea mfumo kutofanya kazi ipasavyo. Tume ya Mipango tayari imefanya mapitio ya mahitaji halisi ya watumiaji wote wa mfumo huo na tayari imefanya marekebisho yanayohitajika.

Ushauri wa Mkaguzi unapokelewa na kuhakikisha mapungufu hayajitokezi tena katika kutengeneza mifumo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Tume ya Mipango kulikuwepo na dosari hiyo. Hata hivyo, Kamati imejiridhisha kwamba Tume imeshaifanyia kazi kasoro iliyobainika. Hivyo, Kamati imeridhika na utekelezaji wa hoja hii na kuifuta.

## Hoja nambari 5.12.1.4: **Kukosekana kwa Sera ya ugawaji haki za watumiaji wamfumo (User Access Policy)**

Kwa mujibu wa viwango bora kubalifu vinataka kuwe na Sera na miongozo ya namna ya ugawaji haki na mipaka ya watumiaji wa mfumo. Haki hizi hutakiwa kuendana na majukumu ya kazi ya muhusika. Ukaguzi umebaini kuwa ZPC hainamiongozo inayoelezea ugawaji wa haki hizo.

Kukosekana kwa Sera na miongozo ya kugawa haki hizo kumepelekea mfumo kuwaruhusu watu wa idara moja kufanya kazi ya idara nyengine, kwa mfano idara ya “Monitoring and Evalution” ambayo inajukumu la kufuatilia na kutathminimiradi imebainika kufanya kazi za uidhinishaji wa maombi ya miradi wakati kazihiyo ni ya idara ya “National Plan”.

Ukaguzi unashauri Tume ya Mipango Zanzibar (ZPC) kuandaa Sera na miongozo ya ugawaji haki za watumiaji wa mfumo na kuhakikisha kuwa mfumo utamzuwia mtu wa idara moja kufanya kazi ya idara nyengine.

**Majibu ya uongozi wa Tume**

Kwa sasa Tume ya Mipango kupitia mfumo wa M&E imefanya mgawanyiko wa haki za watumiaji kulingana na majukumu na wadhifa walionao watumiaji wa mfumo.

Tume ya Mipango kwa kushirikiana na kitengo cha TEHAMA cha Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ipo katika hatua za kuandaa Sera na Miongozo yake ya TEHAMA ambayo itahusisha pia Sera ya ugawaji haki za watumiaji wa mifumo iliyopo (User Access Policy). Ushauri wa Mkaguzi umezingatiwa ili kuwa na mfumo wenye tija na vigezo vinavyokubalika kama ilivyoelekezwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati imebaini kwamba ni kweli Tume haikuwa na Sera ya ugawaji haki za watumiaji wamfumo (User Access Policy) ili kukidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa katika matuimizi ya TEHAMA. Hata hivyo, bado Tume haijakamilisha uandaaji wake hali ambayo hoja hii inaweza kuja kujitokeza tena kwa kipindi kijacho.

Sambamba na hilo, Kamati imeshindwa kujua sababu zilizopelekea mfumo huo kuandaliwa bila ya kuwa na Sera, hasa ukizingatia Sera huwa inaanza mwanzo a baadae taratibu nyengine za utengenezaji mfumo zinafuata. Kwa msingi huo, Kamati haikuridhishwa na majibu ya Tume na kumtaka Mkaguzi kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Tume ya Mipango uhakikishe unashirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao katika uandaaji wa Sera ya ugawaji wa haki za watumiaji haraka iwezekanavyo ili hoja kama hii isijirudie tena.

## Hoja nambari 5.12.1.5: ZPC kuingiza kwenye mfumo taarifa za fomu za maombi ya miradi zinazotoka katika "Sector"

Kutokana na wadau wanaoomba miradi kutoka "sector" tofauti kuwa na ufikiaji wa mfumo, ni vyema taarifa za kuomba miradi yao kuingiza wenyewe ndaniya mfumo ili ZPC iendelee na majukumu ya kuidhinisha maombi (approval), ufuatiliaji na kufanya tathmini.

ZPC kufanya kazi ya kuingiza taarifa kutoka "Sector" zinazoomba miradi kunaweza kuongeza muda wa utekelezaji wa majukumu yake kutokana na kutingwa na kazi za

uingizaji wa taarifa (data entry) ambazo waombaji wangeweza kuziingizawenyewe.

Ukaguzi unashauri Tume ya Mipango Zanzibar (ZPC) kuhakikisha “Sector” zote ambazo ni wadau wamepatiwa mafunzo na wanauelewa wa kujaza maombi hayo kwenye mfumo na kazi ya ZPC iwe ni kuidhinisha maombi, kufuatilia na kutathmini.

**Majibu ya uongozi wa Tume**

Tume ya Mipango baada ya kufanya mapitio ya mahitaji ya watumiaji wa mfumo tayari uingizaji wa miradi unafanywa na 'sector" wenyewe. Mafunzo ya 'Sector" ya kuingiza miradi kwa watendaji yametolewa na yanaendelea kutolewa ili kuhakikisha utiaji wa taarifa unafanyika kwa ufanisi zaidi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake kasoro hii ilijitokeza. Hata hivyo, Tume tayari imeshachukua juhudi ya kurekebisha kasoro hiyo. Hivyo Kamati imeridhika na majibu ya Tume na kuiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 5.12.1.6: Kukosekana kwa muundo wa Kitengo cha TEHAMA

Muundo wa kitengo cha TEHAMA unaonesha tofauti ya majukumu baina ya Afisa TEHAMA mmoja na mwengine jambo ambalo hupelekea uwajibikaji mzuri katika kazi na kuepusha migongano katika kazi.

Ukaguzi umebaini kuwa ZPC ina wafanyakazi watatu wa TEHAMA ambao wote wanaweza kufanyakazi zote za kitengo chao kwa usawa.

Kutokuwepo kwa muundo kunaweza kupelekea kupungua kwa ufanisi wa kitengo hicho kutokana na wafanyakazi hao kutokujua tofauti ya majukumu na mgawanyiko wa kazi za kitengo chao.

Ukaguzi unashauri Tume ya Mipango Zanzibar (ZPC) kuandaa muundo wa kitengo cha TEHAMA ili kuweza kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kitengo hicho.

**Majibu ya uongozi wa Tume**

Kitengo cha TEHAMA kina wafanyakazi wanne (4). Kwa sasa kitengo kina wafanyakazi wawili (2) tu. Kati ya wafanyakazi wanne mmoja yupo katika masomo ya muda mrefu na mwengine ameazimwa Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kitengo cha Kuzuia Fedha haramu. Ushauri umepokelewa kuhakikisha kila mmoja anapangiwa majukumu ya kazi ambayo hayalingani na wenziwe.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba mpaka tarehe 14/11/2023 ambapo Kamati ilifanya kikao chake cha kiuchunguzi na Tume ya Mipango, kitengo hicho bado hakijafanyiwa mgawanyo wa majukumu katika muundo wake jambo ambalo linapelekea kukosekana kwa ufanisi katika utendaji wa kazi zao. Hivyo, Kamati haijaridhika na majibu yaliyoteolewa na hoja hii inaendelea kubakia ili Mkaguzi aweze kufutatilia utekelezaji wake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kufanya mgawanyo wa majukumu ya wafanyakazi wake wa TEHAMA ili kuweza kutenganisha majukumu yao na kuongeza ufanisi katika kazi zao.

## Hoja nambari 5.12.1.7: Kitengo cha TEHAMA kutengewa kiwango hafifu kidogo cha Bajeti

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Tume ya Mipango Zanzibar iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 11,264,594,638 kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Taasisi hiyo. Aidha kwa upande wa kitengo cha TEHAMA kilikadiria kupatiwa bajeti ya shilingi 11,500,000 kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya kitengo hicho. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Kitengo hicho kiliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 1,728,000 sawa na asilimia 15.03 ya makadirio.

Ukaguzi umebaini kiasi cha fedha kilichoingizwa ni kidogo sana jambo ambalo linapelekea kukidumaza kitengo hicho kiutendaji na kusababisha kutokufikia malengo yake ya kusaidia na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa njia ya kiteknolojia (Business enabler).

Ukaguzi unashauri Tume ya mipango Zanzibar (ZPC) kukipa kipaumbele kitengo cha TEHAMA kwa kukiongezea uwezo wa fedha katika bajeti yake ili kuweza kutekeleza kazi zake kwa ufanisi na weledi zaidi na kwa mujibu wa mipango mikakati iliyopangwa na kitengo hicho.

**Majibu ya uongozi wa Tume**

Bajeti kwa kazi za utekelezaji wa majukumu ya kitengo cha TEHAMA ziko chini ya Idara ya Utumishi na Undeshaji wa Tume ya Mipango, inapotokea mahitaji ya fedha za ziada Kitengo kinazingatiwa. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kitengo cha TEHAMA kimeongezewa bajeti yake kulingana na kazi walizojipangia na kufikia TZS 29,450,000.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba fedha za matumizi mengineyo kwa ajili ya Kitengo cha TEHAMA zinabebwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kadhalika, Kamati imegundua kuwa kwa mwaka 2022/2023, Tume imekiongezea bajeti Kitengo cha TEHAMA hadi kufikia milioni 29 jambo ambalo litakisaidia kitengo hicho kutatua baadhi ya changamoto zake. Kwa msingi huo, Kamati imeridhika na utekelezaji wa hoja hii na imeiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 5.12.1.8: Kukosekana kwa mpango wa usimamizi wa matukio(Incidence Management Plan)

Usimamizi wa matukio (incidence management plan) ni orodha ya hatua zinazochukuliwa ili kutambua, kuchanganua na kutatua matukio muhimu, ambayo yanaweza kusababisha matatizo katika taasisi ikiwa hayatorekebishwa. Hata hivyo, ukaguzi umebaini ZPC haina mpango huo wa usimamizi wa matukio.

Kutokuwa na muongozo rasmi unaotumika kuripoti na kutatua matatizo kunaweza kusababisha kuchelewa kutatuliwa matukio hayo na kupelekea kutopatikana huduma kwa muda mrefu.

Ukaguzi unashauri kwamba Tume ya Mipango Zanzibar (ZPC) kuandaa mpango rasmi (incidence management plan) utakaokuwa unafuatwa kwa ajili ya kutatua matatizo yanayojitokeza na baada ya kutatua matatizo hayo kuandikwe ripoti (incidence management report) ya utatuzi wa matatizo hayo.

**Majibu ya uongozi wa Tume**

Tume ya Mipango ipo katika hatua za awali za maandalizi ya mpango wa usimamizi matukio. Ushauri wa Mkaguzi umepokelewa na utafanyiwa kazi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikuridhishwa na utekelezaji hoja hii kwa vile mpango wa usimamizi wa matukio(Incidence Management Plan) bado haujakamilika. Kwa msingi huu, hoja hii inabakia na Kamati inamtaka Mkaguzi kufuatilia utekelezaji wa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Tume ya Mipango Znzibar uhakikishe unachukua juhudi za makusudi kukamilisha kwa haraka mpango wa usimamizi wa matukio (Incidence Management Plan) ili hatua za kutambua, kuchanganua na kutatua matukio muhimu ziweze kufanyika.

# 6.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

## Hoja nambari 6.5.1.1: Mikataba kutopitiwa na Mwanasheria Mkuu

Kwa mujibu wa kifungu cha 27(3) cha Sheria 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinachobainisha kuwa makubaliano yote yanayohusiana na bodi ya zabuni, baada ya kukubaliwa na bodi ya zabuni, kuombwa au mapendekezo yaliyotolewa, chini ya sheria hii yataridhiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa na pande mbili za mkataba.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na kitengo cha TEHAMA pamoja na idara ya ufundi na kupata maelezo ya kuwa mikataba ya mfumo wa eHMS, iDelivery and MRI haijapitiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata ushauri maelekezo kutoka katika Taasisi hiyo jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

Hali hii inaweza kusababisha hasara kwa Hospitali na Serikali kutokana na kuingia gharama za utengenezwaji wa mifumo bila ya mikataba kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu hususan ikitokea changamoto katika mikataba na utoaji wa huduma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mnazi Mmoja kupitia upya mikataba ili kuepusha hatari ya kisheria kwa Serikali na kwa maslahi mapana ya Serikali.

### Majibu ya Uongozi wa Hospitali

Kweli, Mkataba wa (Maintanance and Support) haukupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa vile thamani ya Mkataba huo ni ndogo (minor value) Tzs 18,000,000/= ambayo haujafikia kiwango cha kutangazwa zabuni, hii ni kwa mujibu wa kifungu 27(3) Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, namba 11 ya 2016 na kifungu cha 47(1) na 48(2) vya Kanuni za Ununuzi (Public Procurement Regulation) ya 2021.

***TANBIHI:*** *Kwa upande wa Mikataba ya MRI, Idelivery mchakato wote umesimamiwa na Wizara ya Afya*

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika ufuatiliaji wa hoja Kamati imebaini kuwa baadhi ya Mikataba bado inaendelea kusimamiwa na Wizara ya Afya wakati kiuhalisia usimamizi huo unatakiwa ufanywe na Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa vile inajitegemea kiutendaji na inayo 'vote' yake ya mapato na matumizi. Hali hiyo husababisha malalamiko na mgongano hususan wakati

wa utekelezaji na matengenezo ya vifaa vilivyopatikana kutokana na utekelezaji wa mikataba husika. Kwa msingi huo, Kamati imebaini kwamba mifumo yote kwenye hoja hii imesimamiwa na Wizara ya Afya yenyewe na Hospitali ya Mnazi Mmoja haikuwa na nafasi kuingilia mikataba hiyo.

Kwasasa Kamati imebaini kuwa mikataba inawasilishwa katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kama inavyoelekezwa na Sheria, Licha ya kujitokeza kwa kasoro hiyo wakati wa ukaguzi

## Hoja nambari 6.5.1.2: Kutokuwepo kwa mkataba baina ya Hospitali ya Mnazi mmoja na watoa huduma wa mifumo

Ukaguzi umebaini kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja haina mikataba ya huduma za matengenezo (maintanance and support) kwa mfumo ya PAC, mashine za CT scan pamoja na Xray, jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa mashine ya Xray iliwahi kufanyiwa huduma za matengenezo "maintanance" mara moja tangu mashine hiyo itumike na hadi sasa ina miaka saba. Kukosekana kwa makubaliano ya Mkataba kunaweza kukapelekea kutokuwekwa wazi kwa haki na wajibu wa kila upande, kutojua gharama kamili za mifumo, kutojua hatua za kufuatwa katika upatikanaji wa msaada wa kiufundi (technical support).

Kwa kuzingatia mapungufu hayo yaliyobainika ukaguzi unashauri Hospitali ya Mnazi Mmoja ikishirikiana na watoa huduma kuweka makubaliano ya maandishi kwa mujibu wa sheria na taratibu za manunuzi na kuhakikisha kwamba kuna uzingatiaji wa maslahi mapana ya Serikali.

### Majibu ya Uongozi wa Hospitali

Ni kweli Hospitali ya Mnazi Mmoja haikua na Mikataba ya moja kwa moja na watoa huduma kwa sababu fedha zote za Miradi ya Maendeleo zilikua zipo chini ya Wizara ya Afya. Hivyo michakato yote ya zabuni ikifanyika Wizarani na mikataba hio ipo Wizarani.

*Kwa upande wa Mikataba ya PAC, CT-scan na X-ray Idelivery mchakato wote umesimamiwa na Wizara ya Afya.*

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeelezwa kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipewa "Vote" yake tangu Mwaka

2016, lakini “Vote” hiyo ilikuwa inaingiziwa fedha za “Reccurent” tu na miradi yote ya maendeleo. Hata hivyo, bajeti yake ilikuwa ikibebwa na Wizara ya Afya yenyewe.

Kadhalika, Kamati imebaini kwamba mashine ya X-ray hazina mkataba/maelezo ya kimaandishi ambayo yanaeleza haki ya kila upande na wajibu wa kila upande jambo ambalo litapelekea kushindwa kumkamata mhusika endepo mashine hizo zikiharibika, hali inayopelekea kuweza kupotea kwa uwekezaji wa Serikali.

Sambamba na hilo, Kamati imebaini kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja iliandika barua kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ya Tarehe 17/10/2022 inayohusiana na Ombi la kutaka ushauri wa kuendelea au kutoendelea kufunga mkataba wa mashine ya mri ya hospitali ya mnazi mmoja, barua ambayo mpaka Kamati inamaliza kikao chake cha Tarehe 16/11/2023 haikujibiwa.

Kamati imebaini kwamba kuna mashirikiano na mawasiliano yasiyoridhisha baina ya Watendaji wa Wizara ya Afya na Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, ambapo mikataba, hususani ya “maintainance & Support” ambayo kimsingi inaratibiwa na Wizara ya Afya, kushindwa kufungwa na hatimae kunaweza kupelekea kuharibika kwa mali ya Serikali.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wizara ya Mnazi Mmoja uhakikishe unakabidhi usimamizi wa Miradi inayotekelezwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa Hospitali hiyo ili kuiwezesha Hospitali hiyo kuweza kujiendesha yenyewe kwa ufanisi bila kuwepo kwa urasimu usiokua na tija.

## Hoja nambari 6.5.1.3: Usimamizi Usioridhisha wa Miradi ya Mifumo ya TEHAMA

Ukaguzi umebaini uwepo wa udhaifu kwenye usimamizi wa Miradi ya TEHAMA na vile vile Mfumo kutojaribiwa na “quality assurance” ambapo hadi unakamilika haukupatiwa nyaraka muhimu zilizoombwa kwenye mradi wa eHMS, iDelivery, PAC, CT-Scan, Xray.

Miongoni mwa nyaraka zilizoombwa na hazikupatikana kwa ajili ya ukaguzi kwenye mradi ni pamoja na: -

i. General ICT Project Management policy.
ii. System Users requirements documents for each of the MMH’s systems and only ehms received.
iii. Approved Business Case/Proposal document for each of the systems that are

internally developed or outsourced and only ehms received.

iv. Quality evaluation report for all system.

v. Post-implantation review report of all system (eHMS, i Delivery, Sygonovia MRI, CT Scan, PAC, Biometric Attendance System).

vi. Feasibility study report of eHMS and iDelivery.

vii. UAT (User Acceptance Test report) reports for I delivery and Ehms

viii. System Design Documentation.

ix. Mpango wa Mradi (Project Schedule/Plan).

Udhaifu huo unatokana na Menejimenti kushindwa kutekeleza wajibu wake kwenye uendeshaji wa TEHAMA ndani ya hospitali ya Mnazi Mmoja, ambapo Kamati Tendaji ya TEHAMA ilitakiwa kusimamia hayo yote. Kukosekana kwa nyaraka hizo kumepelekea athari zifuatazo: -

(a) Kuwepo kwa mifumo inayofanana kazi kwa kuwa mfumo mmoja ungeweza kuboreshwa na fedha zilizobaki kutumika kwa matumizi mengine ya hospitali hivyo kumepelekea hasara kwa Serikali.

(b) Kukosekana kwa tija na ufanisi kwenye mradi kwa kuwa uwepo kwa mifumo kumesababisha kuzorota kwa huduma na wakati mwengine kutotumika mifumo hiyo na kueka mianya ya ubadhirifu katika mifumo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuunda kamati tendaji ya TEHAMA ili ianze kazi za kusimamia miradi ya TEHAMA kwa ukaribu wa kutosha.

Aidha, hospitali hiyo inashauriwa kuhakikisha kwamba inaandaa nyaraka zote zilizoombwa na ukaguzi kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na viwango kubalifu vya TEHAMA (best practices) na kuona kwamba nyaraka hizo zinapatikana kwa ajili ya ukaguzi.

**Majibu ya Uongozi wa Hospitali**

Ni kweli Hospitali ya Mnazi Mmoja haikua na Usimamizi wa Miradi ya mifumo ya TEHAMA, mifumo yote ziliku chini ya Wizara ya Afya.

Kuhusu Uongozi kamati tendaji Taasisi imelichukua suala hili na kulifanyia kazi japokuwa tumekosa muongozo kutoka Wakala wa Serekali Mtandao Zanzibar (egaz).

Hospitali ulichukua jitihada ya kuwapelekea barua Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) ya tarehe 09/01/2023 yenye kumbukumbu namba MMH/274/WSM/01 kwa ajili

ya kutushauri juu ya utumiaji wa mifumo na usalama wa taarifa za mifumo na tulitarajiwa kupatiwa miongozo ya utumiaji wa mifumo hata hivyo tulikosa ushirikiano kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) vile vile vyaraka za mifumo hii hazikutengenezwa na hospitali ya Mnazi mmoja kazi hii tumeirithi kutoka wizara ya Afya kuja Hospitali ya Mnazi mmoja, hata hivyo ushauri tunaupokea wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuufanyia kazi

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba awali mfumo wa eHMS haukuwa katika umiliki wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hata hivyo, baada ya kukosekana kwa nyaraka muhimu na mikataba ya mfumo huo, Uongozi wa Mnazi Mmoja ulifuatilia Shirika la Afya Duniani (WHO) ambae kimsingi ndie alienunua mfumo huo, na kuelezwa kwamba Mkataba ya mfumo huo upo kwa mtoa huduma anaeitwa ‘GPITG Limited’ ambae baadae alifanya mazungumzo na Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo mtoa huduma huyo hakuwa tayari kutoa ushirikiano mpaka uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ulipotishia kuvunja mkataba huo.

Lakusikitisha, mkataba huo ulikosa kipengele chochote ndani kinaoonesha kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio mmiliki halali wa mfumo huo. Kwa msingi huo, Kamati imeamua kwamba hoja hii iendelee kubakia hadi Hospitali ya Mnazi Mmoja utakapokabidhiwa rasmi Mfumo huo na Wizara.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wizara haraka iwezekanavyo ikabidhi rasmi Mfumo huo kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ili iweze kuumiliki kikamilifu.

## Hoja nambari 6.5.1.4: Kutofanya kazi kwa kifaa cha Biometric

Kifaa cha Biometric ni kifaa kinachosaidia katika usimamizi wa mahudhurio na hufuatilia saa za mfanyakazi. Hospitali ya Mnazi Mmoja wameweka mfumo wa Biometric System kwa lengo la kuondosha tatizo la uchelewaji wa wafanyakazi wa kuingia kazini na kuwahi kutoka bila ya kufikia muda halali uliopangwa kulingana na sheria.

Hivyo ukaguzi umebaini kwamba tangu tarehe 15/01/2022 wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja wamekosa huduma ya utambuzi wa mahudhurio kwa wafanyakazi kupitia mashine ya Biometric System kwa sababu ya kuisha muda kwa leseni ya matumizi ya mashine hiyo hali inayopelekea baadhi ya vitengo kujaza taarifa zao za mahudhurio katika madaftari na wengine kutojaza kabisa.

Kutokana na kifaa cha kukusanya taarifa za mahudhurio (Biometric System) kupata hitilafu ya utendaji kazi ukaguzi umebaini kitengo cha TEHAMA kiliomba kununuliwa orodha ya vifaa tofauti vya TEHAMA ikiwemo kifaa hicho cha Biometric System kwa uongozi wa MMH kupitia barua ya tarehe 26/01/2021 na barua ya tarehe 13/07/2021. Hata hivyo vifaa vyengine vilivyoombwa vimewasilishwa isipokuwa kifaa hicho cha Biometric System (ZKTECO) hakikuwasilishwa.

Hali hii ni kwasababu mzabuni aliyepewa kazi ya kusambaza vifaa vya Hospitali ya Mnazi Mmoja alikuwa anaidai hospitali hiyo, hivyo mzabuni alitaka alipwe deni lake ndipo aweze kukamilisha vifaa walivyokubaliana kwa mujibu wa barua ya tarehe 13/12/2022 ambayo imeainisha kuwa mchakato wa kumlipa deni msambazaji utachukua muda hivyo yafanyike manunuzi ya vifaa kwa mujibu wa mahitaji ya Hospitali, na vifaa hivyo vilifanikiwa kuletwa kupitia msambazaji mwengine lakini vilikuwa kinyume na vigezo vilivyotolewa na kitengo cha TEHAMA, jambo ambalo limepelekea kurejeshwa pasi na kununuliwa tena hadi tunamalizia ukaguzi wetu tarehe 22/02/2023.

Ukaguzi unashauri Hospitali ya Mnazi Mmoja kutumia teknolojia ya kisasa kulingana na hali halisi ya majengo ili kuweka udhibiti wa wafanyakazi kwa mfano kununua Facial Recognition Camera ambazo zitaekwa kwenye sehemu za kuingia (entrance point) za Hospitali ya Mnazi Mmoja na kuweza kuwadhibiti wafanyakazi ambao huenda katika hospitali binafsi wakati wa muda wa kazi bila ya kujali majukumu na wajibu wao wa kisheria vile vile utaweza kudhibiti uingiaji na utokaji wa wafanyakazi hospitalini.

Aidha, kwa kutumia mfumo wa eHMS kikamilifu kwa maeneo yote tutaweza kupima utendaji wa kila mfanyakazi kwani mfumo huo unarikodi na unatoa ripoti ya utendaji kazi wa kila mfanyakazi kwa sehemu yake kwa kuangalia idadi ya waliohudumiwa na hatua alizochukua kumuhudumia mgonjwa, hivyo itaweza kuondosha tatizo la kuwepo wafanyakazi/madaktari ambao hukaa muda wote kazini bila ya kufanya kazi yoyote au kufanyakazi kwa maslahi yake binafsi tu na kusaidia kufanya tathmini ya kila mfanyakazi.

Aidha, ukaguzi unashauri Serikali kupitia uongozi wa hospitali hiyo kutumia teknolojia ya kisasa kwenye majengo ikiwemo milango (Smart Door) ili kuepusha kusambaza maradhi na kwa kuwa hivi karibuni kuzuka maradhi mengi ya mripuko na kusababisha wafanyakazi na wagonjwa kuhudumiwa/kuhudumia katika mazingira hatarishi ya kuambukizana maradhi kupitia vifaa vya hospitali na tukumbuke kuwa lengo la hospitali ni kutibu wagonjwa na sio kusambaza/kueneza magonjwa baina yetu.

### Majibu ya Uongozi wa Hospitali

Uongozi wa Mnazi mmoja umepokea ushauri wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

natutaufanyia kazi lakini, Mnamo tarehe 23/01/2023 Hospitali ya Mnazi Mmoja ilingia mkataba na kampuni ya JUMA FOUM TRADERS kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa machine za biometric.Mkataba huo ulikuwa na thaman ya Tsh 6,530,000/- baada ya kampuni ya JUMA FOUM TRADERS kukabidhi mashine za biometric kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, mashine hizo zipo chini ya kiwango kulingana na sifa za kiufundi zilitolewa (Technical specification) Kwa mujibu wa utaratibu na sheria za ununuzi, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeandika barua kwa mzabuni JUMA FOUM TRADERS kuja kuzichukuwa machine hizo na kuleta machine nyengine zinazoendana na sifa za kiufundi (Technical specification) zilizotolewa na endapo atashindwa kuleta machine hizo ndani ya siku kumi nan ne(14), Hospitali ya mnazi mmoja itakuvunja mkataba wake na kuingia mkataba na kampuni yengine itayokuwa na uwezo wa kuleta mashine zenye ubora na sifa zinazofaa na Hospitali.

*TANBIHI: Kwa sasa Hospitali ya Mnazi MMoja tayari inatumia mfumo wa biometric tayari unafanya kazi.*

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba mfumo wa "facial recognition" ni bora zaidi kuliko mfumo wa "biometrics" kwa vile utambuzi wa uwepo wa watendaji wa Hospitalini kupitia vidole kunaweza kwa asilimia kubwa kupelekea mwanya kwa watendaji kujisajili na baada ya muda mchache kuondoka, jambo ambalo katika mfumo ataonekana yupo kazini lakini kiuhalisia yupo nje ya maeneo ya kazi.

Aidha, Kamati imeridhika na ubunifu wa Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kutengeneza "Time schedule" ambayo kila daktari ataeleza na kuhakikisha kwamba muda huo atakuwepo kazini na katika eneo la kazi, na kutakuwepo na Kamati maalum ambayo itafatilia ahadi za madaktari hao, mda wowote na bila taarifa, jambo ambalo litaengeza uwajibikaji.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaushauri Uongozi wa hospitali ya Mnazi Mmoja kutumia zaidi mfumo wa "facial recognition" na mfumo wa eHMS ili kudhibiti na kujua watendaji ambao kiuhalisia wapo kazini na ambao hawapo kazini.

## Hoja nambari 6.5.1.5: Mifumo kutotumika kikamilifu

Ukaguzi umebaini kuwa mifumo ya eHMS na iDelivery haitumiki kikamilifu ambapo kwa upande wa eHMS mfumo ambao una moduli 24, kati ya hizo ni moduli 8 tu ndio

zinazotumika na 16 hazitumiki hii ni sawa na asilimia 33 ya moduli zinazotumika.

Jadweli lifuatalo linaonesha moduli zinazotumika na zisizotumika katika mfumo wa eHMS.

**Jadweli Nambari 13: Hali halisi ya Matumizi ya Mfumo wa eHMS**

| Numbari | Moduli Inayotumika | Moduli Isiyotumika |
|---|---|---|
| 1. | Reception Works | Admission Works |
| 2. | Laboratory Works | General Ledger Works |
| 3. | Storage And Supply Work/(STOCK) | Finence Center Work |
| 4. | Doctors Work Page | Patient Billing Works |
| 5. | Nurse Station Works | Quality Assurance Works |
| 6. | Dispensing Work(Phamace) | Procedures Works |
| 7. | DHIS2 Report | Procurement Works |
| 8. | Patient Records | Theater Work |
| 9. | Nurse Station Works | Morque Works |
| 10. | Dispensing Work(Phamace) | Optical Work |
| 11. | DHIS2 Report | HIV WORK |
| 12. | - | Dialiysis Works |
| 13. | | RCH WORKS |
| 14. | - | Management Riport |
| 15. | - | Radiology Work |
| 16. | - | Human Resources/Payroll |

Hivyo imepelekea baadhi ya taarifa za wagonjwa kuwepo katika mifumo na nyengine kuwepo katika mabuku na baadhi ya taarifa hazirikodiwi badala yake huandikwa katika daftari la mgonjwa na likitokea limepotea basi taarifa hizo hazipatikani, hii inatokea pale mfumo unapokuwa haupatikani au umepatwa na khitilafu vile vile kwa mujibu wa madaktari na wagonjwa ambao tulifanya mahojiano ni kwamba wafanyakazi kuwa hafifu licha ya kuwepo na wagonjwa wengi wanaowasili na wakati mwengine kuwa na hali mbaya zaidi hupelekea kutorikodi katika mfumo kwasababu ya kutaka kumuokoa

mgonjwa na kwa kuwa kipaombele cha mwanzo ni kumhudumia/kumuokoa mgonjwa. Licha ya kuwa ukaguzi uliomba ripoti za tathmini ya utoshelevu wa wafanyakazi na kutokuwepo kwa ripoti hiyo na vile vile kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu jambo ambalo lingesaidia katika kufanya maamuzi juu ya kuweka mfumo ama kujipanga kwa ajili ya kutafuta nyenzo ili baadae kuweza kuweka mifumo hiyo, badala yake kumewekwa mifumo bila ya kufuata taratibu za kuanzisha mradi (project manangement).

Ukaguzi unashauri kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kufuata taratibu zote muhimu za kuanzisha miradi ili kuepusha hasara kwa Serikali kwa kuanzisha miradi ambayo haitatumika na kuleta tija kama ilivyokusudiwa.

Aidha, ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhakikisha unanunua mfumo kwa mujibu wa mahitaji na vile vile kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kununua mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya matumizi ya hospitali ili kuepusha kujitokeza gharama za ziada ambazo hazina tija.

### Majibu ya Uongozi wa Hospitali

Ni kweli kwamba mfumo haujaenea maeneo yote ya Hospitali ya mnazi mmoja kutokana na ukosefu wa vitendea kazi ikiwemo komputa lakini Uongozi wa Hospitali ya mnazi mmoja imechukua jitihada ya kununua komputa 100 kwa ajili ya kukamilisha maeneo yaliokua hakufika kwa mfumo huo

Mzabuni tayari ameshapatikana (Quality Trader) nakilichobakia ni taratibu za ndani za manunuzi.

*TANBIHI: Kwa sasa Hospitali ya Mnazi MMoja imenunuwa Computer 100 na taratibu za ghalani zinaendelea kwa ajili ya kuziweka katika maeneo ambayo yalikuwa na mapungufu.*

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeona kwamba kuna baadhi ya “modules” za mfumo wa eHMS kama ‘procurement works na finance centre works’ tayari zimeshafanyiwa kazi na Serikali kwa ujumla kupitia utambulisho ya mifumo ya eProcurement na mifumo mengine ya uhasibu.

Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja tayari imeongeza “modules” za admission works na theater works, “modules” ambazo zilionekana na ukaguzi kwamba hazikua zikitumika. Kamati imeridhika na majibu yaliyowasilishwa na hatimae kuiondoa hoja hii.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja uhakikishe unaendelea kuitumia mifumo waliyonao pamoja na kuifanyia matengenezo ili iweze kufanya kazi kwa muda mrefu.

## Hoja nambari 6.5.1.6: Kutokuwepo kwa utekelezaji wa bajeti kwa upande wa vitengo ICT

Kutokana na upatikanaji wa fedha kutokulingana na mahitaji ya kitengo ukaguzi umebaini kitengo hicho kimeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo jambo ambalo huenda likapelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa na kutokukamilika kwa utekelezaji wa mpango wa kitengo husika.

Aidha, kutokana na upatikanaji wa fedha hafifu imebainika jumla ya shilingi 9,000,000 zilitumika kama ni malipo ya awali kwa ajili ya kufanya huduma za matengenezo ya mfumo wa eHMS na kupelekea uwepo wa deni la shilingi 9,000,000 hadi ukaguzi unakamilika.

Kutokana na uwepo wa changamoto hiyo ukaguzi umefanya mahojiano na mtengenezaji wa mfumo wa eHMS na kubainisha ya kwamba zaidi ya kipindi cha mwaka mmoja anatoa huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja bila ya kulipwa jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mkataba na kupelekea utendaji kazi usiofikia malengo waliojipangia.

### Majibu ya Uongozi wa Hospitali

Nikweli kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja inadaiwa na wazabuni mbalimbali akiwemo Kampuni ya GPITG lakini uhaba wa fedha zinazopatikana au zinazoingika/tunazopewa kutoka serekalii kuu (other cherge) ni ndogo ukilinganisha na uwezo ulipo pamoja na mahitaji makubwa ya Hospitali ya mnazi mmoja hata hivyo ushauri tunaupokea wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuufanyia kazi wakati uwezo wa fedha ukiruhusu.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli deni hilo lilikuwepo. Hata hivyo, tayari deni hilo la shilingi 9,000,000 limeshalipwa. Kwa vile hoja hiyo tayari imeshatekelezwa, Kamati haikuwa na maelezo zaidi na hatimae kuiondosha hoja hii.

## Hoja nambari 6.5.1.7: Udhaifu wa udhibiti wa matumizi kwenye mfumo wa eHMS

Ukaguzi ulifanya mapitio ya mfumo wa eHMS na kubaini uwepo wa matumizi ya mfumo yasiyo ya kawaida ambayo yanaiweka Hospitali ya Mnazi mmoja kwenye hatari kubwa ya upotoshaji wa taarifa zake zinazotolewa kupitia ripoti mbali mbali. Dosari hizo ni kama zifuatazo:

i. Watumiaji wa mfumo kwa upande wa ghala kutumia moduli ya GRN bila ya uwepo wa hati ya manunuzi (purchasing order) hali ya kuwa kwa sasa Hospitali ya Mnazi Mmoja dawa wananunua wenyewe na baadhi ya dawa wanapata kupitia Bohari Kuu kwa mfumo wa eLMIS hii imesababishwa na kutokuwepo kwa moduli ya GRN against Purchasing order kwa toleo la 4 ya eHMS na inapelekea kuchanganya taarifa tofauti za dawa ambazo zimenunuliwa na zilizokuwa hazijanunuliwa na kuweza kupeleka kupata tathimini ambayo sio sahihi katika mfumo wa eHMS.

ii. Kutotumia mfumo wa eHMS ulokuwa ni toleo jipya la “version 5” ambao umetatua madhaifu mengi yaliomo katika eHMS “version 4” na umeweka vidhibiti/control katika uingizaji na utoaji wa dawa bila ya kujua sababu muhimu ya kutotumia version hiyo.

iii. Kutoweza kurejesha taarifa za dawa kama taarifa hizo zimekosewa katika mfumo wa Ehms version 4 hivyo inapelekea kuwepo kwa taarifa zisizosahihi katika mfumo.

iv. Maombi ya vifaa kufanyika kwa mkono na mengine kufanyika kwa mfumo na vile vile “physical counting” kurikodiwa katika “excel sheet” hali ya kuwa mfumo unaweza kufanya kazi hiyo hii inapelekea kupoteza taarifa za dawa na kueka mianya ya uchukuwaji dawa kwa maslahi binafsi.

v. Dawa kurikodiwa na mifumo miwili tofauti eHMS na eLMIS hali ya kuwa mfumo wa eHMS unaweza kurikodi “GRN without purchasing order” na “GRN with purchase order” hivyo imepelekea kutojua sababu ya kutumia mifumo yote miwili kwa pamoja, hali hii inaashiria hali hatarishi katika usimamizi wa dawa.

vi. Kukosekana kwa baadhi ya vifaa na dawa kwa muda mrefu na kuwepo uhaba wa vitendeakazi kama vile kompyuta.

vii. Kutotumika kwa mfumo kwa ghala ya chakula na stationary na badala yake kutumia manual licha ya kuwepo kwa mfumo huo na kulipiwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja.

viii. Kukosekana kwa vipimo ambavyo hutumika sana katika wodi ya watoto wachanga na hadi ukaguzi unamalizika vifaa hivyo havipo kama ifuatavyo:-

a) Renal Function Test.

b) Liver Function Test.

c) Sisum Electrolyte.

d) Mashine ya phototherapy zipo chache ambapo mashine moja hutumiwa watoto wawili mpaka wanne.

e) Dawa za kufanyia vipimo cha CT- Scan hakuna na inawabidi wagonywa wanunue.

Ukaguzi unashauri uongozi uchukue juhudi za haraka katika kuhakikisha kwamba taasisi inatumia mfumo mmoja ili kueka vithibiti na kuondoa mianya ya uchukuaji dawa kwa maslahi ya mtu binafsi.

**Majibu ya Uongozi wa Hospitali**

Kwa sasa Hospitali ya Mnazi mmoja imeaza kutumia toleo la tano (Version 5) kwa ajili kuingiza taarifa za dawa na vifaa katika bohari kuu ya dawa.

Vile vile Hospitali ya mnazi mmoja tayari imeshafanya physical invertory kwa lengo kutumia toleo jipya la tano (5) katika Bohari kuu ya dawa ya Hospitali kwa ajili ya udhibiti wa dawa na vifaa tiba.

Kuhusu taarifa za zilizokosekana au kurejeshwa katika mfumo kwa sasa mfumo unafanyika chelezo (back up) kwa ajili ya kupatikana kwa taarifa nyuma.

Vile vile mfumo wa eLMS unatumia kuomba baadhi ya dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa (CMS) ambazo hazinunuliwi na Hospitali ya Mnazi mmoja.

*TANBIHI:* Ni kweli matatizo hayo yalikuwepo katika kitengo cha uchunguzi ila kwa hivi sasa serikali yetu tukufu imebinafsisha (outoscoure) ili kuboresha huduma hizo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia majibu yaliyowasilishwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja, Kamati imegundua kwamba wakati Mkaguzi anafanya kazi zake za ukaguzi, Hospitali ilikuwa katika mabadiliko ya mfumo wake wa eHMS (transition period) ya kutoka katika toleo la 4 kwenda toleo la 5 la mfumo huo na kubaini dosari nyingi zilizopelekea kupatikana kwa hoja hii.

Aidha, Kamati imebaini kwamba sehemu ya Famasia imebinafsishwa na sasa masuala yote ya dawa yatafanywa na Kampuni iliyopewa dhamana ambapo kazi ya Hospitali ni kufuatilia na kuleta udhibiti wa dawa. Kwa vile kasoro zilizobaika tayari zimeshafanyiwa marekebisho, Kamati imeridhika na utekelezaji wa hoja hiyo na hatimae kukubali kuifuta.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja uhakikishe unasimamia ipasavyo mifumo yake pamoja na wote aliyawapatia kazi ili kasoro kama hizi zisiweze kujirudia tena.

## Hoja nambari 6.5.1.8: Dosari katika usajili na ufuatiliaji wa akaunti zinazotumika katika Mifumo na Kanzidata

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa MMH haina program maalum za kuchunguza na kusimamia akaunti zinazotumika katika uendeshaji wa mifumo, hivyo imepelekea kutumia akaunti za ujumla (Generic account) katika mifumo ya iDelivery, eHMS na PAC, hii inapeleka uwezekano wa matumizi mabaya ya mfumo yanayoweza kufanywa na watendaji wasio waaminifu ambao mara nyingi huzitumia akaunti hizi kwa maslahi binafsi kwa mfano kuchukua kwa baadhi ya taarifa za wagonjwa na kuzisamba ikiwa ni mitandaoni n.k, hali ya kuwa taarifa ya mgonjwa ni taarifa za siri vile vile kutumia account hizo kwa kuzibadilisha taarifa za mgonjwa ili aweze kupata huduma fulani kama usafiri wa matibabu nje ya nchi.

Aidha, kwa kuwa akaunti hizo hazina majina mahsusi ya watumiaji kunaweza kupelekea kujitokeza vitendo vya ubadhirifu wa fedha ama wizi kama uchukuwaji wa dawa kwa maslahi binafsi na kuingiza hasara Serikali.

Vile vile imebainika kuwa hata kwa upande wa venda hutumia generic account jambo ambalo linawia vigumu kujua tukio/marekebisho fulani yamefanywa na muhusika au vyenginevyo.

Baadhi ya akaunti zilizobainika ambazo hazijafanyiwa usajili katika System na hazifuatiliwi na kuboreshwa matumizi yake ni kama zifuatazo: -

**Jadweli Nambari 14: Akaunti za ujumla zinazotumika katika mfumo**

| Nambari | Jina la Akaunti | Sehemu Zinazotumika |
|---|---|---|
| 1. | Root | eHMS database |
| 2. | ehms-bckend | eHMS database |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | MMH | eHMS database |
| 4. | Administrator | Front end |
| 5. | Account | eHMS Front end |
| 6. | Admin | I delivery front end na mfumo wa PAC |
| 7. | IT | PAC front end |

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhakikisha kwamba kila mtumiaji anapewa akaunti kwa mujibu wa miongozo na taratibu na kuhakikisha anawekewa mipaka ya matumizi katika mfumo, aidha kuhakikisha kwamba hakuna utengenezaji na utumiaji wa akaunti za jumla kukiwa hakuna umuhimu wa matumizi yake, na kama zikihitajika kutumiwa zinatakiwa kusajiliwa na kupewa idhini ya matumizi kwa watu maalum katika mfumo.

**Majibu ya Uongozi wa Hospitali**

Ni kweli changamoto hii ipo na hoja zote zilizotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tutazifanyia kazi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kukiri kuwepo kwa kasoro hizo na kuendelea kuzifanyia kazi hususan kwa kuweka udhibiti katika akaunti zinazotumika katika Mifumo na Kanzidata hususan kwa kila mtumiaji kupatiwa account yake na kuondokana na matumizi ya 'generic account'. Aidha, Kamati imegudua kuwa kwasasa Hospitali inazijafanyiwa usajili katika System na kuzifuatilia ipasavyo. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuridhika na majibu ya Uongozi wa Hospitali na kumtaka Mkaguzi kuenedelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Hospitali uhakikishe unaendelea kufuatilia kwa karibu watumiaji wa mifumo yake na kuwadhibiti ipasavyo ili watumiaji waweze kudhibitiwa na kuepusha kuvuja kwa taarifa za wagonjwa.

## Hoja nambari 6.5.1.9: Uwepo wa mifumo zaidi ya mmoja inayofanyakazi zinazofanana

Ukaguzi umefanya mahojiano na kitengo cha ICT na kubaini kuwa mfumo eHMS ambao ni ERP unauwezo wa kufanya kazi tofauti zinazofanywa na mifumo ya PAC system na Laboratory Information System vile vile na mfumo wa iDelivery ingawa mfumo wa iDelivery uko vizuri zaidi, pia ukaguzi umebaini mfumo wa PAC hawana support na kupelekea kupata ugumu katika kuusimamia mfumo huo vile vile kushindwa kufikia malengo ya mfumo wa PAC ambayo ni kutumika Zanzibar mzima badala yake kutumika baadhi ya Hosipali chache tu ikiwemo Hospitali ya Mnazi Mmoja na badala ya kutumia mfumo wa PAC ili kupata picha hulazimika mgonjwa kufanya tena vipimo ili kupata huduma hiyo ama inamlazimu picha hizo kuzitia katika DVD ama kuzitia katika flashi ili ziweze kusomwa na kupata huduma.

Kufanya hivyo kunahatarisha taarifa za wagonjwa wengine kupotea kwa sababu ya kuweza kuingiza virus ambavyo inaweza kuigharimu Serikali jambo ambalo kwasasa ni tatizo kubwa duniani.

Ukaguzi unashauri kuwa uongozi wa MMH kutengeneza Sera ya TEHAMA kwa kuzingatia miongozo na sera za Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar pamoja na miongozo ya Kimataifa kama vile COBIT, AFROSAI-E, n.k na kuhakikisha kwamba pamoja na mambo mengine yatakayo kuwemo kwenye sera hiyo liwepo takwa la kufanyika kwa tathmini ya mifumo iliyopo pindi Idara au kitengo fulani kinapopanga kununua mfumo wowote ili kujiridhisha kama mifumo iliyopo inaweza kutimiza haja na mahitaji ya watumiaji hao. Kwa ajili ya kuondoa mgongano wa maslahi ni vyema tathimini hii ifanywe na "team" ambayo itakuwa huru ya wataalamu wa TEHAMA na watumiaji wa mifumo iliyopo Wizarani na kuwasilisha ripoti yake kwenye uongozi wa Wizara kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi ya kununua mfumo mpya, kufanya maboresho kwenye mifumo iliyopo ili kukidhi haja, au kutumia mifumo iliyopo kama ilivyo kwa kuzingatia tathmini ya gharama na manufaa (cost benefits analysis) pasipo kuathiri sera za nchi za TEHAMA wakati ikiweka msisitizo kwenye kupatikana thamani ya fedha, tija na ufanisi.

### Majibu ya Uongozi wa Hospitali

Ni kweli mifumo ipo zaidi ya mmoja lakini mfumo mkuu wa Hospitali ni eHMS na mifumo mengine ni Picture archiving and communication system (PACS) unaotumika katika Depertment ya Uchunguuzi (Radiology) na Laboratoty Information System (LIS) unaotuma maabara pamoja na mfumo wa i-delivery unaotumiwa Marternity, Mifumo yote hiyo ina umuhimu wake kwa Hospitali katika utoaji wa huduma, Hospitali inatarajia

kufanyika kwa mawasilano ya mifumo hii (Intergration) kwa lengo la kuondosha tatizo hili kama alivyoshauri Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili Hospitali kuweza kutumia mfumo mmoja kwa lengo la utoaji bora wa huduma za Hospitali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kukiri kuwepo kwa kasoro iliyoelezwa na Mkaguzi. Hata hivyo, bado Uongozi una kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha mifumo waliyonayo inaunganishwa pamoja. Hilo litasaidia na kurahisisha utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi wetu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja uhakikishe unaiunganisha mifumo yao ili iweze kusomeka kwa pamoja na kurahisisha utendaji wa shughuli zake.
2. Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja uhakikishe unatengeneza Sera ya TEHAMA kwa kuzingatia miongozo na sera za Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar pamoja na miongozo ya Kimataifa kama vile COBIT na AFROSAI-E na kuhakikisha kunafanyika tathmini ya mifumo yao.

## Hoja nambari 6.5.1.10: Kutokuwepo kwa usalama na udhibiti mzuri wa taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja

Ukaguzi umebaini kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja ipo katika hatari ya kupoteza taarifa za wagonjwa, dawa na vifaa tiba zinazohifadhiwa ndani ya mifumo yake kutokana na kutotumia njia salama za udhibiti wa taarifa zilizomo ndani ya mifumo hiyo. Hali hii imesababishwa kutokana na kujitokeza kwa mambo yafuatayo: -

- Kwa upande wa mfumo wa eHMS Test Seva na backup Seva kuwekwa katika seva moja vile vile Seva ya Test kuwekwa kwenye chumba kimoja na live Seva, hata hivyo, Seva room inatumika kama ICT office vile vile seva moja kuwekwa juu ya UPS na seva nyengine kuwekwa juu ya cabinent, kushare ID card katika access control ili kuingia kwenye seva room /ICT office hata hivyo kipooza hewa kilichopo hakifanyi kazi vizuri.
- Aidha, ukaguzi umebaini kuwepo kwa wafanyakazi wanaotoa huduma kwa muda wa ziada bila ya kuwepo posho la wafanyakazi hao kwa mfano kitengo cha TEHAMA hukaa muda wa ziada na kuja siku za mapumziko inapolazimu kwa ajili ya kurekebisha na kutatua mifumo inayotumika hospitalini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa MMH kuwajengea uwezo wasimamizi wa mifumo hiyo ikiwemo kuwatengenezea mazingira mazuri ya maslahi kama ni motisha ya kuweza kutekeleza vizuri majukumu yao kulingana na muda mwingi wanaotumia wakiwa kazini pasi na malipo yoyote, hata hivyo ni vyema kuwapatia mafunzo ya udhibiti na usalama wa mifumo ili kuweza kusimamia vizuri na kuimarisha usalama wa taarifa zilizomo.

**Majibu ya Uongozi wa Hospitali**

Ni kweli tatizo hili limejitokeza kutokana na uhaba wa nafasi hali ambayo inapelekea kitengo cha ICT kutumia chumba cha server kama Ofisi.

Hospitali ya Mnazi mmoja inayo Backup server na live server haziko pamoja zipo maeneo tofauti kwa mfano live sever ya mfumo wa eHMS ipo jengo la Utumishi katika chumba maalum cha server na back up sever ipo katika majengo mapya ya Dodoma katika chumba cha ICT, hata vivyo Tayari server hizo zimeshawekwa katika maeneo maalumu yanayositahiki kuwekwa kama vile kwenye Rack maalumu yenye back up ya umeme.

Kuhusu uhifadhi wa data tayari (Storage) tayari uongozi umeshawasiliana na Wakala wa Serikali wa Miundombinu ya Tehama Zanzibar (ZICTIA) kwa ajili ya kupewa nafasi ya kuhifadhia Taarifa (data).

*TANBIHI:* Hospitali ya Mnazi MMoja inatarajia kufanyiwa ukarabati mkubwa kupitia mradi wa BADEA hivyo tunatarajia tatizo la ufinyu wa nafasi litakuwa limetatuka.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati iligundua kwamba ‘sever’ za Hospitali ya Mnazi Mmoja hazipo katika hali ya usalama kwani kiutaratibu hutakiwa kuwekwa katika chumba chake chenye ubaridi wa kutosha ambapo kitakuwa na ulinzi na udhibiti wa watu kuingia na sababu za kuingia. Aidha, ‘sever’ hizo pia hutakiwa kuwekwa nje ya maeneo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa usalama mzuri na udhibiti.

Kadhalika, ili ‘sever’ hizo ziweze kutumiwa ipasavyo ni lazima kuwepo na wafanya kazi wenye uelewa na mafunzo. Lakushangaza, fedha za mafunzo za Hospitali bado zipo katika Mfuko wa Wizara ya Afya, jambo ambalo linaifanya Hospitali kushindwa kutoa mafunzo hayo kwa watendaji wake na kwa wakati, na kuzidi kividhoofisha vitengo muhimu kama hiki cha TEHAMA.

Kamati pia imegundua kuwa Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja unashindwa kuwajengea uwezo watendaji wake hususan wanaosimamia mifumo ya TEHAMA kutokana na ukosefu wa fedha kutoka Serikalini. Aidha, Kamati imeelezwa kwamba fuko la mafunzo mpaka sasa lipo katika Wizara ya Afya, jambo ambalo linaifanya Hospitali

kushindwa kutoa mafunzo hayo kwa wakati, na kuzidi kividhoofisha vitengo muhimu kama hichi cha TEHAMA. Sambamba na hilo, Kamati imeshangazwa na uhalisia kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja, tangu Mwaka 2016 ilifanikiwa kupata "Vote" yake na kujitegemea katika masuala yote ya kibajeti ikiwemo kupanga Mishahara na Matumizi mengineyo, lakini inashindwa kujipangia mafunzo katika bajeti yao.

Kamati imebaini kuwa bado uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja haijalifanyikazi ipasavyo eneo hilo, hivyo hoja hii inaendelea kubakia kwa utekelezaji.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja uwajengee uwezo wasimamizi wa mifumo hiyo ikiwemo mafunzo ya udhibiti na usalama wa mifumo ili kuweza kusimamia vizuri na kuimarisha usalama wa taarifa zilizomo.
2. Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja uhakikishe unawapatia maslahi mazuri wafanyakazi wake wa TEHAMA ili iwe motisha ya kuwawezesha kutekeleza vizuri majukumu yao.
3. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe inaipatia Hospitali ya Mnazi Mmoja fedha za kutosha ili waweze kulipia madeni yanayowakabili pamoja na kutoa huduma zilizo bora.
4. Wizara ya Afya ihakikishe inarudisha Fungu la Mafunzo kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ili waweze kujipangia na kutoa mafunzo kwa watendaji wa Taasisi hiyo na kuweza kuleta tija na hamasa ndani ya Taasisi hiyo.

## Hoja nambari 6.5.1.11: Kutokuwepo kwa gharama halisi ya matibabu

Ukaguzi umebaini kuwa bei za dawa na vifaa tiba zilizomo katika mfumo wa eHMS ni za kubuni na sio halisi. Hali hii imebainika kutokana na kutokuwepo kwa miongozo ya bei ya gharama za matibabu kwa kuwa huduma za first track kwa mwaka wa ukaguzi zilikuwa zinakusanywa kwa fedha taslim ambapo imethibitisha kutokana na barua ya tarehe 13/09/2021 ilioandikwa na kitengo cha ICT ya kupata muongozo wa gharama za vipimo na huduma za wagonjwa zinazotolewa ikiwemo cost sharing (wagonjwa wa Serikalini) na first track (wagonjwa wa cash) japo kuwa gharama za bima za NHIF zinajulikana na zimewekwa na Hospitali husika ili ziingizwe kwenye mfumo lakini haukufanikiwa kupata miongozo hiyo.

Ukaguzi unashauri kuwepo na miongozo ya gharama za vipimo na huduma za wagonjwa ili kusaidia katika kufanya tathmini ya upatikanaji wa kiwango cha dawa/vifaa tiba.

**Majibu ya Uongozi wa Hospitali**

Ni kweli kwamba kitengo cha 'Fast Track' kinatoa huduma za bima na huduma za malipo (cash) ambapo huduma za bima zina muongozo wake kutoka kampuni husika ya bima, kuhusu Mfumo wa Zanmalipo.

Toleo la ndani la malipo lipo na linatumika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwepo kwa Dosari hii wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, kasoro hiyo tayari imesharekebishwa. Kwa msingi huo Kamati imeiondoaa hoja hii.

## 9.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR

### Hoja nambari 9.4.1.1: Matumizi hafifu ya Mfumo wa SAGE kwenye kufanya malipo.

SUZA makao makuu hayapitii kwenye mfumo, yaani hufanywa nje ya mfumo. Halihii inaashiria kwamba asilimia 28.52 za matumizi pekee ndiyo yanayopitishwa kwenye mfumo wa SAGE ambayo ni ndogo sana ukilinganisha na gharama za kuutengeza na kuutumia.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa SUZA kuhakikisha unasimamia matumizi ya mfumo wa SAGE kikamilifu kwa lengo la kuleta tija iliyokusudiwa.

**Majibu ya Kamati ya Uongozi wa Chuo**

Chuo kinakiri kuwepo kwa matumizi hafifu ya mfumo wa SAGE. Udhaifu huo umetokana na kuchelewa kuungwa kwa Mkonga wa Mawasiliano wa SMZ katika kampasi za SUZA kulikotokana na hali ya bajeti ya Chuo ambapo kumepelekea baadhi ya matawi ya Kampasi za SUZA kushindwa kuwa na mawasiliano ya moja kwa moja au kupitia VPN na Makao Makuu ulipo Mfumo wa SAGE. Kwa sasa zoezi la kuunganishwa kampasi zote za SUZA na mkonga wa mawasiliano wa SMZ limekamilika, matarajio hadi kufika mwisho wa mwaka wa fedha 2022/2023, huduma za mfumo wa SAGE itakuwa imeshasogezwa kwenye matawi ya kampasi za SUZA.

Aidha, matumizi hafifu ya Mfumo wa SAGE pia yamechangiwa na utaratibu wa malipo ya mishahara ambayo hulipwa moja kwa moja kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar bila ya kupitia katika mfumo wa SAGE.

Chuo kipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mkataba baina yake na mtoa huduma wa mfumo wa SAGE hatua ambayo itasaidia kuimarisha matumizi ya mfumo huo katika kampasi nyengine na pia kutawezesha kuwapatia mafunzo ya matumizi sahihi ya mfumo wahasibu. Kwa barua kumb. Namba DB.135/142/01/G/139 ya tarehe 30/06/2023 kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Matumizi hafifu ya Mfumo yamechangiwa na malipo ya mishahara ambayo hulipwa moja kwa moja kupitia Wizara ya Elimu. Hata hivyo kwa sasa matumizi hayo ya mishahara yanapitishwa kwenye mfumo kama "dummy transactions" kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024.

Hatua hii imechukuliwa kwa dokezo la tarehe 22/01/2024 kutoka kwa Mkurugenzi fedha kwenda kwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Utawala.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya sababu ambazo SUZA wamezieleza mbele ya Kamati ya PAC. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba matumizi ya Mkonga wa Serikali inaipelekea SUZA kutumia gharama kubwa za malipo, kuwepo kwa 'speed' ndogo ya upatikanaji wa mtandao pamoja na upatikanaji wa kiwango kidogo cha 'Bandwidth'.

Aidha, Kamati imegundua kuwa SUZA wamekubaliana na kampuni ya TERNET iliopo Tanzania Bara ambayo itawapatia huduma kwa gharama ndogo na kupata 'bandis' 1,000 kutoka 200 wanazopata kutoka ZICTIA ambazo hazitoshelezi kwa mahitaji ya Chuo pamoja na matawi yake.

Ili kuepusha changamoto za kimtandao ambazo Chuo (SUZA) wanakabiliana nazo, Chuo kimechukua juhudi za kuiandikia barua Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) kupitia barua ya tarehe 19 Juni, 2023 yenye kumbukumbu nambari AD.17/40/02/05 kwa lengo la kutaka wawaruhusu Kampuni ya TERNET kutumia mkonga wao waweze kufikisha mtandao katika Chuo chao kupitia 'fibre' inayomilikiwa na ZICTIA.

Sambamba na hilo, Kamati imebaini kuwa Chuo kilikuwa na Mkataba na Mtoa huduma (SAGE) ambae walikuwa wakifanya kazi nae bila ya kuwa na usajili hapa Zanzibar jambo ambalo limepelekea kuikosesha Serikali kupata kodi yake ya zuio na kushindwa kutanua wigo wa utoaji huduma hususan katika Matawi ya Chuo. Hadi Kamati inakamilisha kazi zake za kiuchunguzi, bado huduma za mtandao zilikuwa zinapatikana Makao Makuu ya Chuo - Tunguu pekee na sio katika Matawi yake. Hivyo, pamoja na juhudi zilizochukuliwa na SUZA lakini bado hoja hiyo inaendelea kubakia hadi watakapokamilisha matumizi kamili ya mfumo huo wa malipo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. SUZA ihakikishe inafanya matumizi ya Mfumo wa SAGE katika maeneo yote ya Chuo pamoja na Matawi yake ili uweze kurahisisha matumizi ya TEHAMA ipasavyo.
2. SUZA ihakikishe inafanya kazi na watoa huduma ambao wamesajiliwa Zanzibar ili kodi ya zuio iweze kupatikana na kuingia katika Mfuko wa Hazina.
3. Ili kuimarisha utoaji wa huduma za mtandao katika Chuo cha SUZA na Matawi yake, Kamati inaishauri Serikali kupitia Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) kuiruhusu Kampuni ya TERNET kutumia Mkonga wa Serikali ili ifikisha huduma kwa bei rahisi na rafiki katika Chuo cha SUZA.

**Hoja nambari 9.4.1.2: Mfumo wa SAGE kutokuwa na uwezo wa kuingiza bajeti ya SUZA.**

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa SAGE hauna moduli ya kuingiza bajeti ya mapato na matumizi hali iliyopelekea Chuo kukosa udhibiti wa matumizi kwa kuzingatia bajeti iliyopangwa na kushindwa kutumia mfumo kufanya ulinganifu wa mipango (bajeti) na uhalisia kwenye makusanyo ya mapato na matumizi yaliyofanywa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa SUZA kuhakikisha kwamba unaweka mipango na kutekeleza uboreshaji wa Mfumo wa SAGE ili kuuwezesha kuingiza bajeti zote ya mapato na matumizi na kuhakikisha kwamba mfumo unatumika kudhibiti matumizi yasifanyike nje ya bajeti iliyoidhinishwa na iliyoingizwa kwenye mfumo. Aidha, tunashauri kwamba mfumo wa SAGE ufanyiwe maboresho ya ripoti za utekelezaji wa matumizi na mapato ili ziweze kutoka kwenye mfumo moja kwa moja.

**Majibu ya Kamati ya Uongozi wa Chuo**

Chuo kupitia Wakala Serekali Mtandao Zanzibar (eGAZ) kipo katika hatua za awali za kuwa na moduli za kuingiza bajeti ya SUZA kupitia mfumo utakaotolewa na Wakala Serekali Mtandao Zanzibar. Matumizi ya moduli hizo yanategemewa kuanza kutumika kwenye mwaka wa fedha 2023/2024. Chuo kupitia Wakala wa Serekali Mtandao (eGAZ) kimeshafanya maombi ya kuungwa na mfumo wa Serikali wa ERMS kwa barua kumb. Namba AD.17/401/02/13 ya tarehe 25/10/2023 kutoka SUZA, na hivi sasa Wakala Serekali Mtandao Zanzibar (eGAZ) inaendesha mafunzo maalumu ya mfumo wa ERMS ambao unategemewa kutumika kwa kazi hiyo.

• Watendaji wa SUZA wa vitengo vya Uhasibu, Mipango na Manunuzi wako kwenye

mafunzo kazi ya mfumo ERMS. kwa barua kumb. Namba CAB.109/139/01/71 ya

tarehe 05/01/2024 ya eGAZ,

• Chuo kimeshapewa mfumo wa kufanya majaribio kujiridhisha na utendaji wa mfumo. Mfumo wa majaribio unapatikana kwenye mkonga wa Sereakali kupitia anuani 10.1.77.5. wakati wa mafunzo hayo

• Wakala wa Serekali Mtandao tayari umetuma gharama za kuungwa kwa mfumo wa ERMS kwa matumizi ya chuo kwa barua kumb. Namba CAB.109/139/01/71 ya tarehe 05/01/2024 ya eGAZ.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati katika kuchunguza hoja hii, imebaini kwamba SUZA imeshachukua hatua za kujiunga na Mfumo mpya wa ERMS ambao utatumiwa na Taasisi zote za Serikali kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Aidha, Kamati imebaini kwamba SUZA inaendelea kutumia Mfumo wa SAGE mpaka watakapokamilisha kujiunga na Mfumo huo mpya kwa vile taarifa zao bado zimo katika Mfumo wa SAGE.

Sambama na hilo, Kamati ilitaka kujua kama SUZA katika mwaka huu wa fedha wamepanga bajeti itakayowawezesha kujiunga na Mfumo mpya wa ERMS na kuelezwa kwamba kunahitajika jumla ya shilingi milioni 157 kutekeleza mpango huo lakini Chuo hakijapanga bajeti hiyo ila wanategemea kufanya uhaulishaji wa vifungu vya fedha za Mradi wa HEET. Kwa vile bado hoja hii haijatekelezwa ipasavyo, Kamati ya PAC imeshindwa kuiondoa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaushauri uongozi wa SUZA kuharakisha kujiunga na Mfumo wa ERMS ili Chuo kiwe na udhibiti mzuri wa matumizi yake.

## Hoja nambari 9.4.1.3: Kutokuwepo kwa mikataba ya utengenezaji na utoaji wa msaada wa kitaalamu kwenye Mfumo wa OSIM na SAGE.

Ukaguzi umebaini kwamba SUZA haina makubaliano rasmi kama vile mkataba au “MoU” na watengenezaji wa mifumo ya SAGE na OSIM kwenye hatua ya utengenezaji wa mifumo na kwenye hatua ya kupatiwa msaada wa kiufundi (Technical Support) hali inayopelekea uwepo wa vihatarishi vya usalama, uadilifu na upatikanaji wa taarifa za Serikali zinazoingizwa kwenye mifumo hiyo kwakuwahaijulikani wajibu, haki na mipaka ya mtoa huduma kwa upande mmoja na Chuokwa upande mwengine.

Aidha, kwa upande wa msaada wa kiufundi SUZA haina utaratibu rasmi wa kupatiwa msaada wa kiufundi kama vile "Service Level Agreement" ambao ulitakiwa kuhakikisha kwamba SUZA inapata huduma za usaidizi wa kiufundi kwenye mifumo yake wakati wote ndani ya mwaka mzima.

Kukosekana kwa makubaliano rasmi baina ya SUZA na watoa huduma wa mifumo hiyo kunapelekea vihatarishi vifuatavyo: -

- Mfumo kuendelea kuwa mali ya mtoa huduma kwa asilimia 100 wakati taarifa (data) zilizomo kwenye mfumo huo ni mali ya Serikali ambazo hazijawekewa utaratibu wa kuzilinda.
- Kukosekana kwa usiri wa taarifa za Serikali zinazoingizwa kwenye mifumo husika kwani mtoa huduma ndiye mwenye udhibiti wa mifumo kwa asilimia 100.
- Uadilifu wa taarifa za Serikali kuwa mashakani kwa kuwa Serikali haina udhibiti wa mifumo husika.
- Upatikanaji wa taarifa za Serikali zilizomo kwenye Seva za mtoa huduma kuwa mashakani kwani SUZA haina udhibiti wa Seva hizo na haina haki yoyote kwenye Seva na mifumo husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa SUZA kuhakikisha unafanya mambo yafuatayo: -

- Unaandaa makubaliano rasmi kama vile mikataba kati yake na watoa huduma wa mifumo yote kwa haraka iwezekanavyo kwa kuzingatia Sheria, Sera, Kanuni na Miongozo ya Kitaifa na Kimataifa.
- Kuweka bayana hali ya usalama, usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa za Serikali muda wote.
- Kufanya malipo stahiki kwa watoa huduma kwa mujibu wa Sheria za nchi.
- Kutatua changamoto zote zinazohusiana na mifumo husika.

### Majibu ya Uongozi wa Chuo

Mkataba wa utengenezaji na utoaji wa msaada wa kitaalamu wa mfumo wa SAGE upo na nakala zake zilitumwa wakati wa zoezi la ukaguzi. Nakla hizo zimeambatanishwa pia kwenye ripoti hii. Kulikuwa na ubadilishwaji wa mtoa huduma kutoka kwa mtoa huduma wa awali kwenda kwa mtoa huduma mwengine ili kupata huduma bora zaidi.

Utaratibu wa SAGE kwenye kubadilisha mtoa huduma unampa mtoa huduma mpya

kuendelea na makubaliano ya awali ya mtoa huduma wa awali. Hata hivyo Chuo kimeona udhaifu wa utaratibu huu na kipo katika hatua za kuingia makubaliano rasmi na mtoa huduma aliyebadilishwa kwa utaratibu wa SAGE.

Makubaliano ya awali ya matumizi ya mfumo wa OSIM yalikuwa ni baina ya Taasisi ya Mtandao wa Elimu na Tafiti ya Tanzania (TERNET) na SUZA. SUZA kama vilivyo vyuo vyengine vya Tanzania ni mwanachama mwasisi wa TERNET. Kupitia malipo ya uanachama wa Taasisi hio, SUZA na vyuo vyengine hupokea huduma tofauti za TEHAMA zinazotolewa na taasisi hiyo kwa gharama nafuu kwa vile gharama nyengine zinabebwa kwa pamoja na muunganisho wa vyuo wanachama takriban ni vyuo vyote vya Tanzania.

Mfumo wa OSIM matumizi yake SUZA yalianza kwa makubaliano baina ya SUZA na TERNET. Kutokuwepo kwa mawasiliano mazuri baina ya wenye mfumo wa OSIM na taasisi ya TERNET, viliviacha njia panda vyuo vilivyoanza matumizi ya mfumo huo na hivyo kutafuta mbadala wa kuendelea na huduma hiyo.

Hatua iliyofikiwa hivi sasa kwa upande wa SAGE, Chuo kimeandaa mkataba na mkandarasi na mkataba umepelekwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kwa ushauri na baadae kupatiwa Mtoa huduma huyo pamoja na kumtaka kusajili kampuni yake kwenye mamlaka za kodi Zanzibar.

Mtoa huduma wa SAGE tayari ameshafanya usajili wa kampuni yake katika mamlaka za Zanzibar na ameanza usajili wa Mamlaka za kodi za Zanzibar. Kwa sasa Mtoa huduma huyo yupo katika hatua ya kubadilisha TIN namba yake TRA iweze kuonyesha kuwa kampuni ina tawi Zanzibar. Kwa upenda wa OSIM, Chuo kimeanza kuchukua hatua zifuatazo kukabiliana na changamoto zilizojitokeza:

Kutengeneza mfumo ulio na umiliki wa Chuo ambao utaweza kuanza kutumika mwishoni mwa mwaka mpya wa fedha 2023/2024. Ili kusubiri kukamilika kwa mfumo unaotengenezwa, SUZA, imechukua hatua za kuwa na mkataba wa muda wa “transition period‟ baina yake na OSIM na sasa upo kwa mtoa huduma ya OSIM kwa ajili ya kusainiwa. Pia SUZA imeandaa mfumo wake wenyewe wa masuala ya ujasili na mitihani kwa kutumia wataalamu wake wa ndani ambao unapatikana kwa anuani: http://suzims.suza.ac.tz/

Mfumo huo hivi sasa upo katika hatua ya majaribio ili kuunganishwa na mfumo wa Serekali wa ZanMalipo. Barua ya maombi ya kuunganishwa inategemea kutoka wiki ya mwisho wa mwezi wa Januari na unatarajiwa kuanza kutumika rasmi 2024/25 baada ya kukamilika wa hatua zote muhimu zinazohitajika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba wakati wa ukaguzi kulijitokeza dosari ambazo Mkaguzi ameziainisha lakini kwasasa, uongozi wa Chuo umeshachukua hatua stahiki kurekebisha kasoro hizo kwa kuandaa Rasimu ya Mkataba ambayo tayari imeshawasilisha katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kuainishwa ushauri wake wa kisheria. Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhika na hatua zilizochukuliwa na Chuo na kuiondoa hoja hiyo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Chuo uhakikishe unatekeleza ushauri wa kisheria uliotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili utekelezaji wa Mkataba huo uweze kufanyika kwa misingi ya sheria.

### Hoja nambari 9.4.1.4: Mazingira yasiyoridhisha katika Vyumba vya kuhifadhia Mifumo ya TEHAMA.

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali za kiusalama katika Kituo Kikuu chakuhifadhia na kusambaza Taarifa (Data center) kilichopo makao makuu ya Chuo cha SUZA Tunguu pamoja na matawi mengine ya Chuo hicho. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kukosekana kwa mkusanyiko wa seva za mfumo ambazo ziloungwa na kufanya kazi kwa pamoja (clustering & load balancing) ili kuweza kupunguza mzigo wa kufanya kazi kwa Seva moja na kuondoa tatizo la kuzidiwa kiutendaji (slowness) na kuongeza uhakika wa kupata huduma.
- Kukosekana kwa nakala za ripoti “back up” ambazo zitaonesha muda gani back up imeanza na muda gani imemaliza na muhusika aliyefanya mchakato huo na muhusika aliyethibitisha kama back up hiyo ipo kamili na inafanya kazi.
- Chumba cha SUZA Tunguu cha kuhifadhia taarifa upande mmoja wa ukuta umeathirika na maji ya mvua ambayo yamepelekea kuta za chumba hicho kubanduka na kufyonzeka kwa maji, jambo ambalo linaweza kusababisha hitilafu ya umeme na kusababisha moto au kuharibika na maji kwa vifaa vya TEHAMA vilivyomo ndani ya chumba hicho na kupelekea kukosa huduma.
- Kukosekana kwa mlango madhubuti ambao utaongeza usalama wa kuingia ndani ya chumba hicho.

- Uchakavu wa chanzo mbadala cha umeme (Alternative power supply). Vifaa vya kuhifadhia umeme (Battery Backup) havifanyi kazi na endapo kutatokea hitilafu ya upandaji na ushukaji wa umeme Seva pamoja na vifaa vyengine vinaweza kupata hitilafu na kusababisha hasara na upotevu wa taarifa za Serikali zilizohifadhiwa kwenye Seva.

Ukosefu wa programu za usalama dhidi ya virusi (Antivirus) ndani ya Seva ambazo zimehifadhi mifumo ya SAGE pamoja na nakala za mfumo wa OSIM. Dosari zilizotajwa hapo juu zinaweza kusababisha athari ya upotevu wa taarifa muhimu za kifedha na zile za wanafunzi zilizomo katika mfumo wa SAGE na OSIMkwa mtiririko.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo kuhakikisha dosari zilizobainika ndani ya chumba hicho zinatatuliwa kwa haraka kwa kuzingatia miongozo ya viwango bora kubalifu kwenye vyumba vya Seva ili kuweza kunusuru taarifa za mifumo zilizomo ndani ya chumba hicho.

Majibu ya Uongozi wa Chuo

Uongozi wa SUZA utalifanyia kazi suala hili katika mipango ya bajeti zake ili kuweka mazingira ya „clustering & load balancing‟ na kuwa na ripoti nzuri za “backup.” Chuo kimezingatia marekebisho ya kuta zilizoathirika na maji kwenye chumba cha SEVA Tunguu na uwekaji wa mlango wa geti kwenye vyumba vya seva katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2023/2024. Chuo kimeshafanya mpango wa manunuzi wa “alternative power supply” kwenye chumba chake cha seva cha Tunguu na kitaingiza mpango wa marekebisho wa “power supply” za chumba cha seva kwenye mpango fedha wa 2023/2024. Kutokana na changamoto za awali za utaratibu mpya wa manunuzi kupitia mfumo wa manunuzi, Chuo kimechelewa kupata “Antivirus” ambazo utaratibu wake wa manunuzi ulipitia kwenye mfumo huo wa manunuzi.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 SUZA iliweza kutenga kiasi cha TZS. 778,045,000.00 kwajili ya ununuzi wa vifaa vya Tehama. SUZA imetangaza tenda namba SMZ/K0108/G/NCB/2021 ya vifaa hivyo vya TEHAMA. Hata hivyo zabuni hiyo ilichelewa kukamilika kwa uharaka kwasababu ilitakiwa irudiwe tena kutokana na changamoto za kimanunuzi zilizojitokeza. na mzabuni aliyeshinda hata hivyo SUZA tumefanikiwa kuingia mkataba na Mzabuni MS CHODA GENERAL SUPPLY na tayari ameanza kuleta vifaa hivyo awamu kwa awamu. kwa barua kumb. Namba AH.129/365/01/99 ya tarehe 14/06/2023 kutoka SUZA.

Tunategemea atakapokamilisha vifaa hivyo baadhi ya changamoto zilobainishwa na mkaguzi kama vile kukosekana kwa Antivirus zitaanza kutatuka. SUZA pia kupitia Mradi

wa Tanzania Education Authority (TEA) kimeanzisha “Data Center” mpya kwenya kampasi ya Willium Benjamin Mkapa - Mchanga Mdogo Pemba. Chuo kinategemea “setup” ya Data Center hiyo itakapokamilika itasaidia uwezo wa Data Center ya Tunguu.

Kwa upande wa “Data center” ya Tunguu chuo tayari kishaweka bajeti katika kifungu namba H3448 (53, 050,000/=) na kuanza ukarabati katika jengo la Kompyuta ikiwemo Data Center ikiwa ni miongoni mwa maeneo ya ukarabati huo katika robo hii ya tatu na ya nne ya mwaka 2023/2024. Kupitia Mradi wa HEET katika bajeti yake ya mwaka 2024/2025, Mradi kupitia kifungu 5.2.4 kimetenga USD 125,425 kwa ajili ya kuimarisha chumba hicho na kukiwekea vifaa vya kisasa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati imegundua kuwa hatua kadhaa zimetekelezwa katika ‘data centre’ ya Pemba kupitia Mradi wa ‘Tanzania Education Authority’ ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 70. Changamoto iliyopo ni kwa upande wa Makao Makuu ya Chuo - Tunguu ambapo kunakosekana kwa umeme wa uhakika na Chuo hakina njia mbadala ya upatikanaji wa umeme huo ambapo kupitia Mradi wa HEET, Chuo kinakusudia kuutekeleza katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, bado changamoto ya uingiaji wa maji katika vyumba vya kuhifadhia Mifumo ya TEHAMA ipo isipokuwa wanategemea kuifanyia kazi katika robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha (2023/2024) kupitia Mradi wa HEET.

Kwa vile hoja hii bado inaendelea kutekelezwa na Chuo, Kamati imeshindwa kuiondoa hoja hii hadi hapo itakapokuja kujiridhisha katika kipindi chengine cha kazi za Kamati.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaushauri uongozi wa Chuo unarekebisha dosari zilizobainika katika ukaguzi kwa kuzifanyia kazi ipasavyo ili maeneo ya kuhifadhia Mifumo ya TEHAMA iweze kukaa katika mazingira mazuri na kuiwezesha kudumu kwa muda mrefu.

## Hoja nambari 9.4.1.5: Mapungufu yaliyobainika kwenye Kamera za ulinzi (CCTV)

Chuo Kikuu cha Zanzibar kimefunga kamera za ulinzi (CCTV) kwenye majengo yake yaliyopo makao makuu ya Chuo na kwenye baadhi ya majengo ya matawiya SUZA kama vile Chuo cha Utalii n.k kwa lengo la kupata taarifa za kiusalama kupitia matukio yanayorikodiwa na kuhifadhiwa na mfumo wa Kamera hizo.

Ukaguzi umebaini mapungufu katika usimamizi na uendelezaji wa Kamera hizo, miongoni mwa mapungufu hayo ni kama yafuatayo:-

- Kamera za ulinzi za SUZA zinahifadhi matukio kwa kusuasua yaani matukio yanahifadhiwa vipande vipande bila kuzingatia mtiririko halisi.
- Chuo kupitia watumishi wa TEHAMA kutokuwa na udhibiti wa Kamera zilizofungwa katika Chuo cha Utalii na badala yake Kamera hizo kuendelea kuwa chini ya udhibiti wa wakandarasi waliojenga jengo la Chuo.
- Kutofanyiwa matengenezo ya mara kwa mara (regular maintenance services) kwa Kamera na kusababisha baadhi yake kushindwa kufanya kazi.
- Kushindwa kusimamia Kamera ambazo zimefungwa "Campus" za SUZA kunaweza kupelekea kukosekana kwa tija na ufanisi wa Kamera hizo, na kusababisha hasara kwa Serikali. Aidha, hali ya usalama wa jamii ya wanachuo na mali zao (watumishi na wanafunzi) kuendelea kuwa dhaifu. Ukaguzi unaushauri Uongozi wa SUZA kufanya mambo yafuatayo:-
- Kutengeneza Sera za usimamizi na uendeshaji wa Kamera na usalama na kuhakikisha kwamba SUZA inatoa elimu juu ya Sera hizo kwa jamii yote ya wana chuo pamoja na matawi yake yote.
- Uwekwaji wa Kamera za usalama uzingatie maeneo ya kimkakati ili kupata matukio yote muhimu yanayotokea hususani kwenye milango ya Afisi za viongozi, kumbi/ vyumba vya kufanyia mitihani, Afisi zote muhimu kama vile Maabara, Uhasibu n.k.
- Kuhakikisha kwamba kuna nafasi ya kutosha kuhifadhi matukio yanayorikodiwa angalau kwa miezi mitatu (3) kabla ya kufutwa.
- Kuhakikisha kwamba Kamera zote zinawekewa mpango na kufanyiwa matengenezo ya angalau mara moja kila mwaka.
- Kuhakikisha kwamba watumishi wa TEHAMA wa SUZA wanapatiwa mafunzo stahiki ya usimamizi na uendeshaji wa kamera za ulinzi na kwamba wanasimamiwa ipasavyo kwenye kutekeleza majukumu yao.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kulichunguza suala hili, Kamati imebaini kuwa Mkandarasi wa uwekaji mfumo mzima wa CCTV kamera katika Chuo cha Utalii Maruhubi umesimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo Amali. Kufuatia ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti

wa Baraza la Mapinduzi, jengo hilo pamoja na 'component' ya uwekaji wa CCTV kamera ulikabidhiwa kwa Chuo kikuu cha SUZA ambapo Kamera hizo zilikuwa na kasoro ambazo Mkaguzi amezibainisha zikiwemo kutounganishwa kwa kamera hizo, kututimia kwa idadi waliyokubaliana pamoja na kamera hizo kupitwa na wakati (out dated version).

Aidha, hadi Kamati inakamilisha kazi zake, dosari zilizoibuliwa bado hazijafanyiwa kazi. Hata hivyo, Chuo kimekusudia kuzifanyia kazi changamoto zilizojitokeza katika bajeti ya mwaka ujao wa 2024/2025. Kwa msingi huo, Kamati ya PAC imeshindwa kuiondoa hoja hiyo kwa hatua za ufuatiliaji hapo baadae.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na uongozi wa Chuo cha SUZA wahakikishe wanazifanyia kazi kasoro zote zilizoibuliwa na Mkaguzi ili hoja hii isiweze kujitokeza katika Ripoti zijazo.

## Hoja nambari 9.4.1.6: Uhaba na uchakavu wa Kompyuta za kufundishia wanafunzi pamoja na Kompyuta za wafanyakazi wa SUZA wanaotumia mifumo na shughuli nyengine za kiutendaji katika vyuo vya SUZA.

Ukaguzi umebaini kwamba SUZA inakabiliwa na changamoto ya uhaba na uchakavu wa Kompyuta za kufundishia wanafunzi pamoja na Kompyuta za wafanyakazi wa SUZA ambazo hutumika katika matumizi mbali mbali katika Chuo cha SUZA.

Hata hivyo, tulibaini uwepo wa mazingira duni kwenye chumba cha kufundishia Kompyuta ambapo Chuo wa Uandishi wa Habari Kilimani hakina Kiyoyozi (AC) na kupelekea Kompyuta zinazotumika kuwa na joto zaidi ya uwezo wake (Over heat) na kusababisha kushindwa kufanya kazi ipasavyo, ubovu wa Kompyuta nakukosekana kwa mpangilio mzuri kwenye madarasa ya kufundishia Kompyuta pamoja na vyumba vya madarasa kutumika kama stoo za kuhifadhia vifaa chakavu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa SUZA kuhakikisha kwamba SUZA inawekewa mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunza Kompyuta kuanzia kwenye vifaa vyaTEHAMA, vyumba vya madarasa, ulinzi na usalama wa vifaa kama vile kuweka "UPS" kwenye vifaa vyote vya TEHAMA, kuweka programu halisi za ulinzi/usalama (antivirus) wa Kompyuta na Seva zinazotumika ili kuleta tija na kuongeza ufanisikwa Chuo.

**Majibu ya Uongozi wa Chuo**

SUZA kimefanya manunuzi ya kompyuta mpya kwenye mwaka wa fedha tulionao wa

2022/2023 ila changamoto hizo. Utaratibu mpya wa mfumo wa manunuzi zimechelesha upatikanaji wa kompyuta hizo. Chuo kinataraji kuondoa kompyuta chakavu na kuweka kompyuta mpya kwenye maabara za kompyuta pamoja na kuwapatia watendaji wake kompyuta hizo. Sambamba na hili, bajeti za fedha za SUZA na miradi tofauti iliopo SUZA italipa kipaumbele suala la upatikanaji kompyuta mpya kwa ajili ya maabara na watendaji.

Hatua iliyofikiwa kwa sasa Mzabuni wa vifaa hivyo vya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ameanza kuviwasilisha SUZA na vinategemewa kufungwa sehemu tofauti za kampasi zenye uhitaji mkubwa wa vifaa hivyo. Zabuni ya vifaa tofauti vya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ipo katika mfumo wa manunuzi wa Serekali kwenye hatua za kumchagua mzabuni ili kuweza kutatua changamoto hizo. Kupitia mradi wa HEET, mzabuni ameshapatikana na tayari yuko katika hatua ya kukabidhi vifaa hivyo. Barua ya tarehe 26/12/2023 yenye Kumb. Namb CA.79/182/08/55 kutoka SUZA.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli SUZA ilikuwa inakabiliwa na changamoto ya uhaba na uchakavu wa Kompyuta za kufundishia wanafunzi pamoja na Kompyuta za wafanyakazi wao wanaotumia mifumo na shughuli nyengine za kiutendaji. Hata hivyo, Chuo kinampango wa kununua 'computer' 120 katika awamu ya mwanzo, 105 awamu ya pili na awamu ya tatu 180.

Katka kuthibitisha hayo, Kamati ilihitaji kupatiwa 'delivery note' na 'store ledger' na kuelezwa kwamba muhusika hakuwepo kwa vile alikuwa anasumbuliwa na maradhi ya macho. Kwa msingi huo, Kamati imeshindwa kujiridhisha juu ya ununuzi na uwasilishwaji wa 'komputer' hizo.

Kadhalika, Kamati imegundua kuwa pamoja na juhudi hizo za ununuzi watakaoufanya, bado changamoto hiyo itaendelea kuwepo kwani Kamati imeelezwa kwa makisio Chuo kinahitaji zaidi ya 'komputer' 500 ambapo SUZA inatarajia itakapofika mwaka 2025 wanategemea kuiondosha changamoto hiyo. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuweza kuiondoa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa SUZA uharakishe upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA ili ufanisi katika utendaji kazi zao uweze kuongezeka.
2. Uongozi wa SUZA uhakikishe unafuata Sheria za matumizi ya fedha za Serikali ili kuepukana na kasoro za kiukaguzi.

## Hoja nambari 9.4.1.7: Udhaifu kwenye mfumo wa kuzima moto SUZA.

Ukaguzi umebaini kwamba Chuo kikuu cha SUZA hakikubadilisha kwa wakati mitungi ya gesi ya kuzimia moto (fire extinguisher). Mitungi ya gesi iliyopo SUZA iliisha muda wake tangu Julai, 2021 lakini katika hali isiyo ya kawaida mpaka tunamaliza ukaguzi ilikuwa bado haijafanyiwa “services”.

Kukosekana kwa mitungi ya kuzimia moto iliyohai kunakiweka Chuo pamojana vifaa vyote vya TEHAMA kwenye mazingira hatarishi kwani ikitokea janga la moto ni wazi kwamba linaweza kuteketeza miundombinu yote ya TEHAMA na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali ukilinganisha na gharama za kubadilisha mitungi ya gesi. Aidha, kwa upande wa chumba cha Seva (data center) tulibaini kutokuwepo kwa mfumo rasmi wa kuzima moto chumba cha Seva (Fire Supression System) kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu kwenye chumba cha Seva.

Kwa kuzingatia umuhimu wa mfumo wa kuzima moto kwenye majengo na ule wachumba cha Seva ukaguzi unashauri SUZA kufanya tathmini ya ukubwa wa tatizo la mfumo wa kubaini na kuzima moto wenyewe kwenye majengo na kuweka kipaumbele kwenye chumba cha Seva (data center) na kisha kutengeneza mpango fedha na mpango kazi katika kutatua changamoto ya mfumo wa kubainikuzima moto wenyewe “Automatically”.

Aidha, ukaguzi unashauri ni vyema kufanya maboresho ya mitungi ya kuzimia moto kwenye maeneo yote kwa mujibu ya miongozo ya Kikosi cha Kuzima Motona Uokozi na kwamba SUZA iweke utaratibu utakaohakikisha kwamba mitungi ya kuzima moto inabadilishwa siku chache kabla ya kuisha kabisa muda wake wa matumizi ili kuweka ulinzi kwenye rasilimali zote zilizomo kwenye majengo yake.

Kwa ajili ya chumba cha Seva (data center) kunatakiwa kuwekewa mfumo wakemaalumu wa kukabiliana na moto (fire suppression system) ambao utajiendesha wenyewe na usio tumia maji kama maeneo mengine.

### Majibu ya Uongozi wa Chuo

SUZA imeyachukua mapendekezo ya kuwa na utaratibu mzuri wa kubadilisha mitungi ya kuzima moto iliyomaliza muda wake na mapendekezo ya kuwa na “automatic fire suppression system” kwenye vyumba vya kuhifadhia mifumo yataingizwa kwenye bajeti za Chuo kuanzia bajeti ya mwaka mpya wa fedha wa 2023/2024. Chuo tayari kishafanya upembuzi yakinifu na kujua mahitaji halisi pamoja na kuweka bajeti kwa ajili ya kazi hiyo. Hivi sasa inafanya mazungumzo na Uongozi wa Kikosi cha Zimamoto ili kuwa na njia sahihi ya kukamilisha kazi hiyo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa bado Chuo cha SUZA hakijaifanyia kazi hoja hii hasa ukizingatia kwamba vifaa vilivyobainishwa kutokuwepo (fire extinguisher) katika chumba cha kuhifadhia mifumo 'data centre' bado havijanunuliwa. Hata hivyo, Chuo kimeanza kufanya mazungumzo ya mdomo na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kuhusiana na matumizi bora ya mfumo wa kuzimia moto ikiwemo ubadilishaji wa mitungi ya gesi katika chumba cha 'data centre'. Kwa vile majibu yaliyowasilishwa hayajatosheleza kujibu hoja iliyoibuliwa, Kamati imeibakisha hoja hiyo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa SUZA uhakikishe unaipelekea maombi rasmi (kwa barua) Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar ya kubadilishiwa mitungi ya gesi katika chumba cha kuhifadhia taarifa za kielektroniki 'data centre' ili kuepusha athari za moto iwapo utakapotokea.

## Hoja nambari 9.4.1.8: Kukosekana kwa Muunganiko baina ya Mfumo wa SAGE na Mfumo wa OSIM.

Ukaguzi ulibaini kwamba hakuna muunganiko "Integration" baina ya mfumo waSAGE na OSIM pamoja na ukweli kwamba sehemu kubwa ya mapato yanayotokanana ada pamoja na gharama nyengine zinazolipwa na wanaChuo hutambulika kwa hatua ya kwanza kupitia mfumo wa OSIM ambao hutoa nambari za ankara(control numbers) na kupata uthibitisho kama fedha zimepokelewa kwenye benkiau la kwa kila nambari ya ankara iliyotengenezwa, na kwa kuwa mfumo wa SAGE ndio mfumo mama wa kihasibu ambao kimsingi unatarajiwa kuwa na taarifa zote za mapato na matumizi ya SUZA wakati wote kwa usahihi kwani mwisho wamwaka ni lazima SAGE isaidie kutoa taarifa za kuandaa hesabu.

Kukosekana kwa "integration" baina ya OSIM na SAGE kunapelekea changamoto mbali mbali zikiwemo:-

- Kufanya kazi mara mbili - taarifa zilizoingizwa kwenye mfumo wa OSIM kuingizwa tena kwa mkono kwenye mfumo wa SAGE na kupoteza muda usiokuwa wa lazima.
- Taarifa kuwa na makosa - kwa kuwa taarifa za mapato huwa ni nyingi sana na huingizwa kwenye mfumo wa SAGE kwa njia ya kawaida (manually) na wahasibu ambapo huathiriwa na makosa ya kibinadamu (human errors) na kupelekea kupoteza sifa ya usahihi (correctness).

- Ucheleweshwaji wa taarifa kuingizwa kwenye mfumo wa SAGE – Sehemu kubwa ya taarifa haziingizwi kwenye mfumo kwa wakati na kusababisha upotoshaji wa mapato ya SUZA, hali ya madeni ya wanafunzi kwa SUZA na SUZA kwa wanafunzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa SUZA uhakikishe mfumo wa SAGE pamoja na mfumo wa OSIM inaunganishwa kwa kuzingatia miongozo ya Kitaifa na Kimataifa ili kuwepo na udhibiti imara wa taarifa za kifedha pamoja na taarifa muhimu za wanafunzi zilizomo ndani ya mifumo hiyo.

**Majibu ya Uongozi wa Chuo**

Swala la kuunganishwa kwa mfumo wa SAGE na mfumo wa OSIM litafanyiwa kazi mara tu mkataba baina ya SUZA na OSIM utapokamilika kama maelezo yalivyotolewa kwenye sura 2.7 ya jadweli hili. Katika kutafuta njia ya kudumu ya kuondoa tatizo hilo SUZA tayari imeshatayarisha mfumo wake kwa kutumia wataalamu unaopatikana kwa anuani hii:http://suzims.suza.ac.tz/ Mfumo huo upo katika hatua za majaribio na mashauriano ya kuunganishwa na mfumo wa Serikali wa ZanMalipo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati imebaini kwamba bado Mfumo wa SAGE na OSIM haujafanyika kwa vile OSIM hajafanya usajili wake Zanzibar kama inavyoelekezwa na Sheria zinazoongoza masuala ya ununuzi Zanzibar. Hata hivyo, Chuo kina mpango wa kuachana na Mtoa huduma huyo watakapokamilisha mfumo waliouandaa hususan kwa kazi hiyo ya kutoa matokeo na kudahili wanafunzi. Kamati imegundua kwamba utekelezaji wa hoja hii bado unahitaji muda ili uweze kufanyiwa kazi, hivyo hoja inabakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa SUZA uharakishe unakamilisha hatua zilizobakia za Mfumo wao ili uweze kutumika ipasavyo.
2. Uongozi wa SUZA uhakikishe unakamilisha Mfumo huo kwa kufuata miongozo inayotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao.

## Hoja nambari 9.4.1.9: Udhibiti Duni wa Taarifa zinazoingizwa katika Mifumo ya SAGE.

Ukaguzi umebaini udhaifu kwenye udhibiti wa mfumo wa SAGE katika uingizaji wa taarifa

za wanafunzi ambapo tulibaini kwamba muhasibu mapato anafanya kazi ya kuingiza taarifa za mapato peke yake mpaka mwisho bila ya kuwepo na mtu mwengine anayekagua/kuidhinisha taarifa hizo kabla ya kurikodiwa kwenye kitabu kikuu cha kwenye mfumo wa SAGE (General Ledger) na kupelekea mfumo kuwa na taarifa nyingi zisizo sahihi ambazo pia hutokea kwenye ripoti na kupotosha watumiaji mbali mbali ikiwemo Umma, Uongozi wa SUZA, Wakaguzi na Wanafunzi wenyewe.

Katika kupitia taarifa zilizoingizwa kwenye mfumo wa SAGE kwa mwaka 2021/2022ukaguzi ulibaini kuwepo kwa deni wanalodaiwa wanafunzi linalozidi shilingi Bilioni 5 na deni linalodaiwa Chuo na wanafunzi linalozidi shilingi bilioni 1 jambo ambalo sio kweli katika uhalisia na limepatikana na kuingizwa taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo wa SAGE.

Ukaguzi unashauri SUZA kufanya mambo yafuatayo:-

- Kuongeza udhibiti wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo wa SAGE kwa kuweka mtu atakayekuwa anakagua/kuidhinisha taarifa zote kabla ya kufanyiwa “posting” kwenye kitabu kikuu (General Ledger) ili kuhakikisha kuwa ziko sahihi na kwamba zimekamilika.
- Uongozi wa Chuo kushiriki katika kupitia na kukagua taarifa mbali mbali kupitia ripoti za mapato za “General Ledger” zinazotoka kwenye mfumo wa SAGE kila mwisho wa mwezi ili kuelewa ukubwa wa tatizo na kushiriki katika utatuzi wake kwa wakati.
- Kufanya zoezi la kusafisha taarifa zote zilizowahi kuingizwa kwenye mfumo wa SAGE ili kupata picha halisi ya mapato na matumizi ya Chuo kwa ajili ya maamuzi sahihi ya uongozi.
- Kupeleka mfumo wa SAGE kwenye matawi yote ya SUZA na kutoa mafunzo stahiki kwa watumiaji wa mfumo mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba mfumo unatumika ipasavyo.

**Majibu ya Uongozi wa Chuo**

SUZA unachukua ushauri wote uliotolewa, ikiwamo zoezi la kusogezwa SAGE kwenye matawi ya SUZA, pamoja na kukamilisha zoezi la “segragation of duties”.

SUZA tayari imeufanyia kazi ushauri wa mkaguzi kwa kuweka mtu anayeidhinisha taarifa kabla ya kufanyiwa “posting” katika General Ledger. Hatua hii imechukuliwa kwa dokezo la tarehe 22/01/2024 kutoka kwa Mkurugenzi fedha kwenda kwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Utawala.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa hoja hii imefanyiwa kazi ipasavyo ambapo tayari Chuo kimeshamuweka mtu maalum kushughulikia taarifa hizo kabla ya kurikodiwa kwenye kitabu kikuu cha kwenye mfumo wa SAGE (General Ledger). Hivyo, Kamati imeridhika na hatua zilizochukuliwa na kuiondoa hoja hiyo.

## Hoja nambari 9.4.1.10: Udhaifu wa ulinzi na Kutumia programu za bure kwenye vifaa vya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kuwa Kompyuta nyingi za Chuo zimewekewa programu za bure ambazo sio rasmi kama vile programu za kuzuia virusi (anti-viruses) na programu za "Microsoft Office" na baadhi ya Kompyuta hazina kabisa programu za kuzuia virusi kinyume na kifungu namba 4.10.1.2(b) cha Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2013 kinachoelezea kwamba taasisi zote za Umma zitatumia programu zilizolipiwa leseni kwa kumiliki au za wazi.

Aidha, kwa upande wa ulinzi wa vifaa vya TEHAMA ukaguzi ulibaini kwamba baadhi ya vifaa vya Chuo havina ulinzi dhidi ya athari zinazotokana na umeme (UPS) hali ambayo inaweza kupelekea uharibifu mkubwa kwenye vifaa vyenye thamani kubwa na kusababisha hasara kwa Serikali.

Kuhatarisha usalama wa taarifa za taasisi kwa kutumia programu za bure zenye udhaifu wa kiusalama na zinazoweza kuwa na madhara na kuleta athari kwenye mifumo ikiwa ni pamoja na kuvujisha au kuharibu taarifa. Aidha, hali hii inaashiria udhaifu mkubwa wa usimamizi na ufuatiliaji wa Kitengo cha TEHAMA katika vitendea kazi vya Afisi kwa ujumla.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Chuo kutatua changamoto hizi mara moja kwani zinahatarisha usalama wa vifaa vya TEHAMA na taarifa zilizomo kwenye vifaa husika.

### Majibu ya Uongozi wa Chuo

Chuo tayari kimeshafanya manunuzi ya programu "genuine" za Microsoft Office na Windows. Changamoto za manunuzi kupitia kwenye mfumo zimecheleweshа upatikanaji wa programu hizo. Pia Chuo kitaendelea kuwa na mpango wa manunuzi wa "genuine software" katika kila bajeti zake za fedha.

Mzabuni wa vifaa hivyo vya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ameanza kuviwasilisha SUZA na vinategemewa kufungwa sehemu tofauti za kampasi zenye uhitaji mkubwa wa vifaa hivyo. kwa barua kumb. Namba AH.129/365/01/99 ya tarehe

14/06/2023 kutoka SUZA. Zabuni ya vifaa tofauti vya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ipo katika mfumo wa manunuzi wa Serekali kwenye hatua za kumchagua mzabuni ili kuweza kutatua changamoto hivyo. Kupitia mradi wa HEET, mzabuni ameshapatikana na tayari yuko katika hatua ya kukabidhi vifaa hivyo.

#### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na juhudi ambazo uongozi wa Chuo umeweza kuzichukua lakini Kamati haikuweza kuthibitisha upatikanaji wa programu za kuzuia virusi (anti-viruses), programu za "Microsoft Office" pamoja na UPS. Kwa msingi huo, bado hoja hii inahitaji kufuatiliwa zaidi katika kazi zijazo za Kamati, hivyo, hoja hii inaendelea kubakia.

#### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa SUZA uhakikishe unaharakisha upatikanaji wa programu na vifaa vya 'computer' hivyo ili kuviweka salama kimatumizi vifaa hivyo vya TEHAMA.

### Hoja nambari 9.4.1.11: Kukosekana kwa Daftari la kurikodi mali za kudumu (Asset Register) za Chuo kwenye mfumo wa Sage.

Ukaguzi ulibaini kwamba SUZA haijaingiza kwenye mfumo wa SAGE "Asset register" pamoja na ukweli kwamba SAGE ina uwezo wa kupokea daftari hilo. Hali inayochangia matumizi madogo na hafifu ya mfumo husika na kuikosesha Serikalikupata tija na ufanisi kwenye usimamizi wa Mali za kudumu kupitia mfumo huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa SUZA kuweka mpango na kuutekeleza kwa kuingiza mali zote za kudumu kwenye mfumo wa SAGE ili kurahisisha kazi za Wahasibu kwenye kuandaa hesabu za kila mwaka na kuwa na udhibiti imara wamali za Serikali.

#### Majibu ya Uongozi wa Chuo

Chuo kupitia Wakala Serekali Mtandao Zanzibar (eGAZ) kipo kaika hatua za awali za kuwa na moduli za "asset register" kupitia mfumo utakaotolewa na Wakala wa Serekali Mtandao Zanzibar. Wafanyakazi wa Chuo tayari wanapatiwa mafunzo ya mfumo wa Serekali wa ERMS ambao una moduli ya "Asset Register". Chuo kimeandaa daftari la "manual" la asset register na uhamishaji wa taarifa kutoka katika daftari hilo kwenda katika mfumo wa Serekali wa ERMS utafanyika mfumo huo utakapokamilika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Katika kukamilisha uchunguzi wa hoja, Kamati imebaini kuwa tayari Serikali imeshachukua hatua ya kuanzisha mfumo maalum wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu zote za Serikali ambapo Chuo tayari kimeanza kutumia Mfumo huo mwaka 2022. Hivyo, Kamati imeridhika na majibu ya hoja hiyo na kuiondoa.

## Hoja nambari 9.4.1.12: Mapungufu yaliyobainika katika mfumo wa OSIM

**a. "Dash board" ya mfumo wa OSIM haitoi taarifa sahihi zilizomo ndani ya mfumo huo kama ilivyokusudiwa. Taarifa za kwenye dashboard zinavyotofautiana na taarifa zilizomo kwenye mfumo wa OSIM.**

Ukaguzi unaushauri uongozi wa SUZA kutatua mapungufu yote yaliyobainika kwenye ukaguzi huo kwa lengo la kuhakikisha tija iliyokusudiwa inapatikana.

**Majibu ya Uongozi wa Chuo**

Chuo kinairi uwepo wa mapungufu hayo na kimepokea ushauri wa ukaguzi kwa kuufanyia kazi. Katika kutafuta njia ya kudumu ya kuondoa changamoto hiyo SUZA tayari imeshatayarisha mfumo wake kwa kutumia wataalamu wa ndani unaopatikana kwa anuani hii: http://suzims.suza.ac.tz/Mfumo huo upo katika hatua za majaribio na mashauriano ya kuunganishwa na mfumo wa Serekali wa ZanMalipo. Mfumo huu tayari umehifadhiwa katika SEVA za chuo kwa majaribio.

**b. Mfumo wa OSIM kuhifadhiwa kwenye Seva za mtoa Huduma nje ya mipaka ya Zanzibar kinyume na Sheria za nchi.**

**Majibu ya Uongozi wa Chuo**

Nakla za mfumo wa OSIM tayari zimehifadhiwa "local" kwenye chumba cha kuhifadhia mifumo Maruhubi. Nakla ya "live" nayo itakuwa hapo hapo Maruhubi mara taratibu za Mkataba zitakapokamilika.

**c. Uwepo na module nyingi ambazo hazitambuliwi na kutotumika na wafanyakaziwa SUZA.**

**Majibu ya Uongozi wa Chuo**

Uwepo wa moduli nyingi kwenye mfumo wa OSIM unatokana na "business process" za SUZA. Kuna moduli za udahili, akaunti za walimu, akaunti za wanafunzi, matokeo, fedha

na nyenginezo. Moduli hizo nyingi zinapaikana kwa utaratibu wa “segragration of duties”. Ukiwa mwalimu utapata moduli zinoendana na shughuli za uwalimu, mwanafunzi, mhasibu, Afisa Udahili, Afisa Mitihani hivyo hivyo.

**d. Kukosekana kwa ruhusa ya kufunguliwa account kwa watumiaji wa mifumo katika Chuo kikuu cha SUZA.**

**Majibu ya Uongozi wa Chuo**

Ruhusa isio rasmi kimaandishi kutoka kwa mkuu wa taasisi husika huwa haiwezi kutolewa. Waombaji ruhusa wengine huomba ruhusa hio kimdomo tu bila kuwa na maandishi rasmi yanayoelezea kazi zao kwenye mfumo. Ruhusa zilizo rasmi zote hutolewa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imezifanyikazi kwa pamoja hoja hizo kwa kubaini kuwa uchunguzi wa mapendekezo yake yanafanana na hoja nambari 9.4.1.8. hivyo Kamati haikuwa na maelezo zaidi.

## Hoja nambari 9.4.1.13: Tovuti ya SUZA kutofanyiwa uboreshwaji kwa wakati

Kifungu cha 4.1.1 cha muongozo wa eGAZ kwenye utengenezaji, uendeshaji na usimamizi wa tovuti za Serikali wa mwaka 2022 umeweka orodha ya taarifa za msingi zinazotakiwa kuwekwa Tovuti ya taasisi za Umma ambapo taarifa hizo ni pamoja na muundo wa taasisi, majukumu, Sera, sheria, ripoti za utendaji kazi wa Taasisi, mipango ya taasisi, miradi, zabuni na huduma zinazotolewa na taasisikwa njia za kielektroniki.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba tovuti ya Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) haifanyiwi maboresho (update) na kusababisha kuwepo kwa taarifa za zamani ambazo haziendani na mazingira ya sasa na kupelekea upotoshaji kwa Umma. Pia, tulibaini kwamba kazi ya kuingiza taarifa kwenye Tovuti inafanywa na AfisaTEHAMA badala ya kufanywa na Afisa uhusiano mwenye jukumu hilo.

Kwa kuwa SUZA ni taasisi ya Elimu ya juu inatazamwa kama kioo kwenye jamii, hivyo uwepo wa taarifa zisizo na uhalisia katika Tovuti ya Chuo unaweza kuleta mtazamo hasi kwa jamii inayohitaji kupata taarifa na huduma zinazotolewa na Chuo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa SUZA kuyafanyia kazi mapungufu yaliyobainika kwenye mapitio ya Tovuti ili kwenda sambamba na matakwa ya miongozo ya Serikali iliyopo na

kuongeza umahiri katika uwasilishaji wa habari.

Aidha, SUZA inashauriwa kuzingatia mgawanyo wa majukumu kwa kuhakikisha kwamba Afisa uhusiano anatekeleza jukumu lake la kuweka taarifa zote muhimu kwenye Tovuti mara kwa mara na kwamba Afisa TEHAMA ahakikishe kwamba Tovuti inafanya kazi kama inavyotakiwa.

### Majibu ya Uongozi wa Chuo

Uongozi wa SUZA tayari umeandaa kikosi kazi kitofanya maboresho makubwa kwenye tovuti ya SUZA. Maboresho hayo yataanza kuonekana kabla ya mwaka mpya wa fedha wa 2023/2024 kuanza. Chuo kimetengeneza tovuti mpya ambayo imefanyiwa maboresho yaliyobainishwa na mkaguzi wakati wa ukaguzi na tayari tovuti hiyo ipo katika hatua za mwisho za uwekaji taarifa za maskuli tofauti kabla ya kuzinduliwa rasmi. Katika kufanikisha kazi hiyo tayari timu ya wataalamu kutoka SUZA wamepewa kazi hiyo. Tayari wataalamu wameshatengeneza Tovuti hiyo mpya ambayo bado haijazinduliwa inapatikana kwa anuani: https://suzademo.suza.ac.tz

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya uongozi wa Chuo kukiri kuhusiana na kupitwa na wakati kwa tovuti yao. Hata hivyo, Kamati imeelezwa kwamba Chuo kimeshachukua hatua ya kuziimarisha taarifa zilizomo katika tovuti hiyo kwa kuweka taarifa zinazoendana na wakati. Kinachofanyika ni kuipeleka katika Kamati yao a uongozi kwa ajili ya kuidhinishwa na kutumika rasmi.

Sambamba na hilo, Kamati ilitaka kujua kwamba katika utengenezaji wa tovuti hiyo umefuta miongozo ya uandaaji, uendeshaji na usimamizi wake kutoka Wakala wa Serikali Mtandao na kuelezwa kwamba hatua zote zilifuatwa. Hata hivyo, Kamati haikuweza kupata kielelezo chochote kuthibitisha ukweli na usahihi wa maelezo hayo na kupelekea hoja hiyo kuendelea kubakia.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Chuo cha SUZA uharakishe hatua zilizobakia za ukamilishaji tovuti yao ili iweze kufanyakazi kulingana na wakati uliopo na wanafunzi pamoja na wananchi wapate taarifa sahihi.

## ZIARA YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSIANA NA UFUATILIAJI WA HOJA NAMBARI 9.4.1.1 JIJINI DAR ES SALAAM

## UTANGULIZI:

Katika kufuatilia hoja za Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2021/2022 inayohusiana na Ukaguzi wa Mifumo, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ilikutana na Watendaji wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) ambapo pamoja na mambo mengine, Kamati kwa pamoja ilijadili hoja nambari 9.4.1.1 inayohusiana na Matumizi hafifu ya Mfumo wa SAGE kwenye kufanya malipo, ambapo SUZA walieleza kwamba tayari kuna hatua wameshazichukua ikiwemo kukutana na watendaji wa Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA), kuwaandikia barua kadhaa pamoja na kukutana na Viongozi wa Serikali kujadili suala la upatikanaji wa 'internet' yenye nguvu, nafuu na rafiki zaidi.

Kamati ya PAC ilibaini kuwa hoja hiyo inahitaji kufuatiliwa zaidi kwa kupata majibu ya upande mwengine wa Kampuni ya 'Tanzania Education Research Network (TERNET) ili iweze kupata ukweli na usahihi wa majibu yaliyotolewa na kuweza kuishauri ipasavyo Serikali.

Kwa msingi huo, Kamati ya PAC ilifanya ziara ya kukutana na Uongozi wa Kampuni ya TERNET, siku ya Jumanne ya tarehe 06/2/2024 katika ukumbi wa Ofisi zao uliopo Chuo Kikuu Dar es Salaam na kufanikiwa kukutana nao na kufanya kikao hicho.

## WASHIRIKI WA ZIARA

Ziara hiyo iliwashirikisha wafuatao:

1. Ujumbe wa Kamati ya PAC ukiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo;
2. Watendaji kutoka Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ukiongozwa na Makamo Mkuu wa Chuo hicho; na
3. Mjumbe kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) ambae ni Ndugu Shekhe Abdalla Ali.

## LENGO LA ZIARA

Ziara hiyo ililenga kwenye mambo yafuatayo:

1. Kuiwezesha Kamati kufahamu ukweli na usahihi wa majibu yaliyowasilishwa na SUZA;
2. Kutambua hatua zilizochukuliwa na TERNENT katika utatuzi wa changamoto iliyopo;
3. Maamuzi ya Kamati katika kadhia hiyo (the way forward);

## UFUNGUZI WA KIKAO

Baada ya kujitambulisha kwa pande zote tatu (Kamati na CAG, Watendaji kutoka SUZA pamoja na Watendaji wa TERNET), Kikao kilifunguliwa saa 3:35 za asubuhi na Mwenyekiti wa Kamati ambae pamoja na maelezo yake mafupi alimruhusu Katibu Mtendaji wa TERNET Dkt. Frank P. Seth kuwasilisha alichokiandaa mbele ya Kamati.

## UWASILISHAJI WA TERNET

Katika uwasilishaji wake, Katibu Mtendaji aligusia mambo yafuatayo;

**Historia ya kuanzishwa kwa Kampuni ya TERNET, majukumu yake pamoja na malengo.**

Kiufupi, TERNET ilianzishwa mwaka 2007 na kupata usajili wake mwaka 2008 ikiwa na jukumu la kurahisisha upatikanaji wa huduma ya 'internet' katika Vyuo Vikuu vya Tanzania na Hospitali ili shughuli za masomo pamoja na utafiti ziweze kufanyika na kuisaidia jamii ya Walimu na Wanafunzi kusomesha na kusoma kwa urahisi hasa ukizingatia utaratibu wa utoaji na upatikanaji elimu wa siku hizi ni tofauti na kipindi cha zamani kwa vile Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa Ulimwengu tulionao ndio nyenzo kuu ya upatikanaji wa elimu usioweza kuepukika.

Kufuatia matumizi sahihi ya TEHAMA kumepelekea kuwepo kwa tofauti kubwa ya matokeo ya elimu katika ya wanafunzi wa Tanzania Bara na Zanzibar.

TERNET ni Taasisi ambayo ina shirikiana na jumuiya tofauti Ulimwenguni zinazohusiana na utoaji wa 'Bandwidth' zikiwemo Ubuntu Alliance, GEANT ambazo nchi kadhaa kubwa Duniani ni wanachama wakiwemo Marekeni, Ufaransa, Holand na Uingereza.

Kwasasa TERNET inatoa huduma zake katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kilimanjaro, Mwanza na Arusha. Aidha, Chuo Kikuu cha Tanzania ambacho kinapatiwa 'bandwidth' hadi 3,400 na Hospitali ya Muhimbili ni wanufaika wao.

Kwa upande wa Zanzibar, TERNET imeshafikisha huduma zake Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kwa kuwapatia MBPs 200 kati ya 500 walizopanga. Aidha, wameanza kufika katika

maeneo ya kisiwa cha Pemba.

### Utaratibu wa Kujiunga na TERNET

Ili mwanachama aweze kujiunga na kupata huduma za TERNET anatakiwa alipe gharama za usajili ambazo ni milioni Moja na Laki Tano (1,500,000). Malipo hayo yatamuwezesha Mwanachama kupata huduma zote zinazotolewa na Taasisi hiyo na kuchangia gharama kidogo kwa baadhi ya huduma.

Aidha, TERNET kwasasa inasambaza huduma zake kuwafikia wateja wake kupitia Makampuni ambayo yamenunua nafasi ya kutumia Mkongo wa Taifa (Fibre). Hivyo Taasisi hiyo huingia makubaliano na Makampuni hayo kwa vile huwa hawatumii nafasi yote walipatiwa.

### Faida ya kujiunga na TERNET

1. Upatikanaji wa ‘internet’ yenye nguvu zaidi kwa bei nafuu;
2. Upatikanaji wa huduma ya Walimu na Wanafunzi kufundisha na kujisomea nje ya maeneo yao ya huduma kwa wepesi zaidi;
3. Upatikanaji wa msaada wa kiufundi katika masuala ya TEHAMA;
4. Upatikanaji wa msaada kwa huduma za ‘e Meeting, e Registry, Webdesign, Student Registration and Management System;
5. Upatikanaji wa huduma kwa gharama ndogo za Eduroam, Free Nuren Services, eduGAIN na Open Science.
6. Kuongeza nguvu ‘speed’ ya mtandao bila ya kuongeza gharama za ununuzi au kubadilisha masharti ya Mkataba husika.

## CHANGAMOTO YA UFIKISHAJI HUDUMA ZANZIBAR

TERNET imekusudia kuletwa huduma ya ‘internet’ ya Bandwidth 1000 Zanzibar lakini kumekuwa na changamoto wanazokabiliana nazo. Miongoni mwa hizo ni pamoja na:

1. TERNET kutopatiwa nafasi ya kutumia Mkonga unaotumilikiwa na Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) licha ya juhudi kadhaa walizochukua kuhakikisha lengo hilo linafanikiwa zikiwemo:

   a) TERNET kuiandikia barua ‘ZICTIA’ bila ya kupatiwa majibu yoyote ambapo tarehe

22 Febuari, 2023 yenye kumbukumbu nambari TERNET/ZICTIA/205/VOL.I/001

b) Taasisi ya TERNET imefanya kikao kazi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na kumueleza faida itakayopatikana iwapo wataruhusiwa kuingiza huduma zao kupitia Mkonga 'free of cherge' lakini hakukuwa na utekelezaji wenye tija.

2. Taasis ya TERNET inaangaliwa na ZICTIA kama ni Taasisi ya kibiashara, Hivyo, wanaitaka ilipe gharama za matumizi ya Mkonga kama zinavyolipia Makampuni ya KibIashara ya Simu wakati kiuhalisia, taasisi ya TERNET imejikita na upelekaji wa huduma wezeshi za elimu na utafiti kwa Vyuo Vikuu na Hospitali.

3. Uwepo wa gharama kubwa za kodi.

4. Uchakavu wa Miundombinu katika Taasisi zinazopelekewa huduma.

5. Uhaba wa Dola.

## MICHANGO YA WAJUMBE

Waheshimiwa Wajumbe walitaka kujua sababu ya ZICTIA kukataa kuiruhusu Taasisi hiyo kutumia Mkonga wake.

1. Kwa upande wa Tanzania Bara, Taasisi ya TERNET inapeleka vipi huduma zake katika Vyuo na Hospitali.

2. Jee jambo gani ambalo Taasisi ya TERNET inahitaji ili Kamati iweze kuipatia msaada.

Hata hivyo, SUZA wameeleza kwamba bado wanaendelea kutumia Mkonga wa ZICTIA na huku wanatumia kwa kiasi kidogo huduma za TERNET. Aidha, bado gharama za ZUCTIA ni kubwa mno na nguvu ya internet' ni ndogo sana tofauti na matarajio yao wakati ZICTIA inaundwa na wanaingia katika makubaliano nao. Aidha, ZICTIA hawana huduma ambatanishi za kielimu za TEHAMA za Vyuo Vikuu kama walivyo TERNET hasa ukizingatia wao ndio shughuli zao (wameungana na Vyuo Vikuu vingi) na wamejikita katika utoaji wa huduma zaidi lakini ZICTIA wamelenga kufanya biashara kwa faida. Mfano halisi ni kwamba ZICTIA wamekitaka Chuo kilie shilingi milioni Hamsini na Saba (57,000,000) ikiwa ni ada ya usajili wa matumizi ya Mkonga wakati TERNET imetaka walipe milioni Moja na Laki Tano (1,500,000)

Taasisi hiyo imefanikiwa kutoa ufafanuzi kwa Kamati.

## MAPENDEKEZO YA KAMATI YA PAC

Kamati kwa pamoja imeazimia mambo makuu mawili yafuatayo:

1. Kuwasilisha taarifa maalum kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi kuhusiana na kuwepo kwa changamoto ya kukwama kwa Taasisi ya TERNET katika ukamilishaji wa malengo yake kwa kutopatiwa mashirikiano yenye lengo la kujenga Rasilimali Watu (human Resource Capital) ambao ndio viongozi wa kesho kutokana na mtazamo uliopo wa Shirika la Mawasiliano Zanzibar kujikita zaidi katika kupata au kukusanya mapato kuliko kuwezesha Walimu na Wanafunzi wetu kuwa na uweledi mkubwa wa matumizi ya TEHAMA.

2. Kamati kwa kushirikiana na ZICTIA, SUZA na Taasisi ya TERNET kwa pamoja kufanya kikao mbele ya Makamu wa Pili wa Rais ili kufikisha uelewa kwa Serikali na kutiliwa nguvu utekelezaji wa maombi ya Taasisi hiyo. Hili limepangwa kufanyika kwa vile kuna hatua kadhaa ambazo Taasisi hiyo imezichukua ikiwemo kukutana na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi bila ya kuwepo mafanikio yoyote.

## HITIMISHO

Kikao hicho kilifungwa na Mwenyekit wa Kamati ya PAC saa 7:32 mchana na kuazimia kutekeleza kivitendo mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati yake haraka iwezekanavyo watakapofika Zanzibar.

## UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA TAWALA ZA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022

## 6.0 TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ

## 6.1 TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

### Taarifa ya Mapato

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 98,461,575,171 kati ya fedha hizo shilingi 98,378,213,171 ni kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na shilingi 83,362,000 ni kutokana na vyanzo vya ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 39,079,444,918 sawa na asilimia 40 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 31,881,019,184 ni kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 32 ya makadirio na shilingi 7,198,425,734 kutokana na vyanzo vya ndani sawa na asilimia 8635 ya makadirio.

#### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haikupokea majibu kwa hoja hii ya Taarifa ya Mapato kama inavyoelekeza Kanuni ya Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ambapo nyaraka na vielelezo vyote vinatakiwa viwasilishwe mbele ya Kamati siku mbili kabla ya majadiliano. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kwamba Kikosi cha KMKM kinapangiwa mapato makubwa kulingana na uwezo wao wa wa vyanzo vya mapato wanavyovitegemea.

Aidha, Kamati imebaini kwamba katika taarifa za fedha ilizopatiwa, kuna kutofautiana baina ya wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na maafisa wanaohusika na masuala ya fedha wa Kikosi cha KMKM ambapo Ofisi ya Mkaguzi wameona kuna jumla ya Sh 7,198,425,734 ya makusanyo ambapo ni sawa na asilimia 8635 ya makadirio ya Sh 83,362,000, ambapo Kamati imeshtushwa na kupanda kwa ukusanyaji huo. Kamati imegundua kuwa fedha hizo zilitakiwa kuoneshwa mchanganuo wake katika "Financial Statement" ya Kikosi ikiwa Sh 83,362,000 ni mapato yatokanayo na Hazina na Fedha zilizobaki ni mapato mengineyo ili katika ukaguzi, Kikosi kiweze kukaguliwa kwa ufanisi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe inakipangia kikosi cha KMKM makadirio ya mapato yenye uhalisi na vyanzo vyao vya ndani ili kuepusha kujitokeza kuwepo kwa mpishano mkubwa katika asilimia ya makusanyo.

## Taarifa ya Matumizi

Kikosi Maalum cha kuzuia Magendo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 98,461,575,171 kati ya fedha hizo shilingi 30,390,936,400 zilipangwa kutumika kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo na shilingi 68,070,638,771 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimetumia jumla ya shilingi 37,532,738,085 sawa na asilimia 38 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 23,683,256,200 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 77.9 ya makadirio, shilingi 4,217,128,400 ni kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 6.2 ya makadirio, na shilingi 9,632,353,485 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 14.15 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haikupokea majibu ya kwa hoja hii ya Taarifa ya Matumizi kama inavyoelekeza Kanuni ya Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ambapo nyaraka na vielelezo vyote vinatakiwa viwasilishwe mbele ya Kamati siku mbili kabla ya majadiliano. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Fungu la Mshahara limeingiziwa fedha sawa na Asilimia 77.9 ya mshahara wa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kulikotokana na kuondoshwa kwa posho na baadhi ya Wapiganaji hao kustaafu. Halkadhalika, Kamati imepokea ripoti kwamba Kikosi cha KMKM wamepokea jumla ya asilimia 20.35 ya fedha za makadirio kwa ajili ya matumizi mengineyo pamoja na matumizi ya miradi ya maendeleo.

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha za matumizi mengineyo (OC) pamoja na za miradi ya maendeleo, Kikosi kimekosa kufanya kazi zake za kupiga doria za kuzuia magendo kwa ufanisi. Kamati imeelezwa kwamba Kikosi cha KMKM mpaka sasa bado kinapokea makadirio ya fedha za mafuta sawa na miaka mitatu iliyopita, jambo ambalo linapunguza utendaji kazi ukizingatia mafuta kwa miaka ya karibuni yamepanda kwa takribani shilingi 1000 kwa lita moja.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Imefikia muda kwasasa, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kukipatia KMKM fedha kwa ajili

kufanya doria zao paoja na shughuli za uokozi zinazotokana na matukio mbali mbali baharini.

## Hoja nambari 6.1.1.1: Kutoandaliwa kwa Mapitio ya Mpango wa Matumizi ya kipindi cha kati

Kanuni ya 15(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021, inaeleza kwamba "Afisa Masuuli wa kila Taasisi za Bajeti atatayarisha Mpango wa Matumizi ya Kipindi cha Kati (Updated Medium Term Expenditure Plan) kwa mpangilio ulioainishwa katika miongozo ya uandaaji wa bajeti na kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali."

Ukaguzi umeshindwa kupata uthibitisho wa kuandaliwa na kuwasilishwa Mapitio ya Mpango wa Matumizi ya Kipindi cha Kati kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, ikiwa ndio taarifa muhimu katika utaarishaji wa bajeti ya Serikali.

Kufanya hivyo kunapelekea kufanyika kwa matumizi mengi nje ya bajeti, aidha ni kwenda kinyume na kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma iliyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM kuhakikisha unasimamia utekelezaji wa Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### Majibu ya Uongozi wa KMKM

Uongozi wa KMKM umeshachukua hatua stahiki za kuhakikisha kuwa Kikosi kinaendelea na utaratibu wa kuandaa Mapitio ya Mpango wa Matumizi ya kipindi cha kati (updated Medium Term Expenditure Plan) pamoja na kuhakikisha kuwa matumizi yote yanafanyika kwa mujibu wa mpango kazi wa kipindi husika. Suala hili lilikuja kama ushauri na Kikosi kueleza kuwa limeshafanyiwa kazi kwa mwaka wa fedha 2022-2023 na 2023-2024.

Taarifa hizo zimeambatanishwa pamoja na majibu haya kwa uthibitisho.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Kikosi cha KMKM kulijitokeza kasoro ya kutoandaliwa kwa Mapitio ya Mpango wa Matumizi ya kipindi cha kati. Hata hivyo, Kikosi kimechukua juhudi kurekebisha kasoro hiyo na Kamati imejiridhisha kwamba kwasasa wanaendelea na uandaaji wa mapitio hayo kama inavyotaka Sheria. Kwa msingi huo, Kamati imeiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 6.1.1.2: Kutokuidhinishwa Kwa Mkataba na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kanuni nambari 47(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2020 inaeleza kwamba "Makubaliano yoyote yanayohusiana na manunuzi ambayo thamani yake ipo juu ya thamani ndogo kwa mujibu wa utaratibu wa manunuzi yataidhinishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa na wahusika".

Tarehe 25 Novemba, 2021, KMKM ilisaini mkataba na Kampuni ya M/S Mosal Trading Enterprises kwa ajili ya usambazaji wa huduma ya chakula cha wapiganaji kwa Unguja na Pemba. Ukaguzi umefanya uhakiki wa kumbukumbu za manunuzi, na kubaini kuwa hakukuwa na kumbukumbu inayoonyesha kuwa Makubaliano hayo yameidhinishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Utekelezaji wa mkataba bila kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali unaweza kuleta hatari ya kutoelewa masharti ya mkataba, aidha kunaweza kuingiza serikali katika hasara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM kuhakikisha kuwa Mikataba yote ya manunuzi inawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa ili kupunguza hatari ya kuingia katika mikataba yenye kuikandamiza Serikali.

### Majibu ya Uongozi wa KMKM

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) ni miongoni mwa Taasisi za Serikali ambayo inaitumia ipasavyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika masuala mbali mbali ya kisheria.

Kuhusu suala la mkataba kutokupelekwa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni kwamba KMKM ilipokea maelekezo kupitia barua ya tarehe 30 Disemba 2020 yenye kumbukumbu WN- OR/TMIM/MW.1/VOL.I/22 kutoka kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ yenye kuelekeza kwamba rasimu ya mikataba ipelekwe Wizarani kwa ajili ya kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu, ambapo KMKM ilitekeleza ipasavyo maelekezo hayo kwa kuwasilisha rasimu hiyo ya mkataba kupitia barua ya Tarehe 30 Agosti 2021 yenye kumbukumbu Namb KM/HQ/0IH/158B/2021.

Hivyo, Uongozi wa KMKM kwa kuendeleza mashirikiano na uhusiano na Uongozi ngazi ya Wizara ulifanya mawasiliano ya maandishi na kupata ruhusa ya kuendelea na mchakato wa zabuni ya ununuzi wa chakula kutoka kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia barua ya Tarehe 11

Novemba 2021 yenye kumbukumbu Namb. WN-OR/TMSMIM/C.I/VOL.XII/32. Msingi wa maombi hayo na ruhusa hiyo ni kuwaondolea usumbufu maafisa na wapiganaji wa KMKM wakiwa katika majukumu yao ya kazi.

Aidha wakaguzi walipewa maelezo na ufafanuzi wa kutosha pamoja na kuoneshwa nyaraka zote hizo ambazo waliziomba na kujiridhisha.

Barua zote zinazohusika zimeambatanishwa katika majibu haya.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuifutatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba Wizara inayohusiana na Vikosi vya SMZ imetoa maelezo kwamba Vikosi vyote vya SMZ vinatakiwa kupeleka Mikataba yao Wizarani ili Mikataba hiyo ipelekwe kwa Mwanasheria Mkuu kupitia Wizara. Aidha, Kikosi cha KMKM kimechukua hatua ya kuupeleka Mkataba huo Wizarani na baadae kurudushiwa majibu kutoka Wizarani ya kuruhusu kuendelea kwa taratibu za kufunga mkataba huo wa Usambazaji wa chakula kwa wapiganaji wa Kikosi cha KMKM.

idha, Kamati ilitaka kupatiwa barua kutoka Wizarani iliyokwenda Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na ushauri ambao Afisi hiyo imeutoa kwa KMKM ambapo Watendaji wa Wizara walishindwa kuwasilisha barua hizo (vithibitisho) na Kamati kubaini kwamba ni kweli Mkataba huo haukuthibitishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kupelekea kukosa uhalali wa utekelezaji wake.

Hata hivyo, kwasasa KMKM imerekebisha kasoro hiyo kwa mikataba wanayoingia na Wakandarasi tofauti. Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhika na majibu ya KMKM na kuiondosha hoja hiyo kwa vile tayari marekebisho yamefanyika.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. KMKM wahakikishe wanafuatilia Wazarani kwao barua wanazozipeleka za maombi ya kupatiwa ushauri wa kisheria kwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.
2. Wizara ihakikishe inaiandikia barua ya kupatiwa ushauri wa kisheria Vikosi haraka iwezekanavyo baada ya kupokea maombi hayo.
3. Wizara ifanye mrejesho wa majibu ya barua ya ushauri wa kisheria uliowasilishwa kwako kwa niaba ya Kikosi husika ili haraka Kikosi kichukue hatua stahiki.

## Hoja nambari 6.1.1.3: Malipo yaliyofanyika kabla ya kusainiwa Mkataba shilingi 131,840,600

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 ukaguzi umepitia nyaraka za uhasibu na taarifa mbali mbali za manunuzi ambapo imebainika mnamo tarehe 25 Novemba, 2021, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kilisaini hati ya makubailano na mtoa huduma M/S Mosal Trading Enterprises kwa thamani ya shilingi 808,149,000 kwa ajili ya usambazaji wa Chakula cha Wapiganaji. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa malipo yenye thamani ya shilingi 131,840,600 kabla ya kusainiwa kwa mkataba wa kutoa huduma.

Kufanya malipo kabla ya kusainiwa kwa mkataba kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za Serikali pindipo Mtoa huduma atakaposhindwa kutekeleza makubaliano ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM kuhakikisha malipo yote ya fedha yanafuata utaratibu na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 44: Malipo yaliyolipwa kabla ya kusainiwa kwa mkataba.**

| Tarehe | Aliyelipwa | Nambari ya hati | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 20/06/2021 | Mosal Trading Enterprise | D04PV2100000493 | 40,000,000.00 |
| 27/07/2021 | | D04PV2100000016 | 16,993,000.00 |
| 03/09/2021 | | D04PV2100000048 | 37,071,000.00 |
| 17/09/2021 | | D04PV2100000059 | 37,776,600.00 |
| **Jumla** | | | **131,840,600.00** |

### Majibu ya Uongozi wa KMKM

Kikosi cha KMKM katika kutekeleza majukumu ya ulinzi na usalama wa mipaka ya bahari yetu, mfumo wake wa ulinzi umegawika katika masaa 24, wiki (siku 7) na kubaki kambini muda wote kama makaazi kwa upande wa Kambi za Pemba.

Makundi yote matatu (3) yanahitaji kupatiwa huduma ya chakula kwa kila siku ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya ulinzi bila ya usumbufu na kushindwa

kupatikana kwa huduma hiyo ni kozorotesha utendaji kazi.

Wakati Uongozi wa Commodore Azana Hassan Msingiri unaingia madarakani kulikuwa hakuna mzabuni wa usambazaji wa chakula kwa wapiganaji na kusababisha usumbufu mkubwa. Msingi wa tatizo hilo ni mkataba wa usambazaji wa chakula uliokuwepo kuvunjwa na uongozi uliopita hali ambayo ilisababisha usumbufu mkubwa kwa Maafisa na Wapiganaji wa kikosi cha KMKM.

Hivyo kikosi kikalazimika kununua chakula katika kipindi hicho cha mpito ili kunusuru hali iliyokuwepo na kuandaa makubaliano madogo kwa kipindi hicho ili kuondoa tatizo hilo ambalo lilikuwa linakwaza utendaji hasa upande wa Pemba na Operesheni za baharini. Aidha wakati hayo yanaedelea, mchakato wa kumpata mzabuni kwa mujibu wa taratibu za kisheria ulikuwa unaendelea na wakaguzi walipewa maelezo ya kutosha juu ya mchakato huo sambamba na kuoneshwa nyaraka mbali mbali ikiwemo nyaraka zilizotajwa katika hoja 6.1.1.2 wakaonyeshwa lakini hawakuridhika na ufafanuzi uliotolewa pamoja na kutozingatia mazingira na mahitaji ya wakati huo.

Hivyo baada ya kukamilika rasimu ya mkataba iliandaliwa na kupelekwa wizarani kwa ajili ya kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu kupitia barua ya Tarehe 30 Agosti 2021 yenye kumbukumbu Namb KM/HQ/0IH/158B/2021 hali ambayo inathibitisha kuwa Kikosi kilikuwa na dhamira njema ya kuheshimu na kutekeleza sheria za nchi sambamba na kuangalia kwa uzito unaostahiki ustawi wa maofisa na wapiganaji.

Suala hili lililenga zaidi kuboresha mazingira ya ustawi wa maofisa na wapiganaji na mategemeo ya Kikosi ni kwamba suala hilo lilipaswa kupewa uzito unaostahiki kwa kuthamini juhudi zilizokuwa zinafanywa na kikosi.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Kikosi cha KMKM kuwa na nia njema ya kuhakikisha wapiganaji wake wanapata haki zao za Msingi za kupatiwa chakula kwa muda ambao watakuwa katika maeneo yao ya kazi, Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwa Kikosi cha KMKM kilishindwa kufuata taratibu za Sheria na Kanuni za Fedha ambazo zinaelekeza wazi kwamba malipo yafanyike baada ya kusainiwa kwa mkataba wa kutoahuduma.

Kwa msingi huo, Kamati haikuridhishwa na majibu ya kikosi na hoja hii inabakia kwa hatua za ufuatiliaji wake katika kipindi chengine.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati inashauri Kikosi cha KMKM kuhakikisha muda wote wanafuata Taratibu, Kanuni na Sheria hususani zinazohusiana na masuala ya Fedha na Manunuzi, na ikitokea kuna

jambo la dharura, basi dharura hiyo ifuate miongozo ambayo itapelekea kutovunjwa kwa Sheria za nchi

### Hoja nambari 6.1.1.4: Kukosekana kwa ushahidi wa kuidhinishwa kwa nyongeza ya shilingi 982,047,375 katika zabuni ya ufungaji wa Decompretion Chamber

Kanuni nambari 125 (1) (2) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2020 inaeleza kwamba kutakuwa na makadirio ya thamani ambayo ni misingi ya kazi za ununuzi; na zabuni yoyote iliyotathiminiwa na iko juu au chini ya makadirio ya thamani ya manunuzi, kadiri itakavyokuwa, haitaidhinishwa isipokuwa ikiwa inakidhi masharti kama ilivyoainishwa katika miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar.

Aidha, kifungu nambari 43(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali ya Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Ununuzi au uondoshaji wa mali za umma utaanzishwa au kuendelea baada ya kuthibitishwa kwamba fedha zote kwa kiwango kamili na kwa muda wote zitakuwepo wakati wa kuingia mkataba".

Ukaguzi umebaini kwamba KMKM ilitangaza zabuni ya ufungaji wa Decompression Chamber kwa njia ya ushindani usio wa wazi ikiwa na makadirio ya shilingi 1,200,000,000. Nyaraka za wazabuni watatu zilifunguliwa tarehe 21 Oktoba 2021 na kufanyiwa tathmini. Mnamo tarehe 17 Disemba 2021, KMKM ilisaini mkataba na M/S Rom Solution Limited wa pendekezo la usambazaji na ufungaji wa Decompression Chamber kwa shilingi 2,182,047,375 kuwa ndie mzabuni aliyekuwa na kiwango cha chini jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa ongezeko la shilingi 982,047,375 sawa na asilimia 82 ukilinganisha na makadirio ya awali.

Kwa mujibu wa taratibu za manunuzi zabuni hiyo haikupaswa kuidhinishwa, aidha ilipaswa kuombewa bajeti ya ziada kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au kuombewa ruhusa ya kuendelea na utekelezaji wa zabuni hiyo jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika hatukuweza Kupatiwa nyaraka iliyotowa idhini ya utekelezaji wa zabuni iliyopindukia bajeti iliyoidhinishwa awali.

Kufanya matumizi ya fedha zilizo nje ya bajeti kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za Umma kunakotokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kinyume na mpango wa Ununuzi na hatimae matumizi mabaya ya fedha za Umma hayatoweza kuepukika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM kuhakikisha matumizi yote ya fedha yaliyopindukia makadirio ya bajeti yanapata ruhusa kutoka kwa mlipaji mkuu wa Serikali

hata hivyo ni vyema kufanya tathmini ya kina kabla ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuepuka kuitia hasara Serikali kwa kutekeleza Miradi isiyokuwa na tija.

### Majibu ya Uongozi wa KMKM

Kikosi cha KMKM miongoni mwa miradi yake ni Mradi wa Kimkakati wa Serikali wa Uzamiaji na Uokozi ambao umetengewa na kuidhinishiwa fungu lake maalum ambalo linajumuisha Ujenzi wa Chelezo, Ununuzi wa Boti, Ununuzi wa Vifaa vya Uzamiaji na Uokozi, Ununuzi wa Rada na Decompresheni Chember. Kikosi katika utekelezaji wa mradi huo hakuna fedha iliyotumika kutoka nje ya bajeti ya mradi husika au kutumika bila ya kupata idhini ya mamlaka husika na kama haitoshi utaratibu wa kumpata mzabuni umefuatwa ipasavyo.

Aidha Kikosi baada ya kukamilika kwa taratibu za kumpata mzabuni wa Decompression Chamber kiliendelea na hatua za maombi na malipo ya fedha kwa mzabuni. Fedha hizo zimelipwa kwa bajeti mbili tofauti, bajeti ya mwaka 2021/2022 ililipwa asilimia 20% na bajeti ya mwaka 2022/2023 ililipwa 80% kutokana na hali ya upatikanaji wa fedha. Aidha hakuna fedha iliyolipwa bila ya kufanyika maombi, malipo yaliyopindukia kima kilichopo katika mkataba au kinyume na utaratibu uliopitishwa katika zabuni husika.

Pia Fedha hizo zimetoka katika fungu la Vituo vya uzamiaji na uokozi ambapo kuliizinishiwa jumla ya shilingi 2,100,000,000/- kama ni malipo ya vituo vya uzamiaji na uokozi. Kikosi cha KMKM kabla ya matumizi ya fedha za mradi huo kilifuata utaraatibu wa maombi ya fedha hizo kwa kupitia barua tofauti ikiwemo barua ya tarehe 10 January 2022 yenye kumbukumbu namb. KM/HQ/01C/02/2022 na barua ya tarehe 30 Mei 2022 yenye kumbukumbu namb. KM/HQ/01C/80/2022.

Hivyo basi bajeti hiyo ni sahihi na matumizi yake ni sahihi kwani yanatokana na mradi husika wa Uzamiaji na uokozi ambao umeanza kwa mwaka wa fedha 2019/ 2020 na ulitarajiwa kumalizika 2024/2025. Hata hivyo matumizi hayo yametokana na mkataba halali baina ya KMKM na ROM SOLUTION uliothibitishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya kikao halali cha bodi ya zabuni kushinda mzabuni huyo.

Kwa ufafanuzi zaidi, ni kwamba mzabuni huyo ndiye mwenye kiwango kidogo cha fedha kulingana na wazabuni wengine ambao waliweka kiwango cha juu kabisa, hata hivyo ongezeko la fedha hizo zilitoka kwenye fungu husika ambalo lilikuwa na fedha za kutosha na kwa kuwa maombi ya fedha hizo yalikuwa tayari yameshafanyika kabla na kuridhiwa na mamlaka husika, ilikuwa hakuna haja ya kuandika maombi mengine ya kuomba fedha hizo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na hoja ya Mkaguzi na kubaini kwamba utaratibu husika wa kuongeza fedha katika zabuni ya ufungaji wa 'decompretion chamber' haukufuatwa ipasavyo. Kamati imebaini kwamba ili matumizi hayo ya nyongeza ya Shilingi 982,047,375 yawe halali, Kikosi cha KMKM kilitakiwa kipate kibali kutoka kwa Kamishna wa Bajeti na baadae kupeleka marekebisho hayo kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, na hatima ndio waendelee na Zabuni hiyo. Kwa msingi huo, hoja ya Mkaguzi inaendelea kubakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inakishauri Kikosi cha KMKM kuhakikisha kinafuata taratibu zote zinazohusiana na masuala ya Fedha na Manunuzi ili kuepusha kuwepo na wasiwasi wa matumizi mabaya ya fedha za Umma.

## Hoja nambari 6.1.1.5: Hasara itokanayo na ukiukwaji wa taratibu za utoaji wa zabuni shilingi 1,004,077,219

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 ukaguzi umefanya mapitio ya nyaraka za zabuni pamoja na Ripoti ya Tathmini iliyofanywa na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo na kubaini uwepo wa wazabuni wawili (2) waliowasilisha zabuni ya kazi ya usambazaji wa vifaa vya ujenzi ambapo mambo yafuatayo yamebainika:-

a) Msambazaji M/S Mosal Trading alibainika kuwasilisha zabuni yenye thamani ya shilingi 4,119,128,276 ambapo alikuwa ni mshindi katika zabuni hiyo.

b) Msambazaji M/S United Traders aliwasilisha zabuni kwa thamani ya bei ya juu ya shilingi 5,123,205,495 kukiwa na tofauti ya shilingi 1,004,077,219 ukilinganisha na zabuni ya Msambazaji M/S Mosal Trading.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa udanganyifu wa kumuondoa Msambazaji M/S Mosal Trading na kumtunuku zabuni hiyo M/S United Traders kwa sababu zilizotumika ya kwamba M/S Mosal Trading kutokuwa na ghala la kuhifadhia saruji na nondo pamoja na kutokuwa na vifaa na sehemu ya kufyatulia matofali.

Ukaguzi umebaini sababu zilizotolewa hazikuwa na mashiko ya kisheria hasa ukizingatia ya kwamba vigezo hivyo vyote vilivyotumika kumuondoa M/S Mosal Trading havikuainishwa kwenye nyaraka ya zabuni ambapo nyaraka hiyo ya zabuni ilieleza kwenye kifungu cha 35.3 ya kwamba mambo ambayo hayajajumuishwa katika hati ya zabuni hayatatumika katika tathmini ya uhakiki wa wazabuni. Kufanya hivyo ni Kwenda

kinyume na Kanuni ya 122(1)(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2020.

Kutokana na uwepo wa dosari hiyo ukaguzi umetathmini kitendo cha kumbariki M/S United Traders zabuni kwa thamani ya juu ya ziada ya shilingi 1,004,077,219 ni kuisababishia hasara Serikali na kuibebesha mzigo wa malipo yasiyokuwa na ulazima.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuhakikisha hatua za kinidhamu zinachukuliwa dhidi ya wale wote waliokosa maadili katika usimamizi wa majukumu yao na kupelekea kuitia hasara Serikali ikiwemo kurejesha fedha zilizopotea. Mchanganuo wa ushindani wa zabuni hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 45: Bei iliyosomwa kwenye ufunguzi kwa TZS Pamoja na VAT**

| Jina la Mzabuni | Loti 1 | Loti 2 | Loti 3 | Loti 4 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| United Ram | 0 | 849,845,400 | 0 | 0 | 0 |
| Mosal Trading | 1,433,470,910 | 428,898,712 | 941,924,480 | 1,314,834,174 | 4,119,128,276 |
| Unite Trader | 1,760,004,850 | 576,354,700 | 1,163,128,745 | 1,623,717,200 | 5,123,205,495 |
| Zan Forwards | 1,483,045,589 | 0 | 0 | 0 | 0 |

**Majibu ya Uongozi wa KMKM**

Kikosi cha KMKM katika utekelezaji wa miradi mbali mbali kina angalia zaidi uwezo wa mzabuni katika kufanikisha mradi husika ndani ya muda na kwa kiwango cha ubora unaohitajika.

Kwa upande wa mradi wa mahanga ni kwamba nyaraka ya zabuni (Tender document)

husika kipengele cha **Post Qualification** kimeandikwa, hivyo kamati ya tathmini ikamfanyia post qualification mzabuni M/S Mosal Enterprises na kujiridhisha kuwa hana uwezo wa kuendesha zabuni hiyo, hivyo Kamati ya Tathmini imezingatia maeneo ya msingi ya zabuni husika kabla ya kumuondoa.

Aidha kumbukumbu ziaonesha kuwa Mzabuni huyo alipewa kazi ya usambazaji wa vifaa kwa ujenzi wa hanga la Wete Pemba wenye thamani ya shilingi 350,000,000 ambapo kazi hiyo ilimshinda kwa kutegemea alipwe ndipo awasilishe vifaa. Kikosi kiliamua kuachana naye na kutafuta mzabuni mwengine mwenye uwezo ili Mradi uweze kukamilika kwa wakati husika ambapo barua ya tarehe 13/12/2021 yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01E/213C/2021 inahusika.

Pia kigezo cha bei ndogo hakimfanyi mzabuni kuwa na uhalali wa kushinda zabuni ikiwa amekosa vigezo vya kimsingi vya kutunukiwa zabuni husika kwa mujibu wa Kanuni 127(a) cha Kanuni ya Manunuzi ya mwaka 2020. Mzabuni M/S Mosal Enterprises baada ya kufanyiwa tathmini alithibitika kuwa ana mapungufu yafuatayo:-

- Kutokuwa na ghala la kuhifadhia saruji.
- Kutokuwa na ghala la kuhifadhia nondo.
- Kutokuwa na sehemu ya kuzalishia matofali.
- Kutokuwa na vifaa vya kuzalishia matofali.

Pamoja na hayo kikosi kilibaini kuwa mzabuni huyo ni wakala tu na hana uwezo wa kifedha wa kusambaza vifaa vya kukamilisha Mradi mkubwa wa ujenzi.

Kwa hivyo Kikosi kiliona kuingia makubaliano na mzabuni huyo ambaye ameshashindwa kufanya kazi ya usambazaji wa vifaa vya ujenzi kwa jengo moja tu la hanga ingeliweza kupelekea kushindwa utekelezaji wa mradi mkubwa uliojumuisha ofisi KMKM Unguja Ukuu, Ofisi na Hanga KMKM Kibwengo, Ofisi KMKM Wete Pemba na Ujenzi kambi (hanga, hospitali, nyumba ya mkuu wa kambi na kibanda cha walinzi) KMKM Gando Pemba.

Mzabuni aliyepewa zabuni hiyo amethibitisha kwa vitendo kuwa ana uwezo wa utekelezaji wa mradi huo lakini mzabuni M/S Mosal Enterprises kama angelipewa zabuni hiyo leo hii tungelikuwa tunaongelea suala la kupewa zabuni ya usambazaji wa vifaa vya ujenzi kwa mzabuni asiyekuwa na uwezo na kupelekea kukwama kwa mradi huo kama ilivyotokea kwa miradi mbali mbali ya Serikali kushindwa kukamilika kutokana na uwezo dhaifu wa wazabuni.

Suala hili hata Mheshimiwa Rais Dr Hussein Ali Mwinyi ameelekeza kupokonywa kwa baadhi ya wazabuni kutokana na kuzorota kwa ujenzi katika miradi hiyo.

Aidha Kikosi cha KMKM hakina nia ovu na mzabuni M/S Mosal Enterprises kwa sababu mzabuni huyo ndiye anaendelea kutoa huduma ya usambazaji wa Chakula katika Kikosi baada ya kujiridhisha na uwezo wake kwa upande huo, lakini kwa upande wa ujenzi Kikosi kimejiridhisha kuwa hakuwa na uwezo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba Mzabuni M/S Mosal Trading alishindwa Zabuni hiyo licha ya kuwa na Bei ndogo kuzidi M/S United Traders kutokana na uhalisia kwamba Mzabuni M/S Mosal alikosa sifa za kushinda Zabuni hiyo baada ya kufanyiwa "due Deligence" na kubainika kwamba hakuwa na uwezo wa kutekeleza mradi huo. Kamati imebaini udhaifu uliopelekea kwa hoja hii kuwepo ni kutokana na Kikosi cha KMKM kilishindwa kuandika katika ripoti yake ya Kamati ya tathimini ya Zabuni hiyo sababu zilizopelekea kwa Mzabuni huyo kukosa Zabuni hiyo.

Aidha, katika kipengele cha Zabuni kinachojulikana kama "post qualification", Kikosi kilifuatilia uwezo wa Mzabuni huyo kwenye eneo la kazi "site meeting" na kujiridhisha kwamba Mzabuni huyo asingeweza kuutekeleza mradi huo na hakukuwa hata na ghala la kuhifadhia vifaa mbali mbali. Licha ya kuwa na fedha ndogo za thamani kuliko M/S United Traders, Kamati, Kimsingi imekubaliana na Majibu ya Kikosi cha KMKM pamoja na maelezo yao waliyoipatia Kamati na kujiridhisha kuiondoa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

KMKM ihakikishe kwamba Ripoti ya Kamati ya Tathmini inainisha kiuwazi sababu zote zinazopelekea Mzabuni kukosesa ushindi wa Zabuni ili kuondoa dhana ya kuwepo upendeleo kwa Wazabuni wengine.

## Hoja nambari 6.1.1.6: Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu shillingi 340,000,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 9 cha Mkataba kinataka kufanyika kwa tathmini ya pamoja baina ya Muajiri na Muajiriwa ya thamani ya Ujenzi kwa kutumia nyaraka zilizotumika katika manunuzi ya vifaa vya Ujenzi.

Aidha, kifungu nambari 4.3 cha Mkataba kinamtaka Muajiriwa kuwasilisha kwa Muajiri gharama za Ujenzi wa Ukuta, Maduka, Afisi, Vyoo pamoja na Mtaro alizotumia baada ya kukamilika kwa ujenzi huo.

Ukaguzi umepitia hati za malipo na kubaini kuwepo kwa malipo ya shillingi 340,000,000

ambayo yamelipwa kwa United Ram Construction Company Limited bila ya kuwasilishwa kwa gharama za Ujenzi wa ukuta, Maduka, Afisi, Vyoo na Mtaro pamoja na kufanyika tathmini ya pamoja na kukubaliana juu ya gharama zilizotumika ukilinganisha na thamani halisi ya Ujenzi uliofanyika (Value for Money).

Kutokuwasilishwa kwa gharama za ujenzi kwa mujibu wa makubaliano ya awali kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za Serikali kutokanako kwa kukosekana kuwasilishwa kwa nyaraka zinazothibitisha uhalali wa kufanyika kwa malipo hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuwatumia wataalamu wa Wakala wa Majengo Zanzibar kufanya tathmini na vipimo vya kutambua thamani halisi ya fedha iliyotumika pindipo mzabuni anaposhindwa kuwasilisha tathmini ya matumizi ili kuweza kujua thamani halisi ya fedha iliyotumika kabla ya kuanza kufanya malipo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 46: Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu**

| Hati namba | Ankara/Risiti Namba | Kiasi cha fedha Kilicholipwa (Tshs) | Anayelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 8/03 ya 08/03/2022 | 6251 | 255,000,000 | United Ram Construction Company Ltd | Malipo kwa ajili ya Ujenzi wa Ukuta Kambi ya KMKM Makao Makuu |
| - 23/05/2022 | | 85,000,000 | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Kibweni |
| **Jumla** | | **340,000,000** | | |

Majibu ya Uongozi wa KMKM

Uongozi wa KMKM Awamu ya nane wakati unaingia madarakani ulikutana na chagamoto ya malalamiko ya wananchi juu ya kituo cha daladala kupigwa marufuku kutokana na uwepo wa kambi, kukosekana kwa stara ya kambi kutokana na uzio mbovu, kuingia kwa maji katika majengo ya ndani ya kambi yenye kuhatarisha usalama na uhai wa majengo hayo ikiwemo jengo la Ofisi Kuu.

Kwa dhamira ya kuifanya KMKM kuwa karibu ya jamii na kuwapunguzia masafa ya hospitali wagonjwa wanaoshuka daladala pamoja na kunusuru majengo yaliyokuwa hatarini kuanguka ilionekana kuna haja ya dharura ya kujengwa kwa ukuta pamoja na mtaro wa kupitishia maji. Juhudi hizo zilizaa matunda kwa kujitokeza Mkandarasi Mzalendo ambaye alikuwa tayari kuondoa changamoto hizo kwa kujenga ukuta na mtaro kwa njia ya mkopo hali ambayo imeleta heshima kubwa kwa Kikosi na furaha kwa wananchi baada ya kurejeshwa kwa kituo chao cha daladala.

Uongozi wa KMKM umefanya malipo ya Tzs 340,000,000 kwa mujibu wa mchanganuo wa gharama (BOQ) halisi za malipo ambazo Mjenzi ameziwasilisha Kikosini na kujiridhisha gharama hizo baada ya kupitiwa na wahandisi wa Kikosi cha KMKM. Kufuatia kukamilika kwa hatua hiyo zilianza hatua za maombi ya malipo ya fedha hizo na kufanyika malipo hayo kwa mujibu wa taratibu za malipo.

Pia wakaguzi walishauri kusitisha malipo ya ujenzi huo mpaka ukaguliwe kwa kufanyiwa tathmini na ZBA. Hivyo Kikosi kikachukua hatua za kuwasiliana na ZBA kwa ajili ya tathmini ya ujenzi huo ili kupata gharama sahihi na kuokoa fedha za Serikali. Majibu ya ZBA yanawasilishwa kwa Kamati yako ili Kamati kuona hatua zilizochukuliwa na Kikosi kwa dhamira ya kuhakikisha kuwa taratibu zote zipo sawa.

Matokeo ya malipo hayo ya awali ni kukamilika kwa ujenzi wa ukuta, maduka, afisi, vyoo pamoja na mtaro ambavyo vimeleta stara na heshima kubwa kwa KMKM Makao Makuu. Ujenzi huo ulifanyika kwa njia ya mkopo kwa makubaliano ya kulipana kwa awamu kati ya Kikosi na Mjenzi na kabla utekelezaji wake hatua za tathmini zimeshafanyika.

Hata hivyo njia iliyotumika katika ujenzi huo ni ya dharura (Emergency Procurement) kupitia barua ya tarehe 29 Disemba 2021 yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01C/222/2022 ambayo imeambatanishwa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba tathmini iliyofanywa na ZBA kwa ujumla ilikuwa Shilingi 853,201,215.00 ambapo haikutofautiana sana na tathmini ya Mkandarasi iliyokuwa na jumla ya Shilingi 799,616,505. Kamati imeridhika na Majibu ya KMKM na juhudi zao za kuhakikisha Vikosi hivi vinapata stara na kuleta urahisi kwa wananchi kutumia kituo cha daladala ambacho kabla ya ukuta kujengwa kilizuia kutumiwa kwa sababu za kiusalama.

## Hoja nambari 6.1.1.7: Kutokubainishwa kwa gharama za ujenzi katika mkataba

Kwa mujibu wa kifungu nambari 3.3 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC) kinaeleza kwamba "Muendeshaji wa Maduka atabeba gharama zote za Ujenzi kwa mujibu wa Mkataba na atawasilisha Makisio ya Gharama za Ujenzi (Bill of Quantity) ya miundombinu zinazohitajika kutumika.

Ukaguzi umepitia Mkataba ulioingiwa baina ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo na Bei Poa Limited na kubaini ya kwamba hakukuwekwa wazi kwa gharama za Ujenzi wa Maduka ya KMKM (Special Department Duty Free Shop) ambapo mkataba huo unaruhusu ujenzi kufanywa na Kampuni ya Bei Poa Limited kwa gharama zake na baada ya hapo kuendelea na Mkataba kwa kulipa faida kwa mgawanyo wa asilimia 75 kwa Kampuni ya Bei Poa Limited na asilimia 25 kwa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM).

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokubainishwa kwa gharama halisi itakayotumika katika ujenzi wa maduka pamoja na kujulikana muda wa kulipwa kwa gharama iliyotumika jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa uwepo wa malipo ya ziada ukilinganisha na malipo halisi yaliyotumika kutokana na kutokujulikana kwa gharama za awali zilizotumika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuhakikisha unamtaka Mkandarasi kuwasilisha makisio ya gharama za ujenzi na kuomba ushauri elekezi kwa Wakala wa Majengo kwa ajili ya kuzipitia gharama hizo na kushauri ipasavyo kabla ya kuanza kuchukua hatua ya kugawana faida.

### Majibu ya Uongozi wa KMKM

Ujenzi wa majengo ya Duty Free haukufanywa na Kikosi wala haukutumia fedha za kikosi au Serikali, ujenzi huo umefanywa baina ya taasisi binafsi kwa Taasisi binafsi ambao ni Mkandarasi UNITED RAM na kampuni ya BEI POA LIMITED, hivyo Kikosi hakihusiki katika

mkataba wa ujenzi huo kwa asilimia 100%.

Wakaguzi walioneshwa nyaraka na kupatiwa maelezo ya ziada na kuridhika lakini hoja hiyo imerejeshwa tena wakati ambapo KMKM ni mtu wa tatu (Third Party) katika mkataba wa Ujenzi baina ya BEI POA LIMITED na UNITED RAM CONSTRUCTION CO. LTD.

Majengo hayo kwa mujibu wa mkataba yalikuwa chini ya BEI POA LIMITED na yatamilikiwa na Kikosi baada ya miaka 10. Hata hivyo, kutokana na maelekezo ya Serikali juu ya Duty Free imepelekea makubaliano baina ya KMKM na Bei Poa Limited kuvunjika na jengo hilo limekuwa mali ya KMKM. Hatua za kulikamilisha suala hilo zimeshachukuliwa kwa kuzihusisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na ZBA.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuifuatilia hoja hii hususan kwa kupitia nyaraka zilizoelezwa, Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli KMKM ilikuwa ni mnufaika wa kazi iliyofungwa Mkataba na Kampuni mbili tofauti. Hata hivyo, tayari Serikali imeshalitolea maelekezo suala hilo na yameshafanyiwa kazi na KMKM. Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhika na majibu ya KMKM na kuiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 6.1.1.8: Kukosekana kwa ramani na michoro ya ujenzi wa maduka

Kwa mujibu wa kanuni nambari 43(2) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inaeleza kwamba Kitengo cha Manunuzi kabla ya kualika watoa huduma kinatakiwa kiwasilishe kwa Bodi ya Zabuni (Tender Board) Barua ya Mualiko, nyaraka za manunuzi ambazo zitaambatana na specification, mkataba ambao bado haujakamilika, makisio ya Gharama za Ujenzi (Bill of Quantity), michoro na nyaraka nyenginezo.

Ukaguzi umepitia Mkataba na kubaini kutokuwepo kwa Ramani na Michoro ya Ujenzi wa Maduka jambo ambalo linaweza kusababisha kufanyika kwa Ujenzi uliokuwa haukupangwa kupitia michoro na ramani zilizowekwa, pia kunaweza kusababisha kuwepo kwa hasara kwa Kikosi na Serikali kwa kufanyika malipo ambayo hayaendani na Ujenzi uliokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM kuhakikisha miradi ya ujenzi inatekelezwa kwa mujibu wa ramani na michoro iliyokubalika ili kuepusha uwezekano wa kufanyika kwa ujenzi huo kinyume na makubaliano yaliyoingiwa na hatimae kupelekea hasara Serikali.

**Majibu ya Uongozi wa KMKM**

Uongozi wa KMKM unatoa ufafanuzi kuwa Wahandisi wa KMKM walishirikiana kwa pamoja na Mkandarasi kuandaa michoro hiyo na kujiridhisha na michoro hiyo kabla ya kuanza kwa kazi ya ujenzi. Kikosi kimejiridhisha kuwa ujenzi huo umefanyika kama ilivyokusudiwa na pia ujenzi huo ulijengwa kwa njia ya mkopo baada ya Kikosi kupata ushauri kutoka ngazi ya Wizara.

Nyaraka hizo walioneshwa wakaguzi na kupatiwa maelezo ya ziada ambapo Kikosi kilitegemea kupongezwa kwa juhudi hizo ukizingatia kuwa ukuta huo wenye maduka mbali na kuongeza miradi ya uzalishaji mali katika Kikosi lakini pia umeondoa kero mbali mbali kwa Kikosi na Raia. Matokeo yake Kikosi kilipongezwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuwapunguzia usumbufu wananchi kwa kutembea masafa marefu kufuata huduma za Afya katika hospital ya KMKM Kibweni pamoja na kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kuzitaka Idara Maalum za SMZ kuanzisha miradi ya uzalishaji ili kuweza kujitegemea.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati licha ya kuwepo tofauti kati ya maelezo ya Mkaguzi na Wizara, Kamati imebaini kwamba wakati Wakaguzi wanafika katika eneo la ukaguzi nyaraka za michoro na ramani zilikuwepo, changamoto iliyojirokeza ni kwamba Watendaji wa KMKM walishindwa kuwapatia nyaraka hizo Wakaguzi na kupelekea kujitokeza kwa hojaa hii. Hivyo majibu Kamati imeyaridhia na kuiondosha hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa KMKM uhakikishe unampatia ushirikiano Mkaguzi anayekuja Ofisini kwao kufanya kazi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar hususan kwa kumpatia vielelezo vinavyohitajika.

## Hoja nambari 6.1.1.9: Kushindwa kufanya tathmini ya matumizi ya shilingi 600,000,000

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kiliingia mkataba na M/S Rom Solution Limited mnamo tarehe 17 Disemba 2021, kwa ajili ya huduma ya upembuzi yakinifu kwa uwekaji wa RADA kwa thamani ya shilingi 600,000,000.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwepo kwa mchanganuo wa matumizi yaliyofanyika jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kufanya tathmini ya

matumizi hayo. Aidha, ukaguzi haukupatiwa Ripoti ya upembuzi yakinifu iliyofanywa na mtoa huduma huyo ili kuweza kupima thamani ya fedha iliyotumika ikilinganishwa na aina ya kazi iliyofanyika jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kutoa maoni ya kitaalamu kutokana na uwepo wa matumizi ya rasilimali za umma yasiyofuata taratibu za kisheria kunakopelekea taarifa za matumizi kutokuonesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM kuhakikisha unafuata taratibu za fedha kama zilivyoelekezwa na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### Majibu ya Uongozi wa KMKM

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo hakijafanya malipo yoyote yanayohusiana na Upembuzi yakinifu wa Rada **(Feasibility Study of Radar)** kwenda kwa mzabuni M/S Rom Solution Limited. Aidha Kikosi kiliingia mkataba na M/S Rom Solution Limited mnamo tarehe 17 Disemba 2021, kwa ajili ya huduma ya upembuzi yakinifu kwa uwekaji wa RADA kwa thamani ya shilingi 600,000,000 ambazo hadi sasa hazijalipwa.

Aidha mchanganuo wa malipo ya Fedha hizo umeainishwa katika mkataba husika na hadi sasa kikosi hakijaingiziwa fedha za kumlipa Mshauri huyo na hakuna malipo yaliyofanyika kama ilivyoelezwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ripoti ya upembuzi yakinifu iliyofanywa na mtoa huduma huyo ipo kupitia barua ya tarehe 18/02/2023 yenye kichwa cha habari "Contract – Feasibility of Radar (Tender Number KM/HQ/OIE/207B/2021) Final Report" iliyowasilishwa, hata hivyo Mzabuni huyo anaidai Serikali baada ya kukamilika kwa jukumu hilo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika uchunguzi wake, Kamati ya PAC imebaini kuwa hakukuwa na mashirikiano mazuri ya Mkaguzi na Wapiganaji wa KMKM. Hali hiyo imepelekea hoja nyingi kujitokeza katika kitabu cha ripoti wakati uwezekano wa kuziepuka ulikuwepo. Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya uongozi wa KMKM kuhusiana na hoja hii kwa vile hakuna fedha yoyote iliyolipwa na kusababisha hasara kwa Serikali. Aidha, Kamati ilifanikiwa kupatiwa kielelezo cha ripoti ya Tathmini iliyonakiliwa hapo juu na kuridhika nayo. Kwa mnasaba huo, Kamati imeiondoa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa KMKM uhakikishe unampatia Mkaguzi vielelezo stahiki ili kuepusha hoja kujitokeza dhidi yao.

## Hoja nambari 6.1.1.10: Kufanya malipo kinyume na makubaliano ya mkataba shilingi 460,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imebainika mnamo tarehe 9 Mei 2022 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimesaini hati ya makubaliano yenye thamani ya shilingi 460,000,000 na Mtoa Huduma M/S Regalia Tanzania Limited kwa ajili ya ununuzi wa sare (uniform) za wapiganaji wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo. Kwa mujibu wa makubaliano ya hati ya Mkataba mtoa huduma alitakiwa kulipwa malipo ya awali ya asilimia 60 ndani ya siku 30 baada ya kupokelewa kwa sare na malipo yaliyobaki ya asilimia 40 atalipwa baada ya kukubaliwa kwa sare hizo.

Dosari mbali mbali ziliweza kubainika katika utekelezaji wa makubaliano ya mkataba huo miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kufanywa malipo ya asilimia 100 yenye thamani ya shilingi 460,000,000 bila ya kuzingatia makubaliano ya mkataba jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 18.6 cha Makubaliano ya Mkataba.
- Kutokuwasilishwa kwa bidhaa iliyokusudiwa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wao jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika mnamo tarehe 07/03/2023 hatukupatiwa hati ya utambulisho wa mapokezi ya bidhaa hiyo (Delivery Order)
- Kutokupatiwa taarifa za kupokelewa na kurikodiwa kwa bidhaa hiyo.

Aidha, pamoja na uwepo wa dosari hizo tumebaini uwepo wa ukiukwaji wa kutokutekeleza maagizo yaliyotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kufanya maboresho ya utekelezaji wa makubaliano ya mkataba kabla ya kutiwa saini hati ya mkataba huo jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 47(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2020. Miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatavyo:-

- Mzabuni atalazimika kuwasilisha hati ya dhamana (Perfomance Security) ya asilimia 10 ya bei ya mkataba wake jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika hatukupatiwa ushahidi wa kutekelezwa kwa pendekezo hilo.
- Mkataba ulitakiwa kuainisha kipindi cha dhamana ya matumizi (warranty) ya mwaka mmoja jambo ambalo halikutekelezwa.

- Mkataba uainishwe kipindi cha uwasilishwaji na mapokezi ya bidhaa (delivery period) jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika halikuweza kufanyiwa kazi na kupelekea kutokufahamika tarehe sahihi ya mapokezi ya bidhaa hizo licha ya fedha zote kulipwa kwa mtoa huduma kinyume na utaratibu.

Kutokana na dosari nilizozibainisha hapo juu kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma kwa kutokuwa makini katika utekelezaji wa taratibu za manunuzi kwa kushindwa kuzingatia Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM kuhakiksha unafanya ufuatiliaji wa karibu kwa mtoa huduma huyo ili kuhakikisha huduma ya ununuzi wa sare za wapiganaji wa Kikosi hicho zinapatikana kama ilivyokusudiwa. Aidha, uongozi unapaswa kuzingatia taratibu za matumizi ya fedha za Umma ili kuepuka kujitokeza kwa matumizi yasiyozingatia Sheria ambayo yataitia hasara Serikali.

### Majibu ya Uongozi wa KMKM

Uongozi wa KMKM unaeleza kuwa umepokea sare hizo na tayari zimesha kabidhiwa kikosini (KMKM). Kwa upande wa Fedha hizo ni kwamba ziliingizwa mwishoni mwa mwaka wa fedha na kupelekea kulipwa zote kwa pamoja mzabuni ili kuendana na mwaka husika wa fedha 2021 - 2022. Uamuzi huo ulizingatia kuwa mzabuni huyo ni mzoefu na muaminifu kwa kusambaza Sare za kijeshi katika vyombo mbali mbali vya Ulinzi na Usalama vya SMZ na SMT.

Kikosi cha KMKM kinapenda kuthibitisha kuwa hakukuwa na dhamira yoyote ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali isipokuwa suala la msingi ni kuweza kuwapatia sare maofisa na wapiganaji na kutokana muda wa kuingia kwa fedha hizo ilionekana ni vyema kulipwa mzabuni huyo ili kutimiza lengo lililokusudiwa la kuwajengea unadhifu wapiganaji. Hata wakaguzi walipokuja kufanya verification walioneshwa uniform hizo ghalani KMKM Kibweni na kwa sasa mgao wa fomu hizo umeshafanyika kwa wapiganaji.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba kasoro zilizotajwa na Mdhibiti mpaka ukaguzi unamalizika zilishindwa kupatiwa ufumbuzi. Kamati imebaini kwamba hata taarifa ya kupatikana na kupokelewa kwa bidhaa hizo ilipatikana tarehe 29/03/2023, kipindi ambacho ukaguzi ulishamalizika mnamo tarehe 07/03/2023.

## KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - PEMBA

### Hoja nambari 6.1.1.11: Malipo yaliyolipwa kwa njia ya Udanganyifu shilingi 62,356,872

Kwa mujibu wa mwaka wa fedha 2020/2021 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimeingiziwa jumla ya shilingi 350,000,000 kupitia Hesabu ya Kamandi ya KMKM Zanzibar kutoka (OR) Fedha na Mipango Zanzibar kwa ajili ya ujenzi wa hanga la kulalia wapiganaji lililopo Wete Pemba, na fedha hizo kufanyiwa malipo kupitia hati nambari D04PV2000000317 ya tarehe 29/04/2021.

Aidha, ukaguzi ulibainisha kupitia Hoja ya Ukaguzi Nambari 4.4.3.1 katika Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwamba Kikosi Maalum cha KMKM kiliingiziwa jumla ya shilingi 350,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Hanga la Wete Pemba. Kutokana na bajeti ya ujenzi huo ilibainika fedha hizo zilitumika bila ya kuwepo vielelezo vilivyothibitisha uhalali wa malipo hayo. Hata hivyo kwa mujibu wa makadirio ya ujenzi ulipaswa ujenzi huo kukamilika kwa vile fedha yote iliyoombwa iliingizwa kwa wakati.

Ukaguzi umebaini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kikosi cha KMKM ilifanya malipo mengine yenye thamani ya shilingi 62,356,872 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hanga la Wete jambo ambalo Hanga hilo lilishatiliwa fedha zote zilizostahiki kwa mwaka wa fedha uliopita na kutia shaka ya kutokukamilika kwake na uwepo wa malipo yaliyotumika kwa njia ya udanganyifu bila ya kuwepo kwa mahitaji ya kuendelezwa ujenzi wa Hanga hilo. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha KMKM kuhakikisha unazidisha umakini katika matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha iliyotumika inaendana na uhalisia wa kazi iliyofanyika. Ufafanuzi wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 47: Malipo ya ujenzi wa Hanga kwa njia ya udanganyifu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Fedha zilizolipwa (Tshs) | Maelezo ya Malipo |
|---|---|---|---|---|
| 2/12 ya 10/12/2021 | 001565 | Jazira Construction | 31,615,392 | Malipo kwa ajili |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8/12 ya 21/12/2021 | 001568 | Limited | 5,360,000 | ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Hanga la Maaskari wa KMKM. |
| 29/12 ya 29/12/2021 | 001570 | | 5,283,000 | |
| 9/12 ya 22/12/2021 | 001571 | | 4,224,000 | |
| 13/12 ya 29/12/2021 | 001575 | | 2,090,000 | |
| - 28/12/2021 | - | | 13,288,600 | |
| 3/1 ya 7/01/2022 | - | Jazira Construction Limited | 495,880 | |
| **Jumla** | | | **62,356,872** | |

Majibu ya Uongozi wa KMKM

Kikosi kimeshangaa na taarifa ya kufanya udanganyifu wa malipo ya Tsh. 62,356,872/= kuwa ni nyingeza ya mradi wa hanga la Wete Pemba wenye thamani ya Tsh. 350,000,000/- kwa sababu taarifa hiyo sio sahihi.

Kikosi kinapenda ifahamike kuwa hakuna udanganyifu katika matumizi ya fedha shilingi 62,356,872 kwa sababu matumizi ya fedha hizo yanatokana na shilingi 70,000,000 zilizohaulishwa kutoka akaunti ya Mkuu wa KMKM Zanzibar na kwenda akaunti ya Mkuu wa KMKM Pemba ambazo zimetokana na fedha ya mradi shilingi 350,000,000. Hata hivyo fedha hizo ziliingia katika kipindi cha mwisho wa mwaka wa fedha 2020 - 2021 na kuendelea kutumika hadi wa mwaka wa fedha 2021 - 2022.

Kikosi kinasisitiza kwamba hakuna fedha iliyotumika kwa ujenzi wa Hanga la Wete Pemba ambayo ilikuwa nje ya bajeti ya fedha ya mradi huo ambayo ni shilingi 350,000,000 kwa sababu mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo hadi sasa upo kama hivi ifuatavyo:-

Jumla ya fedha za mradi Tsh. 350,000,000/=.

Jumla ya fedha iliyokwishatumika wakati wa ukaguzi. Tsh.254, 155,300/=.

Fedha iliyosalia ya kumalizia mradi wakati wa Ukaguzi ni Tsh.95, 844,700/=.

Aidha ujenzi huo ulisita kutokana na zoezi la Operation Karafuu ili kupisha makaazi ya wapiganaji katika jengo hilo na baada ya operesheni karafuu jengo hilo lilitumika kuhifadhia vifaa vya ujenzi wa madarasa na masoko ya wajasiriamali katika miradi ya covid 19.

Kufuatia hali hiyo ya kusimama kwa ujenzi, Kikosi cha KMKM kiliandika barua kwa mamlaka husika ya kusitisha ujenzi kupitia barua ya tarehe 29 April 2022 yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01C/16/2022 kwenda kwa Katibu Mkuu (OR) Fedha na Mipango hali ambayo inathibitisha kuwa ujenzi huo haujawahi kusita kwa sababu ya kifedha.

Hivyo basi ujenzi huo umeshakamilika na kufunguliwa katika shamra shamra za kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Vielelezo vya ujenzi huo vitawasilishwa kwa Katibu Mkuu Wizara kwa kuwa ujenzi huo umekamilika kwa ajili ya ukaguzi na kujiridhisha. Kupitia hili Kikosi kimeshangaa kuaminishwa umma kuwa kuna udanganyifu wa fedha bila ya kufanya ukaguzi wowote wa nyaraka na kutafuta taarifa za msingi za mradi huo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021, jumla ya Shilingi 350,000,000 ziliingizwa katika akaunti ya Kikosi cha KMKM Makao Makuu kutoka (OR), Fedha na Mipango, na jumla ya Shilingi 70,000,000 zilifanyiwa uhaulishaji na kuingizwa katika akaunti ya KMKM Pemba kwa ajili ya ujenzi wa Hanga la kulalia Wapiganaji liliopo Wete, Pemba. Kamati ilijiridhisha kuhusiana na kufuatwa taratibu za uhaulishaji. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa hakukuwepo na mashirikiano mazuri ya kiutendaji kati ya Mkaguzi na Makamanda wa KMKM hasa ukizingatia Mkaguzi alipopita hakupatiwa vielelezo na ndio maana hoja. Kwa msingi huo Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara na kuamua kuifuta hoja hii.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Makamanda wa KMKM wahakikishe wanakuwa karibu kiutendaji na Mkaguzi hususan kwa kumpatia vielelezo anavyovihitaji kwa mujibu wa ssheria.

2. Wakaguzi wa CAG waifuatilia kwa kina hoja ya ukaguzi mpaka mwisho fedha zilipotumika kwani Kamati imebaini kuwa Mkaguzi aliyeibua hoja hii aliishia katika taarifa zilizopatikana Makao Makuu Zanzibar na fedha ilipofanyiwa uhaulishaji kuja Pemba, Mkaguzi husika hakuenda kufuatilia kwa ajili ya kujiridhisha.

## Hoja nambari 6.1.1.12: Kukosekana kwa muongozo wa malipo ya kodi ya nyumba shilingi 9,000,000

Kwa mujibu wa kanuni nambari 127(1) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 imetoa ufafanuzi kwa wanufaika wanaopaswa kulipiwa kodi ya nyumba. Hata hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Idara Maalum pamoja na Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ hakuna sehemu iliyotoa ufafanuzi wa uwepo wa uhalali wa kufanyika malipo ya kodi ya nyumba kwa wapiganaji.

Ukaguzi umebaini Kikosi cha Kuzuwia Magendo (KMKM) kimefanya malipo yenye thamani ya shilingi 9,000,000 kwa ajili ya kuwalipia wapiganaji wanaoishi katika nyumba za Shirika la Nyumba Zanzibar pasi na kuwepo kwa muongozo halali wa kufanya hivyo.

Kuendelea kufanya malipo pasi na kuwepo kwa muongozo kunaweza kukapelekea upotevu wa fedha za umma unaotokana na kutokuzingatiwa kwa Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha KMKM Pemba kuhakikisha unasimamia miongozo ya Idara Maalum ya SMZ pamoja na kuzingatia matakwa ya sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 ili kuepuka kufanyika kwa matumizi mabaya ya fedha za umma. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 48: Malipo ya kodi ya nyumba yasiyokuwa na muongozo**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Fedha iliyolipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 01/10 ya 30/09/2021 | - | Shirika la Nyumba | 900,000 | Malipo ya huduma ya nyumba kwa ajili ya maaskari |
| 06/11 ya 24/11/2021 | | | 1,500,000 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20/04 ya 14/04/2022 | | | 6,600,000 | wa<br><br>KMKM Pemba. |
| **Jumla** | | | **9,000,000** | |

Majibu ya Uongozi wa KMKM

Kikosi cha KMKM kimeshtushwa na hoja hii kuingizwa katika kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa sababu imeleta taharuki kwa maofisa na wapiganaji wanaopata uhamisho kwenda kamandi ya Pemba huku wakijua kuwa KMKM haina nyumba kwa maofisa na wapiganaji wake zaidi ya mahanga.

Hoja hii haisadii kujenga ufanisi wa kazi kwa watendaji na badala yake inaenda kushusha ari na kuwachonganisha wapiganaji wanaopata uhamisho kwenda kuendelea na kazi Pemba na Serikali yao suala ambalo halileti afya.

Kibaya zaidi suala hili lipo kwa zaidi ya miaka 30 sasa inakuwaje kuzungumzwa malipo ya kodi ya nyumba katika uongozi huu wa Commodore Azana Hassan Msingiri, kulikoni? Kikosi kinapenda ifahamike kuwa Kamandi ya Pemba suala la mahitaji ya nyumba kwa maakazi ya watendaji ni suala lenye umuhimu wa kipekee, pamoja na kwamba Kikosi hakina nyumba zake za maakazi kwa ajili ya maafisa na wapigaji ambapo kiasi cha 90% ya maofisa na wapiganaji wanaofanya kazi Kamandi ya Pemba ni wageni wa kisiwa hicho.

Aidha wapo maofisa wakubwa na wadogo ambao kwa mujibu wa dhamana zao upande kamandi ya Pemba hawastahiki kukaa katika mahanga na wanastahiki kuwa na nyumba za kuishi nje ya mazingira ya ndani ya kambi ili kuwapa utulivu wa kutekeleza majukumu yao ya kazi.

Kufuatia changamoto hiyo ya makaazi kwa miaka zaidi ya 30 Kikosi kimekuwa kikitumia nyumba ambazo zinamilikiwa na Shirika la Nyumba kwa kuingia mikataba ya ukodishwaji wa nyumba na Shirika hilo ambapo kwa mikataba hiyo KMKM inawajibika kulipa Kodi katika shirika hilo la Serikali. Hata hivyo Kikosi kitafarajika kama watapewa amri ya kuishi bila ya malipo katika nyumba hizo.

Hivyo basi suala la kukodi na kulipa kodi ya nyumba za Shirika la Nyumba kwa upande wa KMKM Pemba ni jambo lenye umuhimu wa kipekee kutokana na mazingira yaliyopo na kwa kiasi fulani limewapunguzia usumbufu wa maakazi baadhi ya watendaji wake.

Kimsingi dhamira ya kukodi nyumba hizo ni kupunguza changamoto ya maakazi kwa watendaji wanaopata uhamisho wa kikazi kwenda Pemba wakiwa ni wageni. Kikosi kitakapokuwa na nyumba zake suala la kukodi nyumba litamalizika kwa sababu posho la nyumba kwa Afisa ni Tsh.15,000/- kwa mwezi ambazo haziwezi kutosheleza kulipa kodi ya nyumba.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa ni kweli malipo ya kodi yalilipwa na KMKM pasi na kuwepo kwa muongozo kama ilivyoelezwa na Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa kulikuwa na sababu ya msingi iliyopelekea kasoro hiyo kujitokeza kwa vile kulikuwa na uhaba wa makazi kwa watendaji wa Kikosi cha KMKM hususani Maofisa Wakuu wa Kikosi hicho ambapo ilifikia hatua chumba kimoja waliweza kulala mpaka Maofisa Wakuu wanne (4), kitu ambapo kinaenda kinyume na masuala mazima ya utawala bora na haki za kibinadamu hasa katika kipindi hiki cha amani ya nchi yetu.

Kamati ya PAC imegundua kwamba Wizara ya KMKM inayo Kanuni ya ya mwaka 1993 ambayo haijaeleza kikamilifu masuala ya malipo ya kodi za nyumba kwa Wapiganaji. Vile vile, Kamati imebaini kuwa Wizara inayoshughulikia Vikosi inayo Kanuni yake ambayo wameanza kuifanyia marekebisho na wameieleza Kamati kwamba wataingiza kanuni itakayoelezea uwezo wa kila Kikosi kuwa na uwezo wa kutengeneza miongozo yake ya malipo ya kodi za nyumba

Kwa mnasaba huo, hoja hii itaendelea kubakia hadi pale Wizara au Kikosi kitakapotoa muongozo wake wa malipo ya kodi za makaazi

Kwa vile fedha ya Serikali haikupotea na badala yake ilitumika kwa maslahi ya Maaskari wa Kikosi. Kamati iliridhika na majibu ya Kikosi na kuiondoa hoja hiyo.

**Maoni, Ushauri, na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaushauri Uongozi wa Wizara kukaa na kuzifanyia marekebisho Kanuni zake za Tume ya Utumishi ya Idara Maalmu za SMZ ili ziweze kwenda sambamba na wakati uliopo ikiwemo kuingiza suala la Vikosi kuweza kuunda miongozo ya ulipaji kodi za Makaazi.

## Hoja nambari 6.1.1.13 Hati za malipo ambazo hazijarikodiwa katika daftari la fedha taslim shilingi 43,288,600

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 43,288,600 zimetumika

kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Kamandi ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Pemba lakini hati husika za malipo hazikurikodiwa katika daftari la fedha taslim (Cash book).

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea taarifa za ufungaji wa mahesabu katika daftari la fedha taslim kutokuwa sahihi, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamandi ya KMKM kuongeza juhudi katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo kiukamilifu ikiwemo kurikodi malipo ya fedha katika daftari la fedha taslim. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 49: Hati za malipo ambazo hazijarikodiwa katika daftari la fedha taslim**

| **Hati Namba** | **Hundi Namba** | **Fedha iliyolipwa (Tshs)** | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|
| _ 28/12/2021 | - | 13,288,600 | Hamoud Salim Suleiman | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Hanga |
| 26/3 27/3/2022 | T.T | 30,000,000 | Mkuu wa KMKM Pemba | Malipo ya VAT kwa ZRB |
| **Jumla** | | **43,288,600** | | |

Majibu ya Uongozi wa KMKM

Hoja hii ni muendelezo wa hoja ambazo hazina usahihi zilizowasilishwa katika kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Usahihi wa matumizi hayo ni kwamba hati za malipo hayo zimerikodiwa katika daftari la fedha taslim (Cashbook) na vielelezo vya hati hizo vilikuwepo na wakaguzi walijirishisha kwa kuweka alama ya vyema katika daftari la fedha taslim walipokwenda kufanya *Verification* baada ya kupewa majibu ya

hoja za awali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hata hivyo Kikosi hakikutegemea kurejeshwa kwa hoja hiyo na kuingizwa katika kitabu cha CAG wakati ambapo katika kikao cha Watendaji wa CAG na KMKM Pemba kwa pamoja walikubaliana kuwa hoja hiyo imejibika na kuondolewa lakini kwa sababu ambazo Kikosi hazikifahamu hoja hiyo imeandikwa katika kitabu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Kikosi cha KMKM hati hizo hazikuwepo katika daftari la fedha taslim na uongozi wa KMKM. Hata hivyo, Kamati katika uchunguzi wake ulibahatika kuziona hati hizo na kuridhika nazo. Hivyo, hoja hii imeondolewa na Kamati.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa KMKM uweke vizuri kumbukumbu za matumizi ya fedha ili ziweze kupatikana wakati zitakapohitajika.

### 6.1.2 FUNGU D02: JESHI LA KUJENGA UCHUMI

## Taarifa ya mapato

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Jeshi la Kujenga Uchumi lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 117,657,000 kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 JKU lilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 117,657,000 sawa na asilimia 100 ya makadirio.

**Majibu ya Uongozi wa JKU**

Jeshi la Kujenga Uchumi lina vyanzo vyake vya ndani vinavyotumika kuwasilisha au kuchangia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwaka wa fedha kama ifuatavyo:-

Mapato ya kodi za maduka

Mapato ya Karafuu

Mapato ya Mpunga

Mapato ya mazao ya Bustani

Mazao ya Baharani

Mapato ya kazi ya Useremala

Ada ya Mafunzo/Wanafunzi

Mapato ya mifugo

Kwa mwaka 2021/2022 JKU imevuka lengo la makusanyo kutokana na sababu ya ustawi mzuri wa mazao ya uzalishaji. Lifuatalo ni jeduweli linaloonyesha makadirio na makusanyo pamoja na asilimia ya makusanyo kwa kila fungu.

MPANGO WA UKUSANYAJI MAPATO YA JKU KWA MWAKA 2021/2022

| GFS CODE | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO YA MAPATO KWA 2021/2022 | MAKUSANYO HALISI 2021/2022 | ASILIMIA YA MAKUSANYO KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|
| 1415004 | Kodi ya Maduka | 8,386,000 | 10,657,000 | 127.0 |
| 1415010 | Karafuu | 10,000,000 | 10,000,000 | 100.00 |
| 1421004 | Mapato ya Mpunga | 10,000,000 | 10,000,000 | 100.00 |
| 1421006 | Mapato ya mazao ya Bustani | 15,000,000 | 15,000,000 | 100.00 |
| 1422027 | Mazao ya Baharani | 5,000,000 | 5,000,000 | 100.00 |
| 1422052 | Mapato ya Viwanda Vidogo vidogo | 10,000,000 | 10,000,000 | 100.00 |
| 1422088 | Ada ya Mafunzo/Wanafunzi | 35,500,000 | 45,500,000 | 128.17 |
| 1421011 | Mapato ya mifugo | 10,000,000 | 10,000,000 | 100.00 |
| **Jumla** | | **105,386,000** | **117,657,000** | **112** |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kutathmini utekelezaji wa hoja hii, Kamati imebaini kwamba mapato ya Jeshi la Kujenga Uchumi yameongezeka katika mwaka 2021/2022 ukilinganisha na mwaka 2020/2021. Hali hiyo imesababishwa na kuwepo na mipango mizuri ya uzalishaji unaotekelezwa na makambi yao hususan katika uzalishaji wa mazao mbali mbali ikiwemo karafuu, mazao ya chakula pamoja na ufugaji. Aidha, Mikarafuu hiyo ipo katika maeneo ya Machui na Kitope na maeneo mengine ya makambi yao.

## Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Jeshi la Kujenga Uchumi lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 38,952,705,700, kati ya fedha hizo shilingi 28,072,548,825 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo na shilingi 10,814,623,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Jeshi la Kujenga Uchumi limeingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 30,058,175,567 sawa na asilimia 77 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 28,072,548,825 kwa ajili ya mishahara na kazi za kawaida sawa na asilimia 100 ya makadirio na shilingi 1,985,626,742 kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 18.36 ya makadirio.

### Majibu ya Uongozi wa JKU

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 JKU iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi TZS 37,474,723,000 kati ya fedha hizo TZS 24,016,100,000 kwa mshahara, TZS 2,644,000,000 kwa kazi za kawaida na TZS 10,814,623,000 kwa kazi za maenedeleo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Juni, 2022 JKU ilishaingiziwa na kutumia jumla ya Shilingi 30,058,174,767 kati ya fedha hizo TZS 23,996,013,025 kwa ajili ya mshahara TZS 4,076,535,000 kwa ajili ya kazi za kawaida (OC) na TZS 1,985,626,742 kwa kazi za maenedeleo.

Lifuatalo ni jeduweli linaloonyesha makadirio na matumizi halisi ya mshahara, matumizi mengineyo (OC) na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

| S/NO | MAELEZO | MAKADIRIO | MATUMIZI HALISI |
|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 24,016,100,000 | 23,996,013,025 |
| 2 | Matumizi mengineyo | 2,644,000,000 | 4,076,535,000 |
| 3 | Maendeleo | 10,814,623,000 | 1,985,626,742 |
| | | **37,474,723,000** | **30,058,174,767** |

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba matumizi mengineyo ya Jeshi la Kujenga Uchumi yameongezeka kwa jumla ya shilingi 1,432,535,000. Ongezeko hilo lilitokana na baadhi ya Maafisa wa wake kuongezwa vyeo na kupelekea kuongezeka kwa fungu la Maposho.

Aidha, posho za vijana wanaojenga Taifa zilikuwa zikitoka katika Fungu la mshahara katika mwaka 2020/2021 na kupelekwa katika Fungu la Matumizi Mengineyo, jambo ambalo limepelekea kupunguza Fungu la Mshahara.

Hata hivyo, kuna baadhi ya shughuli za ujenzi zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa mwaka 2020/2021 zenye jumla ya shilingi bilioni 10 hazikuweza kutekelezwa kutokana na kutoingiziwa fedha badala yake zilihamishiwa katika mwaka 2021/2022. Sambamba na hilo, Kamati imegundua kuwa baadhi ya wakati vielelezo vinakuwepo katika ngazi za utawala lakini zikihitajika na Mkaguzi zinakuwa haziwasilishwi na Mkaguzi kuamua kuandika hoja katika ripoti yake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa JKU uhakikishe unaweka vizuri kumbukumbu na vielelezo vya Fedha, ili vikihitajika kwa ukaguzi viweze kupatikana

## Hoja nambari 6.1.2.1: Malipo yaliyolipwa bila ya uwepo wa mkataba wa nyongeza (Addendum) shilingi 825, 000, 000

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ukaguzi umefanya mapitio ya nyaraka za uhasibu ikiwemo hati za malipo, taarifa za benki, ankara za malipo, mpango wa manunuzi, pamoja na taarifa nyenginezo na kubaini Jeshi la Kujenga Uchumi limeingia makubaliano na mzabuni M/S Sabaha Store kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kujengea Skuli ya Mtoni vyenye thamani ya shilingi 825,000,000 ambapo ukaguzi umebaini uwepo wa dosari zifuatazo:-

1. Kukosekana kwa mkataba wa nyongeza (Addendum).
2. Kukosekana kwa ripoti ya tathmini iliyotolewa na Bodi ya Zabuni.
3. Kukosekana kwa mchanganuo wa vifaa na thamani ya vifaa vyenyewe.
4. Kukosekana kwa mkataba wa awali unaoonesha gharama halisi ya fedha kwa mujibu wa kazi iliyofanywa ambayo itathibitisha uhalali wa uwepo wa ongezeko la bei.
5. Kukosekana kwa utaratibu wa kufanyika kwa malipo (mode of payment).
6. Kukosekana kwa nyaraka zinazothibitisha uhalali wa uwepo wa gharama za nyongeza.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa na nyaraka za matumizi ya muamala huo jambo ambalo huenda likapelekea kufanya matumizi kusikozingatia

mpango wa matumizi pamoja na bajeti ya taasisi husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakiksha unafanya matumizi kwa kuzingatia mpango wa matumizi pamoja na bajeti husika ili kuepusha kujitokeza kwa matumizi yasiyokuwa ya lazima ambayo hayatakuwa na tija. Mchanganuo wa malipo yaliyofanyika ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 50: Malipo yaliyolipwa bila ya kuwepo kwa mkataba wa nyongeza**

| Hati Nam. | Aliyelipwa | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1/11 ya 5/11/21 | Sabaha Store | 702,944,760 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 3/11 ya 5/11/21 | TRA Domestic Revenue | 14,359,440 | Malipo kwa ajili ya kodi ya zuio |
| 2/11 ya 5/11/21 | Zanzibar Revenue Board | 107,695,800 | Malipo kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT). |
| **Jumla** | | **825,000,000** | |

### Majibu ya Uongozi wa JKU

Fedha hii ililipwa kama deni kwa mzabuni wa vifaa vya ujenzi baada ya mzabuni kukamilisha uletaji wa vifaa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba kulikosekana mashirikiano baina ya uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi na Mkaguzi hususan katika suala zima la upatikanaji wa vielelezo. Kamati inaeleza hivi kwasababu vielelezo zilivyohitajika Kamati ilipatiwa kwani wakati wa Mkaguzi hakupatiwa kwa vile vilikuwa vipo vilichukuliwa na ZAECA kwa uchunguzi wa Makamanda waliosimamishwa kazi.

Aidha, Kamati imebaini kuwa shilingi milioni 825,000,000 zilizoelezwa na Mkaguzi ni miongoni mwa jumla ya shilingi bilioni 2.4 ambazo zilikuwa katika Mkataba mmoja (wa awali) isipokuwa Mzabuni alichelewa kulipwa. Hivyo, kulikuwa hakuhitajiki Mkataba wa nyongeza (Addendum). Kamati imeridhika na maelezo yaliyowasilisha mbele yake na kuiondoa hoja hii.

### Maoni, Ushauri na Mapendeezo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa JKU uhakikishe unampatia Mkaguzi mashirikiano ya kutosha hususan kwa kumtafutia nyaraka zote anazozihitaji ili aweze kuzitumia kwa kazi zake za ukaguzi.
2. Uongozi wa JKU uhakikishe vielelezo vya fedha, vitawekwa vizuri ili vikihitajika kwa ajili ya ukaguzi viweze kupatikana
3. Kamati inazitaka mamlaka nyengine zote zinazochukua vielelezo vya fedha katika Ofisi za Umma zitoe mashirikiano na Wakaguzi kwa kuwapatia nyaraka pale zinapohitajika

## SKULI YA MTONI YA JESHI LA KUJENGA UCHUMI

## Hoja nambari 6.1.2.2: Fedha iliyotolewa wa msambazaji wa vifaa bila ya uwepo wa mkataba shilingi 135,000,000

Ukaguzi umebaini Kikosi cha JKU kimemkopesha jumla ya shilingi 135,000,000 mtoa huduma M/S Sabaha Store kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Ujenzi vya Skuli ya Mtoni Ufundi na Sekondari bila ya uwepo wa Makubaliano ya kisheria (Mkataba). Aidha, Ukaguzi haukuweza kupatiwa mchanganuo wa bei za vifaa hivyo (BOQ) kwa ajili ya kujiridhisha na Orodha ya idadi ya Vifaa vilivyowasilishwa na Mtoa huduma huyo kwa ajili ya ujenzi huo.

Kutoa fedha za Serikali na kumkopesha mtoa huduma ni jambo ambalo haliwezi kukubalika kwa mujibu wa miongozo ya Sheria ya Fedha kwani kufanya hivyo kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za Umma. Aidha, Ukaguzi haukuweza kuthibitisha uhalali wa kufanyika kwa matumizi hayo kutokana na kutokupatikana kwa orodha halisi ya ununuzi wa vifaa hivyo pamoja na kurikodiwa katika daftari la kuwekea kumbukumbu za vifaa vya ghalani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unafuata taratibu za manunuzi ili kuepuka kujitokeza kwa matumizi yasiyo ya lazima ambayo hayatakuwa na tija kwa Serikali.

### Majibu ya Uongozi wa JKU

Mradi huu wa ujenzi wa Skuli ya Ufundi ya JKU Mtoni ulianza katika mwaka wa fedha 2019/2020 ukitarajiwa kufanyika kwa awamu mbili ambazo ni-

Awamu ya kwanza: Kujenga jengo la ghorofa mbili lenye karakana na madarasa

kwa ajili ya matumizi ya walimu na wanafunzi 1640 wa Skuli ya Ufundi.

Awamu ya pili: Kumalizia kazi za ujenzi zilizobakia ambazo zimeelezwa kwenye para namba 6 ya taarifa hii, na

Kuipatia Skuli hiyo vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia kwa elimu ya ufundi.

Mradi huu ulikuwa ni muendelezo ya Mradi wa kumalizia ujenzi wa jengo la ghorofa tatu la Skuli ya Sekondari ambapo Mzabuni wa kazi hiyo na nyuma wa uletaji wa vifaa vya ujenzi alipewa zabuni ya kuendelea kuleta vifaa kwa ajili ya mradi huu mpya kulingana na Bodi ya Zabuni.

Mradi huu ulijengwa na Kikosi cha Ujenzi cha JKU ambacho hutumia wafanyakazi wa Jeshi la Kujenga Uchumi na Wanafunzi wa Skuli ya Ufundi ya JKU Mtoni wa fani ya uashi (Masonry and Bricklaying), ufundi bomba (Plumbing and Pipe fitting), ufundi umeme (Electrical Installation), ufundi mchundo (Fitting and Turning) na ufundi vyuma na usanifu (Welding and Fabrication). Kwa msingi huo, mradi huu ujenzi wake ni sawa na miradi mengine au kazi nyengine za ujenzi ndani ya JKU hivyo haukuwa na mkandarasi aliyechaguliwa kwa wakati wowote.

## KUSITA UTEKELEZAJI WA MRADI NA AGIZO LA KUENDELEA

Katika mwezi wa Septemba, 2020 Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ alifanya ziara mara baada ya kuteuliwa na alikuta Mradi huo unaendelea kwa spidi ndogo sana na alipotaka sababu za kuwepo kwa hali hiyo alijulishwa kuwa Mkandarasi wa uletaji wa vifaa amesitisha uletaji wa vifaa kutokana na kutolipwa fedha yake kwa muda mrefu ambapo kwa wakati huo deni lake lilikuwa zaidi ya TSZ 820,000,000/=. Agizo la Mhe. Waziri kwa wakati ule wa kwanza na kufanyiwa uchunguzi mradi huo na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ambao unaonekana kwa wakati ule haukuona tatizo lolote la kiutendaji wala kifedha.

Mhe. Waziri alipokuja Skuli kwa mara nyengine na kuona mkwamo wa wanafunzi wa Skuli ya Ufundi katika kupata elimu iliyowaleta Skuli aliuagiza uongozi wa JKU kwa jumla na hususan ule wa Skuli kutumia fedha ya ndani inayozalishwa kupitia ada za wanafunzi wa Skuli ya Sekondari na kazi za Skuli ya Ufundi ili kukamilisha ujenzi uliokuwa umefikia zaidi ya asilimia 75 kwa wakati huo. Uongozi wa Skuli kutokea hapo ulizuia baadhi ya matumizi ya Skuli (kama vile posho za kazi za ziada za walimu) na kuelekeza fedha hiyo katika kukamilisha ujenzi huo.

Kazi zilizokuwa zikihitaji kukwamuliwa kwa kipindi hiki zilihusiana zaidi na plasta katika

ghorofa za juu, mfumo wa umeme kwa ajili ya karakana za ufundi, umeme wa kawaida, mfumo wa maji safi na maji taka, upakaji wa rangi, kazi za ceiling, gutters na zinazofungamana na kazi za aina hiyo. Fedha hii ilifikia takriban zaidi ya TZS 120,000,000/= na hivyo kulifanya jengo kuweza kutumika japo lilikuwa halijakamilika kwa ujumla wake kwa kipindi hicho.

KAZI ZA SABAH STORE ZILIZOKUWA BADO KUKAMILIKA KUFIKIA HAPO

Kazi za Sabah Store zilisita kutekelezwa hadi mwishoni kabisa mwa kukaribia kufunguliwa kwa mradi huu. Kazi hizo ni pamoja na:

Kukamilisha usuguaji wa tarazo katika baadhi ya maeneo na kupiga polish ya mwisho kwa ajili ya kukabidhi.

Kukamilisha kazi ya uwekaji wa interlocks katika sehemu ya ubavuni na nyuma ya jengo na sehemu zenye miti na pembeni ya majengo.

Kukamilisha kazi ya milango na madirisha ya alluminium katika upande wa mmoja wa ghorofa ya kwanza.

Kufunga milango mikubwa (gates) katika vyumba vyote vya karakana za ufundi katika ghorofa ya chini.

KUSOMEKA FEDHA HIYO KAMA MKOPO KWA SABAH STORE

Kufuatia kuwa ujenzi wa Skuli ya Ufundi Mtoni ni mradi ambao ulikuwa umetengewa fedha katika bajeti ya Serikali kwa miaka takriban mitatu, kwa lengo la kutofautisha matumizi ya Skuli yaliyokuwa yakifanyika baada ya agizo la kutumia fedha ya Skuli kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo, uongozi wa Skuli ulimtaka Mshika fedha wa Skuli kutumia jina la "mkopo MMJKU" licha barua hizo zote kutoka ndani ya Skuli kwa ajili ya kazi za ujenzi wa jengo la Skuli ya Ufundi. Hakuna hata shilingi moja ya fedha hii iliyoandikwa katika voucher au sehemu nyengine kuwa huo ni mkopo kwa Sabah Store. Inaonekana istilahi hii ya "mkopo wa Sabah Store" imebuniwa na Wakaguzi. JKU haielewi ni kwa msingi gani au kipimo kipi fedha hiyo waliandika kuwa ni mkopo kati ya Skuli na Sabah Store.

Wakati wa Sherehe za Mapinduzi kutumiza miaka 58, JKU ilifanikisha uzinduzi wa majengo yake ya kuishi vijana katika Kikosi cha JKU Msaani huko Pemba. Kufuatia uharaka wa shughuli hiyo, JKU ilimtaka Sabah Store kufanya baadhi ya kazi za ukamilishaji wa ujenzi ambazo zilianza mwaka wa fedha uliokuwa unaendelea. Kufuatia kazi hizo kufanyika kwa mkopo, JKU iliwiwa na deni la zaidi ya TZS 250,000,000/= kwa kazi ya ujenzi wa Kikosi cha Msaani ambazo inaonekana bado hazijalipwa hadi kufikia sasa.

Kuna wakati ulipaji wa deni hilo uliihusisha Skuli kupitia fedha iliyotumwa na Makao Makuu kwa lengo la kuharakisha kumalizika kwa kazi zilizobakia za Sabah Store [angalia para namba 7 juu] ambazo alisita kuzifanya kutokana na kutolipwa fedha yake hiyo.

#### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli kulikuwa na agizo la Waziri la ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia kwa elimu ya ufundi Skuli ya Ufundi pamoja na ukamilishaji wa baadhi ya shughuli za ujenzi ili Wanafunzi waweze kupata elimu iliyokusudiwa. Hili lilifanyika kutokana na kuharakisha kukamilika kwa ujenzi huo ili liweze kuzinduliwa katika sherehe za Mapinduzi za kutimiza miaka 58.

Kimsingi, Kamati imebaini kuwa fedha zilizotumika zilikuwa ni fedha zilizokusanywa kutoka katika ada za Wanafunzi zilitumika kama mkopo wa ndani ambapo JKU Mtoni waliwaruhusu JKU Makao Makuu kufanya kazi hiyo kwa kutumia nguvu kazi ya vijana wa kujenga Taifa pamoja na Wafanyakazi wao.

Pamoja na kuwepo kasoro za ukiukwaji wa taratibu za kimatumizi hasa ukizingatia fedha ya Skuli haikuwa na muongozo wake wa matumizi ya aina hiyo lakini suala hilo lilifanyika kwa maslahi ya umma. Sambamba na hilo, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) uliifuatilia kadhia hiyo na kushindwa kubaini uwepo wa ubadhirifu wowote. Kwa msingi huo. Kamati imeridhika na majibu na kuiondosha hoja hii.

#### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa JKU uhakikishe unapoamua kutumia fedha zinazotokana na malipo ya Wanafunzi wawe na muongozo au idhini kutoka Bodi ya Zabuni ili kuhalalisha matumizi hayo na kuepuka hoja zisizo za msingi.

## JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) PEMBA

### Hoja nambari 6.1.2.3: Kutokufuatwa kwa utaratibu wa mapokezi na utoaji wa bidhaa za ghalani

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Zone ya Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba imepokea bidhaa kutoka Makao Makuu ya Jeshi hilo Zanzibar kwa ajili ya wafanyakazi lakini bidhaa hizo hazikuingizwa katika daftari la kuhifadhia bidhaa za ghalani, aidha ukaguzi haukubaini kuwepo kwa kadi ya mapokezi ya bidhaa hizo (delivery note)

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo kutokuthibitika kisheria, aidha ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi

na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kufuata miongozo ya kisheria kiukamilifu ikiwemo kurikodi bidhaa za ghalani katika daftari la kuhifadhia bidhaa hizo kabla ya kutumika. Mchanganuo wa bidhaa hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 51: Kutokufuatwa kwa utaratibu za mapokezi na utoaji wa bidhaa za ghalani**

| Namba | Aina ya Chakula | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Sembe | 120 pcts |
| 2. | Sukari | 10 pcts |
| 3. | Tomato past | 17 ktns |
| 4. | Mafuta ya kula | 8 dum |
| 5. | Mchele | 59 pcts |

**Majibu ya Uongozi wa JKU**

Jeshi la Kujenga Uchumi linafuata kikamilifu sheria nambari11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za uma ya mwaka 2016 pamoja na sheria Nambari 12 ya Usimamizi ya Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Katika utekelezaji wa sheria hizo JKU inapokea bidhaa kutoka Makao Makuu Unguja kwa kufuata utaratibu wa sheria ikiwemo kuingizwa katika daftari la kuhifadhia bidhaa za ghalani na kwenye kadi ya mapokezi ya bidhaa (Delivery) hivyo basi kutokana na ukweli huo hakuna bidhaa ambazo zimepokelewa bila kufuata utaratibu kama ilivyodaiwa katika kitabu cha CAG 21/22.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kwamba ni kweli kasoro zilizoelezwa na Mkaguzi katika ripoti yake zilikuwepo ambapo Kamati baada ya kuviulizia vielelezo hivyo ilielezwa kwamba ‘delivery note’ shughuli zake zote zinafanyika Unguja. Kwa msingi huo, vielelezo navyo vilikuwepo Makao Makuu yao (Unguja).

Kamati haikuridhishwa na majibu hayo kwa vile uwezekano wa kupatikana kwake ulikuwepo lakini Makamanda wa JKU walishindwa kuchukua juhudi za kuvifuatilia ili kumpelekea Mkaguzi kabla ya Mkaguzi kuandika hoja hii katika ripoti yake.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa JKU uhakikishe unachukua juhudi za kufuatilia vielelezo vilivyokosekana wakati wa Ukaguzi kwa vile vipo Unguja ili waweze kumpatia Mkaguzi kwa kazi zake za ukaguzi.

## Hoja nambari 6.1.2.4: Kukosekana kwa mikataba ya ununuzi wa bidhaa na huduma shilingi 163,291,347

Kwa mujibu wa kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma itapanga mpago wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususani utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inyoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba imefanya ununuzi wa bidhaa na huduma kwa thamani ya shilingi 163,291,347 kwa wafanyabiashara mbali mbali bila ya kuwepo kwa mikataba ya ununuzi wa bidhaa na huduma hizo kutoka kwa wafanyabiashara hao.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kununuliwa kwa bidhaa na huduma zisizo na ubora na hatimae kupelekea kuwepo kwa upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba kuhakikisha unafuata miongozo na taratibu kama zilivyobainishwa katika kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

### Majibu ya Uongozi wa JKU

Jeshi la Kujenga Uchumi kwa mwaka wa fedha 21/22 limeingia mikataba ya kununua bidhaa na huduma kwa Wazabuni tofauti kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa mafuta JKU iliingia mkataba na Zanzibar Petrolium

Chakula Yes Boss General Supplier

Madawa Magogoni Phamacy

Suala la malipo na ununuzi wa bidhaa na huduma kwa wafanyabiashara wasio na mikataba lilitokana na ugeni kwa Watendeji wetu katika maeneo hayo, pia dhana ya kuwa na bajeti maalumu kwa ajili ya Pemba ilipelekea makosa hayo kutokea.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Zoni ya Pemba haina Mamlaka ya kuingia mkataba na Mtoa huduma yoyote isipokua Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar. Hata hivyo, Kamati ilipofika upande wa Makao Makuu (JKU - Unguja) ilibaini Mikataba hiyo haikuwepo kama alivyoeleza. Kwasasa Kamati imebaini kuwa kasoro hiyo imesharekebishwa ambapo Watoa huduma wanafunga nao Mikataba kama zinavyoelekeza sheria. Hivyo, Kamati imeridhika na hatua zilizochukuliwa na JKU Zanzibar na kuiondoa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa JKU - Pemba uhakikishe kwamba unafuata taratibu zote za manunuzi hususan za kuwapatia mikataba Watoa huduma wanaowapatia huduma mbali mbali.

## Hoja nambari 6.1.2.5: Dosari katika umiliki wa vyombo vya moto

Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba linamiliki vyombo mbali mbali vya usafiri kwa ajili utekelezaji wa shughuli za kikosi kwa mujibu wa utaratibu.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imebainka uwepo wa dosari mbali mbali ambazo zinaweza kupelekea kulinyima jeshi fursa za umiliki wa vyombo hivyo ikiwa dosari hizo hazikufanyiwa kazi na kusimamiwa kwa misingi ya Sheria na taratibu zilizopo. Miongoni mwa dosari hizi ni kama ifuatavyo:-

- Umiliki wa vyombo vya moto vya Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba kusajiliwa kwa jina la mtu binafsi na kuwekewa namba za jeshi.
- Kutokukatiwa kwa bima kwa vyombo hivyo.
- Kutokujulikana kwa mmiliki halali wa vyombo hivyo.
- Kukosekana kwa mpango maalumu wa matengenezo wa vyombo hivyo.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa mali za Serikali kwa kuchukuliwa au kuuzwa pasi na kujuwa mali hiyo ilipo aidha ni kwenda kinyume na Sheria nambari 6 ya Afisi ya msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba kuhakikisha mali zote

zinasajiliwa kwa jina la kikosi pamoja na kuwepo kwa umiliki halali wa mali hizo kwa mujibu wa Sheria.

Aidha, uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi ni vyema kufuata utaratibu wa kuzihaulisha mali hizo kutoka katika jina la mmiliki binafsi na kuwa katika jina la umiliki wa Jeshi ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza baina wa wananchi na Jeshi. Mchanganuo wa vyombo hivyo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 53: Dosari katika umiliki wa vyombo vya moto**

.

| Namba | Aina ya Gari | Jina la Umiliki | Namba ya Usajili | Namba Inayotumika |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Prado S/Wagon | Rashid Moh'd Soud | Z 912 FY | JKU 140 |
| 2. | Coaster Bus | Mariam Shabani Chavala | Z 593KA | JKU 150 |
| 3. | Suzuki Escudo | Kombo Ali Hamdu | Z164JA | JKU 143 |
| 4. | Mazda | Ali Azizi Ali | Z387GJ | JKU141 |
| 5. | Carry Suzuki | Taarifa za umiliki zimekosekana | Z971 JG | Nambari haikupatikana |

**Majibu ya Uongozi wa JKU**

Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar tayari linaendelea kuzipatia ufumbuzi dosari hizi ambapo hatua za kuomba kubadilishiwa majina ya umiliki na kukatia bima tayari zimeshachukuliwa. Aidha, Mpango maalumu wa mategenezo wa vyombo umeandaliwa na unafuatwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Jeshi la Kujenga Uchumi – Zoni ya Pemba kueleza kwamba imechukua juhudi za kurekebisha kasoro hizo. Hata hivyo, Kamati ilitaka kupatiwa kielelezo (barua) inayothibitisha kwamba wameomba kubadilishiwa umiliki wa vyombo vyao vya moto lakini hadi Kamati inakamilisha kazi zake za kiuchunguzi, haikuweza kupaitiwa kielelzo hicho. Kwa msingi huo, Kamati haikuridhika na majibu ya hoja hii na kupelekea hoja hii kubakia ili Mkaguzi aweze kufuatilia utekelezaji wake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Uongozi wa JKU Zoni ya Pemba kuhakikisha mali zote zinasajiliwa kwa jina la kikosi pamoja na kuwepo kwa umiliki halali wa mali hizo kwa mujibu wa Sheria.

## Hoja nambari 6.1.2.6: Dosari katika ukusanyaji na matumizi ya mapato shilingi 291,151,575.41

Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba limetekeleza majukumu yake ya ulinzi katika vituo mbali mbali vya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo jumla ya shilingi 291,151,575.41 zimelipwa kama ni malipo ya deni lililokuwa linadaiwa kwa muda mrefu kutokana na huduma ya ulinzi katika Afisi ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari mbali mbali za kiutendaji ambazo zimepelekea kutokufuatwa kwa Sheria na miongozo mbali mbali ya Usimamizi wa fedha za Umma. Miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatazo:-

> Kutokuwepo kwa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kutokuingizwa kwa fedha za makusanyo katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Kufanya matumizi kwa fedha za mapato nje ya bajeti. Kukosekana kwa idhini (muongozo) ya matumizi kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali jambo ambalo linaweza kupelekea kukwamisha kwa jitahada za Serikali katika usimamizi wa makusanyo ya makadirio na matumizi ya mapato.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea uwepo wa upotevu wa fedha za Umma zinazotokana na kufanya matumizi kusikozingatia Sheria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba kuhakikisha unafanya matumizi kulingana na bajeti husika au kuomba idhini kwa mlipaji mkuu wa Serikali.

Mchanganuo wa makusanyo na matumizi hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 54: Makusanyo na matumizi ya mapato kinyume na sheria**

| Namba | Mwezi | Kiasi cha fedha kilichokusanywa na kutumika (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Julai 2021 | 14,823,963 |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Agosti 2021 | 11,280,000 |
| 3. | Septemba 2021 | 11,709,680 |
| 4. | Oktoba 2021 | 6,705,000 |
| 5. | Novemba 2021 | 13,046,920 |
| 6. | Disemba 2021 | 25,435,320 |
| 7. | Januari 2022 | 4,400,000 |
| 8. | Februari 2022 | 7,220,760 |
| 9. | Machi 2022 | 17,097,660 |
| 10. | Aprili 2022 | 804,400 |
| 11. | Mei 2022 | 14,171,792 |
| 12. | Juni 2022 | 164,456,080 |
| **Jumla** | | **291,151,575** |

### Majibu ya Uongozi wa JKU

Jeshi la Kujenga Uchumi lina Miradi mingi ya uzalishaji ikwemo Kilimo na Ufugaji. Mapato yanayotokana na Miradi hiyo yanatumika kuendeleza Miradi husika na faida inayopatikana inapelekwa Serikalini kupitia Mfuko wa Hazina.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imepokea majibu ya Uongozi wa JKU Zoni ya Pemba. Aidha, Kamati haikupata vielelezo na maelezo ya kutosha ya kuweza kuiondoa hoja hii.

## 4.0 UKAGUZI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA FEDHA ZA MKOPO WA AHUENI YA UVIKO-19 ZANZIBAR

## 4.3 MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA YA AFYA

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga fungu maalum la utekelezaji wa miradi mbali mbali katika Sekta ya Afya ikiwemo kujenga na kukarabati Hospitali za Mikoa na Wilaya, kutoa huduma za matibabu na vifaa muhimu pamoja na kuzipatia Hospitali hizo gari za kubebea wagonjwa. Aidha, ujenzi wa Hospitali kumi (10) za Wilaya na moja (1) ya Mkoa umesaidia kwa kiasi kikubwa Sekta ya Afya kupunguza msongamano wa wagonjwa na kuboresha upatikanaji wa huduma za matibabu, jambo ambalo litapelekea kuboresha mfumo mzima wa huduma ya afya nchini.

### Hoja Nambari 4.3.1.1: Malipo ya ziada yaliyolipwa awali kwa Mkandarasi shilingi bilioni 3.28

Wizara ya Afya ilifunga mkataba na Mkandarasi Ms Estim Construction Company Ltd tarehe 7 Januari 2022 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya Mkoa iliyopo Lumumba Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja kwa thamani ya shilingi bilioni 24.72 pamoja na VAT.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 25 cha masharti maalum ya mkataba huo, Wizara ya Afya ilitakiwa kulipa kiasi cha malipo ya awali ya asilimia 20 ya jumla ya fedha za mkataba kwa Mkandarasi. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa malipo ya awali ya shilingi bilioni 7.66 sawa na asilimia 35 jambo ambalo limepelekea uwepo wa malipo ya ziada ya asilimia 15 sawa na shilingi bilioni 3.28 kinyume na makubaliano ya mkataba.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya uzingatie vifungu vya mkataba ili kuepusha kuingiza hasara Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hali halisi ya malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 6: Malipo ya ziada yaliyolipwa awali kwa Mkandarasi**

| Maelezo | Kiasi cha Fedha (Tshs) |
|---|---|

| | |
|---|---|
| Contract sum VAT inclusive | 24,717,192,531.32 |
| Less: 15% VAT | 3,223,981,635.00 |
| VAT Contract price VAT Exclusive | 21,493,210,896.52 |
| Less: PC and Provisional Sum | 2,450,130,000 |
| Contract sum excluding Provisional sum | 19,043,080,896.32 |
| Advance payment (19,043,080,896.32 x 35%) | 6,665,078,313.71 |
| Add: 15% VAT Amount | 999,761,747.06 |
| Total advance amount paid (A) | 7,664,840,060 |
| Amount supposed to be paid (Tshs) | |
| Contract sum VAT inclusive | 24,717,192,531.32 |
| Less: 15% VAT | 3,223,981,635.00 |
| Contract price VAT Exclusive | 21,493,210,896.52 |
| Less: PC and Provisional Sum | 2,450,130,000 |
| Contract sum excluding Provisional sum | 19,043,080,896.32 |
| Advance payment (19,043,080,896.32 x 20%) | 3,808,616,179.30 |
| Add: 15% VAT Amount | 571,292,426.89 |
| Total advance amount to be paid (B) | 4,379,908,606.19 |
| Amount Overpaid (A – B) | 3,284,931,454 |

Chanzo: Faili za Mkataba

## Majibu ya Uongozi wa Wizara

Ni kweli katika mkataba mkandarasi alitakiwa kulipwa advance payment ya 20% ya thamani ya mkataba, ila wakati wa utekelezaji kutokana na uharaka wa kazi, ikaonekana kuwa mkandarasi anahitaji kulipwa 35% kama advance payment ili kuharakisha kazi kama ilivyotakiwa. Hata hivyo malipo yote hayo ya 35% yaliwekewa bank guarantee ya thamani husika. (Advance payments guarantee imeambatanishwa).

Pia Kipindi cha makubaliano ya kimkataba, Mkandarasi aliiomba Wizara kumpatia asimilima 35 badala ya 20 kutokana na uharaka wa mradi huo ili kuwawezesha kununua vifaa nje ya Nchi ambapo makubaliano hayo yaliwekwa kwenye kumbukumbu za mkataba huo. (Kopi ya kikao cha negotiation imeambatanishwa)

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa makubaliano yaliyofanyika mara ya pili ya kubadilisha gharama za malipo ya awali kwa Mkandarasi kwamba alipwe asilimia 35 na sio asilimia 20 hayakufuata masharti yaliyoainisha katika mkataba kwani uongozi wa Wizara ya Afya ulishindwa kubadilisha masharti ya

makubaliano Mkataba wa mara ya pili ili kuweka sawa masharti ya mkataba wa awali. Hali hiyo imepelekea kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Kwa mantiki hiyo, Kamati ya PAC haikuridhika na majibu ya hoja hii na hatimae hoja imebakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa Wizara ya Afya uhakikishe unatekeleza masharti ya mikataba katika utekelezaji wa Miradi yao ya Maendeleo ili matumizi mabaya ya fedha za Serikali.
2. Uongozi wa Wizara ya Afya uwashirikishe wataalamu wote wanaohusika na utekelezaji wa Miradi wanayoifanyia kazi ili ufanisi uweze kupatikana na kuondoa hoja zisizokuwa za lazima.

## Hoja Namabari 4.3.1.2: Malipo ya kazi ambayo hayajaidhinishwa na Bodi ya Zabuni na Mlipaji Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 1.04

Wizara ya Afya ilifunga mkataba na Mkandarasi Bi. Rans Company Ltd tarehe 15 Januari 2022 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe iliyopo Mkoa wa Magharibi “A” Unguja kwa thamani ya shilingi bilioni 5.07 pamoja na VAT.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Afya ilisaini mkataba wa nyongeza (addendum No.1) wa kazi za ziada tarehe 11 Novemba 2022 wenye thamani ya shillingi bilioni 1.037 sawa na asilimia 20.5 ya Mkataba wa awali bila ya kupata kibali kutoka Bodi ya Zabuni na Mlipaji Mkuu wa Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na Kanuni ya 49 (4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2020.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha malipo yoyote ya kazi ya ziada yaliyozidi asilimia 20 yanawasilishwa kwa Bodi ya Zabuni pamoja na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa lengo la kutolewa ushauri ili kuepusha kufanyika kwa malipo ya ziada ambayo huenda yakapelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Aidha, ni vyema kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa ujenzi ili kuepuka kujitokeza kwa gharama za ziada ambazo huenda zikapelekea kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara inathibitisha kwamba malipo yote ya kazi za ziada yalipelekwa kwenye Bodi ya Zabuni ya Wizara na kuidhinishwa kupitia kikao nambari 03/2022/23 cha tarehe

20/09/2022. Aidha kazi hizo za ziada zilifanyiwa maombi kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kupitia barua ya Wizara ya tarehe 7/11/2022 yenye kumb. Nambari CB.244/274/01/10 (Angalia vielelezo).

Maombi ya matumizi ya fedha ya ziada katika miradi ya ahueni ya UVIKO-19 yalipelekwa Wizara ya fedha sio tu kwa Mradi wa Mwera Pongwe bali miradi yote ya Ujenzi wa Hospitali za Wilaya.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kutafuta ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imegundua mambo yafuatayo:-

1. Mkaguzi hakupatiwa uthibitisho wa barua ya ruhusa ya kuendelea na kazi za ziada kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, Kamati ilifanikiwa kupatiwa uthibitisho huo wa barua ya ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali yenye kumbukumbu nambari AB.2/282/01/10/50 ya tarehe 18 Oktoba 2023.
2. Kuchelewa kupatikana kwa majibu ya barua kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu kuombwa nyongeza ya matumizi ya fedha za ziada za ujenzi wa Mradi huo. Hata hivyo, uongozi wa Wizara ulichukua maamuzi ya kutekeleza Mradi bila ya kupatikana ruhusa hiyo. Kamati, katika uchunguzi wake ilibaini kuwa barua ya majibu ilikuwa imeshapitwa na wakati kwa kipindi cha mwaka mzima bila ya kupata majibu ya idhini ya matumizi ya fedha za asilimia 20 zilizoongezeka.
3. Kamati imebaini ongezeko la asilimia 20 ya kazi za ziada imetokana na sababu mbali mbali ikiwemo eneo la mradi kujengwa ukuta, ‘landscape’ pamoja na kuinua msingi wa jengo. Mambo ambayo hayakuwemo katika Makubaliano ya awali ya Mkataba.
4. Kutokuwepo kwa mashirikiano ya karibu ya kiutendaji hasa ukizingatia kwamba watendaji wa Wizara ya Afya walishindwa kufuatilia majibu ya barua ya ruhusa kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.
5. Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu wa Mradi huo na kusababisha ongezeko katika matumizi ya fedha ziada.

Kufuatia majibu yasiyoridhisha ya Wizara ya Afya, kamati haikuridhika na majibu yaliyowasilishwa na kupelekea hoja hii kubakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati inapendekeza kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa ujenzi ili kuepuka kujitokeza kwa gharama za ziada ambazo huenda zikapelekea kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati.
2. Uongozi wa Wizara ya Afya uftuatilie kwa makini utekelezaji wa maombi ya barua zao ili ziweze kupata majibu kwa wakati.
3. Uongozi wa Wizara ya Afya uandae utaratibu maalum utakaotumika kutoa mashirikisano kwa Mkaguzi hususan wakati wa kuwasilishiwa vielelezo/vithiibitisho.

## Hoja Nambari 4.3.1.3: Kutokulingana kwa bei ya mkataba shilingi 92,720,245

Ukaguzi ulipitia nyaraka za makubaliano ya Mkataba, Barua ya makubaliano ya kuanza kazi, pamoja na muhtasari wa kikao cha mazungumzo baina ya Mkandarasi na Uongozi wa Wizara ya Afya yaliyofanyika kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Pangatupu Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja, ukaguzi umebaini kutokulingana kwa bei ya mkataba kwa mujibu wa makubaliano hayo.

Kwa mujibu wa kikao cha tarehe 14 Disemba 2021 kifungu nambari (ix) cha mkataba kilibainisha gharama za ujenzi ni shilingi 4,385,864,538 ambapo kwa mujibu wa barua aliyopewa mkandarasi ya tarehe 14 Disemba 2021 ilinakili kifungu cha (ii) cha mkataba gharama za ujenzi huo ni shilingi 4,478,584,783. Vile vile, makubaliano ya mkataba yaliyosainiwa tarehe 15 Disemba kifungu nambari (i) cha mkataba huo kilibainisha gharama za ujenzi ni shilingi 4,478,584,783.

Kutokana na kutofautiana kwa kiasi cha fedha kilichobainishwa kinaweza kikapelekea uwepo wa migogoro au kutokufahamiana wakati wa kufanyika kwa malipo jambo ambalo wakati wa kikao cha mazungumzo ilikubaliwa kuwa kiasi cha fedha kilichobainishwa katika mkataba kitazingatiwa, dosari iliyobainika kiasi hicho hakikuoneshwa kwa usahihi katika nyaraka za makubaliano ya mkataba. Hata hivyo, kiasi kilichoainishwa katika fomu ya makubaliano ya mkataba haikuwa bei ya mazungumzo na kupelekea kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 92,720,245.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wiraza ya Afya kuwa makini wakati wa uandaaji wa makubaliano wakati wa mazungumzo (Letter of acceptance) na kuhakikisha wanasaini kile walichokubaliana kwenye mkataba husika ili kuepusha migongano inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mkataba husika.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hata hivyo Kiwango halisi cha mkataba huo ni 4,478,584,783, tofauti iliyojitokeza ni kutokana na makosa ya kiuandishi yaliyosomeka kwenye kifungu nambari (ix).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilifanikiwa kupitia Mkataba uliokuwepo na kushindwa kujiridhisha na makosa hayo ya kiundaishi kwani tofauti ya fedha iliyojitokeza ya 92,720,245 ilikuwa ni kubwa mno ambapo kiutaratibu wa kimahesabu haikubaliki kujitokeza kosa kama hilo. Kwa msingi huo, licha ya Uongozi wa Wizara kukubali lakini Kamati haikuridhika na majibu ya hoja hiyo na hoja hiyo imebakia.

**Maoni, ushauri na Mapendekezo ya kamati ya PAC**

Uongozi wa Wiraza ya Afya uwe makini hususan wakati wa uandaaji wa makubaliano na uhakikishe wanasaini kile walichokubaliana kwenye mkataba husika ili kuepusha migongano inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mkataba husika.

## Hoja Nambari 4.3.1.4: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kushirikishwa Idara husika (user department) shilingi 48.59 bilioni

Ukaguzi umebaini Wizara ya Afya imefanya manunuzi ya bidhaa mbali mbali zenye thamani ya shilingi bilioni 48.59 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya za Unguja na Pemba ambapo manunuzi hayo yalifanyika kupitia maafisa manunuzi wa Wizara bila ya kushirikishwa idara husika za watumiaji jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha 31 (1)(b) na (c) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali ya Umma nambari 11 ya 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unazingatia na kufuata matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya 2016 kwa lengo la kupatikana uwazi, uwajibikaji na thamani halisi ya fedha.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara inakiri kufanya manunuzi ya bidhaa mbali mbali zenye thamani ya shilingi bilioni 48.59 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya za Unguja na Pemba ambapo manunuzi hayo yalifanyika kupitia maafisa manunuzi wa Wizara. Aidha, maandalizi ya orodha na sifa (Technical Specifications) yalifanywa na Idara ya Tiba ambayo ndio Idara tumizi

(User Department) na pia walishiriki katika kazi ya tathmini ya vifaa hivyo kama inavyonekana katika viambatanisho

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini Wizara ilifanya ununuzi mbali mbali na Idara husika ya Manunuzi ilishirikishwa. Hivyo, Kamati ilihitaji kupatiwa dokezo ambalo linatoka kwa muhasibu kwenda kwa Afisa Manunuzi ili kuthibitisha ushirikishwaji wao. Kamati iliridhika na majibu ya hoja baada ya kupitia dokezo hilo na kuamua kuiondoa hoja hiyo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba Watendaji wa Wizara hawakutoa mashirikiano ya kutosha kwani walishndwa kumpatia vielelezo Mkaguzi na kupelekea kuiandika hojahii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara ya Afya wawe wanatoa mashirikiano ya kutosha kwa Wakaguzi hususan wanapofika katika Ofisi zao kutekeleza majukumu yao.

## Hoja Nambari 4.3.1.5: Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi shilingi milioni 656.69

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wizara ya Afya imesaini hati ya makubaliano ya mkataba na HAB Consultant Ltd tarehe 15 Novemba 2021 kwa thamani ya shilingi milioni 656.69 kwa ajili ya kupata huduma ya ushauri wa kusanifu michoro, hati ya zabuni na Sheria ya Viwango (BOQ) wakati wa ujenzi wa Hospitali ya Mkoa - Lumumba.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutumia njia ya nukuu moja ya manunuzi (single source procurement) bila ya kupatiwa sababu zilizosababisha kutumia njia hiyo jambo ambalo linaweza likapelekea kujitokeza kwa matumizi ya gharama kubwa zaidi bila ya kuwepo kwa ushindani wa bei halisi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 79(2) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali ya Umma nambari 11 ya 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya manunuzi kwa mujibu wa matakwa ya sheria, vyenginevyo kuwe na sababu za msingi zitakazopelekea ukiukwaji wa matakwa ya msingi ya kifungu nilichokinakili hapo juu.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara inakiri kuingia makubaliano ya mkataba na kampuni ya HAB Consultant Ltd kwa kutumia njia ya nukuu moja ya manunuzi (single source procurement). Hii ilitokana na

muda mdogo wa mradi wa UVIKO -19 (miezi 9 tu) na lengo la Serikali ilikuwa ni kujenga Hospitali ya ghorofa 6 ndani ya muda huo. Hivyo Kampuni ya Hab Consult ndiyo iliyochora mchoro wa Hospitali kama hiyo iliyojengwa huko Tabata Dar es Salaam, hivyo ikaonekana muda ataotumia utakuwa mdogo na utaendana na uharaka wa kazi hiyo. (Angalia kielelezo).

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Uongozi wa Wizara ya Afya kukubaliana na hoja ya Mkaguzi kwamba ni kweli kulikuwepo ukiukwaji wa taratibu za manunuzi hususan wa kutumia njia ya nukuu moja ya manunuzi (single source procurement) bila ya kuwepo kwa sababu za msingi au kuomba ruhusa kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma. Kwa msingi huo, Kamati ya PAC haikuridhika na majibu ya hoja na hoja imebakia.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Wizara ya Afya uhakikishe unafanya ununuzi kwa mujibu wa matakwa ya sheria, vyenginevyo kuwe na sababu za msingi zitakazopelekea ukiukwaji wa matakwa.

## Hoja Nambari 4.3.1.6: Mkataba uliotolewa kwa Kampuni zilizozuiliwa kutoa huduma Zanzibar (Blacklisted Companies) shilingi bilioni 4.98

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba BLM/30/M/C.35/78 ya tarehe 16 Disemba 2021 kutoka Baraza la Mapinduzi kwenda kwa Mhe. Waziri wa Afya pamoja na mambo mengineyo yaliyojadiliwa katika kikao cha Baraza la Mapinduzi kilichofanyika tarehe 15 Disemba 2021 kikao hicho kilipitia na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa matumizi ya fedha za mkopo wa dharura kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) na kuiagiza Wizara ya Afya.

"Ihakikishe kuwa haitowi zabuni kwa Kampuni ya Group Six International Limited na Kampuni ya Hainan ambazo hazina sifa nzuri katika utekelezaji wa miradi yake hapa Zanzibar. Aidha, kikao hicho kiliagiza Wizara ya Afya ihakikishe kuwa kiasi kikubwa cha fedha za mkopo wa dharura kutoka IMF zinatumika hapa nchini kwa kuwapa kazi Wakandarasi wa ndani ambao wamekidhi vigezo".

Ukaguzi wangu umebaini Wizara ya Afya imesaini hati ya makubaliano (Mkataba) na Kampuni ya Group Six International Limited tarehe 15 Disemba 2021 wenye thamani ya shilingi bilioni 4.98 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kinyasini, Wilaya ya Wete Pemba jambo ambalo ni kwenda kinyume na utekelezaji wa maamuzi ya kikao halali cha Baraza la Mapinduzi.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unatekeleza mambo yafuatayo kabla ya kutoa zabuni: -

- Kujiridhisha juu ya ubora, viwango na ufanisi wa kazi zinazofanywa na wazabuni kabla ya kuingia nao mikataba ya utoaji wa huduma hiyo ili kuepusha kuwapa kazi wazabuni ambao wamepoteza sifa (blacklisted companies) za ufanyaji wa kazi husika.
- Kuhakikisha inatoa zabuni kwa Kampuni za ndani zilizokidhi vigezo kwa lengo la kuzinyanyua Kampuni hizo na kutengeneza mzunguko mzuri wa fedha ndani ya nchi.
- Kutekeleza maagizo halali ya Serikali na pindipo itakapobainika maagizo hayo hayatekelezeki ni vyema kwa Taasisi za Umma kurudi Serikalini kwa lengo la kupata ushauri elekezi ili kuepusha kujitokeza kwa mgongano wa maamuzi na hatimae kuitia hasara Serikali kwa kutekeleza miradi isiyokuwa na ubora.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara ya Afya

Wizara inakiri kupokea barua yenye kumbukumbu namba BLM/30/M/C.35/78 ya tarehe 16 Disemba 2021 kutoka Baraza la Mapinduzi iliyotutaka kutoa zabuni kwa Kampuni ya Group Six International Limited na Kampuni ya Hainan ambazo hazina sifa nzuri katika utekelezaji wa miradi yake hapa Zanzibar. Hata hivyo, Wizara ilianza Mchakato wa zabuni za ujenzi wa Hospitali 10 za Wilaya mnamo tarehe 10 Novemba 2021 na kufikia kusaini mikataba tarehe 15 Disemba 2021. Barua hii iliyotoka Baraza la Mapinduzi ilimfikia Mheshimiwa Waziri tarehe 22 Disemba 2021 muda ambao tulishasaini mkataba na Kampuni zote za ujenzi huo ikiwemo Group Six International Limited. Kwa hivyo, agizo hili tumelichukuwa na kulitekeleza ila kwa mkataba huu tulishachelewa. Kuanzia hapo mradi uliofuata ulikuwa ni ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba Kampuni hii ilikuwa ndiyo iliyoleta bei ndogo na kukidhi vigezo vya zabuni lakini katika kutekeleza agizo hili Wizara haikuweza kumpa kazi hiyo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya kutolewa kwa agizo kutoka Baraza la Mapinduzi lenye kumbukumbu namba BLM/30/M/C.35/78 ya tarehe 16 Disemba 2021 kuhusiana na kuzuiliwa kwa Kampuni za Group Six International Limited na Kampuni ya Hainan kutoa huduma Zanzibar (Blacklisted Companies). Kamati ya PAC imechukua juhudi ya kufuatilia ukweli wa hoja hii kwa kuiandikia barua Bodi ya Usajili wa Wakandarasi Zanzibar ya tarehe 30 Januari, 2024 yenye kumbkumbu nambari CE.81/204/02/36 ili kuweza kujua kama kweli Kampuni

hizo zilizuiliwa au zimezuiliwa kufanyakazi Zanzibar.

Lakushangaza, Kamati imebaini kwamba Bodi hiyo haina taarifa yoyote kwamba Kampuni hizo zimezuiliwa kufanya kazi Zanzibar kwani bado zinaendelea na usajili ambao unatambulika na Bodi hiyo. Hili linathibitisha kwamba baadhi ya Wizara/Taasisi za Serikali hushindwa kuyachukulia hatua ya kufuatilia utekelezaji wake. Ni matumaini ya Kamati kwamba mara tu baada ya kutolewa agizo hilo na Baraza la Mapinduzi, Wizara/Taasisi husika ilitakiwa kuwasilisha ombi maalum kwa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi kuhusiana na uzuiaji wa Kampuni hizo kwa maslahi ya umma.

Kutochukuliwa hatua agizo hilo, kunapelekea hoja hii kuendelea kubakia kwa ufuatiliaji zaidi.

**Maoni, ushauri na Mapendekezo ya kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha inatoa zabuni kwa Kampuni za ndani zilizokidhi vigezo kwa lengo la kuzinyanyua Kampuni hizo na kutengeneza mzunguko mzuri wa fedha ndani ya nchi.
2. Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuwa makini juu ya ubora, viwango na ufanisi wa kazi zinazofanywa na wazabuni kabla ya kuingia nao mikataba ya utoaji wa huduma hiyo ili kuepusha kuwapa kazi wazabuni ambao wamepoteza sifa (blacklisted companies) za ufanyaji wa kazi husika.
3. Wizara ya Afya ihakikishe inatekeleza maagizo yanayotolewa na Serikali kivitendo ili kuondokana na utekelezaji usiokuwa na tija kwa umma utakaopelekea hoja za Mkaguzi kujitokeza.

## Hoja Nambari 4.3.1.7: Ukiukwaji wa maamuzi ya kikao cha Kamati ya Tathmini

Kwa mujibu wa taarifa za kikao cha Tathmini juu ya zabuni zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa LOT No. 5, 7, 8 na 10 zilibainisha gharama ya utekelezaji wa miradi hiyo ni shilingi bilioni 18.985.

Aidha, Wizara ya Afya ilishindwa kutekeleza maamuzi ya kikao halali cha Kamati ya Tathmini kwa bei elekezi iliyotolewa na kamati hiyo badala yake ilikuja na maamuzi ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa gharama ya shilingi bilioni 19.940 jambo ambalo limepelekea kuisababishia Serikali hasara ya shilingi milioni 955.559 kutokana na kukiukwa kwa maamuzi ya kikao hicho.

Ukiukwaji wa maamuzi halali ya kikao cha kamati ya tathmini bila ya uwepo wa sababu

za msingi za kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 138 (1) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2020.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuwa makini katika utoaji wa zabuni ili kuepusha kuibebesha mzigo usiokuwa wa lazima Serikali pamoja na kuheshimu maamuzi ya Kamati ya Tathmini kuzingatia kifungu nambari 138 (1) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2020 wakati wa utoaji wa zabuni. Hali halisi ya utoaji wa zabuni kwa Wakandarasi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 7: Mikataba iliyotolewa kwa Wakandarasi ambayo haijapendekezwa na Kamati ya Tathmini**

| **Aina ya Zabuni** | **Wakandarasi walioshinda zabuni na kupendekezwa na Kamati ya Tathmini** | | **Wakandarasi waliokuwa hawakushinda zabuni na wakapewa zabuni** | | **Upotevu wa fedha (Tshs** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Jina la Mkandarasi** | **Thamani ya Mkataba (Tshs)** | **Jina la Mkandarasi** | **Thamani ya Mkataba (Tshs)** | |
| Lot -5<br><br>Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini "B" Kivunge | M/S Ltd WCECL | 4,495,819,763 | MAZRUI<br><br>Building Construction | 4,854,044,141 | 358,224,378 |
| Lot -7<br><br>Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kati - Mwera Pongwe Unguja | M/S Ltd CRJE | 4,720,856,520 | RANS Company | 5,071,148,905 | 350,292,384 |
| Lot– 8<br><br>Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Wete - Kinyasini Pemba | M/S Mack Engineering | 4,806,492,438 | Group Six International | 4,976,732,967 | 170,240,529 |
| Lot -10 | M/S | 4,961,866,940 | SALEM | 5,038,669,138 | 76,802,198 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake – Vitongoji Pemba. | Group Six International | | Construction | | |
| **Jumla** | | **18,985,035,661** | | **19,940,595,151** | **955,559,489** |

Chanzo: Ripoti za tathmini na faili za manunuzi

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imeupokea ushauri na kuufanyia kazi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha cha kuwepo kwa nia njema ya kutaka kuwasaidia Wakandarasi Wazawa kiuchumi hususan katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo ndani ya Zanzibar, hata hivyo, taratibu stahiki za kuwawezesha Wakandarasi hao hazikufuatwa, Kamati ililithibisha hilo kwa kuwataka Watendaji wa Wizara ya Afya kuwasilisha mbele ya Kamati Ripoti ya Kamati ya Tathmini ili kubaini kama kuna sababu au maelekezo hayo lakini kwa bahati mbaya haikuweza kuziona sababu hizo badala yake Wizara iliamua kuchukua hatua za kuwapatia kazi Wakandarasi Wazawa pasi na kufuata utaratibu wa kurudi katika Kamati ya Tathmini. Hivyo, Kamati haikuridhika na majibu ya Wizara na kukubaliana na hoja ya Mdhibiti na hatimae hoja inabakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa Wizara ya Afya uwe makini katika utoaji wa Zabuni ili kuepusha kuibebesha mzigo usiokuwa wa lazima Serikali.
2. Watendaji wa Wizara ya Afya wahahkikishe wanafuata na kuheshimu maamuzi ya Kamati ya Tathmini ili uhalali wa utekelezaji wa Miradi yao uweze kupatikana.

## Hoja Namabari 4.3.1.8: Ukosefu wa machomeo ya Taka Ngumu (incinerators) katika Hospitali zote za Wilaya na Hospitali ya Mkoa - Lumumba

Kwa mujibu wa Kiambatisho cha 2 (b) uk. 59 - 72 cha Viwango vya Msingi vya Vifaa vya Afya vya Machi 2015 toleo la 3, Hospitali ya mkoa inatakiwa kuwa na kichomea cha

teknolojia ya juu kwa ajili ya kudhibiti taka. “According to Annex 2 (b) p.59-72 of the Basic Standards of Health Facilities of March 2015 Volume 3, the regional hospital is required to have a high technology incinerator for waste management”.

Ukaguzi ulitembelea na kufanya mahojiano na wahusika pamoja na kujiridhisha kutokana na michoro iliyochorwa pamoja na BOQ, umebaini hakukuwa na eneo lililojengwa maalum kwa ajili ya vifaa vya kuchomea taka katika Hospitali zote za Wilaya zilizojengwa na Hospitali moja ya Mkoa Lumumba. Hata hivyo ujenzi wa machomeo ulibuniwa katika Hospitali za mikoa lakini Wakandarasi waliagizwa kutojenga badala yake kujengwe eneo maalum ambalo litakuwa kati kati baina ya Hospitali zote kuweza kulitumia kama ni chomeo la taka hizo.

Ukaguzi unashauri Serikali kupitia Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba inazingatia muongozo wa afya duniani kwa lengo la kuzipandisha hadhi ya Kimataifa Hospitali zote za Wilaya na Mkoa zilizojengwa ili kuepusha kujitokeza kwa mrundikano na kuzagaa kwa taka ngumu pindipo patakapojitokeza changamoto ya kuharibika au kuzisafirisha kutoka kituo kimoja kwenda sehemu nyengine kwa sababu mbali mbali zitakazojitokeza.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Mkandarasi kwa ajili ya Centralized Incinerator itakayojengwa eneo la Kibele Zanzibar amepatikana kwa ajili ya ujenzi wa machomeo ya taka ngumu, aidha pia mkandarasi wa kuchimba na kujengea machomeo madogo katika kila hospitali za Wilaya nae amepatikana na tayari ameshaanza kazi hiyo (Mikataba husika).

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ni kweli ‘Centralized Incineration’ ilikuwa bado haijajengwa kwa vile Mkandarasi alikuwa hajapatikana isipokuwa mpango wa kujenga ulikuwepo. Kamati ilipotaka kujua kwanini machomeo hayo hayajajengwa ilielezwa kwamba kulitokea kuchelewa kumpata Mkandarasi mwenye uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hizo.

Hata hivyo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu na hatua zilizochukuliwa na Wizara kwa vile tayari machomeo hayo yameshajengwa hususan katika hospitali za Wilaya na Mkoa. Kutokana na juhudi zilizochukuliwa, Kamati imeridhika na kuiondoa hoja hii.

## Hoja Namabari 4.3.1.9: Mapungufu yaliyobainika katika Usanifu wa Majengo ya Hospitali ya Wilaya

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa mapungufu mbali mbali katika Michoro na BOQ zilizowasilishwa katika ujenzi wa Hospitali za Wilaya zilizojengwa ambapo imebainika kukosekana kwa vipengele muhimu na kulikuwa na mapungufu ya baadhi ya mahitaji maalum jambo ambalo limepelekea kwenda kinyume na kifungu namba 58 (8) cha Sheria ya Usajili ya Wabunifu Majengo, Wahandisi na Wakadiriaji Majenzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2014. Mapungufu hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 8: Mapungufu yaliyobainika katika ujenzi wa Hospitali za Wilaya**

| Namba | Eneo | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|---|
| 1. | Chumba cha X-Ray | Ukuta wa 230mm ulijengwa bila ya kuwekewa karatasi maalum za kuzuwia kupenya kwa mionzi. |
| 2. | Chumba cha kuhifadhia Maiti | Ukosefu wa sehemu maalum ya uchunguzi wa maiti (a post-mortem room) |
| 3. | Sehemu ya Kufulia | Hakuna eneo la kukaushia nguo |
| 4. | Maabara | Milango ya maabara inafunguliwa kwa ndani na hakuna uwekaji wa tabaka juu ya sakafu. |
| 5. | Chumba cha Operation | Milango na madirisha haipitishi hewa ya kutosha, kukosekana kwa sehemu ya kuhifadhia taka za upasuaji, haikuoneshwa katika michoro eneo la uwekaji wa tabaka la juu ya sakafu. |
| 6. | Eneo la Nje | Hakuna mikingo ya jua na mvua katika njia za kutembea. |

Aidha, ukaguzi ulifanya matembezi katika chumba cha X-Ray ambacho ukuta wake una unene 230mm na kubaini ukuta huo haukuwekewa karatasi maalum ya kuzuia kupenya mionzi pamoja na kuwekewa framu ya mlango uliyojengwa kwa mbao ngumu ambayo haifai kuwekwa kwenye chumba cha X-Ray kwa mujibu wa viwango vya afya vya Kimataifa duniani. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini: -

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kukahikisha dosari zilizoainishwa hapo juu zinafanyiwa kazi ili Hospitali hizo ziendane na vigezo vya afya vya Kimataifa ambavyo vitapelekea kupandisha hadhi kwa Hospitali zilizojengwa kwa Unguja na Pemba.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Kufuatia uharaka wa ujenzi wa hospitali za Wilaya na Mkoa, ililazimika kuanza kazi na

kasoro hizo ambazo zilirekebishwa wakati ujenzi unaendelea, Aidha, ukuta ulifanyiwa marekebisho, kuongezewa thickness na kufikia 300mm, pia vyumba vyote vya x-ray katika hospitali za Wilaya zimewekewa lead glass size 600 x 600mm kwenye dirisha na mlango maalum kwa ajili ya chumba hicho ambao nao una kizuia mionzi (lead sheet). Postmterm pamoja na eneo la kukaushia nguo zilikuwepo kwenye design ya awali na zimejengwa kama ilivyopaswa. Vile vile, chumba cha operation hakikupaswa kuwa na madirisha wala milango ya kupitisha hewa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anafanya ukaguzi wake, kulikuwepo changamoto ambazo ameziainisha katika kitabu chake lakini Kamati imejiridhisha kwamba mapungufu hayo tayayri yameshafanyiwa kazi. Hata hivyo, Kamati ilikubaliana na maelezo ya Watendaji wa WIzara kwamba milango na madirisha ya chumba cha 'operation' hayatakiwi kuwa na madirisha wala milango ya kupitisha hewa kama ilivyoelezwa na Mdhibiti kwasababu zitaweza kukwaza ufanisi wa kazi za upasuaji kwa wagonjwa. Kwa mnasaba huu, Kamati imeridhika na majibu ya Wizara na kuiondoa hoja hii.

## Hoja Nambari 4.3.1.10: Kuongezeka kwa gharama za ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba Shilingi 503, 527, 340.

Katika ukaguzi uliofanyika kumebainika uwepo wa ongezeko la gharama za makadirio ya kazi zinazotarajiwa kufanyika kusikolingana na uhalisia wa maandalizi ya BOQ. Hali halisi ya ongezeko hilo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 9: Gharama za ziiada katika ujenzi wa Hospitali**

| Na. | Aina ya Kazi zinazohitajika kufanywa | PC Sum amount | BOQ | Gharama za ziada |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Laundry | 192,794,374 | 60,000,000 | 132,794,374 |
| 2 | Mortuary | 206,903,662 | 170,000,000 | 36,903,662 |
| 3 | Isolation Ward | 325,520,557 | 240,000,000 | 85,520,557 |
| 4 | Guard House | 41,000,000 | 35,000,000 | 6,000,000 |
| 5 | Stabilizer House | 30,636,860 | 20,636,869 | 9,999,991 |
| 6 | Underground water tank | 82,634,780 | 65,000,000 | 17,634,780 |
| 7 | Sewerage/Bio Digester | 209,702,250 | 175,000,000 | 34,702,250 |
| 8 | Solar Hot water System | 247,330,000 | 150,000,000 | 97,330,000 |
| 9 | Medical Gas | 753,013,000 | 700,000,000 | 53,013,000 |
| 10 | Garbage chute | 99,628,726 | 70,000,000 | 29,628,726 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Total** | **2,189,164,209** | **1,685,636,869** | **503,527,340** |

Chanzo: PC ya Mshauri na jumla ya muda na Ref No. HAB/LUM/HOSP/10/2021 tarehe 28 Juni 2022.

Kutokana na jadweli liliopo hapo juu linabainisha ya kwamba ongezeko la gharama limesababishwa na uwepo wa ongezeko la michoro iliyotolewa kwa lengo la kutekelezwa vitu ambavyo havikuweza kupimika kwa wakati wa utayarishaji wa michoro hiyo.

Kutokana na hali hiyo upo uwezekano mkubwa wa kufanyika kwa matumizi kwa kazi ambazo hazikupangwa kufanyika au hazina ulazima kufanyika kwa wakati husika.

Picha ifuatayo inayoonyesha sehemu ya Paa (roof slab) iliyotengenezwa kwa ajili ya chumba cha kuhifadhia maiti kilichojengwa katika Hospitali ya Mkoa – Lumumba ambapo ukaguzi umebaini uwepo wa ongezeko la gharama kutoka shilingi milioni 170 hadi shilingi milioni 206.90 jambo ambalo linaweza kupelekea uwepo wa matumizi mabaya ya fedha yanayokinzana na uhalisia wa makadirio ya BOQ.

Ukaguzi unashauri kwamba Wizara ya Afya ihakikishe inafanya mapitio ya kina ya majengo kama ilivyowasilishwa na Mshauri elekezi ili kuepusha gharama zisizo za lazima.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Uharaka kwenye utekelezaji wa miradi hii ya ahueni ya UVIKO-19 ambao ulimnyima nafasi Mshauri elekezi ya kuandaa BOQ ya jengo hilo na mengineyo kwenye vipimo sahihi na kupelekea kiwango chake kuwa kwenye makisio madogo yaliyowasilishwa kwenye 'Provisional sum'.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa Wtendaji wa Wizara walikosa usimamizi mzuri wa utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa ya Lumumba. Hali iliyopelekea kujitokeza kasoro lukuki na hatimae gharama za ujenzi huo kuongezeka. Kamati imelieleza hilo kwasababu ilihitaji vielelezo kadhaa bila ya mafanikio ikiwemo Ripoti ya Kitaalamu ya tathmini ya utekelezaji wa Mradi huo, Ripoti ya Bodi Zabuni na Ripoti ya 'Site meeting' ya kila hatua ya maendeleo ya ujenzi wa Mradi.

Aidha, Kamati ilishindwa kuthibitisha uwepo wa BOQ ya ujenzi wa shughuli za ziada zilizotekelezwa na Mkandarasi katika Mradi huo. Kwa mantiki hiyo, Kamati haikuweza kuridhika na ongezeko la fedha za Mradi na kushindwa kuiondoa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inaushauri Uongozi wa Wizara ya Afya kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa karibu hususan katika utekelezaji wa Miradi mikubwa ya maendeleo.
2. Uongozi wa Wizara uhakikishe unaandaa michoro iliyokamilika kulingana na mahitaji ya shughuli iliyokusudiwa ili kuepuka kujitokeza gharama za ziada nje ya bajeti iliyotengwa kutekeleza Miradi husika.

ihakikishe inafanya mapitio ya kina ya majengo kama ilivyowasilishwa na Mshauri elekezi ili kuepusha gharama zisizo za lazima.

## Hoja Nambari 4.3.1.11: Kutokuwepo kwa upembuzi yakinifu wa kutosha kabla ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa ya Lumumba

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika hakukuwa na upembuzi yakinifu wa kutosha kubaini asili ya udongo na vipengele vingine vinavyohitajika kabla ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa ya Lumumba. Matokeo yake, kulikuwa na mabadiliko ya muundo wakati wa ujenzi ambayo yalisababishwa na udongo dhaifu uliopatikana katika eneo lililoteuliwa kujengwa Hospitali ya Mkoa.

Kutokana na dosari iliyobainika imepelekea kwenda kinyume na kifungu nambari 2.3 cha Mwongozo wa Upangaji wa Miradi na Majadiliano ya Kuongeza Mikopo, Kutoa Dhamana na Kupokea Ruzuku ya Novemba 2020. (Section 2.3 of Guidelines for Project Planning and Negotiations for Raising Loans, Issuing Guarantees and Receiving Grants of November 2020).

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa miradi ya ujenzi ili kuepusha kuisababishia Serikali kutumia gharama kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo bila ya uwepo wa ulazima wa kufanya hivyo.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Uharaka wa utekelezaji wa Miradi ya Ahueni ya Uviko -19 ilikuwa ni vigumu kufanya upembuzi yakinifu katika kutekeleza Miradi hii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kwa vile masharti ya Shirika la Fedha Duniani (IMF) ilitaka Miradi yote ya fedha za UVIKO - 19 ilipaswa kutekelezwa ndani ya miezi sita

ambapo kitaalamu ili upembuzi upembuzi yakinifu uweze kufanyika ipasavyo, unahitaji kutumia muda wa miezi sita au nane. Aidha, Kamati imegundua kuwa katika Miradi hiyo (COVID - 19) hakukuwemo na fungu la fedha lililotengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu hasa ukizingatia kuwa fedha nyingi huhitajika katika utekelezaji wake.

Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kwa upande wa mchoro wa ujenzi wa hospitali ya Mkoa - Lumumba, Mkandarasi kwa kushirikiana na Wizara walichukua mchoro ya hospitali kama hiyo ilizojengwa Ilala Tanzania Bara ili kupunguza gharama za uandaaji michoro. Sambamba na hilo, Kamati ya PAC imegundua Miradi yote iliyojengwa kwa kupitia fedha za Ahueni ya UVIKO - 19 haikuwa na fungu la fedha za kuwepo kwa Mshauri Elekezi jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa mapungufu mengi katika utekelezaji wake.

Kutokana na changamoto hizo, Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwa vile ni kweli katika ujenzi wa Mradi wa Hospitali ya Mkoa - Lumumba hakukufanyika upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa Mradi huo. Hivyo, hoja hii inaendelea kubakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa miradi ya ujenzi ili kuepusha kuisababishia Serikali kutumia gharama kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## Hoja Nambari 4.3.1.12: Kuchelewa kwa ujenzi wa Hospitali za Wilaya

Kwa mujibu wa barua yenye kumbu kumbu namba BLM/30/M/C.35/78 ya tarehe 16 Disemba 2021 kutoka Baraza la Mapinduzi kwenda kwa Mhe. Waziri wa Afya pamoja na mambo mengineyo yaliyojadiliwa katika kikao cha Baraza la Mapinduzi kilichofanyika tarehe 15 Disemba 2021 kikao hicho kilipitia na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa matumizi ya fedha za mkopo wa dharura kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) na kuiagiza Wizara ya Afya" Ihakikishe kuwa mchakato wa zabuni unakamilika ndani ya mwezi Disemba 2021 na ifikapo Januari 2022 kila mradi uanze utekelezaji wake".

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 1 cha masharti maalum ya mkataba, tarehe ya kukamilika kwa kazi zote ilitarajiwa ndani ya kipindi cha miezi sita tangu kuanza kwa tarehe ya umiliki wa eneo husika.

Ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea miradi yote ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya mnamo tarehe 18 Oktoba, 2022 na kubainika hali halisi ya ujenzi wa Hospitali hizo bado unaendelea katika hatua tofauti jambo ambalo limepelekea uwepo wa nyongeza ya muda wa ukamilishaji wa miradi hiyo ambapo ilitarajiwa kukamilika na kukabidhiwa mnamo

tarehe 31 Agosti 2022. Hata hivyo, hadi ukaguzi unakamilisha ziara ya kutembelea miradi hiyo tarehe 25 Oktoba 2022 hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 10: Hatua zilizofikia katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

| Na. | Aina ya Mradi | Hata iliyofikiwa |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Mjini Magharibi – Lumumba | 69% |
| 2. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kaskazini A –Kivunge | 90% |
| 3. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Magharibi A- Mbuzini | 85% |
| 4. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kaskazini B – Pangatupu | 80% |
| 5. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Chumbuni | 85% |
| 6. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Magharibi B–Magogoni | 92% |
| 7. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kusini – Kitogani | 90% |
| 8. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kati Mwera – Pongwe | 90% |
| 9. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake - Vitongoji | 80% |
| 10. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Wete – Kinyasini | 85% |
| 11. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Micheweni – Micheweni | 85% |

Kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali za Wilaya na ya Mkoa kulitokana na muda usio halisi wa mkataba uliowekwa wa miezi 6 kukamilika kwa ujenzi huo. Hii ilionekana kwenye programu iliyowasilishwa ya kazi za ujenzi wa sakafu ya chini (first floor) pamoja na sakafu ya juu (second floor) ambapo uwiano wa shughuli za kiufundi haukuwa ukilingana. Vile vile, uwepo wa mabadiliko ya vipimo vya muundo (change of design specification) yalisababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo kwa wakati.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unasimamia maamuzi na maelekezo yanayotolewa na Serikali kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo unakamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa, vile vile ni vyema katika utekelezaji wa miradi kwa mara nyengine kuweka muda halisi wa mikataba kabla ya kuanza kwa mradi wowote.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Kiuhalisia muda uliopendekezwa haukuwa sahihi kulingana na ujenzi husika ambao ulikusanya utaalamu mwingi wa huduma tofauti (Service works).

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kuchelewa kwa kumalizika kwa ujenzi wa hospitali kulitokana na mabadiliko ya baadhi ya sehemu ya jengo, ambayo hapo awali Mshauri Elekezi hakushauri katika mchoro ikiwemo miundombinu ya kitelenojia. Aidha, kwa nia

njema ya kujenga, ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nao walikuwa wakitoa maelekezo kadhaa ambayo awali hayakuwemo katika mpango wa ujenzi. Kutokana na kuwepo sababu hizo, Kamati imeridhika na kuiondoa hoja hii.

### Hoja Nambari 4.3.1.13: Kuchelewa kuwasilishwa kwa Gari za Kubebea Wagonjwa (Ambulance) zenye thamani ya shilingi bilioni 1.97

Wizara ya Afya iliingia makubaliano ya mkataba na Kampuni ya Zenj Motors Co. Limited tarehe 5 Aprili, 2022 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.97 kwa ajili ya ununuzi wa magari 12 ya kubebea wagonjwa (Ambulance).

Ukaguzi umebaini mnamo tarehe 1 Juni, 2022 Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya malipo yenye thamani ya shilingi milioni 789.73 sawa na asilimia 40 ya malipo ya awali ya makubaliano hayo. Kutokana na makubaliano ya mkataba Kampuni ya Zenji Motors ilitarajiwa kuwasilisha magari ya kubebea wagonjwa ndani ya kipindi cha siku 90 baada ya kusainiwa kwa mkataba ambapo Kampuni hiyo ilitakiwa kuziwasilisha gari hizo mnamo tarehe 5 Julai, 2022. Hadi ukaguzi unakamilika Novemba, 2022 Kampuni ya Zenji Motors haikuwasilisha gari hizo.

Aidha, ukaguzi umebaini Wizara ya Afya imeshindwa kutekeleza makubaliano ya kifungu cha 25.1 cha masharti maalum ya mkataba huo ambacho kinatoa maelekezo ya kutoza fidia ya shilingi milioni 47.38 kutokana na asilimia 0.1 ya bei ya mkataba kwa siku 24 alizochelewa kuwasilisha magari kama inavyoonekana katika mchanganuo ufuatao: (1,974,324,600 x 0.1% x siku 24 siku = 47,383,790).

Zaidi ya hayo, Mzabuni alitakiwa kuwasilisha nyaraka ambazo zilionekana kuwa sehemu ya makubaliano ikiwa ni pamoja na idhini ya Mtengenezaji kutoka kwa mzabuni ambaye aliainishwa kwenye hati ya Zabuni kama Toyota Japan.

Hadi ukaguzi unakamilika Novemba 2022 hakukuwa na ushahidi kwamba msambazaji aliwasilisha uidhinishaji unaohitajika wa Mtengenezaji wa magari hayo. Kulingana na Usimamizi, Fomu za uidhinishaji wa watengenezaji ziliwasilishwa kutoka Kampuni ya Western Auto Group. Hata hivyo, hati ya zabuni ilibainisha Toyota Japan.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kuhakikisha inatekeleza yafuatayo: -

Kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa magari ya kubebea wagonjwa pamoja na fomu za kuidhinisha watengenezaji wa magari hayo zinawasilishwa kwa mujibu wa utaratibu wa makubaliano hayo.

Masharti ya mkataba yanatekelezwa ipasavyo ikiwemo kukamilisha taratibu za kutozwa fidia ya shilingi milioni 47.38 zinazotokana na ucheleweshwaji wa kuwasilisha magari

hayo kwa mujibu wa makubaliano ya awali.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Ni kweli Mzabuni Zenj Motors alichelewa kuwasilisha ‘Ambulances’ kama ilivyo kwenye Mkataba. Hata hivyo, Mzabuni huyo tayari ameshawasilisha ambulances hizo zote (Viambatanisho - delivery notes).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli gari za kubebea wagonjwa zilichelewa kuletwa. Hilo lilitokana na kuwepo kwa maambukizi ya UVIKO – 19 iliyosababisha Kampuni ya Zenj Motors kushindwa kukabidhisha gari ndani ya wakati uliopangwa. Hata hivyo, Kampuni hiyo ilichukua juhudi ya kuiandikia barua kabla ya muda wa Mkataba kumalizika wa kuongezwa muda wa kuleta gari hizo kupitia barua yenye kumbukumbu ZM/22/EX/137 ya tarehe 4 Julai 2022.

Aidha, Kampuni hiyo ilichelewa pia kuzishusha katika meli gari hizo kwa takriban mwezi mmoja na nusu hadi miwili kutokana na kushindwa kupata ukuta kwa vile kulikuwa na meli nyingine. Hata hivyo, gari hizo tayari zimeshaletwa na kugawanywa katika hospitali tofauti, Kamati imelithibitisha hilo baada ya kuangalia ‘delivery notes’ za uletajwi wake (DO ya tarehe 23 Juni, 2022 kwa uwasilishaji wa gari 7 na DO ya tarehe 28 Disemba, 2022 kwa gari 5). Kwa msingi huo, Kamati imeridhika na hatua zilizochukuliwa na hoja hii imeondolewa.

## Hoja Nambari 4.3.1.14: Kuchelewa kufikisha vifaa vya Hospitali vyenye thamani ya shilingi bilioni 10.41.

Uongozi wa Wizara ya Afya mnamo tarehe 29 Juni 2022 uliingia makubaliano ya mikataba saba (7) na Wakandarasi wa usambazaji wa vifaa tofauti vya Hospitali kwa Hospitali nane (8) za Zanzibar kwa thamani ya shilingi bilioni 10.41.

Kwa mujibu wa mikataba hiyo, vifaa hivyo vilitakiwa kuwasilishwa ndani ya siku 90 baada ya kusainiwa kwa mikataba hiyo. Hadi ukaguzi unakamilika tarehe 22 Novemba 2022, vifaa hivyo havikuwasilishwa. Kiambatisho Nambari 1 Kinahusika. Aidha, ukaguzi umebaini Wizara ya Afya haikukata fidia ya shilingi milioni 249.83 kinyume na kifungu cha 25.1 cha sharti maalum la mkataba ambacho kinatoa marejesho ya asilimia 0.1 ya bei ya mkataba kwa siku iliyochelewa kuwasilishwa kwa bidhaa hizo. Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha inafanya yafuatayo: -

a) Kufuatilia na kuhakikisha vifaa vya Hospitali vinaletwa bila kuchelewa; na
b) Kutekeleza vifungu vya mkataba ikiwemo kutoza fidia kwa idadi ya siku zilizochelewa kwa mujibu wa mkataba husika.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Kwa sasa vifaa vyote vya hospitali tayari vimeshawasilishwa na kufungwa katika hospitali husika (angalia viambatanisho)

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa sababu ya kuchelewa kufika kwa vifaa vya hospitali kumetokana na uongozi wa Wizara ya Afya kuchelewa kulipa malipo ya awali (Advance Payment) kulikotokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha hizo. Kwasasa, Kamati imejiridhisha kwamba vifaa hivyo vimeshafungwa katika Hospitali zote za Mkoa na Wilaya. Kwa majibu hayo, Kamati imeridhika na hatua zilizochukuliwa na Wizara na hatimae hoja hiyo imeondelewa.

## 4.5 MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

### Hoja nambari 4.5.1.1: Boti zilizowasilishwa na bidhaa nyengine ambazo bado hazijalipwa shilingi milioni 552.99 na USD 934,200

Kwa mujibu wa kifungu nambari 18.6 cha mikataba iliyoingiwa kati ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na wasambazaji mbalimbali wa usambazaji na utoaji wa boti za uvuvi na mwani kinahitaji malipo kamili ndani ya siku 30 baada ya kuwasilisha na kukubalika kwa bidhaa.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilishindwa kufanya malipo yenye thamani ya shilingi 552.99 milioni na USD 934,200 kwa boti na bidhaa zilizowasilishwa kati ya kipindi cha Juni 2022 na Septemba 2022.

Aidha, kutokana na kushindwa kukamilisha: malipo kwa mujibu wa mkataba ukaguzi ulibaini Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilielekeza matumizi ya fedha kwenye mambo mengineyo ambayo hayakuwemo kwenye mpango kazi ulioidhinishwa kwa mujibu wa utaratibu jambo ambalo huwenda likapelekea kuitia hasara Serikali ya kuweza kulipa tozo ya fidia inayotokana na ucheleweshaji wa kufanya malipo kwa wakati pamoja na kuzorotesha kukamilika kwa miradi kwa wakati uliopangwa.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhakikisha unafanya matumizi kwa mujibu wa mpango kazi uliopangwa kwa shughuli za miradi ili kuepusha kujitokeza kwa mrundikano wa madeni ya Wazabuni ambayo yatazalisha kiwango kikubwa cha tozo ya fidia na kupelekea kuibebesha mzigo Serikali usiokuwa wa lazima.

Hali halisi ya utofauti huo ni kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 20: Utofauti wa Vigezo (Vipimo) baina ya mikataba na uhalisia**

| Nam. | Nambari ya Mkataba | Aina ya Boti | Jina la Muuzaji | Idadi | Vigezo kwa mujibu wa mkataba | Vipimo halisi | Eneo husika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SMZ/02/G/ RT/2021-2022/22 | Boti ya Mita 5 | Qiro Group Co Ltd | 22 | Urefu wa Mita 5 | Urefu wa Mita 4.96 | Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja |
| 2 | SMZ/02/G/ RT/2021-2022/08 | Boti ya Mita 7 | Songoro | 4 | Urefu wa kina cha chini 0.64M | Urefu wa Kina cha chini Mita 0.60 | |
| 3 | SMZ/02/G/ RT/2021-2022/22 | Boti ya Mita 5 | Qiro Group Co Ltd | 25 | Urefu wa Mita 5 | Urefu wa Mita 4.9 | Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini “A” Unguja |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Malipo ya wazabuni wa utengenezaji wa boti ya hatua za awali yalifanyika baada ya kupata maelekezo ya Serikali kuhusu mfumo wa malipo ambao ungefaa kutumika kwa ufafanuzi ufuatao.

1. Fedha za programu ya UVIKO 19 zilizopangiwa kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni za aina mbili. Kuna Fedha za mafunzo ambazo ni Shilingi Milioni 695 zilizopatikana moja kwa moja kwa utaratibu wa kawaida Wizarani kupitia Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango). Hizi hazikuwa fedha za kulipia boti bali zilikuwa ni fedha za mafunzo, kutoa elimu ya ubunifu, elimu ya mitaji, elimu ya ujasiriamali na uwezeshaji, pamoja na uratibu wa mipango hiyo kwa mujibu wa Mpango Wa Utekelezaji uitwao "Blue Economy Intervention Plan". Hakuna fedha iliyopangiwa kazi isiyohusu au liyobadilishiw matumizi kinyume na taratibu.
2. Fedha zilizotakiwa kugharamia malipo ya boti zote za Uvuvi na Wakulima wa Mwani, ikiwemo ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa Kama ni Shilingi Bilioni 28.8. Hizi ni fedha ambazo tangu hapo awali hazikuwepo Wizarani kwa utaratibu tuliouzoea. Kuziweka chini ya utaratibu tuliouzoea kungehatarisha zaidi matumizi yake. Kuepuka hatarishi za wizi, uzembe, matuizi mabaya ya fedha, n.k. Fedha hizi zilihifadhiwa kupitia Benki ya CRDB, na kwa sababu kuu ya usalama wa matumizi yake na uwepo wa mifumo bora na imara ya kuhakiki (Accountability and Transparency) na kurejesha mikopo ya boti hizo hapo baadaye.
3. Hii ni baada ya maelekezo na makubaliano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya CRDB. Fedha hizo ndizo hadi hii leo zinaendelea kulipa wazabuni kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kwa ajili ya Malipo ya Boti, ambao unaendelea kwa uwazi kabisa
4. Utaratibu wa uratibu wa malipo kupitia Benki ya CRDB unaendelea na kuratibiwa kwa pamoja na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango), na malipo yanalipiwa kupitia Kampuni ya Uvuvi Zanzibar ZAFICO kwa kufuata Mwongozo wa Serikali. Na hii ni kwa sababu Kisheria Wizara haiwezi kuchukua mkopo moja kwa moja kutoka CRDB kwa ajili ya kulipia wazabuni wa boti hizo. Na badala yake Kampuni ya ZAFICO itakuwa ndio mkopaji na mlipaji kwa kupitia benki ya CRDB. Hatua zilizochukuliwa:
    - ❖ Wazabuni wanaendelea kulipwa kadri wanavyowasilisha Boti zao kwa ukamilifu na kwa mujibu wa mkataba.
    - ❖ Boti zinaendelea kusambazwa kwa wanufaika kwa mujibu wa taratibu zote

zilizowekwa na kwa uwazi.

- ❖ Muongozo wa Biashara wa Programu ya UVIKO 19 baina ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Benki ya CRDB (Business Model) umeundwa kwa pamoja na unatakelezwa kwa karibu kabisa na wadau wa CRDB na kwa mashirikiano yote yanayohitajika.
- ❖ Fomu maalum za mikopo ya boti zimeandaliwa na kuendelea kusambazwa kwa wananchi kwa mujibu wa taratibu zilizopo.
- ❖ Mikutano ya Wilaya kuhusu uchukuaji wa fomu, mifumo ya mikopo na malipo inaendelea. Kwa hivi sasa mfumo wa malipo upo vizuri na unaendelea bila ya tatizo lolote.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC iliamua kufanya ziara ya kwenda kuitembelea Kampuni ya Songoro Marine Transport Limited inayofanya kazi za utengenezaji wa Boti iliyopo eneo la Kigamboni Jijini Dar es Salaam. Lengo kuu la ziara hiyo ilikuwa ni kuchunguza kama ujenzi wa Boti hizo umefanyika kwa mujibu wa vigezo vilivyoainishwa katika Mkataba wa utengenezaji. Kufuatia ziara hiyo, Pamoja na mambo mengine, Kamati imegundua yafuatayo:

1. Mkataba wa awali wa utengenezaji wa boti za mita 5 ulikuwa umemaliza muda wake na boti zote zilizotakiwa kutengenezwa zilikamilika.
2. Kampuni ya Songoro ilipatiwa zabuni ya kutengeneza boti 68 za mita nane ambapo tayari alikuwa kishakamilisha boit 17.
3. Kulikuwa na ucheleweshwaji wa malipo kwa Kampuni hiyo kutoka katika Serikali kunakopelekea ucheleweshwaji wa katika utengenezaji wa boti hizo na kuwafikia walengwa (Vikundi vya Wavuvi) kwa wakati pamoja na kushindwa kwa Kampuni kununua mzingo kwa ‘bulk’.
4. Kabla ya boti hiyo kukabidhiwa kwa Wizara, timu ya pamoja ya usimamizi huthibitisha ufanywaji wa majaribio ili kujiridhisha na umadhubuti wa boti hizo. Timu hiyo imeundwa na Watendaji kutoka Idara ya Uvuvi, Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA), Wavuvi.
5. Boti hizo zinakuwa na ‘warrant’ wa mwaka mmoja pamoja na bima kwa muda wa miaka mitatu kwa chombo na mtu husika.
6. Kuna ucheleweshwaji katika tengenezwaji wa boti ambapo zilitakiwa ziwasilishwe katika Mkataba wa awali. Boti hizo ni 73 za mita nane, 75 za mita tano na 35 za

mita saba. Kampuni imeahidi kukamilisha ujenzi wake ifikapo mwezi wa Novemba, 2023.

Kiujumla, Kamati imeridhika na utekelezaji wa hoja hii licha ya kuwepo kasoro katika hatua za awali.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Serikali ihakikishe inafanya malipo ya utengenezaji wa boti hizo kama ilivyoelezwa katika Mkataba.
2. Wizara ihakikishe inatengeneza boti kwa mujibu wa mahitaji ya Wavuvi wa eneo husika.
3. Timu ya Usimamizi ihakikishe inasimamia ipasavyo utengenezaji wa boti hizo ikiwemo kuzifanyia majaribio kabla ya kuwafikia walengwa.

## Hoja nambari 4.5.1.2: Kutokuwasilishwa kwa Boti 427

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika hadi kufikia Novemba 2022, Wakandarasi sita wa ujenzi wa boti za uvuvi na mwani, walishindwa kuwasilisha boti 427 kati ya boti 502 sawa na asilimia 85 ya ucheleweshwaji.

Kutokana na hali hiyo imebainika Wizara ilisaini hati ya makubalino mwezi March 2022 kwa lengo la kupokea boti hizo ifikapo mwezi wa Julai 2022. Hadi ukaguzi unakamilika Wakandarasi hao walishindwa kuwasilisha boti hizo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba. Mchanganuo wa boti ambazo hazijawasilishwa ni kama unavyoonekana katika majadweli yafuatayo:-

**Jadweli Nambari 21: Boti za urefu wa mita 8 ambazo hazijawasilishwa**

| Na. | Nambari ya Mkataba | Msambazaji wa boti (Mita 7) | Tarehe ya kusaini wa kwa Mkataba | Tarehe ya kumaliza Mkataba | Kiasi cha Mkataba /Boti za Mita 8 | Kiasi kilichowasilishwa kwa mujibu wa mkataba/ Boti za Mita 8 | Idadi ya Bodi ambazo hazijawasilishwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ/02/G/RT/2021-2022/08 | M/s Songoro Marine LTD | 02/03/2022 | 02/07/2022 | 73 | 0 | 73 |
| 2. | SMZ/02/G/RT/ 2021- | M/s Dar es Salaam | 08/03/2022 | 08/07/2022 | 131 | 0 | 131 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2022/09 | Merchant Group LTD | | | | | |
| 3. | SMZ/02/G/RT/ 2021-2022/07 | Amos Industrial Limited | 02/03/2022 | 02/07/2022 | 73 | 0 | 73 |
| **Jumla** | | | | | **277** | **0** | **277** |

**Jadweli Nambari 22: Boti za urefu wa mita tano (5) na saba (7) ambazo hazijawasilishwa**

| Na. | Nambari ya Mkataba | Wauzaji wa Boti (Mita 5 na Mita 7) | Tarehe ya Kusainiwa Mkataba | Tarehe ya Kumaliza Mkataba | Kiasi cha Mkataba /Boti za Mita 7 | Kiasi kilichowasilishwa kwa mujibu wa mkataba/ Boti za Mita 7 | Idadi ya Bodi ambazo hazijawasilishwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ/02/G/RT/ 2021- 2022/08 | M/s Songoro Marine LTD | 02/03/2022 | 02/07/2022 | 75 | 35 | 40 |
| 2. | SMZ/02/G/RT/ 2021- 2022/04 | M/s Dhow-licious LTD | 02/03/2022 | 02/07/2022 | 75 | 40 | 35 |
| 3. | SMZ/02/G/RT/ 2021- 2022/02 | Amos Industrial Limited | 02/03/2022 | 02/07/2022 | 75 | 0 | 75 |
| **Jumla** | | | | | **225** | **75** | **150** |

Majibu ya Uongozi ya Wizara

Changamoto za utengenezaji wa boti zilianza tangu hapo awali kutokana na mdororo wa uzalishaji wa kiviwanda kulikosababishwa na athari za UVIKO 19 uliozorotesha upatikanaji wa malighafi za kutengenezea boti kutoka nje ya Zanzibar, lakini pia upatikanaji wa mashine za boti za YAMAHA ambazo ni “Original” na kutambuliwa na Kiwanda mama kutoka Japan.

Uzalishaji kwa wazabuni uliendelea na changamoto hizo, na kwa kuwa kwa mujibu wa Mkataba, Mkandarasi/Mzabuni alipaswa kuwasilisha kila kitu kwa pamoja (Yaani Boti, Mashine ya Yamaha, Vifaa vya GPS, Vifaa vya Fish Finder, Makoti ya Uokozi, Mishipi n.k.) Huu ulikuwa ni mfumo wa manunuzi ya moja kwa moja. Mzabuni analeta bidhaa na hapo

ndipo analipwa. Hakukuwa na “Advance Payment” au upotevu wowote ule wa fedha katika mchakato huu. Mzabuni akileta analipwa, na kama hakukamilisha badi hakuna malipo anayolipwa.

Pia, changamoto ya pili ya malipo ilikuwa ni mchakato wa kupata muafaka uliochukua muda mrefu baina ya Serikali na Benki ya CRDB ya kukubalika kwa mfumo imara, bora na wa uwazi utakaohakikisha “Quality Assurance” na “Value for Money” ya malipo na ukopeshaji wa boti hizo kwa wanufaika. Kupitia mwongozo wa pamoja wa Serikali na Benki ya CRDB, mchakato wa uhakiki, malipo, ukopeshaji na ufuatiliaji hatimae ukakamilishwa. Mchakato huu unaendelea hadi hii leo. Boti zaidi zimeshapokelewa, wazabuni wanaendelea kulipwa, boti pia zishagawiwa kwa wanufaika nwa mfumo wa mkopo, na kuwa Benki ya CRDB inafuatilia mikopo hiyo.

**Hatua zilizochukuliwa**

- ❖ Kwa kufuata taratibu za manunuzi, Wizara iliongeza muda wa mikataba ya wazabuni wanaohusika.
- ❖ Wazabuni wameendelea kukamilisha utengenezaji wa boti zilizobaki kwa kasi kubwa.
- ❖ Mashine za YAMAHA Original zimepatikana kutoka kwa Kampuni Mama ya Japan kupitiakwa wakala anayetambulika Japan.
- ❖ Vifaa mbali mbali vimeendelea kupatikana na wazabuni wamekuwa wakiwasilisha boti na vifaa vyake kwa malipo na kupokelewa.
- ❖ Utaratibu wa ugawaji wa boti umeendelea Unguja na Pemba kote na kwa uwazi kabisa na kwa Ushahidi wa kutosha wa hatua zilizofikiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.
- ❖ Boti zaidi zimewasilishwa kwa utekelezaji

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa ni kweli kulijitokeza kasoro ambazo alizibainisha Mkaguzi katika Ripoti yake kulikosababishwa na mripukoa wa Uviko 19. Hata hivyo, baadhi ya boti hizo zimeshawasilishwa na kugaiwa kwa walengwa isipokuwa takriban boti 180 zinaendelea kufanyiwa kazi. Kwa mnasaba huo, hoja hii inabakia kwa hatua ya utekelezaji zaidi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu uhakikishe inafuata masharti

yaliyobainishwa katika Mikataba ya utengenezaji Boti.

2. Uongozi wa Wizara iharakishe ukamilishaji wa boti zilizobakia ili ziweze kukabidhiwa kwa Walengwa na sio kuchelewa zaidi.

## Hoja nambari 4.5.1.4: Mapungufu katika ujenzi wa mabwawa ya samaki

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilisaini makubaliano na Kampuni ya Scenic Construction and Consultancy Limited kwa ajili ya kukarabati mabwawa 10 ya samaki kwa thamani ya shilingi milioni 536.78. Kutokana na makubaliano hayo ukaguzi umebaini uwepo wa mapungufu katika utekelezaji wa mkataba huo. Mapungufu hayo ni kama ifuatavyo: -

a) Mabwawa matatu ya samaki yenye thamani ya shilingi milioni 76.84 yalikamilika kwa wakati kwa upande wa Kitogani, Bumbwini na Mkokotoni, lakini Wizara ilishindwa kukabidhi mabwawa hayo kwa wakati kwa vikundi vya Haturudi Nyuma, Makoba na Umoja ni Nguvu kwa ajili ya ufugaji wa samaki.

b) Uwepo wa ukarabati wa mabwawa matatu ya samaki yenye thamani ya shilingi milioni 132.95 ambayo yalitarajiwa kuanza kujengwa tarehe 25 Agosti 2022 kwa vikundi vya Unguja Ukuu, Mafufuni na Chwaka (Kikundi cha Tupe Kheri, Kazi ipo Hapa) hadi ukaguzi unakamilika tarehe 23 Novemba 2022 mabwawa hayo hayajaanza kujengwa.

c) Mabwawa matatu ya samaki yaliyokamilika yenye thamani ya shilingi milioni 76.84 katika eneo la Kitogani, Bumbwini, na Mkokotoni kwa Vikundi vya Haturudi Nyuma, Makoba na Umoja ni Nguvu yalikarabatiwa kinyume na maelekezo ya kitaalamu

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ihakikishe kwamba:

a) Maelezo ya mabwawa yaliyokamilishwa yanalingana na BoQ;

b) Mabwawa ya samaki yaliyokamilika yatatolewa kwa vikundi husika na kwa wakati, na

c) Mabwawa yaliyobaki wahakikishe yanakamilishwa kwa mujibu wa makubaliano. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 23: Mabwawa ya samaki yamekarabatiwa kinyume na vigezo vya kiufundi**

| Nambari ya Bili | Jina la Kikundi | Eneo Husika | Vigezo kwa mujibu wa | Vipimo Halisi (M) | Gharama za BOQ (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | BOQ (M) | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Bill NR2 | Haturu di Nyuma | Mkokotoni | 25.695 X 22.5 X 1.5 | 20.6 X 21 X 1.8 | 32,109,000 |
| Bill NR4 | Makoba | Bumbwini | 21 X 20 X 1.5 | 18.9 X 17.5X1.7 | 27,934,000 |
| Bill NR9 | Umoja ni Nguvu | Kitogani | 15.59 X 14.095X1.5 | 10.5 X6.65X 2 | 16,800,000 |
| **Jumla** | | | | | 76,843,000 |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Ujenzi wa mabwawa ya Samaki ulianza pale tu baada ya kufanyika kwa uhakiki mwengine na kwa kuangalia "Demand" ya wanufaika ikiwemo kama ni samaki wa maji baridi au samaki wa maji chumvi. Pia katika upatikanaji wa vifaranga vya samaki vya maji chumvi ukiliganisha na vifaranga vya maji baridi ambavyo vilikuwa tayari vinapatikana kirahisi.

Makabidhiano ya mabwawa haya mapya ya samaki yalihitaji na kutegemea sana kukamilika kwa mabwawa hayo, upatikanaji wa vifaranga, na uhakiki wa vikundi vilivyoomba kupewa mabwawa hayo na utayari wa wanavikundi hao katika kuyaendesha mabwawa hayo. Hakukuwa na mabwawa ambayo yalitengenezwa kinyume na maelekezo ya kitaalamu au Mikataba. Wizara ilisimama kidete katika kuhakikisha kuwa ukandarasi wa mabwawa yote ulitimiza masharti ya Mkataba na maelekezo ya wataalamu. Kwa hivi sasa:

a) Mabwawa yote ishirini kwa Unguja (10) na Pemba (10) yamekamilika na kukabidhiwa kwa wafaidika.

b) Mkandarasi anaendelea kufanya Ukarabati kwa maeneo ambayo yanajitokeza kuwa na matatizo/mapungufu na mchakato unaendelea uvuvi.

**Hatua zilizochukuliwa**

Kuhusiana na hitilafu za baadhi ya mabwawa, Wizara ilimuandikia barua Mkandarasi kufanya marekebisho ya kasoro zote zilizojitokeza uhusiana na mabwawa hayo yaliyoonekana na Wizara kuwa na hitilafu, kwa upande wa Unguja na Pemba na tayari yasharekebishwa na timu ya Wizara tayari ishaenda kukaguwa kwa kujiridhisha marekebisho hayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imekubaliana na hoja ya Mkaguzi kutokana na dosari ambazo ameziainisha. Sambamba na hilo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Mabwawa katika eneo la Bumbwini ambayo yalibainika kuwa na dosari zifuatazo:-

1. Bwawa la kikundi cha Haturudi Nyuma limejengwa chini ya kiwango na kupelekea madhara tofauti ikiwemo kufanya ufa na kuvujisha kwa maji.
2. Kufariki kwa vifaranga vya samaki vilivyoingizwa awali ndani ya bwawa hilo.
3. Ukosefu wa chakula cha kuwalisha samaki wanaowafuga
4. Ukosefu wa ulinzi wa kutosha katika mabwa husika.
5. Upatikanaji hafifu wa vifaranga vya samaki. Hali hiyo imepelekea Wanakikundi kuokota vifaranga katika bahari na kurudisha nyuma malengo ya Mradi huo.
6. Kukosekama kwa elimu na uelewa wa shughuli za ufugaji wa kitaalamu wa samaki hao. Hali hiyo, inapelekea kufa kwa vifaranga hivyo na kukosekana tija iliyokusudiwa. Kadhalika, ufugaji wa aina hiyo hautoiwezesha Serikali kufikia malengo ya uzalishaji wa tani tatu hadi nane kwa Bwawa.
7. Ujenzi wa baadhi ya Mabwawa umefanyika pasi na kufanyikia upembuzi yakinifu (feasibility study).
8. Wizara tayari imeshaagizia vifaranga 120,000 kutoka nchini Indonesia kwa ajili ya Mabwawa yote ya Unguja na Pemba. Kabla ya vifaranga hivyo kusambazwa kwa Walengwa.

Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwa Mabwawa hayo tayari yameshafanyiwa ukarabati na Kampuni husika chini ya usimamizi wa Wizara na yanaendelea na shughuli za ufugaji wa vifaranga.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu uwe makini katika usimamizi wa ujenzi wa Miradi yao hususan katika hatua za awali ili kuepusha kutofikiwa malengo ya Serikali ya kuwaondolea ugumu wa maisha wananchi hususan wa kipato cha chini.
2. Wizara ihakikishe inavifanyia tathmini vifaranga vitakavyoletwa nchini juu ya uhimilifu wa mazingira tuliyonayo.
3. Wizara iandae utaratibu mzuri wa utoaji uelewa kwa walengwa ili waweze kufuga vifaranga hivyo kitaalamu na kuwapati tija katika maisha yao.

4. Wizara iweke utaratibu mzuri wa usambazaji wa vifaranga hivyo kwa vikundi vya wafugaji ili kunusuru kuwepo upendeleo.

## Hoja namabari 4.5.1.5: Kutokuletwa kwa mashine ya kutengenezea chakula cha samaki shilingi 139,500,000

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilisaini hati ya makubaliano na Kampuni ya COMFIX & Engineering tarehe 23 Mei 2022 kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa mashine ya kutengeneza chakula cha samaki kwa thamani ya shilingi milioni 139.5 ambapo mashine hiyo ilitarajiwa kupokelewa ndani ya kipindi cha miezi miwili mara baada ya kusainiwa kwa mikataba hiyo ambayo si zaidi ya tarehe 23 Julai 2022. Hadi ukaguzi unakamilika tarehe 23 Novemba 2022 mashine ya chakula cha samaki haikuwasilishwa.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhakikisha muuzaji analeta na kufunga mashine kwa mujibu wa makubaliano pamoja na kutozwa fidia inayotokana na kuchelewesha kuwasilisha mashine hiyo kwa mujibu wa makubaliano.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Kampuni ya COMFIX & Engineering imeeleza kwamba kutokana na janga la UVIKO19, mashine hiyo kuchelewa kusafirishwa kutoka China hadi Zanzibar. Aidha mzabuni ameleta taarifa kuwa mashine hiyo imeshafika bandarini Dar es Salaam na wakati wowote italetwa Zanzibar.

Wizara ilituma maafisa wake kwenda kuhakikisha uwepo wa mashine hiyo Bandari ya Dar es Salaam na Mamlaka husika ya Bandari (TPA) imethibitisha kuwepo kwa "Container" yenye mashine hiyo ndani yake.

Barua ya uthibitisho kwa mashine ipo Dar-ES-Salaam imeambatanishwa.

### Uchunguzi wa kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa mashine ya kutengenezea Chakula cha Samaki ipo Bandari ya Dar es Salaam. Hata hivyo, Wizara ya Uchumi wa Buluu bado haijalipia fedha ya ununuzi wa mashine hiyo kwa Kampuni ya COMFIX & Engineering hadi itakapokabidhiwa kwa Wizara.

Aidha, Kamati ya PAC haikuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara hasa ukizingatia lengo la Serikali halijafikiwa kwamba kutokana na makubaliano yaliyopo, (MUDA WA MKATABA) hivi sasa wananchi walitakiwa wawe wananufaika na matunda yatokanayo na mashine hiyo. Kwa mnasaba huo, hoja hii bado inaendelea kubakia.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa Uchumi wa Buluu uhakikishe unachukua juhudi za haraka zitakazowezesha mashine inaletwa Zanzibar si zaidi ya miezi sita ili lengo lililokusudiwa na Serikali lifikiwe.
2. Uongozi wa Uchumi wa Buluu unasimamia ipasavyo masharti yaliyoainishwa katika mikataba yao ili iweze kutekelezwa ipasavyo.

## Hoja nambari 4.5.1.6: Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi yenye thamani ya shilingi milioni 229.80

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliingia makubaliano ya mkataba na Kampuni ya EasyFix Co. Limited kwa ajili ya usambazaji wa vitendea kazi vya unenepeshaji wa kaa matope katika mashamba 60 Unguja na Pemba kwa thamani ya shilingi milioni 229.80. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutekelezwa kwa mapendekezo ya kamati ya tathmini iliyotaka zabuni hiyo kuitishwa tenda badala yake Uongozi wa Wizara ulitumia njia ya nukuu jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 2(1)(c) cha Sheria ya Uanunuzi Uondoaji wa Mali Umma, 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ufuate mapendekezo ya kamati ya tathmini ili kuepusha kufanya malipo kwa thamani ya juu ukilinganisha na uhalisia wa upatikanaji wa vifaa hivyo.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Programu ya ujenzi wa mabwawa ilichelewa kwa ajili ya kutafuta Mkandarasi mwenye sifa na uzoefu. Hivyo, Wizara imeichukua kampuni tajwa kama “Single Source” badala ya kushindwa kujitokeza kwa wazabuni wengine wowote wale. Ikumbukwe kuwa lengo na msingi wa program kama hii ya Ahweni ya UVIKO19 ilikuwa ni kuhakikisha kuwa wazawa wanapata fursa za mwanzo ya ajira katika utengenezaji pamoja na wanufaika wa Mradi huo.

Kwa kuwa hakukuweko na ishara yoyote ya kupata wazabuni zaidi ya EasyFix/Wakulima Hai katika ujenzi wa majongoo bahari na mashamba ya kaa, na kwa kuangalia muda wa kutangaza zabuni kama hizo dhidi ya masharti ya IMF ya mkopo huo ndani ya miezi sita, hatua ya mwisho kabisa ilikuwa ni kuthibitisha Kampuni ya EasyFix Co/Wakulima Hai ambayo ilikuwa tayari ikifanya kazi za ujenzi wa vizimba vya ufugaji wa mazao ya Baharini na Ufugaji wa viumbe hai hata kabla ya Programu ya UVIKO19 hapa Zanzibar. Hatuazilizochukuliwa Wizara imekuwa ikifuatilia kwa karibu ujenzi wa mshamba ya

majongoo bahari na kaa na ikiwemo maedneleo ya karibuni kabisa ya kuhakikisha maliziaji na ugawaji wamashamba hayo pamoja na ubora unaotarajiwa.

- ❖ Ujenzi wa mashamba ya majongoo bahari na kaa unaedelea vizuri na unafikia shabaha na malengo yaliyokusudiwa.
- ❖ Utaalamu zaidi wa ujenzi wa mashamba ya majongoo bahari na kaa kwa wanajamii kwa siku za baadaye tayari pia unatolewa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa kutokana na uharaka wa mradi ililazimika Wizara kutumia njia ya ununuzi ya kumchagua Mzabuni mmoja (Single souce). Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa hakukuwa na sababu ya msingi iliyopelekea Wizara kukiuka taratibu za zilizoainishwa katika Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya 2016 kwani waliieleza Kamati kuwa kulikuwa na shida ya kumpata mtaalamu wa ujenzi wa Mabwawa hayo. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuridhika na majibu ya hoja.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu ufuate taratibu zote za Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya 2016 hususan katika taratibu za kumpata Mzabuni kama ilivyoelekezwa na Kamati ya Tathmini ili kujiepusha na hoja zisizokuwa za msingi.

## Hoja nambari 4.5.1.7: Marekebisho ya Mkataba yaliyofanyika bila ya idhini ya Bodi ya Zabuni

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilisaini mikataba miwili na Kampuni ya Qiro Group Company Limited ambapo kila mmoja una thamani ya USD 987,500 kwa ajili ununuzi wa boti 250 za mwani zenye mashine ya Horse Power 9.9 kwa kila mkataba.

Aidha, kutokana na kampuni ya Qiro Group kushindwa kutekeleza makubaliano ya mkataba wa awali uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ulibadilisha matakwa ya maamuzi ya Kamati ya Bodi ya Zabuni na kuingia mkataba na kampuni ya Nile Fishnet Co. Ltd kwa ajili ya ununuzi wa mashine zenye Horse Power 9.9 kwa thamani ya shilingi bilioni 2.2.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa mikataba ya awali ilirekebishwa kwa kuondoa kipengele cha ununuzi wa mashine za Boti kwa Kampuni ya Qiro Group na kupewa Kampuni ya Nile Fishnet Co. Ltd bila ya kushirikishwa bodi ya Zabuni jambo ambalo

limepelekea kubadilika kwa thamani ya mikataba kutoka USD 987,500 hadi USD 511,000 kwa kila mkataba.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhakikisha inafuata utaratibu, Kanuni na Sheria ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma namba 11 ya 2016 kwa kuwashirikisha Bodi ya Zabuni kufanya maamuzi na marekebisho ya mikataba pale panapotokezea uwepo wa mabadiliko ya kiutendaji ili kuepusha kuipa zabuni Kampuni isiyokuwa na uwezo au kufanya manunuzi kwa thamani kubwa zaidi na kupelekea kuingiza hasara Serikali.

## Majibu ya Uongozi wa Wizara

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi haikuwa tayari kukubali kuweka pembeni "Quality" na "Value" ya Mashine za Yamaha Original 9.9 HP kwa wakulima wa mwani. Kwa kuwa mashine hizi katika kipindi hicho cha UVIKO19 hazikuwepo katika masoko, Mzabuni, yaani QIRO Group Company, alipendekeza kuwa Wizara ibadilishe msimamo huo wa QUALITY & ORIGINAL PRODUCTS, na badala yake tununue mashine ambazo ni "GENERIC" na sio ORIGINAL. Athari yake ingekuwa kubwa na kusababisha hasara za muda mrefu kwa walengwa.

Wizara ilichukua uamuzi wa kuendelea na kuzitafuta mashine za YAMAHA ORIGINAL 9.9 HP kutoka Japan. Wizara ikachukua jitihada ya mawasiliano na Japan kupitia Ubalozi wa JAPAN Tanzania na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA) ili iweze kupata mashine za YAMAHA Original kutoka kiwandani Japan kwa sababu hazikuwepo kunako masoko ya kawaida ya kimataifa. Ndipo JICA ikipoisaidia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kuwasiliana na kampuni mama ya YAMAHA Japan ambayo ilikubali kuanza kuzitengeneza mashine hizo na kuzisafirisha kuja Tanzania kwa awamu kupitia Wakala anayetambuliwa na Japan kwa mashine original za YAMAHA hapa Tanzania aitwaye Nilefishnet Motors Ltd.

Wizara itahahakisha upatikanaji wa mashine aina ya YAMAHA original na kuepuka upatikanaji wa mashine feki, pia kupitisha maamuzi yote ya manunuzi katika bodi ya zabuni ya Wizara

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa Wizara ya Uchumi wa Buluu imevunja taratibu za Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya 2016 na kupelekea kuchukua uamuzi wa kubadilisha maamuzi ya Bodi ya Zabuni baada ya mtoa huduma wa mwanzo kushindwa kutoa huduma.

Kamati imelithibitisha hilo baada ya Watendaji wa Wizara kushindwa kuwasilisha mbele ya Kamati kielelezo kutoka Bodi ya Zabuni (Kumbukumbu za kikao) ambacho kiliwataka waache kumtumia Mzabuni aliyependekezwa na Bodi hiyo na kuamua kuendelea na Mzabuni mwengine. Kwa mnasaba huo, hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake, kielelezo hicho hakikupatikana na kupelekea Kamati ya PAC kushindwa kuridhika na majibu ya Watendaji wa Wizara. Hivyo, hoja inaendelea kubakia.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Uchumi wa Buluu uhakikishe unatekeleza maamuzi ya Bodi ya Zabuni ili kujiepusha hoja kama hizi kujirudia.

## Hoja nambari 4.5.1.8: Ununuzi wa mashine za boti bila ushindani wa zabuni shilingi bilioni 2.2

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliingia katika hati ya makubaliano na Kampuni ya Nile Fishnet Co. Ltd kwa ajili ya ununuzi wa mashine za boti aina ya YAMAHA bila kuwashirikisha wazabuni wengine kushiriki katika mchakato wa ununuzi.

Kufanya manunuzi bila ya kuzingatia ushindani wa bei ni kwenda kinyume na kifungu nambari 38 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kufuata zabuni ya ushindani ya manunuzi kwa mujibu wa sheria za manunuzi ya umma ili kuepusha kujitokeza kwa manunuzi yasiyoendana na uhalisia wa bei.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Wizara ilichukua uamuzi wa kuendelea na kuzitafuta mashine za YAMAHA ORIGINAL 9.9 HP kutoka Japan. Wizara ikachukua jitihada ya mawasiliano na Japan kupitia Ubalozi wa JAPAN Tanzania na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA) ili iweze kupata mashine za YAMAHA Original kutoka kiwandani Japan kwa sababu hazikuwepo kunako masoko ya kawaida ya kimataifa. Na pia katika kuokoa muda wa mkopo wa IMF wa miezi sita. Ndipo JICA ilipoisaidia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kuwasiliana na Kampuni mama ya YAMAHA Japan ambayo ilikubali kuanza kuzitengeneza mashine hizo za HP 9.9 na kuzisafirisha kuja Tanzani kwa awamu kupitia Wakala anayetambuliwa na Japan.kwa mashine original za YAMAHA hapa Tanzania aitwaye Nilefishnet Motors Ltd.

Upatikanaji wa mashine moja kwa moja kutoka kwa Wakala wa YAMAHA Tanzania ndio njia ambayo imetuwezesha kupata mashine madhubuti za YAMAHA na Bei rahisi kuliko

pahala pengine popote Tanzania.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Wizara ililenga kununua mashine halisi (Original) moja kwa moja kutoka Wakala wa YAMAHA na kufanikisha lengo hilo bila ya kusababisha gharama za ziada kwa Serikali, Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi na kuridhika na majibu ya hoja. Hivyo, hoja hii inaondolewa.

## Hoja nambari 4.5.1.9: Kutosambazwa kwa Boti 444 kwa ajili ya shughuli za uvuvi wa mwani.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilipokea jumla ya boti 600 kutoka kwa Kampuni nne ambazo ziliwasilisha boti hizo kwa ajili ya kusambazwa na kutumika kwa shughuli za uvuvi kwa walengwa. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kati ya boti 600 zilizopokelewa boti 156 ziliweza kugawiwa kwa vikundi mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uvuvi wa mwani ambazo ni sawa na asilimia 26 ya boti zote.

Aidha, boti 444 zilizopokelewa sawa na asilimia 74 hadi ukaguzi unakamilika boti hizo bado hazikusambazwa (hazikugaiwa) kwa ajili ya kupelekwa kwa walengwa na kutumika kwa lengo lililokusudiwa.

Kutokusambazwa kwa boti hizo kwa wakati pamoja na kutokuhifadhiwa katika maeneo mazuri na salama kumepelekea kujitokeza kwa uharibifu mkubwa wa kupasuka, kutoboka na hatimae kutokufaa kabisa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Kutokana na hali hiyo ukaguzi umebaini uwepo wa uzembe uliosababishwa na waliokabidhiwa kushindwa kufanya maamuzi ya haraka na yenye tija kwa Serikali na hatimae kupelekea kuitia hasara Serikali na kuviza jitihada za Serikali katika kuwaondoshea wananchi ukali wa maisha.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kusimamia utekelezaji wa maamuzi na jitihada za Serikali za kuwaondoshea ukali wa maisha wananchi kwa kuzigawa boti hizo kwa walengwa na zile zilizoharibika jitihada za marekebisho zifanyike ili kufikia tija iliyokusudiwa.

Aidha, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ichukue hatua za haraka kuhusu boti ambazo hazijasambazwa kwa lengo la kuiepushia Serikali kupata hasara endapo boti hizo zitaendelea kuachwa kwenye mazingira ya uharibifu. Halisi halisi ya boti hizo ni kama inavoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 24: Kutokusambazwa kwa Boti zilizonunuliwa kwa walengwa**

| Na | Nambari ya Mkataba | Taarifa za Wauzaji na Vigezo vya Boti | Idadi ya Boti zilizopokelewa | Idadi ya Boti zilizogaiwa | Idadi ya Boti zilizokuwa hazijagaiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ/02/G/ RT/20212022/08 | M/S Songoro Marine Ltd (Boti yenye urefu wa Mita 7) | 35 | | |
| 2. | SMZ/02/G/ RT/2021-2022/03 | M/S Captain Andy's Fishing Ltd (Boti yenye urefu wa Mita 7) | 25 | | |
| 3. | SMZ/02/G/ RT/2021-2022/04 | M/S Dhow-Licious Ltd (Boti yenye urefu wa Mita 7) | 40 | | |
| Jumla Ndogo | | | 100 | 52 | 48 |
| 4. | SMZ/02/G/ RT/2021-2022/22 | Qiro Group Company Ltd (Boti yeye urefu wa Mita 5) | 500 | 104 | 396 |
| **Jumla Ndogo** | | | **500** | **104** | **396** |
| **Jumla Kuu** | | | **600** | **156** | **444** |

Kutokana na kuchelewa kuchukuliwa kwa maamuzi ya kugawiwa boti hizo kwa wenye kuhitaji imebainika kujitokeza kwa maharibiko ya boti hizo yanayotokana na kutokuhifadhiwa sehemu nzuri na salama na hatimae kuachwa katika sehemu ya wazi ambayo iliruhusu kupigwa na jua na mvua na hatimae kuharibika kama zinavyoonekana katika picha hapo chini: -

**Majibu ya Uongoza wa Wizara**

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi tuna imani kubwa sana kuwa hapakuwepo na

uzembe wowote katika utekelezaji wa programu ya UVIKO19. Hii ni programu ambayo Zanzibar inaitekeleza kwa mara ya mwanzo kabisa na kwamba haijapata kutokea Tanzania. Pia ni mara ya kwanza kwa programu kama hii kuanzishwa katika ukanda huu wa magharibi ya bahari ya hindi. Pamoja na changamoto mbali mbali ikiwemo ya muda na athari za mdororo wa UVIKO19, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilipambana kwa hali na mali kufanikisha malengo ya programu hii.

Moja ya ishara kubwa ya mafanikio ya SMZ na Wizara ya Uchumi wa Buluu kwa ujumla ni kuona wataalamu kutoka Tanzania Bara na pia hata kutoka Afrika Kusini wakija Zanzibar kujifunza, kusoma kwetu SMZ na WUBU, na kubuni miradi yao kutokana na utaalamu walioupata kwetu na programu hii ya uwezeshaji ya UVIKO19 iliyoasisiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane.Kuchelewa kugawiwa kwa Boti hasa za ukulima wa mwani ulitokana na kutokuwepo kwa mashine za YAMAHA ORIGINAL HP 9.9 katika masoko yote makuu ya kimataifa kama ilivyoelezwa hapo awali.

Tatizo hili ndilo lililochukua muda mrefu na hadi Wizara ilipochukua uamuzi wa kuendelea na kuzitafuta mashine za YAMAHA ORIGINAL 9.9 HP kutoka Japan. Ndipo JICA ilipoisaidia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kuwasiliana na kampuni mama ya YAMAHA Japan ambayo ilikubali kuanza kuzitengeneza mashine hizo za HP 9.9 na kuzisafirisha kujaTanzania kwa awamu kupitia Wakala anayetambuliwa na Japan kwa mashine original za YAMAHA hapa Tanzania aitwaye Nilefishnet Motors Ltd.

Changamoto nyengine ambayo Wizara inaiona ni ile ya kuwepo kwa mwamko mdogo wa vikundi vya akina mama (tofauti na vikundi wa wavuvi ambao wengi wao ni wanaume) katika kuchangamkia fursa za mikopo ya maboti. Pamoja na kuwa uhamasishaji umefanyika kwa Mikoa yote na kwa hivi sasa wanufaika wa boti za Uvuvi wamejitokeza zaidi, hili ni ene ambalo linahitaji msisitizo zaidi. Vilevile wakulima wa mwani hivi sasa wanaendelea kuchukua boti hizo.

Changamoto ya kutokuwepo kwa mabohari ya kutosha ni ya wazi kabisa na Wizara ilifanya jitihada mbali mbali za kuzihifadhi boti katika maeneo salama ya Weni (Pemba) na Kizimbani (Unguja). Pamoja na changamoto hizo, boti hizo kwa sasa zimehifadhiwa vizuri Weni Wete Pemba na Kizimbani Unguja. Tofauti na maoni ya Ripoti ya CAG, hakuna boti zilizoharibika na kuitia hasara Serikali.

Boti zote zipo accounted for na taarifa zote zipo wazi kabisa, na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inaendelea kusonga mbele na utekelezaji wa jitihada wa Serikali za kuwaondoshea wananchi ukali wa Maisha, na hasa wakulima wa mwani, kwa kuwaongezea miradi mingine kama ile ya IFAD, FAO, na inayokuja ya KOICA na Benkiya Dunia ya TASFAM.

Wizara inaendelea utekelezaji wa program hii ya UVIKO19 na mikopo yake na pia kuendelea kuwashajihisha wananchi juu ya mkopo huu kwa lengo la kuwakwamuwa kiuchumi kutokana na janga la Uviko 19 na kwamba mkopo huu ni nafuu na hauna riba.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake, ni kweli kasoro hii ilikuwepo. Hata hivyo, Wizara tayari imechukua juhudi ya kuzisambaza boti hizo katika maeneo husika kama ilivyokusudiwa. Kamati imegundua kuwa kwa upande wa boti za mita tano wakulima wengi wa mwani hawajazikubali kwa sababu ni nyepesi ila wanachi wameendelea kupatiwa muamko.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wizara uhakikishe kabla ya kufanya maamuzi yoyote yanayowagusa wananchi wafanye utafiti kabla ya utekelezaji kuanza hususan katika utengenezaji wa viwango vya boti husika.

# 6.0 MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA KWA FEDHA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR NA WAHISANI WA MAENDELEO - PEMBA

## 6.3 MIRADI YA UJENZI WA MADARASA NA MASOKO MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Taarifa hii ya ukaguzi wa miradi inatolewa kuhusu Miradi ya Ujenzi wa Madarasa na Masoko inayojengwa katika maeneo mbali mbali ya Mkoa wa Kaskazini Pemba iliotekelezwa na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo ambae ni Mkandarasi wa miradi hiyo. Ukaguzi umefanywa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu za ukaguzi wa hesabu. Matokeo ya ukaguzi yanatokana na uchunguzi na tathmini za kumbukumbu za Miradi ya Ujenzi wa Madarasa na Masoko inayojengwa kupitia fedha za UVIKO 19 pamoja na kuchunguza mfumo wa tathmini wa udhibiti wa ndani (Internal Control) ambao unahitaji uangalifu wa uongozi.

### Hoja Nambari 6.3.1.1: Kutokukatwa kwa kodi ya ongezeko la thamani shilingi 60,101,175

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 400,674,500 kwa ajili ya huduma ya

ununuzi wa vifaa mbalimbali vya Ujenzi wa madarasa na masoko bila ya kukatwa asilimia 15% kodi ya ongezeko la thamani (VAT 15%) ambapo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yanayotokana na kodi hiyo. Kufanya malipo bila ya kuzingatia pato la Serikali ni kwenda kinyume na Sheria ya Kodi ya Mapato ya Tanzania ya mwaka 2004.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo KMKM - PEMBA kuongeza juhudi katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo kiukamilifu ikiwemo kukata kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kuiwasilisha katika Mamlaka husika kwa ajili ya kukuza mapato ya Serikali.

Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya ongezeko la thamani VAT ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 83: Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT)**

| Na. | Hati Nambari | Hundi Nambari | Aliyelipwa | Fedha Zilizolipwa (Tshs) | Kodi iliyokosekana (VAT 15%) (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 23/06 20/06/2022 | - | Mohammed Khalfan Adeyyoum | 3,825,000 | 573,750 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa saruji kwa ajili ya ujenzi wa madarasa. |
| 2. | 17/06 20/06/2022 | | Iddi Hamad Ali | 3,000,000 | 450,000 | |
| 3. | 24/04 25/04/2022 | T.T | United Trade Enterprises | 170,000,000 | 25,500,000 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi katika Mradi wa Ujenzi wa Madarasa na Masoko |
| 4. | 19/04 13/04/2022 | - | Iddi Hamad Ali | 36,882,000 | 5,532,300 | |
| 5. | 11/04 08/04/2022 | | | 31,860,000 | 4,779,000 | |
| 6. | 6/04 04/04/2022 | | | 17,887,500 | 2,683,125 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7. | - 01/02/2022 | T.T | United Trade Enterprises | 100,000,000 | 15,000,000 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi katika Mradi wa Ujenzi wa Madarasa na Masoko |
| 8. | 17/03 15/03/2022 | - | Tanga Cement Company Limited | 23,600,000 | 3,540,000 | |
| 9. | 13/05 20/05/2022 | T.T | Mahafoudhi Iddy Ally | 13,620,000 | 2,043,000 | |
| **Jumla ya kodi iliyokosekana** | | | | | **60,101,175** | |

## Majibu ya Uongozi wa KMKM

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimetekeleza Mradi wa Ujenzi wa Madarasa na Masoko (Uviko 19) kama ni operation maalum na agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ kwamba fedha za mradi huu zisikatwe kodi, hata hivyo kuna baadhi ya malipo yalikatwa kodi na tuliomba marejesho ya kodi hiyo kupitia barua ya tarehe 08/11/2022 yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01C/148/2022 na kujibiwa kupitia barua ya tarehe 28/11/2022 yenye kumbukumbu namba HD.248/333/03/48 na fedha hizo zilirejeshwa kikosini.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia na kuchunguza ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za upatikanaji wa ruhusa ya msamaha wa kodi kwa vile KMKM ilitumia barua iliyotolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango yenye kumbukumbu nambari CBC.195/551/01/36 ya tarehe 17 Oktoba, 2022 ambayo iliyowataka fedha hizo zirudishwe Kikosini. Kiutaratibu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ndio muhusika pekee anayetambulika kisheria kutoa msamaha wa kodi kwa niaba ya Mheshimiwa Rais,kwa msingi huo, Kamati imebaini kuwa KMKM haikufuata utaratibu kama ulivyoainishwa na Sheria.

Aidha, Kamati ilijadili kwa undani hoja hii kwa kutaka ipatiwe uthibitisho (Risiti) wa kulipwa kwa kodi hiyo kutoka Mamlaka ya Mapato Zanzibar lakin kwa bahati mbaya hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake, kielelezo hicho hakikuweza kuwasilishwa mbele ya Kamati na kupata mashaka juu ya ulipwaji wa kodi hiyo.

Hata hivyo, Kamati ya PAC haikuridhika na hoja hii kwa vile taratibu na miongozo ya

ulipaji kodi haikufutwa na kupelekea hoja hii kubakia.

**Maoni Ushauri na Mapendekezo wa Kamati ya PAC**

Uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) pamoja na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba inafuatwa miongozo na taratibu za msamha wa kodi ili kuepuka ukiukwaji wa taratibu za ulipaji kodi pamoja na kuikosesha mapato Serikali.

## Hoja Nambari 6.3.1.2: Kutokukatwa kwa kodi ya zuio shilingi 57,060,856.4

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimefanya malipo ya shilingi 2,927,979,692.22 kwa watoa huduma mbali mbali kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya Ujenzi wa Madarasa na Masoko. Dosari iliyobainika ni kutokukatwa kwa kodi ya zuio yenye jumla ya shilingi 57,060,856.4

Kufanya hivyo ni kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo, aidha ni kwenda kinyume na Sheria ya Kodi ya Mapato ya Tanzania ya mwaka 2004.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo KMKM-PEMBA kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo ya malipo iliyopo kiukamilifu ikiwemo kukata Kodi ya zuio na kuwasilisha kodi hiyo kwenye Mamlaka husika kwa ajili ya kukuza mapato ya Serikali. Malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 84: Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio**

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Aliyelipwa | Fedha zilizolipwa (Tshs) | Kodi iliyokosekana (VAT 2%) Tshs | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 10/1 28/06/2022 | | Aboubakar Mohammed Abdallah | 8,308,750 | 166,175 | |
| 35/06 29/06/2022 | | | 19,703,000 | 394,060 | |
| 34/06 29/06/2022 | | | 13,923,000 | 278,460 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 27/06<br>25/06/2022 | - | Iddi Hamad Ali | 30,000,000 | 600,000 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya madarasa na masoko. |
| 20/03<br>20/06/2022 | | | 15,300,000 | 306,000 | |
| 12/06<br>08/06/2022 | | | 45,804,630 | 916,092.6 | |
| 6/06<br>01/06/2022 | | | 10,948,000 | 218,960 | |
| 27/05<br>27/05/2022 | | | 22,610,000 | 452,200 | |
| 26/05<br>27/05/2022 | | | 9,180,000 | 183,600 | |
| 11/05<br>19/05/2022 | | | 27,880,000 | 557,600 | |
| 15/05<br>23/05/2022 | | | 41,412,000 | 828,240 | |
| 19/05<br>20/05/2022 | | Mohammed Khalfan Adeyem | 10,710,000 | 214,200 | |

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Aliyelipwa | Fedha zilizolipwa (Tshs) | Kodi iliyokosekana (VAT 2%) Tshs | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 16/05 20/05/2022 | | Massoud Abrahman Masoud | 9,078,000 | 181,560 | |
| 4/06 01/06/2022 | T.T | United Trader Enterprises | 425,000,000 | 8,500,000 | |
| 01/05 02/05/2022 | | | 600,000,000 | 12,000,000 | |
| 21/05 25/05/2022 | | | 260,868565.22 | 5,217,371.3 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya madarasa na masoko. |
| 27/02 27/03/2022 | | | 200,000,000 | 4,000,000 | |
| 22/03 17/03/2022 | | | 200,000,000 | 4,000,000 | |
| 22/04 25/04/2022 | | Iddi Hamad Ali | 54,250,000 | 1,085,000 | |
| 24/04 25/04/2022 | | United Trader Enterprises | 170,000,000 | 3,400,000 | |
| 08/04 04/04/2022 | | | 255,000,000 | 5,100,000 | |
| 18/04 13/04/2022 | | Iddi Hamad | 36,882,000 | 737,640 | |
| 11/04 | | | 31,860,000 | 637,200 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 08/04/2022 | | Ali | | | |
| 06/04 04/04/2022 | - | | 17,887,500 | 357,750 | |
| 17/03 15/03/2022 | | Tanga Cement Company Limited | 23,600,000 | 472,000 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya madarasa na masoko. |
| 06/03 02/03/2022 | | Massoud Abrahman Massoud | 5,825,000 | 116,500 | |
| 11/02 17/02/2022 | | | 14,730,375 | 294,607.5 | |
| 26/03 25/02/2022 | | Tanga Cement Company Limited | 6,882,000 | 137,640 | |
| 09/02 17/02/2022 | | | 17,700,000 | 354,000 | |
| 20/02 24/02/2022 | | | 17,700,000 | 354,000 | |
| 02/02 04/02/2022 | | Abdulla Mohamed Abeid | 50,000,000 | 1,000,000 | |

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Aliyelipwa | Fedha zilizolipwa (Tshs) | Kodi iliyokosekana (VAT 2%) Tshs | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 19/02 23/02/2022 | | United Trader Enterprises | 100,000,000 | 2,000,000 | |
| - 01/02/2022 | | | 100,000,000 | 2,000,000 | |
| Jumla ya kodi iliyokosekana | | | | 57,060,856.4 | |

**Majibu ya Uongozi wa KMKM**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimetekeleza Mradi wa Ujenzi wa Madarasa na Masoko (Uviko 19) kama ni operation maalum na agizo la Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ kwamba fedha za mradi huu zisikatwe kodi, hata hivyo kuna baadhi ya malipo yalikatwa kodi na tuliomba marejesho ya kodi hiyo kupitia barua ya tarehe 08/11/2022 yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01C/148/2022 na kujibiwa kupitia barua ya tarehe 28/11/2022 yenye kumbukumbu namba HD.248/333/03/48 na fedha hizo zilirejeshwa kikosini.

**Uchunguzi na Mapendekezo wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa uchunguzi na mapendekezo ya hoja hii yanafanana na uchunguzi na mapendekezo ya hoja iliyopita (nambari 6.3.1.1). hivyo Kamati haikuwa na maelezo zaidi.

## Hoja Nambari 6.3.1.3: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 370,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba hati za malipo zenye jumla ya shilingi 370,000,000 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya ujenzi wa madarasa na masoko na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Pemba lakini hati za malipo hayo pamoja na vielelezo vyake hazikupatikana kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea uhalali wa malipo hayo kutokuthibitika kisheria, aidha

ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamandi ya KMKM Pemba kuongeza juhudi katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo kiukamilifu ikiwemo kuzitayarisha na kuzihifadhi hati zote za malipo kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Hati hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 85: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi**

| Hati Namba | Hundi Namba | Fedha Iliyolipwa (Tshs) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 22/3<br>18/03/2022 | T.T | 140,000,000 | United Traders Enterprises |
| 25/03<br>25/03/2022 | | 60,000,000 | Transfer T.T ZRB |
| 26/03<br>28/03/2022 | | 170,000,000 | United Traders Enterprises |
| **Jumla** | | **370,000,000** | |

**Majibu ya Uongozi wa KMKM**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kuhusu hati za malipo zilizotajwa na Mdhibiti na Mkaguuzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zilikuwepo wakati wa ukaguzi na zimekaguliwa na kuwekwa alama za vyema, Kikosi cha KMKM kinashangaa hoja hiyo kuwekwa katika kitabu na kinaomba kuziwasilisha kwa uthibitisho wa hilo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kulikuwa na makosa katika uandishi wa hoja hii kwani hati namba 26/3 ya tarehe 28/3/2022 iliandikwa kimakosa lakini kiuhalisia ilitakiwa iwe hati namba 27/3 ya tarehe 28/3/2022 ya shilingi 170,000,000 iliyolipwa kwa United Traders Enterprises. Kamati baada ya kupitia vielelezo hivyo, imegundua kuwa vielelezo

hivyo kweli vilikaguliwa na Mkaguzi na kuridhika navyo. Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC imeridhika na vielelezo hivyo na kuiondoa hoja hiyo.

## Hoja Nambari 6.3.1.4: Kutokutayarishwa na kuwasilishwa kwa taarifa za hesabu za miradi

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Pemba imetekeleza miradi mbali mbali ya Ujenzi wa Madarasa na Masoko ambapo kwa mujibu wa taratibu za kisheria KMKM ilitakiwa kutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu za miradi hiyo (Project Financial Statements) katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Pemba imeshindwa kutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu za Miradi ya Ujenzi wa Madarasa na Masoko katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

Kushindwa kuandaa hesabu ya mapato na matumizi pamoja na kuiwasilisha taarifa hiyo kunatoa fursa ya kushindwa kukaguliwa na kutolewa maoni ya kitaalamu kwa dosari zote ambazo zitakazobainika kwa lengo la kuchukua hatua za marekebisho kwa mara nyengine ya utekelezaji wa aina kama hiyo ya miradi.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa mwanya wa kufanyika kwa ubadhirifu wa fedha za Umma, aidha ni kwenda kinyume na Kifungu namba 119(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa KMKM-Pemba kuongeza juhudi katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo kiukamilifu ikiwemo kuandaa na kuziwasilisha taarifa za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka.

### Majibu ya Uongozi wa KMKM

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimetekeleza Mradi wa Ujenzi wa Madarasa na Masoko na kuwasilisha taarifa za hesabu za miradi hiyo kupitia kitabu cha Taarifa ya hesabu ya Mwaka wa fedha 2021-2022 na taarifa za miradi hiyo inaonekana katika page No. 5, 29 na 32 na kitabu hicho kiliwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguuzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama taratibu zinavyoelekeza kwa uthibitisho wa hilo naomba ukione kitabu husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika uchunguzi wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) Pemba kwa mujibu wa taratibu za ufungaji hesabu za mwisho wa mwaka hawakupaswa kuanisha fedha ya matumizi ya mradi katika 'Financial Statements' yao. Hata hivyo, taarifa hiyo ilipaswa kuonekana katika 'Financial Statements' ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwani ndio wasimamizi wa Mradi wa Ujenzi wa Madarasa kwa Mkoa wa Kaskazini - Pemba.

Sambamba na hilo Kamati ya PAC ilitaka kujua muendelezo wa bakaa ya shilingi 1,260,984,034 ambayo KMKM haikuweza kuonekana katika taarifa ya hesabu zao za mwisho wa mwaka ili kujua muendelezo wa matumizi wa fedha hiyo katika mwaka wa fedha uanofuata.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Maafisa Wahasibu wawe makini wanapoandaa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka hususan kwa kuainisha fedha ambazo zinahitajika kutumika katika mwaka unaofuata ili kuondokana na hoja zisizohitajika.

## Hoja Nambari 6.3.1.5: Dosari zilizobainika katika utoaji wa zabuni za usambazaji wa vifaa vya ujenzi

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) Zanzibar kimepewa jukumu la ujenzi wa miradi mbali mbali ya Masoko na Madarasa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Katika utekelezaji wa kazi hizo Kikosi cha KMKM kimetoa zabuni ya usambazaji wa vifaa vya ujenzi kwa Kampuni ya United Traders Enterprises ya Saateni Zanzibar.

Katika ukaguzi uliofanyika dosari mbali mbali kuhusu utoaji wa zabuni hiyo zilibainika kama ifuatavyo:

a) Kutokuwepo kwa kumbu kumbu za utolewaji wa zabuni za ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ukaguzi.

b) Mikataba ya zabuni ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi baina ya Kikosi cha KMKM na Kampuni ya United Traders Enterprises haikupatikana kwa ukaguzi.

c) Uthibitisho wa usajili wa Kampuni hiyo katika Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma haukupatikana kwa ukaguzi.

d) Kutokutambulika kwa usajili wa Kampuni ya United Traders Enterprises katika Mamlaka za kodi za ZRB na TRA.

e) Kikosi cha KMKM imempa zabuni mfanyabiashara ambaye ni Mohammed Muhidini Chache wa Saateni aliyetumia jina la kampuni la United Traders Enterprises katika kuomba zabuni.

f) Risiti za malipo ya zabuni zinaonyesha kwamba malipo hayo yamefanywa kwa mtu binafsi (Mohammed Muhidini Chache) badala ya kufanywa kwa kampuni ya United Traders Enterprises kama ilivyobainishwa katika hati za malipo.

g) Risiti za malipo ya kodi za ZRB zinaonyesha kwamba malipo ya kodi hiyo yamelipwa kwa jina la Mohammed Muhidini Chache badala ya kulipwa kwa jina la Kampuni ya United Traders Enterprises kama ilivyobainishwa katika hati za malipo.

h) Kutokuwepo kwa mchanganuo wa vifaa ambavyo mfanyabiashara huyo amepewa kazi za kuvisambaza.

i) Kutokuwepo kwa sahihi za kupokea na kutolea vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa na kuwasilishwa kwa ajili ya utekelezaji katika madaftari ya kuhifadhia bidhaa za ghalani.

j) Kutokujulikana kwa idadi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa kila mradi pamoja na vifaa halisi vilivyotumika katika kila mradi.

Kuwepo kwa dosari katika utoaji wa zabuni kunaweza kupelekea uwepo wa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na sheria nambari 12 ya usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa KMKM Pemba kuongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo katika kufuata utaratibu wa utoaji wa zabuni.

### Majibu ya Uongozi wa KMKM

A. Kutokuwepo kwa kumbukumbu za utolewaji wa zabuni za ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ukaguzi.

### Majibu ya hoja (a)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kilipokea zabuni ya Ujenzi wa madarasa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na mradi wa ujenzi wa Masoko (Tumbe na Kifumbikai) kutoka Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ikiwa ni maagizo na maelekezo ya Serikali kuu.

Kwa kawaida KMKM hutumika kama mzabuni kwa zabuni zote tunazopokea kutoka

taasisi za Serikali ambapo taratibu zote za manunuzi hufanywa na taasisi husika, hivyo KMKM hupokea malipo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi husika, KMKM hatuwezi kutangaza zabuni ndani ya zabuni kwani itapekeleka kupanda kwa gharama na kutokumalizika kwa kazi husika kwa muda uliopangwa, aidha kazi hizo kwa Idara Maalum hufanywa kwa uzalendo na gharama nafuu kwa maslahi ya taifa na huwa ni maagizo na maelekezo maalum ya kutoka serikalini na kuzifanya kazi hizo kioperation.

B. Mikataba ya zabuni ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi baina ya Kikosi cha KMKM na Kampuni ya United Traders Enterprises haikupatikana kwa ukaguzi.

**Majibu ya hoja (b)**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kilipokea zabuni ya Ujenzi wa madarasa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na mradi wa ujenzi wa Masoko (Tumbe na Kifumbikai) kutoka Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kwa kawaida KMKM hutumika kama mzabuni kwa zabuni zote tunazopokea kutoka taasisi za Serikali ambapo taratibu zote za manunuzi hufanywa na taasisi husika, hivyo KMKM tumefunga mkataba na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na mradi wa ujenzi wa Masoko (Tumbe na Kifumbikai) kutoka Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ hivyo hatuwezi kufunga mkataba ndani ya mkataba.

Uthibitisho wa usajili wa Kampuni hiyo katika Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma haukupatikana kwa ukaguzi.

**Majibu ya hoja (c)**

Kuhusu hoja ya uthibitisho wa usajili wa kampuni ya United Traders Enterprises kwenye mamlaka ya manunuzi, kampuni hii imesajiliwa kihalali na inayo leseni ambayo iko hai kwenye mamlaka hiyo. Aidha kampuni hii kila mwaka inalipia leseni hiyo inapomaliza muda wake. Kwa mwaka 2021 kampuni hii ilisajiliwa na mamlaka hiyo kwa cheti no (Reg No. ZPPDA/G/0589/2021 ambao usajili wake umemaliza 26 May 2022 na kwa mwaka 2022 kampuni hii imesajiliwa na mamlaka hii kupitia Reg No G001058, tunaambatanisha na vivuli vya vyeti vyote hivyo kwa ajili ya uthibitisho zaidi.

D. Kutokutambulika kwa usajili wa Kampuni ya United Traders Enterprises katika Mamlaka za kodi za ZRB na TRA.

**Majibu ya hoja (d)**

Kuhusu usajili wa kampuni ya United traders enterprises kwa upande wa TRA na ZRB

(ZRA) kampuni hii ina usajili kamili wa muda mrefu na ni katika walipa kodi wakubwa sana (large tax payer) kwenye nchi yetu kwa mamlaka zote hizo za kodi.

- Kwa upande wa TRA, kampuni hii imeajiliwa mnamo 05/10/2001 na kupitia namba ya mlipa kodi (TIN) No: 101-200-493.
- Uthibitisho wa usajili wa Kampuni hiyo katika Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma haukupatikana kwa ukaguzi.

**Majibu ya hoja (c)**

Kuhusu hoja ya uthibitisho wa usajili wa kampuni ya United Traders Enterprises kwenye mamlaka ya manunuzi, kampuni hii imesajiliwa kihalali na inayo leseni ambayo iko hai kwenye mamlaka hiyo. Aidha kampuni hii kila mwaka inalipia leseni hiyo inapomaliza muda wake. Kwa mwaka 2021 kampuni hii ilisajiliwa na mamlaka hiyo kwa cheti no (Reg No. ZPPDA/G/0589/2021 ambao usajili wake umemaliza 26 May 2022 na kwa mwaka 2022 kampuni hii imesajiliwa na mamlaka hii kupitia Reg No G001058, tunaambatanisha na vivuli vya vyeti vyote hivyo kwa ajili ya uthibitisho zaidi.

D. Kutokutambulika kwa usajili wa Kampuni ya United Traders Enterprises katika Mamlaka za kodi za ZRB na TRA.

**Majibu ya hoja (d)**

Kuhusu usajili wa kampuni ya United traders enterprises kwa upande wa TRA na ZRB (ZRA) kampuni hii ina usajili kamili wa muda mrefu na ni katika walipa kodi wakubwa sana (large tax payer) kwenye nchi yetu kwa mamlaka zote hizo za kodi.

- Kwa upande wa TRA, kampuni hii imeajiliwa mnamo 05/10/2001 na kupitia namba ya mlipa kodi (TIN) No: 101-200-493.
- Kwa upande wa ZRB (ZRA) kampuni hii ilisajiliwa rasmi mnamo 22/02/2010 na kupatiwa ZRB No: 07000606C na Z0025338071

Tunaambatanisha na vivuli vyote hivi kwa ajili ya uthibitisho zaidi.

E. Kikosi cha KMKM imempa zabuni mfanyabiashara ambaye ni Mohammed Muhidini Chache wa Saateni aliyetumia jina la kampuni la United Traders Enterprises katika kuomba zabuni.

**Majibu ya hoja (e)**

Kuhusu kumpa zabuni mfanyabiashara Mohammed Muhidini Chache ambae ametumia jina la kampuni ya United Traders Enterprises, hoja hii jawabu lake lipo wazi kwani Ndugu Mohammed Muhidin Chache ndie mmiliki pekee na mkurugenzi mkuu wa kampuni ya

United traders Enterprises. Na yeye ndie mmiliki wa asilimia 100 ya hisa za kampuni hiyo, na yeye ndie anefahamika na mamlaka zote za usajili wa kampuni za nchi hii kwa sheria za nchi hii ya kuwa ndugu Mohammed Muhidini Chache ndio sawa na United Traders Enterprises.

Kwa kifupi kabisa kamuni hii ni single member company na ndugu Mohammed Muhidini Chache ni sole proprietor wa kampuni hiyo, hili linathibitishwa na certificate of reg, yenye reg No Z0000047281 kutoka business Entities reg, ACT No.12 ya 2012.

F. Risiti za malipo ya zabuni zinaonyesha kwamba malipo hayo yamefanywa kwa mtu binafsi (Mohammed Muhidini Chache) badala ya kufanywa kwa kampuni ya United Traders Enterprises kama ilivyobainishwa katika hati za malipo.

**Majibu ya hoja (f)**

Kuhusu risiti za malipo kwa ndugu Mohammed Muhidin Chache badala ya United Traders Enterprises, hoja hii usahihi wake ni kwamba malipo yote yamefanyika kwa akaunti ya United Traders Enterprises kwa Pbz Bank na nambari ya akaunti ni 0767695001 na Nmb Bank kupitia namba ya akaunti 23410003093, zote hizi ni akaunti za United Trades Enterprises.

Mara tu baada ya kupokea kwa malipo hayo kampuni ilileta risiti zinazosomeka kwa jina la United Traders Enterprises, pia tunaambatanisha baadhi ya vivuli vya risiti hizo za malipo kwa ajili ya ushahidi zaidi.

G. Risiti za malipo ya kodi za ZRB zinaonyesha kwamba malipo ya kodi hiyo yamelipwa kwa jina la Mohammed Muhidini Chache badala ya kulipwa kwa jina la kampuni ya United Traders Enterprises kama ilivyobainishwa katika hati za malipo.

**Majibu ya hoja (g)**

Kuhusu risiti za malipo ya kodi kuandikwa kwa jina la Mohammed Muhidini Chache na badala ya United Traders Enterprises, hoja hii kama inavyojionesha kwenye usaajili wa TRA Na ZRB ya kuwa United Traders Enterprises kwenye miamala ya kodi ni sawa na Mohammed Muhidini Chache, uthibitisho wa hili unaonekana kwenye vivuli vya TRA na ZRB tulivyoviambatanisha kwenu.

H. Kutokuwepo kwa mchanganuo wa vifaa ambavyo mfanyabiashara huyo amepewa kazi za kuvisambaza.

**Majibu ya hoja (h)**

Kuhusu kutokuwepo kwa mchanganuo wa kwenye usambazaji huo, mchanganuo wa gharama kwa kila shule au soko husika upo na tunaambatanisha tena kupitia taarifa hii

kwa ushahidi zaidi.

I. Kutokuwepo kwa sahihi za kupokea na kutolea vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa na kuwasilishwa kwa ajili ya utekelezaji katika madaftari ya kuhifadhia bidhaa za ghalani.

**Majibu ya hoja (i)**

Kuhusu hoja ya kutokuwepo kwa sahihi za kupokea na kutolea vifaa kwenye madaftari ya ghalani, kimsingi hoja hii sio ya kweli, ukweli ni kwamba vifaa vyote vimepokelewa na kutolewa kwa kuwekwa sahihi katika madaftari husika.

Kutokujulikana kwa idadi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa kila mradi pamoja na vifaa halisi vilivyotumika katika kila mradi.

**Majibu ya hoja (j)**

Kikosi Maaalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimetekeleza mradi wa ujenzi wa Masoko kwa gharama ya TZs 2,289,463,035 vile vile KMKM imetekeleza mradi wa ujenzi wa Madarasa kwa gharama ya Tzs 3,652,371,780.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kulikuwa na changamoto za kiutendaji ambapo fedha za Miradi ya Maendeleo ya Ujenzi wa Madarasa zilikuwa zikiingizwa katika hesabu ya Mkuu wa KMKM badala ya kuingizwa moja kwa moja katika Kampuni ya Ujenzi ya KMKM Marine Engeneering General Contruction pamoja na kwamba inamilikiwa na KMKM lakini kiutaratibu wa ufungaji Hesabu za mwisho wa mwaka, Kamapuni huwa inajitegemea na fedha hizo zilihitajika kuonekana katika hesabu ya Kampuni na sio hesabu ya Mkuu wa KMKM. Kutokana na kuwepo kwa kasoro hiyo, Kamati haikuridhika na majibu ya KMKM na kupelekea hoja hiyo kubakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kikosi cha Kuzia Magendo - Pemba kihakikishe kinachukua juhudi za makusudi kutenganisha hesabu (akaunti) za fedha za Mradi na za matumizi ya uendeshaji wa Ofisi (hesabu ya Mkuu wa KMKM) ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

## Hoja Nambari: 6.3.1.6: Dosari katika malipo ya miradi ya ujenzi wa Masoko na Madarasa

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo KMKM Zanzibar kimepewa jukumu la utekelezaji wa miradi mbali mbali ya ujenzi wa Masoko na Madarasa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba

ambapo baadhi ya fedha za utekelezaji wa miradi hiyo huingizwa katika Akaunti ya KMKM Pemba kutoka Akaunti ya KMKM Zanzibar kwa ajili ya kumlipa mfanyabiashara ambaye ni United Traders Enterprises wa Saateni Zanzibar kwa ajili ya usambazaji wa bidhaa mbali mbali za ujenzi, na baadhi ya malipo kwa mfanyabiashara huyo hulipwa na Makao Makuu ya KMKM Zanzibar na mfanyabiashara huyo kutakiwa kuwasilisha vifaa vya ujenzi kwa Kamandi ya KMKM Pemba. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa dosari mbali mbali za kiutendaji kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo: -

Kamandi ya KMKM Pemba kutokufungua akaunti maalum (Force Account) kwa ajili ya kupokea na kulipa fedha za miradi.

Kutokubagua kumbu kumbu za kimahesabu zinazohusu miradi na matumizi ya kawaida.

Kamandi ya KMKM Pemba hupokea baadhi ya fedha kwa njia ya uhaulishaji kutoka Makao Makuu ya KMKM Zanzibar na baadae kutakiwa kufanya malipo kwa Kampuni ya United Traders Enterprises ya Saateni bila ya Kamandi ya KMKM Pemba kuwa na vielelezo vinavyoruhusu kufanya malipo hayo.

Ankara ya malipo (Tax Invoice) kutokuanisha bidhaa za ujenzi zilizonunuliwa pamoja na bei halisi za bidhaa hizo.

Kutokuwepo kwa hati ya mapokezi ya bidhaa (Delivery Note) inayothibitisha kwamba bidhaa hizo zimepokelewa kiukamilifu.

Kutokuwepo kwa baadhi ya madaftari ya ghalani kwa ajili ya kurikodia mapokezi na matumizi ya bidhaa za ghalani.

Kutokuwepo kwa B.O.Q ya miradi ya ujenzi iliyotekelezwa.

Kutokuanishwa kwa viwango halisi vya fedha zilizotumika, vifaa vilivyotumika pamoja na bakaa ya vifaa hivyo katika kila skuli na soko.

Kuwepo kwa dosari katika malipo ya mzabuni kunaweza kupelekea uwepo wa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamandi ya KMKM Pemba kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo pamoja na kusimamia vyema utekelezaji wa vipengele vyote vya mradi ambavyo vimeainishwa katika mikataba ya ujenzi.

**Majibu ya Uongozi wa KMKM**

Kamandi ya KMKM Pemba kutokufungua akaunti maalum (Force Account) kwa ajili ya kupokea na kulipa fedha za miradi.

**Majibu ya hoja (a)**

Mwazoni mwa utekelezaji wa miradi yetu kutokana na uharaka wa miradi hiyo tulikuwa hatuna account maalum (Force Account ) lakini mnamo mwezi wa October 2022 account maalum (Force Acount) ilifunguliwa kupitia Pbz Bank tawi Wete yenye No 0831015001 na mnamo Tarehe 01/11/2022 Account hiyo ilianza kufanya kazi na kutumika Rasmin na inaendelea kufanya kazi kama kawaida.

B. Kutokubagua kumbu kumbu za kimahesabu zinazohusu miradi na matumizi ya kawaida.

**Majibu ya hoja (b)**

Tulishindwa kubagua kumbukumbu za mahesabu zinazohusu miradi na matumizi ya kawaida, hii ni kutokana na kuwa na akaunti moja ya kupokea na kutumia fedha hizo, kutokana na ujio wa ghafla wa miradi ya masoko na madarasa ilitulazimu kutumia akaunti hiyo hiyo moja lakini kwa sasa tumeshatenganisha kumbukumbu za kimahesabu baina ya akaunti hizo mbili baada ya kufungua akaunti maalum ya miradi.

Kamandi ya KMKM Pemba hupokea baadhi ya fedha kwa njia ya uhaulishaji kutoka Makao Makuu ya KMKM Zanzibar na baadae kutakiwa kufanya malipo kwa Kampuni ya United Traders Enterprises ya Saateni bila ya Kamandi ya KMKM Pemba kuwa na vielelezo vinavyoruhusu kufanya malipo hayo.

**Majibu ya hoja (c)**

Mkaguzi (CAG) aliibua hoja hiyo baada ya kukosa kuona vielelezo kwenye vocha za malipo, ukweli ni kwamba vielelezo hivo vipo ila vilitenganishwa na vocha hizo, hii ilitokea baada ya mzabuni kusambaza vifaa vingi kwa maaneo tofauti na nyakati tofauti ikapelekea kupata changamoto ya kupata vilelelezo kwa wakati uleule na baadae mzabuni alipata maelekezo kutoka ZRA ya kuandaa Tax Invoice za pamoja kwa mfumo wa kitabu zinayoonyesha usambazaji wa vifaa kwa kila skuli na masoko, Hivyo basi Tax Invoice hizo ziliwasilishwa ofisi ya KMKM Kamandi ya Pemba Kwa taratibu za malipo husika.

D. Ankara ya malipo (Tax Invoice) kutokuanisha bidhaa za ujenzi zilizonunuliwa pamoja na bei halisi za bidhaa hizo.

**Majibu ya hoja (d)**

Mkaguzi (CAG) aliibua hoja hiyo baada ya kutokuona Tax Invoice ilioanisha bidhaa za ujenzi zilizonunuliwa pamoja na bei halisi za bidhaa hizo kwenye vocha za malipo, ukweli ni kwamba Tax Invoice hizo zipo ila zilitenganishwa na vocha, hii ilitokea baada ya

mzabuni kusambaza vifaa vingi kwa maaneo tofauti na nyakati tofauti ikapelekea kupata changamoto ya kupata vilelelezo kwa wakati ule ule na baadae mzabuni alipata maelekezo kutoka ZRA ya kuandaa Tax Invoice za pamoja kwa mfumo wa kitabu zinayoonyesha usambazaji wa vifaa kwa kila skuli na masoko, Hivyo basi Tax Invoice hizo ziliwasilishwa ofisi ya KMKM Kamandi ya Pemba Kwa taratibu za malipo husika.

E. Kutokuwepo kwa hati ya mapokezi ya bidhaa (Delivery Note) inayothibitisha kwamba bidhaa hizo zimepokelewa kiukamilifu.

**Majibu ya hoja (e)**

Hoja ya kutokuwepo kwa hati ya mapokezi ya bidhaa (Delivery Note) hoja hii sio kweli ukweli ni kwamba hati hizo zilikuwepo wakati wa ukaguzi, zikakaguliwa na zipo zimehifadhiwa vizuri ambapo muda wake ukifika zitawasilishwa kunakohusika kama ambavyo sheria inavyoelekeza, hata hivyo CAG baada ya kutoziona hati hizo za malipo alishindwa kuwasiliana na wahusika sahihi ili kupata majibu na ufafanuzi sahihi juu ya hati hizo

F. Kutokuwepo kwa baadhi ya madaftari ya ghalani kwa ajili ya kurikodia mapokezi na matumizi ya bidhaa za ghalani.

**Majibu ya hoja (f)**

Hoja ya kutokuwepo kwa madaftari ya ghalani kwa ajili ya kurikodia mapokezi na matumizi ya bidhaa za ghalani, hoja hii sio kweli ukweli ni kwamba madaftari ya ghalani yamehifadhiwa vizuri ambapo muda wake ukifika yatawasilishwa kunakohusika kama ambavyo sheria inavyoelekeza, hata hivyo CAG baada ya kutokuyaona madaftari hayo alishindwa kuwasiliana na wahusika ili kupata majibu na ufafanuzi juu ya madaftrai hayo.

G. Kutokuwepo kwa B. O. Q ya miradi ya ujenzi iliyotekelezwa.

**Majibu ya hoja (g)**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimetekeleza Mradi wa Ujenzi wa Madarasa na Masoko (Uviko19) kama ni operation maalum na agizo la Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ, kwa upande wa mradi wa ujenzi wa madarasa tulikuwa hatuna B.O.Q bali tulikabidhiwa schedule of material kama ni sample ya darasa moja kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Kwa upande wa mradi wa Ujenzi wa Masoko B.O.Q ipo na imetumika ipasavyo.

G. Kutokuanishwa Kwa viwango halisi vya fedha zilizotumika, vifaa vilivyotumika pamoja na bakaa ya vifaa hivyo katika kila skuli na soko, kuwepo kwa dosari katika malipo ya

mzabuni kunaweza kupelekea uwepo wa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

**Majibu ya hoja (h)**

Kwa upande wa KMKM Kamandi ya Pemba tulipokea jumla ya Tshs 5,445,834,000/- kutoka account ya mkuu wa KMKM Zanzibar na zilitumika zote bila ya bakaa katika ujenzi wa madarasa na masoko (UVIKO 19), na kwa upande wa vifaa vilivyobakia katika mradi wa ujenzi wa madarasa na masoko vimehifadhiwa stoo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya kamati kupata maelezo ya kina kuhusiana hoja hii imeridhika na majibu ya hoja.

**Uchunguzi na Mapendekezo wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa uchunguzi na mapendekezo ya hoja hii yanafanana na uchunguzi na mapendekezo ya hoja iliyopita (nambari 6.3.1.5). Hivyo, Kamati haikuwa na maelezo zaidi.

## Hoja Nambari 6.3.1.7: Malipo yenye vielelezo pungufu shilingi 2,201,281,405

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 2,201,281,405 zimelipwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Pemba lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea uhalali wa malipo hayo kutokuthibitika kisheria jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016.

**Majibu ya Hoja ya KMKM**

Vielelezo husika vyote vipo na vimembatanishwa na hati za malipo husika kama utaratibu wa kisheria unavyoelekeza ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kulikuwa na changamoto za kiutendaji ya kutowasilishwa vielelezo ambavyo Mkaguzi alivihitaji. Hali hiyo, ilipelekea kujitokeza kimakosa katika

kitabu. Hata hivyo, Kamati ilivipitia vielelezo husika na kuridhika navyo na hatimae kuiondoa hoja hii.

## 6.6 MRADI WA UJENZI WA TUTA LA KUZUIA MAJI CHUMVI KATIKA BONDE LA TOVUNI KIUNGONI UNAOTEKELEZWA NA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO - PEMBA

### Hoja Nambari 6.6.1.1: Malipo ambayo hayakufuata utaratibu wa zabuni shilingi 132,946,020

Kwa mujibu wa kifungu 68(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, kinaeleza isipokuwa pale ilipoelezwa vyenginevyo katika Sheria hii au kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itatumia utaratibu wa wazi wa ushindani wa ndani wa zabuni.

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 132,946,020 kwa ajili ya kuwalipa watoa huduma mbali mbali katika ununuzi wa udongo uliotumika katika ujenzi wa Tuta la kuzuia maji chumvi bila ya kuitisha zabuni ili kuweza kupima uwezo wa utendaji wa mzabuni aliyechaguliwa, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 68(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuongeza juhudi katika kufuata Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuitisha zabuni pale inapohitajika kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Mchanganuo wa ununuzi wa udongo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 87: Malipo kwa ajili ya ujenzi wa Tuta la Bonde la Tovuni**

| Hati namba | Kiasi Kilicholipwa (Tshs) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 17/2 18/2/2022 | 13,170,638 | Said Suleiman Maktubu | |
| 18/2 18/2/2022 | 11,697,672 | | |
| 19/2 18/2/2022 | 13,925,800 | Mbarouk Sultan Mbarouk | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 22/2 21/2/2022 | 5,644,558 | Said Suleiman Maktubu | Malipo kwa ajili ya kazi ya kuleta udongo kwa Ujenzi wa Tuta la Bonde la Tovuni. |
| 23/2 21/2/2022 | 9,748,060 | | |
| 24/2 21/2/2022 | 3,540,322 | Mbarouk Sultan Mbarouk | |
| 27/2 21/2/2022 | 9,748,060 | Haji Ali Makame | |
| 32/2 25/2/2022 | 4,177,740 | Said Suleiman Maktubu | |
| 33/2 25/2/2022 | 1,412,230 | Mbarouk Sultan Mbarouk | |
| 34/2 25/2/2022 | 4,177,740 | Haji Ali Makame | |
| 40/2 28/2/2022 | 9,748,060 | Ali Yahya Abdalla Building Material Supplier | |
| 43/2 28/2/202 | 4,177,740 | | |
| 1/3 1/3/2022 | 9,748,060 | Haji Ali Makame | Malipo ya kazi ya kuleta udongo kwa ajili ya ujenzi wa tuta katika bonde la Tovuni. |
| 6/3 3/3/2022 | 4,177,740 | | |
| 10/3 7/3/2022 | 9,748,060 | Bin Salim Contractors and Materials Transporter CO | |
| 11/3 7/3/2022 | 4,177,740 | | |
| 16/3 10/3/2022 | 7,659,190 | | |
| ¾ 14/4/2022 | 6,266,610 | | |
| **Jumla** | **132,946,020** | | |

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Wizara inapenda kuijulisha Kamati yako kuwa kazi hii ilifanyika kwa kutumia njia ya mialiko mitatu (Three quotations) katika utekelezaji wake kwa sababu ya muda mfupi (miezi mitatu tu - Januari hadi Machi 2022) wa utekelezaji wa kazi hiyo. Hata hivyo, Wizara iliweka vigezo katika kufanikisha kazi hiyo: Usajili wa ZRB, TRA na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA). Wadau ambao walikidhi vigezo ndio ambao walichaguliwa kutekeleza mradi huo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati ya PAC imebaini mambo yafuatayo:-

1. Mradi wa Ujenzi wa Tuta la Kuzuia Maji ya chumvi katika Bonde la Tovuni ulidhaminiwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na kutekelezwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo - Pemba ambapo jumla ya shilingi 132,946,020 zilitolewa kwa ajili ya kukamilisha Mradi huo.
2. Kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za ununuzi kwa vile Sheria ya Ununuzi haikufuatwa kwani Wizara ilitumia 'three quotation' badala ya kutangaza Zabuni kwa umma. Aidha, waliamua kutumia njia hiyo bila ya kupata kibali kutoka Mamlaka ya Manunuzi kama inavyoelekezwa na Sheria.
3. Mradi huo haukuwemo katika Mpango kazi wa Wizara wala Wizara haikufanya mapitio (review) ya Mpango kazi wake hasa ukizingatia fedha hizo zilito nje ya bajeti ya Wizara.
4. Watendaji wa Wizara walitekeleza Mradi huo kwa utaratibu wa kuzigawanya fedha hizo (spliting) ili kuepuka utaratibu wa kuitisha Zabuni.
5. Wataalamu wa Wizara wanatoa ushauri wao kiholela bila ya maandishi na kupelekea kukosekana vielelezo vya utoaji ushauri husika (kutokuwepo kumbukumbu za maandishi).
6. Kiwango cha fedha za Mradi huo (shilingi 132,946,020) kilitakiwa kutumika kwa utaratibu wa kutangazwa Zabuni.

Kwa mnasaba huo, Kamati haikuridhishwa na majibu ya hoja hii na kukubaliana na maelezo ya Mkaguzi. Hivyo, hoja hii inaendelea kubakia.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaushauri Uongozi wa Wizara mambo yafuatayo:-

1. Watendaji wa Wizara katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo wahakikishe wanafuata Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kutangaza zabuni kulingana na kiwango cha fedha kiliopo ili kujiepusha na dosari za ukaguzi.
2. Watendaji wa Wizara wahakikishe wanatoa ushauri kwa maandishi kwa ajili ya kupata kumbukumbu ya matumizi sahihi ya utaalamu wao.
3. Watendaji wa Wizara wafanye mapitio ya Mpango kazi wao wanapopata fedha kutoka nje ya bajeti yao.

## Hoja Nambari 6.6.1.2: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 58,427,624

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Aidha kifungu namba 23(2) kinafafanua kuwa zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Kilimo imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali kwa ununuzi wa udongo ambapo watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Uanunuzi, kwa mujibu wa Sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Kilimo kuhakikisha unaongeza juhudi katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kufanya ununuzi wa bidhaa kutoka kwa wafanyabiashara waliosajiliwa na Mamlaka husika. Mchanganuo wa manunuzi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 88: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati namba | Fedha iliyolipwa (Tshs) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 18/2<br>18/2/2022 | 11,697,672 | | |
| 19/2 | 13,925,800 | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18/2/2022 | | Mbarouk Sultan Mbarouk | Malipo ya fedha ya kazi ya kuleta udongo kwa kazi ya ujenzi wa tuta katika bonde la tovuni. |
| 24/2 21/2/2022 | 3,540,322 | | |
| 33/2 25/2/2022 | 1,412,230 | | |
| 10/3 7/3/2022 | 9,748,060 | Bin Salim Contractors and Materials Transporter CO | |
| 11/3 7/3/2022 | 4,177,740 | | |
| 16/3 10/3/2022 | 7,659,190 | | |
| 3/4 14/4/2022 | 6,266,610 | | |
| **Jumla** | **58,427,624** | | |

**Majibu ya Ungozi wa Wizara**

Napenda kuieleza Kamati yako kwamba watoa huduma wote waliolipwa walikuwa wamesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) kama ifuatavyo:

1. Said Suleiman Maktubu; REG. NO. G000396
2. Mbarouk Sultan Mbarouk; REG. NO. W000081
3. Haji Ali Makame; REG. NO. G000409
4. Ali Yahya Abdalla Building Material Supplier; REG.NO. G000395
5. Bin Salim Contractors and Materials Transporter CO; REG NO. ZPPDA/AC/0781/2021

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia na kuchunguza ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini mambo yafuatayo:-

1. Kuwepo kwa utofauti wa majina ya usajili wa watoa huduma baina ya Taasisi

za Usajili (Msajili wa Makampuni na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma). Kwa mfano, Kamati imebaini kuwa Mtoa Huduma; Ndugu Mbarouk Sultani Mbarouk kwenye cheti cha Usajli kinachotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma imeandikwa jina la 'Muba and Son Construction Servuce Ltd'. Wakati katika Usajili wa Makampuni anatambulika kwa jina la Mbarouk.

2. Mtoa Huduma Bin Salim Contractors and Materials Transporter amesajiliwa kihalali na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kwa majina yake na muda husika wa utoaji huduma. Hivyo, Kamati imejiridhisha na usajili wake na imemuondosha katika orodha ya watoa Huduma waliokuwa hawakusajiliwa kama inavyojionesha katika Kitabu cha Mdhibiti.
3. Kuhusiana na Watoa Huduma Said Suleiman Maktubu, Mbarouk Sultan Mbarouk, Haji Ali Makame na Ali Yahya Abdalla Building Material Supplier wamebainika hawakusajiliwa wakati Kamati inafanya uchunguzi wake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo wa Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa Wizara ya Kilimo - Pemba uhakikishe wanafanya kazi na Watoa Huduma ambao wamesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma katika wakati husika.
2. Taasisi za Serikali zihakikishe zinatumia jina halisi la Mtoa Huduma katika usajili wao ili kuepusha mgongano na kuwepo utambulisho wa jina moja tu katika matumizi yake hususan majina ya usajili kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na Msajili wa Makampuni.

## Hoja Nambari 6.6.1.3: Kutokuhaulishwa kwa fedha zenye thamani ya shilingi 14,245,355 na USD 3,279.9

Kwa mujibu wa Toleo nambari AD./184/01/07/80 la tarehe 9/6/2021 kutoka Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mujibu wa kipengele ''D'' kinaeleza kwamba "Bakaa ya fedha za Wizara/Idara/Mikoa na Taasisi za SMZ (Central Government) zilizokua zimepangiwa matumizi ya baadae (Commitment) zote ziingizwe katika hesabu Kuu ya Serikali iliyoko Benki Kuu nambari 9928161804 (C. Miscellaneous Deposit Account) na bakaa ambazo hazina Commitment zirejeshwe Mfuko Mkuu wa Hazina (Mfuko Mkuu wa hazina hesabu nambari 0404381000)".

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 14,245,355

na USD 3,279.9 ni bakaa ya fedha za Mradi ambazo hazikuhaulishwa na kupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali hesabu nambari 0404381000 ili kuendana na miongozo iliyotolewa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuongeza juhudi kusimamia utekelezaji wa mikataba ya miradi iliyopitishwa kwa lengo la kuwanufaisha wananchi kutokana na kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Napenda kuieleza Kamati yako kwamba fedha zote zilizoingizwa kwa ajili ya ujenzi wa tuta zilitumika kwa kazi husika. TZS. 14,245,355 ambazo zimeainishwa katika Ripoti ya CAG zilitumika kwa kutekeleza kazi ambazo awali hazikuwemo katika mpango. Hili lilifanyika baada ya kuomba ruhusa ya kuzitumia fedha hizo kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Raisi kwa barua ya tarehe 25/05/2022 yenye nambari za kumbukumbu WKUMM/P/ERCZP/5/27.VOL I/2022. Ruhusa ya kutumia fedha hizo ilitolewa kama barua yenye nambari za kumbukumbu SMZ/OMKR/B/17/VOL. I/03 inavyoonesha. Fedha hizi zilitumika kwa kufanya kazi za upandaji wa majani kwenye tuta, utiaji wa mtomo katika baadhi ya maeneo ya tuta, mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa tuta kwa Jumuiya ya Wakulima na Viongozi wa Shehia na ujenzi wa bango la Mradi.

Kuhusu USD 3,279.9 (TZS 7,525,758); fedha hizi hazikuwa sehemu ya bajeti ya ujenzi wa tuta; bali ni fedha za uchimbaji wa mtaro wa kutolea maji ya ziada mashambani na ujenzi wa ploti, kazi ambazo zilikuja kutekelezwa Machi na Aprili, 2023. Fedha ziliombwa kwa barua ya Katibu Mkuu ya tarehe 13/02/2023 na kuingizwa Wizara ya KUMM kama barua ya Afisa Mdhamini (WKUMM) ya tarehe 10/03/2023 inavyoonesha.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya kamati kupata kupoka majibu ya watendaji wa Wizara, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

1. Wizara ya Kilimo Pemba haikufua Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya 20216 inayoelekeza bakaa ya fedha zinazopitiwa na Mwaka wa fedha husika zinatakiwa kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina na badala yake ilitumika kwa kazi nyengine ambazo hazimo kwenye mpango kazi wa Wizara.
2. Wizara ya Kilimo - Pemba iliomba ruhusa ya matumizi ya fedha shilingi 14,247,355,000 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia barua yenye kumbukumbu nambari WKUMM/P/ERCZP/5/27.VOL/2022 ya tarehe

27/05/2022 ambapo miongozo hairuhusu kufanya hivyo na badala yake walitakiwa kuzirudisha katika hesabu ya Mfuko Mkuu (Hazina), Kamati haikuridhika na utaratibu uliotumika uliopelekea ukiukwaji wa taratibu zilibainishwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

3. Kuhusiana na fedha za USD 3,279.9 (7,525,758), Kamati imeridhishwa na majibu ya Wizara kwa vile imebaini kuwa fedha hizo ziliingizwa mwishoni wa mwaka wa fedha kwenye akaunti ya Wizara kama majibu yanavyojieleza, ila Mkaguzi alikagua taarifa ya utekelezaji na sio 'Cash book'. Hivyo, Kamati imeiondoa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo wa Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wizara ya Kilimo - Pemba uhakikishe unafuata Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya 20216 katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hususan katika kufuata taratibu za fedha zinazopitwa na mwaka wa fedha husika kwa kuomba ipasavyo idhini ya matumizi.

## Hoja Nambari 6.6.1.4: Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 48,520,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 48,520,000 zimetumika kwa ajili ya kuwalipa vibarua waliofanyakazi katika Mradi wa ujenzi wa Tuta la kuzuia maji chumvi la Tovuni Kiungoni lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliofanyika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuongeza juhudi katika kusimamia na kutekeleza matakwa ya Sheria kiukamilifu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

**Jadweli Nambari 89: Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Kiasi kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 13/2 ya 13/2/2022 | | 4,880,000 | |
| 5/2 ya 7/2/2022 | | 2,600,000 | |
| 30/2 ya 25/2/2022 | | 4,320,000 | |
| 16/2 ya 16/2/2022 | | 4,000,000 | |
| 32/3 ya 29/3/2022 | | 3,550,000 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 19/3 ya 15/3/2022 | Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Mali Asili na Mifugo | 3,360,000 | Malipo kwa ajili ya kuwalipa vibarua wanaofanyakazi sehemu ya ujenzi wa tuta bonde la tovuni |
| 9/3 ya 4/3/2022 | | 3,420,000 | |
| 1/4 ya 6/4/2022 | | 3,670,000 | |
| 2/4 ya 6/4/2022 | | 3,370,000 | |
| 3/5 ya 6/4/2022 | | 3,680,000 | |
| 32/3 ya 29/3/2022 | | 3,550,000 | |
| 22/3 ya 21/3/2022 | | 3,120,000 | |
| 1/6 ya 15/6/2022 | | 5,000,000 | |
| **Jumla** | | **48,520,000** | |

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Napenda kuieleza Kamati yako kwamba malipo ya fedha hizo zilizotajwa yanahusu malipo ya vibarua waliohusika katika ujenzi wa tuta katika Bonde la Tovuni Kiungoni. Vielelezo vya malipo hayo vipo na vimejumuisha barua za maombi, majibu ya barua za maombi, vocha za malipo, karatasi za mahudhurio ya kila siku kwa wiki zinazoonyesha jina la muhusika, Shehia anayotoka na nambari za simu, pamoja na mikataba ya vibarua hao.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa mikataba yote ilikuwepo kwa mujibu wa ‘Management letter’, Vibarua wote wamelipwa kwa mujibu wa taratibu ila wakati wa ukaguzi vielelezo vya malipo vilikuwa vingi na Mkaguzi alikagua baadhi ya Mikataba tu. Hata hivyo, Kamati ilikagua Mikataba na fomu za mahudhurio zinazoonesha siku walizohudhuria kufanya kazi, Kamati imeridhika na majibu na kuiondoa hoja hiyo.

Katika kutathmini msingi wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba haikuwa jukumu la watendaji wa Wizara ya Kilimo - Pemba kufuatilia mahudhurio ya vibarua wa Kampuni ya ujenzi wa Tuta hilo badala yake Mkaguzi alitakiwa kuhoji kuhusiana na utekelezaji wa Mradi husika kwa kupatiwa ripoti ya utekelezaji wake na sio mahudhurio ya vibarua kwani ni utaratibu wa ndani wa Kampuni.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo wa Kamati ya PAC

Watendaji wa Wizara wampatie mashirikiano ya karibu Mkaguzi hususan kwa kumueleza taarifa zinazohusiana na utekelezaji wa Mradi (Mahudhurio ya Vibarua) ili kuondokana na hoja zisizokuwa na mantiki.

## Hoja Nambari 6.6.1.5: kutokukatwa kwa kodi ya ongezeko la thamani shilingi 4,263,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasli na Mifugo Pemba imefanya malipo yenye jumla ya shilling 28,420,000 kwa ajili ya ununuzi wa udongo kwa ajili ya ujenzi wa tuta la kuzuia maji chumvi katika bonde la Tovuni bila ya kukatwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) 15% jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato yenye jumla ya shilingi 4,263,000 yanayotokana na kodi hiyo. Aidha, ni kwenda kinyume na sheria ya kodi ya Mapato kifungu cha 83(1)(c) na 84(1) vya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa mwaka 2019).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuongeza juhudi katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo kiukamilifu ikiwemo kukata na kuwasilisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kuiwasilisha katika mamlaka husika kwa lengo la kukuza mapato ya Serikali. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonesha katika jadweli lifuatalo:

**Jadweli Nambari 90: Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT)**

| Hati Namba | Fedha iliyolipwa | Kodi | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 10/3 ya 7/3/2022 | 9,947,000 | 1,492,050 | Bin Salim Contractors and Materials Transporter CO | Malipo kwa ajili ya kuleta udongo wa ujenzi wa tuta katika bonde la Tovuni. |
| 11/3 ya 7/3/2022 | 4,263,000 | 639,450 | | |
| 16/3 ya 10/3/2022 | 7,815,500 | 1,172,325 | | |
| 3/4 ya 14/4/2022 | 6,394,500 | 959,175 | | |
| **Jumla** | **28,420,000** | **4,263,000** | | |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Napenda kuijulisha Kamati yako kwamba Watoa Huduma wote ambao walitumika katika kazi hii walikatwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Kodi nyengine wanazostahili kukatwa. Mikato hiyo ya Kodi inaonekana wazi katika 'Cash Book' ambalo limekaguliwa na kivuli chake kimeambatanishwa: Mifano michache:

| Na. | Tarehe na Jina | Kiwango kilicholipwa | Kilicholipwa ZRA | Kilicholipwa TRA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 08/02/2022 Nd. Massoud Abrahman Massoud | TZS 3,523,100 | TZS 539,250 | TZS 71,900 |
| 2. | 18/02/2022 Nd. Mbarouk Sultan | TZS 13,925,800 | TZS 807,874 | TZS 791,716 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mbarouk | | | |
| 3. | 21/02/2022 Haji Ali Makame | TZS 9,748,060 | TZS 203,000 | TZS 198,9540 |
| 4. | 28/02/2022 Nd. Ali Yahya Abdulla | TZS 9,748,060 | TZS 203,000 | TZS 198,940 |
| 5. | 07/03/2023 Bin Salim Contractors and Materials Contractor Co. | TZS 9,748,060 | TZS 203,000 | TZS198,940 |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba Wizara haikuwa na kielelezo kinachothibitisha kufanyika kwa malipo yaliyoelezwa kwani baada ya kuangalia majibu ya Wizara yaliyotokana na 'Management letter' ilibaini kuwa Watoa huduma hao walikaptwa kimakosa kodi ya 'Stamp duty' ya asilimia 2% badala ya asilimia 15% ya VAT. Hivyo, kuna kodi ya asilimia 13% haijalipwa ambapo Kamati haikudhibitisha kufanyika malipo hayo. Kwa msingi huo, Kamati imeshindwa kujiridhisha malipo hayo kwa vile vielelezo havikupatikana na kupelekea hoja kuendelea kubakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo wa Kamati ya PAC**

1. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kodi ya Serikali iliyokuwa haijalipwa inalipwa ipasavyo.
2. Watendaji wa Serikali wawe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu za matumizi ya fedha za Serikali ili vinapohitajika viweze kupatikana (kupatiwa Mkaguzi).

## Hoja Nambari 6.6.1.6: Kukosekana kwa Mkataba wa Ujenzi wa Tuta

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeingia makubaliano na Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Mali Asili na Mifugo kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa Tuta la kuzuia maji chumvi katika bonde la Tovuni.

Dosari iliyobainika ni kukosekana kwa mkataba wa Ujenzi huo ili kuweza kujiridhisha juu ya mambo yaliyokubaliwa katika mkataba huo kwa lengo la kuweza kupima ufanisi na

tija itakayopatikana kulingana na makubaliano pamoja na fedha iliyotumika.

Kutokuwepo kwa mkataba kunapelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa utekelezaji wa mradi huo pamoja na malipo yaliyofanyika. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu nambari 28(1)(j) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Sheria ya mwaka 2016.

### Majibu ya Uongozi wa Wizara

Kweli hakukuwa na Mkataba wa ujenzi kati ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo. Aidha, kulikuwa na muongozo wa utekelezaji wa kazi hiyo ambao ni mchanganuo wa bajeti ya kazi yenyewe. Mchanganuo huu ndio uliotumika kuhakikisha kazi zilizoainishwa kwenye bajeti zinatekelezwa. Aidha, mikataba midogo midogo na watoa huduma binafsi ilifungwa ili kuhakikisha kazi hii inakamilika katika muda mfupi uliopangwa (Jan. 2022 - Machi, 2022).

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Wizara kukiri kwamba kulikuwa hakuna mkataba baina ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa hakuna ulazimu kwa Taasisi/Wizara za Serikali hususan katika fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kufunga Mkataba wa utekelezaji wake isipokuwa kunahitajika kupatikane vielelezo vinavyothibitisha uhaulishaji wa fedha za Mradi husika.

Kwa mantiki hiyo, Kamati imebaini hakutakiwa kuwepo kwa hoja hii katika Kitabu cha Mdhibiti na kwamba hoja hii imeondolewa.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo wa Kamati ya PAC

Uongozi wa Wizara ya Kilimo - Pemba ihakikishe inafuata taratibu zilizoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya 2016 hususan zinazohusiana na uhalishaji wa fedha kutoka Taasisi kwa Taasisi katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

# UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022

## 4.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## 4.1 UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA

## 4.1.3 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC)

### Taarifa ya Mapato

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika la Bandari Zanzibar limefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 43,444,877,222.55 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ukilinganishana makusanyo halisi ya shilingi 39,897,236,524.39 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la shilingi 3,547,640,698.16 ambalo ni sawa na asilimia 8.89 ya makusanyo halisi ya mwaka 2020/2021.

#### Majibu na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikupatiwa majibu kuhusiana na hoja ya taarifa ya Mapato ya Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(3) ya Kadumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020) kwamba majibu ya Kamati yawasilishwe kwa Kamati siku mbili kabla ya kikao husika. Hata hivyo, katika majadiliano ya hoja hii, Kamati imebaini yafuatayo:-

1. Shirika limefanikiwa kuvuka lengo la makusanyo ambapo ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 42,317,367,347.54 na kuweza kupata jumla ya shilingi Bilioni 43,444,877,222.55 sawa na asilimia 103 ya makusanyo. Ongezeko hilo limetokana na kuanzishwa na kutumika kwa mifumo ya makusanyo ya Shirika hilo ikijumuisha mfumo wa ‘Single Wondow Area’, ‘Account Basis’ na ZanMalipo. Pamoja na ongezeko hilo, hakuna ongezeko la tozo lililobadilishwa kutokana na huduma zinazotolewa na Shirika.
2. Shirika halina utaratibu mzuri wa uhifadhi wa kumbukumbu hususan katika eneo la uhifadhi wa Makontena (mizigo). Hili limebainika baada ya Kamati kutaka kujua

misamaha ya kodi iliyotolewa na Shirika na kuelezwa kwamba misamaha ya kodi inatolewa ila hakuna kumbukumbu ambazo zinahifadhiwa na Shirika.

3. Shirika linakabiliwa na changamoto ya kukaa muda mrefu wa makontena katika eneo la Bandari zaidi ya siku 21 (overstay) kama taratibu zinazvyoelekeza. Hali hiyo imetokana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kukosa eneo la kuhifadhia makontena hayo (whare house) na kupelekea wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili (Shirika na TRA).
4. Kamati pia imebaini kwamba Shirika linakabiliwa na changamoto ya madeni ya muda mrefu yanayotokana na ukodishwaji wa nyumba ya Shirika iliopo eneo la Shangani ambapo hadi Kamati inapokea majibu ya hoja hii, Mkodishwaji wa nyumba hiyo anadaiwa jumla ya shilingi milioni 66,960,000 ambapo Shirika limejaribu kuchukua hatua kadhaa kufuatilia deni ikiwemo kumuandikia barua za ukumbusho na ufanyaji wa vikao vya pamoja kuhusiana na ulipwaji wa deni hilo bila ya mafanikio yoyote. Hata hivyo, Kamati ilitaka kupatiwa nakala ya Mkataba wa ukodishwaji pamoja na barua za ukumbusho lakini hakuna kielelezo chochote kilichowasilishwa mbele ya Kamati.
5. Kuwepo kwa ukiukwaji wa taratibu za uhamishaji wa mali za Serikali kutoka Mamlaka moja kwenda nyengine. Kamati imegundua Shirika limepata maelekezo kwamba LCT Jitihada ihamishiwe Shirika la Meli Zanzibar. Hata hivyo, Shirika halikuweza kuiandikia barua Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kupata ithibati ya uhamishaji wa mali ya umma kwa vile Ofisi hiyo ndio pekee yenye mamlaka ya kutoa ruhusa ya uhamishwaji wa mali za Serikali.
6. Kukosa kwa mapato ya Shirika yanayotokana kuwepo kwa meli ya MV. Sepide katika eneo la Chelezo la Shirika. Kamati imegundua kwamba meli hiyo imewekwa Chelezoni kwa muda kutokana na kuwepo kwa kesi Mahakamani. Hali hiyo, hulipekelea Shirika kukosa mapato yanayotokana na matumizi ya Chelezo hicho ambapo ni aslimia 25 tu iliyoweza kukusanywa na Shirika kupitia chanzo hicho. Katika kufuatilia hoja hiyo, Kamati ilitaka kupatiwa vielelezo vya kuthibitisha maelezo yaliyotolewa na watendaji wa Shirika lakini hadi kamati inamaliza kikao hakuna kielelezo chochote kilchowasilishwa mbele ya Kamati.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Shirika lihakikishe linaweka vizuri kumbukumbu zake hususan zinazohusiana na misamaha ya kodi ili zitakapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati.

2. Uongozi wa Shirika uhakikishe unashirikiana ipasavyo na Serikali pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania kulitafutia ufumbuzi changamoto ya upatikanaji wa eneo la uwekaji wa Makontena nje ya Bandari ili kuwaepusha Wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili.
3. Shirika lifuate ipasavyo taratibu za uhamishaji wa mali ya umma kutoka katika umiliki wao kwenda Shirika la Meli ili kuepusha mkanganyiko wa kumbukumbu za uhifadhi wa mali za Shirika.
4. Shirika litafute ufumbuzi wa haraka kuhusiana na uwepo wa muda mrefu wa meli ya MV Sepide katika Chelezo ili sehemu hiyo iweze kutumika kwa shughuli nyengine muhimu.

## Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika la Bandari Zanzibar limefanikiwa kutumia jumla ya shilingi 26,493,189,236.82 ukilinganisha na matumizi halisi ya shilingi 26,946,333,554.87 ya mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na upungufu wa matumizi ya shilingi 453,144,318.05 sawana asilimia 1.68 ya matumizi halisi ya mwaka 2020/2021.

### Majibu na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikupatiwa majibu kuhusiana na hoja ya taarifa ya Matumizi ya Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(3) ya Kadumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020) kwamba majibu ya Kamati yawasilishwe kwa Kamati siku mbili kabla ya kikao husika. Hata hivyo, katika majadiliano ya hoja hii, Kamati imebaini yafuatayo:-

1. Shirika lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi Bilioni 32,245,948,236.06 na kupata jumla ya shilingi Bilioni 26,493,189,236.42 sawa na asilimia 96. Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba kati hizo, jumla ya shilingi Bilioni 8,832,316,485.59 ni matumizi yaliyotokana na kupungua kwa thamani kwa mali za Shirika (depreciation expenses) ambayo imefanyika kinyume na utaratibu kwa vile hawakufanya ‘physical depreciation’ badala yake walifanya mlinganisho wa thamani za mali zao.
2. Shirika linakabiliwa na madeni ya muda mrefu yasiyoweza kulipika jumla ya shilingi Bilioni 11,792,372,565.06.
3. Shirika kushindwa kutoa asilimia 50 ya gawio kwa Serikali. Kamati imebaini kwamba Shirika limepata faida ya Bilioni 11 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na

kutakiwa kuwasilisha gawio la Bilioni 5 katika Mfuko Mkuu wa Serikali (Hazina) lakini Shirika lilifanikiwa kuwasilisha Bilioni 2 tu. Hali hiyo imetokana na kubadilishwa kwa asilimia 20 ya gawio iliyopangwa awali hadi kufikia asilimia 50. Aidha, wakati mabadiliko hayo yanatokea, Shirika lilikuwa tayari limeshafanya uwekezaji kwa kununua vifaa vipya na vya kisasa vitakavyowahakikishia utoaji bora wa huduma kwa Wateja wao. Miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na 'wretch takers' 5 na Crine.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Shirika la Bandari Zanzibar lihakikishe linafuatilia kwa karibu madeni yote ya muda mrefu inayodai na ikithibitika hakuna uwezekano wa kulipika wafuate utaratibu wa kuyaondoa kwa mujibu wa Sheria Usimamizi wa Fedha za Umma, Nambari 12 ya mwaka 2016.
2. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inapopanga gawio kwa Mashirika ya Serikali ikae na wahusika kabla ya kupanga gawio hilo ili mgao husika uendane na uwezo wa makusanyo ya Shirika husika.

## Hoja nambari 4.1.3.1: Kukosekana kwa takwimu sahihi za kontena zinazoingia kutoka Nje ya Nchi

Kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya Ukaguzi (ISA) nambari 505 vinavyohusu matumizi ya ushahidi wa mkaguzi kutoka nje ya taasisi anayoikagua "external confirmation" kwa lengo la kupata ushahidi wa ukaguzi kwa mujibu wa viwango vya kimatafa vya ukaguzi ISA nambari 3301 na ISA nambari 500.2.

Viwango vya kimataifa vya ukaguzi nambari 500 vinaonyesha kuwa kuaminika kwa ushahidi wa ukaguzi kunaathiriwa na chanzo chake na asili yake, na ushahidi unatakiwa uwe huru kwa mujibu wamazingira ya upatikanaji wa ushahidi huo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa taarifa za takwimu za kontena zinazoingia kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu cha Shirika la Bandari ni 14,421 ambapo kwa mujibu wa takwimu kutoka Shirika la Meli idadi ya kontena zilizoingia ni 15,814 na hivyo kupelekea kuwepo kwa tofauti ya kontena 1,393 ambazo zinatiliwa shaka juu ya usahihi wa taarifa zinazoripotiwa na Shirika la Bandari, jambo ambalo linapelekea uwepo wa uvujaji wa mapato yatokanayo na uingiaji wa kontena.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhakikisha unaongeza umakini katika kusimamia mfumo kiukamilifu ili kuweza kupata taarifa sahihi za idadi ya

kontena zinazoingia nchini ambazo zitalingana na idadi za kontena zinazoripotiwa na Shirika la Meli Zanzibar. Mchanganuo wa tofauti ya idadi ya kontena zinazoingia nchini kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 01/01/2022 hadi tarehe 30/06/2022 baina ya Shirika la Bandari na Shirika la Meli ni kama inavyoonekana katikajadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 19: Tofauti ya takwimu za kontena zinazoingia kutoka nje ya nchi.**

| Tarehe | Ukubwa wa Kontena | Takwimu kutoka Shirika la Meli | Takwimu kutoka Shirika la Bandari | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| 01/01/22-31/03/2022 | 20 Futi | 4,761 | 4,377 | 384 |
| | 40 Futi | 2,686 | 2,278 | 408 |
| **Jumla ndogo** | | **7,447** | **6,655** | **792** |
| 01/04/22-30/06/2022 | 20 Futi | 5,549 | 5,070 | 479 |
| | 40 Futi | 2,818 | 2,696 | 122 |
| **Jumla ndogo** | | **8,367** | **7,766** | **601** |
| **Jumla kuu** | | **15,814** | **14,421** | **1,393** |

**Majibu ya Uongozi wa Shirika**

Utofauti ulionekana kutokana na takwimu za Makontena ulitokana na sababu zifuatavyo.

1. Shirika la Meli ambao ndio Wakala wa Meli zote za nje zinazoingia Zanzibar, hunakili makontena yote ambayo yanakuja kwenye meli husika kupitia katika mfumo wao, wakati Shirika la Bandari hurikodi kupitia *tally* zake makontena yanayoshushwa tu na kukatwa mzigo (striping), na inafahamika kuwa katika meli kunakuwa na makontena ambayo yatashushwa na baadae kupakiwa tena (short landed) na mengine yanakuwemo kwenye manisefti lakini hayashushi katika Bandari ya Zanzibar ( transit) hiyo ndio sababu zilizopelekea kuwa na utofauti wa takwimu baina ya Shirika la Bandari na Shirika la meli. Katika Bandari ya Malindi kuna taasisi tofauti ambazo zinachukua takwimu za makontena, na kila taasisi huchukua takwimu hizo kulingana na mahitaji yao, Utofauti na takwimu za makontena ni kulingana na aina ya taarifa kila taasisi wanazotunza.
2. Aidha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika la Bandari ililkuwa linatumia mfumo kidijital wa Tancis ambao unamilikiwa na Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA), wamiliki wa makontena hufanya malipo ya kodi ya Serikali (custom) na baadae kufanya malipo ya Ada za Shirika kupitia mfumo huo huo. Hivyo takwimu za Shirika mara zote hazitofautiani na Taarifa za Mamlaka ya Mapato (TRA). Hata

hivyo, Shirika liliona umuhimu wa kufanya Usuluhisho (reconciliation) wa idadi ya Makontena baina ya Shirika la Meli ikiwa kama ni taasisi inayofanya uwakala wa meli zote zinaingia Zanzibar na zile za Shirika.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika kufuatilia hoja hii imebaini uwepo wa sababu mbali mbali zilizopelekea utofauti wa utoaji wa Takwimu sahihi za uingiaji wa makontena kama ifuatayo:-

1. Kutokuwepo kwa utaratibu wa kufanya "Reconcilliation" katika taarifa za takwimu zinazohusiana na uingiaji wa makontena kwa meli zinazoingia katika Bandari ya Zanzibar kutoka nje ya nchi kwa Taasisi zinazohusika ikiwemo Shirika la Bandari na Shirika la Meli. Hali inayopelekea kuwepo kwa tofauti ya taarifa za uingiaji wa makontena nchini.
2. Kukosekana kwa matumizi ya mfumo wa pamoja katika Kituo cha "One Stop Center" kilichopo Bandarini. Hii pia inamepelekea kuwepo kwa utofauti wa takwimu sahihi za uingiaji wa makontena bandarini.

### Moani, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wakala wa Serikali Mtandao (e- Government) kuharakisha uungaji wa mfumo katika Kituo cha "One Stop Center" kilichopo Bandarini ili kuepusha utoaji wa takwimu zisizo sahihi na zisizoenda na Viwango vya Kimataifa (ISA).
2. Kamati inaushauri Uongozi wa Shirika la Bandari na Shirika la Meli kufanya kazi kwa mashirikianao pamoja na kuhakikisha wanasimamia ipasavyo matumizi ya mfumo katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na ingiaji wa makaontena nchini.

## Hoja nambari 4.1.3.2: Mkataba ulioingiwa bila ya kuridhiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikalishilingi 430,000,000

Kifungu nambari 27 (3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinasema kwamba "mikataba yote inayohusiana na bodi ya zabuni, baada ya kukubaliwa na bodi ya zabuni, ombi au mapendekezo yaliyotolewa chini ya Sheria hii, itaridhiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa na pande zote mbili". Aidha, Kanuni ya 47(1)(2) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2021

inaelezea kwamba makubaliano yoyote yanayohusiana na manunuzi ambayo thamani yake ni juu ya matumizi madogo kwa mujibu wa njia za manunuzi yatathibitishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa.

Ukaguzi ulipitia mchakato wa zabuni na kubaini kuwa Shirika la Bandari Zanzibar liliingia mkataba wenye kumbukumbu nambari SMZ/F.123/G/DP/2021-22/19 wa tarehe 11/06/2022 na thamani ya shilingi 430,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa Engine Liebherr.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kusainiwa kwa mkataba huo kabla ya kuthibitishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali jambo ambalo linaweza kupelekea Shirika la Bandari kuingia mikataba isiyo na tija au kuingia mkataba na wakandarasi wasiokuwa na vigezo na hatimae kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari kuhakikisha unaongeza umakini katika kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo mbali mbali inayotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuingia mikataba ambayo imeridhiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

### Majibu ya Uongozi wa Shirika

Ni kweli, Shirika katika mwaka wa fedha 2021/2022 lilitenga bajeti ya jumla ya Tshs.430,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa injini ya Mobile Habour Crane ya tani 64, na katika kutekeleza manunuzi hayo Shirika iliipa ununuzi wa injini hiyo zabuni nambari SMZ/F.123/G/DP/2021-22/19 kama inavyonekana katika Mpango wa Manunuzi wa Shirika.

Shirika lilinunua injini hiyo kutoka kwa kampuni ya Liebherr kwa jumla ya Dolla za Kimarekani 102,536.98 sawa na Tshs 240,961,903 kama inavyoonekana katika hati ya malipo namba 01/04 pamoja na mkataba. Mkataba wa Tshs.240,961,903 ni kweli haukuweza kupelekwa ulikuwa ni wa ununuzi wa mashine ya Kreni kubwa ya Shirika, kutokana na uharaka wa manunuzi hayo ili kuokoa hali tete ilikuwepo.

Kwa sasa Shirika limejipanga kuhakikisha kuwa mikataba yote inasajiliwa kwa mujibu wa matakwa ya kanuni ya fedha na pia kuhakikisha kuwa inapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata ushauri wa kisheria

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Uongozi wa Shirika la Bandari kukubaliana na hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati imebaini yafuatavyo katika utekelezaji wa hoja hii:-

1. Fedha iliyopangwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022 ya ununuzi wa Injini ya

Mobile Habour Crane ya Tani 64 ilikuwa ni jumla ya Shilingi 430,000,000. Ambapo kwa mujibu wa majibu ya Uongozi katika hoja hii Shirika lilifanya manunuzi ya Injini hiyo kwa Jumla ya Shilingi 240,961,903.00 isipokuwa majibu hayo yanakizana na majibu waliojibu katika "Management Letter" waliopatiwa wakati wa ukaguzi.

2. Kamati pia imebaini hakukuwa na udharura wa kufanya manunuzi bila ya kufuata taratibu zilizopo katika Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya Mwaka 2016 pamoja na Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2021 kwa kutoupelekea Mkataba Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama Vifungu vya Sheria na Kanuni vinavyoelekeza. Kwani, Kamati wakati wa majadiliano ya hoja hii imegundua Zabuni ilitangazwa yenye Nambari SMZ/F.123/G/DP/2021-2022/19 na Bodi ilikaa na kuidhinisha matumizi hayo.
3. Sambamba na hilo, pia Kamati imegundua kutokana na Majibu yao wakati wa majadiliano kwamba katika Mpango wa Manunuzi wa Shirika pia Ununuzi wa Injini ulitengewa jumla ya Shilingi 430,000,000. Vile vile, Kamati ilihitaji kupatiwa vielelezo vyote vinavyohusiana na Ununuzi huo hadi Kamati imemaliza kazi yake havikuwasilishwa.

**Moani, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati inaushauri Uongozi wa Shirika la Bandari kuhakikisha unasimamia ipasavyo matumizi ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbali mbali inayotolewa na Serikali katika manunuzi wanayofanya ili kuepusha upotevu wa fedha za Serikali.
2. Kamati inawashauri Afisa Mhasibu, Afisa Manunuzi pamoja na Afisa Sheria kutumia utaalamu wao pamoja na kufanya kazi kwa mashirikiano wakati wa ukaguzi ili kuondokana na hoja zisizo na msingi ukaguzi unapokamilika.

## Hoja nambari 4.1.3.3: Dosari zilizobainika katika zabuni ya mfumo wa kieletroniki wenye thamaniya Dola za Kimarekani 6,569,143.3

Ukaguzi ulipitia taarifa mbali mbali za Shirika la Bandari Zanzibar na kubaini kuwepo kwa Mkataba nambari SMZ/F123/CS/SSS/2020-21/04 wenye thamani ya Dola za Kimarekani 6,569,143.3 ulioingiwa baina ya Shirika la Bandari na Kampuni Fortris & Wartsila Voyage LTD kwa ajili ya utoaji wa huduma ya Ushauri elekezi wa mfumo wa kieletroniki wa Bandari "E-Port". Katika ukaguzi uliofanyika kupitia mkataba wa zabuni ya Mfumo wa Kieletroniki dosari mbali mbali za kiutendaji ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Mshauri elekezi kutumika kutengeneza mfumo bila ya ridhaa ya Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshajiwa Mali za Umma.
- Kutokupatiwa muhtasari wa kikao cha Bodi ya wakurugenzi kilichoojadili uamuzi wa kubadilisha Fortris na Wartsila Voyage Limited kutoka kuwa Mshauri elekezi hadi kuwa mtengenezaji wa mfumo.
- Kati ya modeli tano ndani ya Mfumo wa kielektroniki wa Bandari “e-Port modeli” moja tu ya usimamizi wa mafuta iliwasilishwa na kuanza kutumika ambayo si miongoni mwa kazi kuu za uendeshaji wa Bandari.
- Kutokuanishwa kwa kazi iliyofanywa katika mpango wa manunuzi wa mwaka wa Shirika kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
- Kukosekana kwa baadhi ya vielelezo muhimu vinavyohusiana na mkataba wa mfumo wakielektroniki wa Bandari.
- Kukosekana kwa barua inayobainisha utekelezaji wa maoni Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikalibaada ya kuwasilishwa kwa rasimu ya mkataba ili kuidhinishwa.
- Kukosekana kwa mshauri elekezi ambae atasimamia ubora wa kazi inayofanywa na mtengenezajiwa mfumo.

Kuwepo kwa dosari zilizobainishwa hapo juu kunapelekea kutia shaka juu ya thamani halisi ya fedhailiyotengwa katika utekelezaji wa mradi jambo ambalo ni kwenda kinyume na makubaliano kupitia mkataba uliobainishwa hapo juu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhakikisha unasimamia Sheria, Kanunina Miongozo iliyopo ikiwemo kusimamia makubaliano yaliyofikiwa katika mkataba kwa lengo la kupata thamani halisi ya fedha.

**Majibu ya Uongozi wa Shirika**

Shirika linakiri kuwa kulikuwa na dosari katika zabuni ya mfumo wa kielektronik, majibu na ufafanuzi wa dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kwa vile, Mamlaka ya Ununuzi hutowa Ridhaa mara moja juu ya mpango wa ununuzi wa mwaka husika, hivyo mpango huo uliridhiwa kutoka mamlaka ya ununuzi kwa Mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa barua yenye kumbukumbu nambari, BA.353/370/07/23 ya tarehe 09/09/2020
- Kuwa Bodi ya Wakurugenzi si muhimili kati ya mihimili ya kimanunuzi kwa mujibu wa Sheria ya manunuzi nambari 11 ya mwaka 2016. Hivyo, uamuzi wa kubadilisha upo kwa bodi ya zabuni.

- Kwa mujibu wa mahitaji ya mradi kulihitajika utayarishaji wa nyaraka na vifaa (Mobilization of resources) hata hivyo, moduli moja ya mfumo iliweza kukamilika kutokana na vifaa vya utengenezaji wa moduli hiyo vilipatikana mapema na ikaonekana vifanyiwe kazi mapema, kwa sasa module nyengine zimekamilika moduli hizo ni TOS - Terminal Operating System, ERP imo mwishoni kukamilika na moduli nyingine mbili zinaendelea kufanyiwa kazi.
- Mpango wa manunuzi wa kazi hii ulikuwemo katika mwaka wa fedha 2020/2021 na utekelezaji wake kufanyika mwaka 2021/2022.
- Kutopatikana baadhi ya taarifa alizohitaji kwa wakati kulitokana na wakati CAG alipozihitaji nyaraka hizo kulikuwa na ukaguzi unaendelea kutoka kwa Mamlaka ya Manunuzi Zanzibar.
- Shirika la Bandari lilipeleka barua kwa Mwanasheria kwa ajili ya marekebisho, ambapo yalifanyiwa kazi na mwisho watendaji walienda kuonana nao ana kwa ana ili kukamilisha marekebisho na mkataba kuidhinishwa.
- Kukosekana kwa mshauri elekezi ambae atasimamia ubora wa kazi inayofanywa na mtengenezaji wa mfumo ilitokana na Shirika lilikuwa linatumia e-port steering committee na E-port project Management team kwa ajili ya usimamizi wa mradi huo, hata hivyo kumeonekana umuhimu wa kumpata mshauri elekezi ili kushirikiana na kamati hizo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii imebaini yafuatavy:-

1. Kwa mujibu wa majibu ya Uongozi baadhi ya Vielelezo vilivyokuwa vikihusiana na hoja hii wakati wa ukaguzi vilikuwepo Mamlaka ya Ununuzi kwa ajili ya ukaguzi wakati mmoja kulifanyika ukaguzi mbili tofauti ndio sababu kuu iliyowasababishia Shirika kushindwa kuviwasilisha vielelezo hivyo kwa wakati. Isipokuwa baada ya kurudi kwa vielelezo hivyo Shirika ililchukua juhudi ya kuviwasilisha katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kujibiwa muda wa ukaguzi ushakamili hali iliyopelekea kukosekana kwa baadhi ya vielelezo katika hoja hii.
2. Kutokana na maelezo hayo, Kamati ya PAC ilihitaji kupatiwa vielelezo kwa ajili ya kujiridhisha na walichojibiwa hadi Kamati inamaliza kazi yake vielelezo hivyo havikuwasilishwa mbele ya Kamati ikiwemo Barua ya kuomba idhini ya kufungiwa Mfumo wa (e- Port System) kutoka Wakala wa Serikali Mtandao, "Concept Note" Mpango wa Manunuzi na kibali, Barua waliokabidhi vielelezo Mamlaka ya Ununuzi

na Uondoaji wa Mali za Umma, Barua ya Uteuzi wa Technical Team pamoja na Barua kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu utekelezaji wa Mkataba huu.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati inaishauri Shirika la Bandari katika utekelezaji wa majukumu yao Kusimamia vyema Sheria na Kanuni zilizopo katika makubaliano ya mkataba yanayofikiwa na Serikali kwa lengo la kutambua thamani halisi ya fedha.

## Hoja nambari 4.1.3.4: Kutokufanya kazi kwa Kitengo cha Uhakiki wa Ubora na Usimamizi waVihatarishi

Muundo wa Shirika la Bandari Zanzibar unabainisha kuwepo kwa Kitengo cha Uhakiki wa Ubora na Usimamizi wa Vihatarishi. Kitengo hiki kinashughulikia na kusimamia masuala ya udhibiti wa ubora wa huduma zinazotolewa na Shirika. Aidha, dhamira kuu ya Shirika la Bandari ni “kuongoza katika utoaji wa huduma bora katika Ukanda wa Afrika Mashariki”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Kitengo cha Uhakiki wa Ubora na Usimamizi wa Vihatarishi hakikuweza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa muundo jambo ambalo linapelekea kukosekana kwa ufanisi katika utoaji huduma bora bandarini, kushindwa kutatua changamoto za kuchelewa kupeleka mizigo bandarini pamoja na kuengezeka kwa foleni ya meli zinazosubiri kuhudumiwa kwa muda mrefu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari kuimarisha Kitengo cha Uhakiki wa Ubora na Usimamizi wa Vihatarishi ili kuimarisha ufanisi wa huduma zinazotolewa bandarini

### Majibu ya Uongozi wa Shirika

Ni kweli katika kipindi cha ukaguzi, Shirika halikuwa na Mkuu wa Kitengo cha Uhakiki wa Ubora na Usimamizi wa Vihatarishi kutokana na aliyekuwepo kupata uhamisho. Hata hivyo, Shirika limetekeleza mapendekezo yaliyotolewa na tayari Mkuu wa kitengo huyo amepatikana.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Pamoja na Uongozi wa Shirika kukubaliana na hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kamati inaushauri Uongozi wa Shirika pale nafasi ya utendaji inapokuwa wazi kufuata taratibu za kiutumishi kwa haraka sio mpaka aje mkaguzi baada ya kbaini ndio

uongozi unachukua hatua za kuomba mtendaji na kupelekea kuikosesha Serikali mapato na utoaji wa huduma bora za Bandari.

## SHIRIKA LA BANDARI - PEMBA

### Hoja nambari 4.1.3.5: Malipo ya fedha yenye vielelezo pungufu shilingi 26,138,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 26,138,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Bandari Pemba lakini baadhi ya vielelezo vya matumizi hayo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Hali hii inaweza kupelekea matumizi ya fedha za Umma yasiyoridhisha.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari kuongeza juhudi katika kusimamia Sheria zilizopo ikiwa ni pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ili kuepusha kujitokeza kwa matumizi yasiokuwa halali. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo.

**Jadweli Nambari 20: Malipo ya fedha yenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 21/7<br>13/7/2021 | | 340,000 | Shirika la Bandari Pemba | Malipo ya posho la safari kikazi |
| 9/7<br>16/7/2021 | 002641 | 1,500,000 | | Malipo ya posho la Ulinzi wa Askari wa JWTZ |
| 28/7<br>13/7/2021 | T/O | 1,600,000 | | Malipo ya posho la safari kikazi |
| 1/8 | 002656 | 1,500,000 | | Malipo ya posho la Ulinzi wa Askari waJWTZ |
| 10/9<br>13/9/2021 | 002679 | 1,500,000 | | Malipo ya posho la Ulinzi wa Askari waJWTZ |
| 2/10<br>4/10/2021 | | 1,020,000 | | Malipo ya posho la safari kikazi Unguja |

**Majibu ya Uongozi wa Shirika**

Mpaka kufika kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali vielelzo hivi vilikuwepo isipokua kulitokea changamoto ya uwekaji wa kumbukumbu za nyaraka, hii imetokana na kufariki kwa mshika fedha wa Shirika.

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/8 | 002656 | 1,500,000 | Shirika la Bandari Pemba | Malipo ya posho la Ulinzi wa Askari wa JWTZ |
| | | | | |
| 4a/8 | 002656 | 795,000 | | Malipo kwa ajili ya ujumbe |
| 6/8 | 002658 | 4,450,000 | | Malipo kwa ajili ya huduma ya chakula. |
| 31/8 | 002733<br>22/11/21 | 1,500,000 | | Malipo ya posho la Ulinzi wa Askari wa JWTZ |
| 6/11 | T.O | 565,000 | | Malipo kwa ajili ya safari kikazi |
| 34/12<br>21/12/2021 | 002769 | 1,350,000 | | Malipo ya posho la Ulinzi wa Askari wa JWTZ |
| 18/2 | 002827 | 570,000 | Masonry BuildingCotractors ltd | Malipo kwa ajili ya matengenezo yaCCTV |
| 40/2 | TO | 1,948,000 | Mkoani Hotel | Malipo kwa ajili ya mafunzo. |
| 41/2 | TO | 1,500,000 | Shirika la Bandari - Pemba | Malipo ya posho la Ulinzi wa Askari wa JWTZ |
| ¼ | 002871 | 1,500,000 | | |
| 2/4 | 002872 | 1,500,000 | | |
| 42/6 | 002945 | 1,500,000 | | |
| Jumla | | 26,138,000 | | |

Mchanganuo wa Matumizi ya Tshs.26,138,000 ni kama ifuatavyo:- Jumla ya Tshs.14,850,000 zilitumiwa na Shirika kama posho la Ulinzi kwa Askari wa JWTZ ambao wapo Bandarini kwa mujibu wa Mkataba wa tarehe 14 Januari 2019 kati ya Uongozi wa

Shirika la Bandari (ZPC) na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Kwa mujibu wa Mkataba huo Shirika la Bandari lilikubali kulipa jumla ya Tshs.150,000 kwa kila mwanajeshi ambae atafanya kazi za ulinzi katika Bandari za Zanzibar kwa mwezi, nyaraka za kusaini fedha hizo kwa maafisa wa JWTZ zipo kwa ajili ya uchunguzi na kwa sasa shirika hufanya malipo ya fedha zao moja kwa moja kupitia katika hesabu za Maafisa hao. Aidha, Tshs.1,925,000 zilitumika kwa ajili ya safari za kikazi kwa kwenda makao makuu Unguja. Pia, Tshs.9,363,000 zilitumika katika matumizi mengine na vielelezo vyake vimekamilika ambavyo 4 vimeshaambatanishwa katika hati za Malipo husika. Vielelezo vyote vipo kwa ajili ya uhakiki. Uongozi wa Shirika la Bandari umepokea ushauri wa CAG na utaufanyia kazi.

**Uchunguzi wa Kamati ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC baada ya kupata maelezo ya kina katika hoja hii imebaini fedha yote iliyotumika ilikuwa ni shilingi 58,999,859 kwa ajili ya kufanya malipo mbali mbali ya Shirika kwa Upande wa Pemba ambapo baadhi ya hati hizo za malipo ya shilingi 26,138,000 hadi ukaguzi unakamilika hazikuweza kupatikana vielelezo vyake vya matumizi. Kwa mnasaba huo, Kamati haijaridhika na utekelezaji wa majibu haya na hoja hii inabakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaushauri Uongozi wa Shirika la Bandari kuhakikisha inasimamia ipasavyo utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya Mwaka 2016 pamoja na Sheria nyengine pale inapofanya matumizi yoyote ya Serikali ili kuepusha kujitokeza kwa hoja zisizo na lazima.

Vile vile, Kamati inapendekeza kwa Wahasibu pamoja na Washika Fedha "Cashier" kuandaa utaratibu Mzuri wa uhifadhi na uwekaji wa kumbukumbu na nyaraka za Afisi kwa matumizi yote yanayofanyika na Shirika ili zinapohitaji ziweze kupatikana kwa ajili ya ukaguzi. Kwani Kamati imebaini kwamba baada ya kutopokea majibu ya hoja hii kuwa vielelezo hivyo ilivyokosekana wakati wa ukaguzi baadhi vilikuwepo Ofisi kuu ya Shirika Unguja.

## Hoja nambari 4.1.3.6: Malipo ya Mishahara kwa wafanyakazi wasiokuwa na mikataba shilingi 5,478,824

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 5,478,824 zimelipwa kwa wafanyakazi wanne (4) wa muda (daily pay) wa Shirika la Bandari tawi la Pemba bila ya kuwepo kwa mikataba ya kazi jambo ambalo linaweza kupelekea kutokuthibitika kwa malipo hayo. Aidha kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 135(1) ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari kuhakikisha kwamba unasimamia Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwa ni pamoja na kanuni ya Utumishi wa Umma katika upatikanaji wa mikataba ya ajira kwa wafanyakazi ili kuepusha kujitokeza kwa malipo yasiokuwa halali. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 21: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda ambao hawana**

mikataba

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 7/7 15/7/2021 | 002641 | 1,465,432 | | Malipo kwa ajili ya Vibarua wakutwa |
| 31/9 17/3/2021 | 002688 | 1,470,159 | Shirika la Bandari Pemba | Malipo kwa ajili ya mshahara naposho |
| 35/10 25/10/2021 | 002705 | 1,470,159 | | |
| 48/12 30/12/2021 | 002774 | 1,073,074 | | |
| **Jumla** | | **5,478,824** | | |

**Majibu ya Uongozi wa Shirika**

Ni kweli Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Shirika la Bandari linakiri kwamba mpaka kufika kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kulikua na wafanyakazi wakutwa ambao sio wa Mkataba na wala hawapokei mshahara bali wanapokea malipo ya kazi kwa kila siku kama ilivyo katika kanuni nambari 17(c) ya Kanuni za Utumishi za Shirika la Bandari ya mwaka 2012 ambayo imeitambua ajira ya kutwa kuwa ni miongoni mwa ajira zitakazotolewa na Shirika la Bandari.

Hivyo, Shirika la Bandari limekuwa na utaratibu wa kuwachukua vibarua kila inapobidi kutokana na kuongezeka kwa kazi au upungufu wa watendaji katika baadhi ya vitengo vyake. Malipo ya Tshs.5,478,874 ni malipo ya wafanyakazi wa kutwa (casual labour) ambao wapo katika Shirika kwa utaratibu wa ajira ya kutwa, Katika hali ya kawaida vibarua hawa huwa hawana Mkataba wowote na Shirika kwa vile malipo yao ni kwa kila siku wanayotumikishwa kwa mujibu wa masaa waliyoyafanyia kazi.

Pia, kutokana na upungufu mkubwa wa wafanyakazi ambao unalikabili tawi la Shirika hivi sasa baadhi ya vibarua hawa huwa wanafanya kazi kwa masaa mengi katika vituo tofauti jambo ambalo kwa mujibu wa jiografia ya Kisiwa chetu cha 5 Pemba haiwi rahisi kuwafikia na kuwalipa kwa kila siku waliotumika. Kwa misingi hii, Shirika hulazimika kuyakusanya malipo yao na kuwalipa kwa pamoja mwisho wa mwezi ama pale kazi waliyopewa inapokamilika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Mamlaka kukiri kuwepo kwa kasoro ya kutokuwepo kwa Mikataba ya kazi. Hata hivyo Kamati imebaini mambo yafuatayo:

1. Kanuni ya 17(c) ya Shirika inatofautiana na Kanuni ya 135(1) ya Kanuni ya Utumishi ya mwaka 2014. Hali hiyo imepelekea kuajiri wafanya kazi wa muda (vibarua) kinyume na utaratibu wa sheria kwa vile Kanuni Mama haikuzingatiwa ipasavyo.
2. Kutowapatia mikataba wafanyakazi kunaweza kupelekea kutotambulika kwa wafanyakazi husika na kuwakosesha haki zao wafanyakazi hao.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Shirika uhakikishe unafuata Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma katika kutekeleza masuala yao ya uajiri wa vibarua wa muda mfupi.

## ZIARA YA MAFUNZO YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KATIKA MAMLAKA YA BANDARI TANZANIA (TPA)

## UTANGULIZI:

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ilifanikiwa kufanya ziara ya siku moja katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) mnamo tarehe 10 Disemba, 2023. Ujumbe wetu ulipokelewa na watendaji wa Mamlaka hiyo wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Ndugu Plasduce Mkeli Mbossa.

## WASHIRIKI WA ZIARA

Ziara hiyo iliwashirikisha wafuatao:

1. Ujumbe wa Kamati ya PAC ukiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo; na
2. Watendaji kutoka Shirika la Bandari Zanzibar wakiongozwa na Mkurugenzi Mipango.

## LENGO LA ZIARA

Madhumuni ya ziara hiyo ni kuiwezesha Kamati kufahamu majukumu, utofauti uliopo

pamoja na utendaji wa Mamlaka ya Bandari Tanzania ili kuweza kuishauri ipasavyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusiana na utendaji wa Shirika la Bandari ili tija ipatikane kwa maslahi na maendeleo ya Zanzibar na Watu wake Wote.

Mkurugenzi Mkuu kiufupi aliieleza Kamati huduma wanazozitoa za kuwezesha uchumi wa Tanzania kukua ikiwemo upokeaji na utoaji wa mizigo kwa nchi za Zanzbia, Congo, Malawi na Ximbabwe. Aidha, Mamlaka inawapatia huduma takriban watu milioni mia Saba (7,000,000) kupitia mageti 14 ya Shehena za Makasha (Containers), Mafuta na Magari.

Mkurugenzi huyo alimazia kwa kueleza changamoto ambazo Mamlaka inakabiliana nazo ikiwemo:

1. Uchakavu wa miundombinu ya gati na vifaa vya kupakulia mizigo;
2. Ufinyu wa maeneo ya kuhudumia bandari; na
3. Miundombinu isiyotosheleza ya Reli na Barabara.

Mamlaka pia inayo mikakati ya muda mfupi na muda mrefu kuhusiana na utatuzi wa changamoto zinazowakabili ambazo ni:

1. Kuboresha utendaji wa gati nambari 1 hada nambari 7 kwa kuwapatia wawekezaji wa DP World kwa njia ya ukodishwaji wa kuzingatia masharti waliyokubaliana ikiwemo kuwatumia wafanyakazi waliowaajiri katika utekelezaji wa majukumu yao.
2. Kufanya utanuzi katika eneo la kuhifadhia matenki ya mafuta kwa vile eneo walilonalo ni dogo la kuchukua tani 300,000 jambao ambalo huwapelekea kukodi matenki ya watu binafsi na kuongeza gharama za ununuzi wa mafuta kwa wananchi.
3. Kufanya ujenzi wa gati mpya za nambari 13 hadi 15 ambazo zitasaidia katika utoaji wa huduma hususan kuhudumia shehena zinazoingia.
4. Kuandaa mpango wa ujenzi wa Kurasini Logistic Centre ambao kwa kiasi kikubwa utaongeza uhudumiaji wa Shehena za mizigo Bandarini hapo..

## MICHANGO YA WAJUMBE

Wajumbe walitaka kujua kuhusiana na mambo yafuatayo:

1. Jee kuna mikakati gani ya ziada ya uboreshaji huduma katika Mamlaka.
2. Suala la Mwekezaji DP World limefikia hatua gani.
3. Mashirikiano yaliyopo kbaina yao na Shirika la Bandari Zanzibar.

4. Jee Mamlaka inafuata 'tarrif' za Jumuiya za Kikanda.
5. Changamoto ziliopo za kibiashara na nchi nyengine za jirani.
6. Mipango waliyopanga katika kuboresha utoaji huduma za Bandari hazitoathiri uwekezaji wa 'DP World' atakapoanza kazi zake.
7. Hali ya usalama wa Sudan Kusini haitoyumbisha utendaji wa Bandari kutokana na kukubaliwa kwao kuwa ni Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kufuatia michango hiyo, Watendaji wa Mamlaka ya Bandari Tanzania walitoa ufafanuzi kama ifuatavyo:

Mikakati iliyopo katika utoaji huduma ni kwamba:

a) Mamlaka imeandaa mifumo tofauti ya 'ICT' ambao unawawezesha kurahisisha utendaji na kupunguza muda wa wafanyabiashara kusubiri huduma kwani 'container' kabla, wakati na baada ya kutoka linahudumiwa na mifumo.
b) Aidha, wameongeza motisha kwa wafanyakazi wao na kuwafanya watekeleze majukumu yao kwa masaa 24 bila ya kuwepo shida yoyote.
c) Pia, wanavifanyia matengenezo haraka vifaa vinavyoharibika pamoja na kununua vifaa vipya, kwa mfano wamenunua 'mobile crines' mbili kubwa ambapo kila moja imegharimu bilioni sitini.
d) Hata hivyo, Mamlaka inashirikiana ipasavyo na Mawakala wao kwa kufanya vikao vya kila mwezi na kutumia malori yao kutolea huduma za Bandari.
e) Mamlaka ina mpango wa kujenga matenki mapya 17 ya kuhifadhia mafuta wakati hivi sasa wanayo 12 pamoja na kuongeza mita 100 kwa ajili a ujenzi wa matenki mapya ya uhifadhi wa mafuta.

## HITIMISHO

Kikao hicho kilifungwa na Mwenyekiti saa 7:46 Mchana ambapo Mwenyekiti aliwashukuru wenyeji wetu (TPA) pamoja na Shirika la Bandari Zanzibar kwa kuwawezesha kutambua jinsi gani Taasisi mbili hizo zinavyotekeleza majukumu yao.

## 4.1.4 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)

### Taarifa ya Mapato

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika la Biashara la Taifa limefanikiwa

kukusanya jumla ya shilingi 154,496,959,260.25 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ukilinganisha na makusanyo halisi ya shilingi 11,249,249,577.94 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la shilingi 143,247,709,682.31 ambazo ni sawa na asilimia 92.72 ya makusanyo halisi ya mwaka 2020/2021.

### Majibu ya Uongozi wa Shirika

Mapato ya Shirika kwa kiwango kikubwa yanatokana na Mauzo ya Karafuu hivyo kupanda au kushuka kwa msimu wa Karafuu huchangia kupanda au kushuka kwa mapato ya Shirika. Mwaka 2021/2022 Shirika liliuza jumla ya tani 8,322 Kwa thamani 144.5 bilioni ukilinganisha na mwaka 2020/2021 ambapo mauzo yalikuwa ni tani 260.6 zenye Thamani ya TZS 2.99 bilioni.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haikupokea majibu ya hoja hii ya Taarifa ya Mapato kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(3) ya Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ambapo nyaraka na vielelezo vyote vinatakiwa viwasilishwe mbele ya Kamati siku mbili kabla ya majadiliano. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, ZSTC ilikadiria kuuza jumla ya tani 9,000 za Karafuu kama chanzo kikuu cha mapato na kufanikiwa kuuza jumla ya tani 8,322.

Licha ya ZSTC kuwa na mipango mzuri wa kuilinda “Brand” ya Karafuu ya Zanzibar ambayo imepata umaarufu mkubwa katika soko la kimataifa. Kadhalika, Kamati imebaini kwamba bado kuna wafanyabiashara wengine wanaitumia vibaya ‘ brand’ hiyo kinyume na taratibu ili kujipatia fedha kupitia jina la Karafuu ya Zanzibar.

Kutokana na changamoto ya kushuka kwa uzalishaji wa karafuu ya Zanzibar kunakochangiwa na sababu tofauti ikiwemo kuchakaa kwa mikarafuu yenyewe. Shirika linaandaa mpango wa kuinunua karafuu katika mashamba ya Tanga na Morogoro ambapo ZSTC itatafuta Mnunuzi kwa njia ya “advanced payment”, na karafuu hiyo itapitia “processing” zote kama zinazofanywa Karafuu za hapa Zanzibar. Hii itasaidia na kupunguza watu ambao wanatumia jina la ZSTC kuuza karafuu katika soko la kimataifa nje ya utaratibu pamoja na kuiwezesha ZSTC katika kufikia malengo yao ya Tani 9,000 za mauzo kutokana na “order” inazopokea.

Mbali na hayo, Kamati imebaini mambo mengine yafuatayo:

1. Kuwepo kwa duka la uuzaji wa bidhaa zitokanazo na karafuu liliopo Dar es Salaam ambalo linaendeshwa kihasara kwani gharama za uendeshaji ni kubwa

ukilinganisha na mapato yanayopatikana. Kamati imebaini kuwa duka hilo limo katika nyumba zinazomilikiwa na Shirika la Nyumba la Taifa la Tanzania Bara ambapo kwa mwezi linalipa zaidi ya shilingi milioni 2,000,000 kwa mwezi.

Hata hivyo, wameomba wapatie Ofisi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliyopo Kivukoni - Tanzania Bara ili waweze kuratibu shughuli za Mpango wa biashara watakaouanzisha wa ununuzi na uuzwaji wa Karafuu kutoka Morogoro na Tanga. Katika utekelezaji mpango huo, ZSTC haitozichanganya karafuu za Zanzibar na karafuu hizo.

2. Kwa upande wa kodi ya jengo la ZSTC liliopo Kinazini, kulitegemewa kupatikane shilingi milioni 600,000,000 hatimae wamepata shilingi milioni 468,000,000. Upungufu huo umetokana na kukatwa fedha za uendeshaji unaofanywa na Mawakala (developer) wa ukodishwaji huo ambao ni sawa na asiilimia 4. Aidha, Kamati imebaini kwamba baadhi ya mapato hayalipwi hususan kutoka kwa Taasisi za Serikali zilikodishwa katika jengo hilo.
3. 'Rest house' ziliopo katika kiwanda cha Makonyo Pemba zimechakaa na hivi sasa hazitumiki kibiashara. Hivyo zinaikosesha mapato Serikali lakini ZSTC ina mpango wa kuzifanyia ukarabati. Aidha, nyumba moja katika hizo amepewa Mwekezaji wa Kiwanda cha Makonyo ili aweze kuifanyia matengenezo na kuitumia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. ZSTC ihakikishe inaingia katika soko la ununuzi na uuzaji wa karafuu za Morogoro na Tanga bila ya kuathiri 'brand' ya karafuu ya Zanzibar kwani haifanani na karafuu nyengine ulimwenguni.
2. Kabla ya kuingia katika biashara za karafuu za Tanga na Morogoro, ZSTC ifanye utafiti wa hali ya juu kuhakikisha wanaingia katika biashara itakayowaletea faida na tija kwa Serikali.
3. ZSTC wahakikishe wanaandaa mpango mzuri utakaohakikisha wanapata Mawakala (Developer) watakaosimamia ipasavyo kodi za jengo lao la kinazini.
4. ZSTC ihakikishe inadhibiti ipasavyo 'brand' ya karafuu ya Zanzibar licha ya kiwanda cha Makonyo kupatiwa Muwekezaji.

## Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika la Biashara la Taifa limefanikiwa kutumia jumla ya shilingi 137,497,839,974.39 ukilinganisha na matumizi halisi ya shilingi

18,964,932,273.18 ya mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la matumizi ya shilingi 118,532,907,701.21 sawa na asilimia 86.21 ya matumizi halisi ya mwaka 2020/2021.

### Majibu ya Uongozi wa Shirika

Matumizi ya Shirika kwa mwaka 2021/2022 yanaonekana kupanda kwa asilimia 86.21 ukilinganisha na mwaka 2020/2021, hii inatokana na ongezeko la manunuzi ya Karafuu, ambapo kwa mwaka 2021/2022 jumla ya tani 8,738.15 Zilinunuliwa kutoka kwa Wakulima ukilinganisha na tani 213.05 kwa mwaka 2020/2021.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haikupokea majibu ya hoja hii ya Taarifa ya Matumizi kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(3) ya Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ambapo nyaraka na vielelezo vyote vinatakiwa viwasilishwe mbele ya Kamati siku mbili kabla ya majadiliano. Hata hivyo, kuwepo kwa tofauti kubwa ya matumizi baina ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 na 2021/2022. Kutokana hilo, Kamati ilitaka kujua kwa kiasi gani ZSTC iliathirika kutokana na kukosekana kwa bajeti yote waliyoikadiria kuipata na kuelezwa kwamba shughuli za uendeshaji za Shirika hilo zilikuwa hazifanyiki kwa ufanisi zaidi.

## Hoja nambari 4.1.4.1: Kuwepo kwa Usimamizi usioridhisha wa madeni ya Shirika

Kwa mujibu wa Kanuni nambari 23(1)(e) ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inawataka maafisa wanaohusika na ukusanyaji mapato kuchukua hatua stahiki, pale inapobidi ili kupata malipo yanayostahili.

Katika ukaguzi uliofanyika kuhusiana na uhakiki wa taarifa za wadaiwa wa Shirika la Biashara la Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilibainika kuwepo kwa ongezeko la deni kutoka shilingi 418,458,713.08 lililoripotiwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia jumla ya shilingi 1,296,796,776.93 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kupelekea kuwepo kwa ongezeko la shilingi 878,338,063.85 ambalo ni sawa na asilimia 67.7.

Kuwepo kwa Usimamizi usioridhisha wa madeni kunaweza kupelekea kuongezeka kwa madeni ya Shirika jambo ambalo linapelekea kuiongezea mzigo Serikali na hivyo kukwamisha shughuli za uendeshaji zilizopangwa kutokana na fedha nyingi kubakia mikononi mwa wakopeshwaji bila ya uwepo wa juhudi za kurejeshwa kwa fedha hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kuongeza juhudi katika

kusimamia, kufuatilia na kuboresha njia sahihi za ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mikopo iliyotolewa kwa wananchi.

### Majibu ya Uongozi wa Shirika

Ni kweli madeni kwa mwaka 2021/2022 yaliongezeka hadi kufikia 1.2 bilioni. Hii imetokana na kuongezeka kwa madeni kwa wateja wa Karafuu na mafuta ya mimea ambao ni jambo la kawaida kwao kutokana na namna Shirika linavyofanya biashara na wateja hao, kwani madeni yao huongezeka na kupungua kulingana na usafirishaji wa karafuu na Fedha za malipo zinavyopokelewa kutoka kwao.

Ikumbukwe kuwa Shirika huwa linafanya biashara na wateja hawa kwa uaminifu mkubwa sana kiasi ya kwamba kuna baadhi ya wakati wateja hutanguliza fedha za manunuzi ya karafuu kabla ya kupelekewa karafuu na hivyo kulidai Shirika.Hata hivyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 deni hilo limeshuka hadi kufikia shilingi 633,346,747.52.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya ZSTC kuchukua juhudi za kupunguza deni hilo ambalo inadai kutoka kwa wafanyabiashara tofauti, hata hivyo, Kamati imebaini bado juhudi zaidi zinahitajika kuchukuliwa kwani deni lililobakia bado ni kubwa. Hali hiyo haileti picha nzuri kiukaguzi na haiwezi kulifikisha Shirika na Serikali kwa ujumla katika muelekeo wa mafanikio.

Kamati haijaridhishwa kwani imebaini Shirika ndio kwanza lipo katika hatua ya kuyafanyia uhakiki madeni hayo. Hivyo, kuna haja kwa Shirika likawa na mikakati madhubuti ili kuweza kuokoa fedha hizo ambazo zipo katika mikono ya Wanaowadai.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati inaushauri uongozi wa Shirika kuandaa mpango wa ulipwaji madeni ili yaweze kukusanywa kwa wakati

Uongozi wa ZSTC uwachukulie hatua za kisheria wadaiwa wote hususan wadaiwa ambao washakuwa sugu ili kurudisha fedha za Serikali.

## Hoja nambari 4.1.4.2: Kukosekana kwa sera ya mikopo ya Shirika

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Biashara la Taifa limekua na utaratibu wa kutoa baadhi ya huduma zake kwa njia ya mkopo bila ya kuwepo kwa sera maalum ya mikopo iliyoandaliwa ambayo itaainisha vigezo vya kupatiwa mikopo jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa madeni na hatimae kulitia hasara Shirika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kuhakikisha unaongeza juhudi katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo mbali mbali iliyopo ikiwa ni pamoja na kuandaa sera ya mikopo itakayoainisha vigenzo vitakavyotumika katika kutoa mikopo hio.

**Majibu ya Uongozi wa Shirika**

Shirika limekuwa na utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa wafanyakazi wake ili kuwasaidia kukabiliana na matatizo mbali mbali yanayowakabili. Aidha, Shirika limeandaa Sera maalum kwa ajili ya kuweka utaratibu wa utoaji na usimamizi wa mikopo hiyo. Sera ambayo imeanza kutumika Julai, 2022.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ni kweli kulikuwa na kasoro hiyo. Hata hivyo, Kamati imeridhika na majibu ya hoja hii kwa vile tayari Shirika limeshakamilisha kuandaa Sera ya Mikopo na imeanza kufanya kazi tnagu Julai, 2022. Kamati imebahatika kuiona na kukubaliana nayo. Kwa msingi huo, hoja hii imeondolewa na Kamati.

## Hoja nambari 4.1.4.3: Kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa majengo

Kwa mujibu wa kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kuwa Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa baadhi ya Majengo ya Vituo vya ununuzi wa karafuu vinavyomilikiwa na Shirika la Biashara la Taifa Kisiwani Pemba lakini nyaraka zinazothibitisha umiliki wa majengo ya vituo hivyo zimekosekana kwa ukaguzi, hivyo kupelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha umiliki halali wa mali hizo.

Kukosekana kwa nyaraka kunaweza kupelekea kuwepo kwa uwezekano wa kujitokeza kwa migogoro ya ardhi baina ya Shirika na wananchi na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kama kilivyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kuhakikisha unasimamia na kufuatilia upatikanaji wa nyaraka za mali zake zikiwemo vituo vya ununuzi wa karafuu. Mchanganuo wa majengo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 22: Majengo ya vituo ambayo hayana nyaraka za umiliki

| Nam. | Jina la Kituo | Mahali Kilipo |
|---|---|---|
| 1. | Kituo Cha Kununua Karafuu Kisiwani | Kisiwani |
| 2. | Kituo Cha Kununua Karafuu Makongeni | Mtambwe |
| 3. | Kituo Cha Kununua Karafuu Chanjaani | Mtambwe |
| 4. | Kituo Cha Kununua Karafuu Pandani | Pandani |
| 5. | Kituo Cha Kununua Karafuu Chonga | Chonga |
| 6. | Kituo Cha Kununua Karafuu Mtambile | Mtambile |
| 7. | Kituo Cha Kununua Karafuu Chambani | Chambani |
| 8. | Ngomeni Kituo Cha Kununua Karafuu | Ngomeni |
| 9. | Kituo Cha Kununua Karafuu Ngwachani | Ngwachani |
| 10. | Kituo Cha Kununua Karafuu Mkanyageni | Mkanyageni |
| 11. | Kituo Cha Kununua Karafuu Mjimbini | Mjimbini |
| 12. | Kengeja Kituo Cha Kununua Karafuu | Kengeja |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| 13. | Kituo Cha Kununua Karafuu Wambaa | Wambaa |
| 14. | Kituo Cha Kununua Karafuu Kilindi | Kilindi |
| 15. | Kituo Cha Kununua Karafuu Junguni | Gando |

### Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika linakiri kuwepo kwa baadhi ya Majengo ya Vituo vya ununuzi wa Karafuu Pemba kutokuwa na nyaraka zinazothibisha umiliki wake. Shirika kwa kuhakikisha usalama katika umiliki wa Majengo yake liliomba kupatiwa Hati hizo kwa Mamlaka husika ambayo ni Kamisheni ya Ardhi Pemba.

Hata hivyo, kituo cha Ngwachani si mali ya Shirika, na ameshakabidhiwa mwenyewe kwa ajili ya matumizi yake. Aidha, kituo cha Kisiwani kimeshavunjwa kupisha ujenzi wa barabara na Shirika limenunua kiwanja chengine eneo la Ziwani kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba kuna juhudi kubwa ambayo Shirika imetumia na kufanikiwa kuhakikisha upatikanaji nyaraka za umiliki wa vituo vingi vya kununulia Karafuu. Kati ya vituo ambavyo Mkaguzi amevibainisha katika Ripoti yake, ni vituo vitatu tu vya Wambaa, Chambani pamoja na Chanjaani ndio vituo ambavyo bado havijapatikana nyaraka za umiliki. Kwa vile, kwa asilimia kubwa hoja hii imetekelezwa, Kamati imeridhika na majibu ya Shirika. Hata hivyo, imemtaka Mkaguzi kufanya ufuatiliaji wa hoja nyengine zilizosalia.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati inaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kuhakikisha wanafuatilia upatikanaji wa nyaraka za umiliki ya vituo vilivyosalia ili Shirika liwe na umiliki kamili ya vituo vyote vya kununulia Karafuu.

### Hoja nambari 4.1.4.4: Kutokukamilika kwa jengo la Kitega Uchumi la Madungu lenye thamani ya shilingi 6,923,355,649

Kwa mujibu wa kanuni nambari 58(1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 inaelezea kwamba "Muda wa mkataba unaoruhusiwa utakuwa ni kwa mujibu wa tathmini ya kweli ambayo itamuwezesha mzabuni kukamilisha uwasilishaji wa bidhaa, kukamilisha kazi au kutoa huduma, kwa kuzingatia tarehe inayotarajiwa ya kukamilika na eneo".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Biashara la Taifa liliingia mkataba nambari SMZ/FO121/W/ICB/2018/2019 wa tarehe 15 Julai, 2019 na Mkandarasi Salem Construction Limited kwa thamani ya shilingi 6,923,355,643 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi la Madungu ambapo kwa mujibu wa mkataba huo jengo hilo lilipaswa kukamilika tarehe 15 Julai 2022.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo kwa wakati uliopangwa kulingana na mkataba jambo ambalo linaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama za mradi kunakotokana na kupanda kwa bei za bidhaa za ujenzi na hatimae kupelekea kuingia mkataba wa nyongeza (Addendum) ambapo ni kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuhakikisha unasimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya ujenzi ili iweze kutekelezwa kwa mujibu wa mkataba ulioingiwa na kuepusha uwezekano wa kuitia hasara Serikali.

#### Majibu ya Uongozi wa Shirika

Kuchelewa kukamilika kwa Jengo la Madungu kunatokana na ukosefu wa Fedha (2019/2020) pamoja na Janga la COVID19. Hali hii imepelekea kutopatikana kwa fedha za kumlipa Mkandarasi kwa wakati na kufanya mradi kusimama kwa muda miezi 14.

Kwasasa mradi huu wa Ujenzi wa Jengo la ZSTC Madungu umekamilika na umefunguliwa Rasmi na Rais wa Jamhuri ya Tanzania Mh. Dr. Samia Suluhu Hassani.

#### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na kwamba Mkaguzi alibaini kutokukamilika kwa jengo la Kitega Uchumi la Madungu lenye thamani ya shilingi 6,923,355,649. Hata hivyo, hivi sasa jengo hilo limeshakukamilika na kuzinduliwa. Kwa msingi huo, hoja hii imeshatekelezwa na Kamati imeiondoa.

### Hoja nambari 4.1.4.5: Mapato yaliyokosekana kutokana na kutokufanyakazi ipasavyo kwa mashine ya kuzalishia mafuta shilingi 3,715,987,500

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kiwanda cha Makonyo kilichopo Wawi Pemba kinafanya uzalishaji wake kupitia mashine (mtambo) ambayo ina njia mbili za uzalishaji.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutumika kwa njia moja ya mashine katika uzalishaji kwa muda mrefu kutokana na njia nyengine kutokufanyakazi kulikotokana na kuharibika kwa kipindi kirefu bila ya kufanyiwa matengenezo jambo ambalo limepelekea kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika la Biashara la Taifa kushindwa kukusanya jumla ya shilingi 3,715,987,500. Aidha, kunaweza kupelekea njia ambayo inatumika kwa sasa kutumika kwa ziada kunakoweza kupelekea kuharibika na hatimae kukosekana kwa mapato yanayokusanywa kupitia uzalishaji wa mafuta unaofanywa na mashine hiyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuhakikisha unatenga fedha za kutosha katika bajeti yao ya mwaka ili kuweza kuifanyia matengenezo mashine hiyo na kuweza kuipatia mapato Serikali. Mchanganuo wa mapato yanayokosekana ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 23: Mapato yanayokosekana kutokana na mashine kutokufanya kazi ipasavyo**

| Jina | Faida kwa kilo 1 (A) | Wastani wa uzalishaji kwa siku (Kg)(B) | Faida kwa siku (Tshs) AXB = C) | Faida kwa mwaka kwa mashine (Tshs) (CX261 = D) | Mapato yaliyokosekana (Tshs) (DX5) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Shina la Karafuu** | **33,500** | **85** | **2,847,500** | **743,197,500** | **3,715,987,500** |
| Jumla | | | | | 3,715,987,500 |

**Majibu ya Uongozi wa Shirika**

Kiwanda cha Makonyo kilichopo Wawi Pemba kinafanya uzalishaji wake kupitia mashine (mtambo) ambayo ina njia mbili za uzalishaji, kutokana na kuharibika kwa njia moja kulipelekea Kiwanda kutumia njia moja ya Uzalishaji tu ambayo imesababisha kupungua kwa uzalishji hatimae kupungua kwa Mapato ya Kiwanda. Shirika limeamua kukikodisha

Kiwanda hicho kwa Kampuni ya SPICE ISLAND AROMATICS.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kiwanda hicho kimekodishwa kwa Kampuni ya Spice Island Aromatics kwa muda wa miaka ………. Ili kiweze kufanyiwa matengenezo na kujikata mapato gharama na faida yake kwa mujibu wa muda uliokubaliwa. Kamati imebaini kwamba maamuzi hayo ni ya msingi kwa vile kutokana na uchakavu unaokibili, uzalishaji wake unapungua kila baada ya muda. Kwa msingi huo, Kamati imeridhika na juhudi hizo na kuiondosha Kamati hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Shirika uhakikishe unafuatilia kwa karibu masharti yote yaliyoelezwa katika Mkataba ili Serikali iweze kupata tija kutokana na ukodishwaji huo.

## Hoja nambari 4.1.4.6: Kutokufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Biashara la Taifa liliweka makadirio ya ukusanyaji wa mapato ya shilingi 4,560,135,000 yatokanayo na mauzo ya makonyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 makusanyo halisi ya mauzo ya makonyo ni shilingi 126,139,000 sawa na asilimia 2.8 ya makadirio na kupelekea kuwepo kwa tofauti ya shilingi 4,433,996,000 sawa na asilimia 97.2 ya makadirio jambo ambalo linaonyesha kwamba Shirika la Biashara la Taifa kupitia Kiwanda cha Makonyo limeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji mapato iliyojiwekea.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kuhakikisha kwamba maandalizi ya Bajeti yanakuwa na uhalisia, kutafuta njia bora za kuweza kusimamia mauzo ya makonyo pamoja na kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

**Majibu ya Uongozi wa Shirika**

Shirika katika mwaka wa Fedha 2021/2022 lilikadiriwa kukusanya jumla ta Tzs 4,560,135,000.00 yatokanayo na mauzo ya Mafuta. Hadi kumalizika Mwaka Shirika lilikusanya Shilingi 126,139,000.00 zilizotokana na mauzo ya mafuta. Hii inatokana na Kiwanda kushindwa kufanya kazi yake ipasavyo kulikosababishwa na ubovu wa mashine ya kuzalishia mafuta.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kwamba kutofikia malengo ya Shirika hili kulitokana na mashine za kuzalishia mafuta kushindwa kufanya kazi ipasavyo. Kwa msingi huo, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ni kama yalivyoainishwa katika hoja nambari 4.1.4.5 inayohusiana na mapato yaliyokosekana kutokana na kutokufanyakazi ipasavyo kwa mashine ya kuzalishia mafuta. Kwa vile hatua za ukodishwaji wa kiwanda hicho ikijumuisha na mashine zake zimeshafanyika, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

## Hoja nambari 4.1.4.7: Tofauti iliobainika baina ya Karafuu zilizonunuliwa na kusafirishwa kutoka Pemba kwenda Unguja shilingi 276,621,000

Ukaguzi uliofanyika kwa ZSTC ulibaini utofauti mkubwa baina ya karafuu zilizonunuliwa kutoka Pemba na kusafirishwa kwenda Unguja, na idadi halisi ya Karafuu zilizopokelewa Unguja. Ukaguzi ulibaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya kilo za karafuu 8,445,578 zilisafirishwa kutoka Pemba na jumla ya kilo 8,421,524 zilipokelewa Unguja hali iliyopelekea utofauti wa kilo 24,054 za karafuu ambazo thamani yake ni sawa na shilingi 276,621,000. Tofauti iliyobainika inaweza kupelekea kupungua kwa faida.

Mchanganuo wa Karafuu zilizonunuliwa na kusafirishwa kutoka Pemba kwenda Unguja ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSTC kutafuta na kuwashirikisha wataalamu wa masuala ya karafuu katika mchakato mzima kuanzia hatua ya awali ya usafirishaji, uzani na mapokezi ya karafuu ili kuweza kutatua changamoto hizi zilizobainika.

**Jadweli Nambari 24: Tofauti kati ya karafuu iliyosafirishwa kutoka Pemba hadi Unguja**

| PEMBA | | | UNGUJA | | | | TSHS | TSHS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Gunia** | **Kgs** | **Tarehe** | **Gunia** | **Kgs** | **Tofauti (Kgs)** | Wastani wa bei kwa kilo | Jumla |
| 30/07/2021 | 1,500 | 67,076.00 | 01/08/2021 | 1,500 | 66,449.00 | 627 | 11,500 | 7,210,500.00 |
| 08/01/2021 | 8,000 | 359,149.00 | 08/04/2021 | 8,000 | 357,325.00 | 1,824.00 | 11,500 | 20,976,000.00 |
| 08/07/2021 | 3,000 | 134,761.00 | 08/08/2021 | 3,000 | 134,387.00 | 374 | 11,500 | 4,301,000.00 |
| 08/08/2021 | 5,600 | 251,475.00 | 08/10/2021 | 5,600 | 250,909.00 | 566 | 11,500 | 6,509,000.00 |
| 13/08/2021 | 6,000 | 269,110.00 | 15/08/2021 | 6,000 | 268,558.00 | 552 | 11,500 | 6,348,000.00 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 15/08/2021 | 6,600 | 296,511.00 | 17/08/2021 | 6,600 | 295,749.00 | 762 | 11,500 | 8,763,000.00 |
| 17/08/2021 | 3,000 | 134,560.00 | 19/08/2021 | 3,000 | 134,203.00 | 357 | 11,500 | 4,105,500.00 |
| 19/08/2021 | 6,000 | 268,763.00 | 22/08/2021 | 6,000 | 268,423.00 | 340 | 11,500 | 3,910,000.00 |
| 22/08/2021 | 6,000 | 269,060.00 | 24/08/2021 | 6,000 | 267,617.00 | 1,443.00 | 11,500 | 16,594,500.00 |
| 24/08/2021 | 3,000 | 134,528.00 | 26/08/2021 | 3,000 | 134,121.00 | 407 | 11,500 | 4,680,500.00 |
| 27/08/2021 | 6,000 | 268,670.00 | 29/08/2021 | 6,000 | 268,321.00 | 349 | 11,500 | 4,013,500.00 |
| 29/08/2021 | 6,600 | 296,098.00 | 31/08/2021 | 6,600 | 294,479.00 | 1,619.00 | 11,500 | 18,618,500.00 |
| 09/03/2021 | 7,000 | 313,113.00 | 09/05/2021 | 7,000 | 312,650.00 | 463 | 11,500 | 5,324,500.00 |
| 09/05/2021 | 7,000 | 313,937.00 | 09/07/2021 | 7,000 | 312,178.00 | 1,759.00 | 11,500 | 20,228,500.00 |
| 09/07/2021 | 5,000 | 223,897.00 | 09/09/2021 | 5,000 | 223,470.00 | 427 | 11,500 | 4,910,500.00 |
| 09/10/2021 | 7,000 | 313,051.00 | 09/12/2021 | 7,000 | 312,696.00 | 355 | 11,500 | 4,082,500.00 |
| 09/12/2021 | 7,000 | 314,005.00 | 14/09/2021 | 7,000 | 312,329.00 | 1,676.00 | 11,500 | 19,274,000.00 |
| 14/09/2021 | 3,000 | 134,290.00 | 16/09/2021 | 3,000 | 134,150.00 | 140 | 11,500 | 1,610,000.00 |
| 16/09/2021 | 5,000 | 223,856.00 | 19/09/2021 | 5,000 | 223,589.00 | 267 | 11,500 | 3,070,500.00 |
| 19/09/2021 | 6,000 | 268,965.00 | 21/09/2021 | 6,000 | 267,472.00 | 1,493.00 | 11,500 | 17,169,500.00 |
| 21/09/2021 | 2,800 | 125,333.00 | 23/09/2021 | 2,800 | 124,978.00 | 355 | 11,500 | 4,082,500.00 |
| 24/09/2021 | 6,000 | 268,209.00 | 26/09/2021 | 6,000 | 267,933.00 | 276 | 11,500 | 3,174,000.00 |
| 26/09/2021 | 5,994 | 268,933.00 | 28/09/2021 | 5,994 | 267,543.00 | 1,390.00 | 11,500 | 15,985,000.00 |
| 28/09/2021 | 3,000 | 134,363.00 | 30/09/2021 | 3,000 | 134,192.00 | 171 | 11,500 | 1,966,500.00 |
| 10/01/2021 | 1,800 | 80,561.00 | 10/03/2021 | 1,800 | 80,411.00 | 150 | 11,500 | 1,725,000.00 |
| 10/03/2021 | 3,000 | 134,648.00 | 10/05/2021 | 3,000 | 133,994.00 | 654 | 11,500 | 7,521,000.00 |
| 10/08/2021 | 3,000 | 134,295.00 | 10/10/2021 | 3,000 | 134,081.00 | 214 | 11,500 | 2,461,000.00 |
| 10/10/2021 | 3,000 | 134,578.00 | 10/12/2021 | 3,000 | 133,956.00 | 622 | 11,500 | 7,153,000.00 |
| 15/10/2021 | 3,500 | 156,867.00 | 17/10/2021 | 3,500 | 156,369.00 | 498 | 11,500 | 5,727,000.00 |
| 17/10/2021 | 2,600 | 116,729.00 | 19/10/2021 | 2,600 | 116,194.00 | 535 | 11,500 | 6,152,500.00 |
| 22/10/2021 | 3,000 | 134,167.00 | 24/10/2021 | 3,000 | 133,786.00 | 381 | 11,500 | 4,381,500.00 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 24/10/2021 | 2,000 | 89,756.00 | 26/10/2021 | 2,000 | 89,433.00 | 323 | 11,500 | 3,714,500.00 |
| 29/10/2021 | 3,000 | 134,103.00 | 31/10/2021 | 3,000 | 134,023.00 | 80 | 11,500 | 920,000.00 |
| 31/10/2021 | 1,800 | 80,852.00 | 11/02/2021 | 1,800 | 80,682.00 | 170 | 11,500 | 1,955,000.00 |
| 11/05/2021 | 3,000 | 133,913.00 | 11/07/2021 | 3,000 | 133,887.00 | 26 | 11,500 | 299,000.00 |
| 11/07/2021 | 1,240 | 55,685.00 | 11/09/2021 | 1,240 | 55,552.00 | 133 | 11,500 | 1,529,500.00 |
| 13/11/2021 | 2,600 | 116,223.00 | 14/11/2021 | 2,600 | 116,193.00 | 30 | 11,500 | 345,000.00 |
| 16/11/2021 | 800 | 35,927.00 | 16/11/2021 | 800 | 35,873.00 | 54 | 11,500 | 621,000.00 |
| 21/11/2021 | 1,800 | 80,554.00 | 20/11/2021 | 1,800 | 80,405.00 | 149 | 11,500 | 1,713,500.00 |
| 28/11/2021 | 1,800 | 80,596.00 | 28/11/2021 | 1,800 | 80,443.00 | 153 | 11,500 | 1,759,500.00 |
| 12/04/2022 | 1,000 | 44,822.00 | 12/04/2021 | 1,000 | 44,658.00 | 164 | 11,500 | 1,886,000.00 |
| 01/06/2022 | 2,000 | 89,008.00 | 01/06/2022 | 2,000 | 88,771.00 | 237 | 11,500 | 2,725,500.00 |
| 01/09/2022 | 3,600 | 160,188.00 | 01/09/2022 | 3,600 | 159,540.00 | 648 | 11,500 | 7,452,000.00 |
| 01/01/2022 | 1,600 | 71,659.00 | 01/11/2022 | 1,600 | 71,517.00 | 142 | 11,500 | 1,633,000.00 |
| 13/01/2022 | 2,000 | 88,934.00 | 13/01/2022 | 2,000 | 88,833.00 | 101 | 11,500 | 1,161,500.00 |
| 16/01/2022 | 2,600 | 115,660.00 | 16/01/2022 | 2,600 | 115,552.00 | 108 | 11,500 | 1,242,000.00 |
| 19/01/2022 | 42 | 840 | 19/01/2022 | 42 | 840 | ORG | 11,500 | #VALUE! |
| 23/01/2022 | 3,200 | 142,834.00 | 23/01/2022 | 3,200 | 142,717.00 | 117 | 11,500 | 1,345,500.00 |
| 23/01/2022 | 458 | 9,160.00 | 23/01/2022 | 458 | 9,160.00 | ORG | 11,500 | #VALUE! |
| 28/01/2022 | 2,000 | 89,261.00 | 28/01/2022 | 2,000 | 89,221.00 | 40 | 11,500 | 460,000.00 |
| 02/04/2022 | 2,000 | 89,405.00 | 02/06/2022 | 2,000 | 89,236.00 | 169 | 11,500 | 1,943,500.00 |
| 02/11/2022 | 2,000 | 89,077.00 | 02/12/2022 | 2,000 | 88,969.00 | 108 | 11,500 | 1,242,000.00 |
| 25/02/2022 | 1,200 | 53,606.00 | 27/02/2022 | 1,200 | 53,591.00 | 15 | 11,500 | 172,500.00 |
| 03/04/2022 | 581 | 25,877.00 | 03/05/2022 | 581 | 25,868.00 | 9 | 11,500 | 103,500.00 |
| 29/03/2022 | 540 | 24,080.00 | 31/03/2022 | 540 | 24,048.00 | 32 | 11,500 | 368,000.00 |
| **Jumla** | **188,855** | **8,445,578** | | **188,855** | **8,421,524** | **24,054** | | **276,621,000** |

### Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika katika shughuli zake za ununuzi na usafirishaji wa Karafuu limekuwa likisafirisha karafuu kutoka Pemba kuja Unguja. Ni kweli kumekuwa na utofauti wa karafuu baina ya karafuu zilizonunuliwa kutoka Pemba na kusafirishwa kwenda Unguja, na idadi halisi ya Karafuu zilizopokelewa Unguja kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya kilo za karafuu 8,445,578 zilisafirishwa kutoka Pemba na jumla ya kilo 8,421,524 zilipokelewa Unguja hali iliyopelekea utofauti wa kilo 24,054 za karafuu ambazo thamani yake ni sawa na shilingi 276,621,000.

Katika kutatua tatizo hili Shirika limechukua hatua mbali mbali kama vile kuwashirikisha Maafisa kutoka ZAECA, Maafisa kutoka Mamlaka ya vipimo wakati wa zoezi zima la usafirishaji wa Karafuu. Aidha Shirika limeamua kubadilisha mizani na kuweka mizani mpya ambazo pia zitawekwa eneo moja bila yakuhamishwa hamishwa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba kuna tafiti za kitaalamu zimefanywa na kugundua kuwa katika usafirishaji wa karafuu kutoka sehemu moja kwenda nyengine huwa unajitokeza kupungua kwa uzito wa karafuu hizo kunakosababishwa zaidi na kusinyaa kwa asilimia 0.002 kwa kila kilo moja. Aidha, karafuu pia huwa zinadondoka na kupoteza ule uhalisia wake wa awali.

Kutokana kuwepo kwa sababu hizo za kitaalamu zilizobainishwa na uongozi wa Wizara, Kamati ilitaka kujua kwamba Mkaguzi alipopita hakuelezwa sababu hizo na kuelezwa kwamba alielezwa na kushangaa kuiona hoja hiyo imebakia kitabuni. Hali hiyo inaonesha kwamba kulikosekana mashirikiano ya karibu baina ya pande mbili hizo. Hata hivyo, Kamati imekubaliana na majibu yao na kuiondoa hoja hii.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Shirika uwe karibu na Wakaguzi wanapokuja kutekeleza majukumu yao katika Afisi zao ili kuepusha hoja zenye majibu kujitokeza katika Ripoti ya Mkaguzi.

## Hoja nambari 4.1.4.8: Kukosekana kwa ufanisi wa kiutendaji wa Tawi la ZSTC Dar es Salaam

Ukaguzi wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022 ulifanya tathmini ya kupima ufanisi wa kiutendaji wa Shirika, kwa kuzingatia uwiano wa gharama zinazotumika katika shughuli za uendeshaji wa Shirika na kiasi halisi kinachozalishwa.

Tathmini iliofanyika kwa Tawi la ZSTC Dar es Salaam ilibaini kwamba, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Tawi la ZSTC Dar es salaam liliendeshwa kwa hasara ukilinganisha gharama halisi zilizotumika kwa ajili ya uendeshaji wa tawi na mapato yaliopatikana.

Kukosekana kwa ufanisi katika utendaji wa Tawi kunaweza kuliongezea Shirika gharama kubwa na hata kulisababishia Shirika hasara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSTC kufanya maboresho ya namna ya kujiendesha kwa faida ili kuepuka kuisababishia mzigo wa hasara Serikali kutokana na uwepo wa tawi lisilo na faida vyenginevyo ni vyema kufanya maamuzi yatakayoileletea faida Shirika kwa mujibu wa malengo ya uanzishwaji wa Shirika hilo. Mchanganuo wa gharama na mapato kwa Tawi la Dar es Salaam ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 25: Gharama na mapato halisi kwa Tawi la Dar es Salaam**

| Maelezo | Gharama za Undeshaji (Tshs) | Mapato yaliyokusanywa (Tshs) | Hasara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Mshahara wa Wafanyakazi | 8,916,000 | 737,385,173 | 114,746,718.08 |
| Kukodisha kwa jengo lililokodishwa | 30,010,651.53 | | |
| Gharama zingine za Uendeshaji | 30,786,585.82 | | |
| Gharama ya mauzo | 782,418,653.73 | | |
| **Jumla** | **852,131,891.08** | **737,385,173** | **114,746,718.08** |

## Majibu ya Uongozi wa Shirika

Ni kweli kwa muda mrefu ufanisi wa Tawi la ZSTC - Dar es Salaam sio mzuri kutokana na kushindwa kupata faida. Shirika limeamua kulifunga Tawi hilo na kubakisha Mtendaji

mmoja tu ambae atakuwepo Ofisi ya Uratibu wa shughuli za SMZ - Tanzania Bara.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli tawi hilo linaendeshwa kihasara. Hali hiyo imachangiwa zaidi na kufanya kazi zake katika jengo la kukodi ambalo linahitaji kulipiwa jumla ya shilingi zaidi ya milioni 2,000,000 kwa mwezi na kuongeza gharama za uendeshaji wake.

Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado mahitaji ya harakati za ununuzi na uuzwaji wa karafuu zinatakiwa zifanyike Jijini Dar es Salaam hasa ukizingatia kuna idadi kubwa ya watumiaji bidhaa zinazozalishwa Zanzibar sio tu karafuu bali kuna nyengine za viungo zikiwemo pilipili manga, hiliki na mafuta mbali mbali ya mimea.

Kutokana na umuhimu huo, Kamati ya PAC ilifanya ziara rasmi Jijini Dar es Salaam kuangalia kwa lengo la kuangalia kama kweli duka hilo limefungwa pamoja na kufuatilia rasilimali ya nyumba ya Shirika iliopo Sinza (Maelezo zaidi ya hoja hii yatapatikana katika Ripoti ya Kamati ya ziara hiyo). Kiujumla, Kamati imeridhika na hatua ambazo Shirika imezichukua za kulifunga duka hilo lakini kuweka Ofisi ndogo ya kuratibu shughuli za ununuzi na uuzwaji wa karafuu (chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliyopo Dar es Salaam) hususan zitakazonunuliwa Tanga na Morogoro pamoja na bidhaa nyengine tofauti.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa ZSTC uhakikishe unawezesha upatikanaji wa Ofisi hiyo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Jijini Dar es Salaam na kuwezesha ufanisi wake ili uratibu wa shughuli za ununuzi na uuzwaji wa karafuu uweze kufanyika ipasavyo.

## SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)- PEMBA

## Hoja nambari 4.1.4.9: Dosari katika ununuzi wa Vespa na Pikipiki shilingi 392,562,500

Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) Pemba limetuwasilishia barua yenye kumbukumbu namba ZSTCP/MI/1/82 ya tarehe 30/09/2022 inayotutaka kufanya ukaguzi wa kina unaohusiana na ununuzi wa Vespa 55 na Pikipiki 55 zenye thamani ya shilingi 392,562,500 baada ya kujitokeza kwa changamoto ya wakopaji kushindwa kulipa madeni yao kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba midogo midogo walioingia na ZSTC Pemba.

Katika kulifanyia kazi ombi hilo Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba iliwasilisha barua yenye kumbukumbu namba AUD/P/W/BMV/SBT/11/1/76 ya tarehe 03/10/2022 yenye lengo la kupatiwa taarifa zifuatazo kwa lengo kukamilisha zoezi la ukaguzi huo:

- Mpango wa manunuzi wa mwaka uliohusisha ununuzi wa vyombo hivyo.
- Barua ya maombi ya ununuzi wa Pikipiki na Vespa hizo.
- Tangazo la zabuni ya ununuzi wa Pikipiki na Vespa hizo.
- Tathmini ya zabuni iliyofanyika (Tender evaluation).
- Mkataba uliotumika katika ununuzi wa Pikipiki na Vespa hizo.
- Hati za malipo zilizotumika katika ununuzi wa vyombo hivyo.
- Sera ya ukopeshaji wa vyombo vya moto vya Shirika.
- Mchanganuo wa mkopo wa Pikipiki na Vespa (taarifa ya aliyekopeshwa na shehia aliyopo, kiwango cha fedha alichotakiwa kulipa, kiwango cha fedha alicholipa, pamoja na bakaa ya fedha anayodaiwa).
- Barua za malalamiko kutoka kwa masheha pamoja na majibu yake kutoka kwa Shirika.

Kutokana na Shirika la ZSTC kushindwa kuwasilisha taarifa hizo ukaguzi umebaini uwepo wa dosari zifuatazo:-

- Kukiukwa kwa taratibu za manunuzi kulikopelekea Shirika kufanya matumizi yenye thamani ya shilingi 392,562,500 bila ya kuzingatia thamani halisi ya fedha na tija inayoweza kupatikana kutokana na ununuzi huo.
- Kutokuwepo kwa Sera ya ukopeshwaji wa vyombo vya moto iliyoandaliwa na kupitishwa na Bodi ya Shirika la ZSTC.
- Kukosekana kwa mchanganuo wa deni halisi analodaiwa kila mkopaji, kiwango cha fedha alichorejesha pamoja na bakaa inayodaiwa.
- Kukosekana kwa vielelezo vyote vinavyothibitisha uhalali wa kufanyika kwa malipo hayo.
- Kukosekana kwa dhamira au muongozo kutoka kwa uongozi wa Bodi ya Shirika la ZSTC ulioruhusu kufanyika kwa malipo hayo.
- Kufanya manunuzi nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka.

- Kufanya manunuzi bila ya uwepo wa bajeti ya matumizi hayo.

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu zinaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kujitokeza kwa matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija na hatimae kuisababishia Serikali hasara ya matumizi ya fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kuhakikisha malipo ya fedha yanarejeshwa kwa wale wote walionufaika na mikopo hiyo pamoja na kuchukuwa hatua stahiki kwa watumishi waliohusika na matumizi mabaya ya fedha za umma ikiwemo kukata malipo ya madeni ambayo hayatarejeshwa na wakopaji.

### Majibu ya Uongozi wa Shirika

Shirika katika mwaka wa fedha 2018/2019, lilinunua Pikipiki 55 na Vespa 55 kwa ajili ya kuwakopesha mkopo, usio na riba Masheha wa Mikoa miwili ya Pemba kwa lengo la kurahisisha kazi mbali mbali za karafuu katika Shehia zao, sambamba na kazi zote za Serikali Vijijini.

Uamuzi huu wa kununua vyombo hivyo ulifanywa na Shirika la ZSTC 2019, ili kutekeleza Agizo la Serikali kupitia kwa aliyekuwa Waziri wa Biashara na Viwanda Mhe. Balozi Amina Salim Ali kwa Barua Nam. WBV/U.120/C.1 VOL.I ya tarehe 17/03/2018.

Aidha, Katika kutekeleza Agizo hilo Shirika kupitia Kikao cha tisa cha Bodi ya Zabuni chini ya Mwenyekiti wake Marehemu Ndugu Habib Ali Moh'd, kiliridhia ununuzi wa Pikipiki na Vespa 110 kwa njia ya moja kwa moja kutoka kwa Muagizaji. (Supplier).

Vespa hizo zilikabidhiwa kupitia kwa Masheha Ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Kusini na Kaskazini Pemba baada ya kila Sheha kufunga Mkataba wa mkopo huo na Shirika la ZSTC. Aidha marejesho ya mikato hio ilikuwa ilikatwa kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa ambao hufanya malipo kwa Shirika.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika uchunguzi wa hoja hii, Kamati imebaini kwamba ni kweli Masheha walikopeshwa vyombo vya moto kwa nia njema ya kurahisisha utendaji kazi wao. Hata hivyo, kamati imegundua kwamba kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za kisheria katika hatua za awali za utekelezaji agizo hilo kwani hakukuwa na barua zilizoonesha uhitaji wake na kutia shaka kwamba kuna uwezekano wa Masheha kununuliwa vespa bila ya kuwepo ridhaa zao. Aidha, hakukufanyika zabuni kwa vile fedha ya ununuzi ni kubwa (shilingi 392,562,500).

Sambamba na kasoro zilizojitokeza katika ununuzi wa vespa na pikipiki hizo, Kamati

imebaini kwasasa hoja hiyo imeshatekelezwa kwa vile hakuna Sheha ambae anadaiwa kwani madeni yote yameshalipwa isipokuwa masheha wawili ambao wamefariki. Kamati imelithibitisha hilo baada ya kujiridhisha na vilelezo vya ununuzi huo wa vyombo vya moto.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inashauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kuhakikisha wanafuata Sheria, Kanuni na taratibu zinazoelekezwa na Serikali ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za Serikali Pamoja na kuepusha kutokea kwa Hoja kama hii kwani lengo lake ni zuri lakini utekelezaji wake ndio uliokiuka baadhi ya taratibu.

## Hoja nambari 4.1.4.10: Malipo ya fedha ambayo hayakukatwa kodi ya zuio shilingi 37,420,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 37,420,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Biashara la Taifa Pemba.

Dosari iliyobainika ni kutokukatwa kodi ya zuio kwa malipo yaliyofanyika kwa watoa huduma jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Pemba kuhakikisha kwamba unaongeza juhudi katika kusimamia na ufuatiliaji wa mapato ya Serikali.

Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwa ni pamoja na Sheria ya kodi ili kuweza kusimamia uzuiaji wa kodi kwa watoa huduma husika. Mchanganuo wa malipo ni kama inavyoonekana katika jadueli lifuatalo hapo chini.

**Jadweli Nambari 26: Malipo ya fedha ambayo hayakukatwa kodi ya zuio**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tzs) | Aielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| SP01418/2022 6/4/2022 | T.T | 3,200,000.0 | Mayusa Aluminium Trading PartnerShip | Malipo ya fedha za kazi ya kutengeneza madirisha na milango |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| SP02162/2022 | T.T | 15,870,000.0 | Salmin Juma Khamis | Malipo ya fedha kwa kazi ya kusafisha pamoja na matengenezo ya mashimo ya karo za majengo ya ZSTC |
| SP02803/2022 01/6/2022 | T.T | 18,350,000.0 | Abdalla Omar Abdalla | Malipo ya fedha kwa kazi ya kusafisha pamoja na matengenezo ya ukuta ,mashimo ya karo katika majengo ya ZSTC. |
| **Jumla** | | **37,420,000.0** | | |

**Majibu ya Uongozi wa Shirika**

Shirika limepokea na linakubaliana na maelezo yaliyoelezwa kupitia hoja hii kwamba kiasi cha fedha zilizotajwa hapo juu zinazohusiana na malipo ya fedha ambayo hayakukatwa kodi ya zuio.

Kwa muda mrefu Shirika limekuwa Wakala mkubwa wa kuzuia kodi za Serikali kutoka kwa watoa huduma na Wafanyabiashara kwa ujumla hadi kujipatia sifa za kuwa miongoni mwa wakusanyaji bora wa kodi za Serikali.

Hata hivyo, Shirika linakubaliana na kasoro iliyojitokeza ambayo ilitokana na mabadiliko yaliyofanyika kupitia Bodi ya Mapato kutoka risiti za mkono na kwenda risiti za

kielektoniki ambapo kulikuwa na uhaba wa elimu kwa baadhi ya Watendaji kuhusiana na ukataji wa kodi.

Aidha, baada ya kukaa pamoja na uongozi wa Bodi ya Mapato kasoro hizo tayari zimefanyiwa kazi na wale wote ambao hawakukatwa kodi tayari wamewasilishwa Bodi ya Mapato kwa ajili ya kufanyiwa mapitio ya malipo yatokanayo na huduma walizotoa kwa Shirika na ulipaji wa kodi kwa ujumla.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati katika kuifuatilia ukweli wa hoja hii, imebaini kwamba ni kweli uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa halikuzuia kodi zinazotokana na huduma zilizotolewa kwao kutokana na uzembe wa Watendaji wake. Kamati ilipoambiwa kwamba kodi hiyo imelipwa kama yanavyoeleza majibu ya Shirika ilitaka ipatiwe risiti (kielelezo) kuthibitisha ukweli wake lakini watendaji wa Shirika walishindwa.

Kwa msingi huo, Kamati imeamua kuna ulazimu wa kodi hiyo kulipwa ili mapato ya Serikali yaweze kupatikana. Kwa vile hoja hiyo haijatekelezwa ipasavyo, Kamati inamtaka Mkaguzi kuendelea kuifuatilia kwa karibu hadi itakapolipwa, hivyo hoja hiyo inabakia.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati inaishauri Uongozi wa ZSTC kufuatilia na kuwasilisha mbele ya Kamati kielelezo cha ulipaji wa kodi hiyo.
2. Iwapo Shirika litabaini kwamba kodi hiyo haijalipwa, lihakikishe linakamilisha malipo hayo ili kodi ya Serikali iweze kupatikana.
3. Kamati inaushauri uongozi wa Shirika kuhakikisha unakuwa Wakala mzuri wa kuzuia kodi ya Serikali ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Sheria za kodi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

## ZIARA YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KATIKA NYUMBA NA DUKA LA SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) - JIJINI DAR ES SALAAM

## UTANGULIZI:

Siku ya tarehe 7 Febuari, 2024, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) imefanya ziara ya kuitembelea nyumba inayomilikiwa na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) iliopo katika eneo la Sinza Jijini Dar es Salaam panoja na kufanya ziara na

kikao katika nyumba hiyo. Mazungumzo yaliyofanyika yalihusu maendeleo ya nyumba ya ZSTC pamoja na ufanyaji kazi wa duka lao liliopo mtaa wa Sinza ikiwa ni ufuatiliaji wa hoja za Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2021/2022 inayohusiana na Ukaguzi wa wa Taasisi Mashirika na Taasisi zinazojitegemea.

## WASHIRIKI WA ZIARA

Ziara hiyo iliwashirikisha wafuatao:

1. Ujumbe wa Kamati ya PAC ukiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo;
2. Watendaji kutoka ZSTC wakiongozwa na Katibu Mkuu wao Ndugu Ali Khamis; na
3. Mjumbe kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) ambae ni Ndugu Shekhe Abdalla Ali.

## UFUNGUZI WA KIKAO

Baada ya kufanya matembezi ya ukaguzi wa nyumba hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya PAC alikifungua kikao saa 3:42 za asubuhi kwa kumtaka Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZSTC ambae alieleza kwa ufupi historia ya nyumba ya Sinza pamoja na uendeshaji wa duka lao.

## UWASILISHAJI WA ZSTC

Katika uwasilishaji wake, Mkurugenzi Mwendeshaji aligusia mambo yafuatayo:

1. Nyumba ya ZSTC Sinza ni ya zamani na kongwe ambayo haiwezi kuitumika tena kibiashara. Hivyo, wametakiwa na Serikali kupeleka andiko maalum (proposal) litakaloonesha Mpango wa kibiashara utakaowawezesha kupata kibali cha Serikali cha kufanya ujenzi katika eneo hilo;
2. Mpango walionao ni kuweka kipambele cha kukopa fedha katika Taasisi za kibenki kwa ajili ya ujenzi wa eneo hilo kuliko kufanya ubia na Taasisi nyengine. Aidha, wana mpango wa kuinunua nyumba iliyopo jirani yao ili kuliongeza eneo lao la ujenzi.
3. ZSTC wapange fedha katika bajeti yao ya mwakani za uandaaji michoro wa jengo lao na wawatumie Wakala wa Ujenzi Zanzibar kufanya kazi hiyo kabla ya kutumia Taasisi au Kampuni binafsi.
4. Nyumba hiyo inayo hatimiliki ambapo kwasasa vyumba vya kwenye banda (vitatu)

vimekodishwa kwa wapangaji wawili kwa shilingi elfu 40 kwa chumba na maduka matatu yamekodishwa kwa shilingi 70,000 kila moja. Kwa upande wa nyumba kubwa inatumiwa na Mfanyakazi na familia yake.

5. Kwa upande wa duka la ZSTC, wana mpango wa kulifunga kwa vile halifanyi vizuri kibiashara na wanalipa zaidi ya shilingi milioni 2,000,000 ikiwa ni kodi ambayo ni kubwa tofauti na kodi zinazolipwa na nyumba nyengine katika eneo hilo. Hata hivyo, wameomba wapatie Ofisi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliyopo Kivukoni - Tanzania Bara ili waweze kuratibu shughuli za Mpango wa biashara watakaouanzisha wa ununuzi na uuzwaji wa Karafuu kutoka Morogoro na Tanga. Katika utekelezaji mpango huo, ZSTC haitozichanganya karafuu za Zanzibar na karafuu hizo.
6. ZSTC tayari wameshafanya mazungumzo na Halmashauri za Morogoro na Tanga kuhusu mpango wao wa kununua karafuu zao na kwa hatua za awali watatafuta Kampuni itakayotoa malipo ya awali yatakayotumika kukodi maghala ya Jumuiya ya Vyama vya Ushirika (AMCOS). ZSTC watakuwa wanatumia wafanyakazi wa muda na kuwapatia utaalamu wa uchumaji, uchungaji na uchambuaji wa karafuu kwa vile maeneo hayo yanakarafuu nyingi lakini hawana utalaamu wa kuzishughulikia ipasavyo.
7. Mpango wa baadae wa ZSTC ni kutanua wigo wa biashara katika maeneo hayo kwa kufanya biashara ya mazao ya viungo ya vanila, hiliki na pilipili manga.

## MAPENDEKEZO YA KAMATI YA PAC

1. ZSTC ihakikishe inaweka fedha katika bajeti ya mwakani (2024/2025) ili kuweza kuandaa michoro ya ujenzi wa jengo lao katika nyumba ya Sinza.
2. ZSTC iweke kipaumbele cha kutafuta mikopo katika mabenki ya kibiashara (Commercial Banks) na sio kufanya ubia katika ujenzi watakaoufanya.
3. ZSTC iwe makini katika ununuzi na uuzwaji wa karafuu za Tanga na Morogoro wa kutokuzichanganya na karafuu za Zanzibar hali itakayopelekea kuharibu thamani yake.
4. Katika utekelezaji wa Mpango wa biashara ya Tanga na Morogoro, ZSTC ihakikishe inakuwa na mikataba mizuri itakayohakikisha upatikanaji wa faida itokanayo na biashara hiyo.

5. ZSTC ihakikishe inafuata taratibu katika matumizi ya wafanyakazi wa muda ili kuepuka dosari za kiukaguzi.
6. ZSTC ihakikishe inatanua wigo wa kufanya biashara ya mazao ya viungo katika maeneo ya Tanga na Morogoro.

## HITIMISHO

Kikao hicho kilifungwa na Mwenyekit wa Kamati ya PAC saa 5:04 za asubuhi na kuwatikia ZSTC utekelezaji mwema wa malengo yao na Kamati inakubaliana nayo.

# 5.0 MAMLAKA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## 5.1.4 MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA) - UNGUJA

### Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 101,495,528,432, kati ya fedha hizo shilingi 18,208,200,000 ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na shilingi 72,416,837,232 ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, Mamlaka ya Maji Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 10,870,491,200 kutoka vyanzo vyake vya ndani vya mapato.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Mamlaka ya Maji Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi21,741,185,977.54 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 119.4 ya makadirio, na jumla ya shilingi 94,982,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo sawa na asilimia 0.13 ya makadirio. Aidha, Mamlaka ya Maji Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 3,426,482,334.16 kutoka vyanzo vyake vya ndani vya mapato sawa na asilimia 31.52 ya makadirio.

#### Majibu ya Uongozi wa Mamalaka

Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Mamlaka ya Maji imepangiwa kukusanya Tsh 10,870,491,200 kutoka vyanzo vya ndani na Tsh 18,208,200,000 kutoka Serikali kuu kwa shughuli mbali mbali za miradi ya maendeleo na Tsh 72,416,837,232 ni fedha za Wahisani wa Maendeleo.

Ni kweli Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilifanikiwa kupata Tsh 94,982,000 kutoka kwa wahisani wa maendelea sawa asilimia 0.13 ya makadirio

Hii imetokana na wakandarasi ambao kwa kawaida hulipwa kwa mujibu wa asilimia ya

kazi waliyoikamilisha hata kama bajeti inaruhusu malipo kufanyika zaidi. Katika kipindi hicho wakandarasi hawakuweza kukamilisha utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka huo kutokana na:-

I. Upatikanaji wa mali ghafi za ujenzi ambazo kwa asilimia 75% zilikuwa zinapatikana nje ya Tanzania

II. Changamoto za upatikanaji wa vibali vya kupata mali ghafi za ujenzi kutoka Tanzania Bara

Uchelewaji wa vifaa kutoka bandarini hapa Zanzibar.

Tsh 21,741,185,977.54 zilipatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanya wastani wa asilimia 119.4 ya makadirio ya bajeti hii imesababishwa na uwepo wa matumizi ya fedha za ahueni ya Covid-19 ambayo hayakuwa kwenye bajeti ya awali ya Mamlaka.

Aidha, Tsh 3,426,482,334.16 zilikusanywa kutoka vyanzo mbali mbali vya ndani ambapo matarajio yalikuwa Tsh 10,870,491,200 sawa na asilimia 31.52 kulikosababishwa na sababu zifuatazo:-

I. Mamlaka ya Maji haikuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa asilimia Mia Moja kama ilivyokadiria kutokana na uhaba wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa kipindi hicho

II. Kukosekana kwa huduma ya maji katika baadhi ya maeneo ya kimkakati ya uwekezaji hasa Mkoa wa Kaskazini na Kusini Unguja

Muamko mdogo wa malipo kwa wateja wanaopata huduma ya maji ambayo

haikuwa ya uhakika.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa mapato ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) haikuweze kufikia malengo yake ukusanyaji kwa vile walikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 10,870,491,200 na kubahatika kukusanya jumla ya shilingi bilioni 3,426,482,334.16 sawa na asilimia 31.52 ya makadirio. Hali hiyo inasababishwa na kukosekana kwa upatikanaji wa huduma ya maji hususan katika Mahoteli. Aidha, kujitokeza kwa UVIKO 19 pamoja na kutopata mapato kutokana na kukosekana kwa maji pamoja na kwamba wateja waliokuwa tayari wameshafungiwa mita za maji.

Kufuatia upatikanaji huo, Kamati imetaka kujua kwa kiasi gani ZAWA iliathirika na kujulishwa kuwa Miradi mingi ya maji ilishindwa kukamilik kwa wakati uliopangwa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. ZAWA iongeze nguvu katika ufungaji wa mita za maji hususan katika maeneo ambayo huduma ya maji inapatikana ipasavyo ili kuongeza mapato katika hesabu zao.
2. Uongozi wa ZAWA uendelee zaidi na harakati za utoaji wa elimu kwa jamii kuhusuiana na suala zima la uchangiaji wa huduma ya maji.

## Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa kutumia jumla

ya shilingi 101,495,548,432, kati ya fedha hizo shilingi 11,521,214,295 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 89,974,334,137.00 ni kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo.Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Mamlaka ya Maji Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 24,785,748,448.69 sawa na asilimia 24.4 ya makadirio, kati ya fedha hizo shilingi 5,438,229,783.57 ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia 47.2 ya makadirio na shilingi 19,347,518,665.12 ni matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 21.5 ya makadirio.

Aidha, Mamlaka ya Maji Zanzibar ilitarajia kutumia jumla ya shilingi 72,416,917,232 katika Mradi wa maji unaotokana na mkopo wa Benki ya EXIM ya India ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 jumla ya shilingi 67,924,570,393 sawa na asilimia 93.8 ya makadirio zililipwa na Benki ya EXIM ya India kwa ajili ya Wakandarasi na Washauri Elekezi wa Mradi huo

**Majibu ya Uongozi wa Mamalaka**

ya matumizi ya kawaida na shilingi 89,974,334,137.00 ni kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo.Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Mamlaka ya Maji Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 24,785,748,448.69 sawa na asilimia 24.4 ya makadirio, kati ya fedha hizo shilingi 5,438,229,783.57 ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia 47.2 ya makadirio na shilingi 19,347,518,665.12 ni matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 21.5 ya makadirio.

Aidha, Mamlaka ya Maji Zanzibar ilitarajia kutumia jumla ya shilingi 72,416,917,232 katika Mradi wa maji unaotokana na mkopo wa Benki ya EXIM ya India ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 jumla ya shilingi 67,924,570,393 sawa na asilimia 93.8 ya makadirio zililipwa na Benki ya EXIM ya India kwa ajili ya Wakandarasi na Washauri Elekezi wa Mradi huo. Ni kweli Mamlaka iliweza kutumia. Kiasi kidogo cha matumizi yote kulinganisha na makadirio ya Bajeti. Hii inasababishwa na upatikanaji finyu wa wa mapato kutoka katika maeneo yote ikiwemo fedha kutoka serikali kuu na makusanyo ya

ndani. Aidha matumizi na malipo ya Wahisani hutegemea asilimia ya kazi iliyofanywa na mkandarasi husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuchunguza hoja hii ya taarifa ya Matumizi, Kamati imebaini kuwa awali mishahara ya Mamlaka ya Maji Zanzibar ilikuwa ikilipwa kupitia fungu la Mamlaka hiyo lakini kwasasa mishahara hiyo inaendelea kulipwa kupitia Wizarani. Kiutaratibu, ZAWA ni Mamlaka inayojitegemea ambayo hutakiwa kujiendesha yenyewe ikiwemo ulipajji wa maslahi ya Watendaji wake. Kwa msingi huo, suala hilo linafanyika kinyume na miongozo ya uendeshaji wa Mamlaka hiyo. Hivyo, kuna haja ya suala zima la ulipaji wa maslahi hayo ufanywe kupitia fungu la Mamlaka husika.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe inaruhusu ulipaji wa mishahara ya Watendaji wa ZAWA ufanywe na Mamlaka yenyewe.

## Hoja nambari 5.1.4.1: Dosari katika mfumo wa uandaaji wa taarifa za Fedha (Financial Reporting Framework)

Kwa mujibu wa taarifa za Afisa Masuuli, tamko la Mkuu wa Kitengo cha Hesabu pamoja na maelezo ya taarifa za fedha (notes) za hesabu za mwisho wa mwaka 2021/2022 za Mamlaka, Hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka ya Maji Zanzibar zimefungwa kwa kuzingatia msingi wa fedha taslim (Cash basis) ambapo taasisi inatambua mapato pale inapopokea fedha taslim na kutambua matumizi. pale inapolipa fedha taslim.

Tathmini ya ukaguzi katika mfumo wa uandaaji wa taarifa za Fedha za Mamlaka (Financial Reporting Framework) umebaini kuwa msingi uliotumika wa “cash basis” haukidhi katika kupima ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za Mamlaka kutokana na kuwa msingi huo unapelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka. Baadhi ya taarifa zinazokosekana katika msingi wa fedha taslim ni pamoja na taarifa ya mali za kudumu za Mamlaka (Non-current Asset), uchakavu wa mali za kudumu za Mamlaka (Depreciation), Ukwasi wa Mamlaka (Liquidity), Madeni ya Mamlaka (Payables), Mtaji wa Mamlaka (Tax Payers Fund), Ziada au nakisi ya mwaka ya Mamlaka (Surplus or Deficit) na faida au hasara inayotokana na kupanga au kushuka kwa thamani ya fedha za kigeni (gain or loss on foreign exchange).

Kuendelea kutumia msingi wa fedha taslim (Cash basis) katika uandaaji wa hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka kunapelekea kukosekana uwazi na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za Umma katika uendeshaji wa Mamlaka na pia Mamlaka kushindwa kuandaa taarifa za Fedha za mwisho wa mwaka zinazotakiwa kuandaliwa kwa mujibu wa kifungu nambari 121 cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Kwa mujibu wa taarifa za Afisa Masuuli, tamko la Mkuu wa Kitengo cha Hesabu pamoja na maelezo ya taarifa za fedha (notes) za hesabu za mwisho wa mwaka 2021/2022 za Mamlaka hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka ya Maji Zanzibar zimefungwa kwa kuzingatia msingi wa fedha taslim (Cash basis) ambapo taasisi inatambua mapato pale inapopokea fedha taslim na kutambua matumizi pale inapolipa fedha taslim.

Ni kweli hadi CAG anamaliza zoezi la ukaguzi wa hesabu za Mamlaka zinazoishia Juni 30, 2022 Mamlaka ilikuwa inatunza hesabu zake kwa mfumo wa Fedha taslim (Cash Basis). Kwa sasa mamlaka imebadilika na kuandaa hesabu zake kwa mfumo Accrual Basis ambapo taarifa zote muhimu zinazohitajika na viwango na maelekezo mbali mbali ya kifedha yatazingatiwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii Kamati ya PAC imeridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) katika kutatua kasoro iliyoainishwa na Mkaguzi katika ripoti. Hivyo Kamati imeiondoa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ihakikishe inasimamia ipasavyo Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016 katika kutekeleza majukumu yao ili kuepusha migongano na upotevu wa fedha za Umma.

## Hoja nambari 5.1.4.2: Kuchelewa kupitishwa kwa bajeti ya Mamlaka ya mwaka 2022/2023

Kwa mujibu wa kifungu nambari 32(3) cha Sheria nambari 4 ya Maji (2006), Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka inatakiwa kukutana kwa ajili ya kupitisha bajeti ya mwaka ya Mamlaka katika kipindi kisichozidi miezi miwili kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha na

kuiwasilisha kwa Waziri dhamana kwa ajili ya kupata idhini.

Ukaguzi umebaini kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar imefanya kikao maalum cha kuidhinisha bajeti ya mapato na matumizi ya ZAWA kwa mwaka wa fedha2022/2023 tarehe 26 Juni, 2022 ambapo ni siku 5 kabla ya mwaka mpya wa fedha kuanza kinyume na sheria ya Mamlaka.

Kutofanyika kwa vikao vya bajeti kwa wakati kunapelekea bajeti ya Mamlaka kutoweza kuidhinishwa kwa wakati kama inavyotakiwa na Sheria.

#### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 32(3) cha Sheria nambari 4 ya Maji (2006), Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka inatakiwa kukutana kwa ajili ya kupitisha bajeti ya mwaka ya Mamlaka katika kipindi kisichozidi miezi miwili kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha na kuiwasilisha kwa Waziri dhamana kwa ajili ya kupata idhini Ni kweli Mamlaka ilichelewa kuwasilisha rasimu ya bajeti kwenye Bodi ya Wakurugenzi kwa kujadiliwa na kuidhinishwa kama taratibu zinavyoelekeza. Mamlaka imechua hatua za kuhakikisha kwamba bajeti zijazo zinawasilishwa na uidhinishwa na Bodi ya wakurugenzi ndani ya muda unaotakiwa kwa mujibu wa taratibu na miongozo.

#### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na Mamlaka kukiri kuwepo kwa kasoro ya kuchelewa kupitishwa kwa bajeti na kuidhinishwa kama taratibu zinavyoelekeza. Hivyo, Kamati ya PAC imeshindwa kuionda hoja hii kutokana kutokukamilika kwa taratibu za utekelezaji wake.

#### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ihakikishe inafuata taratibu zilizopo katika Sheria, Kanuni na Miongozo mbali mbali katika uidhinishwaji wa bajeti ili kuepusha hoja kama hii kujitokeza tena katika mwaka wa fedha ujao.

### Hoja nambari 5.1.4.3: Kukosekana kwa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework)

Kwa mujibu wa kanuni nambari 154, 155 na 156 za Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021, Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma anapaswa kutengeneza, kutekeleza na kuimarisha Mfumo) wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework). Aidha, Afisa Masuuli anapaswa kuhakikisha kuwa ripoti za usimamizi wa

vihatarishi (risk management reports) zinawasilishwa katika kamati ya ukaguzi angalau mara nne (4) kwa mwaka.

Ukaguzi umebaini kuwa bado Mamlaka ya Maji Zanzibar haina Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk management Framework) kunakoendana sambamba na kukosekana kuwasilishwa ripoti za usimamizi wa vihatarishi kwa kamati ya ukaguzi.

Kukosekana kwa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework) katika Mamlaka kunapelekea Mamlaka kushindwa kutambua na kuingiza katika mikakati na mipango ya Mamlaka vihatarishi vilivyopo na vinavyoweza kuwepo katika utendaji kazi wa Mamlaka ikiwemo vihatarishi vya kisheria (legal risks), vihatarishi vya uhalifu mitandaoni (cyber security risks), na vihatarishi vya mazingira ya utendaji kazi (operational risks).

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Kukosekana kwa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework)

Ni kweli Mamlaka ya Maji Zanzibar haina Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework). Mamlaka ya Maji imepokea ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Maji imeandaa bajeti kwa ajili ya kutayarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi. Kwa hivi sasa, Mshauri Elekezi wa kuifanya kazi hiyo amepatikana na anaendelea na kazi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC baada ya kupokea majibu ya utekelezaji wa hoja hii, imeshindwa kujiridhisha na kupelekea kuibakisha hoja hii kwa hatua za utekelezaji.

**Maoni, Ushauri na Mapendeko ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji kufuata ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuondokana na hoja zisizo na msingi.

## Hoja nambari 4.1.4.4: Kutokuwepo kwa sera ya utoaji huduma kwa mkopo (Credit policy)

Mamlaka ya Maji Zanzibar katika kutekeleza majukumu yake ya kukuza na kuendeleza kutoa huduma ya upatikanaji wa maji Zanzibar huwa inatoa huduma zake kwa kutoza ada mbalimbali ambazo hupelekea Mamlaka kuzidai kampuni, mahoteli na wananchi ambao wanapokea huduma kutoka kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar. Uwepo wa sera ya

utoaji huduma kwa mkopo (credit policy) husaidia taasisi kubainisha ni wateja gani wanastahiki kupewa mkopo au huduma gani inastahiki kutolewa kwa mkopo na pia inabainisha hatua zitakazochukuliwa na taasisi ili kukusanya madeni wanayodai.

Ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba Mamlaka ya Maji Zanzibar haina sera ya utoaji huduma kwa mkopo (credit policy) licha ya ukweli kuwa Mamlaka kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022 ilikuwa na wadaiwa wenye jumla ya shilingi 24,299,279,785.3.

Kutokuwepo kwa Sera ya madeni kunaweza kupelekea kuongezeka kwa madeni ya wadaiwa wa Mamlaka na hatimae kupelekea Mamlaka kupoteza mapato yanayotokana na vyanzo vyake vya mapato vya ndani.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Ni kweli Mamlaka ya haina Sera ya Utoaji Huduma kwa Mkopo (Credit Policy).

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Maji imeandaa bajeti kwa ajili ya kutayarisha Sera ya Utoaji Huduma kwa Mkopo (Credit Policy) Kwa hivi sasa, Mshauri Elekezi wa kuifanya kazi hiyo amepatikana na anaendelea na kazi.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa kabla ya ukaguzi kufanyika Mamlaka ya Maji ilikuwa haina uwelewa juu ya umuhimu wa utumiaji wa Sera ya Utoaji Huduma kwa Mikopo (credit policy), na kupelekea kujitokeza kwa dosari hii. Hadi Kamati inamaliza uchunguzi wake Sera hiyo haijakamilika.

Kwa mnasaba huo, hoja hii imebakia kwa ajili ya hatua za ukamilishaji wa Mshauri Elekekezi katika kuifanyia kazi Sera hiyo.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji ikamilishe uandaaji wa Sera ya Utoaji wa Huduma za Mikopo pamoja na Sera ya madeni ili Mamlaka kuweza kuondokana na upotevu wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

## Hoja nambari 4.1.4.6: Manunuzi kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya ZPPDA shilingi 1,826,609.60.

Kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za

Umma ya mwaka 2016 inazitaka taasisi za utoaji huduma au uuzaji bidhaa kusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili ziweze kushiriki katika manunuzi ya umma. Vile vile kifungu nambari 23(2), kinakataza manunuzi kufanywa kwa watoa huduma au wauzaji bidhaa ambao hawajasajiliwa.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar katika mwaka wa fedha 2021/2022 imetumia jumla ya shilingi 1,826,609.60 kwa ajili ya ununuzi wa chakula na viburudishaji kutoka kwa wauzaji mbalimbali ambao wakati wanatoa huduma hizo hawakuwa wamesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA).

Kufanya malipo kwa wauzaji bidhaa au watoa ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ni kwenda kinyume na sheria ya Ununuzi wa Uondoaji wa Mali za Umma na kunaweza kupelekea kupoteza mapato ya Serikali.

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa mamlaka kuhakikisha kua inafuata sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma ya mwaka 2016 kwa kufanya manunuzi kupitia watoa huduma ambao wamesajiliwa na Mamlaka ya ZPPDA ili kukuza uadilifu na imani katika michakato ya manunuzi ya umma.

### Majibu ya Uongozi wa Mamalaka

Manunuzi kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya ZPPDA shilingi 1,826,609.60. Kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 inazitaka taasisi za utoaji huduma au uuzaji bidhaa kusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili ziweze kushiriki katika manunuzi ya umma. Vile vile kifungu nambari 23(2), kinakataza kufanywa kwa watoa huduma au wauzaji bidhaa ambao hawajasajiliwa.

Ni kweli Mamlaka ya maji ilifanya manunuzi kwa kutumia watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi ZPPDA. Kwa sasa Mamlaka ya Maji inafanya manunuzi yake yote kwa kutumia mfumo na watoa huduma walioasajiliwa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa Mamlaka imefanya huduma kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa katika Mamalaka ya Manunuzi jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria ya Mamlaka ya Maji (ZAWA) inashauriwa kufuata Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 katika utekelezaji wa kazi za Serikali.

Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nambari 11 ya mwaka 2016.

Kwa msingi huo, Kamati imeridhishwa na hatua za utekelezaji zilizochukuliwa na Uongozi wa Mamlaka katika kuondokana na changamoto ya kufanyakazi na watoa huduma ambao hawajasajiliwa na kupelekea hoja kuondoka.

## Hoja nambari 4.1.4.7: Kuwepo kwa visima ambavyo vimesimama na havifanyi kazi

Mamlaka ya Maji Zanzibar inatoa huduma ya usambazaji maji maeneo yote Unguja na Pemba na kwa kiasi kikubwa Mamlaka inategemea visima vya maji ambapo kwa sasa Mamlaka inatumia jumla ya visima 303 katika uzalishaji wa maji hayo, kwa upande wa Unguja kuna visima 172 na Pemba kuna visima 131.

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya visima 39 vya unguja na 15 vya Pemba vimesimama na havifanyi kazi ya uzalishaji maji kwa kipindi kirefu kutokana na sababu ya kuharibika mashine ya kupandishia maji, kukatika kwa shaft za pampu, kuungua kwa vifaa vya umeme kama ‘mp 204’, ‘circuit breaker’ na kubomoka kwa visima. Kwa mujibu wa majibu ya Uongozi, Mamlaka ya Maji imeshanunua pampu kupitia Mradi wa Ahueni ya UVIKO-19 pampu 123 kwa visima vilivyokosa kutoa huduma kwa muda mrefu ambapo hatua za ufungaji wa pampu hizo zimeshaanza kwa baadhi ya visima. Kuwepo kwa baadhi ya visima visivyofanya kazi kunapelekea baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba kukosa huduma ya maji na kupelekea Mamlaka ya Maji Zanzibar kutofikia malengo yake ya utoaji wa huduma ya maji Zanzibar kwa ufanisi.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Kuwepo kwa visima ambavyo vimesimama na havifanyi kazi. Mamlaka ya maji Zawa inachukuwa ushauri wa mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kuufanyia kazi na kwa hivisasa Mamlaka inaendelea kufunga pampu za visima vilivyokuwa na khitilafu ya umeme.

Kwasasa mamlaka ya Maji imeboreresha huduma zake kwa kufunga pampu katika visima maeneo ya Unguja na Pemba na huduma ya maji imeimarika.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati wakati kufuatilia utekelezaji wa hoja hii imegundua kwamba Mamlaka imeshazifanyia kazi kasoro zilizoainishwa na Mkaguzi ambapo kati ya Visima 54 vya Unguja na Pemba ambavyo vimetajwa katika ripoti ya mdhibiti visima 21 vimeshafanyiwa matengenezo na visima 49 kupitia Mradi wa Ahueni ya Uviko 19 tayari vimeshafungwa

pump.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Mamlaka ya Maji (ZAWA) uhakikishe visima ambavyo Mkaguzi amevibainisha katika hoja hii na bado havijafanyiwa matengenezo, vitengenezwe ili lengo ya Serikali ya kuwapatia Wananchi wake maji safi na salama lifikiwe.

## Hoja nambari 5.1.4.8: Kuwepo kwa uchafuzi wa mazingira kwa baadhi ya maeneo ya vianzio vya maji vya Mamlaka.

Chemchem ya maji ya Mtopepo ni moja miongoni mwa vyanzo vya maji safi muhimu kinachotumiwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa ajili ya usambazaji maji safi maeneo mbali mbali katika Mji wa Unguja.

Baada ya kutembelea baadhi ya maeneo ya vyanzo vya Maji vya Mamlaka, ukaguzi umebaini kuwepo kwa uharibifu wa mazingira yanayozunguka chanzo cha maji cha Mtopepo, uharibifu ambao umesababishwa kwa kuwepo kwa mtaro wa maji machafu ambao unapita pembezoni mwa chanzo hicho cha maji cha Mtopepo.

Kuwepo kwa uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji kunapelekea kuhatarisha usalama wa kiafya kwa watumiaji maji ya Mamlaka.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Kuwepo kwa uchafuzi wa mazingira kwa baadhi ya maeneo ya vianzio vya maji vya Mamlaka.

Mamlaka ya Maji kupitia Idara ya Rasilimali Maji imechukua juhudi za kuhakikisha kuwa chemchem ya maji ya Mtopepo inabakia kuwa salama kwa matumizi ya binadamu ambapo wakati wa ujenzi wa mtaro husika iliwaelekeza wakandarasi wa Mradi wa ZUSP kujenga na kuhifadhi kingo za chemchem ambapo ujenzi wa 'Gabion" katika eneo husika umefanyika pamoja na uwekaji wa kifusi ili kuzuwia mmong'onyoko. Aidha, Mamlaka ya maji imechukuwa jitihada za kupanda miti katika eneo hilo ili kuimarisha na kuhifadhi mazingira, Pamoja na kufanya usafi wa mazingira yanayozunguka eneo la chemchem zoezi ambalo ni endelevu na hufanyika kila baada ya muda.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Baada ya Kamati ya PAC kuchunguza hoja hii imebaini kwamba Uongozi wa Mamlaka ya Maji umeshakuwa hatua stahiki za kuondosha changamoto hizo katika maeno ya vianzio

ya maji na kupelekea Kamati kuiondoa hoja hiyo.

## Hoja nambari 5.1.4.9: ukosefu wa wafanyakazi

Mamlaka ya Maji Zanzibar ina jumla ya wafanyakazi wanaofikia takriban 501 ambapo Unguja kuna jumla ya wafanyakazi 279 na Pemba kuna jumla ya wafanyakazi 222. Kwa upande wa Unguja Idara ya rasilimali maji ya Mamlaka ina jumla wafanyakazi 17 na idara ya ufundi ina jumla ya wafanyakazi 135.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar ina changamoto ya upungufu wa wataalam hususan katika Idara ya Ufundi na Idara ya Rasilimali maji, ambapo kwa upande wa Unguja ukaguzi umebaini kuwa Idara ya rasilimali maji ina wataalamu 10 tu wenye elimu kuanzia stashahada (diploma) na kuendelea na Idara ya ufundi ina wataalam 12 tu wenye elimu kuanzia stashahada (diploma) na kuendelea.

Kuwepo kwa upungufu wa wafanyakazi wenye taaluma katika idara ya Rasilimali maji na Idara ya Ufundi kunaweza kupelekea kukosekana kwa ufanisi katika usimamizi na uendelezaji wa vyanzo vya maji vya Mamlaka pamoja na matengenezo ya miundombinu ya huduma ya maji inayotolewa na Mamlaka.

### Majibu ya Mamlaka ya ZAWA

Mamlaka ya Maji Zanzibar inakiri kuwa na uhaba wa wafanyakazi hasa katika kada za msingi za Operesheni za Kiufundi na Rasilimali Maji.

Mamlaka ya maji Zanzibar imepata Ridhaa ya kuajiri wataalamu 27 kwa maeneo mbalimbali Operesheni za Kiufundi na Rasilimali Maji kwa mwaka 2022/2023. Aidha Mamlaka imepata kibali chengine cha kuajiri nafasi nyengine mpya za wafanyakazi 68 katika mwaka 2023/2024, kati ya nafasi Sitini na Nane (68) za kazi, nafasi Thelathini na Nane (38) sawa na asilimia 56.72 zimeelekezwa katika idara hizo mbili zikihusisha Wahandisi, Fundi Mchundo na Fundi Sanifu

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati imeridhishwa na hatua ambazo Mamlaka imechukua ya kurekebisha changamoto ya uhaba wa watumishi katika maeneo ambayo Mkaguzi imeyaanisha katika kitabu cha Ripoti na hatimae hoja hii kuondolewa.

## Hoja nambari 5.1.4.10: Kutokufikiwa kwa malengo katika ukusanyaji wa mapato shilingi 10,870,491,197

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ya Maji Zanzibar ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 10,870,491,197 kutokana na vyanzo vyake vya ndani vya mapato. Ukaguzi umebaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Mamlaka ya Maji Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 3,419,798,143.72 ambayo ni sawa na asilimia 31.46 ya makadirio kukiwa na upungufu wa mapato ya makusanyo yenye jumla ya shilingi 7,450,693,053.28 sawa asilimia 68.54 ya makadirio.

Kwa mujibu wa majibu ya uongozi, Mamlaka imeshindwa kufikia malengo ya makusanyo kwa mwaka 2021/2022 kulikosababishwa na kukosekana kwa maji sehemu kubwa ya wateja pamoja na idadi ndogo ya wateja wenye mita, ambapo Mamlaka imepanga kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kuboresha upatikanaji wa maji kupitia miradi ya Maji inayotekelezwa (Exim India na mradi wa Ahueni ya UVIKO 19) sambamba na kuwafungia wateja wa maji mita za kisasa (Smart Meter na Prepaid).

Kutokufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka kama ilivopangwa katika bajeti yake ya mwaka kunapelekea Mamlaka kukosa fedha za Uendeshaji na kupelekea huduma ya maji kutopatikana vizuri kwa wananchi na hatimae kupelekea kutofikiwa kwa malengo ya Mamlaka katika usambazaji wa huduma za maji katika maeneo yote ya mijini na vijijini kwa ufanisi.

### Majibu ya Mamlaka ya ZAWA

Ni kweli Mamlaka ya Maji kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 haikufikia Malengo ya ukusanyaji wa Mapato kulikotokana na sababu zifuatazo:-

1. Mwamko mdogo wa wananchi katika kulipia maji
2. Kutokamilika kwa miradi kwa wakati iliyotegemewa kukamilika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo ilitegemewa kuengeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato.
3. Idadi kubwa ya wateja kutokuwa ma mita na kutumia bei za makisio
4. Kukosekana kwa huduma ya maji kwa baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba.

Aidha ZAWA imeanza kuwaunganishia huduma wananchi walioko katika maeneo yote ambayo miradi imekamilika ili kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato, vilevile jumla mita 45,000 zinategemewa kufungwa kwa wateja waliyopo katika maeneo ya mradi mpya ambapo tunauhakika wa kupata huduma ya maji.

Vipindi vya kuelemisha wananchi juu ya umuhimu wa kulipia maji Pamoja na athari za kutolipia zinaendelea ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na jitihada ambazo Mamlaka ya Maji imechukua, katika kuhakikisha malengo ya ukusanyaji wa Mapato yanafikiwa kwa kuwafungia Wananchi mita 200 katika maeneo mbali mbali kupitia utekelezaji wa mradi wa Exim benki. Kwa msingi huo, Kamati imeionda hoja hii.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji (ZAWA) kufuatilia kwa kina vyanzo vyote vya makusanyo ya mapato ili kuepusha uvujaji wa mapato ya Serikali.

## Hoja nambari 5.1.4.11 Kutokukamilika kwa taratibu za kuwaombea ajira ya kudumu wafanyakazi wa kutwa wa Mamlaka ya Maji Zanzibar.

Kwa mujibu wa kanuni 135 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, hakutakiwi kuwepokwa wafanyakazi wa kutwa katika Utumishi wa Umma na kama kuna ulazima wa kuwepo Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika kuomba kibali kwa Tume ya Utumishi husika na kumjazisha mkataba, ambapo mtumishi wa utumishi wa kutwa hatozidi miezi sita.

Ukaguzi umebaini katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ya Maji Zanzibar ilikuwa na wafanyakazi wa kutwa wanaofikia idadi ya mia mbili na thelathini na tisa (239) Unguja na Pemba waliokuwa wakitumika katika shughuli za ulinzi wa maeneo tofauti ya vyanzo vya maji vya Mamlaka. Wafanyakazi hao wamekuwa wakiitumikia ZAWA kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano (5) na wamekuwa ni chachu katika kuzilinda na kuzitunza rasilimali za Mamlaka ya Maji Zanzibar.

Ukaguzi ulishindwa kupata ithibati ya kuwepo kwa kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kupata idhini. Kukosekana kwa kibali cha utumishi kinachoruhusu uajiri wa wafanyakazi wa kutwa ni kwenda kinyume na Kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2014.

## Majibu ya Mamlaka ya ZAWA

Kutokukamilika kwa taratibu za kuwaombea ajira ya kudumu wafanyakazi wa kutwa wa Mamlaka ya Maji Zanzibar.

Mamlaka ya Maji Zanzibar hadi sasa ina jumla ya wafanyakazi wa kutwa 278 kati ya hao 238 Unguja na 40 Pemba ambao taratibu zao za kufanyiwa ajira ya kudumu hazijakamilika. Hata hivyo kwa mwaka huu wa fedha na ndani ya Robo ya Tatu Mamlaka inatarajia kuanza na awamu ya kwanza ya kuwaajiri vijana 20 kati ya hao kumi na Tano wa Karakana ya Saateni Unguja na watano Pemba. Mpango ni kuendelea kuajiri awamu kwa awamu vijana ambao tayari wanajitolea kila wakati Mamlaka itakapopata kibali cha kuajiri.

Kwa upande wa uajiri wa ulinzi katika vianzio vya maji Mamlaka ya maji inaiomba kamati yako ya kuchunguza na kudhibiti hesabu za Serikali (PAC) itupelekee maombi yetu ili kuagizwa vyombo vya ulinzi kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji na mamlaka ya maji ibaki na kazi yake ya msingi ya kutoa huduma ya Maji.

Ulinzi kutoka JKU una gharama kubwa sana Tsh 1,080,000 kwa kila mlinzi mmoja ambapo kwa kila kituo kina hitaji walinzi wawili, gharama hio ni kubwa kwa Mamlaka kuweza kuhimili kwa vyanzo vyake vyote vya maji. Aidha Mamlaka inatoa huduma kwa jamii na sio Taasisi ya Biashara.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika majadiliano ya hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa Mamlaka tayari imechukua hatua za kuwaombea watumishi hao ajira za kudumu kama majibu yanavyojieleza hapo juu.

Kwa upande wa ajiri za ulinzi katika vianzio vya maji Mamlaka ya Maji imetekeleza ipasavyo agizo la Mhe.Rais la kutaka maeneo yote ya Serikali ambayo yanahitaji ulinzi kutumiwa kikosi cha JKU.

Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini Mamlaka inatumia gharama kubwa kwa ajili ya kuwalipa walinzi hao na kupelekea Mamlaka kushindwa kugharamia gharama hizo.

**Maoni, ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Serikali kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuandaa kikao cha pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kulitafutia ufumbuzi suala la ulipaji wa gharama kubwa za ulinzi katika maeneo ya vianzio vya maji viliopo Unguja na Pemba.

**Hoja nambari 5.1.4.12: Kukosekana kwa hati miliki (title deeds) kwa maeneo**

**yanayotumiwa na Mamlaka ya Maji kwa uzalishaji na usambazaji maji**

Kifungu namba 41 cha Sheria namba 4 ya Maji ya mwaka 2006 kinakataza kufanyika shughuli za ujenzi wa makaazi ya kudumu au ya muda mfupi katika maeneo ya vyanzio vya maji na maeneo ya usambazaji wa maji.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa upande wa Unguja inamiliki maeneo 28 kati ya maeneo hayo ni maeneo 5 tu ndio waliyopata hati miliki (ambayo ni Welezo Matangini, Chuini, Gulioni, Mtoni-base camp na Miembeni Madema) na maeneo 23 bado hawana hati miliki.

Kukosekana kwa hati miliki kwa maeneo ambayo Mamlaka ya Maji Zanzibar inayatumia kwa ajili shughuli za uzalishaji na usambazaji maji kunaweza kupelekea migogoro ya ardhi baina ya Mamlaka ya Maji na wananchi wa maeneo husika, Uvamizi wa Maeneo ambayo yanamilikiwa na Mamlaka ya maji unaofanyanywa na wananchi na pia kunaweza kupelekea hasara ya kulipia fidia mara mbili.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Ni kweli Mamlaka ya Maji bado haina hati miliki katika maeneo ya vianzio vya maji.

Hatua za utekelezaji wa kupata hati miliki zimeanza kwa Mamlaka ya maji Zanzibar kwa kushirikiana na Kamisheni ya ardhi imekamilisha zoezi la utambuzi wa maeneo ya vyanzo vya maji kwa mkoa wa Kaskazini maeneo hayo ni kama yafuatayo:

Visima 54, matangi ya maji 7 na Mapango 8.

Kamisheni ya ardhi ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha repoti za utambuzi wa maeneo ya maji na kuwasilisha kwa ZAWA hatua. zinazofuata katika ukamilishaji wa zoezi la upatikanaji wa hatimiliki.

Baada ya kukamilika utambuzi wa maeneo ya maji katika mkoa wa Kaskazini, Mamlaka ya maji kwa kushirikiana na kamisheni ya ardhi tayari ishaanza zoezi la utambuzi wa maeneo ya maji katika Mkoa wa Kusini na inaendelea na maeneo mengine yaliosalia.

### Uchunguzi WA Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa licha ya Mamlaka ya Maji kuchukua juhudi za kuyaombea maeneo hayo hatimiliki, lakini bado Kamisheni ya Ardhi haijakamilisha zoezi hilo.

Ambapo Mamalaka ya Maji imechukua juhudi za kuandika barua Kamisheni ya ardhi yenye kumbukumbu ZAWA/A.10/8/VOL.1/15 ya tarehe 05/01/2023 kuhusu upatikanaji wa hati miliki za maeneo yote ya vianzo ya maji. Hata hivyo, hadi kamati ya PAC

inakamilisha uchunguzi wake hakuna majibu ya barua kutoka Kamisheni ya Ardhi.Kamati ya PAC imeibakisha hoja hii kwa ajili ya hatua za utekelezaji.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Katika kuitafutia ufumbuzi hoja hii kamati ya PAC imeshauri yafuatayo:-

- Mamlaka ya Maji ihakikisha inaendelea kufuatilia upatikanaji wa hati miliki kwa maeneo yote ya vianzio vya maji ili kuepusha migogoro ya Ardhi na wananchi.
- Kwa upande wa Kamisheni ya Ardhi kuchukua hatua za haraka ili kukamilisha upatikanaji wa hati miliki za Mamlaka katika maeneo ya vianzio vya maji vya Unguja na Pemba.

## Hoja nambari 5.1.4.13: Kuwepo kwa uvamizi wa wananchi katika baadhi ya maeneo ya vyanzo na miundombinu ya usambazaji maji

Mamlaka ya Maji Zanzibar inatumia maeneo mbalimbali kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa huduma za Maji Unguja na Pemba. Baadhi ya maeneo hayo yamepatikana baada ya kulipwa fidia kwa wananchi walioathirika na miradi mbalimbali ya ujenzi wa vyanzo na miundombinu ya usambazaji maji.

Ukaguzi ulifanya ziara katika maeneo mbalimbali ya vyanzo vya maji pamoja na maeneo iliyopita miundombinu ya maji na kubaini kuwepo kwa uvamizi katika maeneo mbali mbali vya vianzio vya maji (Mto-upepo, Welezo, Mwanyanya na mengineyo) ambapo baadhi ya maeneo hayo tayari yalikwishalipwa fidia kwa waathirika ili kupisha miradi ya maji.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya maeneo ya vianzio vya maji na njia za miundombinu ya usambazaji inayotumiwa katika mradi wa maji unaofadhiliwa na Benki ya EXIM ya India haijadhibitiwa na kuhatarisha kutokezea kwa uvamizi katika maeneo hayo kwa siku za usoni. Kuwepo kwa uvamizi wa wananchi katika maeneo ya vyanzo vya maji kunapelekea uharibifu mkubwa wa rasilimali maji na kuathiri upatikanaji wa maji safi na salama

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Kuwepo kwa uvamizi wa wananchi katika baadhi ya maeneo ya vyanzo na miundombinu ya usambazaji maji Mamlaka ya Maji Zanzibar inatumia maeneo mbalimbali kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa huduma za Maji Unguja na Pemba

Idara ya Rasilimali Maji inaendelea na taratibu za kufanya mawasiliano, ufuatiliaji, upimaji na kuwasilisha taarifa za maeneo ya vyanzo vya maji ambazo taaarifa hizo

zitatumika katika zoezi la utambuzi na hatimae kupatiwa hatimiliki kutoka kamisheni ya ardhi. Hadi sasa zoezi hilo limekamilika katika Mkoa wa kaskazini Unguja pamoja na baadhi ya maeneo yaliopitiwa na mradi wa UVIKO-19 kwa upande wa Pemba, na linaendelea kwa maeneo mengine nchini ikiwa na lengo la kukamilisha maeneo yote yenye vyanzo vya maji Unguja na Pemba. Aidha Mamlaka ya Maji kupitia miradi inayotekeleza imeweka kipaumbele ujenzi wa uzio katika maeneo yote yanayo husika na vyanzio vya maji pamoja na ujenzi wa matangi, vile vile kwa maeneo ya zamani ambayo hayana uzio Mamlaka ya Maji imejipangia kujenga uzio kwa kadri ya upatikanaji wa fedha unavyo ruhusu. Baadhi ya visima vya zamani vya Ras el khema tayari vimeanza kujengewa uzio.

**Uchunguzi wa Kamati wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeibakisha hoja hii kutokana bado hatua hazijakamilika za utekelezaji.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji kuhakikisha maeneo yote yenye miundombinu ya vianzio ya Maji yanadhibitiwa na kuhifadhiwa na uvamizi wa maakazi ya wananchi.

## Hoja nambari 5.1.4.14: Dosari zilizobainika katika hesabu za mwisho.

Ukaguzi umebaini kuwa hesabu za mwisho wa mwaka 2021/2022 za Mamlaka zina dosari mbalimbali zilizotokana na kutokuandaliwa vizuri taarifa za fedha za mwisho za Mamlaka pamoja na maelezo ya taarifa za fedha (notes) za hesabu hizo za mwisho wa mwaka.

Baadhi ya dosari zilizobainika ni kama ifuatavyo:-

i) **Kutokuwepo kwa vielelezo vinavyothibitisha kupungua kwa madeni ya wadaiwa (Receivables) wa Mamlaka kwa kiasi cha shilingi 9,887,416,396.69** ambapo madeni ya wadaiwa wa Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2020/2021 walikuwa ni shilingi 34,186,696,182 na kwa mwaka wa fedha 2021/2022 walikuwa ni shilingi 24,299,279,785 na kupelekea kupungua madeni ya wadaiwa kwa shilingi 9,887,416,396.69. Aidha hesabu za Mamlaka za mwisho wa mwaka wa fedha 2021/2022 zimeonyesha kuwa fedha taslim zilizokusanywa na Mamlaka kutokana na vyanzo vyake vya ndani vya mapato ni shilingi

3,426,482,334.

ii) **Kutokuwepo kwa vielelezo vinavyothibitisha kupungua kwa madeni ya wanaoidai Mamlaka (Payables)**

Ukaguzi umebaini kuwa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka wa fedha 2021/2022 hazikuonyesha madeni ya wanaoidai Mamlaka ambao walionyeshwa katika taarifa fedha za mwisho wa mwaka wa fedha uliopita 2020/2021 ambapo ushahidi wa vielelezo vinavyothibitisha kupungua kwa madeni hayo havikupatikana kwa ukaguzi. Kuwepo kwa dosari zilizobainika katika hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka kunapelekea Taarifa za hesabu za Mamlaka za mwisho wa mwaka 2021/2022 kutotoa sura sahihi na halisi.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

I. Madeni hayo yamepungua kutokana na uhakiki uliofanyika wakati wa mabadiliko ya kuhama kutoka mfumo wa SBM2 kuja mfumo wa MAJIS, ambapo baadhi ya taarifa zilifanyiwa marekebisho wakati wa kuhama katika mfumo huo. Aidha ZAWA kwa sasa inaendelea na Utengenezaji wa Credit Policy ili iweze kutoa muongozo zaidi unaohusiana na madeni ya wateja.

II. Mamlaka imekubaliana na ushauri wa Mkaguzi wa kuweka sawa taarifa zake za Madeni kwa watoa huduma na wadai wengine. Aidha mamlaka imechukuwa hatua za kuhakikisha taarifa zote za madeni za mamlka zinawekwa kwenye taarifa za kifedha kama taratibu za kifedha zinavotaka

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii imebaini kuwa licha ya Mamlaka kuchukua juhudi za kuweka taarifa sawa za madeni kwa watoa huduma na wadaiwa wengine kwa kufanya marekebisho ya mfumo ambapo, hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake Mamlaka haijakamilisha Utengenezaji wa Credit Policy ili iweze kutoa muongozo zaidi unaohusiana na madeni ya wateja.

Kutokana na hali hiyo, hoja hii inaendelea kubaki kwa ajili ya kukamilisha hatua za utekelezaji.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Mamalaka ya ZAWA kukamilisha uandaaji wa Sera ya Ulipaji wa Madeni ili kusaidia Mamlaka kuwa na taarifa sahihi za wadaiwa.

## MAMLAKA YA ZAWA PEMBA

## Hoja nambari 5.1.4.15: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 190,372,654.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Maji Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 190,372,654 na watoa huduma mbali mbali kutokana na kupatiwa huduma jambo ambalo linaweza kupelekea Mamlaka ya Maji kutokupewa huduma na hivyo kushindwa kuendesha shughuli zake za kila sikukwa ufanisi na kupelekea uwezekanowa kutokea kwa migogoro isiyokua yalazima baina ya Mamlaka na watoa huduma hao.

Uwepo wa madeni ya muda mrefu katika Taasisi za Umma yanayodaiwa au kudai kutokana na huduma

Iliyotolewa yanatoa kiashiria cha kwamba Afisa Mhasibu wa Taasisi za Umma ameshindwa kusimamia ulipwaji wa madeni hayo kwa wakati kutokana na kukosekana kwa sera au muongozo wa ulipwaji wa madeni kwa wanufaika jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Kwa kupitia hoja hii, ni kweli kuwa Mamlaka ya Maji Tawi la Pemba ina malimbikizo ya madeni ya muda mrefuya watoa huduma mbali mbali, ambayoyanafanya jumla ya fedha za kitanzania Shilingi **190,372,654**. Hatua za kulipwa madeni hayo zimechukuliwa kadiri tunavyopata fedha, awali deni hilo lilikuwa shilingi za kitanzania **205,145,754** na shilingi **14,773,100** zimeshalipwa. Hii ni kutokana na ufinyu wa mapato yanayotokana na mauzo ya maji kulikotokana na uhaba wa upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo mengi ya Zanzibar.

Kwa kuwa Mamlaka inalazimika kurudisha huduma ya maji muda wote,hivyo hulazimika kutafuta vifaa vya kurudisha huduma hiyo kwa njia ya mkopo ili kuenda sambamba na Sera na matarajio ya Serikali ya kuwapatia wananchi huduma ya maji.

Vile vile, ZAWA–Pemba imejipanga kuyalipa madeni ambayo yanadaiwa pamoja na kuweka mikakati yakutokuongezeka kwa madeni kila unapomalizika Mwaka wa Fedha.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Mamlaka kukiri kuwepo kwa deni hilo la muda mrefu, Kamati ya PAC imebaini kuwa watu ambao wanaidai ni watoa huduma ambao wanawapatia Mamlaka vifaa

wakati dharura inapotokea.

Hata hivyo, hadi Kamati inamaliza uchunguzi wake watoa huduma wote ambao Mkaguzi wameorodheshwa katika Ripoti ya Mdhibiti hawajalipwa. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuridhika na utekelezaji wa hoja hii na kupelekea kubakishwa kwa hoja.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Mamlaka Maji Pemba iharakishe ulipaji wa madeni ya watoa huduma ambao Mdhibiti amewaorodhesha ili kuondokana na madeni ya muda mrefu.

## Hoja nambari 5.1.4.16: Utumiaji wa watumishi wa kutwa kinyume na utaratibu Kanuni ya 135 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Zanzibar za mwaka 2014

inaeleza kwamba “Hakutakuwa na utumishi wa kutwa katika utumishi wa Umma, kama kuna ulazima Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika kuomba kibali kwa Tume ya Utumishi

husika na kumjazisha mkataba Utumishi wa mtumishi wa kutwahautozidi miezi sita (6) na atalipwa pale ambapo anamaliza kazi yake kwa siku.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mamlaka ya Maji Pemba imeajiri watumishi wa kutwa ambao huwajazisha mikataba kila baada ya miezi mitatu (3) na kuwalipa mishahara kila mwisho wa mwezi bila ya kuwepo kwa kibali kutoka Tume ya Utumishi Serikalini. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea uwezekano wa kutokea matumizi mabaya ya fedha za Umma na pia kunaweza kupelekeakuajiriwa kwa mtu asiye na maadili mema. Aidha, ni kwenda kinyume na Kanuni ya 135(1)(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Ni kweli kuwa hadi sasa tunatumia wafanyakazi wa kutwa katika kusimamia, kusafisha na kuvitunza vituo na vyanzo vya maji vilivyoko katika maeneo tofauti Unguja na Pemba. Hili linatokana na Mamlaka yaMaji kuwa na uhitaji wa ulinzi wa uhakika katika vyanzo vya majiambavyo ni visima visivyopungua 400.

Hivyo, Mamlaka hulazimika kuwaajiri wafanyakazi kwa mkataba ili kupunguza na kuzuia kabisa uharibifu na upoteaji wa mali za Serikali unaosababishwa na baadhi ya wahalifu katika vianzio vya maji vilivyoko katika maeneo tofauti Ungujana Pemba.

Mamlaka inaiomba Kamati yako ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) itupelekee maombi yetu Serikali Kuu ili kuagiza vyombo vya ulinzi kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji na Mamlaka ibaki na kazi yake ya msingi ya kutoa huduma ya maji.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kweli Mamlaka imetumia watumishi ambao wa mkataba katika maeneo ya visima na vianzio vya maji, sababu kubwa ya kutokufuata utaratibu ni kwamba usimamizi wa visima unahitaji fedha kubwa hasa kwa upande wa vikosi.

Ambapo gharama inayohitajika ni kubwa katika usimamizi wa miradi mikubwa iliyojengwa na Exim Bank.

Baada ya kupata ufafanuzi wa kina juu ya utekelezaji wa hoja hii, Kamati imebaini kuwa Mamlaka ya ZAWA haina uwezo wa kulipa gharama za ulinzi kwa maeneo yaliyobainishwa na Mkaguzi.

Aidha, Kamati imeelezwa kuwa mlinzi mmoja kutoka Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) anahitaji kulipwa shilingi 1,800,000 kwa siku na kwa kila kisima kimoja kinahitaji walizi wawili na Mamlaka na kama inavyofahamika Mamlaka ipo kwa ajili ya kutoa huduma na sio biashara.

Kutokana na maelezo hayo, hoja hii itaendelea kubakia kwa ajili ya utekelezaji Zaidi.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Mamlaka ya ZAWA kukaa pamoja na Serikali kwa ajili ya kupata muafaka katika suala zima la ulipaji wa gaharama za walinzi katika visima na vianzio vya maji.

### Hoja nambari 5.1.4.17: Kutokuwepo kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta shilingi 124,667,100.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba “Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda” Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 124,667,100 zimelipwa na Mamlaka ya Maji kwa Sharif Petrol Station kwa ajili ya ununuzi wa mafutabila ya kuwepo kwa mkataba.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kutokupata huduma iliyo bora na ya uhakika pamoja na uwezekano wakutokea kwa ununuzi holela wa mafuta. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42(2)(b) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Ni kweli wakati wa ukaguzi unafanyika Mamlaka haikua imeingia kwenye mkataba wa ununuzi wa mafuta na mfayabiashara wa mafuta Sharif Petrol Station kwa mwaka wa fedha unaoishia 2021 – 2022.

Mamlaka ya Maji imepokea na kuufanyia kazi ushauri wa mkaguzi ili kwenda sambamba na Sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma nambari 11 ya 2016.

Mamlaka imechukua hatua za kuingia mikataba wa mauziano ya mafuta kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kuendendelea hadi sasa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kabla ya ukaguzi Mamlaka ilikuwa inatumia mikataba ya kawaida bila ya kufuata Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nambari 11 ya mwaka 2016.

Hata hivyo, kwa sasa Mamlaka inafuata kikamilifu taratibu za manunuzi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa msingi huo, Kamati ya PAC imeridhishwa na hatua ambazo Mamlaka imechukua na kupelekea hoja hii kuondolewa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji kuhakikisha inapoingia Mikataba na watoa huduma kufuata Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

## Hoja nambari 5.1.4.18: Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato.

Mamlaka yaMaji Pemba (ZAWA) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi3,868,877,647 kupitia vianzio vyake mbali mbali vya mapato. H adi kufia tarehe 30 Juni, 2022 ZAWA ilikusanya jumla ya shilingi 896,921,098.57 sawa na asilimia 23.18 ya makadirio. Kutokana na kutokufikia kwa lengo lilikosudiwa ukaguzi umebaini

hali hiyo imechangiwa na uwepo mdogo wa uchangiaji wa huduma ya maji kutoka kwa wananchi mbali mbali ambao wanaonufaika na huduma hiyo.hata hivyo imebainika kutokuwepo kwa msisitizo na ufuatiliaji unaofanywa na Mamlaka ya Maji kwa wadaiwa wa huduma ya Maji ambao wanashindwa kufikia Mamlaka ya Maji kulipa madeni yao licha ya kutumiwa ujumbe mfupi kupitia simu za mkononizinazowajuulisha deni halisi wanalodaiwa deni halisi wanalodaiwa na kutakiwa kulipa deni hilo kwa kutumia miamala ya simu si zaidi ya siku 14 au usitishiwa huduma jambo ambalo Mamlaka ya Maji wanashindwa kulitekeleza.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Kama ilivyo hoja hapo juu, ni kweli kwa mwaka wa fedha 2021 - 2022 Mamlaka ya Maji haikuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa asilimia Mia Moja kama ilivyokadiria kutokana na uhaba wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa kipindi hicho. Hivyo sasa, Mamlaka imeboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama pamoja na kuboresha mifumo ya ulipaji wa huduma ya maji kwa wanaopata huduma hio. Mfano kutumia wakala wa fedha, Matumizi ya POS, Benki, mifumo ya ukusanyaji kupitia simu ya TEHEMA kupelekea Ankara kwa jitihada hizi Mamlaka inaamini kwamba zitapelekea kuongezeka kwa mapato kufikia lengo iliyojipangia

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati katika kufanya uchunguzi wake imebaini kuwa sababu kuu ya Mamlaka kutokufikia malengo ya makusanyo ya mapato, kutokana na kutokuwepo kwa uhalisia wa ufungaji wa mita na malipo ya yanayolipwa na wateja. Hivyo, hoja hii itaendelea kubakia.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji kuhakikisha wanaisimamia ipasavyo mifumo wa TEHAMA wanayotumia ili lengo la ukusanyaji wa mapato ya Serikali kufukiwa.

## Hoja nambari 5.1.4.19: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 1,737,780,511.18

Mamlaka ya Maji Pemba ina jukumu kubwa la kuhakikisha linatoa huduma ya maji safi na salama sehemu mbali mbali katika jamii ya Zanzibar, kutokana na huduma inayotolewa wananchi wa Zanzibar hutakiwa kuchangia shilingi 4000 kwa mwezi kwa wale ambao hawakufungiwa mitaza maji.

Aidha kwa wale waliofungiwa mita hizo watapaswa kuchangia huduma hiyo kwa kadri ya matumizi yatakavyofanywa na muhusika. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ukaguzi umebaini uwepo wa malimbikizo ya madeni ya shilingi 1,737,780,511.18 yanayodaiwa kutoka kwa wananchi katika Wilaya mbali mbali kisiwani Pemba jamboambalo linaweza kudumaza malengoyaliyopangwa na hatimae kukosekana kwa huduma kama hiyo kwa baadhi ya maeneo mengine.

#### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Ni kweli Mamlaka ya Maji Pemba inadai kiasi kikubwa cha fedha ambacho ni madeni ya muda mrefuyatokanayo na utumiaji wa huduma yamaji kwa wateja wake. Sambamba na hilo, Mamlaka ya Maji imechukua jitihada za lazima ili kuhakikisha kuwa inafanikiwa kukusanya fedha zitokanazo na utumiaji wa huduma ya maji kama ilivyojipangia kutoka kwawateja wake tofauti.

Miongoni mwa jitihada ambazoMamlaka inachukua ili kuhakikishamalipo ya huduma ya maji inafanikiwa ni pamoja na kutoa Ankara kwa wateja wake wote kwa kila mwezi.

#### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini Mamlaka itachukua muda mrefu wa kumaliza madeni wanayodai wateja kutokana na kutokuwepo kwa uwelewa wa kutosha wa wananchi wa uchangia wa huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama. Hivyo, Kamati imeibakisha hoja.

#### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Uongozi wa Mamlaka kuendelea kutoa Elimu kwa Wananchi juu ya umuhimu wa kulipia huduma ya maji kila mwisho wa mwezi.

## 5.1.6 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA - ZANZIBAR

### Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 2,147,500,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi zakawaida. Aidha, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilikadiriwa kukusanyajumla ya shilingi 444,420,000 kutoka vyanzo vyake

vya ndani vya mapato.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi 671,364,005 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 31.26, kukiwa na upungufu wa shilingi 1,476,135,995 sawa na asilimia 68.74 ya makadirio.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 193,506,500 kutoka vyanzo vyake vya ndani vya mapato sawa na asilimia 43.54 ya makadirio kukiwa na upungufu wa shilingi 250,913,500 sawa na asilimia 56.46.

### Majibu na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikupatiwa majibu kuhusiana na hoja ya taarifa ya Mapato ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(3) ya Kadumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020) kwamba majibu ya Kamati yawasilishwe kwa Kamati siku mbili kabla ya kikao husika. Hata hivyo, katika majadiliano ya hoja hii, Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuwepo kwa maambukizo ya Uviko 19 kumepelekea kupungua kwa kiasi kikubwa mapato ya Mamlaka hasa ukizingatia kwamba chanzo kikuu ambacho Mamlaka inakitegemea katika kujipatia mapato hayo ni usajili wa wafanyabiashara ambao walishindwa kujisajili kwa vile biashara haikuwa ikifanyika ipasavyo.

Aidha, Kamati imegundua kwamba Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango iliipangia makusanyo Mamlaka kimazoea kwa kuwawekea kiwango kikubwa cha ukusanyaji mapato kinyume na uwezo au uhalisia wa Mamlaka. Kutokana na hilo, hatimae Mamlaka iliweza kukusanya jumla ya shilingi 193,506,500 badala ya 2,147,500,000 ya makadirio sawa na asilimia 43.54 kukiwa na upungufu wa shilingi 250,913,500 sawa na asilimia 56.46.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe inawapangia Mamlaka kiwango sahihi cha makusanyo kulingana na hali halisi ya uwezo wa Mamlaka hiyo.

## Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,147,500,000 kwa ajili ya kazi za

kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 669,474,893.37 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 31.17 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 1,478,025,106.63 sawa na asilimia 68.83 ya makadirio.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Mamlaka imetekeleza shughuli zake kwa kupitia programu kuu mbili ambazo zimetumia jumla ya TZS 174,110,889 /=. Programu hizo ni;-

a) Programu Kuu 1; Mipango Utumishi na Uendeshaji imetumia TZS 162,170,782 /= Kwa kutekeleza shughuli mbali mbali zikiwemo:-

   i. Mafunzo ya muda mfupi,
   ii. Kushiriki katika uzinduzi wa mfumo wa Manunuzi (e-procument),
   iii. Mafunzo ya muda mrefu,
   iv. Kufanya ukaguzi wa ndani wa Mamlaka,
   v. Kikao cha Bodi ya zabuni, na
   vi. Kuimarisha huduma za uendeshaji. Utekelezaji halisi wa shughuli hizo kama inavyoonekana katika kiambatanisho nambari; 1

b) Programu kuu 2: Kusimamia Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma imetumia TZS 11,940,107/= katika kutekeleza shughuli zifuatazo:-

   i. Kufanya ukaguzi kwa Taasisi nunuzi 30 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekaguliwa kwa ajili ya kuhakikisha zinakidhi matakwa ya kisheria (compliance) na thamani halisi ya fedha katika ununuzi (Value for money in Procurement), Taasisi hizo zilizokagliwa ni Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Ujenzi, Mawsiliano na Uchunguzi, Wizara ya Maji na Nishati, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Shirika la Utangazaji (ZBC), Chuo Cha Taifa (SUZA), Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Kikosi

cha kuzuia Magendo (KMKM), Shirika la Bima, Baraza la Wawakilishi, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi, Mamlaka ya Usafiri Baharini, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA), Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, Halimashauri Wilaya ya Micheweni, Taasisi ya Viwango (ZBS), Baraza la Mji Mkoani, Shirika la umeme, Benki ya watu wa Zanziba (PBZ), Mamlaka ya udhibiti wa huduma za maji na nishati(ZURA), Wakala wa usajili wa matukio ya kijamii. Wakala wa maabara ya mkemia Mkuu wa Serikali, kikosi cha valantia (KVZ), Sekta ya Afya, Sekta ya Elimu, 3, Sekta ya maji, Sekta ya Nishati.

ii. Kuchunguza miamala ya Ununuzi juu ya ukiukwaji wa taratibu za ununuzi kwa Taasisi mbili za umma ambazo ni Taasisi ya Viwango, Zanzibar (ZBS) na Chuo cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA) ambapo uchunguzi huo umebaini ukiukwaji mkubwa wa sharia ya ununuzi. Utekelezaji halisi wa shughuli hizo kama inavyoonekana katika kiambatanisho nambari; 1

iii. Kufanya ukaguzi wa manunuzi katika miradi mbali mbali iliyopatiwa fedha za ahuweni ya UVIKO19 juu ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, miradi hiyo ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Afya, Aidha kwa upande wa Pemba ukaguzi umefanya kwa mikao miwili ambapo Mkoa wa kusini ulitekelea ujenzi wa vituo vya wajasiria mali katika eneo la kipitacho na Michakaeni na Mkoa wa kuskazini ulitekeleza ujenzi wa vituo vya wajasiria mali katika eneo la Kifumbikai na Tumbe

iv. Kupewa mafunzo kwa taasisi 12 za ununuzi juu ya Sheria na Kanuni ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na miongozo ili kuimarisha utendaji katika taasisi hizo,

v. Mamlaka imepokea mipango ya manunuzi ya mwaka 90 kwa Taasisis nunuzi kati ya 93 ya taasisi za umma, taasisi 3 hazikuwasilisha mipango yao ya ununuzi,

vi. Kupokea malalamiko ya watoa huduma jumla ya malalamiko mawili (2) yalipokelewa kutoka kwa wazabuni kwa kutoridhika na hatua za zabuni kutoka Chuo cha Mafunzo na Shirika la Meli Zanzibar. Malalamiko hayo yalifanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi kwa pande zote zinazohusika kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma,

vii. Wafanyakazi wane (4) wa Mamlaka wamefaidika kupata utaalamu wa

uzoefu wa kiutendaji kupitia mashirikiano baina ya Mamlaka PPRA na PSPTB Za Tanzania Bara: na

viii. Kupitia Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma nambari 11 ya 2016 ambapo Mamlaka imeanza na kazi ya kukusanya maoni ya rasimu ya sheria mpya ya ununuzi.

**Uchunguzi na Maoni ya Kamati ya PAC**

Kutokana na upungufu wa makusanyo kwa Taasisi zote za Serikali kulikosababishwa na uwepo wa maambukizi ya Uviko 19, Mamlaka imepelekea kupata kiwango kidogo cha fedha za matumizi mengineyo na kushindwa kutekeleza shughuli ilizojipangia. Mamlaka imefanikiwa kupata jumla ya shilingi 669,474,893.37 kati ya Bilioni 2,147,500,000 sawa na asilimia 31.17 ya makadirio kukiwa na upungufu wa shilingi bilioni 1,478,025,106.62 sawa na asilimia 68.83 ya makadirio.

## Hoja nambari 5.1.6.1: Kutokuwasilishwa kwa Ripoti ya mwaka ya Utekelezaji

Kwa mujibu wa kifungu nambari 21(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali zaUmma ya mwaka 2016, inaeleza kwamba Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibarinalazimika ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha na kuwasilisha Ripoti ya mwaka ya Utekelezaji kwa Waziri anayehusika na mambo ya Fedha, ripoti ambayo itakayojumuisha:-

- Taarifa ya fedha na mpango wa usimamizi.
- Tathmini ya uendeshaji wa Mamlaka na Taasisi zinazojihusisha na ununuzi na uondoshaji.
- Taarifa nyengine yoyote kama Bodi itakavyoelekeza n.k.

Aidha kwa mujibu wa kifungu cha 21(2) cha sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar inalazimika ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa ya tathmini ya uendeshaji wa Mamlaka na taasisi zinazojihusishana ununuzi na uondoshaji.

Ukaguzi umebaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma haijawasilisha ripoti hizo kama zinavyotakiwa na Sheria. Kukokuwasilishwa kwa ripoti za utekelezaji za Mamlaka kwa Taasisi husika kunapelekea

kukosekanauwazi na uwajibikaji katika Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kuwa wanawasilisha ripoti zote zilizotajwa katika Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma kwa ngazi zinazohusika ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Mamlaka haikuwasilisha ripoti hizo kutokana na kutokuwepo kwa muda mrefu kwa Bodi ya wakurugenzi kama chombo kikuu cha kuthibitisha ripoti hizo ili baadae zipelekwe katika hatua za juu Serikalini. Bodi mpya imeshazithibitisha ripoti husika na zimewasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri tayari kwa kupelekwa Serikalini.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anafanya ukaguzi wake, Ripoti hiyo ilikuwa haijawasilishwa kwa Waziri anayehusika na Fedha kama inavyoelekezwa na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, namba 11 ya 2016. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua sababu ya kutowasisilshwa kwake na kuelezwa kwamba Bodi ya Ushauri ilikuwa memaliza muda wake ambapo hivi sasa Bodi hiyo imeshaundwa. Aidha, Kamati imejiridhisha kwamba hoja hiyo imetekelezwa kikamilifu kupitia barua nambari CEA.15/150/01/2 ya tarehe 31/7/2023 iliyothibitisha kuwasilishwa kwake sehemu husika. Kwa mnasaba huo, hoja hiyo inaondolewa.

## Hoja nambari 5.1.6.2: Hoja nambari Kutovikatia Bima Vyombo vya Moto

Kwa mujibu wa kanuni 124(5) ya kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014, Mkuu wa Taasisi anatakiwa kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri vya Serikali vilivyo chini ya mamlaka yake vinapasishwana kukatiwa bima.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wa mali za umma Zanzibar inamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri ikiwemo gari na vyombo vya maringi mawili ambapo baadhi ya vyombo hivyo havijakatiwa bima.

Kutokatiwa bima kwa vyombo vya usafiri vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar kunapelekea kutofikiwa kwa malengo ya Serikali kupitia Uanzishwaji wa Shirika la Bima. Hii inatokana na kutopatikana kwa fedha za mapato zinazoliwezesha Shirika kujiendesha wenyewe bila ya kutegemea ruzuku kutoka

Serikalini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar uhakikishe kwamba kuna kuwepo na udhibiti mzuri wa usimamizi wa vyombo vya moto ikiwemo kuvikatia bima ili kuepusha kujitokeza kwa gharama za zisizokuwa za lazima ambazo zitaitia hasara Serikali kwa kukarabati au kutengeneza vyombo vya moto vitakapopata ajali kwa kutumia fedha zaSerikali. Mchanganuo wa Vyombo hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 50: Vyombo vya moto ambavyo havijakatiwa bima

| Nam. | Nambari ya chombo | Nambari ya Mashine | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | SMZ 999A | 303-04825212-19 | Gari |
| 2. | SMZ 1815C | PFZWKD58014 | Honda |
| 3. | SMZ 1814C | MD625AF77K1K01209 CHASIS | Honda |
| 4. | SMZ 1560C | E12F3150473 | Vespa |
| 5. | SMZ 1558C | E12F3150383 | Vespa |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Vyombo hivyo havikukatiwa bima kutokana na ukosefu wa fedha. Mamlaka imeweka kipaumbele cha mwanzo ni kuvikatia bima vyombo hivyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Malipo ya bima ya vyombo hivyo yameshafanywa tunasubiri kupatiwa bima hizo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa ni kweli vyombo vilivyoainishwa na Mkaguzi vilikuwa havijakatiwa bima. Hata hivyo, tayari vyombo hivyo vimeshakatiwa bima licha ya utekelezaji wake kuchelewa ambapo Honda na Vespa hizo zimekatiwa bima tarehe 22 Novemba, 2023. Aidha, gari nambari SMZ 999A imehaulishwa na kupelekwa Ofisi ya Rais Ikulu kwa mujibu wa utaratibu. Kamati imeridhika na majibu yaliyowasilishwa.

### Hoja nambari 5.1.6.3: Kasoro katika Usimamizi wa madeni ya wadaiwa wa Mamlaka, shilingi59,190,000

Kwa mujibu wa taarifa ya fedha ya Mamlaka ya mwaka wa fedha 2021/2022, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa mali za umma Zanzibar imeonyesha kuwa inazidai taasisi mbalimbali za Serikali jumla ya shilingi 59,190,000 ikiwa ni madeni yanayotokana na tozo za huduma zilizotolewa na Mamlaka kwa taasisi hizo.

Kwa kupitia taarifa zilizopatikana kutoka katika kitengo cha hesabu cha Mamlaka, ukaguzi umebaini kuwa madeni ya wadaiwa ya Mamlaka yamekuwa yakiongezeka kutokana na wahusika kutokulipa madeni yao. Aidha, ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka haijachukua jitihada za kutosha katika kufuatiliamadeni inayodai kwa taasisi za Serikali.

Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa madeni ambayo Mamlaka inadai kutoka kwa taasisi nyengine kunapelekea uwepo wa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ambayo hayatoweza kulipika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuandaa sera ya usimamizi wa madeni kwa lengo la kuwana utaratibu mzuri wa usimamizi wa madeni inayodai Taasisi za Serikali ili madeni hayo yaweze kulipwa kwa wakati. Mchanganuo wa taasisi zinazodaiwa na Mamlaka ni kama inavyoonekana katikajadweli lifuatalo:-

### Jadweli Nambari 51: Taasisi ambazo hazijalipa ada za Matangazo

| Nam. | Jina la Taasisi | Deni linalodaiwa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Mtakwimu Mkuu wa Serikali | 360,000.00 |
| 2. | Wizara ya Habari Utamaduni na Mambo ya Kale | 720,000.00 |
| 3. | Wizara ya Afya | 720,000.00 |
| 4. | Kamishna wa Utalii | 360,000.00 |
| 5. | Tume ya Kurekebisha Sheria | 360,000.00 |
| 6. | Afisi ya Makamu wa Pili | 720,000.00 |
| 7. | Shirika la Meli | 720,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Wizara ya Kilimo Mali Asili Mifugo na Uvuvi | 360,000.00 |
| 9. | Wizara ya Vijana Utamaduni Sanaa na Michezo | 360,000.00 |
| 10. | Halmashauri Wilaya ya Kaskazini A | 360,000.00 |
| 11. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini | 720,000.00 |
| 12. | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 360,000.00 |
| 13. | Tume ya Mipango | 360,000.00 |
| 14. | Wizara ya Ardhi Nyumba na Nishati | 720,000.00 |
| 15. | Mkoa wa Kusini | 720,000.00 |
| 16. | Mahakama Kusini | 360,000.00 |
| 17. | Afisi ya Raisi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi | 720,000.00 |
| 18. | Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wanawake na Watoto | 360,000.00 |
| 19. | Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 500,000.00 |
| 20. | Tume ya Kurekebisha Sheria | 400,000.00 |
| Nam. | Jina la Taasisi | Deni linalodaiwa (Tshs.) |
| 21. | PBZ | 1,250,000 |
| 22. | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 750,000.00 |
| 23. | Zanzibar Marine Authority | 750,000.00 |
| 24. | UMC | 750,000.00 |
| 25. | JKU | 500,000.00 |
| 26. | Kamisheni ya Utumishi wa Umma | 750,000.00 |
| 27. | Baraza la Mji Kati | 750,000.00 |
| 28. | Shirika la Utangazaji | 400,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 29. | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 200,000.00 |
| 30. | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 800,000.00 |
| 31. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Mali na Nishati | 500,000.00 |
| 32. | Bodi ya Huduma za Maktaba | 750,000.00 |
| 33. | Kamisheni ya Utalii | 750,000.00 |
| 34. | Mamlaka ya Mafunzo ya Amali | 750,000.00 |
| 35. | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 200,000.00 |
| 36. | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 600,000.00 |
| 37. | Shirika la Utangazaji | 200,000.00 |
| **Jumla** | | **21,630,000.00** |

**Jadweli Nambari 52: Taasisi zinazodaiwa deni la Mafunzo**

| Nam. | Jina la Taasisi | Kiasi Kinachodaiwa(Tshs.) | |
|---|---|---|---|
| | | Kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 | Kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 |
| 1. | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 2. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 3. | Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 4. | Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 5. | Baraza la Kiswahili | 300,000.00 | 0 |
| 6. | Baraza la Manispaa Magharibi "B" | 300,000.00 | 0 |
| 7. | Baraza la Manispaa Mjini | 600,000.00 | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | Baraza la Sanaa Sensa ya Filamu | 300,000.00 | 0 |
| 9. | Bodi ya Huduma za Maktaba | 300,000.00 | 0 |
| 10. | Bodi ya Mapato | 1,080,000.00 | 1,080,000.00 |
| 11. | Chief Government Chemist Laboratory Agency (Cgcla) | 300,000.00 | 0 |
| 12. | Chuo Cha Mafunzo Zanzibar | 600,000.00 | 0 |
| 13. | Chuo cha Utawala wa Umma | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 14. | Department of Information Services | 300,000.00 | 0 |
| 15. | E-Government Agency | 300,000.00 | 0 |
| 16. | E-Government Agency | 300,000.00 | 0 |
| 17. | Halmashauri Wilaya ya Kaskazini A | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 18. | Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 19. | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini - Unguja | 300,000.00 | 0 |
| 20. | High Court of Zanzibar | 900,000.00 | 0 |
| 21. | Idara ya Michezo | 600,000.00 | 0 |
| 22. | Kamisheni ya Utalii | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 23. | Kamisheni ya utalii | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 24. | Kamisheni ya Utumishi Wa Umma | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 25. | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | 300,000.00 | 0 |
| 26. | Karume Institute of Science and Technology | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 27. | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 600,000.00 | 0 |
| 28. | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 29. | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 30. | Mahkama | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 31. | Ministry of Blue Economy and Fisheries | 900,000.00 | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 32. | Ministry of Labour | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 33. | Ministry of Land and Housing Development | 300,000.00 | 0 |
| 34. | Ministry of Trade and Industrial Development | 300,000.00 | 0 |
| 35. | Ministry of Water Energy and Minerals | 600,000.00 | 0 |
| 36. | Mkoa wa Kusini | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 37. | Mkurugenzi wa Mashtaka | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 38. | Mtakwimu Mkuu wa Serikali | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 39. | North B District Council | 600,000.00 | 0 |
| 40. | Office of The Director of Public Prosecutions Zanzibar | 600,000.00 | 0 |
| 41. | Afisi ya Makamo wa Pili Wa Rais | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 42. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 43. | President Office - Regional Administration, Local Goverment and Special Department | 300,000.00 | 0 |
| 44. | Public Service Commission | 300,000.00 | 0 |
| 45. | School of Agriculture – Suza | 300,000.00 | 0 |
| 46. | School of Business – Suza | 300,000.00 | 0 |
| 47. | The Institute of Public Administration (Ipa) | 300,000.00 | 0 |
| 48. | The Institute of Public Administration (Ipa) | 300,000.00 | 0 |
| 49. | The Second Vice President’s Office | 300,000.00 | 0 |
| 50. | Tume ya Kurekebisha Sheria | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 51. | Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 52. | Tume ya Mipango | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 53. | Tume ya Ushindani wa Biashara | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 54. | Tume ya Utangazaji Zanzibar | 300,000.00 | 0 |
| 55. | Tume ya Utumishi Serikalini | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 56. | Unit of Smugling Unit – KMKM | 600,000.00 | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 57. | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 58. | Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo | 300,000.00 | 0 |
| 59. | Wizara ya Afya | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 60. | Wizara ya Afya | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 61. | Wizara ya Ardhi Nyumba na Nishati | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 62. | Wizara ya Habari Utamaduni na Mambo ya Kale | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 63. | Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wanawake na Watoto | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 64. | Wizara ya Kilimo,Mali Asili,Mifugo na Uvuvi | 720,000.00 | 720,000.00 |
| 65. | Wizara ya Vijana,Utamaduni,Sanaa na Michezo | 360,000.00 | 360,000.00 |
| 66. | Zanzibar Aids Commission (Zac) | 300,000.00 | 0 |
| 67. | Zanzibar Airport Authority (Zaa) | 600,000.00 | 0 |
| 68. | Zanzibar Anti Corruption & Economic Authority | 300,000.00 | 0 |
| 69. | Zanzibar Broadcasting Corporation (Zbc) | 600,000.00 | 0 |
| 70. | Zanzibar Buildings Agency | 300,000.00 | 0 |
| 71. | Zanzibar Commission For Tourism | 600,000.00 | 0 |
| 72. | Zanzibar Drugs Control and Enforcement Authority | 300,000.00 | 0 |
| 73. | Zanzibar Electoral Commission | 600,000.00 | 0 |
| 74. | Zanzibar Fisheries Company | 300,000.00 | 0 |
| 75. | Zanzibar Higher Education Loans Board | 300,000.00 | 0 |
| 76. | Zanzibar Ict Infrastructure Agency (ZICTIA) | 300,000.00 | 0 |
| 77. | Zanzibar Investment Promotion Authority | 900,000.00 | 0 |
| 78. | Zanzibar Labour Commission | 300,000.00 | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 79. | Zanzibar Maritine Authority – ZMA | 600,000.00 | 0 |
| 80. | Zanzibar Multiplex Company – ZMUX | 300,000.00 | 0 |
| 81. | Zanzibar Public Leaders Ethics Commission | 300,000.00 | 0 |
| 82. | Zanzibar Road Agency – Pemba | 600,000.00 | 0 |
| 83. | Zanzibar Shipco Corporation | 300,000.00 | 0 |
| 84. | Zanzibar Youth Council | 300,000.00 | 0 |
| | **Jumla** | **37,560,000** | **16,560,000** |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Mamlaka imechukua hatua kadhaa za kuwataka wadaiwa kulipa madeni hayo. Baada ya uhakiki imebainika kwamba baadhi ya Tasisi zimelipa madeni hayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kati ya madeni yaliyoorodheshwa na Mkaguzi, kuna Taasisi 20 tayari zimeshalipa madeni yao sawa na shilingi 7,920,000 na Taasisi 99 bado hazijalipa. Hivyo, hadi Kamati inakamilisha kazi yake ya ukaguzi jumla ya shilingi 49,230,000 zinaendelea kudaiwa na Mamlaka ambapo shilingi 29,640,000 ni dei linalotokana na mafunzo na shilingi 19,590,000 ni deni linalodaiwa katika Taasisi 35 linalotokana na huduma ya matangazo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe inaandaa utaratibu maalum utakaowezesha madeni yanayodaiwa yanalipwa kwa Mamlaka ikiwemo kuzikata fedha hizo kupitia fedha zao za matumizi mengineyo.
2. Mamlaka iandae utaratibu rafiki ambao utahakikisha Taasisi zinalipa madeni yao kabla ya kupatiwa huduma ili kuepusha mrundikano wa madeni.

## MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA - PEMBA

## Hoja nambari 5.1.6.4: Kukaimu nafasi kinyume na utaratibu

Kwa mujibu wa kanuni ya 20(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 inaeleza kuwa "Hakutokuwa na nafasi ya kukaimu ya zaidi ya muda wa miezi kumi na

mbili (12) mfululizo kutoka tarehe ya uteuzi wa kukaimu isipokuwa muhusika atathibitishwa katika wadhifa huo au mwenye dhamana atakaporejea”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mratibu wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Pemba aliteuliwa kukaimu nafasi ya Mratibu kuanzia tarehe 22/07/2019 kwa barua yenye kumbukumbu nambari AC.161/383/01/70 ya tarehe 22/07/2019.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika mtajwa hapo juu alikaimishwa kuitumikia nafasi hiyo kwa zaidi ya miezi arobaini (40) bila ya kuthibitishwa jambo ambalo ni kinyume na kanuni ya Utumishi wa Umma kama ilivyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kuhakikisha unafuatilia taratibu za kuthibitishwa katika nafasi anayoendelea kukaimu ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka haikuwasilisha ripoti hizo kutokana na kutokuwepo kwa muda mrefu kwa Bodi ya wakurugenzi kama chombo kikuu cha kuthibitisha ripoti hizo ili baadae zipelekwe katika hatua za juu Serikalini. Bodi mpya imeshazithibitisha ripoti husika na zimewasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri tayari kwa kupelekwa Serikalini.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

1. Licha ya Watendaji wa Mamlaka kukubaliana na hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua shida ilikuwa nini hata Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wasiteuliwe, na Mamlaka ilichukua juhudi gani kuhakikisha Wajumbe hao wanateuliwa na Mheshimiwa Waziri na kuelezwa kwamba kulipita Mawaziri wawili lakini wote walishindwa kuteua Wajumbe wa Bodi licha ya juhudi za kuwaandikia barua ya ukumbusho ya tarehe 5 Machi, 2021 yenye kumbukumbu nambari MUUMU.CAB.300/450/01/8 ambapo Aprili, 2023 Mwenyekiti wa Bodi aliteuliwa na kufuatia uteuzi wa Wajumbe wake. Hivyo hivi sasa Bodi na Wajumbe wake wote wapo.
2. Kuhusu Afisa Mratibu kukaimu kinyume na utaratibu, Kamati imebaini ni kweli nafasi hiyo ilikaimiwa kwa zaidi ya mwaka mmoja lakini hivi sasa Mratibu huyo ameshathibitishwa kuwa Mkuu wa Mipango lakini pia anafanya na kazi za uratibu ambapo uteuzi wake ulichelewa kutokana na kutokuwepo kwa Bodi lakini Mamlaka ilichukua juhudi ya kufuatilia Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma na kuelezwa waendelee kusubiri jambo ambalo ni kinyume na utaratibu kwani muda

mwingi umepita na muhusika aliendelea kukosa stahiki zake.

3. Kamati imesisitiza kwamba Mamlaka ijikite zaidi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Utumishi Wala wasiyape nafasi masuala kama hayo kutoka kwani iwapo kutatokea changamoto linaweza kumuingiza muhusika katika matatizo au kushindwa kumpata mtu wa kukuajibisha katika kipindi chote cha kutoteuliwa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Mamlaka uhakikishe unatekeleza majukumu yake kwa kufuata taratibu za Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma ili kuepukana na uwepo wa hoja zisizokuwa za msingi.

## Hoja nambari 5.1.6.5: Kutokukamilika kwa utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka

Kwa mujibu wa kifungu cha 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 ambacho kinaitaka taasisi kupanga mipango yake ya ununuzi na uuzaji katika hali ya kueleweka.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Pemba imeshindwa kutekeleza mpango kazi wa mwaka kutokana na kuingiziwa kiasi kidogo cha fedha ambacho ni sawa na asilimia 13 ya makadirio waliojipangia kwa mwaka jambo ambalo limeathiri utekelezaji wa shughuli walizojipangia na kupelekea kutokufikiwa malengo ya upatikanaji wa huduma na shughuli mbalimbali za Mamlaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha unazipatia bajeti za kutosha taasisi za umma kwa mujibu wa makadirio yaliyopangwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi ili Taasisi hizo ziweze kufikia malengo waliyojipangia.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Vyombo hivyo havikukatiwa bima kutokana na ukosefu wa fedha. Mamlaka imeweka kipaumbele cha mwanzo ni kuvikatia bima vyombo hivyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, na Vyombo hivyo tayari vimeshakatiwa bima

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Kamati kupatiwa sababu ya kutokukamilika utekelezaji wa mpango kazi, Kamati ilitaka kujua ni athari gani ilijitokeza kutokana na uhaba wa fedha na kuelezwa

kwamba kulikuwa na Miradi ya ununuzi michache mno iliyokaguliwa, vifaa vya Ofisi havikuweza kununuliwa pamoja na mafunzo kwa Watendaji hayakuweza kutekelezwa. Kamati pia ilibaini kwa kipindi cha mwaka 2021/2022, Mamlaka ilipata fedha kidogo mno ambapo walipamga kupata shilingi 200,000,000/- kwa upande wa Pemba lakini walipata 25,000,000/- ambazo hata robo hazijatimia.

## Hoja nambari 5.1.6.6: Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Pemba ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 20,000,000 kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Mamlaka imeweza kukusanya jumla ya shilingi 11,875,000 ambazo ni sawa na asilimia 59 ya makadirio.

Kutokana na kutokufikiwa kwa lengo lililokusudiwa ukaguzi umebaini hali hiyo imechangiwa na uwepo wa muamko mdogo wa wafanyabiashara kujisajili katika Mamlaka ya Ununuzi jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa mapato ya usajili pamoja na kutokupatiwa elimu ya kutosha kwa Maafisa Ugavi juu ya umuhimu wa kufanya biashara na watoa huduma waliosajiliwa kisheria jambo ambalo litaipatia mapato Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Pemba kuhakikisha unaongeza bidii ya kuwashajihisha na kuwaelimisha watoa huduma watakaofanya kazi na Serikali kuweza kujisajili kwa lengo la kupunguza upotevu wa mapato yatokanayo na ada za usajili.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka kwa upande wa Pemba haikufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kutokana na kutegemea Chanzo cha mapato cha usajili wa watoa huduma ambapo hawakujisajili kwa wingi kwa mwaka huo na hivyo kusababisha kupungua mapato ya serikali. Mafunzo ya uhamasishaji watoa huduma kujisajili yanaendelea kutolewa kwa wingi ili watoa huduma wajisajili kwa lengo la kuongeza mapato ya serikali.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Mbali na sababu iliyotolewa ya kutofikia lengo. Hata hivyo Kamati ilitaka kujua kwa mwaka husika hakukuwepo vyanzo vyengine vya mapato na kuelezwa kulikuwa na chanzo kimoja tu cha mapato usajili wa Watoa huduma za ununuzi isipokuwa hivi sasa wana vyanzo vingi. Sambamba na hilo, Kamati ilitaka kujua Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilipanga kusajili Watoa huduma wangapi na walisajili wangapi ambapo

Kamati ilijibiwa kwamba majibu yatawasilishwa watakapokutana na Mamlaka hiyo Unguja lakini hadi Kamati inakamilisha kazi zake (Unguja) haikuweza kupatiwa.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Mamlaka iwe makini na iongeze juhudi kufuatilia usajili wa Watoa huduma ambao wamemaliza muda wa usajili kwani Kamati imegundua kuna Taasisi nyingi za Serikali ambazo huwatumia Watoa huduma waliomaliza usajili kufanya baadhi ya kazi zao kutokana na umaarufu na uzoefu wao kitendo ambacho huikosesha Serikali mapato.

## 5.1.9 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI

## Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 1,267,800,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida. Aidha Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 2,534,085,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2022 Mamlaka ilipokea jumla ya shilingi 1,217,289,331 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 96.02 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 50,510,669 sawa asilimia 3.98 ya makadirio. Aidha Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 2,914,802,605.00 kutoka vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimia 115.02 ya makadirio, kukiwa na ongezeko la 380,717,605 sawa na asilimia 15.02 ya makadirio.

**Majibu na Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani haijawasilisha majibu ya Hoja ya taarifa ya Mapato siku mbili kabla ya Kamati kukutana na Mamlaka hiyo kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 97(3) ya Bazara la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua vyanzo inavyovitumia Mamlaka kupata mapato yake na kuelezwa kwamba 'driving test', ukaguzi wa magari, malipo ya kadi za njia, lana pamoja na leseni za wageni ndio vyanzo vikuu vya Mamlaka.

Kuhusiana na ongezeko la mapato kwa asilimia 15, Mamlaka iliieleza Kamati kuwa ongezeko hilo lilitokana na Mamlaka kutekeleza mikakati maalum ikiwemo ya kufanya 'operation' za mara kwa mara barabarani za kukagua gari zilizokuwa hazijapasishwa pamoja na kuanza kutoza faini ya adhabu ya makosa ya papo kwa papo mwishoni mwa mwaka husika (April, 2022) ambazo ziliingizia Mamlaka jumla ya shilingi milioni 130.

Zoezi hilo lilifanyika kwa mafanikio makubwa kwani hakukuwa na ongezeko lolote la faini au adhabu hizo.

Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa katika utekelezaji wa zoezi hilo kulikuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Madereva hususan wa Daladala kulikotokana na kuwepo faini kubwa kwa makosa yaliyokuwa yakifikirika kuwa ni madogo ukilinganisha na kipatoa chao cha siku moja zikiwemo malipo ya faini ya shilingi 400,000 kwa kuziba njia na kusababisha foleni pamoja na gari kutumia namba ya usajili ya gari jengine.

Kupitia ongezeko la makusanyo hilo, Kamati imegundua kuwa Mamlaka imefanikiwa kuanzisha Mfumo wake wa utoaji huduma za usajili magari ambao unatarajiwa kuongeza zaidi mapato katika mwaka ujao.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ihakikishe inaongeza juhudi kukamilisha mifumo yote inayohitajika ili waweze kuwapatia wananchi huduma kwa urahisi zaidi na kuiongezea mapato mengi Serikali yetu.

## Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,267,800,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilitumia jumla ya shilingi 1,072,271,982.49 kwa ajili ya kazi za kawaida saw ana asilimia 84.58 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 195,528,017.51 sawa na asilimia 15.42 ya makadirio.

### Majibu na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani haijawasilisha majibu ya Hoja ya taarifa ya Matumizi siku mbili kabla ya Kamati kukutana na Mamlaka hiyo kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 97(3) ya Bazara la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Kamati ya PAC ilielezwa kwamba jumla ya shilingi takriban milioni 150 Mamlaka haikuzipatikana kutoka Serikalini na kushindwa kutekeleza Programu ya utoaji elimu ya matumizi bora ya Barabara kwa wanafunzi katika Skuli nyingi za Zanzibar, kushindwa kununua gari ya 'operation', ukamilishaji wa uwekaji wa mifumo ya upasishaji gari pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi ikiwemo fomu za ukaguzi.

Katika kupitia hesabu ya mwisho wa mwaka (Financial Statement), Kamati imebaini

kuwa kulikuwa na changamoto fedha za malipo ya Walinzi ambapo walikuwa wachache (walistaafu wengi) na kulipwa ‘overtime’ nyingi kutokana na kuwatumia sana, kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na kupelekea fungu la matumizi ya fedha hizo kuwa kubwa. Kadhalika, Kamati imegundua kuwa kifungu cha ‘other payment’ kilikuwa hakijapangiwa matumizi lakini kumeonekana kuingiziwa shilingi milioni 186 ambapo shilingi 158,747,547.91 zilikuwa ni fedha zilizotoka Serikalini kwa ajili ya kuwalipa Watoa Huduma wa Mamlaka na nyengine walilipa madeni ya ununuzi wa vifaa kwa Wakala wa Uchapaji Zanzibar. Pia, Mamlaka ilinunua ‘computer 1, kipoza hewa 1 viti pamoja na kuanzisha mfumo mmoja kati ya mitatu bila ya kuambatanisha kiambatisho kinatoa mchanganuo wa malipo ya jumla ya shilingi milioni 158.7 wakati wa kufunga hesabu zao.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1) Mamlaka ya Usafiri na Usalama wa Barabarani ihakikishe inafunga hesabu zake za mwisho wa mwaka vizuri zaidi kwa kufanya uchambuzi wa fedha wanazozipata hata kama walikuwa hawakubajeti awali.
2) Mamlaka ihakikishe inakamilisha na kuitumia ipsavyo mifumo ya upasishaji gari ili waweze kukusanya kwa wingi na kuionezea mapato Serikalini.
3) Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe inaipatia fedha Mamlaka hii kama ilivyopangwa katika bajeti yake.

## Hoja nambari 5.1.9.1: Kasoro iliyobainika katika fedha za ulipaji wa madeni

Katika kutatua tatizo la madeni ya Serikali yanayodaiwa na watumishi na watoa huduma mbali mbali wa Taasisi za Umma, mnano mwezi wa Julai, 2021 Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ilitoa maelekezo kwa Taasisi zinazohusika na Bajeti ya Serikali kuwasilisha madeni ya watumishi na Wazabuni wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki na hatimae kulipwa madeni stahiki.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilipokea jumla ya shilingi 186,868,770 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (Hazina)kwa ajili ya kulipa madeni ya Mamlaka. Hata hivyo hadi ukaguzi unakamilika Mamlaka imetumia jumla ya shilingi 158,748,547.91 kati ya fedha walizopokea na kubakisha jumla ya shilingi 28,120,222.09 ambazo bado hazijatumika kwa kulipia madeni yake kama ilivyotarajiwa.

Kutokulipa madeni ambayo tayari Mamlaka imekwishapokea fedha zake ni kwenda kinyume na maelekezo ya Serikali na kunaweza kuibebesha Serikali mzigo usiokuwa ya lazima. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kufanya haraka katika kuhakikisha

kuwa fedha zilizopokewa na Mamlaka kwa ajili ya kulipa madeni zinatumika kwa ajili ya malengo yaliyokusudiwa.

**Majibu ya Uongozi**

Mamlaka imepokea ushauri wa ukaguzi wa kufanya haraka kukamilisha malipo ya madeni kwa kutumia fedha zilizopokelewa kulipia madeni. Madeni yaliyokuwa yamebakia kulipwa tayari yalishalipwa kwa mujibu wa taratibu za fedha. Madeni hayo ikiwemo malipo ya wafanyakazi, malipo ya vifaa vya kuandikia, malipo ya vifaa vya computer vilivyotumika kwa matumizi ya ofisi Pamoja na malipo ya Kampuni ya ZAN FIBER SOLUTION ambapo malipo ya Zan Fiber yamelipwa kwa njia ya Uhaulishaji kiasi cha Tzs.9,458,019 ya 28/08/2022.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Mamlaka ilitakiwa kulipa madeni yenye jumla ya shilingi milioni 186 lakini walifanikiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 158. Hilo lilijitokeza kutokana na kushindwa kuwapata baadhi ya Watoa huduma kupitia anuani zao. Aidha, walipopita Wakaguzi fedha zilizobakia hazikuwepo kwani walikuwa wamezitumia kwa kutengenezea mifumo na utaratibu wa malipo ya usajili huko Karakana lakini walizirudisha walipokuwaja Wakaguzi kufanya 'verification' ya mwaka ujao. Kufuatia majibu na sababu zilizotolewa, Kamati ya PAC imeridhishwa na majibu ya hoja na kuiondosha hoja hiyo.

## Hoja nambari 5.1.9.2: Dosari zilizobainika katika kumbukumbu za vifungu vya mapato ya Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 177 cha Sheria nambari 7 ya mwaka 2003 ya Usafiri Barabarani, Mamlaka imepewa uwezo wa kukusanya ada na tozo nyengine mbalimbali kupitia vyanzo vyake vya ndan vya mapato. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa kasoro kadhaa katika uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za mapato ya Mamlaka zinazotunzwa na watoa huduma (makarani) wa Mamlaka, kumbukumbu ambazo 6 huwa ndio mwanzo wa upatikanaji wa takwimu za utekelezaji wa shughuli za Mamlaka. Kasoro zilizobainika ni kama zifuatavyo:-

- Kutowiana kwa idadi ya lena zilizotolewa kwa mujibu wa daftari la usajili na idadi ya lena zilizoripotiwa katika ripoti za Uongozi kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 58: Tofauti iliyobainika baina ya idadi ya lena zilizotolewa na idadi ya lena zilizoripotiwa.**

| Tarehe | Idadi ya lena kwa mujibu wa daftari la usajili(A) | Idadi ya lena kwa mujiburipoti za uongozi(B) | Tofauti(A-B) |
|---|---|---|---|
| 16-May-22 | 21 | 58 | (37) |
| 17-May-22 | 17 | 39 | (22) |
| 18-May-22 | 70 | 0 | 70 |
| 20-May-22 | 19 | 0 | 19 |
| 23-May-22 | 33 | 0 | 33 |
| 9-Jun-22 | 31 | 42 | (11) |
| 8-Jun-22 | 75 | 31 | 44 |
| 10-Jun-22 | 41 | 45 | (4) |
| 13-Jun-22 | 54 | 33 | 21 |
| 23-Nov-21 | 34 | 0 | 34 |
| 24-Nov-21 | 56 | 86 | (30) |
| 25-Nov-21 | 32 | 20 | 12 |
| 26-Nov-21 | 36 | 0 | 36 |
| 23-Mar-22 | 54 | 106 | (52) |
| 24-Mar-22 | 0 | 96 | (96) |

- Kukosekana kwa daftari la usajili wa taarifa za beji za makonda na madereva zilizotolewa na Mamlaka kwa kila siku, badala yake ukaguzi umebaini kuwepo kwa daftari linaloweka takwimu ya idadi za beji zilizotolewa na Mamlaka. Athari Kuwepo kwa kasoro zilizobainika hapo juu kunapelekea Mamlaka kukosa takwimu zilizo sahihi na zenye kuaminika. Mapendekezo Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kuwa wanaweka mfumo mzuri wa kusajili

taarifa za huduma zinazotolewa na Mamlaka ili kuweza kuhakikisha usahihi wa takwimu za utekelezaji wa shughuli za Mamlaka zinazoripotiwa katika taarifa za uongozi zinaendana na uhalisia wa upatikanaji wa mapato unaotokana na huduma zinazotolewa na Mamlaka.

**Majibu ya Uongozi**

Mamlaka imepokea mapendekezo ya Ukaguzi wa kuweka mfumo mzuri wa usajili wa taarifa za huduma zinazotolewa ili kuhakikisha usahihi wa takwimu za utekelezaji wa shughuli za Mamlaka. 8 Mamlaka kwa sasa ipo katika hatua ya uandaaji wa mifumo katika utoaji wa huduma za msingi ikimo lena, beji, na vibali vya wageni. Mifumo hiyo itatumika kuondoa kasoro za kitakwimu na kuweka kumbukumbu, utoaji taarifa sahihi za utoaji wa huduma hizo. Mifumo hiyo inatayarishwa chini ya kampuni ya UBx ambayo inasimamiwa na E-Government kwa taasisi zote za Serikali zisizokuwa na mifumo ya Utoaji wa huduma. Hata hivyo Mamlaka tayari imeshapendekeza mfumo wa dharura wa Manual kwa kuboresha madaftari ya uwekaji wa kumbukumbu za utoaji na upokeaji wa lena, uwekaji kumbukumbu za vibali vya wageni (permi ts)na Uwekaji kumbukumbu wa beji za madereva na konda. Mfumo huo unajumuisha Column ya Particular, Receipts, Issue na Balance.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua dosari hizo zilisababishwa na kitu gani na kuelezwa kwamba zilichangiwa zaidi na kutumika kwa utaratibu wa ‘manual’ katika ukusanyaji mapato lakini hivi sasa Kamati imegundua kuwa tayari Mamlaka kwa hatua kubwa imeshaanda Mfumo wa ukusanyaji mapato hayo utakaotumika kuondosha changamoto/dosari zilizojitokeza.

Aidha, Kamati ilitaka kujua kwamba Mfumo huo umeandaliwa kwa kufuata muongozo uliotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar na kuelezwa kwamba tangu hatua za awali ‘e-Gaz’ wamewashirikisha ipasavyo na hivi sasa wamo katika majaribio na ifikapo mwezi wa Juni, 2024 wanatarajia rasmi kutumia mfumo huo. Hivyo, Kamati ilipata muda wa kuangalia ufanyaji kazi wa Mfumo huo na kuridhika nao. Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhika na majibu na kuifuta hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Mamlaka ihakikishe inakamilisha uandaaji wa mfumo huo ili dosari kama hii isijitokeze

tena wakati mwengine.

## Hoja nambari 5.1.9.3: Malipo yaliyolipwa kwa fedha Taslim shilingi 42,138,000

Kwa mujibu wa kanuni nambari 58 (1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma (2021), malipo yote ya Taasisi inayohusika na Bajeti ya Serikali lazima yafanyike kwa njia ya uhaulishaji. Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 42,138,000 kwa Wazabuni na Watoa huduma mbalimbali kwa njia ya fedha taslimu badala ya njia ya uhaulishaji wa fedha.

Kufanya malipo kwa njia ya fedha taslim kunaweza kupelekea uwepo wa upotevu wa mapato ya Serikali yanayotokana na kutokukatwa kwa kodi ya zuio au ongezeko la thamani kwa Watoa huduma au Wazabuni waliotoa huduma kwa Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kuwa wanafuata Sheria, Kanuni na miongozo ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma katika ufanyaji wa mapato mabalimbali ya Mamlaka. Mchanganuo wa malipo yaliyobainika ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 59: Malipo yaliyolipwa kwa njia ya fedha taslim**

| Hati Nam | Aliyelipwa | Hundi Nam | KiasichaFedhaKilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 5/2 | Mkurugenzi Mkuu | 000058 | 11,200,000 | Malipo kwa ajili ya utengenezaji wa mifumo |
| 3/9 | | 000034 | 3,617,000 | Malipo kwa ajili ya wajumbe wa Bodi |
| 14/11 | | 000039 | 6,205,000 | |
| 25/12 | | 000042 | 8,800,000 | |
| 3-Jan | | 000062 | 4,534,000 | |
| 13/4 | | 000072 | 987,000 | |
| 14/4 | | 000072 | 6,795,000 | |
| **Jumla** | | | **42,138,000** | |

### Majibu ya Uongozi

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilifanya malipo kwa fedha taslim kwa baadhi shughuli za Mamlaka, malipo hayo yalifanywa kutokana na uharaka na ugumu wa baadhi ya walipwaji katika matumizi ya Account za benki. Mamlaka kwa sasa haitumii mfumo wa kulipa kwa fedha taslim kwa shughuli yoyote ikiwemo malipo ya likizo, malipo ya muda wa ziada, Malipo ya vikao vya bodi hata kwenye kazi maalum zinazofanywa na Mamlaka.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilitaka kujua ni fedha zipi ambazo zililipwa kwa utaratibu wa fedha taslim (cash) wakati tayari Serikali ilikuwa inatoa huduma zake kwa kutumia mfumo na kuelezwa kwamba kulikuwa na Wajumbe wa Bodi ambao walikuwa ni watu wazima hawana hesabu ya benki na walikuwa wakilalamika kwamba wakilipwa kupitia benki wanapata usumbufu. Aidha, kulikuwa na timu ya wafanya kazi wa Jeshi la Polisi ambao walitaka kususia kukamilisha uwekaji wa Mfumo wa utonzaji adhabu za papo kwa papo katka hatua za mwisho.

Kamati imegundua kuwa kulijitokeza uzembe huo na kubainika na Mkaguzi lakini kwasasa kasoro hiyo imesahrekebishwa na malipo yote yanalipwa kupitia hesabu za benki. Kamati imethibitisha hilo kwa kuangalia barua ya tarehe 20/6/2023 yenye kumbukumbu nambari ambayo imefanya maombi ya malipo ya wajumbe wa Bodi kupitia hesabu zao. Hivyo, kutokana na hatua ambayo Mamlaka imechukua, Kamati ya PAC imeridhia kuondolewa kwa hoja hiyo.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Mamlaka ihakikishe inaendelea kufanya malipo ya huduma inazotoa kupitia hesabu za Benki za wahusika ili kuwepo na usalama wa malipo hayo na kujiepusha na hoja zisizo za ulazima.

## MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI - PEMBA.

## Hoja Nambari 5.1.9.4: kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato.

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 866,500,000/- kupitia vianzio vyake mbali mbali vya mapato kwa mwaka wa fedha 2021 /2022. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Mamlaka ilikusanya jumla ya shilingi

395,484,000/- sawa na asilimia 45.6 ya makadirio.

Kutokana na kutokufikiwa kwa lengo lililokusudiwa ukaguzi umebaini hali hio imechangiwa na uwepo wa muamko mdogo wa usimamizi wa tozo za mapato yatokanayo na upatikanaji wa huduma za leseni za barabarani pamoja na upasishaji wa vyombo vya moto.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba kuchukuwa jitihada za makusudi katika kusimamia upatikanaji wa mapato ili kuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Ni kweli kwa Mwaka 2021/2022 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba haikuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato iliyokadiriwa na Serikali, Hali hiyo ilitokana na sababu mbali mbali kama ifuatavyo:-

Makisio makubwa ya kulingana na uhalisia wa vianzio vya mapato viliomo katika Mamlaka, Kwa mfano usajili wa vyuo vya udereva ilikadiriwa kukusanya Tsh 527,000 kwa vyuo 6, jambo ambali ni kinyume na uhalisia kwani kwa Pemba kuna vyuo viwili vilivyosajiliwa, Aidha vibali vya wageni vilipangiwa kukusanya Tsh 975,000 ambazo haziwezi kuzalishwa kulingana na uhaba mkubwa wa wageni waliofika kutembelea Pemba.

Hata hivyo kwa sasa Ofisi ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba inakusanya Tsh. 59,049,600/= kwa mwezi, ukilinganisha Tshs. 20,000,000 mpaka 30,000,000 iliyokuwa ikikusanywa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kiasi ambacho inaonyesha ongezeko kubwa la mapato kwa mwaka ulioanzia Julai 2023/2024.

1. Uhaba wa vitendea kazi, katika utekelezaji wa kazi zake Mamlaka inakabiliwa na uhaba ukubwa wa vitendea kazi, Mamlaka haina gari kwa ajili ya kufuatilia usimamizi wa kazi zake ili kuwadhibiti wanaokiuka kulipa tozo mbali mbali ili kuongeza ukusanyaji wa mapato, jambo hilo limepelekea ugumu katika kufanikisha upatikanaji wa mapato yaliyokusudiwa. Kwa sasa Mamlaka inayo gari moja ambayo inatumika kufanyia ‘opertation’ mbalimbali ambazo zimeisaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuondoa changamoto hiyo.
2. Ufinyu wa bajeti inayopatiwa Mamlaka , kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilikuwa ikitegemea OC kutoka Serikalini ambayo ilikuwa ikipatikana kwa kiwango kidogo au kukosekana baadhi ya miezi jambo hilo lilipelekea uwezo mdogo wa Mamlaka kufanya kazi zake

kama vile kukosekana kwa mafuta kwa ajili ya zoezi la ‘operatio’n barabarani ambazo zinaiwezesha Mamlaka kuongeza ukusayaji. Kwa sasa Mamlaka imepewa uwezo wa kutumia mapato inayoyakusanya na kupeleka gawio Serikalini jambo hilo limeipa nguvu ya kukusanya mapato yaliyokadiriwa na kupeleka gawio kwa wakati.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Mamlaka imekiri kuwepo kwa changamoto ya kutokufikia kwa lengo la ukusanyaji wa mapato, hata hivyo kamati ya PAC imebaini kuwa hali hii imetokana na Wizara ya fedha ndio wahusika wakuu ambao wanapanga makisio ambayo kimsingi hayaendani na uhalisia wa mapato.

Kamati imebaini utofauti wa egezoko la mapato kati ya mwaka wa fedha 2022/2023 mapato yalipungua lakini baada ya jitihada za ziada ambazo Mamlaka ya Usafirishaji imezichukua mapato yameimarika katika mwaka 2023/2024.

Hali hii imetokana na kuwepo kwa adhabu ya papo kwa papo, ambapo lengo la Serikali ni kupunguza ukiukwaji wa Sheria za barabarani na imeonekana wananchi wengi wanakiuka Sheria hizi na kupelekea kulipa faini kwa mara kwa mara na kupelekea kuengezeka kwa mapato kwa kiasi kikubwa.

Kwa upande wa ufinyu wa vitendea kazi kamati imeelezwa kuwa katika kulitatua tatizo hili, kwa kuwa Mamlaka imekwisha andaa mpango wa ununuzi wa gari kwa ajili ya kuipitisha kwenye bajeti ya 2023/2024. Kamati ya PAC imeibakisha hoja hii

**Ushauri, Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

kamati ya PAC inashauri uongozi wa Mamlaka ya Usalama Barabarani kuhakikisha wanachukua jitihada za ziada katika kutatua changamoto ya usafiri ili lengo la serikali lipatikana

## Haja Nambari 5.1.9.5: Upungufu wa vitendea kazi.

Miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba ni kusimamaia huduma za utoaji wa leseni za Barabarani, Upasishaji wa vyombo vya moto, kusimamia taratibu za kufanya mitihani ya leseni pamoja na kukusanya tozo zinazotokana na makosa mbali mbali ya barabarani.

Kutokana na huduma hizo zinazofanywa na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba umebaini uwepo wa vitendea kazi vichache ambavyo havilingani na uhalisia wa

majukumu yanayotekelezwa na Taasisi hiyo hatimae inaweza kupelekea kutofikia malengo iliojipangia kwa ufanisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha kwamba inatenga Bajeti ya kutosha ya kuweza kununuwa vifaa vinavyohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba ili kuweza kufikia malengo iliyojipangia

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Ni kweli Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilikuwa ikikabiliwa na changamoto ya uhaba wa vifaa mbali mbali vya kutendea kazi, hali hiyo inatokana na ufinyu wa bajeti inayopatiwa Wizara ambayo haikidhi mahitaji kulingana na mipango iliyokusudiwa, Wizara imeomba Serikalini kupatiwa 'retatantion' ili kuiwezesha Mamlaka kutumia mapato yake, kwa mwaka 2023/2024 Serikali imeiruhusu Mamlaka kutumia mapato yake ambayo yameiwezesha kununua vitendea kazi mbali mbali kama computer, viti na meza, pamoja na kufanya mataengenezo ya ofisi zake ili kuboresha mazingira ya kazi kwa watendaji.

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Kamati imebaini Mamalaka ya Usalama Barabarani baada ya mkaguzi kubaini dosari hii tayari Mamlaka imechukua juhudi za kutatua changamoto hizi. Hivyo kamati imeridhika na majibu ya hoja.

**Ushauri, Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauro Uongozi wa Mamlaka ya Usalama Barabarani kuendelea kutatua changamoto zote ambazo mkaguzi amezibaini kwa mujibu wa miongozo.

# 6.0 UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## 6.1.4 WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO ZANZIBAR

### Taarifa ya Mapato

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 2,354,100,000 kutoka Serikali Kuu, kati ya fedha hizo shilingi 1,511,800,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na

shilingi 842,300,000 ni kwa ajili ya Mishahara.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ilipokea jumla ya shilingi 1,480,491,036 kutoka Serikali Kuu sawa na asilimia 62.9 ya makadirio, katiya fedha hizo jumla ya shilingi 512,944,870 kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 61 ya makadirio na jumla ya shilingi 967,546,166 kwa ajili ya kazi za kawaida ambayo ni sawa na asilimia 64 ya Makadirio.

Aidha, Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na Zana za Kilimo walijipangia kukusanya jumla ya shilingi 100,000,000 kutokana na vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo walikusanya shilingi 190,156,105 sawa na asilimia 190 ya makadirio.

## Majibu na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikupatiwa majibu kuhusiana na hoja ya taarifa ya Mapato ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(3) ya Kadumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020) kwamba majibu ya Kamati yawasilishwe kwa Kamati siku mbili kabla ya kikao husika. Hata hivyo, katika majadiliano ya hoja hii, Kamati imebaini yafuatayo:-

1. Wakala kwa mwaka wa fedha 2021/2022 walipanga makadirio yasiyokwenda sambamba na uhalisia (under estimate) na kuonekana wamekusanya kiwango kikubwa cha mapato. Hili limebainika baada ya Kamati kupitia Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa mwaka (Financial Statement) na kubaini kuwa jumla ya shilingi 115,034,571.00 Wakala ulikusanya mwaka wa fedha 2020/2021 wakati kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wakala huo ulikadiria kukusanya jumla ya shilingi 100,000,000/-. Kutokana na kiwango hicho kuwa kidogo, Wakala umeonekana umekusanya mapato mengi ya jumla ya shilingi 190,156,105,000 ambapo kiuhalisia utaiona kuwa ni kiwango kikubwa lakini kibajeti walikuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya mapato hayo.
2. Wakala unavyo vyanzo vikuu viwili vya mapato ambavyo ni matengenezo ya gari, zana na vipuri pamoja na huduma za ukulima katika mashamba ya wananchi. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, chanzo cha matengenezo ya gari, zana na vipuri kitahamishwa na kupelekewa Karakana Kuu ya Serikali.
3. Mapato ya Wakala yameonekana kuongezeka kutokana na matumizi ya mfumo wa ulipaji wa ZanMalipo ambao kwa kiasi kikubwa umedhibiti mianya ya upotevu wa mapato yao. Aidha, Bodi ya Ushauri ya Wakala ulifanya mabadiliko ya bei za gharama za kuwalimia wakulima shamba zao kutoka elfu 30 hadi elfu 60.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wakala uhakikishe unapanga makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mujibu wa uhalisia na kuacha kufanya makisio kwa mazoea.
2. Ili kupata udhibiti mzuri wa fedha za Serikali, Wakala uhakikishe unatumia ipsavyo mfumo wa ZanMalipo katika ukusanyaji wa mapato yake.

## Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,454,100,000, kati ya fedha hizo jumla shilingi 842,300,000 ni kwa ajili ya Mishahara na jumla ya shilingi 1,611,800,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ilitumia jumla ya shilingi 1,398,738,964.27 sawa na asilimia 57 ya makadirio, kati ya fedha hizo shilingi 512,944,870 ni kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 60.9 ya makadirio na jumla ya shilingi 885,794,094.27 ni kwa ajili ya kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilimia 63 ya makadirio.

### Majibu na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikupatiwa majibu kuhusiana na hoja ya taarifa ya Matumizi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(3) ya Kadumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020) kwamba majibu ya Kamati yawasilishwe kwa Kamati siku mbili kabla ya kikao husika.

Hata hivyo, katika majadiliano ya hoja hii, Kamati imebaini kwamba Wakala haukuwa na daftari la usajili wa Mali zake (Fixed Asset register) ambalo lingeweza kuisaidia Wakala kutambua thamani ya zana za matrekta (26,438,284) na vipoza hewa (4,170,000) vilivyonunuliwa ambavyo vimeongeza thamani za vifaa vyao.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wakala uhakikishe unalihuisha daftari la usajili wa Mali za Wakala ili liweze kutoa taswira halisi ya mali zinazomilikiwa na Wakala.

## Hoja nambari 6.1.4.1: Mapato yaliyokusanywa nje ya Mfumo wa ZanMalipo shilingi 190,156,105

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Afisi ya Rais Fedha na Mipango ilifanya maamuzi ya kutumika kwa Mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa Mapato ya Serikali unaojulikana kwa jina la ZanMalipo ambao umefanyiwa uunganishwaji kwa taasisi zote za Serikali na Wakala wa Serikali Mtandao (e-Government).

Ukaguzi umepitia taarifa ya hesabu ya Wakala pamoja na taarifa nyengine za ukusanyaji wa mapato na kubaini jumla ya shilingi 190,156,105 zimekusanywa na Wakala kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato bila ya kutumia mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali wa ZanMalipo.

Kufanya makusanyo ya mapato nje ya mfumo kunaweza kupelekea kutokupatikana kwa taarifa sahihiza mapato yaliyokusanywa na kuwasilishwa benki kwa mujibu wa utaratibu

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kuchukuwa hatua za kuwasiliana na Wakala wa Serikali Mtandao ili kuweza kuunganishiwa na Mfumohuo kwa utaratibu ambao Serikali imeziwekea taasisi zake zote.

### Majibu ya Uongozi wa Wakala

Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wakala haikutumia mfumo wa ZanMalipo kutokana na utaratibu wa mfumo huo kuwa fedha inayokusanywa kupitia mfumo zinatakiwa ziingie Mfuko Mkuu wa Hazina, pia kwa wakati ule ilikua haijawekwa wazi makusanyo ya Wakala ambayo yanapaswa kuhesabika kama mapato kwa vile fedha zinazokusanywa hutumika kwa ajili ya huduma ya ukulima mara tu wakulima wanapolipia. Hivyo Wakala ililazimika kuomba ufafanuzi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Barua Kumb. Namb. WSHM/2017/MP/01 ya 24/02/2022 WSHM/2017/MP/02 ya 16/05/2022 EA.184/372/01/02/37 ya 23/05/2022. Baada ya kupata ufafanuzi Wakala tayari imeanza kutumia mfumo rasmi mnamo Disemba 2022 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba ni kweli Wakala ulikuwa unatumia fedha za makusanyoa bila ya kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hilo lilifanyika kutokana na kutopatikana kwa wakati fedha za matumizi mengineyo pamoja na upungufu wa fedha zinazopatikana. Lakini hivi sasa Kamati imejiridhisha kwamba fedha hizo zinaingia katika mfumo wa ZanMalipo kama ilivyoelezwa kupitia barua zilizonakiliwa katika majibu ya Wakala.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kwa vile Wakala upo kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa wananchi na sio kufanya biashara, hivyo Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuandaa utaratibu rafiki utakaohakikisha fedha zinazokusanywa na Wakala kupitia mfumo wa ZanMalipo zinabakia kwa matumizi ya Wakala.

## Hoja nambari 6.1.4.2: Dosari katika uwasilishaji wa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka.

Kifungu nambari 42(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaitaka taasisi ya ununuzi kuandaa na kuwasilisha Mpango wake wa manunuzi wa mwaka wa bajeti kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma katikatarehe itakayoelezwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi umebaini Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 haijawasilisha Mpango wake wa Manunuzi katika Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kama Sheria ya manunuzi inavyoelekeza jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Kutowasilishwa kwa mpango wa manunuzi wa Wakala katika Mamlaka ya Manunuzi kutapelekea kufanya manunuzi ambayo hayajapata idhini za Mamlaka ya Manunuzi jambo ambalo litapelekea kufanya manunuzi kinyume na sheria na kanuni za Manunuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kuhakikisha kuwa kitengo cha manunuzi kinafuata Sheria na miongozo iliyowekwa kwa lengo la kufanikisha malengo waliyojiwekea.

### Majibu ya Uongozi wa Wakala

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta za Zana za Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 haikuwasilisha Mpango wake wa manunuzi katika Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma. Hii ni kwa sababu Mpango wa Manunuzi wa Wakala ulikuwa ni sehemu ya Mpango Mkuu wa Manunuzi wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ambao kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ulijumuisha Idara na Taasisi zote za Wizara.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Wakala hauna 'vote' yake, Wakala haukutakiwa kuwasilisha Mpango wa Manunuzi kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kinyume na ilivyoelezwa katika hoja ya Mdhibiti. Kwa msingi huo, Kamati imeifuta hoja hii.

## Hoja nambari 6.1.4.3: Kuwepo kwa Matrekta ambayo hayajafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu

Ukaguzi ulibaini uwepo wa Matrekta ambayo hayajafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu hivyo kupelekea kuzorota kwa shughuli za Kilimo kutokana na kutokufanya kazi kwa baadhi ya Matrekta kwa muda mrefu.

Kutokufanyiwa matengenezo kwa matrekta hayo kwa muda mrefu kunaweza kupelekea kuendelea kuchakaa na hatimae kutokuweza kutengenezeka kutokana na kuongezeka kwa gharama zamatengenezo kwa mujibu wa hali ya uchakavu ulivyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kuhakikisha unatenga bajeti ya kutosha ya kufanya matengenezo pamoja na kufufua matrekta yaliyochakaa ili kuweza kupatikana kwa tija iliyokusudiwa ikiwemo kuwaondoshea wakulima usumbufu wa kuimarisha mashamba yao. Mchanganuo wa matrekta ambayo hayakufanyiwa matengenezo kwamuda mrefu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 70: Matrekta ambayo yanahitaji matengenezo**

| Nam. | Namba Ya Trekta | Aina ya Trekta | Hali ya Trekta | Kituo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SMZ 116D | FARM TRUCK | Inahitaji Matengenezo | Pemba |
| 2 | SMZ 108D | New Holand TT75 | Inahitaji Matengenezo | Pemba |
| 3 | SMZ 103D | New Holand TT75 | Inahitaji Matengenezo | Pemba |
| 4 | SMZ 117D | New Holand TT75 | Inahitaji Matengenezo | Pemba |
| 5 | T 485 BWG | New Holand TT75 | Bovu | Pemba |
| 6 | T 700 BWE | New Holand TT75 | Bovu | Pemba |
| 7 | T 349 BAQ | New Holand TT75 | Bovu | Pemba |
| 8 | T 449 BWE | New Holand TT75 | Bovu | Pemba |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9 | SMZ 118D | New Holand TT75 | Bovu | Pemba |
| 10 | SMZ 6631 | New Holand TD80 | Bovu | Pemba |
| 11 | SMZ 132D | New Holand | Bovu | Unguja |
| 12 | SMZ 133D | New Holand | Bovu | Unguja |
| 13 | SMZ 135D | New Holand | Bovu | Unguja |
| 14 | SMZ 141D | New Holand | Bovu | Unguja |
| 15 | SMZ 107D | New Holand | Bovu | Unguja |
| 16 | SMZ 6727 | New Holand | Bovu | Unguja |
| 17 | SMZ 6638 | New Holand | Bovu | Unguja |

## Majibu ya Uongozi wa Wakala

Ni kweli Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ilikuwa na matrekta ambayo hayajafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu. Hii inatokana na baadhi yao kuwa ni machakavu na gharama za kuyatengeneza kuwa kubwa, hivyo Wakala iliyaorodhesha matrekta hayo na kuwasilisha katika mamlaka husika (ORFM) kwa ajili ya kuuzwa kwa mnada. Aidha katika orodha iliyoainishwa katika Jadueli Nam. 1 yapo baadhi ya Matrekta yameshatengenezwa na yapo shambani yanatoa huduma na yaliyobakia yanapelekwa Wakala wa Karakana Kuu ya Serikali ya Magari kwa matengenezo.

Aidha, kuwepo kwa matrekta yanayohitaji matengenezo haikusababisha Wakala kushindwa kutoa huduma kwa wakulima kwa wakati kwani maombi yote yaliyowasilishwa na wakulima katika msimu wa ukulima 2021/2022 yalifanyiwa kazi kwa wakati.

### Jadueli Nambari 1: Matrekta ambayo yanahitaji matengenezo

| Nam. | Namba ya Trekta | Aina ya Trekta | Hali ya Trekta | Kituo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ 116D | FARM TRUCK | Inahitaji Matengenezo | Pemba |
| 2. | SMZ 108D | NEW HOLAND TT75 | Inahitaji Matengenezo | Pemba |
| 3. | SMZ 103D | NEW HOLAND TT75 | Inahitaji Matengenezo | Pemba |
| 4. | SMZ 117D | NEW HOLAND TT75 | Inahitaji Matengenezo | Pemba |
| 5. | T 485 BWG | NEW HOLAND TT75 | BOVU | PEMBA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6. | T 700 BWE | NEW HOLAND TT75 | BOVU | PEMBA |
| 7. | T 349 BAQ | NEW HOLAND TT75 | BOVU | PEMBA |
| 8 | T 449 BWE | NEW HOLAND TT75 | BOVU | PEMBA |
| 9. | SMZ 118D | NEW HOLAND TT75 | BOVU | PEMBA |
| 10. | SMZ 6631 | NEW HOLAND TD80 | BOVU | PEMBA |
| 11. | SMZ 132D | NEW HOLAND | BOVU | UNGUJA |
| 12. | SMZ 133D | NEW HOLAND | BOVU | UNGUJA |
| 13. | SMZ 135D | NEW HOLAND | BOVU | UNGUJA |
| 14. | SMZ 141D | NEW HOLAND | BOVU | UNGUJA |
| 15. | SMZ 107D | NEW HOLAND | BOVU | UNGUJA |
| 16. | SMZ 6727 | NEW HOLAND | BOVU | UNGUJA |
| 17. | SMZ 6638 | NEW HOLAND | BOVU | UNGUJA |

## Jadueli Nambari 2: Mchanganuo na hali halisi ya Matrekta husika

| Nam. | Namba ya Trekta | Aina ya Trekta | Hali ya Trekta | Kituo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ 116D | FARM TRUCK | Inahitaji Matengenezo | Pemba |
| 2. | SMZ 108D | NEW HOLAND TT75 | Limeuzwa mwaka 2023 | Pemba |
| 3. | SMZ 103D | NEW HOLAND TT75 | Limeuzwa mwaka 2023 | Pemba |
| 4. | SMZ 117D | NEW HOLAND TT75 | Limeuzwa mwaka 2023 | Pemba |
| 5. | T 485 BWG | NEW HOLAND TT75 | Limeuzwa mwaka 2021 | PEMBA |
| 6. | T 700 BWE | NEW HOLAND TT75 | Limeuzwa mwaka 2021 | PEMBA |
| 7. | T 349 BAQ | NEW HOLAND TT75 | Limeuzwa mwaka 2021 | PEMBA |
| 8 | T 449 BWE | NEW HOLAND TT75 | Limeuzwa mwaka 2021 | PEMBA |
| 9. | SMZ 118D | NEW HOLAND TT75 | Limeuzwa mwaka 2021 | PEMBA |
| 10. | SMZ 6630 | NEW HOLAND TD80 | Limeuzwa mwaka 2021 | PEMBA |
| 11. | SMZ 132D | NEW HOLAND | Limepelekwa Karakana kwa Matengenezo | UNGUJA |
| 12. | SMZ 133D | NEW HOLAND | Limepelekwa Karakana kwa Matengenezo | UNGUJA |
| 13. | SMZ 135D | NEW HOLAND | Limeshatengenezwa na lipo shambani kutoa huduma | UNGUJA |
| 14. | SMZ 141D | NEW HOLAND | Linasubiria matengenezo | UNGUJA |
| 15. | SMZ 107D | NEW HOLAND | Linasubiria matengenezo | UNGUJA |
| 16. | SMZ 6727 | NEW HOLAND | Linasubiria matengenezo | UNGUJA |
| 17. | SMZ 6638 | NEW HOLAND | Linasubiria matengenezo | UNGUJA |

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imegundua kwamba bei ya uuzwaji wa Matrekta mabovu unaofanywa na Ofisi ya

Msajili wa Hazina inakuwa ni ndogo ukilinganisha na thamani halisi ya vifaa husika vya Trekta hayo. Kwa mfano, bei ya trekta huuzwa kwa shilingi 4,000,000 hadi shilingi 5,000,000 lakini baadhi ya vifaa vya trekta hilo vinafikia thamani ya shilingi 30,000,000. Aidha, kutokana na upungufu wa fedha ambazo Wakala huingiziwa, hutumia Matrekta mabovu kutoa vipuri (spare parts) kwa ajili ya matengenezo ya Matrekta mazima ili yaweze kuwapatia huduma wananchi kwa wakati.

Sambamba na hilo, Kamati pia imebaini kuwepo kwa ukiukwaji wa utaratibu wa uuzwaji wa mali chakavu za Wakala unaofanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina ambae hufanya maamuzi ya kuziuza mali zilizoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali bila ya kuzingatia masharti ya kifungu cha 29(a) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nambari 11 ya 2016 na Sheria ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ya mwaka 2021 zinavyoelekeza.

Sheria ya Ununuzi inaeleza kwamba kitengo cha Ununuzi kiandae Mpango wa Manunuzi wakati Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina inavitaka vitengo vya Ununuzi kuwasilisha Mpango wa Matengenezo kwa Msajili wa Hazina na sio Ofisi ya Msajili wa Hazina kutekeleza jukumu la kuuza Mali za Wakala bila ya kuwasilishwa ombi la uuzwaji huo kutoka kwa Taasisi husika.

Kadhalika, Kamati imegundua kuwa Wakala hauna Mpango wa Matengenezo ya mali zake na kupelekea kuwepo kwa idadi kubwa ya matrekta mabovu na chakavu bila ya kufanyiwa matengenezo kwa wakati na hatimae kufikia hatua ya kuuzwa kwa bei isiyoridhisha.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Afisa Masuul pamoja na kitengo cha Ununuzi watekeleze majukumu yao kwa kuzingia maelekezo ya Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nambari 11 ya 2016 kwa kufuata taratibu zote za uuzwaji wa mali za Wakala.
2. Wakala uhakikishe unaandaa Mpango wa matengenezo wa Zana za Kilimo na kuuwasilisha Serikali Kuu ili kurahisisha matengenezo hayo kuweza kufanyika kwa wakati.
3. Ofisi ya Msajili wa Hazina ifanye uuzwaji wa mali za umma baada ya kupata maombi ya uuzwaji huo kutoka katika Taasisi husika.
4. Kuwepo kwa mashirikiano ya karibu katika utekelezaji wa kazi za Serikali baina ya Watendaji wa Wakala na Ofisi ya Msajili wa Hazina ili uuzwaji wa mali za umma ufanyike kwa kuzingatia thamani halisi ya vifaa vinavyouzwa.

## WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO - PEMBA

### Hoja nambari 6.1.4.4: Kutokuzungushiwa uzio jengo la Afisi la Wakala

Kifungu namba 58(d) cha Sheria ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma namba 6 ya mwaka 2021 kinaeleza kuwa "Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma atakuwa na jukumu la kuhakikisha utaratibu wa kuhifadhi unawekwa ili kuondoa wizi, hasara, kupotea na matumizi mabaya".

Baada ya kupitia maeneo mbalimbali yanayomilikiwa na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo - Pemba, ukaguzi umebaini kwamba jengo la Afisi la Wakala halina uzio uliotenganisha Afisi hiyo na nyumba jirani ili kulinda mali walizonazo kutokana na mazingira yaliyozunguka hali ambayo inaonyesha udhibiti usioridhisha wa mali za kudumu. Hali hii inaweza kupelekea uvamizi na uharibifu mkubwa wa mali za Serikali ikiwemo jengo lenyewe pamoja na mali zilizomo ndani yake.

Kutokuzunguushiwa uzio katika jengo la Afisi la Wakala ni kwenda kinyume na Kifungu namba 58(d) cha Sheria ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma namba 6 ya mwaka 2021 pamoja na vifungu vya 29(a) na 112(2)(e) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba kuhakikisha kwamba jengo la Afisi linazunguushiwa uzio ili kuzuia uharibifu, wizi au upotevu wa mali za umma.

#### Majibu ya Uongozi ya Wakala

Kwa hakika Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo - Pemba ina uzio unaozunguka na kutenganisha mipaka ya eneo lote la Wakala. Hata hivyo ni kweli kwamba Uzio uliopo uko katika hali mbaya na unahitaji marekebisho. Wakala imelizingatia hilo na katika bajeti ya kila mwaka hutenga fedha ili kufanikisha marekebisho hayo. Hata hivyo, kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha za bajeti imepelekea kushindwa kufanya matengenezo hayo.

Pamoja na hali hiyo, kutokana na kufahamu umuhimu wa Udhibiti wa Mali za umma Wakala imefunga Mkataba na Kampuni ya Ulinzi ya JKU kwa dhamira ya kuimarisha Ulinzi ili kunusuru upotevu na uharibifu wa Mali za Umma. Utekelezaji wa mkataba huu umeanza mwezi Agosti 2023.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kutokana na upungufu wa fedha ambazo Wakala unapatiwa, haukuweza kufanikiwa kujenga uzio utakaolizunguka eneo la Wakala. Hata hivyo, katika kutatua changamoto ya wizi wa Mali za Wakala zilizomo ndani ya eneo hilo, Wakala katika mwaka wa fedha 2022/2023 umepanga bajeti ya huduma ya ulinzi kupitia Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU).

Sambamba na hilo, Kamati imegundua kuwa fedha walizopata Wakala hadi mwezi wa Oktoba, 2023 hazikuweza kumudu gharama za utekelezaji wa majukumu yao ya msingi ya kuwapatia wakulima huduma kuliko masuala mengine ya Ofisi. yao ukiachia mbali fedha za ujenzi wa uzio huo. Kamati pia imebaini ili ujenzi wa uzio uweze kufanyika, kunahitajika Jumla ya shilingi 64,440,000 ambapo Wakala bado haujapatiwa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe bajeti inayotengwa kwa Wakala huu unapatikana kwa wakati ili Wakala huu uweze kuwahudumia Wakulima wetu kwa ufanisi zaidi.

## Hoja nambari 6.1.4.5: Kutokufikiwa kwa lengo la uanzishwaji wa Wakala

Kwa mujibu wa kifungu cha 4(2)(a) cha Sheria namba 2 ya mwaka 2019 ya Uanzishwaji wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, Wakala ilipaswa kuwa na karakana za matengenezo ya matrekta yaliyosheheni vifaa vya matengenezo vyenye uwezo wa kutosha katika kukabiliana na soko la zana za kilimo.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba haina karakana yenye vigezo vinavyokubalika kama sheria ilivyoelekeza. Hali hii inapelekea kutokufikiwa kwa lengo la uanzishwaji wa Wakala.

Kukosekana kwa karakana yenye vigezo vinavyokubalika ni kwenda kinyume na Sheria nambari 2 ya Uanzishwaji wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kifungu nambari 4(2) (a). Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuhakikisha wanatenga fedha za kutosha katika bajeti zao za mwaka ili kuiwezesha karakana yao kuwa ya kisasa.

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

Hatua mbali mbali za kuimarisha karakana zimechukuliwa kuiwezesha kutimiza vigezo vinavyokubalika kama Sheria ilivyoelekeza. Hata hivyo kutokana na maelelekezo ya

Baraza la Mapinduzi (na baadae mabadiliko ya Sheria ya Wakala), kazi za matengenezo na miundombinu ya Karakana zimehamishiwa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari. Kwa sasa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inashughulika na utoaji huduma ya matayarisho ya mashamba (kuchimba, kuburuga, kuchavanga, 'leveling', kuvuna nk.) kwa wakulima na taasisi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba pamoja na kwamba jukumu la kufanyia matengenezo vyombo vyake hususan Matrekta kuhamishiwa Karakana Kuu ya Serikali lakini kunahitajika kuwepo kwa timu ya ufundi katika Wakala huo ili kuweza kutekeleza matengezo madogo madogo yanayojitokeza na sio kukaa na kusubiri Serikali Kuu kwa matengenezo madogo madogo jambo ambalo linaweza kukwaza utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Wakala. Kwa msingi huo, utekelezaji wa hoja hii unakuwa mgumu kutokana na ukweli kwamba bajeti inayopatiwa Wakala haitoshelezi hata kutekeleza majukumu yake ya msingi. Hivyo, hoja hii itaendelea kuwepo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kutokana na umuhimu uliopo, Serikali iuruhusu Wakala wa Matrekta kufanya matengenezo madogo madogo ya matrekta yao kupitia timu yao ya ufundi ili kunusuru kukwama kwa utoaji wa huduma wakisuburi matengenezo ya matrekta kutoka Karakana Kuu ya Serikali.

## Hoja nambari 6.1.4.6: Wafanyakazi wa Wakala wanafanyakazi katika mazingira yasiyo salama

Kwa mujibu wa kifungu cha 77(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011 kinaeleza "Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara au Taasisi watachukuwa hatua ambazo ni muhimu kuhakikisha kwamba mazingira ya kazi yako salama, yanafaa na hayahatarishi usalama na afya ya waajiriwa kwa mujibu wa Sheria ya Afya na Usalama Kazini".

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyakazi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba hawako katika mazingira salama na rafiki katika kutekeleza majukumu yao ya kazi ya kila siku kwani Afisi yao wanayotumia ipo karibu sana na Karakana ya kufanyia matengenezo na service ya vyombo vya moto yakiwemo Matrekta, magari, vespa na Pikipiki ambapo kunakuwa na zogo na mingurumo mikubwa ya gari na pikipiki inayopelekea kukosekana kwa utulivu wa utekelezaji wa majukumu yao ya kazi za

kawaida.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 77(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011. Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kuhakikisha unachukua jitihada ya kutengeneza mazingira rafiki yatakayowezesha kutekeleza majukumu yao kwa utulivu.

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

Ushauri uliotolewa kwa Uongozi wa Wakala wa kuchukuwa jitahada za kujenga Ofisi ambayo itakuwa mbali kidogo na karakana na yenye nafasi ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza unaendelea kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:

Wakala katika Mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30/2023 imeanzisha ukarabati wa Afisi ambapo utakapokamilika itakuwa na nafasi ya kutosha na mazingira mazuri ya kazi mbali na eneo la Karakana.

Ukarabati huu wa jengo la Afisi unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2024/2025 (kutegemeana na upatikanaji wa fedha) na hivyo kutawawezesha watumishi kufanyakazi katika Mazingira yaliyosalama na tulivu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli hoja iliyoelezwa na Mkaguzi ilikuwepo nab ado inaendeleo kuwepo kutokana na ukweli kwamba fedha wanazozipata Wakala huu hazikidhi kuweza kufanya ukarabati wa jengo la Afisi yao. Hata hivyo, ni busara Wakala ukajipanga vizuri kutekeleza ukarabati huo kwa awamu ambapo kwa awamu ya kwanza waanze kuvifanyia matengenezo vyoo vyake ili kuwafanya wafakazi wa Wakala kunusurika na maradhi hususan yanayohusiana na uwepo wa mazingira machafu ya kazi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe unapanga bajeti ya kutosha kwa Wakala huu kwa ajili ukarabati wa jengo lao la Afisi na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe inawaingizia fedha hizo kwa mwaka wa bajeti 2024/2025.

## Hoja nambari 6.1.4.7: Kutokuuzwa au kufanyiwa matengenezo kwa vyombo vya moto chakavu

Kwa mujibu wa kifungu namba 66 cha Sheria ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma namba 6 ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba Kutakuwa na mpango wa

matengenezo wa mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa. Aidha kifungu cha 69(1)(2) kinaeleza kuwa Kutakuwa na mpango wa uondoaji wa mali wa mwaka utakaoandaliwa na kila taasisi ya umma na kuwasilishwa katika Afisi ya Msajili wa Hazina. Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika Afisi kwa ajili ya kuondoa mali za Umma.

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya vyombo vya moto vinavyomilikiwa na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba ikiwemo matrekta na gari havitumiki, vimetelekezwa au kutokufanyiwa matengenezo kwa muda mrefu bila uongozi kuonyesha juhudi za kuvifanyia matengenezo ili kuvitumia au kuviondoa kama inavyotakiwa na sheria. Hali hii inaweza kupelekea vyombo husika kuzidi kushuka thamani hivyo Serikali kushindwa kunufaika navyo wakati ingeweza kunufaika iwapo Wakala ingeamua kuvifanyia matengenezo au kuviondoa mapema inavyowezekana.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na vifungu nambari 66 na 69(1)(2) vya Sheria ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma nambari 6 ya mwaka 2021 na pia ni kwenda kinyume na kifungu cha 29(1)(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuhakikisha wanavifanyia matengenezo vyombo husika au wanaviombea ruhusa kutoka Afisi ya Msajili wa Hazina ili kuweza kuviondoa. Mchanganuo wa vyombo vyenyewe ni kama vinavyoonekana katika jadweli hapo chini:

## Majibu ya Uongozi ya Wakala

Ushauri uliotolewa unaendelea kutekelezwa ambapo Wakala inendelea na utaratibu wa kuviripoti vyombo vyote vya moto vilivyochakaa ambavyo ni mzigo kwa Taasisi kwa ajili ya kuviondoa; kama ambavyo imefanyika Novemba 2021 amabapo matrekta chakavu 11 yaliuzwa; na Januari na Febuari 2023 ambapo matrekta 6, matela 4, fremu 6 za majembe, gearbox 1 na mabaki ya vyuma yaliuzwa na Msajili wa Hazina kwa njia ya mnada.

Aidha, uongozi wa Wakala unachukuwa juhudi za kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto vinavyoharibika kulingana na upatikanaji wa fedha, na vyombo tajwa (Trekta SMZ 151D, SMZ 109 D na ISUZU SMZ 137 B) tayari vimefanyiwa matengenezo na vinaendelea kutoa huduma iliyokusudiwa.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba Kuna baadhi ya Mali za Wakala hususan Matrekta huondolewa kwa njia ya mnada ambapo bado yanahitajika kuwepo na kutumika. Aidha, mali hizo huuzwa kwa bei ndogo wakati vifaa vilivyomo ndani yake huwa na thamani

kubwa zaidi ya mara Tano ya Mali husika ambapo kama mali hiyo itabakishwa bado itaendelea kutumika ikiwa ni 'spare' kwa chombo kilichoharibika na kukiwezesha kuendelea kutoa huduma kwa maslahi ya wananchi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa Wakala ikae na Ofisi ya Msajili wa Hazina kutafuttia ufumbuzi suala zima la uuzwaji wa Matrekta bila ya kushirikishwa na kupelekea vifaa ambavyo wanavihitaji kama 'spare' kuuzwa kwa bei ndogo ukilinganishwa na uhalisia.
2. Uongozi wa Wakala uandae muongozo utakaosimamia uuzwaji wa vifaa chakavu vya Wakala huo.

## Hoja nambari 6.1.4.8: Kutokufikiwa kwa lengo la kutoa huduma ya ukulima wa ekari 507 kwa wananchi

Miongoni mwa majukumu makubwa ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo - Pemba ni kutoa huduma ya ukulima kwa wananchi katika maeneo mbali mbali yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala ilipanga kutoa huduma ya ukulima kwa wananchi wa maeneo mbali mbali Kisiwani Pemba kwa kulima ekari 3000 za mashamba kwa ajili ya kilimo. Hadi ukaguzi huu unafanyika Wakala imeweza kutoa huduma ya ukulima katika ekari 2493 sawa na asilimia 83.1 ya makadirio hali iliyopelekea kushindwa kufikia malengo waliyojipangia.

Ukaguzi umebaini kwamba kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kunatokana na uwepo wa matrekta ambayo ni chakavu na kukosekana kuleta tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kufanya jitihada za makusudi kuyafanyia matengenezo matrekta ili kuhakikisha kwamba wakulima wote wanaohitaji huduma ya kulimiwa kwa trekta wanalimiwa kwa wakati. Mchanganuo wa makadirio na ukulima halisi kiwilaya ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 72: Kutokufikiwa kwa lengo la kutoa huduma ya ukulima kwa wananchi.**

| Wilaya | Makadirio (Ekari) | Ukulima Halisi (Ekari) | Tofauti (Ekari) |
|---|---|---|---|
| Wete | 1000 | 796 | 204 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Micheweni | 450 | 224 | 226 |
| Chake Chake | 1000 | 994 | 6 |
| Mkoani | 550 | 479 | 71 |
| **Jumla** | **3000** | **2493** | **507** |

### Majibu ya Uongozi ya Wakala

Ni kweli kwamba Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo-Pemba kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ilitoa huduma za ukulima katika eneo la eka 2493 za wanananchi sawa na asilimia 83.1 ya lengo lililokadiriwa la kulima eka 3000. Hata hivyo, hali hii ilitokana na uwepo wa Matrekta chakavu bali ilinatokana na baadhi ya wakulima kutojitokeza kulipia gharama za kulimiwa.

Kiujumla Wakulima wote waliohitaji huduma ya kulimiwa kwa trekta walilimiwa kwa wakati na kwa mara ya kwanza hakukuwa na malalamiko yoyote kutoka kwa wakulima kutokana na kukosekana ama kucheleweshwa kwa huduma hii.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba asilimia iliyobakia haikuweza kutekelezwa kutokana na ukosefu wa fedha za ruzuku za ununuzi wa pembejeo za Kilimo uliotokana na kuongezeka kwa bei ambapo zilipanda kutoka elfu 30,000 hadi 60,000. Vilevile, hivi sasa huduma nyingi wananchi wameshazizoea kuzitekeleza kama vile za uvunaji na uchanganyaji wa pembejeo.

Pia kuna changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo huathiri sana wakulima na ukulima wao. Kadhalika, kuna changamoto ya uvamizi wa maeneo ya Kilimo unaosababishwa zaidi na wananchi kufanya ujenzi katika maeneo hayo na kupunguza au kuondoka shughuli za Kilimo katika maeneo husika.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Wakala uyafanyie matengenezo matrekta ili kuhakikisha kwamba wakulima wote wanaohitaji kupatiwa huduma ya kulimiwa kwa trekta waweze kulimiwa kwa wakati.

## 6.1.6: WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR (ZBA)

## Taarifa ya Mapato

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Majengo ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 330,000,000 kutokana na vianzio mbali mbali vya mapato ya ndani na shilingi 300,000,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Hadi kufikia tarehe 30 June 2022 Wakala wa Majengo ilifanikiwa kukusanya mapato ya shilingi 292,738,220 kutoka vyanzo vya ndani sawa na asilimia 89 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 37,261,780 sawa na asilimia 11 ya makadirio na shilingi 104,230,000 kutoka Mfuko Mkuu Hazina sawa na asilimia 35 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 195,770,000sawa na asilimia 65 ya makadirio.

### Majibu ya Wakala

Kwa mwaka 2021/2022 Wakala wa Majengo ilifanikiwa kukusanya shilingi 292,738,220 kati ya shilingi 330,000,000 zilizokadiriwa kutokana na vianzio vya mapato ya ndani kukiwa na upungufu wa shilingi 37,261,780 uliosababishwa na:-

- Kutokulipwa kwa wakati kwa madeni ya nyumba na mashine ambazo zimekodishwa kwa wananchi.
- Kutokulipwa kwa wakati Ada ya ushauri elekezi ambayo Wakala wa Majengo wanatoa ushauri na uchoraji wa Michoro kwa Taasisi za Serikali.

Aidha Wakala ilikadidiriwa kuingiziwa jumla ya shilling 300,000,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka wa fedha unaoishia juni 2022, hadi kufikia Juni 2022 Wakala ilipokea shilingi 104,230,000 huku kukiwa na upungufu wa shilingi 195,770,000 hali hii ilisababishwa na kutokuingiziwa kwa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kama zilivyopangwa katika bajeti ya Wakala.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

1. Wakala unavyo vyanzo vitatu vya mapato ambavyo ni ukodishwaji wa mashine ya uzalishaji kokoto; kazi za biashara zinazojumuisha ukodishwaji wa nyumba, maduka na maghala na utoaji wa ushauri elekezi.
2. Mapato ya Wakala hayakuwa yakifikia lengo la ukusanyaji kwa kuwa na upungufu wa shilingi 37,261,780 kutokana na uwepo wa madeni ya muda mrefu, ambapo

kwa Unguja wanadai shilingi milioni 13,600,000/-.

3. Wakala kupitia maelekezo ya Serikali, wana mpango wa kuzikabidhi Shirika la Nyumba (ZHC) nyumba zote zilikodishwa kwa Watumishi wa Umma na kubakia na nyumba za Viongozi wa Serikali. Nyumba hizo zinalipiwa kodi tofauti kuanzia shilingi elfu 20,000/- hadi 150,000/- kwa kila mwezi.
4. Pamoja na majukumu ya kufanyia matengenezo nyumba wanazokodisha, Mapato yote yanayokusanywa na Wakala hupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali (Hazina).

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uandae utaratibu mzuri wa kufuatilia madeni wanayodai kupitia nyumba zao ikiwemo kutoa taarifa ya indhari (notice) kwa wale wote wanaodaiwa na iwapo watashindwa kulipa madeni husika, Wakala uchukue hatua za kisheria ikiwemo kuwapeleka Mahakamani na hatimae kuwahamisha katika nyumba hizo.

## Taarifa ya Matumizi

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Majengo ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 300,000,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Wakala wa Majengo imeingiziwa jumla ya shilingi 104,230,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 35 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 195,770,000 sawa na asilimia 65 ya makadirio.

**Majibu ya Wakala**

Kwa mwaka 2021/2022 Wakala wa Majengo imeingiziwa jumla ya shilingi 104,230,000 sawa na asilimia 35 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kati ya shilingi 300,000,000 zilizokadiriwa kukiwa na upungufu wa shilingi 195,770,000 uliosababishwa na kutokuingiziwa fedha kutoka serikalini ambazo tulizipanga katika bajeti yetu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa upande wa matumizi ya Wakala, Kamati ya PAC imebaini kwamba:-

1. Kuna tofauti ya makadirio ya matumizi ya Wakala kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo katika kitabu cha Bajeti pamoja na Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani imeoneshwa makadirio ya shilingi 250,000,000/-, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali shilingi 330,000,000/- na Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa

Mwaka 350,000,000/-.

2. Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka ya Wakala huu haikuonesha mchanganuo wa matumizi ya bajeti ya mwaka 2021/2022. Hali hiyo imesababisha Wajumbe kushindwa kupata taswira halisi ya matumizi ya Wakala huo.
3. Kutokuwepo kwa Bodi ya Wakala kwa muda wa miaka miwili ambapo kwasasa tayari Mwenyekiti wa Bodi hiyo ameshateuliwa lakini Wajumbe hawajateuliwa na Mheshimiwa Waziri husika. Hali hiyo imepelekea Wakala kufanya matumizi kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, nambari 12 ya 2016.
4. Kuwepo kwa ufinyu wa fedha za matumizi wanazoingiziwa na kupelekea baadhi ya shughuli walizojipangia kushindwa kutekelezwa zikiwemo ulipaji wa madeni kwa watoa huduma na kulipa maslahi ya wafanyakazi (likizo na 'overtime').
5. Kuwepo kwa Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani iliyokosa majibu ya Uongozi wa Wakala.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inawashauri Wahasibu, Maafisa Manunuzi na Wakaguzi wa Ndani wafanyekazi kwa kutumia ipasavyo taalum na uzoefu walionao ili kuondoa hoja zisizo za lazima kuingizwa katika kitabu cha Mdhibiti.
2. Uongozi wa Wakala uandae utaratibu mzuri wa kuzifanyia kazi dosari zinaainishwa na Mkaguzi wa Ndani kupitia Ripoti yake ili kudhibiti na kurekebishwa mapungufu yaliyobainishwa na kuyafanyia kazi kwa wakati.
3. Kamati ya PAC inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaingizia Wakala fedha kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kama yalivyopangwa kwa mwaka wa bajeti husika.
4. Kamati ya PAC inaushauri Uongozi wa Wakala kufanya kazi kwa mashirikiano na Mkaguzi wa Ndani ili mapungufu yanayobainika kuweza kuyafanyia kazi na kuyarekebisha kwa wakati.

## Hoja nambari 6.1.6.1: Kutokuainishwa kwa mapato yatokanayo na kodi ya Kiwanda cha KokotoMakunduchi shilingi 4,600,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna mapato yenye thamani ya shilingi 4,600,000 yatokanayo na kodi ya kiwanda cha kuzalishia kokoto ambacho kimekodishwa kwa muekezaji kilichopo Makunduchi lakini mapato hayakuanishwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka ili kuweza kufanya tathmini na kufahamu jinsi

yalivyopatikana. Aidha, ukaguzi ulitembelea katika eneo ambalo kiwanda hicho kipo na kubaini kuwepo kwa uzalishajiwa kokoto wa daraja nne (4). Aina za daraja hizo ni kama zifuatazo:-

- Kokoto ndogondogo zinazotumika kwa matumizi ya chipingi.
- Kokoto za saizi ya kati na kati.
- Kokoto kubwa.
- Unga wa kokoto unaotumika katika kutengenezea matofali.

Kutokuainishwa mapato yatokanayo na kodi ya kiwanda katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka ni kwenda kinyume na kanuni nambari 36(a) ya kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma yamwaka 2021. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba mapato yote yanayotokana na Wakalayanaainishwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka ili kuweza kutambuliwa na kufanyiwa tathmini kwa mujibu wa sheria na kudhibiti upotevu wa mapato hayo.

### Majibu ya Uongozi wa Wakala

Kwa mujibu wa kumbukumbu zetu ni kwamba Mkodishwaji wa Kiwanda cha Kokoto anadaiwa Fedha ya kodi ya Kiwanda hicho kwa muda mrefu na sio kama kuna mapato yamepatikana ambayo hayakuainishwa. Hata hivyo Wakala imechukua juhudi ya kumdai deni hilo ili alisawazishe na kuingiza Mapato yatokanayo na Kiwanda hicho. Pamoja na kukumbushia deni hilo pia Wakala wa Majengo kwa sasa imeirudisha mashine hiyo kwa msajili wa Hazina kwa hatua ya kuipiga mnada kutokana na uchakavu wake.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imegundua kuwa majibu yaliyowasilishwa na Wakala hayakuakisi hoja iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo hoja ilitaka kuainishwa mapato yatokanayo na kodi ya kiwanda cha kokoto - Makunduchi shlilingi milioni 4,600,000/- wakati majibu yamejikita kueleza madeni ya muda mrefu, kwa msingi huo, Kamati haikukubaliana na majibu hayo.

Sambamba na hilo, Kamati imekubaliana na hoja iliyoainishwa na Mdhibiti. Hilo limetokana na ukweli kwamba hata katika Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani amebaini na kueleza kukosekana kwa mapato yatokanayo na kiwanda cha kokoto kiliopo Makunduchi Changani ambapo nikwenda kinyume na kifungu cha 29(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021. Hali hiyo imesababisha Serikali kukosa mapato yatokanayo na Kiwanda hicho.

Kadhalika, Mkataba wa ukodishwaji wa kiwanda hicho unaelekeza kuwa Mmiliki afanye malipo yake kila mwisho wa mwezi, lakushangaza hadi Mkataba unamilizika (miaka miwili iliyopita) hakuna malipo yoyote yaliyofanyika ambapo hadi kamati inapokea mijubu ya hoja hii deni hilo limefikia shilingi milioni 7,000,000/- licha ya kwamba mashine inayotumika katika Mtambo huo iliharibika na mmiliki huyo kuamua kuweka mashine nyengine. Hata hivyo, matengenezo hayo yamefanyika bila ya kuwepo makubaliano ya maandishi baina ya Wakala na Mkodishwaji hususan katika utaratibu wa kujifidia gharama zake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wakala uhakikishe unafuatilia na kusimamia ipasavyo madeni inayodai katika kiwanda cha kokoto Makaunduchi ili yaweze kulipwa na kuongeza mapato ya Serikali.
2. Wakala uhakikishe unakuwa makini hususan wanapojibu hoja za Mdhibiti ili majibu yao yatoe taswira halisi katika utendaji wao.

## Hoja nambari 6.1.6.2: Kutokuwasilishwa mapato yatokanayo na Ushauri Elekezi katika Mfuko MkuuwaHazina shilingi 186,906,960

Baada ya kupitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka za Wakala wa Majengo Zanzibar, ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Majengo Zanzibar hawakuweza kuwasilisha jumla ya mapato ya shilingi186,906,960 yatokanayo na Ushauri Elekezi katika Mfuko Mkuu wa Hazina kama taratibu na sheria za fedha zinavyoelekeza hadi kufikia mwisho wa mwaka husika.

Kutokuwasilisha mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina kunaweza kusababisha upotevu wa mapato na kufanya matumizi ya fedha hizo kinyume na malengo yaliyokusudiwa. Aidha, ni kwenda kinyume na Kanuni nambari 23(4) ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba mapato yote yanayokusanywa yanawasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mujibu wa sheria za fedha husika. HESABU NAMBARI 0406729000

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

Kwa kuwa Fedha hizi zilikuwa kwa ajili ya Ushauri elekezi, hivyo zilitumika kwa shughuli za kusimamia miradi mfano kuwalipa watoa huduma, ununuzi wa mafuta, safari za

wasimamizi wa mradi. Aidha, baada ya kuungaunishwa na ZanMalipo Wakala wa Majengo ilikusanya Mapato kupitia “Control Number” na ziliingizwa katika Hesabu ya Mapato ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na hazipitishwi kwenye nambari yeyote ya Hesabu za Wakala.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba Wakala haukujibu hoja ya Mdhibiti iliyotaka uwasilishwaji Hazina mapato yanayotokana na chanzo cha Ushauri Elekezi. Hivyo, Kamati haikuridhishwa na majibu yaliyotolewa kwa vile Wakala ulishindwa kufuata taratibu na Sheria zinavyoelekeza kwamba Mapato yakishakusanywa yaingizwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali halafu Wakala ulitakiwa kuziomba na kutumia kwa mujibu wa Mpango waliojipangia. Kwa mnasaba huo, Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi lakini changamoto hiyo kwasasa tayari imesharekebishwa kwa vile fedha inalipwa kupitia Mfumo wa ZanMalipo.

Sambamba na hilo, Kamati imebaini kwamba changamoto hiyo imejitokeza kutokana na kuwa Wakala hauna Sera ya Ushauri Elekezi au muongozo wa mgawanyo wa fedha wanazokusanya (uliopata baraka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango) kwa vile ungeweza kueleza wazo asilimia ya mapato ambayo Wakala una mamalaka nayo kuyatumia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wakala uache kufanya matumizi ya mapato yake kwa mazoea na uhakikishe mapato yote unayoyakusanya yanaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kama inavyoelekeza Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sio kufanya maamuzi ya kuzitumia fedha hizo.
2. Wakala kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango uhakikishe unaandaa sera au muongozo wa matumizi ya fedha wanazokusanya ili hoja za matumizi kinyume na utaratibu isiweze kujitokeza tena.

## Hoja nambari 6.1.6.3: Fedha ambazo hazikutumika katika mwaka wa fedha husika shilingi 15,661,240

Kwa mujibu wa kifungu nambari 52(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaelezea kwamba “Bakaa ya matumizi ambayo haikutumika hadi mwisho wa mwaka wa fedha huo zitalipwa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 15,661,240 ambazo ni fedha taslim hazikutumika katika mwaka wa fedha 2021/2022 bila ya kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, ukaguzi umeshindwa kupata ufafanuzi juu ya matumizi ya fedha hizo au kama zimetengwa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya matumizi ya mwaka unaofuata kulingana nataratibu na miongozo ya sheria ya fedha husika.

Kutokutumika fedha hizo katika kipindi husika na kutoingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Majengo kuhakikisha kwamba bakaa ya fedha ambazo hazikutumika katika mwaka husika wa fedha zinawasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria husika ili kuweza kupata uhalali wa matumizi hayo kwa mwaka unaofuata.

### Majibu ya Uongozi wa Wakala

Fedha zilizotajwa ambazo ni shilingi 15,661,240.00 ziliombwa kwa matumizi ya uendeshaji wa Mradi wa Usimamizi wa Ujenzi wa kituo cha Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevywa kilichopo Kidimni ambazo zililipwa na Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevywa kwa usimamizi wa kazi yao kupitia nambari ya hesabu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

Hata hivyo, fedha hizi ziliingizwa ZBA mwezi wa mwisho wa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo zilipangwa kutumika kwa muda usiopungua miezi mitatu kwakuwa kulikuwa na umuhimu na uharaka wa kituo hicho, hivyo basi, Wakala iliziomba fedha hizo ili kuendesha shughuli za usimamizi wa mradi, na kuzirudisha Wizara ya Fedha zingekwamisha shughuli nzima za usimamizi wa mradi huo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu ya hoja hiyo kwa hayakuakisi matakwa yake. Hata hivyo, Kamati imebaini Wakala haukufuata taratibu za urejeshwaji fedha zilipitiwa na mwaka wa fedha Kama inavyoelekezwa na Sheria na kuamua kufanya matumizi yasiyokubalika kisheria. Kwa mnasaba huo, Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wakala wa Majengo uhakikishe kwamba bakaa ya fedha ambazo hazikutumika katika mwaka husika wa fedha zinawasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria husika ili kuweza kupata uhalali wa matumizi hayo kwa mwaka unaofuata.

## Hoja nambari 6.1.6.4: Dosari katika udhibiti wa matumizi ya mafuta shilingi 8,049,760

Kwa mujibu wa barua yenye kumbu kumbu namba CAB.41/112/01/31 ya tarehe 14 Septemba 2022 kutoka Afisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora imetoa muongozo wa utoaji wa mafuta ya gari kwa viongozi wateule wa Serikali na kuelezea ya kwamba kwa mujibu wa toleo lenye kumbukumbu namba CAB.40/158/01/41 la tarehe 25 Oktoba 2013 limeainisha viongozi mbali mbali ambao wanastahiki kulipwa posho la mafuta kulingana cheo cha kiongozi husika.

Aidha, posho hilo hulipwa nje ya mshahara na kusomeka kama ni posho la mafuta ambalo hulipwa moja kwa moja katika vocha za mshahara za kila taasisi kupitia nambari ya hesabu ya muhusika "Personal Account Number" na sio katika "other charge" ya Wizara/Taasisi. Hivyo viongozi waliotajwa katika matoleo ya hapo juu ni wale wateuliwa wa Mhe. Rais tu na si kwa wale waliopata uteuzi wa ndani wa Taasisi zao. Kwa mnasaba huo hakuna kiongozi aliyeruhusiwa kutumia mafuta ya Afisi kwa matumizi binafsi au kwa kazi za taasisi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari ya udhibiti wa matumizi ya mafuta yanayonunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Afisi ambapo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Majengo imebainika kutumia jumla ya lita 3410 za mafuta ya Dizeli na kuyaingiza katika gari SMZ 521B ya Mkurugenzi Mkuu kinyume na miongozo na taratibu za kiutumishi.

Kutumika kwa mafuta yaliopangiwa kwa shughuli za uendeshaji wa Afisi kwa matumizi binafsi kunapelekea kuzorotesha shughuli zilizopangwa kutekelezwa jambo ambalo ni kinyume na miongozo ya matoleo ya Utumishi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Majengo kuhakikisha unatekeleza majukumu yake ya kazi kwa mujibu wa makadirio ya matumizi ya fedha walizopangiwa ili kuepusha upotevu wa fedha za umma unaotokana na matumizi mabaya ya mafuta. Mchanganuo wa matumizi ya mafuta hayo nikama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 77: Dosari katika udhibiti wa matumizi ya mafuta**

| Jina | Risiti Nambari | Tarehe | Lita | Thamanikwa Lita | Idadi ya fedha shilingi |
|---|---|---|---|---|---|
| Fadhil Juma | 23799 | 09/07/2021 | 15 | 2,182 | 32,730 |
| Fadhil Juma | 24004 | 12/07/2021 | 30 | 2,182 | 65,460 |
| Fadhil Juma | 24016 | 16/07/2021 | 20 | 2,222 | 44,440 |

| Jina | Risiti Nambari | Tarehe | Lita | Thamanikwa Lita | Idadi ya fedha shilingi |
|---|---|---|---|---|---|
| Fadhil Juma | 24022 | 20/07/2021 | 30 | 2,222 | 66,660 |
| Fadhil Juma | 24035 | 22/07/2021 | 30 | 2,222 | 66,660 |
| Fadhil Juma | 24039 | 23/07/2021 | 30 | 2,222 | 66,660 |
| Fadhil Juma | 24042 | 23/07/2021 | 30 | 2,222 | 66,660 |
| Fadhil Juma | 24048 | 26/07/2021 | 30 | 2,222 | 66,660 |
| Fadhil Juma | 24407 | 30/07/2021 | 30 | 2,222 | 66,660 |
| Fadhil Juma | 24414 | 03/08/2021 | 30 | 2,222 | 66,660 |
| Fadhil Juma | 24430 | 06/08/2021 | 30 | 2,222 | 66,660 |
| Fadhil Juma | 24438 | 09/08/2021 | 20 | 2,287 | 45,740 |
| Fadhil Juma | 24445 | 13/08/2021 | 30 | 2,287 | 68,610 |
| Fadhil Juma | 24651 | 10/08/2021 | 30 | 2,287 | 68,610 |
| Fadhil Juma | 24659 | 23/08/2021 | 30 | 2,287 | 68,610 |
| Fadhil Juma | 24665 | 25/08/2021 | 40 | 2,287 | 91,480 |
| Fadhil Juma | 24668 | 27/08/2021 | 20 | 2,287 | 45,740 |
| Fadhil Juma | 24673 | 30/08/2021 | 20 | 2,287 | 45,740 |
| Fadhil Juma | 24678 | 02/09/2021 | 30 | 2,287 | 68,610 |
| Fadhil Juma | 24683 | 02/09/2021 | 30 | 2,287 | 68,610 |
| Fadhil Juma | 24685 | 06/09/2021 | 30 | 2,287 | 68,610 |
| Fadhil Juma | 24691 | 07/09/2021 | 30 | 2,287 | 68,610 |
| Fadhil Juma | 24694 | 16/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24952 | 10/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24954 | 13/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24960 | 01/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24963 | 15/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24972 | 17/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24976 | 20/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24982 | 21/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24983 | 23/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24988 | 24/09/2021 | 30 | 2326 | 69,780 |
| Fadhil Juma | 24991 | 21/09/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |

| Jina | Risiti Nambari | Tarehe | Lita | Thamanikwa Lita | Idadi ya fedha shilingi |
|---|---|---|---|---|---|
| Fadhil Juma | 24995 | 28/09/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 24998 | 29/09/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26001 | 01/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26007 | 04/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26011 | 07/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26015 | 08/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26016 | 11/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26022 | 12/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26028 | 15/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26035 | 20/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26041 | 22/10/2021 | 40 | 2245 | 89,800 |
| Fadhil Juma | 26046 | 25/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26048 | 26/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26253 | 28/10/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26268 | 01/11/2021 | 30 | 2245 | 67,350 |
| Fadhil Juma | 26273 | 08/11/2021 | 40 | 2245 | 89,800 |
| Fadhil Juma | 26288 | 11/11/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26292 | 12/11/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26297 | 15/11/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26299 | 16/11/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26451 | 18/11/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26454 | 19/11/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26462 | 22/11/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26467 | 24/11/2021 | 40 | 2262 | 90,480 |
| Fadhil Juma | 26471 | 26/11/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26479 | 30/11/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26487 | 02/12/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26493 | 03/12/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26495 | 04/12/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26500 | 07/12/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |

| Jina | Risiti Nambari | Tarehe | Lita | Thamanikwa Lita | Idadi ya fedha shilingi |
|---|---|---|---|---|---|
| Fadhil Juma | 26705 | 08/12/2021 | 30 | 2262 | 67,860 |
| Fadhil Juma | 26709 | 28/12/2021 | 20 | 2,406 | 48,120 |
| Fadhil Juma | 26725 | 17/01/2022 | 40 | 2415 | 96,600 |
| Fadhil Juma | 26732 | 21/01/2022 | 40 | 2415 | 96,600 |
| Fadhil Juma | 26733 | 24/01/2022 | 30 | 2415 | 72,450 |
| Fadhil Juma | 26737 | 27/01/2022 | 20 | 2415 | 48,300 |
| Fadhil Juma | 26741 | 31/01/2022 | 30 | 2415 | 72,450 |
| Fadhil Juma | 26745 | 03/02/2022 | 20 | 2415 | 48,300 |
| Fadhil Juma | 26749 | 07/02/2022 | 30 | 2415 | 72,450 |
| Fadhil Juma | 28003 | 10/02/2022 | 20 | 2345 | 46,900 |
| Fadhil Juma | 28004 | 14/02/2022 | 30 | 2345 | 70,350 |
| Fadhil Juma | 28008 | 16/02/2022 | 30 | 2345 | 70,350 |
| Fadhil Juma | 28011 | 18/02/2022 | 30 | 2345 | 70,350 |
| Fadhil Juma | 28016 | 21/02/2022 | 30 | 2345 | 70,350 |
| Fadhil Juma | 28020 | 23/02/2022 | 30 | 2345 | 70,350 |
| Fadhil Juma | 28024 | 25/02/2022 | 30 | 2345 | 70,350 |
| Fadhil Juma | 28028 | 01/03/2022 | 30 | 2345 | 70,350 |
| Fadhil Juma | 28032 | 04/02/2022 | 30 | 2345 | 70,350 |
| Fadhil Juma | 28036 | 09/03/2022 | 30 | 2500 | 75,000 |
| Fadhil Juma | 28040 | 14/03/2022 | 30 | 2500 | 75,000 |
| Fadhil Juma | 28045 | 16/03/2022 | 30 | 2500 | 75,000 |
| Fadhil Juma | 28049 | 18/03/2022 | 30 | 2500 | 75,000 |
| Fadhil Juma | 29051 | 21/03/2022 | 60 | 2500 | 150,000 |
| Fadhil Juma | 29055 | 23/03/2022 | 30 | 2500 | 75,000 |
| Fadhil Juma | 29059 | 25/03/2022 | 30 | 2500 | 75,000 |
| Fadhil Juma | 29063 | 28/03/2022 | 30 | 2500 | 75,000 |
| Fadhil Juma | 20067 | 31/03/2022 | 30 | 2500 | 75,000 |
| Fadhil Juma | 29070 | 04/04/2022 | 30 | 2500 | 75,000 |
| Fadhil Juma | 29077 | 11/04/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 29081 | 13/04/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |

| Jina | Risiti Nambari | Tarehe | Lita | Thamanikwa Lita | Idadi ya fedha shilingi |
|---|---|---|---|---|---|
| Fadhil Juma | 29084 | 01/05/2022 | 40 | 2644 | 105,760 |
| Fadhil Juma | 29090 | 10/05/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 29093 | 13/05/2022 | 20 | 2644 | 52,880 |
| Fadhil Juma | 29096 | 16/05/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 30201 | 23/05/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 30207 | 26/05/2022 | 20 | 2644 | 52,880 |
| Fadhil Juma | 30210 | 30/05/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 30214 | 01/06/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 30217 | 03/06/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 30219 | 04/06/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 30220 | 05/06/2022 | 30 | 2644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 30223 | 07/06/2022 | 30 | 2,644 | 79,320 |
| Fadhil Juma | 30225 | 09/06/2022 | 20 | 2,820 | 56,400 |
| Fadhil Juma | 30226 | 13/06/2022 | 30 | 2,820 | 84,600 |
| Fadhil Juma | 30231 | 17/06/2022 | 30 | 2,820 | 84,600 |
| Fadhil Juma | 30237 | 20/06/2022 | 30 | 2,820 | 84,600 |
| Fadhil Juma | 30238 | 21/06/2022 | 30 | 2,820 | 84,600 |
| Fadhil Juma | 30240 | 22/06/2022 | 30 | 2,820 | 84,600 |
| Fadhil Juma | 30241 | 24/06/2022 | 40 | 2,820 | 112,800 |
| Fadhil Juma | 30244 | 27/06/2022 | 30 | 2,820 | 84,600 |
| Fadhil Juma | 30249 | 29/06/2022 | 35 | 2,820 | 98,700 |
| **Jumla** | | | **3,410** | | **8,049,760** |

## Majibu ya Uongozi wa Wakala

Gari yenye usajili namba SMZ 521B ni Gari inayotumika na watendaji wa Wakala ya Majengo na si kwa ajili ya Mkurugenzi, isipokuwa kilichozoeleka kwa Mkurugenzi alietangulia alikuwa akitumia gari hiyo kama gari ya Mkurugenzi wa Taasisi hii. Gari hiyo inatumika kwa kazi mbali mbali za Ofisi ikiwemo ufutiliaji wa miradi tofauti inayosimamiwa na Wakala wa Majengo na hiyo ndio gari pekee mpaka muda huu inayofanya kazi na inatumiwa na wafanyakazi wote wa Taasisi katika utendaji wa kazi zao. Kwa muda mrefu sasa tangu kupata uteuzi, Mkurugenzi wa Wakala wa Majengo anatumia gari yake binafsi kwa kazi zote anazotekeleza akiwa katika uteuzi huo. Mafuta

anayotumia ni kutoka katika posho lake la mafuta na hajawahi hata mara moja kujaza mafuta ya Ofisi katika gari lake binafsi.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika ufuatiliaji wa hoja hii, Kamati imeweza kubaini yafuatayo:-

1. Licha ya majibu ya Wakala kukanusha alichokieleza Mkaguzi lakini Kamati imepata kujua taswira halisi kwamba ni kweli gari hiyo ilikuwa ikiingizwa mafuta ya Ofisi kupitia jina la dereva wa Mkurugenzi (Fadhil Juma) kwa mara kadhaa na kuwepo uwezekanao wa kutumika kwa gari hiyo kwa shughuli za Mkurugenzi. Kwani Kamati ilitaka kujua majibu ya Wakala kupitia 'management letter' lakini kwa bahati mbaya Mdhibiti hakuwa nayo.
2. Chanzo cha Kamati kukubaliana na hoja ya Mkaguzi ni kwamba Wakala haukuwa na 'log book' ambalo lingeithibitisha Kamati utaratibu mzima wa matumizi ya mafuta kwa shughuli za kiofisi au vyenginevyo.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wakala uandae 'log book' yake ili liweze kusimamia matumizi ya mafuta kwa shughuli za kiofisi.
2. Kutokana na upungufu wa gari kwa matumizi ya Ofisi, Wakala utumie gari za Watendaji kwa utaratibu wa kuwapatia 'coupon' za matumizi ya Mafuta.

### Hoja nambari 6.1.6.5: Udanganyifu wa utumiaji wa mafuta ya petroli lita 815 katika VESPA nambari 551C ambayo ni mbovu na imehifadhiwa katika Karakana ya Saateni

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 ukaguzi umebaini jumla ya lita 815 za mafuta ya petroli yenye thamani ya shilingi 1,935,115 yametumika kupitia vespa nambari 551C kwa kuwapatia mafuta hayo Nd. Makame Omar na Ali Juma ambapo Wakala wa Majengo ikijuwa kwamba vespa hiyo ni mbovu na haifanyi kazi kwa sasa na imehifadhiwa katika karakana ya Saateni.

Kutokuwepo kwa udhibiti mzuri wa matumizi ya mafuta kunaweza kupelekea kujitokeza kwa matumizimabaya ya fedha za umma na kushindwa kufikia malengo ya utekelezaji wa kazi walizojipangia.

Aidha, kutumia mafuta kwa chombo ambacho hakifanyi kazi kwa sasa kunapelekea utumiaji mbaya wa mafuta ya Serikali na kusababisha utumiaji wa mafuta kinyume na malengo yaliyokusudiwa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 166(3)(a)

ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Majengo kuhakikisha kwamba mafuta hayatumiki kwa udanganyifu kwa kupitia chombo ambacho hakifanyi kazi ili mafuta hayo yatumike katika malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 78: Mafuta yaliyotumika kwa njia ya udanganyifu**

| Tarehe | Jina la mfanyakazi | Risiti Nambari | Lita | Thamani kwa lita | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 03/08/2021 | Makame Omar | 24419 | 40 | 2,327 | 93,080 |
| 05/08/2021 | Makame Omar | 24425 | 20 | 2,327 | 45,540 |
| 09/08/2021 | Makame Omar | 24441 | 30 | 2,379 | 71,370 |
| 10/08/2021 | Makame Omar | 24655 | 10 | 2,379 | 23,790 |
| 23/08/2021 | Makame Omar | 24662 | 35 | 2,379 | 83,265 |
| 27/08/2021 | Makame Omar | 24671 | 5 | 2,379 | 11,895 |
| 30/08/2021 | Makame Omar | 24677 | 10 | 2,379 | 25,790 |
| 08/09/2021 | Makame Omar | 24682 | 5 | 2,379 | 11,895 |
| 09/09/2021 | Makame Omar | 24697 | 35 | 2,461 | 86,135 |
| 06/09/2021 | Makame Omar | 24688 | 35 | 2,379 | 83,265 |
| 13/09/2021 | Makame Omar | 24955 | 65 | 2,461 | 159,965 |
| 16/09/2021 | Makame Omar | 24967 | 25 | 2,461 | 61,525 |
| 20/09/2021 | Makame Omar | 24979 | 30 | 2,461 | 73,830 |
| 23/09/2021 | Makame Omar | 24985 | 30 | 2,461 | 73,830 |
| 27/09/2021 | Makame Omar | 24994 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 30/09/2021 | Makame Omar | 25000 | 5 | 2,300 | 11,500 |
| 04/10/2021 | Makame Omar | 26008 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 08/10/2021 | Makame Omar | 26014 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 11/10/2021 | Makame Omar | 26020 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 15/10/2021 | Makame Omar | 26032 | 20 | 2,300 | 46,000 |
| 21/10/2021 | Makame Omar | 26040 | 20 | 2,300 | 46,000 |
| 26/10/2021 | Makame Omar | 26251 | 5 | 2,300 | 11,500 |
| 28/10/2021 | Makame Omar | 26259 | 20 | 2,300 | 46,000 |
| 03/11/2021 | Ali Juma | 26272 | 10 | 2,300 | 23,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 08/11/2021 | Ali Juma | 26276 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 09/11/2021 | Ali Juma | 26280 | 5 | 2,300 | 23,000 |
| 11/11/2021 | Ali Juma | 26289 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 15/11/2021 | Ali Juma | 26296 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 19/11/2021 | Ali Juma | 26457 | 20 | 2,300 | 23,000 |
| 23/11/2021 | Ali Juma | 26466 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 25/11/2021 | Ali Juma | 26469 | 20 | 2,300 | 23,000 |
| 30/11/2021 | Ali Juma | 26481 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 02/11/2021 | Ali Juma | 26489 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 06/12/2021 | Ali Juma | 26498 | 10 | 2,300 | 23,000 |
| 28/12/2021 | Makame Omar | 26711 | 5 | 2,420 | 12,100 |
| 03/01/2022 | Makame Omar | 26716 | 5 | 2,420 | 12,100 |
| 06/01/2022 | Makame Omar | 26719 | 5 | 2,420 | 12,100 |
| 10/01/2022 | Makame Omar | 26722 | 5 | 2,418 | 12,090 |
| 17/01/2022 | Makame Omar | 26728 | 7 | 2,418 | 16,926 |
| 24/01/2022 | Makame Omar | 26736 | 7 | 2,418 | 16,926 |
| 31/01/2022 | Makame Omar | 26744 | 7 | 2,418 | 16,926 |
| 07/02/2022 | Makame Omar | 28001 | 7 | 2,418 | 16,926 |
| 14/02/2022 | Makame Omar | 28007 | 7 | 2,295 | 16,086 |
| 18/02/2022 | Makame Omar | 28015 | 5 | 2,298 | 11,490 |
| 21/02/2022 | Makame Omar | 28019 | 7 | 2,998 | 20,986 |
| 01/03/2022 | Makame Omar | 28031 | 7 | 2,298 | 16,086 |
| 09/03/2022 | Makame Omar | 28038 | 7 | 2,459 | 17,213 |
| 21/03/2022 | Makame Omar | 29053 | 8 | 2,459 | 19,672 |
| 25/03/2022 | Makame Omar | 29061 | 5 | 2,459 | 12,295 |
| 28/03/2022 | Makame Omar | 29065 | 7 | 2,459 | 17,213 |
| 04/04/2022 | Makame Omar | 29071 | 7 | 2,459 | 17,213 |
| 11/04/2022 | Makame Omar | 29078 | 7 | 2,642 | 18,494 |
| 13/04/2022 | Makame Omar | 29080 | 3 | 2,642 | 7,926 |
| 02/05/2022 | Makame Omar | 29085 | 7 | 2,642 | 18,494 |
| 06/05/2022 | Makame Omar | 29089 | 7 | 2,642 | 18,494 |
| 10/05/2022 | Makame Omar | 29092 | 7 | 2,642 | 18,494 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 13/05/2022 | Makame Omar | 29095 | 10 | 2,642 | 26,420 |
| 16/05/2022 | Makame Omar | 29098 | 7 | 2,642 | 18,494 |
| 23/05/2022 | Makame Omar | 30203 | 7 | 2,642 | 18,494 |
| 24/05/2022 | Makame Omar | 30205 | 7 | 2,642 | 18,494 |
| 26/05/2022 | Makame Omar | 30209 | 7 | 2,742 | 18,494 |
| 30/05/2022 | Makame Omar | 30212 | 7 | 2,642 | 18,494 |
| 13/06/2022 | Makame Omar | 30228 | 7 | 2,800 | 19,600 |
| 21/06/2022 | Makame Omar | 30239 | 7 | 2,800 | 19,600 |
| 27/06/2022 | Makame Omar | 30246 | 7 | 2,800 | 19,600 |
| **Jumla** | | | **815** | | **1,935,115** |

Hesabu nambari 0406703000

## Majibu ya Uongozi wa Wakala

Chombo kilichotajwa katika hoja hii ni Vespa inayotumiwa na karani wa masjala. Vespa hiyo inafanya kazi japo kuwa ina matatizo. Vespa hiyo imeshauriwa kiufundi ibadilishwe mashine, japo kuwa inatembea, na Karani huyo ameamua kutumia Vespa za Watumishi wengine kufanya kazi za ukarani.

Matumizi: Mafuta yanatolewa kwa kila wiki ni lita saba hadi kumi kwa matumizi ya masjala ambayo chombo chake ni SMZ 551C.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Watendaji wa Wakala kukanusha hoja ya Mdhibiti. Hata hivyo, Kamati kupitia uchunguzi wake imebaini yafuatayo:-

1. Kwa siku moja, vespa moja ilikuwa ikiingizwa hadi lita 65 za mafuta wakati kikawaida vespa ina uwezo wa kujaa tenki lake kwa lita nane tu.
2. Mafuta yote hayo (lita 65) yametolewa kwa risiti moja yenye namba 24955. Wakala ulieleza kwamba hili lilitokana na Watendaji walikuwa wakigawana kwa utaratibu wanaoujua wao wenyewe kupitia risiti moja kwa vyombo tofauti. Hali ambayo inatoa mwanya wa matumizi mabaya ya rasilimali ya umma (mafuta).
3. Tarehe za matumizi ya mafuta hayo zilibainisha wazi kwamba kulikuwa na udanganyifu katika matumizi ya rasilimali hiyo. Kwa mfano, tarehe 9/08/2021 yalitolewa mafuta lita 30 wakati tarehe 10/08/2021 yalitolewa mafuta ya lita 10.
4. Mafuta yaliyotolewa yalikuwa yakiingizwa katika vespa ambayo Mkaguzi aliielezea

kwamba ni mbovu na haitumiki (imelala) na kuhifadhiwa katika karakana ya Saateni.

Kwa mnasaba huo, Kamati haikukubaliana na majibu ya hoja na hatimae hoja ya Mdhibiti imebakia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Wakala wa Majengo kuhakikisha kwamba mafuta hayatumiki kwa udanganyifu kwa kupitia chombo ambacho hakifanyi kazi ili mafuta hayo yatumike katika malengo yaliyokusudiwa

## Hoja nambari 6.1.6.6: Majengo yanayotumiwa na baadhi ya viongozi na Mawizara ambayoyanahitaji matengenezo makubwa

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna baadhi ya majengo ambayo yanamilikiwa na Wakala wa Majengo ambayo yanatumiwa aidha kwa makaazi ya viongozi na kwa ajili ya Afisi za mawizara ambayo hivi sasa yapo katika hali isiyoridhisha, hivyo Wakala wanatakiwa kufanyiwa matengenezo makubwa ili kuyanusuru majengo hayo kutokuharibika zaidi.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya nyumba hizo ni mbovu sana na baadhi yao zimeshaanguka na zinahitaji kujengwa upya na baadhi ya mashine zimekufa kabisa. Kutokuyafanyia matengenezo majumba hayo kunaweza kupelekea upotevu wa raslimali za Serikali na kusababisha majanga makubwa kwa watumiaji wa majengo hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuhakikisha inatenga fungu maalum katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo itawawezesha Wakala wa Majengo kufanya ukarabati mkubwa wa majengo yote ambayo yapo katika hali ya uchakavu kwa lengo la kuwawezesha viongozi wanaoendelea kuishi katika nyumba hizo kuwa na amani ya utekelezaji wa majukumu yao kwa kuishi katika sehemu zenye hadhi kulingana na wadhifa wao.

Zifuatazo katika jadweli hapo chini ni baadhi ya nyumba ambazo ziko katika maeneo tofauti na zinahitaji kufanyiwa matengenezo ya haraka sana:-

**Jadweli Nambari 79: Majengo ya Serikali yaliyo katika hali ya uchakavu mkubwa**

| Jina la Mtumiaji Jengo | Namba ya Nyumba | Muda wa Ukodishwaji | Mkataba wa ukodishwajiJengo | Aina yaJengo | Matumiziya Jengo | Hali halisi ya Jengo hivi sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mohd H. Ismail | 2302 C | - | Hakuna mkataba | Nyumba yaflat. vuga | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wakala Wa Majengo (Jengo la Kiwanda Cha Uchongaji Workshop) | - | 02/11/2021 - 01/11/2022 20/12/2019 - 20/11/2021 | Mikataba ipo miwili (2) imepangishwa sehemu ya jengo. | Jengo lachini. Saateni | Afisi na Biashara | Jengo linahitaji matengenezo makubwa |
| Wakala Wa Majengo (Jengo LaKuhifadhia Vifaa Vya Ujenzi (Store)) | - | 08/07/2020 - 08/07/2022 01/03/2022 - 01/03/2023 | Mikataba ipo miwili (2) imepangishwa sehemu ya jengo. | Jengo la chini-Saateni | Afisi na Biashara | Jengo linahitaji matengenezo makubwa |
| Makame Mshimba | - | - | Mkataba umemalizika | Kiwanda. Makunduchi | Biashara | Mashine zimekufa |
| Khamis Juma Silima | S9A | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat Uzunguni. | Makaazi | Nyumba nimbovu |
| Jongo J. Jongo | SMZ 16 | - | Hakuna mkataba | Nyumba. ya chini --Madungu | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Mohd Kh.Faki | SMZ 117 | - | Hakuna mkataba | nyumba ya chini-Madungu | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizara ya Afya | SMZ 5 | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-ChakeChake | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizara ya Afya | SMZ 6 | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-ChakeChake | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Mhe. Salama Mbarouk | SMZ 7 | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-ChakeChake | Makaazi | Inahitaji metengenezo makubwa |
| Wizaraya Afya | SMZ 12 | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Madungu | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizaraya Afya | SMZ 11 | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Madungu. | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Abdalla | SMZ 10 | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Madungu | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizaraya Afya Zanzibar | SMZ 9 | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Madungu | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Seif S. Seif | SMZ 15 | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Madungu | Makaazi | Inahitaji metengenezo makubwa |
| Wizara ya Afya | S10A | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizara ya Afya | S10B | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizara ya Afya | S10C | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizara ya Afya | S10D | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizara ya Afya | S10E | - | Hakuna mkataba | Nyumbaya flat -Uzunguni. | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizara ya Afya | S10F | - | Hakuna mkataba | Nyumbaya flat -Uzunguni. | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Sharifa Huomud Rashid | S8A | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya chini-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji metengenezo makubwa |
| Salim Said Suleiyum | S8B | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Idd Mohd Juma | S9B | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizaraya Afya | SMZ 9D | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mrajis Wa Mahkama | SMZ 9C | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya chini-Uzunguni | Afisi | Jengo linahitaji kujengwa upya |
| Idrissa Mohd Abdalla | S 2 A | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Yahya A. Juma | S 2 B | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Abdallah. Ali | S 3A | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzunguni | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Wizaraya Afya | S 3B | - | Hakuna mkataba | Nyumbaya flat-Uzununi. | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Mohd A. Juma | S MZ 5 | - | Hakuna mkataba | Nyumba ya flat-Uzununi | Makaazi | Inahitaji matengenezo makubwa |
| Mrajis wa Mahkama | S MZ 6 | - | Hakuna mkataba | Ghorofa mbili-Uzunguni | Afisi | Jengo linahitaji kujengwa upya |
| Kiwanda Cha Kusaga Kokoto | - | - | Hakuna mkataba | Jengo la chini-Vitongoji | Biashara | Jengo linahitaji kujengwa upya |
| Kiwanda cha Uchongaji (Workshop) | - | - | Hakuna mkataba | Jengo la chini-Jadida Wete | Biashara | Inahitaji matengenezo makubwa |

## Majibu ya Uongozi wa Wakala

Wakala wa Majengo mtaji wake ni Fedha kutoka Serikalini. Kila mwaka tunapoandaa bajeti huingiza fedha za matengenezo ya nyumba zinazosimamiwa na Wakala. Kwa bahati mbaya sana fedha hizo hazipitishwi kwa kuwa gharama ni kubwa sana zitakazotumika kukarabati majengo hayo.

Hata hivyo, nyumba nyingi zinazosimamiwa na Wakala zinahitaji kuvunjwa na kujenga majengo mengine yenye tija na sio kuzikarabati na kuingiza hasara Serikalini kutokana na gharama kubwa ya ukarabati majengo hayo ambayo kazi yake ni kutoa huduma ya makaazi tu kwa viongozi na watumishi wa umma.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

1. Wakala hauingiziwi fedha za kutosha za matengenezo ya nyumba. Hali inayopelekea kushindwa kuzifanyia matengenezo na kuendelea kubakia na uchakavu uliopo.
2. Licha ya kuwepo kwa bajeti ndogo kwa Wakala lakini kwa wakati huu Wakala hauna Mpango wa mzuri wa matengenezo ya nyumba zake. Kamati imeelezwa kwamba Mpango huo ulikuwepo lakini haukuweza kutekelezeka kutokana na kuwa na bejeti kubwa na kuelekezwa kuandaa Mpango wa Uendelezwaji wa nyumba za Viongozi ziliopo Mazizini.
3. Baadhi ya nyumba hazina mikataba ya ukodishwaji wake. Hali hiyo husababisha ugumu katika kuwachukulia hatua za kisheria wapangaji wao.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango uhakikishe unaiingizia Wakala wa Majengo fedha za kutosha ili uweze kutekeleza mpango wake wa uendelezaji wa nyumba za Viongozi.
2. Wakala uandae mikataba kwa wapangaji wake ili waweze kuwachukulia hatua za kisheria iwapo kutokea kuvunjwa kwa masharti yaliyomo ndani yake.

## Hoja nambari 6.1.6.7: Madeni ya kodi za nyumba wanayodaiwa baadhi ya wapangaji shilingi19,750,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 19,750,000 zinadaiwa na Wakala wa Majengo kutoka kwa wapangaji ambao wamekodishwa nyumba na Wakala katika maeneo tofauti yaZanzibar.

Kuwepo madeni kwa muda mrefu kunaweza kupelekea kutokuwepo kwa ufanisi katika kutekeleza kazi za Wakala na kusababisha upotevu wa mapato ya kodi ya nyumba kwa Wakala. Aidha, ni kwenda kinyume na mikataba ya ukodishwaji wa nyumba hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuchukua hatua za makusudi ili kuhakikisha kwamba kodi zote zinalipwa kwa wakati ili kuondosha usumbufu wa mrundikano wa madeni kwa Wakala.

**Jadweli Nambari 80: Wapangishwaji wa nyumba zinazosimamiwa na Wakala wa Majengo**

## Unguja

| lamba ya Nyumba | Pahala ilipo nyumba | Jina la Mkodishwaji | Muda wa Mkataba | Bei kwa mwezi (Tshs) | cholipwa (Tshs) | Deni (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2802 A | Vuga | Abdalla Zubeir Marzuk | 01/03/2022 - 01/03/2023 | 100,000 | 100,000 | 500,000 | Nyumba ya kuishi na mkataba unaendelea |
| SH/KX/53J | Mazizini | Fuad Rashid Omar | 01/03/2022 -01/03/2023 | 100,000 | 600,000 | 600,000 | |
| SH/KS/53M | Mazizini | ThuwaybaKisasi | 02/11/2021 - 02/11/2022 | 100,000 | 300,000 | 700,000 | Nyumba ya kuishi na mkataba unamalizika mwezi huu |
| KS/MZ/33 | Mazizini | Ramla Twalib Omar | 05/11/2021 - 05/11/2022 | 100,000 | 100,000 | 900,000 | Nyumba ya kuishi na mkataba unaendelea |
| SH/KS/60M | Mazizini | Juma Hassan Reli | 02/11/2021 - 02/11/2022 | 100,000 | 100,000 | 900,000 | |
| 2266 | Vuga | Lulu Abdalla Shaaban | 05/11/2021 - 05/11/2022 | 100,000 | 600,000 | 400,000 | |
| SH/KS/54 | Mazizini | Masoud Kamal Basha | 02/11/2021 - 02/11/2022 | 100,000 | 700,000 | 200,000 | |
| SH/KS/29M | Mazizini | Nassir Ahmed Abdulrazak | 01/03/2022 - 01/03/2023 | 40,000 | 25,000 | 200,000 | Nyumbaya kuishi(banda) mkataba unaendelea |
| SH/KS/50M | Mazizini | Riziki Yussuf Haji | 01/03/2022 - 01/03/2023 | 100,000 | 400,000 | 200,000 | Nyumba ya kuishimkataba unaendelea |
| - | Saateni | Jumuiya ya Changamoto | 02/11/2021 - 02/11/2022 | 150,000 | 1,200,000 | 1,950,000 | Afisi ya jumuiya |
| - | Saateni | Ame Ramadhani Juma | 20/12/2019 - 20/12/2021 | 150,000 | 2,000,000 | 2,800,000 | Mlango wa bekarymkataba wake umemaliza muda |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| - | Makunduchi | Makame Mshimba Mbarouk | 03/10/2019 - 03/10/2021 | 200,000 | 200,000 | 6,600,000 | Kiwanda cha kokotomkataba wake umemaliza muda |
| - | Saateni | Hassan Khamis Burhan | 01/03/2022 - 01/03/2023 | 150,000 | 450,000 | 3,600,000 | Mlango wa dukamkataba unaendelea |
| SH/KS/49M | Mazizini | Jaffar Simai Pandu | 01/03/2022 - 01/03/2023 | 100,000 | 400,000 | 200,000 | Nyumba ya kuishimkataba unaendelea |
| **Jumla** | | | | | | **19,750,000** | |

## Majibu ya Uongozi wa Wakala

Ni kweli Wakala wa Majengo inadai fedha hizo kutoka kwa wapangishwaji wa nyumba zinazosimamiwa na Wakala.  Juhudi za kudai malipo ya fedha hizo zimechukuliwa. Aidha baadhi ya madeni yameweza kulipwa na kwa sasa kimebaki kiasi cha shilling 13,600,000.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegendua mambo yafuatayo katika ufuatiliaji wa hoja hii:-

1. Licha ya juhudi zinazochukuliwa na Wakala, bado Wakala unadai jumla ya shilingi 13,600,000 kwa wapangaji wake.
2. Baadhi ya nyumba zinadaiwa madeni yanayotokana na malimbikizo kulikosababishwa na wapangaji kushindwa kulipwa madeni yao kwa siku nyingi.
3. Kamati imeelezwa kwamba kwamba nyumba zote zinazotumiwa na watu binafsi zimerudishwa Serikalini kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina lakini kwa bahati mbaya Kamati imeshindwa kulithibitisha hilo kutokana na Wakala kushindwa kuwasilisha barua makabidhiano hayo. Sambamba na hilo, Wakala unamiliki kiwanda cha kokoto ambacho kimeshapelekwa Ofisi ya Msajili wa Hazina bila ya kuwepo barua ya makabidhiano hayo.
4. Wakala unamiliki kiwanda cha kokoto kiliopo Makunduchi ambacho kinadaiwa shilingi 7,000,000 lakini hakuna Mkataba wa ukodishwaji wake. Aidha, mashine ya usagaji kokoto ilinayoendelea kutumiwa na kiwanda hicho sio mali ya Wakala kufuatia mashine ya awali kuharibika na Mkodishwaji kuingia mashine nyengine bila ya kuwepo kwa mkataba utakaotumika kulinda maslahi ya pande zote mbili.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wakala uwe na utaraibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ili zitakapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati.
2. Uongozi wa Wakala uchukue hatua za makusudi ili kuhakikisha kwamba kodi zote zinalipwa kwa wakati ili kuondosha usumbufu wa mrundikano wa madeni kwa Wakala.
3. Wakala uwapatie Mikataba wakodishwaji wake wote ili madeni yaweze kulipwa kwa mujibu wa mikataba hiyo. Iwapo kutatokezea Mkodishwaji kushindwa kufanya malipo, Wakala uweze kuchukua hatua za kisheria.
4. Wakala unapohamisha umiliki wa mali zake uhakikishe unafuata taratibu za sheria ikiwemo kuziwasilisha mali hizo kwa Msajili wa Hazina kwavielelezo kamili.

## Hoja nambari 6.1.6.8: Dosari katika usimamizi wa Mali za Umma

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Majengo inamiliki nyumba katika maeneo mbali mbali ambazo ni chakavu na baadhi yake zinahitaji matengenezo madogo madogo na nyenginematengenezo makubwa.

Hata hivyo, zipo baadhi ya nyumba katika eneo la Mazizini ambazo kutokana na uchakavu wake Wakala wa Majengo italazimika kufanya ukarabati mkubwa au kuanza ujenzi mpya kuanzia hatua ya msingi hadi kukamilika kwa nyumba nzima jambo ambalo litatumia gharama kubwa kuweza kuzirejesha katika ubora wake.

Kutokana na hali hiyo ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kupitia Wakala wa Majengo kuhakikisha maeneo yote yenye nyumba za Serikali au viwanja vya Serikali kuwekewa hati miliki pamoja na uzio wa muda mfupi ili kuweza kudhibiti maeneo hayo kuvamiwa na wananchi kwa kujenga majengo ya kudumu na hatimae kusababisha mgogoro wa ardhi ambao hautakuwa na ulazima.

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

Wakala wa Majengo ilichukua juhudi ya kupeleka barua kamisheni ya ardhi kwa ajili ya kupimiwa na kupatiwa hati miliki.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya maelezo yaliyotolewa na Wakala kwamba wamefuatilia hatimiliki lakini Kamati haijapatiwa kielelezo chochote kinachothibitisha ukweli wa maelezo waliyoyawasilisha.

Hivyo, Kamati haikuridhika na majibu ya Wakala. Kwa msingi huo, Kamati inaungana na hoja ya Mkaguzi. Hivyo hoja hii inabakia.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wakala wa Majengo uhakikishe unafuatilia kwa karibu hatimiliki ya mali zake pamoja na kuweka uzio ili kuweza kudhibiti maeneo hayo kuvamiwa na wananchi kwa kujenga majengo ya kudumu na hatimae kusababisha mgogoro wa ardhi.

## Hoja nambari 6.1.6.9: Kuwepo magari chakavu katika Wakala wa Majengo

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imebainika uwepo wa magari chakavu yaliyohifadhiwa katika karakana ya Saateni na mengineyo katika ghala la Saateni Shaurimoyo.

Kutokana na uwepo wa magari hayo kukaa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo kumepelekea kujitokeza kwa uchakavu mkubwa jambo ambalo limepelekea kupoteza uhalisia na thamani ya gari husika bila ya kufanyiwa matengenezo ya muda mrefu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Majengo kuchukuwa hatua za haraka kuomba kibali Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya kuziuza gari hizo ili kunusuru kukosekana kwa mapato yatokanayo na uuzwaji wa mali chakavu. Mchanganuo wa magari hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 81: Uwepo wa magari chakavu yanayomilikiwa na Wakala wa Majengo

| Nam. | Aina ya Gari | Idadi | Namba ya Usajili |
|---|---|---|---|
| 1. | Gari (Jifang) | 1 | SMZ 330B |
| 2. | Gari (Hino Truck) | 1 | SMZ 329B |
| 3. | Wheel Loader 380 | 1 | SMZ 332B |
| 4. | Gari (Surf) | 1 | SMZ 681A |

### Majibu ya Uongozi wa Wakala

Wakala wa Majengo iliuchukuwa ushauri na kuufanyia kazi na kwasasa gari hizo zimeshauzwa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Ni kweli Mkaguzi alibaini kwamba kulikuwepo magari chakavu yanayomilikiwa na Wakala

wa Majengo ambayo yamekaa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo jambo ambalo limepelekea kupoteza uhalisia na thamani ya gari husika. Hata hivyo, Kamati imeridhika na utekelezaji wa hoja hii kwa vile tayari gari hizo zimeshauzwa kwa mujibu wa utaratibu. Hivyo, hoja hii imeondolewa.

## Hoja nambari 6.1.6.10: Kukosekana kwa tija inayotokana na kazi ya Ushauri Elekezi

Wakala wa Majengo ina jukumu kubwa la kutoa ushauri elekezi pamoja na kusimamia majengo ya Serikali ikiwemo uandaaji wa BOQ, michoro na kufanya ukarabati wa majengo ya Serikali.

Kutokana na mapitio ya taarifa mbali mbali, ukaguzi umebaini Wakala wa Majengo inakosa tija ya kazi inazozisimamia pamoja na zile wanazozifanya kutokana na kukosekana kwa mapato yanayoweza kuendesha usimamizi wa kazi hizo jambo ambalo linapelekea baadhi ya watendaji kukosa ari ya utekelezaji wa majukumu yao kutokana na ukosefu wa fedha za kuweza kujiendesha katika ufuatiliajiwa majukumu yao ya kila siku.

Kutokana na changamoto hiyo ukaguzi umebaini uwepo wa dosari ya mrundikano wa madeni yanayodaiwa kutoka katika Taasisi mbali mbali ambazo zimepewa huduma za ushauri elekezi au kusimamia majengo ambazo zimeshindwa kulipa gharama waliyokubaliana kulingana na ukubwa wa kazi iliyofanyika jambo ambalo limepelekea uwepo wa deni la shilingi 525,131,600 ambazo zinadaiwa kutoka katika Taasisi zilizopatiwa huduma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuhakikisha inaijengea uwezo Wakala wa Majengo kutekeleza kazi zake kikamilifu ikiwemo kuwaruhusu kisheria kutumia fedha zinazopatikana katika usimamizi na ushauri elekezi unaofanywa kwa lengo la kuzidisha ari ya kazi pamoja na kupatikana kwa tija iliyokusudiwa ya uwepo wa Wakala wa Majengo. Mchanganuo wa Taasisi zilizopatiwa huduma na zinadaiwa madeni ya muda mrefu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 82: Taasisi za Serikali zinazodaiwa madeni ya muda mrefu na Wakalawa Majengo**

| Jina la Taasisi | Kazi iliyofanyika | Jumla ya fedha ya Mkataba (Tshs) | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Bakaa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa jengo la msikiti katika kijiji kipyacha Dundua kiliopo Bumbwini. | Usimamizi wa ujenziwa msikiti huo. | 700,000 | - | 700,000 |
| Ujenzi wa jengo la Bodi ya Mapato ChakeChake Pemba. | Ushauri elekezi waujenzi wa jengo laZRB | 18,000,000 | - | 18,000,000 |
| Ujenzi wa jengo la Bo-hari ya Dawa Maruhubi Wizara ya Afya. | Ushauri elekezi waujenzi wa jengo la Bohari ya Dawa | 20,500,000 | - | 20,500,000 |

| Jina la Taasisi | Kazi iliyofanyika | Jumla ya fedha ya Mkataba (Tshs) | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Bakaa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Chake Chake Pemba Wizara ya Afya. | Ushauri elekezi wa ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto | 36,721,600 | - | 36,721,60 |
| Ujenzi wa vyuo vya Amali viliopo Makunduchi Unguja na Daya Pemba( phase 11) Wizara ya Elimu. | Ushauri elekezi kwa ujenzi wa vyuo vya amali viliopo Makun-duchi Unguja na Daya Pemba | 132,000,000 | - | 132,000,00 |
| Ukarabati wa Jengo la kulelea Watoto Maziz-ini. | Ushauri elekezi wa ukarabati wa jengo la kulelea watoto | 18,000,000 | - | 18,000,00 |
| Afisi ya Rais Katiba, Sheria,Utumishi na Utawala Bora. | Malipo ya awamu ya kwanza kazi ya ush- auri elekezi kwa ujen-zi wa jengo la Skuli ya Sheria Zanzibar. | 39,450,000 | 8,860,000 | 30,590,00 |
| Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. | Kazi ya usimamizi ka-tika ujenzi wa jengo la Afisi na maabara liliopo Maruhubi | 18,000,000 | - | 18,000,00 |
| Wizara ya Uchumi wa Buluu. | Kazi ya kuandaa ra- mani na makisio kwaujenzi wa Bwawa la Samaki . | 19,000,000 | - | 19,000,00 |
| Afisi ya Rais Kazi Uchu-mi na Uwekezaji. | Kazi za kuandaa michoro na makisioya ujenzi wa kituo cha kusarifu asali kiliopo Kizimbani | 20,642,500 | - | 20,642,50 |
| Wizara ya Afya,Ustawiwa Jamii, Jinsia na Watoto. | Kazi ya ushauri elekezi kwa ujenziwa maabara iliopoBinguni | 31,395,000 | - | 31,395,00 |
| Idara ya UhamiajiZanzibar. | Malipo ya awamuya kwanza kazi ya kuandaa michoro na makisio kwa ujenzi wa jengo la Afisi na nyumba za wafanya-kazi Chukwani | 172,882,500 | - | 172,882,50 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Bodi ya Mikopo Tanza-nia. | Kazi ya kuandaa michoro ya kugawavyumba | 2,700,000 | - | 2,700,00 |
| ZSTC | Kazi ya usimamizi kwa ukarabati wa kibanda cha mlinzi<br>,ukuta na utiaji wa boom gate katika jengo la kitega uchu-mi ZSTC Gulioni | 4, 000,000 | - | 4,000,00 |
| **Jumla** | | | | **525,131,60** |

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

Ni kweli Wakala wa Majengo inadai fedha nyingi kwa Taasisi za Serikali ambazo inazipatia huduma ya Ushauri Elekezi. Juhudi za kudai malipo ya fedha hizo zimechukuliwa kupitia Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na madeni hayo pia yaliwasilishwa Wizara ya Fedha na yanatambulika Serikalini.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Wakala unadai jumla ya shilingi 525,131,600 kama ilivyoainishwa katika hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali. Kwa kiasi kikubwa, deni hilo linarudisha nyuma ufanisi wa Wakala na iwapo Serikali haijachukua hatua madhubuti ya kulilipa deni hilo kupitia Taasisi zilizopatiwa huduma, hoja hii itaendelea kujitokeza.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe inazikata fedha hizo na kulipwa Wakala kupitia matumizi mengineyo ya Taasisi zinazodaiwa ili Wakala ujilipe kufuatia huduma ulizotoa.

## WAKALA WA MAJENGO - PEMBA

## Hoja nambari 6.1.6.11: Malimbikizo ya deni litokanalo na ukodishaji wa nyumba shilingi 43,425,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 43,425,000 ni fedha za malimbikizo ya mapato zinazotokana na huduma ya ukodishaji wa nyumba za kuishi zilizo chini ya usimamizi wa Wakala wa Majengo Pemba kwa wananchi na taasisi za

umma lakini fedha hizo hazijalipwa kwa kipindi kirefu na kubakia kama deni. Hata hivyo Wakala haijaonyesha kuchukua juhudi za ziada katika kufuatilia ulipwaji wa deni hilo. Hali hii inapelekea Wakala kutokufikia malengo yake iliyojiwekea na pia ni kuikosesha Serikali mapato ambayo yangaliweza kutumika kwa shughuli za maendeleo na kuboresha huduma za kijamii.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 30(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Majengo Pemba kuhakikisha mapato yote ya Serikali yanasimamiwa na kukusanywa kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Majibu ya Uongozi wa Wakala

Wizara kupitia Wakala wa Majengo inakiri kuwepo kwa malimbikizo ya deni litokanalo na ukodishaji nyumba shilingi 43,425,000 wakati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alipokuwa anafanya ukaguzi wake.

Hata hivyo, Wizara kupitia Wakala wa Majengo imekuwa ikichukuwa jitihada mbalimbali ikiwemo kutoa notisi kwa wapangaji wote binafsi ambao walikuwa na madeni kwa wakati huo kuhakikisha kuwa wanalipa madeni yao. Kutokana na jitihada hizo kwa sasa wananchi wote ambao walikuwa na Madeni wameshalipa madeni hayo. Wananchi hao ni Ndugu Raya Mkoko Hassan, Ndugu Seif Salim Seif na Ndugu Jongo Juma Jongo.

Kwa upande wa Taasisi za Serikali Wakala inaendelea kuchukuwa hatua za kuwasiliana na taasisi hizo kupitia vikao pamoja kuandika barua za ukumbusho kuhusu ulipaji wa deni hilo. Hata hivyo, hakuna taasisi iliyolipa licha ya kuwepo kwa baadhi ya taasisi kukiri kulipa deni hilo. Viambatanisho vinavyohusiana na majibu ya hoja hiyo vipo kwa ajili ya uhakiki.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika ukaguzi wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini mambo yafuatayo:-

1. Asilimia kubwa watu binafsi waliokodishwa nyumba za Wakala ndio waliolipa baadhi ya madeni yao.
2. Licha ya juhudi kadhaa za kuziandikia barua, Tasisi za Serikali hususan Wizara ya Afya Pemba ambazo zimepatiwa nyumba hizo hazijalipa madeni yao. Kamati imegundua kuwa Wakala umewahi kutaka kuchukua hatua ya kuwaondosha Madaktari waliokuwa wakikaa katika nyumba hiyo na Wizara ya Afya Pemba ilijibu

kupitia barua ya tarehe 5/7/2021 yenye kumbukumbu nambari AB.3/177/06/30 kwamba Wizara inatambua kuwepo kwa deni la kodi ya nyumba hizo na italipa itakapopata fedha za matumizi mengineyo, lakushangaza hadi Kamati inafuatilia hoja hiyo, hakuna fedha yoyote iliyolipwa kupunguza deni hilo.

3. Mikataba ya ukodishwaji wa nyumba hizo imekiukwa kwani inaeleza kuwa Mpangaji ndio muhusika wa malipo ya kodi lakini Wakala kwa bahati mbaya hushindwa kuwaondoa wapangaji kwa vile Afisi zao huwa zinawakingia kifua.
4. Kuna nyumba tatu nambari 26765, 26764 na 26762 zimekabidhiwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa barua nambari BE.A/32/02/124 ya tarehe 28/1/2023 kinyume na kufuata utaratibu wa makabidhiano hasa ukizingatia Msajili wa Hazina ambae kisheria ndio mmiliki wa Mali za Umma hakushirikishwa. Aidha, Mali hizo hazijaondolewa katika daftari la Mali za Ofisi.
5. Lakushangaza zaidi kuna nyumba za Wapangaji ambao wanalipa kodi zao vizuri lakini ndio walionyang'anywa nyumba hizo na kupatiwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ikiwemo nyumba ya bwana Jongo na Bwana Seif Salim.
6. Wakala unafanya kazi kwa mazoea kwani kulikuwa na malipo ambayo yalikuwa yakilipwa kwa mkupuo wakati Mkataba unataka Kila mwezi mkodishwaji afanye malipo yake. Hali hiyo imetia wasiwasi kwamba kunauwezekano mkubwa wa baadhi ya malipo hayo kutopalipwa ipasavyo.
7. Kuna uandaaji mbaya wa taarifa za malipo kwani Kamati imebaini kwamba baadhi ya taarifa iliyomo katika vitabu vya risiti zinatofautiana na tarehe iliyomo katika ya malipo yaliyomo katika ripoti. Mfano kuna risiti nambari 133148 inaoneshwa kulipwa tarehe 1/7/2021 lakini ripoti imeonesha tarehe 5/7/2021.
8. Katika kujiridhisha na majibu ya hoja hii, Kamati iliagiza kupatiwa Mikataba ya ukodishwaji, idadi ya nyumba zilizokodishwa kwa Wizara ya Afya Pemba pamoja na idadi ya nyumba zilizokodishwa kwa watu binafsi. Aidha, imetaka kuonana na Maafisa Wapangaji wa Wizara ya Afya Pemba wanaodhaminiwa na Afisi zao ili kufuatilia kwa undani.

Katika kutafuta ufumbuzi wa deni hilo, Kamati ya PAC imekutana na Afisa Mdhamini wa Wizara ya Afya siku ya tarehe 13/11/2023 ambae alieleza kwamba Wizara ya Afya inatambua uwepo wa deni la shilingi 44,320,000 linalohusiana na deni la ukodishwa wa nyumba zinazomilikiwa na Wakala wa Majengo Pemba lakini Wizara imeshatoa msimamo wake kwamba kwasasa kila Mfanyakazi anayekaa katika nyumba hizo atalazimika kulipa deni lake mwenyewe.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wakala wa Majengo Pemba uhakikishe unachukua hatua stahiki kwa wadaiwa wote waliokodishwa nyumba za Wakala wa Majengo ili waweze kulipa na Wakala uondokane na madeni ya muda mrefu.
2. Wakala uhakikishe Wakodishwaji wake wanafanya malipo kwa njia ya Mfumo ili kuepusha kukosekana kwa mapato yao kutokana na uwepo wa taarifa usio sahihi.

## Hoja nambari 6.1.6.12: Kutokutayarishwa kwa mpango wa matengenezo wa mali

Kifungu nambari 66 cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba "Kutakuwa na mpango wa matengenezo wa mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa".

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Majengo Pemba hawana utaratibu wa kutayarisha mpango rasmi wa matengenezo wa mali zilizo chini ya umiliki wake hali iliyosababisha baadhi ya nyumba wanazozimiliki kuwa katika hali uchakavu mkubwa ambapo baadhi ya majengo yake yanahitaji matengenezo makubwa au kuvunjwa kabisa na kujengwa upya. Kutokufanyiwa matengenezo kwa nyumba hizo kunaweza kupelekea maafa makubwa kwa wapangaji na uwezekano wa kuitia hasara Serikali. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuhakikisha wanaandaa mpango maalumu wa matengenezo wa mali kama sheria inavyoelekeza na kutenga fedha za kutosha katika bajeti zao za mwaka kwa ajili ya utekelezaji. Mchanganuo wa nyumba chakavu ambazo hazijaandaliwa mpango wa matengenezo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini.

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

Wizara inakiri kuwa Wakala wa Majengo haina mpango wa matengenezo wa mali wakati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alipokuwa anafanya ukaguzi wake.

Wizara imepokea ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa na Mpango wa matengenezo wa mali pamoja na kuweka fedha za kutosha katika bajeti. Wakala wa majengo imepanga itatayarisha mpango wa matengenezo mali zikiwemo nyumba ambazo zinaweza kutengenezeka kwa sasa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kuhusiana na hoja ya kutokutayarishwa kwa Mpango wa matengenezo ya nyumba za Wakala, Kamati imebaini bado Wakala umelala kwani hawajaandaa mpango huo ambao ungewasaidia wao katika uimarishaji wa nyumba zao hususan muda watakaopata fedha. Aidha, ungeisaidia Kamati kuweza kuishauri Serikali vipi itausaidia Wakala huo. Hivyo, Kamati imetoa miezi mitatu Wakala uhakikishe unaandaa mpango huo muhimu.

Aidha, Kamati imebaini kuna mgongano wa majukumu katika ya Shirika la nyumba ambalo ndilo lenye Mamlaka ya ukodishwaji wa nyumba hizo yapo Shirika la Nyumba (ZHC) na sio Wakala wa Majengo (ZBA) ambao wao hushughulikia zaidi utalaamu wa masuala ya vipimo, michoro na majengo kwa ujumla wake. Hivyo, Kamati imegundua kuwa uwepo wa mgongano huo unaupelekea Wakala huu kuwa na nyumba kidogo, mbovu, kodi kuwa ndogo na hakuna fedha inayobakia kwa ajili ya matengenezo kwa vile fedha zote za makusanyo huenda Serikalini na kutegemea ruzuku.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Wakala wa Majengo Pemba uhakikishe unaanda Mpango wa matengenezo wa nyumba zake ili kuzinusu na uharibifu na kuuwezesha Wakala kuzifanyia matengenezo kwa awamu.

## Hoja nambari 6.1.6.13: Kutokuuzwa au kufanyiwa matengenezo kwa gari chakavu

Kwa mujibu wa kifungu namba 66 cha Sheria ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma namba 6 ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba “Kutakuwa na mpango wa matengenezo wa mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa”. Aidha kifungu cha 69(1)(2) kinaeleza kuwa “Kutakuwa na mpango wa uondoaji wa mali wa mwaka utakaoandaliwa na kila taasisi ya umma na kuwasilishwa katika Afisi ya Msajili wa Hazina”. Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika Afisi kwa ajili ya kuondoa mali za Umma.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Majengo ya Serikali - Pemba inamiliki gari aina ya Canter Tone 1.5 yenye namba za usajili SMZ 124B ambayo ni mbovu na ipo gereji kwa muda mrefu sasa bila ya kutengenezwa au kuuzwa. Hali hii inaweza kupelekea gari hiyo kushuka thamani hivyo Serikali kushindwa kunufaika nayo wakati ingeweza kunufaika iwapo Wakala ingeamua kuifanyia matengenezo au kuiondoa mapema inavyowezekana. Kutokuifanyia matengenezo gari hiyo au kushindwa kuiondoa

ni kwenda kinyume na vifungu namba 66 na 69(1)(2) vya Sheria ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma namba 6 ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuhakikisha wanaweka mpango mzuri wa matumizi wa mali zake ikiwa ni pamoja na mali zilizochakaa au kuharibika kwa muda mrefu kuzitengeneza au kuziombea ruhusa kutoka katika Afisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kuondolewa.

### Majibu ya Uongozi wa Wakala

Wizara kupitia Wakala wa Majengo inakiri kuwa kutokuuzwa au kufanyiwa matengenezo kwa mali chakavu ni kwenda kinyume na kifungu na namba 66 na 69 cha Sheria ya Msajili wa Hazina.

Hata hivyo, Gari aina ya canter ton 1.5 yenye namba za usajili SMZ 124 B ambayo ni mali ya Wakala wa Majengo ni mbovu sana na haiwezi kutengenezeka.

Hivyo, Wizara kupitia Wakala wa Majengo imeshachukuwa hatua mbalimbali ikiwemo kuandika barua za kuomba kuondoshwakwa gari hio kwa vipindi tofauti pamoja na juhudi hizo hadi sasa gari hiyo ipo na haijaondoshwa.

Nakala za barua za kuomba kuondoshwa gari hiyo zipo kwa ajili ya ukaguzi.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini yafuatayo katika ufuatiliaji wa hoja hii:-

1. utaratibu wa kisheria wa kuiondosha gari haujafuatwa ipasavyo. Hili limebainika kupitia barua zao maombi ya kuuzwa kwa gari hilo yaliyofanywa na Wakala kupitia Mratibu kumuandikia Afisa Mdhamini. Barua zote zilizowasilishwa zinaonesha hivyo badala ya Afi
2. Afisa Mdhamini kumuandikia Katibu Mkuu ili aweze kuiomba Bodi ya Zabuni kukutana na kubariki uuzwaji wa gari hilo.
3. Miongoni mwa barua hizo ni ya tarehe 20/12/2016 yanye kumbukumbu nambari WUMU/WMP/V.10/1/97, tarehe 8/2/2017 yenye kumbukumbu WUMU/WMP/V.10/1/101, tarehe 19/11/2019 yenye kumbukumbu nambari WAMNN/WMP/V.10/8 na barua ya tarehe 24/2018 yenye kumbukumbu nambari WUMU/WMP/V.10/2/1.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wakala uhakikishe unafuata utaratibu uliowekwa Na Sheria ya Ununuzi na Uondoaji WA Mali za Umma, Nambari 11 ya 2016 wanapotaka kuuzwa na kuondoa mali zao zilizochakaa.

## Hoja nambari 6.1.6.14: Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato

Wakala wa Majengo - Pemba ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 47,840,000 kupitia vianzio vyake mbalimbali vya mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Wakala ilikusanya jumla ya shilingi 13,110,000 sawa na asilimia 27.4 ya makadirio. Kutokana na kutokufikiwa kwa lengo lililokusudiwa ukaguzi umebaini hali hiyo imechangiwa na upatikanaji mdogo wa fedha unaotokana na kushindwa kusimamia vyema vyanzo vyao vya mapato.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Majengo - Pemba kuchukuwa jitihada za makusudi katika kusimamia upatikanaji wa mapato ili kuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato.

### Majibu ya Uongozi wa Wakala

Ni kweli wakati wa ukaguzi kulionekana kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato ambapo tulipangiwa kukusanya jumla ya TSH 47,840,000 na tumefanikiwa kukusanya jumla ya TSH 13,110,000. Upungufu wa makusanyo ulitokana kuwa chanzo kikuu cha mapato kwa Wakala wa Majengo ni huduma ya ushauri elekezi ambapo kwa wakati huo hakukuwa na kazi nyingi tulizozitarajia kuzipata kwa ajili kutoa huduma za Ushauri Elekezi. Pia vifungu vyengine ambavyo ni sehemu za vianzio vya mapato ni chakavu kiasi ambacho havikuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uchunguzi na Mapendekezo ya hoja hii unalingana na uchunguzi na Mapendekezo yaliyotolewa katika hoja nambari 6.1.6.11.

# 7.0 UKAGUZI WA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## 7.1.2 MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

## Taarifa ya Mapato

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Bodi ya Mapato Zanzibar ilikadiriwa kukusanya shilingi 525,095,095,633 kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Bodi ya Mapato Zanzibar imekusanya jumla ya shilingi 374,460,319,449 sawa na asilimia 71.3 ya makadirio.

Aidha, mapato yameonekana kupungua kwa jumla ya shilingi 29,777,068,079.13 kutoka makusanyohalisi ya shilingi 404,537,387,523.09 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 sawa na asilimia 7 ya mapato.

### Majibu ya uongozi wa Mamlaka

Upungufu huo wa mapato umetokana na makusanyo ya mwaka 2020/2021 ya shilingi 404,537,387,523.09 yalijumuisha mapato ya Mawizara yenye jumla ya shilingi 100,194,653,299.19 ambapo katika mwaka 2021/2022 mapato hayo ya Mawizara yalikusanywa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Hali hii ya kutokusanywa kwa mapato ya Mawizara ndio inayoonekana kusababisha upungufu wa mapato ya shilingi 29,777,068,079.13 baina ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022.

Ukitoa mapato ya Mawizara ya shilingi 100,194,653,299.19 makusanyo ya mwaka 2020/2021 yangekuwa ni shilingi 304,342,734,223.9 ambayo ukilinganisha na makusanyo ya shilingi 374,460,319,449 ya mwaka 2021/2022 kuna ongezeko la shilingi 70,117,585,225.1.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa kwa mwaka huo wa fedha (2021/2022) kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za uhaulishaji wa makusanyo ambao ulitakiwa utekelezwe na Mamlaka ya Mapato badala yake yakafanywa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango bila ya kuwepo ithibati/kielelezo kinachoruhusu uhaulishaji huo kufanyika.

Sambamba na hilo, Kamati imebaini imegundua kuwa utataribu unautumiwa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar katika ufungaji wake wa hesabu ni tofauti na Mashirika mengi ya

Serikali ambapo hesabu zao hufungwa kuanzia Januari hadi Disemba ya mwaka husika. Kadhalika, katika utekelezaji wa shughuli za Mamlaka na kuhakikisha uwepo wa uwazi wa makusanyo yao, Mamlaka imeanzisha utaratibu wa kufunga hesabu kwa kutumia vitabu viwili; hesabu itakayoonesha (shilingi 15,000,000,000) ikiwa ni mapato ya uendeshaji wa Mamlaka; na hesabu itayoonesha mapato yanayokusanywa na Serikali (shilingi 374,460,319,449).

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara inayohusiana na masuala ya Fedha pamoja na Mamlaka ya Mapato Zanzibar zihakikishe zinafuata kikamilifu taratibu na miongozo yote iliyopo husasan wanapotaka kufanya uhaulishaji wa makusanyo ya fedha za Serikali.

## Taarifa ya Matumizi

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Bodi ya Mapato Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 16,548,821,948 kwa ajili ya matumizi mbali mbali za Bodi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Bodi ya Mapato Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 14,641,385,420 sawa na asilimia 88.5 ya makadirio.

### Majibu ya uongozi wa Mamlaka

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Mamlaka ya Mapato Zanzibar haikuweza kupatiwa fedha zote za bajeti za matumizi kama ilivyokusudiwa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba kutokana na upungufu wa upatikanaji wa fedha, Mamlaka imeshindwa kutekeleza baadhi ya shughuli zake za kawaida pamoja na miradi ya maendeleo iliyojipangia ikiwemo ujenzi wa Ofisi na kituo vya Mamlaka, kuwajengea uwezo watendaji wao kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu, kukosekana mafunzo kwa wajumbe wapya wa Bodi ya Wakurugenzi, kushindwa kufanya ziara za kimafunzo nje ya Zanzibar, kushindwa kufanya ununuzi wa ‘software’, samani pamoja na vyombo vya usafiri vya Ofisi. Kwa msingi huo, ufanisi wa Mamlaka kwa wastani haukuwa na kuridhisha zaidi.

Sambamba na hilo, Kamati imegundua jumla ya shilingi 1,931,321,986 ziliondolewa (writing off payable) katika hesabu za Mamlaka kwa vile walikuwa na makubaliano ya utengenezaji wa mfumo wa EFMS lakini Mamlaka ilichukua maamuzi ya kuandaa Mfumo wake. Hivyo, Mamlaka haikuweza kulipa gharama hizo na kukubaliana nje ya Mahakama

kulipa kiasi kidogo cha fedha na kupelekea kiasi hicho cha fedha kuondolewa.

Kwa upande wa kupungua fedha za matumizi mengineyo (OC), Mamlaka iliwahamisha wafanyakazi wake 14 na kuwapeleka katika Taasisi mbali mbali za Serikali na kulikuwa na Wafanyakazi 7 walifikia muda wao wa kustaafu na kupelekea upungufu wa fedha za mishahara. Kufuatia maelezo hayo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

### Hoja nambari 7.1.2.1: Bajeti isiyo na uhalisia ya matumizi ya mali za kudumu

Ukaguzi umebaini Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) iliomba kubadilishiwa kwa bajeti mara mbili katika mwaka wa ukaguzi ambapo bodi ya wakurugenzi iliidhinisha maboresho ya bajeti kwa mara ya kwanza katika kikao chake cha 274 (cha kawaida) kilichofanyika tarehe 09.10.2021 ambapo shilingi 105,000,000 ziliidhinishwa kuwa mapitio ya bajeti kwa robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba 2021. Maboresho ya mara ya pili yalipitishwa na Bodi katika kikao chake Na.83 (cha dharura) kilichofanyika tarehe 15.05.2022 ambapo kiasi cha fedha cha shilingi 382,200,000 ziliidhinishwa kuwa mapitio ya bajeti kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022 (mapitio ya miezi 6).

Ukaguzi umebaini kuwa licha ya mapitio ya maboresho ya vifungu vya bajeti yaliyoombwa na kuidhinishwa mara kadhaa, bado bajeti ya matumizi ya manunuzi ya mali za kudumu ilitekelezwa isivyostahili kutokana na tofauti kubwa zilizobainika kati ya kiasi halisi kilichotumika na bajeti iliyorekebishwa ikionyesha kwamba kiasi kilichoombwa kwa ajili ya matumizi ya manunuzi ya mali za kudumu hakikutumika kikamilifu (kwa asilimia 73.75).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha kunakuwepo uhusiano mkubwa kati ya kitengo cha Ununuzi, kitengo cha fedha na idara ya watumiaji kila inapohitajika. Zaidi ya hayo, makadirio ya bajeti yanapaswa kuzingatia taarifa halisi ili kuwezesha utekelezaji sahihi wa bajeti. Mchanganuo wa taarifa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 92: Tofauti kati ya bajeti iliyorekebishwa na kiasi halisi kilichotumika katika matumizi**

| Nam. | Maelez o | Bajeti ya Awali 30.06.2022 (Tshs) | Matumizi ya Bajeti Iliyopitishwa 30/06/2022 | Matumizi Halisi | Tofauti ya Matumi zi | Tofauti (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | (Tshs) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ZRB Land | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 2. | Purchases of Server | 35,000,000 | 35,000,000 | 0 | 35,000,000 | 100 |
| 3. | Purchases of Motor Cycles | 4,600,000 | 4,600,000 | 0 | 4,600,000 | 100 |
| 4. | Purchases of Refrigerator | 1,600,000 | 1,600,000 | 0 | 1,600,000 | 100 |
| 5. | Purchases of Scanners | 31,200,000 | 31,200,000 | 0 | 31,200,000 | 100 |
| 6. | Construction of ZRB OfficePemba | 60,000,000 | 60,000,000 | 0 | 60,000,000 | 100 |
| 7. | Purchases of Air Condition | 70,000,000 | 70,000,000 | 9,049,495.65 | 60,950,504 | 87 |
| 8. | Purchases of Computer | 59,600,000 | 59,600,000 | 46,816,500 | 12,783,500 | 21 |
| 9. | Purchases of Printers | 57,000,000 | 102,000,000 | 37,112,500 | 64,887,500 | 63 |
| 10. | Purchases of Photocopiers | 8,000,000 | 8,000,000 | 0 | 8,000,000 | 100 |
| 11. | Purchases of Projector | 8,600,000 | 8,600,000 | 0 | 8,600,000.00 | 100 |
| 12. | Purchases of Pump | 1,000,000 | 1,000,000 | 0 | 1,000,000 | 100 |
| 13. | Purchases of TV | 1,500,000 | 41,500,000 | 10,000,400 | 31,499,600 | 76 |
| 14. | Purchases of Furniture/Curtains and Carpets | 139,300,000 | 139,300,000 | 45,395,300 | 93,904,700 | 67 |
| 15. | Purchase of Moving Camera | 3,000,000 | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 | 100 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 16. | Purchases of BiometricMachine | 8,000,000 | 8,000,000 | 2,616,250 | 5,383,750 | 67 |
| 17. | Purchases of Fire Equipment | 2,000,000 | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 | 100 |
| | **TOTAL** | **490,400,000** | **575,400,000** | **150,990,445** | **424,409,554** | **73.75** |

**Majibu ya uongozi wa Mamlaka**

Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar umechukuwa ushauri wa Mkaguzi Mkuuwa Hesabu za Serikali ambapo pamoja na uhaulishaji (realocation) uliofanyika ZRA haikuweza kufanya matumizi ya manunuzi ya mali za kudumu inavyostahiki kutokanana na kutokamilika kwa taratibu za manunuzi ambapo imepelekea manunuzi hayo kukamilika ndani ya mwaka 2022 - 2023. Kwa hivi sasa, vifaa hivi vimeshanunuliwa katika mwaka wa mwaka 2022 – 2023.

Aidha ZRA katika mwaka 2021 - 2022 haikuweza kupatiwa bajeti yote kama ilivyokusudiwa na kupelekea kufanya matumizi zaidi katika kazi za kawaida kulinganisha na kazi za maendeleo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kutafuta ukweli wa hoja hii, Kamati imebaini kuwa Mamlaka pamoja na kufanya uhaulishaji wa vifungu vya fedha zake lakini fedha zilizotarajiwa kutumika hazikuweza kupatikana kutokana upungufu wa bajeti. Kamati ilitaka kujua shughuli zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa katika kipindi hicho zitatekelezwaje na kuelezwa kwamba Mamlaka imeshazitekeleza shughuli hizo katika mpango wa fedha wa mwaka 2022/2023.

Hata hivyo, Kamati imehitaji kupatiwa mchanganuo wa utekelezaji wa shuguli hizo ili kujiridhisha na kupatiwa mchanganuo huo na kuiondosha hoja hii.

## Hoja nambari 7.1.2.2: Kukosekana kwa taarifa za ukaguzi wa ndani zinazohusu mwaka wa ukaguzi

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 610 vinahitaji pale ambapo wakaguzi wa nje wanataka kutegemea kazi ya wakaguzi wa ndani ili kupunguza kiwango cha uwajibikaji wa ukaguzi unaofanywa katika mwaka husika, mkaguzi wa nje atapitia na kutathmini

wigo wa kazi iliyofanywa na wakaguzi wa ndani pamoja na uwezo wa wakaguzi wa kitengo cha ukaguzi wa ndani.

Hata hivyo, katika kupitia mpango kazi wa mwaka wa kitengo cha wakaguzi wa ndani ambao uliidhinishwa na kamati ya ukaguzi na vihatarishi katika kikao cha 29 kilichofanyika tarehe 08.09.2021 na taarifa za utekelezaji wa mpango ulioandaliwa na Kitengo cha Ukaguzi wa ndani unaohusu shughuli za Bodi kwa mwaka wa ukaguzi unaoishia tarehe 30.06.2022 haukufanyika. Kwa maana hiyo ripoti za ukaguzi wa ndani kwa mwaka unaokaguliwa hazikuweza kupatikana kwa madhumuni ya ukaguzi. Imebainika kuwa Kitengo kilikuwa nyuma katika utekelezaji wa majukumu yao na hakukuwa na maelezo yanayokubalika ambayo yalitolewa ili kuhalalisha hali iliyobainishwa. Kwa maana hiyo kazi ya kitengo cha ukaguzi wa ndani haikuweza kutegemewa na wakaguzi wa nje na hivyo kuongeza wigo wa kazi kwa wakaguzi wa nje.

Usimamizi mdogo wa kamati ya ukaguzi na viashiria vya hatari vinaweza kupelekea kitengo cha ukaguzi wa ndani kufanya kazi kwa uwezo wa chini na kupelekea kudhoofisha udhibiti wa ndani wa shughuli za Bodi.

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ndicho kinachosimamia na kufuatilia utendaji wa shughuli za kila siku za Bodi ili kubaini maeneo ambayo Bodi haifanyi vizuri na kupendekeza hatua za haraka za kurekebisha. Katika suala hili, uongozi unasisitizwa kuhakikisha kuwa Kitengo kinawezeshwa katika kutekeleza majukumu yake. Maeneo yote ambayo yanazuia utekelezaji mzuri wa shughuli za Kitengo yanapaswa kutambuliwa na kutatuliwa ili kuimarisha udhibiti wa ndani wa Bodi.

Ukaguzi wa Ndani kwa mwaka wa ukaguzi umebaini kuwa kitengo kilifanya ukaguzi wake wa shughuli za Bodi za miaka iliyopita hadi Juni, 2021 ni kama inavyoonekana katika Jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 93: Ukaguzi uliofanywa na kitengo cha ukaguzi wa ndani hadi kufikia mwaka ulioishia tarehe 30.06.2022.**

| Nam | Kazi iliyofanywa | kipindi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Audit of biometric system | January- june 2021 | Audit coverage in respect of board’s activities for the pastyear |
| 2. | Audit of human resource and administration | July 2018-june 2020 | Audit coverage in respect of board’s activities for the pastyears |
| 3. | Audit of tax audit, | July 2020-june 2021 | Audit coverage in respect |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | registration and investigation department | | of board's activities for the pastyear |
| 4. | Audit of department of return processing and collection | July 2020– june 2021 | Audit coverage in respect of board's activities for the pastyear |
| 5. | Pemba sub office | July 2020-june 2021. | Audit coverage in respect of board's activities for the pastyear |
| 6. | Revenue section | July 2020-june 2021 | Audit coverage in respect of board's activities for the pastyear |
| 7. | ICT Audit | July 2020-june 2021. | Audit coverage in respect of board's activities for the pastyear |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Katika kipindi cha mwaka 2021/2022 Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kilifanya ukaguzi na kutoa ripoti za ukaguzi ambazo muda wa ukaguzi ni kuanzia Julai 2020 hadi Juni 2021. Hata hivyo tumepokea ushauri wa Mkaguzi na kwasasa kaguzi zote zinafanyika hadi kufikia muda wasasa. Kama inavyoonekana katika Jadweli linalofuata.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya sababu iliyotolewa na uongozi wa Mamlaka, hata hivyo Kamati imebaini kuwa ukaguzi kweli haukufanyika wakati wa ukaguzi kutokana na uhaba wa Wakaguzi wa ndani waliokuwepo katika mwaka 2021/2022. Kwasasa, Kamati imejiridhisha kwamba kuna Wakaguzi wanane na ukaguzi unafanyika ipasavyo. Kwa msingi huo, Kamati imeiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 7.1.2.3: Ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mkataba baada ya uamuzi wa tuzo za zabuni

Kanuni nambari 139 (1) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 inaeleza kuwa ndani ya siku ishirini na nane (28) za kalenda baada ya kutimiza masharti yote Afisa Masuuli na mzabuni wataingia mkataba rasmi wa

usambazaji wa bidhaa, utoaji wa huduma au kufanya kazi kabla ya kusainiwa mkataba.

Kucheleweshwa kwa utiaji saini wa mikataba husababisha kuchelewa kutekeleza kazi, huduma au bidhaa ndani ya tarehe zilizolengwa za kukamilika na kusababisha usumbufu kwa watumiaji na athari za gharama kwa taasisi nunuz ikiwa itatumia njia mbadala za manunuzi kama vile kufanya manunuzi ya dharura ili kupata huduma/kazi/bidhaa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuhakikisha kuwa michakato yote ya ununuzi inatekelezwa kulingana na mpango wa manunuzi. Hatua yoyote ya mchakato wa manunuzi inayosababisha ucheleweshaji wa mwenendo inapaswa kutambuliwa, kuchunguzwa na hatua za kuzuia hitilafu iliyobainika zinapaswa kuchukuliwa ipasavyo ili kuepusha athari za gharama za manunuzi kwa Bodi zinazosababishwa na mchakato mrefu wa ununuzi. Mapitio ya mchakato wa kusaini mkataba baada ya uamuzi wa tuzo ulionekana kuchukua muda mrefu kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 94: Mikataba iliyochelewa kutekelezwa baada ya tarehe ya tuzo**

| Type of Tender | Notice of intention to Award | Final award | Acceptance by the bidder | Contract signing | Bidder | Contract sumin (Tshs) | Remarks |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Supply of Printing Materials | 11.02.2022 | 22.02.2022 | 03.03.2022 | 19.05.2022 | Ms. Multi-color printers | 247,782,000 VAT exclusive | Procurement process from award date to contract signing stage took about 3 months |
| Supply of furniture | 24.05.2022 | 09.08.2022 | 15.08.2022 | 26.08.2022 | New Jarifashion | 69,779,300 VAT inclusive | Procurement process from award date to contract signing stage took about 3 months |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Supply of Food and refreshments under framework contract | 24.05.2022 | 20.07.2022 | 01.08.2022 | 07.10.2022 | Ms Ram Catering | 43,377,420(lot 1),47,380,000 (lot 2) | Procurement process from award date to contractsigning stage took about 4 months |
| Supply of Sophos Xg 3100 | 11.02.2022 | 22.02.2022<br>19.05.2022 | 01.03.2022<br>30.05.2022 | 14.06.2022 | Ms Computer centre and<br>Ms Rana Technologies | 30,302,051<br>VAT inclusive | Procurement process from award date to contract signing stage took about 3 months |
| Provision of cleaning and gardening services at ZRB office building Gombani<br>Chake Chake Pemba | 24.05.2022 | 15.07.2022 | 15.07.2022 | 25.08.2022 | AKB | 131,396,400<br>VAT inclusive | Procurement process from award date to contract signing stage took about 3 months |

## Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Miongoni mwa sababu zinazopelekea kuchelewa kwa hatua za kusaini mikataba ni pamoja na:

1) Kuchukua muda wa kufanyika kwa mapitio ya kisheria ya mikataba ya ununuzi kabla ya kusaini kwa mikataba husika. Aidha, mikataba hiyo inalazimika kupitiwa

na kitengo cha sheria cha ZRA pamoj na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

2) Kwa hali ya sasa upatikanaji wa fedha unaridhisha. Hivyo tatizo la kuchelewa kusainiwa mikataba baada ya tozo za zabuni limeondoka.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kiujumla, Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Mamlaka hiyo, ni kweli kasoro zilizobainishwa katika kitabu chake zilikuwepo. Hata hivyo, kwasasa kasoro hizo zimeshafanyiwa kazi hasa ukizingatia tayari Mamlaka imeshafanya kikao na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutatua changamoto ya kuchelewa kusaini mikataba yao. Kwa mnasaba huo, changamoto hizo zimeondoka na Kamati imeridhika na kuiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 7.1.2.4: Utekelezaji usioridhisha wa mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022

Ukaguzi ulipitia ripoti za utekelezaji wa shughuli za manunuzi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kubaini kuwa kati ya shughuli za manunuzi 57 zilizopangwa kufanywa, shughuli 24 hazikutekelezwa sawa na asilimia 42 na shughuli 33 zilitekelezwa sawa na asilimia 58. Kwa ujumla hali ya utekelezaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilionekana kutokuridhisha.

Pia ukaguzi ulipitia muhtasari wa vikao vya bodi ya zabuni pamoja mchakato wa manunuzi kwa baadhi ya zabuni ulibaini sababu kuu zifuatazo zilichangia kutotekelezwa ipasavyo kwa mpango wa mwaka wa manunuzi katika mwaka unaokaguliwa:-

**Uratibu hafifu kati ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi (PDMU) na sehemu ya fedha kuhusu utekelezaji wa zabuni:**

Hakukuwa na ushahidi wa kuonyesha ukaribu uliokuwepo baina ya kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) na kitengo cha Fedha ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa zabuni zilizopangwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka kwa kuendana na kiasi cha fedha kilichopo na kuzingatia kipaumbele kwa baadhi ya manunuzi. Kutofanyika kitendo hiki ni kinyume na agizo la bodi ya zabuni lililotolewa tarehe 13.07.2021 wakati wa kikao cha kwanza cha bodi ya zabuni ambacho kilitoa agizo kwamba kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) na kitengo cha fedha kukaa pamoja ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mpango wa ununuzi wa mwaka ulioidhinishwa.

**Uratibu hafifu kati ya kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) na idara ya watumiaji juu ya utoaji wa mahitaji ya mtumiaji/Hadidu Rejea/Vielelezo ili kuwezesha utekelezaji kwa**

**wakati wa shughuli zilizopangwa.**

Katika kupitia taarifa ya zabuni ya usambazaji wa SOPHOS XG 3100 na vifaa vingine vya ICT (rejea memo ya ndani iliyoandikwa na PDMU kwa idara ya ICT ya tarehe 23.11.2021 kukumbusha memo ya ndani ya tarehe 20.09.2021 ya utoaji wa vielelezo kwa ajili ya ununuzi wa zabuni hizo), na uhakiki wa muhtasari wa vikao vya bodi ya zabuni Na.16 uliofanyika tarehe 17.05.2022 ambapo kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) kiliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango wa mwaka wa manunuzi hadi kufikia Februari, 2022. Taarifa hiyo ya utekelezaji ilionyesha idadi ya zabuni ambazo zilikuwa bado hazijatekelezwa hadi kufikia Mei 2022 kulikosababishwa na kuchelewa au kutowasilishwa kwa mahitaji ya mtumiaji/hadidu rejea katika kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) kwa ajili ya mchakato wa zabuni.

Aidha, hali ya utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa mwaka hadi kufikia tarehe 30.06.2022 ukaguzi ulibaini idadi ya zabuni hizo ambazo hazikuweza kutekelezwa kutokana na kushindwa kwa idara ya watumiaji kuwasilisha mahitaji yao/hadidu rejea za zabuni kwa kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) licha ya kupelekewa taarifa za ukumbusho kwa idara husika kutoka katika kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) kama ilivyoagizwa na bodi ya zabuni katika kikao chake Na. 16 kilichofanyika tarehe 17.05.2022 ili kuimarisha ukamilishaji wa zabuni kwa wakati kama ilivyopangwa.

Sababu zilizoainishwa hapo juu zimesababisha kuwepo kwa shughuli nyingi za manunuzi katika mpango wa mwaka wa manunuzi ambazo zimeonekana si za uhalisia kwani nyingi ziliishia kufutwa na kupelekwa mbele katika mpango wa manunuzi wa mwaka uliofuata 2022/2023.

Utekelezaji usioridhisha wa mpango wa manunuzi wa mwaka unapelekea mpango wa manunuzi kuwa sio wa uhalisia na hivyo kuwa vigumu kutekelezwa au kutekelezwa kwa gharama kubwa ambayo ni upotevu wa mapato ya Serikali ambayo yangeweza kuwekezwa ili kupata riba kutoka kwa amana za muda mfupi. Pia kuna uwezekano mkubwa katika Idara za watumiaji kuwa hazifahamu kikamilifu jukumu lao muhimu kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa kila mwaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuhakikisha yafuatayo ili kuimarisha ipasavyo utekelezaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka:-

Maandalizi ya mpango wa ununuzi wa mwaka uwe shirikishi (pooling system). Idara za watumiaji, kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) na kitengo ya fedha zinapaswa kutekeleza shughuli zilizoratibiwa kwa ukaribu.

Kila idara ya watumiaji inapaswa kubainisha kwa uwazi mahitaji na uwezo wake katika

kufanya shughuli zilizopangwa kabla ya kupeleka mipango hiyo kwa kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) kwa hatua za utekelezaji.

Mahitaji yaliyoainishwa na hadidu rejea/vielelezo vya kutosha vya mtumiaji yanapaswa kutumwa kwa wakati katika kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU). Vile vile Kitengo cha manunuzi na ugavi (PDMU) kinapaswa kuwa na utaratibu wa kudhibiti ucheleweshaji wa utekelezaji wa mchahato wa zabuni kwa kuzikumbusha idara za watumiaji kutekeleza jukumu lao muhimu ili kuimarisha utekelezaji wa zabuni kama ilivyopangwa kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka husika. Hali ya utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 95: Hali ya Utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka 2021/22**

| Nam. | Items Not executedas per Plan | Tender No. | Estimated Amount in (Tshs) | Planned ProcurementMethod | Status of implementation | Established reasons for implementation |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | To acquire forensic ICT Hardware and Software including :2FTK 6 SMS, 2NUIX,1 MAC Acquisition andAtola Task Force | SMZ/F0111/ G/ DC/2021-22/04 | 116,269,248 | Direct Contracting | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |
| 2. | Supply and installationof UPS at ZRB Pemba and contact center | SMZ/F0111/ G/ CQ/2021~22/ 05 | 33,800,000 | Competitive Quotation | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department. |
| 3. | Supply of ICT hardware and software | SMZ/F0111/G/ NCB/2021~22/06 | 219,647,500 | National Competitive Bidding | Not implemented | Limited time to execute the tender within financial year. |

| Nam. | Items Not executedas per Plan | Tender No. | Estimated Amount in (Tshs) | Planned ProcurementMethod | Status of implementation | Established reasons for implementation |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | Supply of motor cycles | SMZ/F0111/G / MVP/2021-22/07 | 4,600,000 | Minor Value Procurement | Not implemented | The item was not available in the market |
| 5. | Supply and installationof Air Condition | SMZ/F0111/G / NCB/2021~22 /08 | 70,000,000 | National Competitive Bidding | Not implemented | Time limit to execute tender within FY |
| 6. | Supply of spare parts for ZRB Motor vehicles | SMZ/F0111/ G/ NCB/2021-22/16 | 76,020,000 | National Competitive Bidding | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |
| 7. | Supply and fixing of curtains | SMZ/F0111/ G/ CQ/2021-22/18 | 20,000,000 | Competitive Quotation | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |
| 8. | Supply and installationof car tracking system | SMZ/F0111/G / MVP/2021-22/22 | 10,000,000 | Minor Value Procurement | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |
| 9. | Supply and installationof Oracle Enterprise Edition License for ZITAS | SMZ/F0111/ G/ CQ/2021-22/23 | 50,000,000 | Competitive Quotation | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |

| Na m. | Items Not executedas per Plan | Tender No. | Estimated Amount in (Tshs) | Planned ProcurementMethod | Status of implementation | Established reasons for implementation |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 10. | Minor repairs of ZRBHQ | SMZ/F0111/ W/ NCB/2021 -22/26 | 255,000,000 | National Competitive bidding | Not implemented | Inadequate budget |
| 11. | Bulky SMS services | SMZ/F0111/NC/ MVP/2021-22/27 | 7,000,000 | Minor Value Procurement | Not implemented | |
| 12. | Fumigation services atZRB HQ and Pemba Office | SMZ/F0111/ NC/CQ/2021-22/28 | 19,500,000 | Competitive Quotation | Not implemented | Limited time to execute the tender within financial year. |
| 13. | Services of fire detective system | SMZ/F0111/NC/ MVP/2021-22/33 | 5,000,000 | Minor Value Procurement | Not implemented | |
| 14. | Provision of internalsecurity services at ZRB HQ and Pemba sub office | SMZ/F0111/ NC/ NCB/2021-22/34 | 54,000,000 | National Competitive Bidding | Implemented but unsuccessfully | Due to lackof qualified bidders hence re-advertised for execution in the next Financial year |
| 15. | Provision of Telecommunicationservices to ZRB | SMZ/F0111/ NC/DC/2021-22/36 | 114,000,000 | Direct Contracting | Not implemented | |

| Na m. | Items Not executedas per Plan | Tender No. | Estimated Amount in (Tshs) | Planned ProcurementMethod | Status of implementation | Established reasons for implementation |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 16. | Provision of Ticketing services | SMZ/F0111/ NC/ NCB/2021-22/44 | 167,760,000 | National Competitive Bidding | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |
| 17. | Supply of Mack Books | SMZ/F0111/ G/ CQ/2021-22/48 | | Competitive Quotation | Not Implemented | Inadequate budget |
| 18. | Development of Consultancy strategy | SMZ/F0111/ C/ CQ/2021-22/01 | 20,000,000 | Competitive Quotation | Not Implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |
| 19. | To support the maintenance of ZRB (CRMS License) customer relationship system | SMZ/F0111/ C/ DC/2021-22/02 | 21,137,500 | Direct Contracting | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |
| 20. | To support maintenance of ZRB Enterprise Resource Planning system-ERP | SMZ/F0111/ C/ DC/2021-22/03 | 53,625,000 | Direct Contract | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |
| 21. | To support maintenance of ZRBcontact centre | SMZ/F0111/ C/ DC/2021-22/04 | 20,000,000 | Direct Contracting | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS |

| Na m. | Items Not executedas per Plan | Tender No. | Estimated Amount in (Tshs) | Planned ProcurementMethod | Status of implementation | Established reasons for implementation |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | byuser department |
| 22. | SMS Hosting | SMZ/F0111/ C/ DC/2021-22/04 | 3,600,000 | Direct Contracting | Not implemented | Non submission of TOR/SPECS byuser department |
| 23. | To support maintenance of ZRBrevenue Portal | SMZ/F0111/ C/ DC/2021-22/07 | 50,000,000 | Direct Contracting | Not implemented | Non submission of TOR /SPECS by user department |
| 24. | To support maintenance of ZRBZITAS system | SMZ/F0111/ C/ DC/2021-22/08 | 23,040,000 | Direct Contracting | Not implemented | Non submission of TOR /SPECS by user department |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Miongoni mwa sababu kubwa zilizopelekea utekelezaji usiorisha wa mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022 ni kukosekana kwa fedha kwa asilimia 100 ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za ZRA ikijumuisha utekelezaji wa mpango wa manunuzi. Aidha, fedha zilizopatikana kwa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 baada ya kutoa fedha za mishahara ni asilimia 50.97.

ZRA itazingatia ushauri wa Mkaguzi katika utekelezaji wa zabuni zijazo na ugavi (PDMU) kwa hatua za utekelezaji.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini ni kweli kulikuwa na changamoto ya kutopatikana fedha za kutosha za utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi kama alivyoeleza Mkaguzi wakati wa ukaguzi wake. Hata hivyo, Kamati imejiridhisha kwamba fedha hizo kwasasa zinapatikana kwa wakati kufuatia kufanyika vikao vyao vya ndani kulishughulikia hilo. Kwa vile hatua ya kutatua changamoto hiyo imefanyika, Kamati haikuwa na maelezo zaidi na kuiondosha hoja hii.

## Hoja nambari 7.1.2.5: Posho zisizo na uhalali zilizolipwa kwa watumishi waliohamishiwa taasisinyingine baada ya kuteuliwa na Rais

Ukaguzi ulipitia muhtasari wa vikao vya Bodi ya Wakurugenzi Na. 279 ya tarehe 12.03.2022 na kubaini kuwa ZRB ilipokea barua kutoka kwa Serikali (Baraza la Mawaziri) yenye kumbukumbu namba BLM/102/MS/C.4/38 ya tarehe 14.02.2022 na kupokelewa na ZRB mnamo 25.02.2022 ambayo iliitaka uongozi wa ZRB kueleza sababu za kuendelea kufanya malipo ya mishahara na posho kwa watumishi waliohamishiwa kwenye taasisi nyingine za Serikali baada ya kuteuliwa na Rais jambo lililosababishaupotevu wa fedha za Serikali kupitia malipo hayo ya kiasi cha shilingi 1,063,128,250. Hali halisi kama inavyonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 96: Malipo ya posho kwa watumishi waliohamishiwa Taasisi nyengine kwa uteuzi wa Rais**

| Nam. | Jina la Mtumishi | Tarehe aliyohamishwa | Posho anayolipwa kwa mwezi (Tshs) | Idadi ya Miezi Iliyolipwa | Tarehe ya Ufuatiliaji Malipo | Jumla ya Posho lililolipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Amour Hamil Bakari | 12.03.2018 | 3,991,900 | 45 | Dec 2021 | 179,635,500 | uhakiki wa mishahara na posho za watumishi wa SMZ ili kubaini watumishi hewa. |
| 2. | Asaa Ahmad Rashid | 25.11.2010 | 3,716,900 | 127 | May 2021 | 472,046,300 | |
| 3. | Hafidh Mahfudh Haji | 12.08.2021 | 2,101,450 | 3 | Nov 2021 | 6,304,350 | |
| 4. | Seif Shaaban | 30.08.2012 | 3,716,900 | 109 | Sept 2021 | 405,142,100 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Seif | | | | | | |
| **Jumla** | | | | | | **1,063,128,250** | |

Aidha ukaguzi umeabaini kupitia barua hiyo ZRB ilitakiwa kuwachukuliwa hatua wafanyakazi wote waliohusika katika tukio la hasara. Uchunguzi zaidi juu ya suala hilo ilionyesha kuwa mnamo tarehe17.07.2020 ZRB iliandika barua yenye kumbukumbu namba ZRB/U.16/VOL.1/43 kwenda Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikiomba hatima ya watumishi waliohamishwa kwenda taasisi nyingine ambazo mishahara na marupurupu mengine yalilipwa na ZRB. Tarehe 10.08.2020 na 15.02.2021 Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilijibu hoja iliyotolewa na ZRB kupitia barua yenye kumbukumbu namba CC.174/234/20/30 na barua yenye kumbukumbu namba CCB.174/234 /02/27 kwa mtiririko huo ambapo ZRB iliagizwa kusitisha malipoya mishahara na posho nyinginezo kwa watumishi wote waliohamishwa kwenda taasisi nyingine za Serikali kama ilivyoelekezwa chini ya kifungu nambari 65(2) cha Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 na kanuni nambari 94(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 ambazo zinaeleza kuwa "Mtumishi aliyehamishwa kwenda taasisi nyingine za Serikali zaidi ya miezi kumi na mbili taarifa zote za mfanyakazi pamoja na malipo ya mishahara na posho nyingine zitahamishiwa kwenye taasisi hiyo".

Bodi ya Wakurugenzi ya ZRB ilitekeleza maagizo yaliyotolewa na Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishiwa Umma na Utawala Bora wakati wa kikao chake Na. 267 cha Machi, 2021 ambapo watumishi 22 waliohamishwa kwenda taasisi nyingine za Serikali (wasiokuwa wateule wa Rais) walisimamishwa mishahara na posho nyinginezo kutoka katika mfumo wa malipo ya mishahara ya ZRB (ZRB Payroll) kuanzia Julai, 2021 isipokuwa watumishi 3 ambao uhamisho wao ulitokana na uteuzi wa Rais kwa misingi kwamba kusimamishwa mishahara na maposho yao kunaweza kuonekana kama kushushwa cheo kutokana na viwango vya chini vinavyoweza kutumika kwa watumishi hao katika taasisi waliyohamishiwa.

Wakati wa kutekeleza suala hili, Bodi ya Wakurugenzi iliuagiza uongozi wa ZRB kuomba ushauri kutoka Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu hatima ya kuendelea kulipa mishahara na posho nyingine kwa watumishi 3 waliohamishwa kwenda taasisi nyingine za Serikali kwa uteuzi wa Rais. Hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha agizo lililotolewa na bodi katika suala hili lililotekelezwa.

Aidha, ilibainika kuwa tarehe 29.12.2021 ZRB ilipokea barua yenye kumbukumbu CAC.20/450/01/72 kutoka kwa Katibu Mkuu Afisi ya Rais ikiitaka ZRB ieleze ni kwa nini iliendelea kufanya malipo ya mishahara na posho nyingine kwa watumishi

waliohamishiwa taasisi nyingine za Serikali kwa kuzingatia uteuzi wa Rais licha ya kuagizwa na chombo husika kusitisha malipo hayo tangu tarehe 10.08.2020.

Suala hilo lililotolewa tarehe 29.12.2021 lilijibiwa na ZRB mnamo tarehe 31.12.2021 kwa kupitia baruayenye kumbukumbu namba ZRB/S.10/C/VOL.VI/26 ambapo ilielezwa kuwa sababu za kuendelea kuwalipa watumishi waliohamishwa kwa uteuzi wa Rais ulitokana na agizo lililotolewa na Katibu Mkuu- Afisi ya Rais Wizara ya Fedha na Mipango mara kwa mara likiwemo agizo lililotolewa tarehe 23.12.2021 kupitia barua yenye kumbukumbu namba CAC.20/450/01/18/24 kwa mtumishi wa ZRB ambaye aliteuliwa na Rais kuwa Mhasibu Mkuu wa Serikali katika mwaka wa ukaguzi ulioishia terehe 30 Juni, 2022 ya kwamba aendelee kulipwa na ZRB posho zote stahiki kama ilivyokuwa hapo awali.

Kutokana na mawasiliano ya hapo juu yaliyofanywa kati ya ZRB na vyombo mbalimbali vya Serikali kuhusu malipo ya mishahara na posho nyinginezo kwa watumishi waliohamishiwa kwenye taasisi nyingine za Serikali ambazo mishahara yao na malipo mengine ya posho yalifanywa na ZRB ilibainikakuwa ZRB kushindwa kutekeleza kikamilifu agizo lililotolewa na Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 10.08.2020 na 15.02.2021 na kushindwa kuwasiliana na taasisi yenye dhamana (Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora juu ya hatima ya kusimamisha mishahara na posho nyinginezo kwa watumishi 3 walioteuliwa na Rais kama ilivyoagizwana Bodi ya Wakurugenzi katika kikao chake namba 267 kilichofanyika Machi 2021 ndio chanzo cha hasara ambayo ZRB inatakiwa kulipa na kuwaadhibu watumishi wote waliohusika na suala hilo.

Imebainika pia baada ya mahojiano na watendaji walio chini ya Idara ya Rasilimali Watu na Utawala kuwa barua ya tuhuma za upotevu iliyotolewa tarehe 14.02.2022 na kupokelewa na Bodi tarehe 25.02.2022 ilikuwa bado haijajibiwa na ZRB ili kutoa maelezo ya uhalali wa hasara iliyopatikana lichaya maelekezo ya Bodi ya wakurugenzi yaliyotolewa katika kikao chake Na.279 kilichofanyika tarehe 12.03.2022.

Kutofuata maagizo yaliyotolewa na Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo ndiyo taasisi kuu ya Serikali inayohusika na masuala yote ya watumishi wa umma kuna uwezekano wa kuihusisha ZRB kuwasimamisha kazi watumishi wake waliohusika katika tuhuma hiyo iliyosababishwa na mwingiliano wa majukumu ya kazi na mawasiliano hafifu baina ya taasisi ambazoZRB anatakiwa kuripoti katika majukumu yake ya kila siku.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kujibu tuhuma zilizotolewa kuhusu upotevu wa fedha za Serikali kutokana na malipo ya posho kwa watumishi

waliohamishiwa kwenye taasisi nyingine za Serikali baada ya kuteuliwa na Rais bila kuchelewa ili kutoa ufafanuzi wa tuhuma zilizotolewa kwa lengo la kuwasaidia watumishi wake kuhusishwa katika upotevu huo kwani mazingira yaliyosababisha madai hayo yalifanyika kwa maelekezo kutoka kwa vyombo vya juu vya Serikali.

## Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mnamo tarehe 17/06/2020, Bodi ya Mapato Zanzibar ambayo kwa sasa ni Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) iliiomba Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuipatia muongozo wa malipo kwa wafanyakazi waliohamishwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar na kuendelea na kazi katika Taasisi nyengine za Serikali lakini bado stahiki zao kuendelea kulipwa na ZRA kutokana na mazingira yaliyojitokeza (barua yenye kumb. Namba ZRB/U.16/VOL 1/43 ya tarehe 17/07/2020) inahusika.

Kwa mujibu wa barua kutoka (OR) Sheria, Katiba, Utumishi na Utawala Bora yenye kumbukumbu namba CCB.174/234/02/30 ya tarehe 10/08/2020, pamoja na mambo mengine yalitolewa ufanunuzi katika majibu ya barua hiyo, ZRA ilishauria kwamba ni vyema kuchukua hatua za kuhamisha stahiki za wafanyakazi hao katika Taasisi walizohamishiwa ili kuweka ufanisi wa utekelezaji wa masuala ya kiutumishi.

Katika kusisitiza utekelezaji wa ushauri uliotolewa katika barua iliyotajwa hapo juu, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa barua namba CCB.174/234.02/27 ya tarehe 15/02/2021 ilitaka kujua hatua zilizochukuliwa kutokana na ushauri walioutoa.

Kufuatia hatua hiyo Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar uliandaa waraka maalum na kuuwasilisha katika Bodi ya Wakurugenzi wa ZRA kuhusiana na kupatiwa ridhaa ya kuhamisha stahiki za wafanyakazi wote ishirini na tano (25) waliohamishwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar wakiwemo wateule wa Rais.

Hatua ya kuwasilisha waraka huo kwa Bodi ya Wakurugenzi wa ZRA zilitokana na kwamba baadhi ya wafanyakazi hao ambao ni wateule wa Mheshimiwa Rais barua zao za uteuzi ziliagiza maslahi ya watumishi hao kuendelea kulipwa na ZRA kwa kuhofia kupungua kwa maslahi yao. Vilevile ni kutokana na msimamo wa Wizara ya Fedha wa kutaka wafanyakazi hao kuendelea kulipwa na Taasisi hii kwa kuyarejesha mafaili yao, ambayo yaliwasilishwa Wizarani hapo kama taratibu za uhamisho zinavyoelekeza. Hivyo haikuwa jambo la busara kubadilisha maagizo hayo bila kupata ridhaa ya Bodi ya Wakurugenzi.

Hata hivyo, kwa mujibu wa maamuzi ya kikao cha 267 cha mwezi wa Machi, 2021 cha Bodi ya Wakurugenzi wa ZRA, iliamuliwa kwamba jumla ya wafanyakazi 22 wanaofanyakazi nje ya ZRA kuhamishiwa maslahi yao katika Taasisi wanazofanyia kazi.

Aidha, Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar ulilifanyia kazi agizo hili mwezi April, 2021 na baadhi ya wafanyakazi hao kuhamishiwa maslahi yao mwezi Julai, 2021 hii ni kutokana na maombi yaliyowasilishwa na Taasisi zao kutokuwa na bajeti ya kutosha kwa kipindi hicho.

Kuhusiana na wafanyakazi watatu (3) ambao ni wateule wa Mheshimiwa Rais iliamuliwa kwamba, Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kwa dhamira ile ile ya kutoathiri maslahi ya viongozi hao, uwasiliane na Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora hatua ambayo kutokana na unyeti wake iliendelea kufanyiwa kazi.

Mwisho, ZRA haikuwa na lengo la kupingana na (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, kwani ilifahamu kwamba ofisi hiyo ndio yenye mamlaka ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma. Kilichojitokeza ni kwamba:-

Kwanza, Taarifa ya (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, haikuwa ni agizo ama maamuzi bali ni ulikuwa ni ushauri tu.

Pili, ZRB ililazimika kufuata maelekezo ya Mamlaka nyengine za Serikali zikiwemo maelekezo ya Katibu Mkuu Kiongozi, Mh Waziri wa Fedha na Mipango, Bodi ya Wakurugenzi ya ZRA pamoja na Viongozi wengine wa Wizara (mama) ya Fedha na Mipango.

Hata hivyo taratibu za kuhamisha maslahi ya wafanyakazi watatu (3) walibaki ambao ni wateule wa Rais, zimeshakamilishwa mnamo mwezi Julai, 2022. Aidha, ripoti kamili ya suala hili jinsi ya utekelezaji wake pamoja na vielelezo vyake barua kutoka Mamlaka hizo tayari zimeshawasilishwa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati imebaini kuwa kasoro za kulipwa Wateule wa Rais na Mamlaka ya Mapato Zanzibar lilikuwepo ambalo lilisababishwa zaidi na maamuzi yaliyoelekezwa na vikao tofauti kama ilivyoelezwa katka majibu husika. Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba kati ya Wateule wanne walioorodheshwa katika Jadweli nambari 96 linalohusiana na malipo ya posho kwa watumishi waliohamishiwa Taasisi nyengine kwa uteuzi wa Rais. Mfanyakazi mmoja (bwana Hafidh Mahfudh Haji) hakuwa katika miongoni mwa Wateule wa Rais badala yake alikuwa ni Mkurungenzi anaetokana na uteuzi wa ndani ambao haifanywi na Rais.

Kwa msingi huo, hakuwa akihusika na hoja hii ambapo Kamati ya PAC imelijadili hilo na kukubaliana kumuondoa katika orodha inayohusiana na hoja hiyo. Aidha, hata ukiangalia malipo aliyolipwa mfanyakazi huyo ni kidogo na yanatofautiana na wenzake.

Kwa upande wa Wateule watatu waliobakia, Mamlaka tayari imeshachukua hatua za kuwarudisha katika maeneo yao ya kazi na hawahusiki tena na utaratibu wa kuwalipa maslahi yao. Sambamba na hilo, Kamati imegundua kuwa wakati Mkaguzi anafanya ukaguzi wake uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar ulikuwa katika hatua za mwisho za kukamilisha utekelezaji wa hoja hii ambapo baada ya kulipatia ufumbuzi kasoro hiyo Mamlaka ilitakiwa imuarifu Mkaguzi kwa maandishi hatua walizozichukua ili kuepusha kuwepo kwa hoja kujitokeza. Kwa mnsaba huo, Kamati imeridhika na majibu ya hoja hiyo na kuiondosha.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Mamlaka ihakikishe kwamba iwapo kutakuwa na kosoro iliyobainishwa na Mkaguzi ambayo ipo katika hatua ya utekelezaji, Mamlaka ichukue hatua ya kumuandikia barua Afisi ya Mdhibiti kuhusiana na utekelezaji uliofanyika.

## Hoja nambari 7.1.2.6: Mchakato usiofaa wa Makabidhiano ya Majukumu

Mchakato wa makabidhiano ya majukumu ni kitendo cha mtu anayeacha majukumu au inampasa kuachilia majukumu kwa mtu mwingine ili mtu huyo anayechukua majukumu hayo achukue nafasi kutoka pale ambapo wa kwanza ameishia. Lengo la makabidhiano sahihi ni kuhakikisha mawasiliano sahihi ya kuaminika ya taarifa zinazohusiana na kazi katika mabadiliko ya zamu au kati ya timu na hivyo kuhakikisha uendelevu wa kufanya kazi kwa usalama na kwa ufanisi.

Ukaguzi umepitia mchakato wa makabidhiano ya majukumu yaliyofanywa kati ya maafisa wa ZRB katika mazingira mbalimbali yalidhihirisha udhaifu katika mchakato kama inavyoelezwa hapa chini.

Makabidhiano ya njia ya waraka hayakusainiwa na wafanyakazi husika ili kuthibitisha ukamilifu wa mchakato rasmi wa kukabidhi majukumu. Taarifa za makabidhiano ya majukumu kutoka kwa mfanyakazi anayekabidhi kwenda kwa mrithi hazikutayarishwa ili mrithi wa kazi ajue ni wapi pa kuanzia ili kuhakikisha mwendelezo wa kazi.

Njia isiyo sahihi ya uidhinishaji ilibainika kinyume na kanuni ya 20(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 inayoelekeza wajibu wa makabidhiano ya nyadhifa nyingine (uteuzi usio wa Rais) upelekwe kwa Afisa Masuuli wa taasisi inayohusika ili kuidhinishwa. Hata hivyo, mchakato wa makabidhiano kwa baadhi ya watumishi ulikosa ushahidi wa kupata kibali cha Mkuu wa Taasisi (Kamishna).

Makabidhiano ya majukumu yasiyozingatia mpango wa urithi yalibainika ambapo

mchakato wa makabidhiano ulifanyika kwa kuzingatia viwango sawa vya wasimamizi wa ngazi za juu (ngazi za mameneja/ukurugenzi) badala ya ngazi za juu kwenda chini kinyume na kanuni ya 20(5) ya Kanuniza Utumishi wa Umma za mwaka 2014.

Kwa kuzingatia madhaifu ya hapo juu, utendaji kazi wa kila siku wa Bodi unaweza kuvurugika kwani watumishi wanaochukua majukumu wanaweza kushindwa, kusahau au kuchelewa kutekeleza majukumu yao kwa sababu ya kukosekana kwa maelekezo sahihi kuhusu wadhifa huo. Kwa hivyo, anaweza asifanye kazi kulingana na matarajio ya uongozi. Aidha, kitendo cha kukabidhi majukumu kwa kuzingatia ngazi ya juu ya uongozi (line managers level) badala ya ngazi ya juu kushuka chini (top-downward level) huharibu mpango mzuri wa kurithishana majukumu na kupunguza ari ya kazi kwa wafanyakazi wa chini na kusababisha uzembe wa kazi na kupunguza tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha kuwa mchakato wa kukabidhiana majukumu unafanywa ipasavyo na kutiwa saini kati ya mkabidhi majukumu na mrithi wa majukumu ili kuhakikisha uendelevu na mahusiano salama na yenye ufanisi kazini. Kesi zilizobainishwa zimeonyeshwa kwenyejadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 97: Kesi zilizobainishwa kwenye mchakato wa upokeaji wa makabidhiano**

| Nafasi inayokaimiwa | Nafasi ya Anaekaimu | Tarehe ya makabidhiano | Muda wa makabidhiano | Sababu za Makabidhia no | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Revenu eand Debt Management –Head | Revenue Assurance UnitHead | 03.06.2022 | From 6.6.2022-8.06.2022 | Outside of the working stationto attend other official duties | Handover to line managers instead of immediate staff. The handing over channelled direct to the taking over staff without approval evidence of the |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | accounting officer. |
| Ag Director-(DRPC) | Manager-Taxpayers Service and Education | 08.10.2021 | From 11.10.2021-21.11.2021 | On leave | -do- |
| Manager- Tax investigation Unit | Manager-Forensic Unit | 28.02.2022 | 01.03.2022-11.04.2022 | On leave. | -do- |
| Director – (Research and Planning Department ) | Commissioner/ Manager Research and Planning (Mr. Kayombo T.Kadenge) | 27.5.2022 | 28.05.2022-07.06.2022 | On short course training (ITA) | Handing over rooting channel is well addressed. i.e. addressed to the commissioner and handled over to the immediate Subordinate. |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Katika suala la kukaimu nafasi za Uongozi zilizowazi, ZRA inafuata utaratibu kwa mujibu wa matakwa ya kifungu cha 20 (5) cha kanuni ya utumishi wa umma ya 2014 kama ilivyoonekana kwenye baadhi ya mifano iliyooneshwa na mkaguzi. Aidha, kasoro iliyojitokeza inasababishwa na kukosekana kwa watumishi wenye sifa katika Idara husika kwa baadhi ya wakati kulingana na majukumu yanayotakiwa kufanywa.

Hata hivyo, ZRA inakiri uwepo wa mapungufu kwa baadhi ya nafasi zilizokaimiwa kwa

muda mfupi kukosa idhini ya maandishi ya Kamishna Mkuu Ambapo kwa sasa Idara ya Utawala imewapatia uelewa uongozi wa ZRA juu utaratibu wa kukaimu nafasi kwa mujibu wa kanuni tajwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kuwa ni kweli kasoro hiyo ilikuwepo kama alivyoieleza Mkaguzi kwamba baadhi ya makabidhiano yalikuwa hayafanyiki ipsavyo lakini kwasasa Mamlaka tayari imeshalirekebisha hlio ambapo kuna fomu maalum imeandaliwa ambayo anayeondoka na anayekabidhiwa nafasi huwa wote kunas sehemu wanatia saini zao. Kwa mnasaba huo, hoja hii imeondolewa na Kamati.

## Hoja nambari 7.1.2.7: Kutokufanyika kwa ukaguzi kwa Walipakodi kwa kipindi kirefu

Katika kupitia tathmini ya kodi kwa ajili ya kaguzi mbalimbali za kodi zilizofanywa kwa walipakodi katika mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2022 ilibainika kuwa kaguzi nyingi zilizofanyika zilihusisha vipindi vya ukaguzi vya zaidi ya miaka mitatu nyuma na tathmini kubwa za kodi zilizotolewa. Sababuza mapungufu haya hazikuweza kuthibitishwa.

Kutokufanyika kwa ukaguzi kwa walipakodi kwa kipindi kirefu kunaweza kusababisha mzigo mkubwawa kodi kwa walipa kodi na kusababisha hasara ya upotevu wa mapato ya Serikali kwani walipakodi wengi wanaweza kushindwa kulipa kodi iliyotathminiwa na baadhi wanaweza kuamua kufunga biashara zao au kukimbia nchini. Ugunduzi wa mapema wa maeneo ya kutotii Sheria kwa walipa kodiunaweza kuzuiwa.

Mzigo mkubwa wa kodi husababisha kuongezeka kwa mizozo ya kodi ambayo inaweza kusababishaupotevu wa mapato ya Serikali ikiwa mizozo itaishia mahakamani na mlipa kodi kuamuliwa mshindi. Utaratibu huu pia huongeza usumbufu kwa walipakodi kutokana na muda unaotumika kutafuta nyaraka za ukaguzi za miaka mingi iliyopita ambapo baadhi ya taarifa hizo haziwezi kupatikana. Idadi inayohitajika ya wafanyakazi wenye sifa stahiki, uzoefu na jitihada binafsi kufanya ukaguzi kwawalipakodi kwa wakati vilikosekana jambo ambalo limekuwa ni moja wapo ya chanzo cha kulimbikiza kazi za ukaguzi.

Kwa kuwa mchango wa ukaguzi kwa walipakodi katika kuboresha utii wa Sheria bila shuruti ili kuongezamapato ya Serikali ni muhimu miongoni mwa mambo mengine Bodi ya Mapato inapaswa kutilia mkazo zaidi jukumu la ukaguzi kwa walipakodi kwa kuhakikisha kuwa ukaguzi wa kodi unafanyika kwa wakati ikiwezekana kila mwaka kwa walipakodi wakubwa na wa kati. Mifano inayohusiana na suala hili ni kama inavyoonyeshwa kwenye

jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 98: Orodha ya Ukaguzi wa Kodi uliotumika**

| Jina la MlipaKodi | Tarehe ya Tathmini | Aina ya Tathmini ya Kodi | Muda wa Ukaguzi | Makisio ya Kodi (Tshs) | Makisio ya Kodi (USD) | Idadi ya Miaka |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kisiwa Hotel And Resort Co. | Dated 22.04.2022 | VAT | 2018-2021 | 21,007,182.60 | - | 4 Years |
| Kiwengwa Club Village | Assessment No.23 Dated 31.08.2021 | Hotel Levy | 2018-2020 | 85,911,313.94 | | 3 Years |
| Langilan giBeach Bunglaw | Assessment No. 50 Dated 06.01.2022 | Hotel Levy | 2017-2021 | 38,910,960.73 | 23,327.46 | 5 Years |
| Maisha Co.Ltd | Assessment No. 53 Dated 25.01.2022 | VAT | 2018-2021 | | 75,928.47 | 4 Years |
| Merinvest Co.Ltd | AssessmentDated 31.03.2022 | Hotel Levy | 2017-2021 | | 25,215.53 | 5 Years |
| Mnarani Beach Cottages Ltd | Assessment No.36 Dated 02.11.2021 | Hotel And RestaurantLevy | 2018-2021 | | 29,800.56 | 4 Years |
| Mwamba Investment | Assessment No.54 Dated 25.01.2022 | VAT | 2018-2021 | | 36,491.28 | 4 Years |

| Jina la MlipaKodi | Tarehe ya Tathmini | Aina ya Tathmini ya Kodi | Muda wa Ukaguzi | Makisio ya Kodi (Tshs) | Makisio ya Kodi (USD) | Idadi ya Miaka |
|---|---|---|---|---|---|---|
| My Blue HotelLtd | Assessment No.35 Dated 26.10.2021 | Hotel Levy | 2017-2021 | | 329,185.04 | 5 Years |
| Neptune Hotel Zanzibar Ltd | Assessment No.55 Dated 25.01.2022 | VAT | 2018-2021 | | 82,767.17 | 4 Years |
| Ozti East Africa Co Ltd | Assessment No. 60 Dated 08.02.2022 | VAT | 2017-2021 | 71,124,905.32 | | 5 Years |
| Pongwe BeachHotel | AssessmentDated 31.03.2022 | VAT | 2014.2021 | | 461,021.64 | 8 Years |
| Pristine InvestmentLtd, (Madinat AlBahri) | Assessment No.20 Dated 26.08.2021 | VAT | 2018-2020 | 197,082,095.64 | | 3 Years |
| Zanlink Limited | AssessmentDated 06.05.2022 | Excise Duty | 2017-2021 | 7,118,973,676 | | 5 Years |
| Rock CompanyLtd | AssessmentDated 31.03.2022 | Hotel Levy | 2018-2021 | | 13,136.77 | 4 Years |

| Jina la MlipaKodi | Tarehe ya Tathmini | Aina ya Tathmini ya Kodi | Muda wa Ukaguzi | Makisio ya Kodi (Tshs) | Makisio ya Kodi (USD) | Idadi ya Miaka |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Said OmaryHaji | AssessmentDated 19.05.2022 | VAT | 2017-2021 | 87,523,397.25 | | 5 Years |
| Tanzanite Beach Resort | Assessment No.48 Dated 03.12.2021 | Hotel Levy | 2017-2021 | | 25,404.52 | 5 Years |
| Tembo HouseHotel | Assessment No.61 Dated 10.02.2022 | Hotel Levy | 2017-2021 | | 27,120.74 | 5 Years |
| Uroa Paradise Beach Ltd | Assessment No.47 Dated 01.12.2021 | Hotel Levy | 2016.2021 | | 52,843.47 | 6 Years |
| Vacanze Zanzibar Ltd | Assessment No.38 Dated 24.11.2021 | Hotel Levy | 2017-2021 | | 168,516.57 | 5 Years |
| Vodacom Tanzania Plc | Assessment No.41 Dated 26.11.2021 | VAT | 2014-2021 | 561,396,263.13 | | 8 Years |
| Vr Hotels InvestmentLtd | AssessmentDated 02.06.2022 | Hotel Levy | 2019-2021 | | 89,209.61 | 3 Years |
| Wave Resort | Assessment No.51 | Hotel Levy | 2017-2021 | 82,028,604.02 | 22,983.64 | 5 Years |

| Jina la MlipaKodi | Tarehe ya Tathmini | Aina ya Tathmini ya Kodi | Muda wa Ukaguzi | Makisio ya Kodi (Tshs) | Makisio ya Kodi (USD) | Idadi ya Miaka |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ltd(Uroa) | Dated 17.01.2022 | | | | | |
| White Sands Beach Resort Limited | Assessme ntDated 16.06.202 2 | VAT | 2018-2021 | | 113,427.0 0 | 4 Years |
| Zanzib ar Teleco m Limited | Assessme nt No.17 Dated 27.07.2022 | Vat And ExciseDuty | 2014-2020 | 860,218,998 | | 7 Years |
| Zanzibar Beach Resort | Assessmen t No.16 Dated 22.07.2021 | Hotel Levy | 2017-2020 | 218,493,853 | | 4 Years |
| Zanzibar Milling Corporatio n | Assessme nt No.49 Dated 28.12.2021 | Stamp Duty | 2019-2021 | 176,924,969 | | 3 Years |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

ZRA imeongeza idadi ya wakaguzi ambapo kwa sasa Idara ya Kodi za ndani ndani pekee ina jumla ya wakaguzi 15, Idara ya walipakodi wakubwa ina jumla ya wakaguzi 10, hivyo kufanya jumla ya wakaguzi 25, idadi ya kaguzi zinazotarajiwa kufanywa zitaongezeka maradufu kulinganisha na kipindi kilichopita, kwa mfano kwa kipindi kuanzia Julai 2023 hadi Disemba 2023 jumla ya kaguzi 106 zimeweza kukamilishwa na Idara mbili za ukusanyaji, Idara ya walipakodi za ndani imeweza kukamilisha jumla ya kaguzi 88, na idara ya walipakodi wakubwa kaguzi 18, hivyo hakutakuwa na walipakodi kukaa muda mrefu bila ya kukaguliwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kuwa ni kweli kasoro zilizoelezwa na Mkaguzi zilikuwepo ambapo zilitokana na uwepo wa wafanyakazi wachache (8) waliotakiwa kufanya ukaguzi kwa walipakodi wote na kupelekea kutofanyika kwa ukaguzi kwa zaidi ya miaka mitatu kwa Walipakodi wao Aidha, Kamati pia imebaini kuwa uhaba wa wafanyakazi huo ulichangiwa na kuondolewa kwa baadhi ya watendaji kuhamishwa ZRA na kupelekwa katika Taasisi nyengine kuendelea na majukumu yao.

Kwasasa Mamlaka imeshaifanyia kazikasoro hiyo kama ilivyoelezwa katika majibu yao na Kamati imeridhika nayo na kuiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 7.1.2.8: Taarifa ya msamaha wa riba na adhabu na malipo ya kodi inayodaiwa kwaawamu

Ukaguzi umepitia tathmini ya kodi iliyoibuliwa na mwenendo wa ulipaji na kubaini ukweli kwamba walipakodi wengi waliingia katika maombi ya msamaha wa riba na adhabu kwa mujibu wa kifungu cha 57 cha TAPA na baadhi waliongeza ombi lao la kusamehewa riba na adhabu pamoja na malipo ya awamu kwenye deni la kodi lililosalia kwa mujibu wa kifungu cha 40 cha TAPA. Hata hivyo uhakiki wa msamaha huo na malipo kwa awamu ulibaini udhaifu ufuatao:-

**Kuongezeka kwa mwenendo wa msamaha na kiasi kikubwa cha kodi kuondolewa**

Ukaguzi umepitia taarifa ya tathmini ya kodi na kiwango cha msamaha na umedhihirisha mwenendo unaoongezeka wa msamaha wa riba na adhabu na kiasi kikubwa cha kodi kufutwa. Ilibainika kuwa kuongezeka kwa mwenendo huo kulisababishwa na mzigo mkubwa wa kodi uliotokana na Idara inayohusika na ukaguzi kwa walipakodi kushindwa kufanya ukaguzi wa kodi kwa walipakodi kwa wakati.

**Misingi/vigezo vilivyotumika kutoa idhini ya msamaha/malipo ya kodi kwa awamu kulingana na kifungu cha 57 na 40 cha TAPA havikuwa bayana**

Ukaguzi ulipitia baadhi ya mafaili ya walipakodi na kubaini kuwa misingi/vigezo vilivyotumika kutoa idhini ya msamaha na ulipaji wa kodi kwa awamu kulingana na kifungu cha 57 na 40 cha TAPA havikuweza kubainishwa kutokana na ukiukwaji uliobainika wakati wa uhakiki wa baadhi ya walipa kodi waliopewa idhini ya msamaha na malipo ya kodi kwa awamu kwa mujibu wa Sheria. Mapitio yalibaini kuwa baadhi ya walipa kodi wenye sababu za msingi walinyimwa kuidhinishwa kwa maombiyao na baadhi waliidhinishwa bila kutoa sababu au kuwepo kwa mazingira ya kuhitaji idhini hiyo.

**Ratiba za malipo ya kodi kwa awamu/Makubaliano ya ulipaji kodi kwa awamu ambayo hayajatiwa saini na pande zote mbili**

Ukaguzi ulipitia malipo ya kodi kwa awamu na kubaini kuwa ratiba za ulipaji kodi kwa awamu/ makubaliano ya ulipaji kodi kwa awamu yalitiwa saini na mtumishi wa ZRB mwenye dhamana hiyo pekee; walipakodi hawakuwa wakisaini mikataba hiyo ili kuunda makubaliano ya kisheria kati ya pandezote ili kuwezesha ZRB kuchukua hatua nyingine za kisheria endapo walipakodi watakiuka mashartiyaliyokubaliwa kwani mapitio ya majalada ya baadhi ya walipakodi yalibaini baadhi yakiwa na ratiba za ulipaji kodi kwa awamu ambao walishindwa kuzingatia malipo yao kama ratiba inavyomtaka na ushahidi wa hatua zilizochukuliwa dhidi ya wakiukaji hao ulikosekana.

Kifungu cha 57 ni miongoni mwa mianya ya sheria za kodi ikiwa hatua za makusudi hazitachukuliwa kupitia upya kifungu hicho kinaweza kutumika vinginevyo kuhamasisha rushwa kati ya walipakodi na watumishi wasio waaminifu wa Bodi, kitendo ambacho kinaweza kusababisha hasara ya mapato ya Serikali kutokana na ufutwaji wa misamaha ya riba na adhabu zisizo za lazima.

Kuongezeka kwa mwenendo wa msamaha kunazua shaka ya uwezo wa wakaguzi wa kodi au kupunguza ari yao ya kazi. Uwezekano wa kutendewa isivyo haki kwa walipa kodi katika kutoa idhini ya msamaha wa riba na adhabu na malipo kwa awamu haikuweza kuthibika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha yafuatayo:-

- Ukaguzi wa kodi unafanywa kwa wakati kwa kuwa inatazamwa kama chanzo kikuu cha msamaha mkubwa wa riba na adhabu. Kufanya ukaguzi wa kodi kwa wakati kutapunguza mzigo mkubwa wa kodi kwa walipa kodi na kuongeza utii wa kodi kwa hiari.
- Sheria ya kodi (TAPA) inapaswa kupitiwa upya ikijumuisha kifungu cha 57 ili kuangalia mianya yote inayotumiwa na walipakodi katika kukwepa kodi ambayo inapunguza kwa kiasi kikubwa mapato ya Serikali.

Mikataba/ratiba za malipo ya kodi kwa awamu zinapaswa kusainiwa na pande zote mbili (ZRB na Walipakodi) ili kuwezesha ufuatiliaji wa karibu na kuchukua hatua za kisheria kama ilivyoainishwa katika Sheria ya kodi TAPA Na.7 ya 2009 (kama ilivyorekebishwa) kifungu cha 40.

**Jadweli Nambari 99: Sampuli ya Walipakodi iliyoidhinishwa na msamaha wa riba na adhabu na malipo ya ushuru kwa Awamu**

| Jina la Mlipa kodi | Nambari na tarehe ya tathmini ya Ukaguzi | Jumla ya Tathmini ya Kodi | Kiwango kilichotumika | Riba | Tozo ya Adhabu | Mapungufu yaliyobainika katika majalada ya walipa kodi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| GULF COMPA NYLTD | 38 Dated 28.10.2021 ( 2017-2020) (STAMP DUTY) | Tzs 6,176,163.11 original assessment | 4,255,980 | 1,068,987.11 | 851,196 | Sababu ya kusamehewa Tozo ya adhabu na Riba haikuelezwa kwa uwazi. |
| African Hotels and Tours Co.Ltd (High class Hotels) | 18: 2017-2020 (VAT) | TZS 73,403,898 | 46,913,304 | 17,107,934 | 9,382,661 | Mlipakodi alituma maombiya punguzo mara kadhaa ya Riba na adhabu kwa barua ya tarehe 31.03.2022 na tarehe 26.09.2022, hata hivyo maombi yao yalikataliwa na kutakiwa kulipa deni lote. |
| VODACOM | 41 (2014- 2021) (VAT AND EXCISE DUTY) | TZS 561,396,263 | 189,736,723 | 333,712,195 | 37,947,344 | Ukaguzi wa kodi ulijumuisha kipindi cha miaka minane na kubaini mzigo mkubwa wa madaiya Riba na adhabu umepelekea msamaha wa kodi hadi kufikia |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | shilingi 185,829,769.71 |
| SUNSHINE | | USD 212,012 | 148,119.12 | 34,269.28 | 29,623.82 | Kiwango cha Riba na adhabu kilichosamehewa kilifikia USD 46,758.46 na bakaa ya USD 155,253.76 kutakiwa kulipwa kwa kipindi kisichozidi miezi 12 bila ya kuwepo kwa makubaliano ya mkataba. |
| MY BLUE BOUTIQUE | No.35 26.10.2021 | USD 329,185.14 | 215,144.15 | 71,012.16 | 43,028.83 | Mlipakodi aliomba kufanya malipo tarehe1 Novemba 2021 na alikubaliwa kwa barua ya tarehe 04.11.2021 kwa malipo ya awamu 6 ya USD 329,185.04 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | kutoka novemba 2021 hadi April2022. |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

ZRA imeshasawazisha suala hilo kwa kuweka vitengo vya Ukaguzi na Madeni kwa kila Idara ya Ukusanyaji. Lengo ni kuhakikisha waliapakodi wanakaguliwa kwa wakati na kudaiwa kodi isiyotokana na ukaguzi wa muda mrefu. Hatua hii itaondosha kuwepo kwa wasiokaguliwa kwa kipindi kirefu na kuwepo kwa malimbikizo ya madeni. Aidha hatua hiyo itaondosha kuwepo kwa malimbikizo ya madeni yanayoombewa msamaha wa kodi.

Msamaha wa kodi na malipo ya kodi ya awamu yanatekelezwa kupitia Sheria ya usimamizi wa kodi (TAPA No: 7 ya mwaka 2009) kifungu cha 40. Kwa mujibu wa sheria hio malipo ya awamu yanafanywa kupitia mikataba na misamaha inatolewa kupitia ridhaa ya Kamishna Mkuu. Ridhaa ya msamaha wa adhabu na Riba inatolewa kuzingatia sababu za msingi zilizothibitishwa na kitengo cha madeni na kuwasillishwa mapendekezo kwa Kamishna Mkuu. Miongoni mwa sababu hizo ni kama zilivyoainishwa katika miongozo ya utendajikazi wa divisheni ya madeni ambazo ni:-

1) Namna ya ulipaji kodi wa mlipakodi.
2) Hali ya kiuchumi wa mlipakodi.
3) Namna mlipakodi anavyosaidia jamii
4) Sababu nyengine yoyote ambayo Kamishna ataiona inafaa.

Kwa sasa makubaliano ya ulipaji kodi kwa awamu yanatiwa saini na mtumishi wa ZRA mwenye dhamana hiyo pamoja na mlipakodi aliye ruhusiwa na Kamishna Mkuu kufanya malipo kwa awamu ndani ya kipindi maalum ili kuunda makubaliano ya kisheria kati ya pande zote mbili.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli changamoto hiyo ilikuwepo na kupelekea kujitokeza kwa hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo Kamati imejiridhisha na hatua zilizochukuliwa na uongozi wa Mamlaka ambapo hivi sasa msamaha wa riba na adhabu umewekewa vigezo maalum ikiwemo kuwepo kwa maombi ya mlipa kodi, kutathminiwa

kwa hali ya uwajibikaji wa Mlipa kodi, mchango wa Mlipa kodi kwa maendeleo ya jamii pamoja na kuwepo hali ya mazingira magumu ya kibiashara yanayoweza kupelekea Mlipa kodi kufilisika.

## Hoja nambari 7.1.2.9: Ukaguzi na upelelezi kwa walipakodi unachukua muda mrefu zaidi kukamilika

Ukaguzi ulipitia taarifa mbalimbali za ukaguzi na upelelezi kwa walipakodi uliofanywa kwa walipakodi mbalimbali katika mwaka na kubaini kuwa mchakato wa ukaguzi na upelelezi ulichukua muda mrefu kukamilika yaani kuanzia tarehe ya kuanza kazi hadi tarehe ya kutoa tathmini ya kodi. Hata hivyo, ushahidi wa kuhalalisha sababu za mchakato mrefu wa ukaguzi na upelelezi uliobainika haukuwepo. Aidha, hapakuwa na ushahidi kwamba idara imeweka kigezo cha muongozo wa muda wa kufanya/kukamilisha kaguzi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba kila ukaguzi unakamilika kwa wakati.

Muda mrefu wa ukaguzi/upelelezi wa kodi husababisha kuchelewa kutoa tathmini na ukusanyaji wa kodi kwa wakati jambo ambalo linaweza kuathiri makadirio ya mapato ya Serikali.

Kuna uwezekano mkubwa wa kutoa tathmini ya kodi isiyo sahihi kutokana na kuwa nyuma ya muda kitendo ambacho kinaweza kusababisha tathmini ya kodi yenye utata.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha kuwa ukaguzi na upelelezi kwa walipakodi unafanywa na kuhitimishwa kwa wakati kwa nia ya kuimarisha utii wa sheria za kodi na ukusanyaji mapato ya Serikali kwa kiasi kikubwa kwa wakati. Mifano ya matukio yaliyobainishwa ni kama ilivyoonyeshwa kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 100: Sampuli za kesi za Ukaguzi wa Kodi ambazo zilichukua muda mrefu kukamilika**

| Jina la Mlipakodi | Tathmini ya Kodi | Tathmini ya Kodi | Tarehe ya Kuanza ukaguzi | Tarehe ya Kumaliza Ukaguzi | Tarehe ya Ripoti ya Awali | Tarehe ya Tathmini | Idadi ya Miezi iliyotumika kufanya ukaguzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | | | | | |
| Tahfif Auto Parts | 16,415,894.61 | - | 06/04/2021 | 29/8/2021 | 08/12/2021 | | 3 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tigo | 291,476,458.33 | - | 30/06/2021 | 13/10/2021 | 21/09/2021 | 13/10/2021 | 3 |
| Blue Bay Rosort | - | 70,897.28 | 06/08/2021 | 26/10/2021 | 14/10/2021 | 26/10/2021 | 4 |
| My Blue Hotel | - | 329,185.04 | 31/07/2021 | 26/10/2021 | 23/09/2021 | 26/10/2021 | 3 |
| Mnarani Beach | - | 29,800.56 | 13/07/2021 | 26/10/2021 | | 11/02/2022 | 3 |
| High Class Hotel | 141,161,118.91 | 95,026.74 | 27/08/2021 | 17/11/2021 | 20/10/2021 | 25/11/2021 | 3 |
| Zanzibar Milling Corp | 176,924,969.30 | - | 23/09/2021 | 22/12/2021 | 18/11/2021 | 28/12/2021 | 3 |
| Wave Resort Limited | 82,028,604.02 | 22,983.64 | 9/2/21 | 29/12/2021 | 17/11/2021 | 17/01/2022 | 3 |
| Mwamba InvestmentLtd | | 36,491.28 | 11/10/21 | 19/1/2022 | 16/12/2021 | 25/01/2022 | 3 |
| Palumbo Kendwa | | 16,135.99 | 09/02/21 | 28/01/2022 | 18/01/2022 | 2/7/22 | 4 |
| Merinvest Company Ltd | - | 25,215.53 | 09/02/21 | 2/11/22 | 12/10/21 | 31/03/2022 | 3 |
| Zanlink Limited | 7,118,973,676 | | 09/02/21 | 4/12/00 | 25/01/2021 | 28/04/2022 | 6 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Maripa Zanzibar | 770,465.30 | 10,456.07 | 31/11/2021 | 4/4/22 | 3/3/22 | 28/04/2022 | 3 |
| Nova Hotel Ltd | - | 46,699.97 | 17/01/2022 | 28/04/2022 | 4/4/22 | 28/04/2022 | 3 |
| Rans Company | 16,273,338.21 | | 12/8/21 | 4/12/22 | 4/4/22 | 5/6/22 | 3 |
| Vr Hotel Investment | | 89,209.62 | 15/11/2021 | 18/05/2022 | 2/10/22 | 6/2/22 | 5 |
| White Sands Beach | | 113,427.00 | 27/10/2022 | 13/06/2022 | 16/11/2021 | 16/06/2022 | 6 |
| Z. Hotel | | 74,570.36 | 13/02/2022 | 27/06/2022 | 13/06/2022 | 27/06/2022 | 3 |
| Warere Beach Hotel | | 53,825.03 | 15/11/2021 | 24/06/2022 | 19/11/2021 | 29/06/2022 | 4 |

**Jadweli Nambari 101: Mfano wa kesi za Uchunguzi wa Kodi ambao ulichukua muda mrefu kukamilika**

| Nam. | Jina la Mlipakodi | Tathmini ya Kodi | Tarehe ya Kuanza ukaguzi | Tarehe ya Kukamilika ukaguzi | Tarehe ya kufanya tathmini | Kipindi kilichofanyika | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ZAINAB BOTTLERS | TZS 1,450,036,696.93 | 19/04/2022 | 30/08/2022 | 02/09/2022 | JUNE 2019-JULY2021 | Uchunguzi ulichukuwa miezi 5 kukamilika |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | CMA CGM | TZS 1,585,005,487.91 | 03/03/2022 | 08/11/2022 | 08/12/2022 | JAN 2016-DEC 2020 | Uchunguzi ulichukuwa miezi 8 kukamilika |
| 3 | ZECO Pemba | TZS 137,690,049.19 | 15/02/2022 | 27/10/2022 | 31/10/2022 | JAN 2018-JUNE 2021 | Uchunguzi ulichukuwa miezi 7 kukamilika |
| 4 | ZABWAS-PILIPILI | USD 972,493. | 18.05.2021 | 07.02.2022 | 08.02.2022 | MAY 2018-JUNE2021 | Uchunguzi ulichukuwamiezi 8 kukamilika |

**Majibu ya Uongozi**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar imepokea ushauri na tayari imeandaa muongozo wa ukaguzi (Audit Manual) ambapo upo katika hatua za mwisho za kuidhinishwa ili kuweza kuengeza ufanisi wa ukaguzi na kuhakikisha kazi za ukaguzi zinakamilishwa kwa wakati.

Sababu zilizopelekea baadhi ya kazi za Upelelezi wa Kodi kuchukuwa muda mrefu kukamilika.

1. **Upatikanaji wa Taarifa Sahihi:**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar hufanya uchunguzi wa kina ili kubaini udanganyifu au upotoshaji wa taarifa za kodi. Uchunguzi huu huhitaji muda mwingi kukusanya taarifa na nyaraka za kifedha katika kuthibitisha usahihi wa taarifa za kodi ili kuweza kutoa tathmini sahihi ya Kodi.

Mfano, uchunguzi wa ZECO Pemba ulichukuwa muda mrefu kukamilika kutokana na mfumo wa malipo wa "Postpaid" ulibainika kuwa na hitilafu zilizopelekea kutoa takwimu zisizo sahihi. Hali hii ilipelekea kuchukua muda mrefu kusubiria kufanyika marekebisho

ya mfumo huo.

2. **Ukusanyaji wa Taarifa:**

Mchakato wa upelelezi wa kodi unahitaji ukusanyaji wa taarifa za kifedha kutoka kwa walipakodi na vyanzo vingine vya habari. Kukusanya taarifa hizi kunachukua muda mrefu, hasa ikiwa taarifa hizo ni ngumu kuzifikia au zimeandikwa kwa lugha tofauti. Mfano, wakati wa uchunguzi wa Mlipakodi ZABWAS PILPILI ulibaini taarifa za kifedha za Mlipakodi huyo ziliandikwa kwa lugha ya Kipoland. Hali hii ilipelekea ZRA kumtaka Mlipakodi kutafuta Mkalimani wa kutafsiri taarifa hizo kwa lugha ya Kiingereza. Hii ni kwa mujibu Sheria Kifungu cha 22 (2) na (3) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Na. 7 ya mwaka 2009.

3. **Utata wa Miundo ya Biashara:**

Katika biashara kubwa na yenye miundo tofauti, kubaini utata wa muundo wa umiliki na malipo kunaweza kuwa mgumu. Kampuni hususan za kigeni zenye matawi nchi tofauti duniani hutumia makampuni mengine na biashara za nje kama mbinu ya kukwepa Kodi. Makampuni haya yanaweza kutumika kama njia ya kuhamisha mapato na faida kutoka kampuni kuu kwenda kwenye makampuni mengine ili kupunguza kodi inayolipwa katika nchi husika. Kuchunguza miundo hii kunahitaji umakini na utaalamu, hivyo, huchukua muda mrefu kukamilisha uchunguzi.

Mfano, uchunguzi wa Kampuni ya CMA CGM ulihitaji kufanya uchunguzi zaidi katika Ofisi zake zilizopo Dar es Salaam kwa lengo la kutafuta Kodi halisi iliyopaswa kulipwa kwa upande wa Zanzibar. Aidha, Kampuni ya ZABWAS PILIPILI ilihusisha miamala ya kifedha kutoka Kampuni nyengine zilizoko nje ya nchi. Hivyo, ilichukua muda mrefu kuzifanyia uchunguzi taarifa hizo.

4. **Kukosekana Ushirikiano:**

Kukamilika kwa upelelezi kwa wakati kunategemea na ushirikiano kutoka kwa Mlipakodi. Baadhi ya Walipakodi hawatoi ushirikiano mzuri kuhusiana na biashara zao kwa ZRA kwa sababu huficha mwenendo wa biashara zao. Katika kipindi cha Upelelezi, baadhi ya kesi huchelewa kutokana na mlipakodi kutumia haki yake ya kuahirisha tarehe ya kuendelea na mijadala ya uchunguzi (Meeting Discussion of Investigation Findings) kutokana na sababu mbalimbali zinazowakabili kuhusiana na kesi husika.

Mfano, Kampuni ya ZAINAB BOTTLERS haikutoa ushirikiano mzuri katika kukamilisha hatua za uchunguzi na kupelekea uchunguzi kuchukua muda mrefu kukamilika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Mkaguzi kubaini kuwepo kwa changamoto za uchunguzi wa kesi kuchukua muda mrefu, Kamati imebaini kuwa tayari Mamlaka imeshaandaa muongozo wa ukaguzi ambao ni matumaini ya Kamati Mamlaka utautumia miongozo huo na changamoto zilizojitokeza hazitoweza kujitokeza kwa mara nyengine. Kwa msingi huo, Kamati imeridhika na hatua ziizofikiwa na hoja hiyo imeondolewa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Mamlaka uharakishe unaupeleka katika Bodi ya Wakurugenzi muongozo huo ili uweze kupitishwa, kutumika na kuondoa kasoro ya kuchelewa kumalizika uchunguzi wa kesi za Walipa kodi ndani ya wakati uliopangwa.

## Hoja nambari 7.1.2.10: Uchambuzi wa athari za ukaguzi wa kodi kwenye ukusanyaji wa mapatohaujafanywa na idara inayohusika (TRAI)

Ukaguzi wa kodi unaathiri ukusanyaji wa mapato kwa kuwa unakuza utii wa ulipaji wa hiari wa walipa kodi ambao husaidia kuongeza mapato. Pia hubainisha usahihi wa kodi ili kuhakikisha kwamba kodi zinazofaa zinawasilishwa. Kupitia ukaguzi kwa walipakodi madeni yote yatatambulika na kama kuna marekebisho yatafanywa ili kuhakikisha kodi stahiki inapatikana. Pia husaidia katika kukusanya riba na adhabu za kodi ambazo pia huongeza ukusanyaji wa mapato. Ukaguzi wa kodi pia husaidia kutekeleza mabadiliko ili kutokomeza ukwepaji kodi. Hivyo, ukaguzi kwa walipakodi unahusiana vyema na ukusanyaji wa mapato.

Katika kupitia taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa mpango kazi wa idara ya TRAI ilibainika kuwa idara hiyo ilitakiwa kufanya kaguzi 264 ambapo shilingi bilioni 52.5 zilitakiwa kukusanywa kutokana na kaguzi hizo. Hata hivyo, taarifa ya kujitathmini kama idara (Idara ya Ukaguzi, Usajili na Upelelezi kwa walipakodi) ya kwamba idara imechangia kiasi gani katika mapato yaliyokusanywa katika mwaka wa ukaguzi, kiasi cha shilingi 374,760,319,444 inakosa ushahidi wa kufanyika. Uchambuzi wa tathmini utahitaji kuzingatia idadi ya ukaguzi wa kodi na upelelezi uliofanywa, tathmini za kodi zilizotolewa, tathmini zilizokataliwa, tathmini zilizokusanywa na madeni ambayo bado hayajalipwa kutokana na ukaguzi wa kodi na upelelezi uliofanywa.

Mchango wa idara ya ukaguzi na upelelezi kwa walipakodi katika mapato ya kodi ya mwaka husika huenda usifahamike, hivyo basi mwenendo wa utendaji kazi wa idara hauwezi kupimwa kwa uhakika. Idara ina uwezekano wa kufanya vibaya kwa kuongeza

tathmini nyingi za kodi ambazo haziwezi kukusanywa kutokana na tathmini zenye mzozo na kusamehewa kwa kiasi kikubwa cha adhabu na riba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha kuwa upembuzi wa athari za ukaguzi na upelelezi kwa walipakodi katika mapato yanayokusanywa unafanyika na taarifa inaandaliwa ili kubaini mchango wa idara katika kuhamasisha utii wa sheria za kodi kwa walipakodi wenye nia ya kuongeza ukusanyajiwa mapato ya Serikali.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar imepokea ushauri wa Mkaguzi, na kwa kupitia Divisheni ya ukaguzi imeanza kuonesha athari ya ukaguzi kwa kutoa ripoti za kila mwezi, robo mwaka nusu mwaka na mwaka mzima, pamoja na kuonesha kodi ilioyoibuliwa na Kodi iliyokusanywa, Mfano kwa kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Disemba 2023 kwa Idara ya Kodi za ndani pekee imeweza kuibua kodi ya TZS 3,762,932,598.51 na kuweza kukusanya jumla ya TZS 1,040,832,219.73 kati ya TZS 1,723,247,970.39 iliyotakiwa kukusanywa, ambayo ni sawa na ufanisi wa asilimia 60.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa awali kasoro hiyo ilijitokeza na kuianishwa na Mkaguzi katika Ripoti yake. Hilo lilichangiwa zaidi na uwepo wafanyakazi kidogo wenye majukumu ya uchunguzi wa athari za ukaguzi wa kodi kwenye ukusanyaji wa mapato ambapo awali jukumu hilo lilitekelezwa na Idara ya husika lakini ukusanyaji halisi ulifanywa na Idara ya madeni.

Kwasasa utekelezaji wa hoja hii unafanyika kwa usahihi wake ambapo Idara inayohusiana na Idara ya Ukaguzi, Usajili na Upelelezi kwa walipakodi huwa inayatambua madeni ya walipa kodi na Idara ya walipa kodi hushughulikia na ufuatiliaji na ulipwaji wake. Aidha, Kamati imebahatika kukagua Ripoti ya makusanyo ya mwezi wa Oktoba, 2023 hadi Disemba, 2023 na kuona utekelezaji unavyokuwa. Kwa msingi huo, Mamlaka imeshaufanyia kazi ushauri uliotolewa na Mkaguzi.

## Hoja nambari 7.1.2.11: Tathmini ya mwenendo wa mapato kwa kulinganisha ritani zilizowasilishwa na walipakodi dhidi ya mapato halisi

Ukaguzi ulipitia taarifa ya mwenendo wa mapato ya mwaka 2021/2022 ambayo yalitolewa kwa ajili ya ukaguzi, na kubaini kuwa Bodi ilikadiria kukusanya shilingi 525,095,095,634 ambapo shilingi 374,760,319,444 zilikusanywa sawa na asilimia 71.37.

Hata hivyo, tathmini ya mwenendo wa mapato kwa kulinganisha na ritani zilizowasilishwa na walipakodi dhidi ya mapato halisi yaliyokusanywa kutokana na ritani hizo ilikosekana. Tathmini hiyo inalenga kutambua mapato yote ambayo hayajakusanywa na kuweka utaratibu wa udhibiti kuhakikisha madeni hayo yanakusanywa.

Aidha, ukaguzi ulibaini tathmini ya mwenendo wa ukusanyaji wa mapato iliyoandaliwa katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi ilionekana finyu kwani haikuzingatia taarifa ya mapato yote yaliyokuwa mikononi mwa walipakodi (madeni ya kodi) na hivyo kuweza kusababisha madeni yasifichuliwe kwa kila chanzo cha mapato kwa hatua zaidi za ufuatiliaji wa marejesho yao. Vilevile kiasi cha mapato yaliyokusanywa kwa mwaka wa ukaguzi cha shilingi 374,760,319,444 kilitia shaka katika ukamilifu na usahihi wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha kuwa tathmini ya makusanyo ya mapato inafanywa kwa kuzingatia makadirio pamoja na ritani zilizowasilishwa dhidi ya makusanyo halisi ili kuwezesha kufichua madeni yote ya kodi na kuchukua hatua stahiki za kurejesha madeni ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji mapato. Awepo mtu anayewajibika kutoka katika Kitengo cha Madeni ambaye atasimamia mapato yote ambayo hayajakusanywa kutoka kwa kila chanzo kwa taarifa sahihi na kufuatilia ipasavyo.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka ya Mapato Zanzibar imechukua hatua za kutengeneza muundo mpya wa Idara tatu za ukusanyaji Idara ya Walipakodi Wakubwa, Idara ya Kodi za Ndani na Idara ya Mapato yasiyo ya Kodi.

Kila Idara ina kitengo chake kinachojitegemea cha Uwajibikaji wa kodi na ufuatiliaji wa Madeni ambacho kina jukumu la kufuatilia walipakodi wote ambao hawawasilishi malipo, kuwezesha kufichua madeni yote ya kodi na kuchukua hatua stahiki za kurejesha madeni ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji mapato pamoja na kugomboa madeni yote ya ritani na ya tathmini ya kodi.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Licha ya Kamati kubaini kujitokeza kwa kasoro hii wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, kwasasa kasoro hiyo imesharekebishwa kufuatia kuwepo kwa muundo mpya wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar na tayari umeanza kufanya kazi zake ipasavyo. Kwa msingi huo, Kamati imeridhika na hatua ya mgawanyo wa majukumu na uwepo wa wafanyakazi wanaoshughulikia suala la tathmini ya mwenendo wa mapato na hatimae

Kamati imeiondoa hoja hii.

### Hoja nambari 7.1.2.12: Stakabadhi katika taarifa za benki zilizokosekana katika mfumo wa ZITAS (Miamala katika taarifa ya benki haikutambuliwa katika mfumo wa Mapato wa ZITAS)

Ukaguzi ulipitia taarifa za usuluhishi wa Benki (bank reconciliation statements) ya miamala ya benkikatika hesabu ya mapato kwa benki ya watu wa Zanzibar (PBZ) na kubaini kuwa mifumo ya mapato yaPBZ na ZRB imeunganishwa ili kurahisisha usuluhishi wa fedha na miamala ya benki. Hii inamaanisha kwamba miamala yote inayopita benki inatambuliwa pia katika mfumo wa ZRB (ZITAS). Hata hivyo, mapitio ya taarifa za usuluhisho wa miamala ya benki na mfumo wa mapato wa ZRB (ZITAS) yalibainibaadhi ya miamala ya usuluhisho iliyojulikana kama stakabadhi ambazo hazikupita/kutambuliwa na mfumo wa mapato wa ZRB (ZITAS). Mahojiano na maafisa wanaohusika yalifichua udhaifu katika muunganiko wa mfumo wa PBZ na ZITAS ambapo ilielezwa kwamba baadhi ya miamala iliyopita benki haikuweza kutambuliwa katika mfumo wa ZITAS. Tatizo hili la muunganiko wa mifumo linamlazimu afisa mapato anayehusika kuandaa usuluhishi wa mikono (mannual reconciliation) kwa miamala ambayo haijatambuliwa na ZITAS ili aweze kutoa stakabadhi kwa wateja.

Usuluhishi sahihi wa fedha na miamala ya benki uliathiriwa jambo ambalo linaweza kusababisha ubadhirifu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuchunguza sababu zilizosababisha makosa katika uunganishajiwa mifumo kati ya PBZ na mfumo wa mapato wa ZITAS na kuchukua hatua za kurekebisha ili kuwezesha usuluhishi sahihi na usahihi wa taarifa za ukusanyaji wa mapato. Matukio machache yaliyobainishwa yameonyeshwa kwenye jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 102: Miamala haijanaswa katika ZITAS moja kwa moja “kiotomatiki”**

| Mwezi wa Usuluhishi | Kiwango cha Fedha (Tshs) | Kiwango cha Fedha (USD) |
|---|---|---|
| Juni 2022 | 12,551,584.32 | 15,071 |
| Mei 2022 | 27,637,224.34 | 29,276 |
| Aprili, 2022 | 119,469,892.02 | 16,416 |
| Machi 2022 | 19,158,072.97 | 1,632 |

| | | |
|---|---|---|
| Februari,2022 | 32,962,862 | 27,637 |
| Januari,2022 | 20,048,969.84 | 4,151 |
| Disemba,2021 | 132,848,521.67 | 10,280 |
| Novemba,2021 | 1,056,203,064.76 | 8,515 |
| Oktoba,2021 | 87,462,259.15 | 73,063 |
| Septemba,2021 | 96,631,721.85 | 21,978 |
| Ogasti,2021 | 64,890,897.32 | 15,093 |
| Julai,2021 | 22,691,916.88 | 8,135 |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Uongozi wa ZRA ulichunguza na kubaini kwamba kuna changamoto baina ya mfumo wa ZITAS na PBZ wa kutokuonana kwa mifumo hiyo. Kutokana na hilo Uongozi umelifanyia kazi suala hili kwa kuanzisha mfumo mpya wa ZIDRAS ambao ulianza kufanyakazi mwezi Aprili, 2023. Mfumo huo umeweza kutatua changamoto za awali zilizopo katika mfumo wa Zitas na kwa sasa Mfumo wa ZIDRAS unaonana na Mfumo wa Banki ya PBZ na Zanmalipo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imejiridhisha kwamba hoja hiyo kweli awali ilikuwepo lakini hivi sasa tayari imeshafanyiwa kazi na hakuna tena changamoto katika mifumo hiyo mitatu. Kwa msingi huo, Kamati imeiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 7.1.2.13: Ukosefu wa muunganisho wa mfumo wa ZRB na BOT kwa miamala ya kibenki

Ukaguzi ulipitia usuluhishi wa benki kwa upande wa mapato yote yanayopokelewa katika hesabu za ZRB (Shilingi na dola za Kimarekani) iliyoko katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na kubaini kuwa miamala ya fedha taslimu na benki kati ya BoT na ZRB (ZITAS mfumo wa mapato) haikufanyika kwa mfumo wa moja kwa moja (Automatic) ili kuwezesha usuluhishi kwa wakati na upatikanaji wa taarifa za wakati halisi kwa usahihi. Hivyo basi, usuluhishi sahihi wa fedha na miamala ya benki uliathiriwa jambo ambalo

linaweza kusababisha ubadhirifu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha kuwa miamala ya fedha taslimu na za benki zilizoko BoT inaunganishwa na mfumo wa mapato (ZITAS system) kupitia Mfumo wa IFMIS wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuwezesha usuluhishi na upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu ukusanyaji wa mapato.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Uongozi wa ZRA umechukua mapendekezo ya Mkaguzi na kupelekea kuanzishwa kwa mfumo mpya wa Mapato (ZIDRAS) ambapo umeunganana Bank ya BOT ili kuwezesha miamala yote ya ZRA ya mapato yaweze kupita katika mifumo kama inavyotakiwa. Mfumo huo umeweza kutatua changamoto za awali zilizopo katika mfumo wa ZITAS na kwasasa Mfumo wa ZIDRAS utaonanana Mfumo wa Bank ya BOT

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imebaini uchunguzi na mapendekezo ya hoja hii yanafanana na uchunguzi na mapendekezo yanayopatikana katika hoja nambari 7.1.2.12 yaliyoelezwa hapo juu.

## Hoja nambari 7.1.2.14: Ukaguzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato ya ZRB yatokanayo na Mamlaka za Bandari na Viwanja vya Ndege

Vyanzo vya mapato vinavyotokana na bandari za baharini na anga ni pamoja na malipo ya huduma ya uwanja wa ndege, malipo ya huduma ya bandari ya baharini, ushuru wa usafiri wa baharini, ada ya usalama wa uwanja wa ndege na ushuru wa miundombinu. Tathmini ya taratibu za ukusanyaji ilibaini kuwa vyanzo vya takwimu zinazotumika ili kubaini usahihi na ukamilifu wa mapato halisi yanayohitajika kutoka katika vyanzo hivyo zinategemea zaidi nyaraka zilizotunzwa na mawakala wa mashirika ya ndege na makampuni ya usafirishaji ya bandari ambazo zinaeleza/kuonyesha idadi ya abiria waliotoka Zanzibar kuelekea maeneo mbalimbali. Udhaifu ulioonekana kwenye utaratibu wa kukusanya mapato haya ni kama ifutavyo:-

(a) **Kukosekana kwa ushahidi wa maridhiano/upatanisho kati ya makampuni ya usafirishaji ya bandari, mawakala wa mashirika ya ndege na ZRB.**

Hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha kuwa ZRB na makampuni yanayohusiana na usafirishaji wa bandari ya baharini, na mawakala wa mashirika ya ndege walikuwa wakifanya maridhiano/upatanisho ili kupata idadi sahihi ya abiria waliokuwa wakitoka Zanzibar kwenda sehemu mbalimbali ili kubaini usahihi na ukamilifu wa mapato

yanayotakiwa kupatikana kutoka katika vyanzo hivyo.

**(b) Kutokuunganishwa kwa Mifumo ya ZRB, kampuni za usafirishaji za bandari ya baharini, mawakala wa mashirika ya ndege na vyombo vya udhibiti (ZAA na ZMA).**

Ukaguzi umebaini Mifumo ya ZRB haikuunganishwa na mifumo ya kampuni za usafirishaji za bandariya baharini, mawakala wa mashirika ya ndege na vyombo vya udhibiti (ZAA na ZMA) ili kuweza kusomana na kupatikana kwa taarifa sahihi za idadi ya abiria wote walioondoka Zanzibar na mapato halisi yanayotakiwa kupatikana kutoka katika vyanzo hivyo ili kuongeza ukusanyaji wa mapato kutokavyanzo hivi.

Kutokuwepo kwa nyaraka zitakazotumika kuthibitisha idadi sahihi ya abiria na kusainiwa na wahusika wakiwemo ZRB, ZMA, kampuni za usafirishaji bandarini, Shirika la meli na Mamlaka ya Viwanja vya ndege (ZAA). Nyaraka hizo zitatumika kufanya makubaliano ya kila mhusika kuhusu idadi ya abiria walioondoka katika kipindi fulani. Kwa hivyo ukamilifu na usahihi wa vyanzo vya mapato kutoka kwa mamlaka ya bandari na viwanja vya ndege vilivyoripotiwa mwishoni mwa mwaka haukuweza kuthibitishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi Bodi ya Mapato Zanzibar unapaswa kuhakikisha yafuatayo:-

- Kufanyike Maridhiano/upatanisho kuhusu idadi ya abiria waliondoka Zanzibar kati ya ZRB, kampuni za usafirishaji bandarini na mawakala wa kampuni za ndege ili kujua idadi sahihi ya abiria walioondoka ili iwe kigezo sahihi cha ukokotoaji wa makusanyo ya mapato yanayotakiwakupatikana kutoka kwenye vyanzo hivi.
- ZRB ifikirie kuanzisha hati/nyaraka ambayo inaweza kutumika kupata idadi sahihi ya abiria walioondoka zitakazokubaliwa na kusainiwa na wahusika wakiwemo ZRB, ZMA, kampuni za usafirishaji bandarini, Shirika la meli na Mamlaka ya viwanja vya ndege (ZAA) ili itumike kama hati/nyaraka ya msingi kwa hapo baadae kila inapoonekana inafaa kwa kila mdau.
- Ujumuishaji/uunganishaji wa taarifa za ZRB na wadau wengine unasisitizwa zaidi ili kuwezesha kunasa taarifa zote za muhimu zinazohitajika za abiria kwa wakati na kwa usahihi.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar imezingatia ushauri wa mkaguzi ambapo kwa sasa imefanya muunganiko wa mifumo "Integration" baina ya mfumo wa kampuni ya usafirishaji baharini ya Ikram Sea line na hatua za kuunganisha mifumo ya Azam Marine na Zan Fast Feries zinaendelea.

Aidha, kwa upande wa Uwanja wa ndege ZRA imetengeneza mfumo wa upatikanaji wa taarifa za abiria wanaingia na wanaotoka kupitia viwanja vya ndege unaojuilikana kama "Guest Arrival and Departure Information System" (GADIS). Mfumo huo pia utatumiwa na wadau wengine kama vile ZAA. Hatua hii ya utumiaji wa mifumo utaondoa matumizi ya upatikanaji wa taarifa "manual" na utahakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi. Aidha, wakati ZRA inaendelea kuharakisha matumizi ya mfumo wa GADIS, juhudi za kuunganisha mifumo ya Uhamiaji zimeanza na zinaendelea.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa licha ya juhudi ambazo Mamlaka imezichukua lakini bado kuna changamoto hususan katika upatikanaji wa taarifa sahihi za wasafiri kwa kupitia Bandari na Viwanja vya Ndege. Hili linatokana na uwepo wa usiri na dhana nzima ya usalama wa taarifa hususan kwa muunganiko wa mfumo wa ZRA na Uhamiaji. Hata hivyo, kwa upande wa uwanja wa ndege, changamoto ya upatikanaji wa taarifa imeanza kutatuliwa kwa kuwepo kwa Mfumo mpya wa GADIS ulioanzishwa na ZRA.

Sambamba na hilo, Kamati imegundua kuwa tayari ZRA na Kamisheni ya Utalii zimeshakubaliana juu ya uunganishwaji wa mifumo yao ili taarifa za watalii waliepo Zanzibar zinapatikana kwa usahihi wake na kukuza ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka. Kwa msingi huu, hoja hii inaendelea kubakia hadi itakapotekelezwa kwa ukamilifu wake.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar uhakikishe unaendeleza juhudi za kuunganisha mfumo wao na mfumo wa Uhamiaji ili taarifa sahihi za wageni wanaoingia na kutoka Zanzibar ziweze kupatikana.
2. Uongozi wa Mamlaka uhakikishe unakamilisha mazungumzo na Kamisheni ya Utalii na hatimae wanaunganisha mifumo yao ili waweze kufanyakazi kwa pamoja na kuondokana utaratibu wa ukusanyaji mapato wa 'manual'.
3. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ichukue juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba Kampuni yoyote hususani ya watu binafsi inaunganisha mifumo yao na mfumo ya ZRA ili taarifa za makusanyo yao ziweze kupatikana na kutumika katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

## Hoja nambari 7.1.2.15: Ukaguzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato ya ZRB yatokanayo na sekta ya utalii

Vyanzo vya mapato vinavyotokana na sekta ya utalii ni pamoja na tozo ya hoteli, tozo ya migahawa na tozo ya uendeshaji wa utalii. Tathmini ya taratibu za ukusanyaji ilibaini kuwa takwimu za vyanzo vya mapato ili kubaini usahihi na ukamilifu wa mapato halisi yanayohitajika kutoka katika vyanzo hivyo hutegemea idadi ya watalii wanaowasili Zanzibar ambao taarifa zao zinatunzwa na taasisi za Serikali zinazohusika ambazo ni Idara ya Uhamiaji na Kamisheni ya Utalii. Udhaifu ulioonekana kwenye utaratibu wa kukusanya mapato haya ni kama ifuatavyo:-

**Uwepo wa kumbukumbu zisizoaminika za idadi ya watalii wanaowasili Zanzibar kunakosababishwa na kukosekana kwa maridhiano/upatanis kati ya ZRB na taasisi nyingine za Serikali zinazowajibika.**

Ilibainika kuwa vyombo vinavyohusika na kutunza kumbukumbu ya idadi ya watalii wanaowasili Zanzibar ni Idara ya Uhamiaji na Kamisheni ya Utalii. Hata hivyo ilibainika kuwa hakuna ushahidi unaothibitisha kuwa ZRB ilifanya upatanisho na kuoanisha idadi halisi ya watalii wanaowasili Zanzibar katika mwezi mmoja na takwimu zilizotunzwa na Idara ya Uhamiaji na Kamisheni ya Utalii kwa lengo la kuwezesha makadirio sahihi ya mapato na ufuatiliaji wa makusanyo halisi ya mapato kutoka kwenye vyanzo hivi.

Kukosekana kwa Muunganisho wa mifumo kati ya ZRB, Kamisheni ya Utalii na Idara ya Uhamiaji kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa idadi sahihi ya watalii wanaowasili Zanzibar na mapato sahihi yanayotakiwa kupatikana kutokana na vyanzo hivyo na hivyo kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo hivyo.

**Uwepo wa wafanyabiashara ya ziara za utalii ambao hawajasajiliwa**

Wafanyabiashara ya uendeshaji ziara za watalii wanaweza kujumuisha kampuni, ubia, ushirika au mmiliki pekee. Kila mtalii lazima asajiliwe na Kamisheni ya Utalii kwa mujibu wa Sheria ya Kuanzishwa Utalii Na. 6 ya 2009 (kama ilivyorekebishwa) rejea kifungu cha 15 kisomeke pamoja na kifungu cha 19. Mahojiano na ofisa anayehusika na ukusanyaji wa tozo za uendeshaji watalii yalifichua ukweli kwamba kuna uwepo wa idadi kubwa ya waendeshaji watalii walikuwa wakifanya biashara hiyo bila leseni halali au kibali kutoka kwa Kamishna wa Utalii kama vile beach boys na hoteli nyinginezo zinazotoa huduma za utalii kwa njia isiyo rasmi. Hii inazuia ufuatiliaji wa kumbukumbu sahihi za waendeshaji watalii wote wanaostahiki kulipa kodi.

**Usaidizi Duni kutoka kwa vyanzo vya habari vya nje ili kusaidia upatikanaji wa kumbukumbu sahihi za watalii (Kushindwa kwa Tume ya Utalii kusimamia Sheria ya**

Utalii Na. 6 ya mwaka 2009 kwa wale wote wanaokiuka sheria na taasisi zinazohusiana na Serikali)

Ili kukabiliana na tatizo la waendeshaji watalii haramu ZRB imefanya jitihada kadhaa kwa mujibu washeria ya usimamizi wa kodi (TAPA namba 7 ya mwaka 2009) ili kupata idadi sahihi ya watalii ikiwani pamoja na kuandika barua kwa makampuni mbalimbali ambayo wateja wake ni pamoja na wataliikama kampuni ya Haringford Ltd, Johari Co. Mizingani Beach n.k. Hata hivyo juhudi hizo ziliambulia patupu kwani hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha majibu kutoka kwa taasisi hizo.

Wakaguzi wanaona kwamba kuendelea kuwepo kwa baadhi ya waendeshaji watalii ambao hawajasajiliwa kunachangiwa na Kamisheni ya Utalii kushindwa kuchukua hatua kwa mujibu wa kifungu cha 28 cha Sheria yake ya Kuanzishwa Na. 6 ya mwaka 2009, hivyo basi ZRB inahitajika kufanya juhudi za kuwasiliana na Kamishna wa Utalii ili kuhakikisha tatizo hilo linadhibitiwa.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar imepokea ushauri na tayari imeanza kufanyia kazi ushauri huo ambapo:-

- Mamlaka imeanza kushirikiana na Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa kuwataka wasitoe leseni kwa wafanyabiashara za utalii bila ya kuwa na kibali cha kodi (Tax Clearance)
- Aidha ZRA imekuwa ikifanya mazoezi ya barabarani kwa lengo la kuwabaini watembeza wageni waliokuwa hawajasajiliwa kwa ajili ya kuchukuliwa hatua stahiki.
- Vilevile wakati ZRA inaendelea kuharakisha matumizi ya mfumo wa GADIS, juhudi za kuunganisha mifumo ya Uhamiaji zimeanza na zinaendelea.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya juhudi zilizochukuliwa na Mamlaka za kuhakikisha ukaguzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato ya ZRA yatokanayo na sekta ya Utalii. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba bado kuna changamoto ya upatikanaji wa taarifa sahihi zitokanazo na Sekta ya Utalii na kupelekea kukosekana kwa mapato ya Serikali. Hali hii imabainika baada ya Kamati kutaka kujua upatikanaji wa taarifa za Watalii waliopo Zanzibar na kugundua kuna utata katika ukweli wa taarifa zao. Kwa mnasaba huo, hoja hii inaendelea kubakia ili Mdhibiti aweze kufuatilia zaidi utekelezaji wake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

ZRA iharakishe ufuatiliaji na upatikanaji wa taarifa sahihi zitokanazo na wafanyabiashara ya ziara za utalii, vyanzo vya habari vya nje pamoja na idadi ya watalii wanaowasili Zanzibar ili changamoto ya taarifa zao iweze kutatuliwa.

## Hoja nambari 7.1.2.16: Kuwepo kwa majina tofauti ya usajili wa waendeshaji Watalii katika kanzidata ya ZRB (ZITAS) na ile ya Kamisheni ya kumbukumbu za waendeshaji watalii.

Ukaguzi ulipitia orodha ya waendeshaji watalii kwa mujibu wa kumbukumbu za ZITAS na kubaini baadhi ya waendeshaji watalii wenye majina tofauti ingawa walikuwa ni Kampuni zilezile kama ilivyodhihirika baada ya mahojiano na afisa anayehusika na ushuru wa kampuni za uendeshaji wa biashara ya utalii. Hali hii inazuia ufuatiliaji wa maeneo yao halisi ya kufanyia biashara na usahihi wamakusanyo yanayoweza kupatikana kutoka kwa chanzo hiki. Kwa kuzingatia madhaifu ya hapo juu:-

- Ukamilifu na usahihi wa vyanzo vya mapato vinavyotokana na sekta ya utalii vilivyoripotiwa mwishoni mwa mwaka haukuweza kufahamika.
- Kuongezeka kwa shughuli zisizo za kimaadili kupitia waendeshaji watalii ambao hawajasajiliwa jambo ambalo litaathiri vibaya sekta ya utalii na hivyo kupunguza vyanzo vya mapato ya Serikali kutoka kwenye sekta hii.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha yafuatayo ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wamapato kutoka sekta ya utalii:-

- Mifumo ya ZRB iunganishwe na Kamisheni ya Utalii na Idara ya Uhamiaji kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa idadi sahihi ya watalii wanaowasili Zanzibar na mapato sahihi yanayotakiwa kupatikana kutoka katika vyanzo vya sekta ya utalii hivyo kutaongeza ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo hivyo.
- Uwepo uhusiano wa karibu wa kikazi kati ya ZRB na Kamisheni ya Utalii juu ya kusimamia utekelezaji wa sheria ya biashara ya utalii ambapo TAPA namba 7 ya 2009 (kama ilivyorekebishwa)inathibitisha kushindwa.
- Waendeshaji watalii watambulike katika ZITAS kwa kutumia majina yao halisi ya biashara yaliyosajiliwa kulingana na Kamisheni ya Utalii ili kuepusha kutofautiana kwa majina ambayo huathiri ukusanyaji wa mapato.

Baadhi ya matukio yaliyotajwa kwa ufafanuzi zaidi ni kama inavyoonekana katika jadweli

lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 103: Waendeshaji ziara za Watalii wenye majina tofauti katika mfumo wa ZITAS na Jina la Usajili wa Biashara**

| Nam. | Jina Katika Mfumo wa ZITAS | Jina la Usajili wa Kampuni |
|---|---|---|
| 1. | Abdulhalim Haji Vuaa | Zan Art Tours |
| 2. | Abdulwahid Ali Haji | Zan Voyage Tours And Safari |
| 3. | Abel Lucas Lasiriam | Nyumbani Tours And Safari |
| 4. | Ally Mussa Jape | City Guide Zanzibar |
| 5. | Amina Said Iddi | Heritage Tours |
| 6. | Amour Mohamed Juma | Lemon Tours And Safari |
| 7. | Amour Suleiman Amour | Amo Zanzibar |
| 8. | Arif Abbas Manji | Trancendence |
| 9. | Asha Simai Mahmoud | (Zanview Tour |
| 10. | Awadh Abdalla Almas | Zanzibar Smile |
| 11. | Bakar Duchi Ame | Bkite Duchi Ame |
| 12. | Emanuel Zablon Wagazu | Coconut Kite |
| 13. | Emanuel Zablon Wagazu | Coconut Kite |
| 14. | Fatma Saleh Ali | Chiddy’s Island Tour |
| 15. | Haabir Rashid Mrisho | C And H Tours &Safaris |
| 16. | Habibu Makame Ameir | Kacho Dreams |
| 17. | Habir Rashid Mrisho | C And H Tours &Safaris |
| 18. | Hafidh Abdulla Suleiman (Karibu Kwetu) | KARIBU KWETU |
| 19. | Hassan Adam Suleiman | Cacao Tours |

| | | |
|---|---|---|
| 20. | Hassan Adam Suleiman | Cacao Tours |
| 21. | Hassan Seif Hassan (Kite Boarding Zanzibar) | KITE BOARDING ZNZ |
| 22. | Ismail Nuhu | Suma Tours |
| 23. | Ismail Nuhu Kangeta | Suma Tours |
| 24. | Issa Juma Issa | ZAN CRYSTAL TOURS |
| 25. | Juma Faki Juma | ZAN LOCAL EXPERIENCE |
| 26. | Juma Salum Yussuf | Manji Tour |
| 27. | Kassim Abdallah Kassim | Coral Tour |
| 28. | Kassim Essam Omari (Azadam Tour) | Azadam Tour |
| 29. | Kassim Mohamed Mwalago | Apa Divers |
| 30. | Kassim Mohamed Mwalago | Apa Divers |
| 31. | Khamis Juma Abdallla | Gikli Tour And Safari |
| 32. | Khamis Salum Singu | Jahazi Tours And Safaris |
| 33. | Mohamed Adnan Hamad | Kingnet Tours and Travel |
| 34. | Mohamed Al-Amin Abdy | Amisda Tours |
| 35. | Mohammed Haji Mwinyi | Zanzibar Kite Excotic |
| 36. | Mohammed Kalam Kondo (Munsam Travel) | Munsam Travel |
| 37. | Mousa Mbarouk Shaaban | Explorer Zanzibar |
| 38. | Munir Maulid Ameir | Zansmart Travel And Tours |
| 39. | Muntadhiru Mrisho Abdu | Olamanga Kite |
| 40. | Mussa Ame Silima | Mtutu Tours |
| 41. | Mustafa Dauu Maganga | Zanzibar Nzuri Tours And Safaris |
| 42. | Mzee Mwalim Kwao | Zanzi Kite Junkies |
| 43. | Nahodha Makame Mcheni Captain Findus | Captain Findus |
| 44. | Nassor Ussi Mkubwa | Fun Divers Zanzibar |
| 45. | Omar Mussa Omar | Zan Omar Tour & Safaris |

| | | |
|---|---|---|
| 46. | Pilly Mohammed Ramadhan | Tulia Tours |
| 47. | Rajab Khamis Haji | Urafiki Tours |
| 48. | Rashid Abdalla Rashid | Organisateur Francophone Tours |
| 49. | Sajid Anwar Issack | Zan Jj Adventure |
| 50. | Salim Khamis Salum | My Pickup |
| 51. | Salum Hamidu Salum | Coco Tour And Safari |
| 52. | Seif Ali Seif | Zanzibar Tours And Travel |
| 53. | Seif Masoud Seif | Popo Tours And Safari |
| 54. | Seif Mole Kidongo | Nyota Njema Tours & Safari |
| 55. | Simai Mkadam Haji | Kv Tours |
| 56. | Suleiman Mohammed Suleiman | Costan Tours And Safari |
| 57. | Tausina Omar Mohamed | Body Soul & Spa |
| 58. | Ussi Khatibu Ali | Znz Star |
| 59. | Ussi Sulubu Ussi | Kendwa Community Tours |
| 60. | Yussuf Mbarouk Maulid | Gigi Di |
| 61. | Yussuf Mbarouk Maulid | Gigi Di |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Uongozi wa ZRA umechukua hatua ya kuimarisha kanzidata yake kwa kutengeneza mfumo mpya wa walipa kodi (ZIDRAS) ambao umeanza kutumika na ambao umezingatia usahihi wa taarifa za walipa kodi kuanzia hatua ya usajili kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji na makusanyo ya mapato.

Hata hivyo ZRA imeendelea na jithada za kuimarisha utumiaji wa mifumo ya kielektroniki kwa kuandaa mfumo utakaoiwezesha ZRA pamoja na Taasisi nyengine (ZAA) katika kupata taarifa mbalimbali, na kwa kuanzia ZRA imetengeneza mfumo utakaosaidia upatikanaji wa taarifa za abiria wanaoingia na kutoka kupitia Uwanja wa Ndege unaojuilikana kama GADIS (Guest Arrival and Departure Information System).

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Uchunguzi wa Kamati kwenye hoja hoja hii unalingana na uchunguzi wa Kamati ulioelezwa katika hoja nambari 7.1.2.14. Hata hivyo, Kamati imebaini ni kweli kuna utofauti wa usajili wa majina ya Waendeshaji ziara za Watalii katika mfumo wa ZITAS na jina la Usajili wa Biashara. Hili limetokana na kutokusomana kwa mifumo hiyo.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

ZRA kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii wahakikishe mifumo yao ya usajili wa majina ya Waendeshaji ziara za Watalii katika mfumo wa ZITAS na jina la Usajili wa Biashara yanasomana ili iwe rahisi kutambulika kwa pande zote mbili.

## Hoja nambari 7.1.2.17: Udhaifu uliobainika katika chanzo cha mapato ya tozo ya Petroli

Ukaguzi ulipitia utaratibu wa chanzo cha mapato ya tozo ya mafuta ya petroli na kubaini kuwa tarehe ya mwisho ya malipo ya tozo ya mafuta ya petroli kwa Makampuni husika ni ndani ya siku saba tangu tarehe ya kuwasili kwa mafuta katika bohari ya Mtoni. Bidhaa zote za ushuru zinazotokana na chanzo hiki ambazo ni pamoja na tozo ya mafuta ya petroli, hazina ya barabara/ushuru wa barabara, na kodi ya miundombinu na leseni ya barabara zinatozwa mahali pa kuingilia. Hata hivyo, udhaifu ufuatao ulibainika:-

Ukosefu wa ushahidi wa maridhiano/upatanisho ambayo yalikuwa yakifanywa ili kupata kiasi cha lita zote za mafuta ya petroli yaliyopokelewa katika kumbukumbu za ZITAS dhidi ya taarifa zilizopatikana kutoka bohari ya Mtoni.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Mamlaka ya Mapato Zanzibar ina utaratibu mzuri wa kufanya maridhiano au upatanisho (reconciliation) katika hatua ya upokezi wa mafuta kabla ya kurikodiwa katika mfumo au kanzidata ya ZITAS na rikodi zinafanyika kwa mujibu wa "Certificate of Quantity" ambayo inasainiwa na Mamlaka ya Mapato na wadau wengine nao ni TRA, ZURA, ZBS, ZAWEMA, "Surveyor", "Depot Representatives."

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa hoja nambari 7.1.2.17, 7.1.2.18 na 7.1.2.19 ni hoja moja inayoundwa na vipengele viwili. Hilo limabainishwa na Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kufanya mapitio katika

nyaraka zao. Kwa msingi huo, hoja na majibu yake yatakuwa kama ifuatavyo:-

**(a) Dosari katika Uandaaji wa Taarifa za Mafuta:**

Aidha, ukaguzi ulipitia taarifa za ukusanyaji wa mapato ya tozo ya mafuta ya petroli na kubaini kuwa tarehe ya mwisho ni ndani ya siku 7 baada ya mafuta ya petroli kuwasili kwenye bohari ya Mtoni. Kwa hiyo, kiasi chote cha mafuta ya petroli kinachopokelewa mwishoni mwa mwezi husika ambacho kinadaiwa hulipwa katika mwezi unaofuata. Kwa mantiki hiyo mapato yanayokusanywa katika mwezi uliopita yataripotiwa kidogo ikilinganishwa na mapato yatakayokusanywa mwezi unaofuata.

Hata hivyo, hapakuwa na ripoti ya makusanyo ya mapato iliyotayarishwa ili kuonyesha au kueleza bayana mapato ambayo yamevuka kwenye mwezi unaofuata lakini yanahusiana na mwezi uliopita (ikiwa yalipokelewa kwa sehemu kabla ya tarehe ya mwisho au yanayotarajiwa kupokelewa) kwa ufuatiliaji mzuri na utoaji taarifa sahihi kwa watumiaji wa ripoti hizo ambazo ZRB inawajibika kuripoti kwa kuzingatia ukweli kwamba taarifa za ZRB za mapato zinatokana na fedha taslimu wakati wadau wengine wanaweza kutoa taarifa za mapato zinazojumuisha malipo taslimu na fedha zinazotarajiwa kupokelewa (accrual basis).

Kutotayarisha ripoti ya kiasi cha mafuta ya petroli iliyopokelewa mwezi uliopita ambapo malipo yanatarajiwa kulipwa katika mwezi unaofuata (ikiwa yamepokelewa mapema au yanatarajiwa kupokelewa) husababisha kutolingana kwa taarifa ya mapato kati ya ZRB na wadau wengine wa Serikali na umma kwa ujumla. Kwa hivyo ZRB inaweza kuhusishwa na ubadhirifu wa mapato katikachanzo hiki.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar imepokea ushauri na tayari imeboresha taarifa zake ambapo malipo ya mafuta ya petrol iliyopokelewa mwezi uliopita na yanatarajiwa kulipwa kwa mwezi unaofuata yananakiliwa vizuri katika taarifa za utendaji na ufuatiliaji mapato. Hivyo, kwa vile ZRA inaripoti fedha taslimu, malipo ya fedha za mafuta yanarikodiwa kwa mwezi husika ambao fedha hizo zimelipwa na kuhakikiwa.

**(b) Madeni ambayo hayajaripotiwa yanaweza kupuuzwa na hivyo kupoteza mapato ya Serikali kutoka kwenye chanzo hiki.**

Maridhiano/mapatanisho (Reconcilliation) yafanyike ili kupata idadi sahihi ya lita zilizoingizwa katikamfumo wa ZITAS na zile halisi zilizopokelewa kutoka bohari ya Mtoni. Vilevile usuluhishi wa ritani zamafuta zilizowasilishwa dhidi ya malipo halisi unapaswa kufanywa katika kila mwezi ili kuwezesha

kufichua madeni yatokanayo na mafuta ya petroli kwa kila Kampuni kwa hatua za kufuatilia urejeshaji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha kwamba mapato yote yanayopindukia mwezi unaofuata au mwaka ujao wa fedha ambayo hayajakusanywa yawe na kumbukumbu za kutosha kwa ajili ya ufuatiliaji na kwa madhumuni ya kutoa taarifa sahihi kwa wadau wote.

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar imeshachukua hatua ambapo kwa sasa maridhiano (reconciliation) yanafanyika kila mwezi juu ya mafuta yaliopokelewa mtoni na yale yaliyoingizwa katika taarifa za mfumo wa ndani, na bakaa iliokuwa haijalipwa inawekwa katika kumbukumbu na inalipwa kwa wakati ndani ya mwezi bakaa ilipopindukia.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia majibu hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa bado Mamlaka za ushughulikiaji wa upakiaji na ushushaji wa mafuta Zanzibar kazi zao zinafanyika 'manual' bila ya kutumia mfumo mmoja wa kielektroniki. Ukosefu wa mfumo mmoja imezifanya Taasisi zinazohuaiana na ukusanyaji kodi inayotokana na mafuta kila moja kufanyakazi peke yake. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Taaisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) pamoja na Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC).

Katika hatua ya kutatua changamoto hiyo, ZRA imeshaishauri Serikali juu ya uwepo wa Mfumo mmoja utakaoziunganisha Taasisi zote tano na kuziwezesha kufanya kazi kwa pamoja jambo ambalo litazisaidia kupatikana kwa taarifa sahihi zitakazotumika kuongeza mapato ya Serikali.

## Hoja nambari 7.1.2.20: Dosari zilizobainika katika ukusanyaji wa mapato ya ukodishaji wa ardhi

Ukaguzi ulipitia mchakato wa ukusanyaji wa upangaji ardhi na kubaini kuwa ZRB iliwajibika kwa ukusanyaji pekee, mambo yote muhimu ya ukodishaji wa ardhi kama vile viwango vinavyotozwa, idadi ya wapangaji wanaohitajika kulipa ukodishaji wa ardhi na taratibu zote za mikataba yalifanywa na Kamisheni ya Ardhi. Hata hivyo mapitio ya taratibu za makusanyo katika chanzo hiki cha mapatoyalibaini kuwa Kamisheni ya Ardhi (COLA) inafanya kazi kwa mikono (operates manually) na ZRB inamiamala ya moja kwa

moja (Automatic) ya Ukodishaji wa Ardhi kupitia ZITAS.

Hata hivyo, pamoja na pengo hili la mfumo, hakukuwa na ushahidi wa maridhiano/mapatanisho ya mara kwa mara yaliyokuwa yakifanywa kati ya ZRB na Kamisheni ya Ardhi ili kupata usahihi wa idadi ya mikatabaya ukodishaji ardhi iliyopo na inayotakiwa kulipwa kila mwezi ili kuwezesha ukusanyaji wa mapato yanayotakikana katika chanzo hiki cha mapato.

Ufuatiliaji na uwajibikaji mzuri wa mapato kutoka kwenye chanzo cha ukodishaji wa ardhi ulikwamishwa. Zaidi ya hayo, Upotevu wa mapato ya Serikali kupitia madeni ya ukodishaji wa ardhi yasiyokusanywa(kukwepa kodi au kutoza malipo kidogo) hauwezi kuepukika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha kuwa vyombo viwili vinavyohusika na ukusanyaji wa ukodishaji wa ardhi (ZRB na Kamisheni ya Ardhi) vifanye kazi kwa pamoja ili kuimarisha ufuatiliaji, utoaji taarifa na uwajibikaji wa mapato ya Serikali kutoka kwenye chanzo hiki. Vyombo vyote viwili vinapaswa kukutana angalau kila robo mwaka na kujadili changamoto zinazotokea kwenye usimamiziwa mapato ya ukodishaji ardhi.

Ili kuhakikisha udhibiti mzuri wa ukodishaji wa ardhi Serikali inashauriwa kuazimia moja ya taasisi zake ZRB au Kamisheni ya Ardhi kushughulikia masuala ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuandaa mikataba ya ukodishaji na kufuatilia makusanyo kwa muda uliopangwa. Vinginevyo kuwe na ushirikiano kati ya ZRB na Kamisheni ya Ardhi ili kuhakikisha kila mkataba wa ukodishaji unaodaiwa unakusanywa na hatua za kurejesha zinachukuliwa kwa wakati.

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Katika kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya ardhi, Mamlaka ya Mapato Zanzibar kwa kushirikiana na na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makaazi ilifanya vikao vya pamoja tarehe 21/06/2023 ambacho kiliwashirikisha Kamishna Mkuu wa ZRA na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi na kukubaliana kuunda timu itakayohakiki na kupitia taratibu za ukusanyaji wa kodi ya ardhi. Timu imeundwa iliyojumuisha watendaji wa ZRA na COLA na kwa hatua za awali inahakiki mikataba yote na hatimaye kuwa na taarifa zilizosawa.

Aidha Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Mkaazi kwa kushirikiana na kampuni ya IGN FI imeingia makubaliano ya kuanzisha na kutekeleza mradi wa mfumo wa usajili wa Ardhi "Land Administration Registration Information System" ambao utazingatia upatikanaji wa taarifa za ardhi kwa wadau, ikiwemo ZRA ambao walialikwa kwa barua yenye kumbukumbu CBA.159/197/08/7 ya 27/10/2023 kutoa maoni yao. Kupitia mfumo huo ZRA itaunganishwa kupitia mfumo wa ZIDRAS kwa lengo la kupata taarifa za ukodishwaji

wa Ardhi.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa bado kuna changamoto ya upatikanaji wa taarifa za mapato yatokanayo na kodi ya ardhi. Hili limetokana na kutounganishwa kwa mfumo wa ZIDRAS na mfumo wa usajili wa ardhi na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali. Katika kutatua changamoto hiyo, ZRA imefanya mawasiliano kwa njia ya barua bila ya kupata majibu kutoka Kamisheni ya Ardhi (barua ya tarehe 6 Julai, 2023 yenye kumbukumbu nambari ZRA/BC.178/298/01/32 inahusika).

Kutokuwepo kwa mfumo wa pamoja katika ukusanyaji wa mapato ya kodi ya ardhi, kunasababisha changamoto zifuatazo:

a) Kuwepo kwa udanyanyifu wa taarifa za mapato. Hii inatokana na kwamba baadhi ya Wakodishwaji wa ardhi wanakuwa na mikataba ya ardhi ambayo inaonesha vipimo tofauti na uhalisia ulivyo.

b) Kulipwa kwa kodi ndogo ya ardhi ukilinganisha na ukubwa wa eneo husika.

c) Kutokuwepo kwa uratibu mzuri wa taarifa. Hili linatokana na ukweli kwamba ZRA huhitajika kufiatilia taarifa za ukodishwaji ardhi katika Kamisheni wakati kiuhalisia baada ya hatua za Mkodishwaji kufanyika, Kamisheni izipeleke taarifa za Mkodishwaji ZRA.

Katika kuchunguza utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC iliiandikia barua Kamisheni ya Ardhi siku ya tarehe 14/2/2024 yenye kumbukumbu nambari CE.81/204/02/45 hatua zilizofikiwa katika uungwanishwaji wa Mfumo wa Kodi ya Ardhi na Mfumo wa Mapato wa Mamlaka ya Zanzibar (ZIDRAS). Kamati imegundua mambo yafuatayo:

1. Kwamba sheria ya Kamisheni ya Ardhi nambari 6 ya mwaka 2015 katika kifungu chake cha 22(3)(b) imeainisha kuwa tozo pamoja na kodi za ukodishwaji wa ardhi itakayokusanywa na Kamisheni itakuwa ni chanzo chao cha mapato.
2. Kwamba kupitia Sheria mpya iliyoanzisha Mamlaka ya Mapato Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2022 katika kifungu chake cha 7, kimeeleza usimamizi wa sheria zisizokuwa za kodi zisimamiwe na Mamlaka ya Mapato baada ya Mawaziri wa Taasisi zinazosimamia sheria hizo kukubaliana. Kifungu hichi kimeeleza kwamba:

“Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Waziri anayehusika na sheria zisizokuwa za kodi, kuipangia Mamlaka usimamizi wa Mapato yoyote yanayotozwa chini ya sheria zisizokuwa za kodi”.

3. Kwamba Taasisi hizo tayari zimeshakubaliana kuhusiana maazimio ya uungwanishwaji wa Mifumo hiyo kupitia kumbukumbu (Minutes) za tarehe 21/6/2023.
4. Kwamba bado Kamisheni ya Ardhi haijatekeleza maazimio hayo yaliyofikiwa.

Kwa msingi huo, kwa vile bado kuna utekelezaji haujakamilika na jitihada zinahitajika kutatua kasoro zilizobainishwa na Mkaguzi, Kamati ya PAC inaibakisha hoja hii kwa hatua za utekelezaji.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa ZRA na Kamisheni ya Ardhi uhakikishe unaunganisha mifumo yao ya ukusanyaji mapato ya kodi ya ardhi ili kuiwezesha Serikali kupata mapato halisi kulingana na taarifa za ukodishwaji ziliopo.
2. Kuwepo na utaratibu mzuri wa upatikanaji wa taarifa za mikataba ya ardhi kwa wakati ili ZRA iweze kufuatilia wote watakaoshindwa kutimiza wajibu wao na kuwachukulia hatua stahiki.

## Hoja nambari 7.1.2.21: Madeni ya tathmini za kodi ya muda mrefu (Madeni yenye shida)

Ukaguzi ulipitia madeni ya kodi yaliyoripotiwa na kitengo cha usimamizi wa madeni na kubaini uwepo wa madeni yatokanayo na tathmini za kodi ya muda mrefu ya kiasi cha shilingi 2,600,294,721.80 na dola za Kimarekani 3,760,749.39. Juhudi za kuhakikisha madeni hayo yanalipwa zilionekana sio za kuridhisha. Uwepo usahihi na urejeshaji wa tathmini za kodi zilizochelewa kwa muda mrefu hazikuweza kuthibitishwa. Kwa hiyo, Serikali inaweza kupoteza mapato kutokana na madeni ya kodi yasiyolipika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kuhakikisha usahihi na uwepo wa madeni ya tathmini za kodi ya muda mrefu kwa lengo la kuchukua hatua stahiki za urejeshaji.

**Orodha ya madeni ya muda mrefu ya tathmini ya kodi yanaonekana katika Jadweli lifuatalo:-**

| S/N | Jina la Mlipakodi | Deni Halisi | | Kiasi kilicholipwa | | Kiasi cha Misamaha | | Bakaa ya deni | | Muda wa deni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | USD | TZS | USD | TZS | USD | TZS | USD | |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Dullah Motors Ltd | 40,787,494.00 | - | 8,000,000 | - | - | - | 32,787,494.00 | - | 20.05.2019 |
| 2. | J & Cc Electrical And Plumbing | 11,502,777.00 | 247,904.64 | - | - | - | - | 11,502,777.00 | 247,904.64 | 06.10.2020 |
| 3. | Kassim Daud Othman | 50,414,886.00 | - | - | - | - | - | 50,414,886.00 | - | 15.12.2020 |
| 4. | Mhana Contractor &Enterprises | 71,186,314.66 | - | 17,000,000 | - | - | - | 54,186,314.66 | - | |
| 5. | Stecol Corporation | | 3,018,770.99 | | | | | | 3,018,770.99 | 16.03.2021 |
| 6. | Zawiya Tanzania Traders | 450,730,311.98 | - | 11,000,000 | - | - | - | 439,730,311.98 | - | 12.06.2020 |
| 7. | Salum Ali Abdalla | 8,342,207.00 | - | - | - | - | - | 8,342,207.00 | - | 04.02.2020 |
| 8. | Kivulini Garden Lodge (Nungwi) | 17,065,106.95 | 12,227.76 | 1,000,000 | 200 | | | 16,065,106.95 | 12,027.76 | 14.04.2021 |
| 9. | Teddys Place Ltd | -- | 482,046.00 | -- | -- | -- | -- | -- | 482,046.00 | 13.07.2020 |
| 11. | Frasi Company | 45,074,403.65 | | | | | | 45,074,403.65 | | 27.04.2021 |
| 12. | Yasser Provision Stores | 50,717,592.69 | | 10,000,000 | | 10,885,732.49 | | 29,831,860.20 | | 31.08.2021 |
| 13. | Dezo Civil Contractor | 700,995,054.64 | | 10,000,000 | | | | 690,995,054.64 | | 03.05.2021 |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 14. | Kiwango Security Gurd Limited | 248,809,517.91 | _ | _ | _ | _ | _ | 248,809,517.91 | | 02.02.2021 |
| 15. | A1 Outdoor (T) Ltd | 98,257,911.49 | | 24,000,000 | _ | _ | _ | 74,257,911.49 | | 29.07.2021 |
| 16. | Said Omar Haji | 87,523,397.23 | - | - | - | - | | 87,523,397.23 | | |
| 17. | Supper Market Supplies | 4,278,695.91 | | | | | | 4,278,695.91 | | |
| 18. | Mast International | 856,494,783.18 | | 50,000,000 | | | | 806,494,783.18 | | 28.05.2021 |
| **Total** | | **2,742,180,454.29** | **3,760,949.39** | **131,000,000** | **200** | **10,885,732.49** | **-** | **2,600,294,721.80** | **3,760,749.39** | |

### Majibu ya Uongozi wa Mamlaka

Kwa sasa divisheni ya uwajibikaji na madeni ipo katika mchakato wa kuyaorodhesha na kuyapitia upya madeni yote Pamoja na kuendelea kuyafuatilia kwa lengo la ugomboaji, madeni yatakayobainika kuwa hayalipiki yatawasilishwa kwa Bodi ya wakurugenzi kwa kupata ushauri wa hatua mbadala za kuendelea nazo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kuwa licha ya madeni hayo kuwa ni ya muda mrefu lakini bado ZRA imo katika mchakato wa kuyafuatilia wakati kiuhalisia Kamati ilitegemea ipatiwe hali halisi ya madeni yote yaliyolipwa, yaliyobakia na yaliyosamehewa, yasiyolipika pamoja na taarifa nyengine muhimu za madeni hayo.

Kwa mnasaba huo, Kamati imegundua kuwa uwepo wa madeni hayo ya muda mrefu kunapelekea kutokuwepo kwa thamani halisi ya fedha itakayolipwa. Kwa bahati mbaya hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake, haikupatiwa mchanganuo unaoonesha taarifa hizo kama ilivyoelezwa katika Ripoti ya Mkaguzi. Kwa vile kuna baadhi ya taarifa zimekosekana kuwasilishwa mbele ya Kamati, hoja hii inaendelea kubakia kwa hatua za

utekelezaji.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa ZRA uharakishe unafanya uhakiki wa madeni ya tathmini za kodi ya muda mrefu kwa lengo la kuyatambua na kuchukua hatua stahiki za urejeshaji wa malipo ya madeni hayo.

## Hoja nambari 7.1.2.22: Tathmini za kodi zenye migogoro iliyochelewa kwa muda mrefu (kuanziamwaka 2014 hadi mwaka 2016)

Ukaguzi ulipitia madeni yaliyoripotiwa na kitengo cha usimamizi wa madeni ya kodi yalibaini tathmini ya muda mrefu ya kodi ambayo haijatatuliwa kwa muda mrefu tangu mwaka 2014. Ukaguzi wa hali halisi ya madeni hayo yenye mgogoro yalionyesha hakuna dalili zozote za kurejeshwa kwani juhudi za uongozi za kurejesha madeni hayo hazikuzaa matunda. Hatima ya tathmini za kodi zenye utata kwa muda mrefu hazikuweza kubainishwa na Uongozi. Vile vile madeni hayo yalikosa ushahidi wa kuwasilishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa hatua zaidi za kurejesha.

Uwepo na urejeshwaji wa madeni ya tathmini za kodi zenye migogoro ambazo hazijasuluhishwa kwa muda mrefu zilikuwa zinatia shaka. Kwa hiyo, Serikali inaweza kupoteza mapato kutokana na madeni ya kodi yasiyolipika. Iwapo jitihada zote za kurejesha tathmini za muda mrefu za kodi zenye mgogoro ambazo hazijasuluhishwa hazizai matunda.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRB kupeleka madeni hayo ya kodi kwa Bodi ya Wakurugenzi ili kutafuta ushauri kuhusu hatua mbadala za kurejesha madeni hayo. Hadi ukaguzi unamalizika hali halisi ya madeni hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 105: Kodi ya Muda Mrefu yenye Migogoro Iliyotathminiwa kuanzia 2014-2016**

| S/N | Jina la Mlipa Kodi | Muda wa Tathmini | Deni halisi la Kodi | | Muda wa uwepo wa deni | Maelezo ya Ufuatiliaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | TZS | US $ | | |

| S/N | Jina la Mlipa Kodi | Muda wa Tathmini | Deni halisi la Kodi | | Muda wa uwepo wa deni | Maelezo ya Ufuatiliaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Al-Batna Contractors | JULY 2010 – SEPT 14 | 834,169,111.63 | | 2015 | On 10.02.2022 the taxpayer was served with a notice to appear at zrb vide letter reference number zrb/to/g.4/ vol.1/65 to discuss on this outstanding tax debt for further recovery measures but he could not appear. |
| 2 | Step Two Company Ltd | JAN 11-DEC 12 | 42,044,527.00 | | 2014 | On 09.02.2022 the taxpayer was served with a notice to appear at zrb vide letter reference number zrb/ ht/s.18/vol.1/56 to discuss on this outstanding tax debt for further recovery measures but he could not appear. Review of the tax debt by the debt unit revealed that the taxpayer paid tzs 8,150,000 to fulfil condition of the appeal but he could not be attended. The debt unit recommended the tax assessed to be reviewed by rau. |

| S/N | Jina la Mlipa Kodi | Muda wa Tathmini | Deni halisi la Kodi | | Muda wa uwepo wa deni | Maelezo ya Ufuatiliaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Evidence of review by rau was lacking. |
| 3 | Kasha Boutique Hotel<br>Dhow Inn Hotel/Gusama | AUG 2009<br>-<br>DEC 15 | | 75,868.24 | 2016 | On 14.03.2022 the taxpayerwas served with a notice<br>to appear at zrb vide letterreference number zrb/ ht/k.22/vol.1/36 to discusson this outstanding tax debt for further recovery measures but he could notappear. |

| S/N | Jina la Mlipa Kodi | Muda wa Tathmini | Deni halisi la Kodi | | Muda wa uwepo wa deni | Maelezo ya Ufuatiliaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Zanzibar Tea Packers. | | 55,509,499.16 | | 2015 | On 09.02.2022 the taxpayerwas served with a notice to appear at zrb vide letter reference number zrb/tr/z.4/vol.1/33 to discuss on this outstanding tax debt for further recovery measures but the letter returned to zrb unsuccessful as the companyis owned by new owners since 2019 only company symbol is still in used. |
| 5 | Cristal ResortLtd | | 15,669,585 | 98,515 | 2015 | The taxpayer whereabouts is unknown and new owner who was not aware of the whereabouts of the previousowner owns the company. |
| 6 | Al Mubeen. G.Group | | 45,951,129 | | 2015 | The taxpayer whereabouts is unknown. |
| 7. | Salim Rashid Nassor | | 63,893,008 | | 2014 | |

| S/N | Jina la Mlipa Kodi | Muda wa Tathmini | Deni halisi la Kodi | | Muda wa uwepo wa deni | Maelezo ya Ufuatiliaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Total | | | 1,057,236,859.79 | 174,383.24 | | |

**Majibu ya Uongozi wa Mamlaka**

Kwa sasa divisheni ya uwajibikaji na madeni ipo katika mchakato wa kuyaorodhesha na kuyapitia upya madeni yote Pamoja na kuendelea kuyafuatilia kwa lengo la ugomboaji, madeni yatakayobainika kuwa hayalipiki yatawasilishwa kwa Bodi ya wakurugenzi kwa kupata ushauri wa hatua mbadala za kuendelea nazo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa majibu na mapendekezo ya hoja hii ni kama yalivyooneshwa katika hoja nambari 7.1.2.21 inayohusiana na Madeni ya tathmini za kodi ya muda mrefu.

## ZIARA YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KATIKA KITUO CHA TAIFA CHA KUHIFADHIA TAARIFA CHA SERIKALI (NATIONAL INTERNET DATA CENTRE) NA IDARA YA UKAGUZI NA UPELELEZI WA WALIPAKODI - JIJINI DAR ES SALAAM

## UTANGULIZI:

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) pamoja na Watendaji wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar walifanya ziara ya kimafunzo ya siku moja katika Kituo cha Kuhifadhia Taarifa za Serikali (Data Centre) pamoja na Idara ya Ukaguzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Ziara hiyo ilifanyika siku ya Alhamis ya tarehe 8 Febuari, 2024.

## WASHIRIKI WA ZIARA

Ziara hiyo iliwashirikisha wafuatao:

1. Ujumbe wa Kamati ya PAC ukiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo;

2. Watendaji kutoka ZRA wakiongozwa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Mheshimiwa Juma Makungu Juma.

3. Watendaji kutoka TRA ambao waliongozwa na Naibu Kamishna ‘operation’ Bwana Hashim Mgoda.

4. Mtendaji kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) ambae ni Ndugu Shekhe Abdalla Ali.

## UFUNGUZI WA KIKAO

Baada ya kufanya pande zote mbili kujitambulisha, Mwenyekiti wa Kamati ya PAC alikifungua kikao saa 3:24 za asubuhi kwa kumupmba Mkuu wa Kituo cha ‘National Internet Data Centre’ Mhandisi Sestenesi Malimi kumruhusu Mtaalamu Menaja Francis Ausoni Ntoga kueleza jinsi gani Mfumo wao wa kuchakata taarifa unavyofanya kazi. Aidha, ilipofika saa 8:05 mchana, Kamati ya PAC ilikutana na watendaji wa TRA kujifunza kuhusiana na ufanyaji kazi wa Idara yao ya Ukaguzi na upelelezi wa kodi Naibu Kamishna Ukaguzi na Upelelezi wa Kodi Bibi Felisiana Nkami alifafanua kwa undani majukumu wanayoyatekeleza.

## MAMBO YALIYOZUNGUMZWA KATIKA VIKAO

Katika uwasilishaji uliofanyika, mada mbili tofauti zilizwasilishwa kama ifuatavyo:

**Mada ya Kwanza: Ufanyaji kazi wa Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato kwa njia ya Kielektroniki.**

Mtaalamu Kituo cha ‘National Internet Data Centre’ Menaja Francis Ausoni Ntoga aliieleza Kamati jinsi Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato kwa njia ya Kielektroniki (Electronic Revenue Collection System e-RCS unavyofanya kazi zake kwa kueleza mambo ya msingi yafuatayo:

1. Kituo hicho kimetengenezwa pamoja na Mkonga wa Taifa na kuzinduliwa mwaka 2015 na Rais Jakaya Kikwete ikiwa ni kituo cha kimkakati cha kuhifadhia ‘data’ ambapo wanatoa huduma za kupangisha mifumo yao kwa Taasisi za Serikali na Makampuni ya kibiashara. Wanafanya hivyo, kwasababu wanao mfumo mzuri wa ubaridi (cooing system) pamoja na umeme wa uhakika.

2. Kituo hicho kipo katika kiwango cha namba 3 kati ya nne ziliopo Ulimwenguni. Hivyo, kimekidhi matakwa yote ya kitaifa na kimataifa na kimekosa kufikia namba 4 kwa vile wanategemea chanzo kimoja kikuu cha umeme isipokuwa wanalo

jenereta la 'automatic'.

3. Kituo kinafanaya kazi zake kwa kutumia Mfumo Maalum wa Ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za Mapato kwa njia ya Kielektroniki (umeandaliwa na wazawa na kuzinduliwa tarehe 1 Juni, 2017) ambapo taarifa zilizokusanywa na Taasisi na Makampuni ya ukusanyaji mapato hutuma taarifa zao na kuchakatwa ili kupatikana kodi na tozo ambayo inatakiwa ilipwe katika Serikali zote mbili za Tanzania.

4. Hadi sasa, Mfumo huo umeweza kuiunganisha nao mifumo saba (7) ya mapato/biashara ya Taasisi za kodi ikiwemo Taasisi za Fedha (benki), Watoa huduma za TV na Redio, Makampuni yote ya simu na watoa huduma za uzalishaji viwandani.

5. Taasisi ya Uhifadhi 'Data' inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo wasimamizi wake hawalipi ada yoyote licha ya kuwa wao ndio watumizi wakuu wa kituo hicho, bado mfumo unahitaji kufuatiliwa na kukaguliwa ili kuzuia udanganyifu, Taasisi za kodi bado hazijakamilisha wakuwaunganisha na mifumo yao wote wateja wao na kushindwa kuungwa katika Mfumo huo mfano Taasisi za uleteji fedha nchini mfano Said Mmaka na Watalii wanaoingia nchini na mfumo wa ZanMalipo bado nao haujaungwa,

6. Mfumo huo ni wa Serikali ambao unaongozwa na timu ya Wataalamu kutoka Taasisi Kuu za kodi (TRA na ZRA) ambao mfumo unazitambua kodi zinazotumwa kupitia eneo ambalo huduma imetumiwa.

7. Mpango uliopo ni kuanzisha 'Data Centre' kama hiyo kwa upande wa Zanzibar.

**Mada ya Pili: Ufanyaji kazi wa Idara ya Ukaguzi na Upelelezi wa Kodi**

Naibu Kamishna Ukaguzi na Upelelezi wa Kodi Bibi Felisiana Nkami pamoja na Mkuu wa Ukaguzi wa Kielektroniki Bwana Lebaratus Maboa waliielezea Kamati mambo yafuatayo:

1. Idara ya Ukaguzi wa Kodi wanazo Ofisi katika Kanda Saba ndani ya Tanzania zikiwemo za Kanda za Dar es Salaam, Kaskazini na Nyanda za juu Kusini lakini kwenye uchunguzi wa kieletroniki wanao wafanyakazo 13 tu wanaofanya kazi katika zoni tatu ziliopo Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

2. Idara hiyo inashughulikia malalamiko yanayowasilishwa kwao kutoka katika vyanzo vyao vya taarifa kwa wafanyabiashara ambao hawalipi kodi au wanakwepa kodi ambapo hutumia sheria yao ya 'Tax Administration Act' ambayo kwa ktumia

kibali cha Kamishna Mkuu huwapa nguvu ya kufanya 'search', kuzuia na kupiga mnada mali za Mlipakodi, kuruhusu kulipa kodi kwa awamu pamoja na kusamehe kodi kwa kufuata utaratibu wa kupelekea Bungeni.

3. Idara pia huwa inafanya 'patrol' kwa watu wanafanya magendo na kukwepa ulipaji kodi.

4. 'Digital Forensic Lab' inafanyakazi zake ikiwa na wafanyakazi wachache (13) Tanzania nzima ambapo hupokea maombi ya kufanya uchunguzi wa kielektroniki baada ya kupata maombi ya maandishi kutoka katika Taasisi yao. Hilo linatokana na 'field' hiyo haisomeshwi Tanzania na inahitaji fedha nyingi kuwasomesha nje ya nchi.

5. 'Lab inavifaa vichache vya kufanyia kazi kunakotokana na kwanba gharana za ununuzi ni kubwa sana ambapo 'computer' moja inahitaji dolar' elfu ishirini (20,000 USD).

## MAPENDEKEZO YA KAMATI YA PAC

ZRA ihakikishe inawekeza katika 'Forensic Lab' zake kwa kuwaendeleza kimafunzo wafanyakazi wake na kununua vitendea kazi licha ya kwamba masomo yao yanagharimu fedha nyingi.

## HITIMISHO

Kikao hicho kilifungwa na Mwenyekit wa Kamati ya PAC saa 9:23 za mchana na kuwatika ZRA kujifunza kwa yale yote mazuri waliyoyaona ili nao wakayanfanyie kazi watakapofika katika maeneo yao ya kazi kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali.

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022

# 7.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## 7.2 WIZARA YA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

### 7.2.4 TUME YA UKIMWI

### Taarifa ya Mapato

Katika kipindi cha rnwaka wa fedha 2021/2022 Turne ya Ukirnwi Zanzibar ilikadiriwa kupokea jurnla ya shilingi 1,193,746,400 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Turne ya Ukirnwi Zanzibar ilipokea kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina jurnla ya shilingi 840,231,150 sawa na asilirnia 70 ya rnakadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 353,515,250 sawa na asilirnia 30.

#### Majibu na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Tume ya Ukimwi haijawasilisha majibu ya Hoja ya taarifa ya Mapato siku mbili kabla ya Kamati kukutana kwa majadiliano na Tume hii kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 97(3) ya Bazara la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua kukosekana kwa asilimia 30 ya mapoto iliathiri vipi utekelezaji wa shughuli za Tume na kuelezwa kwamba shughuli za utoaji uelewa kwa jamii kuhusiana na masuala ya maambukizi ya UKIMWI Zanzibar. Kamati pia ilielezwa kwamba hawakuwasilisha majibu ya taarifa ya mapato kutokana na kutokujua utaratibu wa kujibu.

Aidha, Tume hawakuwa na uelewa kwamba fedha za ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina zinatambulika kuwa ni mapato zitakapoingia katika hesabu yao. Hivyo, Kamati imeitaka Tume kuwasilisha majibu hayo kabla ya kumaliza ratiba ya kazi zake.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Tume ihakikishe inazitambua fedha za ruzuku zinazotoka Serikalini kuwa ni miongoni mwa mapato yake na waziingize kwenye hesabu zao za mwisho wa mwaka.

### Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Tume ya Ukimwi ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,193,746,400 kati ya fedha hizo shilingi 963,096,400 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 230,650,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Tume ya Ukimwi Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 840,231,150 kati ya fedha hizo shilingi 807,347,995 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilima 84 ya makadirio, kukiwa na upungufu na shilingi 155,748,405 sawa na asilimia 16 ya makadirio na shilingi 32,883,155 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 14 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 197,766,845 sawa na asilimia 86 ya makadirio.

### Majibu na Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Tume ya Ukimwi haijawasilisha majibu ya Hoja ya taarifa ya Matumizi siku mbili kabla ya Kamati kukutana kwa majadiliano na Tume hii kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 97(3) ya Bazara la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kwamba watendaji wa Tume hawakuwa na uelewa wa kutambua kuwa matumizi ya fedha kutoka kwa Wahisani wa Maendeleo zinahitajika kuonekana katika hesabu yao ya mwisho wa mwaka. Sambamba na hilo mambo ya ziada yafuatayo yalibainika:-

1) Ufinyu wa nafasi ya kufanyia kazi Watendaji wa Tume ya Ukimwi Unguja. Kamati imegundua kwamba Tume inatumia jengo la kukodi linalomilikiwa na Mtu binafsi ambapo wanatumia vyumba saba tu katika jengo hilo visivyotosheleza mahitaji yao. Kutokana na hali hiyo, Tume imelazimika kuhifadhi baadhi ya vifaa vyake katika ‘container’ liliopo nje (pembeni) ya jengo hilo. Eneo hilo halipo salama kwa kuhifadhia vifaa vya Serikali ikiwemo ‘generator’.
2) Kuwepo kwa gharama kubwa ya malipo ya kodi ya Ofisi wanayotumia. Kamati imeelezwa kwamba Tume itahitajika kulipa jumla ya shilingi milioni 18 kwa mwaka ikiwa ni malipo ya kodi ya Ofisi hiyo.
3) Jengo la awali walilokuwa wanatumia Tume ni bovu na bado halijafanyiwa matengenezo na Wawekezaji waliokabidhiwa jengo hilo.
4) Tume imetumia jumla ya shilingi 18,350,000 kulipia gharama tofauti za kuhama

kutoka Mji Mkongwe na kuhamia eneo la Kwa Mchina Mwisho ambapo Mamlaka ya Mji Mkongwe iliahidi kuzilipa. Barua ya tarehe 31 Mei, 2022 yenye kumbukumbu nambari ZAC/SHT.30/4/VOL.IV/8 inahusika.

## Hoja nambari 7.2.4.1: Dosari zilizojitokeza katika utayarishaji, uandaaji na ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka 2021/2022

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, baada ya kupitia taarifa za fedha, ukaguzi umebaini kuwepo na dosari katika utayarishaji wa hesabu hizo za mwisho wa mwaka husika. Dosari zenyewe ni kama ifuatavyo:

a) **Kutojumuishwa fedha za mapato katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 661,520,670**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 661,520,670 hazikujumuishwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka 2021/2022, ikiwa ni makusanyo ya fedha zinazotokana na ruzuku kutoka kwa wahisani wa maendeleo.

Kutojumuishwa fedha za mapato katika uandaaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka ni kwenda kinyume na kifungu nambari 121 cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, aidha ni kinyume na kifungu nambari 18 cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 46: Kutokuoneshwa kwa mapato katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka**

| Namba | Jina la Mfadhili | Hesabu nambari | Kiasi kilichokadiriwa (Shs) | Kiasi kilichoingia (Shs) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | UNFPA | 0404438000 | 80,360,000 | 309,446,400 |
| 2 | GF | 0404125000 | 153,382,000 | 252,860,770 |
| 3 | UNICEF – Tume ya UKIMWI Zanzibar | 0404309000 | _ | 38,015,000 |
| 4 | UNAIDS – Tume ya | 0404309000 | _ | 61,198,500 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | UKIMWI | | | |
| **Jumla** | | | **233,742,000** | **661,520,670** |

**Majibu ya Uongozi**

Fedha ambazo zinadaiwa kuwa hazikujumuishwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka 2021/2022, Tsh 661,520,670, ni fedha za Washirika wa Maendeleo ambazo mara nyingi zinaingia kati kati ya mwaka na husomeka off budget. Miaka ya nyuma tulikuwa tunaziingiza kwenye final account kwa njia ya maelezo (NOTE). Kwa mwaka huu 2021/2022 ufungaji wa hesabu ulibadilika na ulitaka fedha za Wahisani zijumuishwe kwenye mfumo kabla bajeti ya Serikali haijapitishwa na BLW. Hii inashidnikana kwa sababu mwanzoni mwa bajeti huwa hatuna taarifa ya kiwango gani cha fedha Wahisani hao wamaendeleo watatuingizia. Hata hivyo, Fedha ambazo hazikujumuishwa katika mfumo ni fedha ambazo zilikaguliwa na Wakaguzi wa Nje (CAG) pamoja na vielelezo vyake vyote na baadae Wakaguzi walitutaka tuwasilishe tena taarifa hizo za hesabu za mwisho kitu ambacho tulikifanya. Aidha fedha hizo zimekuwa zikikaguliwa kila robo mwaka na Mkaguzi wa Ndani na zikiwasilishwa katika vikao vya robo mwaka vya Bodi ya Tume ya UKIMWI.

Fedha zenyewe ni kama ifuatavyo-:

| | |
|---|---|
| UNFPA UNDAP | TZS 309,446,400 |
| GLOBAL FUND | TZS 252,860,770 |
| UNAIDS | TZS 61,198,500 |
| UNICEF | TZS 38,015,000 |
| **JUMLA** | **TZS 661,520,670** |

**b) Kutokujumuishwa kwa fedha za matumizi katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 613,326,389.29.**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 613,326,389.29 hazikujumuishwa katika taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka 2021/2022, ikiwa ni matumizi ya fedha zinazotokana na ruzuku kutoka kwa wahisani wa maendeleo.

Kutojumuishwa fedha hizo katika taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka ni kwenda kinyume na kifungu nambari 18(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 47: Matumizi ambayo hayakuoneshwa kwenye taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka**

| Namba | Jina la Mfadhili | Hesabu Nambari | Kiasi kilichoingia | Kiasi kilichotumika |
|---|---|---|---|---|
| 1 | UNFPA | 0404438000 | 309,446,400.00 | 306,282,988.88 |
| 2 | GF | 0404125000 | 252,860,770.00 | 234,387,453.67 |
| 3 | UNICEF – Tume ya UKIMWI Zanzibar | 0404309000 | 38,015,000.00 | 11,457,446.74 |
| 4 | UNAIDS – Tume ya UKIMWI Zanzibar | 0404309000 | 61,198,500.00 | 61,198,500.00 |
| **Jumla** | | | **661,520,670** | **613,326,389.29** |

**Majibu ya Uongozi wa Tume**

Kama inavyoonekana kwamba fedha hizo ni za Washirika wa Maendeleo. Na kama ilivyoelzwa katika hoja iliyotangulia kwamba kilichokosekana ni ule utaratibu wa kuingiza taarifa za Fedha za Washirika wa Maendeleo wakati wa makadirio ya Bajeti kama ilivyoelezwa kwenye majibu ya hoja 7.2.4.1 (a). Baada ya kukaa na Wakaguzi walitutaka tufanye marekebisho ya uandishi wa taarifa hiyo na kuiwasilisha tena Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kitu ambacho tulikifanya. Aidha fedha hizo huwa tunaziwasilisha kwa kila robo mwaka wa matumizi ya fedha Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Bodi ya Makamishna Tume ya UKIMWI na kwa Washirika wa Maendeleo. Kumbukumbu za taarifa hizo zote zipo.

c) **Hesabu za mwisho wa mwaka zilizofungwa bila ya kufuata muongozo wa ufungaji wa hesabu ambapo hakuna segment report, disclosure inventory, receivable and payable**

Kufuatia kumalizika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kuanza kwa hatua za uandaaji wa taarifa za fedha (financial statement) za Taasisi za Serikali, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ipo katika maboresho ya uandaaji wa taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2022. Kutokana na miongozo ya Kimataifa ya utayarishaji na uandaaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa “International Public Sector Accounting Standards Board” za

uandaaji wahesabu za mwisho wa mwaka kupitia IPSAS 18-Segment Reporting inazitaka Serikali kuu pamoja na taasisi za serikali ambazo zinaandaa “Consolidated Financial Statement” kuweza kujumuisha taarifa za ziada katika “Notes to the Financial Statements” katika hesabu husika kuonyesha “segment reporting” ambazo zitazingatia “Services or Geographical Segment”.

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini Tume ya UKIMWI Zanzibar haikufuata miongozo ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 ambacho kimempa mamlaka Mhasibu Mkuu wa Serikali kutoa miongozo ya masuala ya ufungaji wa hesabu kwa Maafisa Masuuli (Accounting Officers) ambacho ndicho kilichompa mamlaka Mhasibu Mkuu wa Serikali kufanya hivyo.

Kutofuata miongozo ya uandaaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea kwenda kinyume na miongozo ya kitaifa na kimataifa na kusababisha hesabu zilizoandaliwa kukosa usahihi na ithibati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya UKIMWI kuhakikisha kwamba katika utayarishaji na uandaaji wa hesabu za mwisho wa mwaka unafuata miongozo ya kitaifa na kimataifa ya uandaaji wa hesabu zake na kwa mujibu wa miongozo na sheria husika.

### Majibu ya Uongozi wa Tume

Kama ilivyoelezwa kwenye dosari ya ukaguzi kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ipo katika maboresho ya uandaaji wa taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2022. Ni kweli baadhi ya taarifa zilikosekana (Segment Report) kwenye hesabu za mwisho wa mwaka za Tume. Hii ilitokana na ugeni wa kuandika ripoti hiyo kulingana na maboresho yaliyofanyika. Hata hivyo marekebisho tuliyafanya na kuingiza raarifa zote kama zilivyotakiwa na kuziwasilisha tena Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Mkaguzi kuziainisha hoja katika vipengele vitatu tofauti (yaan (a), (b) na (c)), Kamati ya PAC imegundua kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake kulikuwa na dosari kadhaa katika utayarishaji, uandaaji na ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ambazo zilizchangiwa zaidi na kutokuwa na uelewa kwamba fedha hizo zinatakiwa zionekane katika hesabu zao.

Hali hiyo imesababishwa na Tume kutofuata muongozo nambari 2 uliotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango hususan kwa kushindwa kuziainisha fedha za mapato na matumizi za Wahisani pamoja kutoandaa ‘segment report’ ya hesabu zao. Hata hivyo,

Kamati imeridhika na majibu ya Tume kwa vile tayari wamerekebisha dosari hizo kwa kuziingiza taarifa hizo katika hesabu zao za mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa mnasaba huo, hoja hiyo imeondolewa.

## Hoja nambari 7.2.4.2: Kukosekana kwa taarifa za kumbukumbu zilizothibitisha uhalali wa malipo yaliyolipwa kwa njia ya fedha taslim shilingi 4,066,850

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ukaguzi ulipitia hati za malipo pamoja na vielelezo mbali mbali vilivyofanyiwa malipo na kubaini jumla ya shilingi 4,066,850 zilitumika kwa ajili ya huduma mbali mbali kwa njia ya fedha Taslim, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa malipo kwa njia ya fedha taslim na kukosekana kwa taarifa za kumbukumbu zilizotiwa Saini mapokezi ya fedha hizo kama ni kielelezo kinachothibitisha uhalali wa mapokezi ya fedha hizo.

Kufanya malipo kwa njia ya fedha Taslim kunaweza kupelekea kujitokeza kwa matumizi yasiyo ya lazima ambayo yataambatana na upotevu wa fedha za umma na kupelekea Serikali kupata hasara jambo ambalo litakwamisha utekelezaji wa malengo ya taasisi waliyojipangia.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya UKIMWI Zanzibar kuhakikisha unatekeleza maagizo ya Serikali ya kutotumia malipo kwa fedha Taslim ili kuepuka vishawishi vinvyopelekea upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume kuhakikisha kwamba Sheria za fedha na Kanuni yake ya Usimamizi wa Fedha, 2021 zinasimamiwa ipasavyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

**Jadweli nambari 48: Malipo yaliyolipwa kwa fedha Taslim bila ya uwepo wa kumbukumbu za uthibitisho wa uhalali wa mapokezi**

| Tarehe | Hati Nam. | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 16/06/2022 | CO5PV2100000594 | 1,411,500 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 26/05/2022 | CO5PV2100000577 | 2,655,350 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mapazia |

| | | |
|---|---|---|
| **Jumla** | **4,066,850** | |

**Majibu ya Uongozi**

Tume ilipatiwa barua ya kuhama ofisi zake za Mji Mkongwe ili kupisha mipango ya serikali katika ofisi hizo. Gharama za kuhama zilitakiwa kusimamiwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe. Hata hivyo wakati wa kuhama ulipofika Uongozi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe haukutowa mashirikiano ya kugharamia gharama za kuhama kama tulivyoelezwa, hivyo kupelekea Tume kubeba gharama hizo. Kwa vile kipindi cha kufungwa kwa matumizi ya fedha za serikali kilikuwa kinakaribia njia pekee ya kufanikisha zoezi la kuhama ilikuwa ni kufanya malipo husika kwa njia ya fedha taslim (cash). Jumla ya shilingi 1,411,500/- ni gharama kwa ajili ya ujenzi wa sakafu ya kontena (kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vya ofisi vilokosa nafasi kutokana na ufinyu wa eneo la ofisi), kuweka jenereta (tulilohama nalo kutoka Mji Mkongwe) pamoja na gharama za ufundi. Shilingi 2,655,350 zilitumika kwa ununuzi wa vitambaa vya mapazia, henga, doments pamoja ufundi. Stakabadhi za matumizi hayo zote zinapatikana.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imegundua sababu kuu kujitokeza kwa hoja hii ni kukosekana kwa mashirikiano ya karibu kulikochangiwa na watendaji wa Tume ya Ukimwi kushindwa kumpatia Mkaguzi vielelezo vya malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi na ununuzi wa mapazia. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilipoyapitia madokezo ya tarehe 01/06/2022 na tarehe 14/06/2022 ilibaini vielelezo vya matumizi vipo na vilikuwa ni halali.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Tume ya Ukimwi wafanye kazi kwa karibu na Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kumpatia vielelezo vyote vianvyohitajika wakati wa ukaguzi wake.

## TUME YA UKIMWI - PEMBA

## Hoja Nambari 7. 2. 4.3: Ulipwaji wa posho la likizo kinyume na Kanuni ya Utumishi wa Umma

Kanuni ya 58(1)(a) ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inaeleza kwamba “Mtumishi

wa Umma atastahiki kupewa likizo la siku ishirini na nane za kazi ndani ya miezi kumi na mbili na atastahiki posho la likizo kila baada ya miaka mitatu.”

Baada ya kupitia majalada ya watumishi (Personal File) ukaguzi umebaini kuwa Tume ya UKIMWI Pemba inawalipa watumishi wake shilingi 250,000 kwa kila mtumishi anapokwenda likizo na si kila baada ya miaka mitatu kama kanuni inayvoeleza. Hata hivyo kwa mujibu wa matoleo ya Utumishi, mtumishi yoyote anaekwenda likizo atalipwa stahiki ya shilingi 100,000 kwa ajili ya huduma ya likizo hiyo ambapo malipo hayo yatafanyika kila baada ya miaka mitatu na sio kila mwaka.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Kanuni ya 58(1)(a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya UKIMWI Pemba kuhakikisha unazingatia matoleo na kanuni za Utumishi wa Umma ili kuepusha kujitokeza kwa migogoro ya kiutumishi.

**Majibu ya Uongozi wa Tume**

Ni kweli Tume ya UKIMWI imewalipa watumishi wake shilingi 250,000 mtumishi anapokwenda likizo. Utaratibu huu wa kulipa kiwango hichi ulipitishwa na Kikao cha 46 cha Bodi ya Tume ya UKIMWI Zanzibar kilichofanyika tarehe 30/03/2017 ikiwa ni Ajenda Nam. 3 kifungu namba 9.1.1 na 9.1.2.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Kikao cha Bodi ya Tume ya Ukimwi ndio kilichopitisha uwamuzi wa kulipa posho la 250,000 badala ya kulipa 100,000 kwa watumishi wake, bila ya kupata Muongozo na Maamuzi ya Tume ya Utumishi (kinyume na utaratibu).

Katika kufuatilia utekelezaji wa Bodi ya Tume ya Ukimwi, Kamati ilitaka kupatiwa kielelezo au idhini kutoka kwa Tume ya Utumishi Serikalini iliyoruhusu ulipwaji wa posho husika ili kujua uhalali wa kitendo kilichofanyika. Kwa bahati mbaya, Kamati haikuweza kupatiwa kielelezo hicho. Kiutaratibu, Tume ya Ukimwi baada ya maamuzi yaliyopitishwa katika kikao cha Bodi katika yalilazimika kupelekwa Tume ya Utumishi Serikalini ili kupata muongozo kwa ajili ya hatua za ulipwaji stahiki hizo. Kwa mnasaba huo, Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi na hoja hii inabakia.

**Ushauri, Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaushauri Uongozi wa Tume ya Ukimwi kufuata Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma hususan katika ulipwaji wa posho za likizo kwa Wafanyakazi wake.

### Hoja Nambari 7.2.4.4: Kushindwa kumchukulia hatua mfanyakazi aliyekwenda likizo bila ya malipo na kushindwa kuripoti kazini baada ya kumaliza likizo yake.

Kanuni nambari 64(1) ya kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014, inaeleza kuwa "Mtumishi wa Umma ambaye hajaripoti kazini baada ya likizo bila ya malipo kumalizika Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika:

a) Kumkumbusha mtumishi anayehusika kuripoti kazini.

b) Endapo mtumishi wa Umma atashindwa kuripoti kazini hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kupitia majalada ya watumishi wa Tume ya UKIMWI Pemba ukaguzi umebaini uwepo wa mfanyakazi ambaye amechukua likizo bila ya malipo kwa vipindi viwili (2) vya miaka miwili miwili kwa ajili ya kushiriki katika mradi wa kunusuru kaya masikini (TASAF) bila ya kurejea kazini, ambapo kwa mujibu wa barua ya ukumbusho yenye kumbukumbu namba OMKR/ZAC.P/T.U/OPF/M./94 likizo hiyo inamalizika tarehe 31/05/2021 na kutakiwa kuripoti kazini tarehe 01/06/2021

Hadi ukaguzi unakamilika mwezi wa Machi, 2023 mtumishi huyo hajaripoti kazi na pia Tume imeshindwa kumchukulia hatua yeyote stahili kwa mujibu wa sheria. Kutokuchukuwa kwa hatua yoyote kwa mujibu wa sheria za Utumishi wa Umma kunasabaisha uwepo wa udhaifu wa udhibiti wa ndani katika uongozi wa Tume.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya UKIMWI kufanya mawasiliano na Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora kuona namna bora ya kutatua changamoto hiyo ili kuepusha kujitokeza uwepo wa ukiukwaji wa taratibu za Utumishi kwa watumishi wa Umma.

#### Majibu ya Uongozi wa Tume

Tume ya UKIMWI Pemba ilichukua juhudi za kuhakikisha kwamba sheria za Utumishi wa Umma na Kanuni zake zinafuatwa kwa kumkumbusha Mtumishi huyo kuripoti kazini kwa barua yenye kumbukumbu Namba OMKR/ZAC.P/T.U/OPF/M./93 ya tarehe 18/05/2021 na barua ya ukumbusho yenye kumbukumbu namba OMKR/ZAC.P/T.U/OPF/M./94 ya tarehe 04/06/2021 zote kutoka kwa Mratibu wa Tume ya UKIMWI Pemba.

Kwa mujibu wa barua kutoka Ofisi ya Rais, Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora Zanzibar kwenda kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar yenye kumb CCB.196/234/02/116 ya 07 Mei, 2021 ikinukuu barua kutoka kwa Katibu Mkuu

Kiongozi, Mtumishi huyo aliruhusiwa kisheria kabla muda wake wa kumaliza likizo bila ya malipo kuendelea na kazi katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) (Nakala za barua husika zimeambatanishwa).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa taratibu zote zilifuatwa za kuruhusiwa Mtumishi huyo kuendelea na majukumu yake katika Taasisi nyengine kama taratibu za Utumishi zinavyoelekeza. Hali hiyo inathibitishwa na Kamati kupitia barua yenye kumbukumbu nambari CCB.196/234/ ya tarehe 07 Mei 2021.

Kilichijitokeza, ni kukosekana kwa ushirikiano wakati wa ukaguzi ambapo Mkaguzi hakupatiwa vielelezo vinavyohusiana na uhamisho wa Mtumishi huyo kwa madai kwamba uthibitisho vielelezo vilikuwa Makao Makuu Unguja na kupelekea kujitokeza kwa hoja hii katika ripoti ya Mkaguzi. Kwa mnasaba huo, Kamati imeamua kuiondoa hoja hii.

**Ushauri, Maoni na Mapendekezo ya kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inautaka Uongozi wa Tume ya Ukimwi kumpatia mashirikiano Mkaguzi hususan kwa kumpatia vielelezo anavyovihitaji wakati wa ukaguzi ili kuepusha kuwepo kwa hoja za Taasisi hii.
2. Kamati ya PAC inashauri kumbukumbu zote zinatakiwa kuwepo pande zote mbili Unguja na Pemba kwa ajili ya kuepusha hoja zisizo na msingi.

## Hoja Nambari 7.2.4.5: Malipo kwa Watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 5,098,207.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria nambari 11 ya ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kuwa “mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha ombi au haitoshiriki katika zabuni mpaka mtu, kampuni au taasisi hiyo imesajiliwa kama mtoa huduma”. Aidha, kifungu nambari 23 (2) kinafafanua kwamba maombi ya zabuni kutoka kwa mtu, kampuni, au taasisi ambayo haikusajiliwa hayatokubalika na hayatozingatiwa na taasisi ya zabuni.

Baada ya kupitia hati mbali mbali za malipo ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 5,098,207 zimelipwa na Tume ya UKIMWI Pemba kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma kama mtoa huduma.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1)(2) cha Sheria 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi umeshauri uongozi wa Tume ya UKIMWI Pemba kuhakikisha unafanya manunuzi kwa watoa huduma waliosajiliwa ili kuepusha kujitokeza kwa upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na ada ya usajili. Mchanganuo wa malipo yenyewe ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 49: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|
| 5/11ya 2/11/2021 | T.O | 350,000 | Fresh & Son take away | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji. |
| 10/12 ya 7/12/2021 | 023589 | 1,016,619 | Amour Suleiman Ali | Malipoyaununuzi wa samanizaofisi |
| 05/02 ya 1/2/2022 | | 375,000 | Tume ya UKIMWI | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji. |
| 11/03 ya 8/3/2022 | 025336 | 350,000 | Tume ya UKIMWI | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji. |
| 16/03 ya 10/3/2022 | 025339 | 259,308 | parts | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya vespa SMZ 152C. |
| 18/03 ya 10/3/2022 | 025341 | 672,280 | Slim Environmental Care | Malipo ya fedha kwa ajiliyausafi |
| 03/04 ya 9/3/2022 | 026057 | 300,000 | Tume ya UKIMWI | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma za mawasiliano. |
| 04/04 ya 6/4/2022 | 026058 | 1,775,000 | Bakar Petrol Station | Ununuzi wa mafuta ya petroli lita 406 na dizeli lita 310. |
| Jumla | | 5,098,207 | | |

**Majibu ya Uongozi wa Tume**

Ni kawaida Tume ya UKIMWI kufanya malipo kwa Watoa huduma ambao wamesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Dosari iliyojitokeza kwa watoa huduma Fresh & Son Take Away, Amour Suleiman Ali, Hasaan Motorcycle Spare Parts na Bakar Petrol Station ni kuisha kwa vibali vyao vya manunuzi wakati wa ukaguzi ambapo hapo awali walikuwa wamesajiliwa kwa usajili ambao hufanyika kila mwaka. Kwa sasa Tume ya UKIMWI imeachana na watoa huduma hao ambao hawajasajiliwa.

Kuhusu Slim Environmental Care Mtoa huduma huyu alilipwa bakaa la deni lake la huduma ya usafi ambalo alikua anaidai Ofisi tangu mwaka 2020.

Kuhusu Tume ya UKIMWI, Ofisi ilitenga fedha hizo kwa ajili ya viburudishaji, fedha ambazo zilikuwa zikitolewa kwa njia ya “cash” kwa matumizi ya viburudishaji na mawasiliano ya Ofisi ambapo stakabadhi za matumizi hayo zimeambatanishwa. Hata hivyo Tume ya UKIMWI itaufanyia kazi ushauri wa ukaguzi kuhakikisha manunuzi yote yanaendelea kufanyika kwa mujibu wa taratibu

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuifuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati imebaini kwamba manunuzi yaliyofanyika kupitia Watoa huduma yalikuwa ni matumizi madogo madogo ya ndani ambayo kiutaratibu hulipwa kwa kutumia “imprest’ ambayo hayapaswi kufanyika kwa kutumia Watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Ili kuthibitsha ukweli huo, Kamati iliomba kupatiwa vielelezo (vocha), kuvipitia na kuridhika navyo kwamba vilihusisha matumizi ya Ofisi yenye kiwango kidogo cha fedha. Miongoni mwa vielelezo hivyo ni vocha nambari 5/2 ya tarehe 1/2/2022, 11/3 ya tarehe 8/3/2022 na vocha nambari 3/4 ya tarehe 9/3/2022 na kuridhika navyo. Lakushangaza, Kamati ilitaka kujua kama Mkaguzi alipatiwa vielelezo hivyo na kuelezwa kwamba wakati wa ukaguzi havikuwepo wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, Kamati imeiondoa hoja hii kwa vile imeridhika navyo.

### Ushauri, Maoni na Mapendekezo ya kamati ya PAC

Kamati ya PAC inautaka Uongozi wa Tume ya Ukimwi kumpatia mashirikiano Mkaguzi hususan kwa kumpatia vielelezo anavyovihitaji wakati wa ukaguzi ili kuepusha kuwepo kwa hoja za Taasisi hii.

## Hoja Nambari 7.2.4.6: Dosari katika utoaji wa lilizo la mwaka kwa watumishi.

Kwa mujuibu wa Kanuni ya 58(1)(a) ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inaeleza kwamba “Mtumishi wa Umma atastahiki kupewa likizo la siku ishirini na nane za kazi ndani ya miezi kumi na mbili na atastahiki posho la likizo kila baada ya miaka mitatu au itakavyofafanuliwa katika matoleo kutoka Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma. Aidha kanuni ya 58(1)(c) inafafanua kwamba si ruhusa kwa mtumishi wa umma kuakhirisha likizo yake ya mwaka kwa madhumuni ya kulimbikiza siku zake za likizo ili achanganye na za mwaka mwengine, isipokuwa kwa dharura maalumu iliyokubalika.

Baada ya kupitia majalada ya baadhi ya watumishi (Personal Files) wa Tume ya UKIMWI dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwepo watumishi ambao wamepewa likizo la ziada ya siku ishirini na nane (28) za kazi bila kuwepo kielelezo chochote kinachoonesha uwepo wa dharura au haja ya mtumishi huyo iliyomzuia kwenda likizo. Hali hii inaweza kupelekea kupungua kwa ufanisi kwa watumishi kwa kutokwenda likizo lao la mwaka. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 58(1)(a)(c) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya UKIMWI Pemba kuhakikisha unatoa likizo kwa watumishi kwa mujibu wa miongozo ya Utumishi wa Umma ili kuepusha kujitokeza kwa malalamiko baina ya watumishi.

| Namba | Jina | No. ya Mshahara | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya kumaliza | Idadi ya siku |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Juma Sabour Khamis | 457931 | 30/08/2021 | 22/10/2021 | 38 |
| 02 | Muzna Mohd Kombo | 472810 | 21/02/2022 | 06/05/2022 | 56 |

**Majibu ya Uongozi wa Tume**

Tume ya UKIMWI Pemba imeendelea kusimamia haki za Watumishi wake ikiwemo

kuwapatia likizo kulingana na muongozo wa kifungu cha 58 - (1) (a) (b) na (c). Ni kweli kuwa Nd. Muzna Mohd Kombo alipatiwa siku 48 na sio 56 kama zilivyotajwa katika Ripoti ya Mdhibiti. Aidha siku hizo alipatiwa kufuatia Mtumishi huyo kuomba likizo na kuakhirishiwa na Ofisi kutokana na sababu za msingi. Barua ya kuakhirishwa kwa likizo imeambatanishwa.

Aidha Ndugu Juma Sabour Khamis alipatiwa siku 38 kwa sababu bado Mtumishi huyo alikua na haki ya msingi ya kupatiwa likizo yake hiyo kama kifungu cha 58 - (1) (c) kinavyoelekeza. Kwa sasa Ofisi inahakikisha kua kila Mtumishi anakwenda likizo yake ya mwaka kulingana na tarehe yake ya kwenda likizo (barua ya zuio imeambatanishwa).

Tume ya UKIMWI Pemba inakubaliana na hoja za mkaguzi kwa kuhakikisha kwamba inatoa likizo kwa watumishi kwa mujibu wa miongozo ya utumishi wa Umma ili kuepuka kujitokeza malalamiko baina ya watumishi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Tume ya Ukimwi Zanzibar wanakuwa wagumu kumpatia Mkaguzi vielelezo anavyovihitaji kuthibitisha Ukaguzi wake. Kamati imelisema hilo kwa vile vielelezo vinavyohitajika vilikuwepo na Kamati imepatiwa na kuvikubali. Miongoni mwa vielelezo vilivyotolewa ni uthibitisho wa Ndugu Muzna Moh'd Kombo upo kwa kupitia barua yenye kumbukumbu namba OMKR /ZAC/VOL./19 ambao alipatiwa siku 48 na sio 56 kama zilivyotajwa katika Ripoti ya Mdhibiti. Hivyo kulikuwa na utofauti wa siku alizopatiwa.

Aidha Ndugu Juma Sabour Khamis alipatiwa siku 38 kwa sababu ya uhaba wa Watumishi kwa wakati huo na kupaswa kubakia Afisini ili kutekeleza majukumu. Kwa majibu hayo, Kamati imeridhika na majibu ya Tume na kuiondoa hoja hiyo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo WA Kamati ya PAC**

Kamati inaushauri Uongozi wa Tume ya Ukimwi kuhakikisha unampatia vielelezo Mkaguzi ili hoja zisizo za msingi zisiingizwe katika Ripoti yake.

## Hoja Nambari 7.2.4.7: Malipo ambayo hayakukatwa kodi za zuio shilingi 13,672,000.

Kwa mulibu wa kifungu cha 83(1)(c)(ii) na 84(1) vya Sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa mwaka 2019) vinaeleza kuwa kodi ya zuio inapaswa kukatwa kwenye ada ya huduma, malipo ya manunuzi ya bidhaa na malipo ya mikataba na

kuwasilisha Mamlaka ya Mapato Tanzania ndani ya siku saba baada ya mwisho wa mwezi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Tume ya UKIMWI Pemba imefanya malipo ya shilingi 13,672,000 kwa watoa huduma mbali mbali kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa au upokeaji wa huduma bila ya kuwakata kodi ya zuwio na kuwasilisha Mamlaka ya mapato Tanzania kinyume na Sheria ya Kodi ya mapato.

Kukata kodi ya zuwio kunapunguza gharama za ukusanyaji wa kodi, kusaidia uzingatiaji wa Sheria za kodi, kupunguza ukwepaji wa kodi na pia kunasaidia Serikali kukusanya kodi mapema kitu amnbacho hakikufanyika.

Kushindwa kukata kodi ya zuio kutoka kwa watoa huduma kunaweza kuisababishia Tume hasara zisizo za lazima zinazotokana na malipo ya adhabu pia ni kuikosesha Serikali mapato.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya UKIMWI Pemba kuhakikisha kwamba matumizi yote ya fedha za Umma yanafanywa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ikiwemo kukata kodi ya zuio katika bidhaa au huduma zinazonunuliwa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 51: Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi kilicholipwa | Aliyelipwa | maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 02/09 ya 29/9/2021 | 000257 | 690,000 | Muus tea and refreshments | Malipo ya ukumbu na viburudishaji |
| 02/011 ya 10/11/2021 | 000261 | 3,200,000 | Samail College of Science and Technology | |
| 07/12ya 22/12/2022 | 000277 | 530,000 | | |
| 05/011 ya 15/11/2021 | 000268 | 1,600,000 | | |
| 02/01 ya7/1/2022 | 000279 | 1,524,000 | | |
| 04/01 ya 20/1/2022 | 000281 | 1,628,00 | | |
| 04/06 ya 10/6/2022 | 000295 | 4,500,000 | | |
| **Jumla** | | **13,672,000** | | |

**Majibu ya Uongozi wa Tume**

Tume ya UKIMWI imekua na utaratibu wa kukata kodi za zuio kwa matumizi ya fedha za kawaida kama inavyoonekana katika kumbukumbu za matumizi mengine ya ofisi ambayo si fedha za wahisani. Kiwango cha fedha ambacho kimetajwa ni fedha za Wahisani wa Maendeleo ambao kwa miongozo yao hazitakiwi kukatwa kodi. Hata hivyo tunakubaliana na hoja za ushauri za ukaguzi na Tume ya UKIMWI itaendelea kufuatilia ili kupata muongozo sahihi juu ya jambo hili.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika hoja hii kamati ya PAC inakubaliana na majibu ya Tume ya Ukimwi ambapo kiwango cha fedha kilichoelezwa ni fedha za Wahisani wa Maendeleo ambao kwa mujibu ya miongozo iliopo Miradi hiyo haitakiwi kukatwa kodi. Kwa msingi huo, Kamati imeiondosha hoja hii.

**Ushauri, Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inashauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa makini katika uandikaji wa hoja inazoziibua zizingatie miongozo ya Serikali.

# 7.4 WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO

## 7.4.4 AFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

### Taarifa ya Mapato

Afisi ya Mtakwim Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 12,777,262,922 kutoka katika vyanzo vyake vya kodi na visivyokuwa vya kodi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 jumla ya shilingi 7,070,085,853.23 zimekusanywa sawa na asilimia 53.3 ya makadirio.

**Majibu ya Uongozi wa Afisi**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ilipangiwa kukusanya shilingi 185 milioni kupitia vyanzo vyake vya mapato, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, Ofisi imekusanya jumla ya Shilingi 82.483 milioni sawa na asilimia 44.5 ya makadirio Jadweli Nam. 4 linaonesha makadirio ya fedha zilizopangwa kukusanya na fedha zilizokusanywa.

**Jadweli Nam. 4: Fedha Zizlizopangwa Kukusanywa na Zilizopatikana**

| Na. | Vyanzo vya Mapato | Fedha zilizopangwa | Fedha zilizokusanywa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Vibali | 60,000,000.00 | 28,523,388.00 | 47.5 |
| 2 | Ukodishaji wa Kumbi za Mkutano | 90,000,000.00 | 53,960,000.00 | 60.0 |
| 3 | Kutoa Ushauri Elekezi juu ya Masuala ya Tafiti | 35,000,000.00 | - | 0 |
| | **Jumla** | **185,000,000.00** | **82,483,388.00** | **44.5** |

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022, mapato ya Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali yalishuka kutokana na athari za UVIKO 19 ambapo kwa kiasi kikubwa viliteteresha vyanzo vyao vya ukusanyaji mapato. Hili limetokana na kwamba Afisi hiyo inategemea zaidi mapato yatokanayo na vibali vya tafiti zinazofanywa na Wanafunzi, Taasisi za Serikali pamoja na watu binafsi ndani na nje ya nchi.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ihakikishe inabuni vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato yao ili waondokane na kuwa na vyanzo vichache ambapo ikitokea changamoto yoyote mapato ya Afisi huwa hayapatikani.

## Taarifa ya Matumizi

Katika mwaka wa Fedha 2021/2022 Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliidhinishwa kutumia jumla ya shilingi 12,777,262,922 kwa matumizi ya kawaida na kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 jumla ya shilingi 7,070,085,353.23 zimeingizwa na kutumika sawa na asilimia 55.3 ya makadirio.

### Majibu ya Uongozi wa Afisi

Kupitia Bajeti ya Kazi za Kawaida ya 2021/2022, Ofisi ilikadiriwa kutumia shilingi 3,630 milioni kati ya fedha hizo, shilingi 1,689 milioni sawa na asilimia 46.5 kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 1,941 milioni sawa na asilimia 43.5 kwa ajili ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, shilingi 1,267 milioni zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 34.9 ya makadirio ya fedha.

Kati ya fedha hizo, shilingi 1,107 milioni sawa na asilimia 65.5 kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 160 milioni sawa na asilimia 8.2 kwa ajili

ya matumizi mengineyo (OC) Jadweli Nam. 1 na 2 linaonesha mchanganuo wa fedha zilizopangwa na zilizopatikana.

**Jadweli Nam. 1: Fedha Zilizopangwa na Zilizopatikana 2021/2022**

| Na. | Huduma | Fedha zilizopangwa | Fedha zilizopatikana | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mshahara (PE) | 1,689,200,000.00 | 1,107,784,987.00 | 65.5 |
| 2 | Matumizi Mengineyo (OC) | 1,941,000,000.00 | 160,000,000.00 | 8.2 |
| | **Jumla** | **3,630,200,000.00** | **1,267,784,987.00** | **34.9** |

**Jadweli Nam. 2: Fedha Zilizopangwa na Zilizopatikana kiidara 2021/2022**

| Na. | Idara | Fedha zilizopangwa | Fedha zilizopatikana | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H1: Uratibu wa Takwimu za Kiuchumi | 275,531,000.00 | 18,300,000.00 | 6.6 |
| 2 | H2: Uratibu wa Takwimu za Kijamii | 402,735,000.00 | 20,770,000.00 | 5.2 |
| 3 | H3: Kusimamia Viwango na Mifumo ya Kitakwimu | 71,885,000.00 | 25,725,000.00 | 35.7 |
| 4 | H4: kutoa Huduma za Utawala na Uendeshaji pamoja na Matumizi ya Vitengo Maalim | 2,728,049,000.00 | 1,185,324,987.00 | 43.4 |
| 5 | H5: Uratibu wa Shughuli za Kitakwimu Pemba | 152,000,000.00 | 17,665,000.00 | 11.6 |
| | Jumla | **3,630,200,000.00** | **1,267,784,987.00** | **34.9** |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati kufuatilia hoja hii, Kamati imebaini mambo yafuatayo:

1. Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliingiziwa fedha kidogo ukilinganisha na majukumu wanayojipangia kutekeleza. Afisi hiyo ilijipangia shilingi bilioni **3,630,200,000 na kupata shilingi bilioni 1,267,784,987.00 sawa na asilimia 34.9;**
2. Kamati baada ya kuangalia taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka (Financial Statement) iligundua kuwa Afisi hiyo imeingiziwa kiasi kidogo cha mishahara sawa na asilimia 6.5. Katika kulifuatilia kwa undani suala hilo, imegundua kwamba hadi mwezi wa Julai, 2022, mishahara yao ilikuwa ikilipwa kupitia Tume ya

Mipango Zanzibar kwa vile Afisi hiyo ilikuwa haina 'Vote'; na

3. Kutopatikana kwa fedha za matumizi mengineyo kumeipelekea Afisi kushindwa kulipa fedha za umeme kwa wakati na kusababisha kuwepo kwa madeni, kutofanyiwa gari 'service kwa wakati, kutofanyika kwa tafiti za viwanda na sekta isiyo rasmi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhakikisha inawapatia fedha za matumizi Afisi hii kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Baraza ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

## Hoja nambari 7.4.4.1: Kutokuwasilishwa kwa mapato katika Mfuko Mkuu wa Hazina Shilingi 22,197,940

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 tuliweza kupitia nyaraka na taarifa mbali mbali za uhasibu na kubaini Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imefanya makusanyo kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato yenye jumla ya shilingi 104,411,328. Aidha, kwa mujibu wa taarifa zilizoandaliwa na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali zilionesha kupitia taarifa ya mapato na matumizi uwepo wa shilingi 82,213,388 zilizowasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 22,197,940 ambapo hadi ukaguzi unakamlika hakukuwa na majibu sahihi ya kutokuwasilishwa fedha hiyo kwa mujibu wa utaratibu, hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa uthibitisho wa matumizi ya fedha hizo kwa jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa mapato hayo kutokana na kukosekana kwa kibali cha idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusu matumizi yakufanyika kwa matumizi hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhakikisha mapato yote yanawasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mujibu wa utaratibu na pindipo patakapojitokeza haja ya kutumia mapato ni vyema kupata idhini ya Mlipaii Mkuu wa Serikali.

**Majibu ya Uongozi wa Afisi**

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ilikisiwa kukusanya mapato kupitia vyanzo vyake na kuyawasilisha mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Vyanzo vya mapato ni vibali vya kufanya utafiti (Research Permit), Ukodishaji wa kumbi za Mikutano na Mauzo ya vitabu na ripoti za utafiti. Wananchi au taasisi zinazopatiwa huduma hizo hupatiwa

namba maalum (Control Number) na kufaya malipo kwa njia ya benki au Wakala wa fedha na baadae kupatiwa risiti. Mapato yanayokusanywa kupitia vyanzo hivi huingia moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila ifikapo mwisho wa mwezi. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 shilingi 82,213,388 zilikusanya na kuingia Mfuko Mkuu wa Serikali.

Tofauti iliyojitokeza baina ya mapato yaliyowasilisha Mfuko Mkuu na yaliyokusanywa ni kuwa Ofisi ya Mtakwimu hupokea fedha kutoka Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji Mali za Serikali (ZPPDA) kama ni mchango wa taasisi hiyo kwa matumizi ya huduma ya umeme kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano uliofungwa baina ya OCGS na ZPPDA tarehe 2 Julai 2018. Kwa mwaka 2021/2022 Jumla ya shilingi 12,000,000/- zilipokelewa na kutumika kwa malipo ya umeme.

Aidha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar iliipatia Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Serikali shilingi 8,497,940 kwa ajili ya kazi ya Utafiti wa Uhakiki wa Viashiria vya Elimu kupitia Mradi wa Kukuza Elimu ya Sekondari Zanzibar (Zanzibar Improving Student's Perspective (ZISP)). Utafiti huo ulifanyika na ripoti imewasilishwa Wizara ya Elimu.

Vile vile, Ofisi ilipokea shilingi 1,700,000 ikiwa ni malipo ya uuzaji wa zabuni ya ununuzi wa Komputa, jumla ya Wazabuni kumi na saba walishiriki kwa kila mzabuni alilipa shilingi 100,000. Malipo yote hayo yalipokelewa kwa tarehe tofauti kama inavyofafanuliwa katika Kiambatisho Namba 1.

Fedha zote hizo, zinajumuisha na kufikia shilingi 22,197,940, Fedha hizo hazikuwa sehemu ya makusanyo ya mapato kama ilivyoelezwa na Mkaguzi, ila zilikuwa ni malipo kwa shughuli maalum.

#### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza kazi zake katika Afisi hiyo kweli kasoro hiyo ilikuwepo lakini Afisi imechukua hatua ya kurekebisha. Kwasasa malipo yote ya zabuni yanafanyika kupitia Mfumo wa Ununuzi na kuingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Hivyo, changamoto hiyo imeondoka na kupelekea Kamati kuiondosha hoja hii.

### Hoja nambari 7.4.4.2: Kutokufuatwa kwa taratibu za Utumishi wa Umma

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ukaguzi umepitia taarifa mbali mbali za watumishi ikiwemo majadala binafsi, taarifa za likizo, Pamoja na stahiki za watumishi kwa mujibu wa utaratibu wa utumishi.

Kutokana na mapitio hayo ukaguzi umebaini uwepo wa watumishi watano (5) waliowahi

kufanya kazi kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano (5) ambao walitumikia kipindi chao kwa utumishi wa muda kwa mujibu wa mikataba ya utumishi wao. Kwa mujibu wa kanuni ya 135 ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 imeeleza kwamba "Hakutokuwa na utumishi wa kutwa katika Utumishi wa Umma, kama kuna ulazima Katibu Mkuu wa Mkuu wa Taasisi atalazimika kuomba kibali kwa Tume ya Utumishi husika na kumjazisha mkataba, Utumishi wa mtumishi wa kutwa hautozidi miezi sita na atalipwa pale ambapo anamaliza kazi yake kwa siku na mtumishi wa kutwa hatakuwa na fursa ya kupata likizo na wala hana haki ya kudai kiinua mongo na Mafao ya Uzeeni".

Kutokana na vifungu vilivyonakiliwa hapo juu ukaguzi umebaini Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ilitengeneza viinua mgongo vya watumishi hao vyenye thamani ya shilingi 40,767,000 ambapo kwa kila mtumishi atastahiki kulipwa shilingi 8,153,400 hata hivyo, kwa mujibu wa makubaliano yao watumishi hao watawalipa jumla ya shilingi 25,000,000 ambapo kwa kila mtumishi mmoja atalipwa shilingi 5,000,000. Hadi ukaguzi unakamilika Afisi ya Mtakwim Muu wa Serikali imefanya malipo ya shilingi 15,000,000 ambapo kila mtumishi huyo amelipwa shilingi 3,000,000, malipo hayo yamelipwa kinyume na utaratibu kwa mujibu wa vifungu nilivyovinakili hapo juu na kupelekea kujitokeza kwa matumizi mabaya ya fedha za Serikali na kusababisha mgongano wa kutoelewana baina ya Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na watumishi wa kutwa ambao bado wanafika afisini kudai stahiki iliyobakia ya shilingi 10,000,000 ambapo ni sawa na shilingi 2,000,000 kwa kila mtumishi.

Kufanya matumizi bila ya kuzingatia taratibu za fedha ni kwenda kinyume na utaratibu wa utumishi wa umma hasa ukizingatia kwa mujibu wa kanuni hawakustahiki kulipwa mafao ya uzeeni kutokana na aina ya utumishi wao.

Mchanganuo wa malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 67: Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu wa kiutumishi**

| Malipo ya watumishi wa Mkataba | | | | Kiasi kilicholipwa (Tshs) | | | Bakaa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nam. | Jina | Stahiki | Makubaliano | 2020/21 | 2021/22 | Jumla (Tshs) | |
| | | | | Year 1 | Year 2 | | |
| 1. | Juma Ame Juma | 8,153,400 | 5,000,000 | 2,000,000 | 1,000,000 | 3,000,000 | 2,000,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Nassor Juma | 8,153,400 | 5,000,000 | 2,000,000 | 1,000,000 | 3,000,000 | 2,000,000 |
| 3. | Mohamed Nassor | 8,153,400 | 5,000,000 | 2,000,000 | 1,000,000 | 3,000,000 | 2,000,000 |
| 4. | Ame Nassor | 8,153,400 | 5,000,000 | 2,000,000 | 1,000,000 | 3,000,000 | 2,000,000 |
| 5. | Zainab Ali Khamis | 8,153,400 | 5,000,000 | 2,000,000 | 1,000,000 | 3,000,000 | 2,000,000 |
| **Jumla** | | **40,767,000** | **25,000,000** | **10,000,000** | **5,000,000** | **15,000,000** | **10,000,000** |

### Majibu ya Uongozi wa Afisi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliwaajiri Watumishi watano kwa njia ya Mikataba ya muda ambayo ilifungwa kwa vipindi vya miezi mitatu mitatu hadi sita kuanzia mwaka 2010. Hata hivyo, uajiri wao ulidumu kwa kipindi chote hicho hadi pale Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi na Utawala Bora mnamo tarehe 24 Mei 2021 ilipotoa toleo la Serikali lenye Kumbukumbu Namba CAB.40/158/01/20 ambalo lilielezea juu ya Utaratibu wa ajira kwa Wafanyakazi wa Kujitolea na Ajira za Mikataba.

Baada ya toleo hilo kutoka Serikalini mnamo tarehe 23 Agosti 2021 Menejimenti ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali walikaa, pamoja na mambo mengine walijadiliana juu ya suala la watumishi wa mkataba na kuamua kusitisha mikataba yao. Hata hivyo, kwa kuwa mikataba yao haikueleza namna ya malipo baada ya kumaliza muda wao wa utumishi wao (terminal benefit).

Kwa kuzingatia kuwa watumishi hao walikuwa tayari ni wastaafu, na kwa kuwa waliitumikia Ofisi kwa uadilifu na kulinda mali za Ofisi, Menejimenti kupitia kikao chake hicho walikubaliana kuwasaidia kiasi cha fedha kwa kila mmoja ili iwe kama ni kifutia jasho chao kwa utumishi wao.

Hata hivyo, Ofisi tayari imeshazuia malipo hayo, na kwa wakati huu Ofisi inapokea huduma za ulinzi kutoka kwa Wakala wa Ulinzi wa JKU kama agizo la serikali lilivyoagiza.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Afisi

hii, ni kweli kulikuwepo kasoro hiyo ya kutokufuatwa kwa taratibu za Utumishi wa Umma hususan kwa kufanya malipo kinyume na utaratibu wa uliowekwa na Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014. Hata hivyo, kasoro hizo zimeshafanyiwa kazi kwa kutoendelea kulipa fedha hizo na kutokuwa na wafanyakazi hao. Hivyo, Kamati imeridhika na utekelezaji wa hoja hii na kuiondosha.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uongozi wa Afisi ya Mtamwimu Mkuu wa Serikali uhakikishe unatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sheria Pamoja na Kanuni ya Utumishi ya Mwsks 2014

## Hoja nambari 7.4.4.3: Kuwepo kwa vyombo vya moto ambavyo havijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 umebaini Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inamiliki gari mbili (2) zenye nambari za usaiili SMZ 472A na DFP 7940 ambazo hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu na zipo katika hali ya uchakavu.

Kutokufanyiwa matengenezo kwa vyombo hivyo kwa muda mrefu kunaweza kupekea kuendelea kuchakaa na hatimae kutokuweza kutengenezeka kutokana na kuongezeka kwa gharama za matengenezo kwa mujibu wa hali ya chakavu ulivyo.

Ukaguzi unaushauri ongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhakikisha unatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kufanya matengenezo kwa vyombo vilivyochakaa ili kuweza kupatikana tija iliyokusudiwa.

Aidha, itakapobainika vyombo hivyo havitengenezeki au vitagharimu fedha nyingi za matengenezo ni vyema kuomba kibali kutoka Afisi ya Msajili wa Hazina kuweza kuviondoa kwa kuviuza ili kunusuru kukosekana kwa mapato Serikalini kutokana na kuendelea kuchakaa.

**Majibu ya Uongozi wa Afisi**

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inamiliki gari yenye namba ya usajili SMZ 472 A na DFP 7940. Wakati wa kipindi cha Ukaguzi gari hizi zilikuwa mbovu kwa muda mrefu jambo ambalo Ofisi imeona haja kuliwasilisha pendekezo ya kuuzwa kwa gari SMZ 472 A. Pendekezo hilo liliwasilishwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa barua yenye kumbukumbu namba OCGS/BA/ADM/VOL.11/164 ya tarehe 26 Juni 2023. Ofisi imepokea barua yenye kumbukumbu namba BA.26/454/01/37/70 ya tarehe 14 Oktoba 2023 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango inayotaarifu kuwa gari hiyo imeshauzwa

kwa ndugu Elvis Goodluck Maleko na amekamilisha malipo yote, na kuelekeza kuwa Ofisi imkabidhi gari hiyo Ndugu Maleko kwa matumizi yake binafsi.

Ofisi kupitia barua yenye kumbukumbu namba AB.86/133/03/169 ya tarehe 18 Oktoba 2023 iliikabidhi gari hiyo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (Msajili wa Hazina) kwa hatua za kumkabidhi ndugu Maleko.

Aidha, gari yenye namba ya usajili DFP 7940 imefanyiwa matengenezo na ipo ofisini na inaendelea na matumizi ya Ofisi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa hoja hii kwa vile Afisi tayari imeshachukua jitihada za kuifanyia matengenezo gari moja ambayo inaendelea kutumika kwa shughuli za kiofisi wakati nyengine imeshauzwa kwa mujibu wa taratibu za Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma. Kwa msingi huo, Kamati imeiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 7.4.4.4: Kuwepo kwa malimbikizo ya deni la Mishahara shilingi 60,943,129

Kwa mujibu wa taarifa za hesabu za mwaka wa fedha 2021/2022 zimebainisha uwepo wa deni la shilingi 60,943,129 linalotokana na malimbikizo ya mishahara yatokanayo na watumishi ishirini (20) waliorudi masomoni kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 2018 na kuchelewa kubadilishiwa mishahara yao hadi ukaguzi unakamilika.

Kutokana na mazungumzo yaliyofanyika baina ya wakaguzi na wahusika yamebainisha kwamba deni hilo liliwahi kuombewa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora kufanyiwa malipo, hadi ukaguzi unakamilika ombi hilo bado halijafanyia kazi.

Kuwepo kwa deni la malimbikizo ya mishahara linalodaiwa na watumishi wa umma kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa kazi linaweza kupelekea kupunguza ari na hamasa ya watumishi kujituma zaidi na hatimae manung'uniko na migogoro kazini haitokwisha.

Ukaguzi unaushauri ongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhakikisha unaliandikia na kuliwasilisha deni hilo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuomba ridhaa ya kuweza kuhakikiwa uhalali wa uwepo wake na kuwasilishwa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, tumishi na Utawala Bora kwa ajili ya hatua za utekelezaji. Mchanganuo wa watumishi wanaodai stahiki zao kwa muda mrefu ni kama walivyobainishwa katika jadweli liliopo hapo chini:-

**Jadweli Nambari 68: Watumishi wanaodai stahiki zao kwa muda mrefu**

| Nam. | Jina la Mtumishi | Kiasi cha fedha kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Halima Adam Mohammed | 89,100 |
| 2. | Faida Saleh Juma | 79,199 |
| 3. | Mohammed Said Gharib | 111,600 |
| 4. | Abdulwahid Habib Ali | 3,693,400 |
| 5. | Mhina Khamis Suleiman | 129,600 |
| 6. | Abdi Issa Makame | 206,280 |
| 7. | Hamisa Suleiman Faki | 9,282,200 |
| 8. | Abdallah Othman Makame | 3,444,800 |
| 9. | Aziza Jecha Ameir | 12,150 |
| 10. | Juma Omar Ali | 10,597,400 |
| 11. | Fadhil Ali Hassan | 10,813,000 |
| 12. | Ahmada Hamza Mohammed | 3,123,600 |
| 13. | Suleiman Said Omar | 5,321,200 |
| 14. | Hidaya Ali Khamis | 5,664,400 |
| 15. | Rashid Mjaka Mkuu | 1,394,400 |
| 16. | Othman Ali Khamis | 1,229,400 |
| 17. | Salma Saleh Ali | 1,394,400 |
| 18. | Khalid Chum Haji | 613,400 |
| 19. | Mahmoud Juma Rajab | 1,915,800 |
| 20. | Rahma Said Hassan | 1,827,800 |
| **Jumla** | | **60,943,129** |

**Majibu ya Uongozi wa Afisi**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliwasilisha barua yake Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora yenye kumbukumbu GS/PC/02/VOL.1/94 ya tarehe 21 Juni, 2018 ikielezea juu ya Wafanyakazi wake kulipwa tofauti za mishahara baada ya kurudi masomoni. Kufuatia barua hiyo, Ofisi ya Utumishi iliiandikia barua Wizara ya Fedha na Mipango yenye kumbukumbu Namba CB.174/196/05/74 ya tarehe 5 Julai 2018. kwa ajili ya kulipwa tofauti kwa watumishi wa

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali waliorudi masomoni kupitia fedha za matumizi ya Ofisi (OC) pamoja na mkato wa Asilimia 5% ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), Asilimia 10% ya muajiri na kukatwa kodi ya Mapato (Income Tax).

Kutokana na mda mrefu kupita, Ofisi iliiandikia barua Ofisi ya Rais Fedha na Mipango yenye kumbukumbu namba OCGS/BA/ADM/411/V.III/128 ya tarehe 6 Juni 2023 kwa ajili ya Kukumbushia na kuiomba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kulipa malimbikizo hayo.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Kupitia barua yenye kumbukumbu namba AC.161/399/01/04/98 ya tarehe 27 Septemba 2023 imeelekeza kuwa Utaratibu wa Maombi ya Fedha za Mishahara huwasilishwa Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma, na kushauri kuwa Ofisi iwasilishe maombi hayo katika Afisi ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya uhakiki.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ilitekeleza ushauri husika na kupitia barua ya yenye kumbukumbu namba AB.04/151/01/63 ya tarehe 2 Oktoba 2023 iliwasilisha kwa hatua za kiutumishi. Hadi kufikia leo tarehe 31 Januari 2024 malipo hayo bado hayajafanyika. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu itaendelea kuyafatilia malipo haya.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kufuatia juhudi zilizochukuliwa na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali za kuiandikia barua ya maombi ya ulipwaji malimbikizo hayo Wizara inayohusiana na Utumishi wa Umma ambayo nayo iliyafanyikazi ya kuyawasilisha Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Lakushangaza, badala ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kufanya malipo ya malimbikizo hayo hatimae imemjibu Mtakwimu Mkuu kwamba iandike barua nyengine iende Wizara ya Utumishi wa Umma baada ya Afisi ya Mtakwimu kukumbushia ulipwaji wa wake jambo ambalo Kamati inaona kama ni kukosesha na kuchelewesha upatikanaji wa haki wa Watumishi.

Katika kutafuta utatuzi wa suala hilo, Kamati ililazimika kufanya kikao maalum kilichowakutanisha Kamati, Watendaji wa Afisi ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Afisi ya Mtakwimu siku ya terehe 16 Febuari, 2024 na kubaini kukubaliana mambo yafuatayo:

a) Deni halisi ambalo Watumishi hao wanadai ni shilingi 53,710,880 badala ya 60,943,129. Hili limetokana na kiwango ambacho Mkaguzi amekiainisha kimejumuisha na kodi ndani yake (ZSSF);

b) Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iiandikie barua Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma ili iweze kuyafanyia kazi maombi yao;

c) Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma nayo iifanyie kazi barua hiyo na kuwasilisha maombi yao Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa hatua za malipo; na

d) Kamati ifanye kikao chengine siku ya tarehe 28 Febuari, 2024 muda wa saa 5:00 za asubuhi hapa Baraza la Wawakilishi kitakachowashirikisha Aifisi ya Mtakwimu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Afisi Kuu ya Utumishi pamoja na Afisi ya Mkaguzi kujadili hatua za utekelezaji wake.

Kwa msingi huo, kama malimbikizo hayo ya Watumishi hayajalipwa, hoja hii itaendelea kujitokeza. Hivyo Kamati inaibakisha hoja hii kwa hatua za utekelezaji na Mkaguzi katika mwaka ujao afuatilie hatua ya utekelezaji wake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, kupitia Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, wakishirikiana na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuhakikisha malimbikizo hayo ya madeni yanalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ili malalamiko ya Watumishi yaondoke.

## Hoja nambari 7.4.4.5: Dosari zilizobainika katika matumizi ya fedha shilingi 471,893,112

Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar impoke kiasi cha shilingi 2,726,676,500 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kutoka Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania kama ni mchango wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za sensa kama vile uhamasishaji.

Aidha, Shirika la UNFPA lilichangia jumla ya shilingi 156,436,553 kwa ajili ya kutekeleza shughuli ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu (Demarcation) katika utekelezaji wa sensa ya watu na makaazi.

Katika utekelezaji wa shughuli ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu ukaguzi umebaini Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imetumia jumla ya shilingi 471,893,112. Katika matumizi ya fedha hizo. dosari zifuatazo zimebainika:-

**(a) Kutumia fedha kinyume na malengo yaliyokusudiwa shilingi 110,604,411**

Ukaguzi umebaini Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imefanya matumizi ya shilingi 110,604,411 zinazotokana na mchango URT na kutumika katika shughuli ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu jambo ambalo lilishapangiwa matumizi ya fedha kwa fadhili wa mchango wa UNFPA.

Kufanya matumizi kinyume na malengo yaliyokusudiwa kunaweza kusababisha kukosekana kwa misaada itolewayo na Washirika wa Maendeleo kwa kutokupatikana kwa taarifa sahihi na halisi pindipo zitakapohitajika kwa lengo la kupima ufanisi wa matumizi kwa fedha walizozitoa.

Ukaguzi unaushauri ongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhakikisha unatekeleza malengo iliyojipangia kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa inayohusu matumizi ya fedha zilizopatikana kutoka kwa washirika mbali mbali wa maendeleo ili kupima ufanisi wa kila chanzo cha mapato kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 69: Fedha zilizotumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa**

| Hati Nam. | Hundi Nam. | Alielipwa | Kiasi (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 3/8 ya 18/8 | T.T | Climate Consult LTD | 16,016,788 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kifaa cha internet. |
| 5/8 ya 18/8/21 | T.T | TRA | 326,874 | Malipo kwa ajili ya kodi ya zuio |
| 4/8 ya 18/8/21 | T.T | ZRB | 2,451,549 | |
| 7/10 ya 13/10/21 | 002046 | STATCAP | 11,930,000 | Malipo kwa ajili ya zoezi la utengaji wa maeneo. |
| 12/10 ya 27/10/21 | 002052 | STATCAP | 10,430,000 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vipooza hewa. |
| 18/10 ya 29/10/21 | T.T | OCGS PROJECT PBA | 18,540,000 | |
| 15/10 ya 29/10/21 | T.T | OCGS PROJECT PBA | 21,640,000 | |
| 20/10 ya 4/11/21 | 002054 | STATCAP | 2,240,000 | Malipo kwa ajili ya Posho. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13/4 ya 4/4/22 | 002158 | Colorful Travel Agent | 320,000 | Malipo kwa ajili ya safari kikazi. |
| 14/4 ya 3/4/22 | 002159 | Swisan Enteprises | 156,000 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 15/4 ya 4/4/22 | T.T | TRA | 3,200 | Malipo kwa ajili ya kodi ya zuio |
| 64/5 ya 6/5/22 | 002176 | STATCAP | 10,380,000 | Malipo kwa ajili ya mafunzo. |
| 82/5 ya 20/5/22 | 002182 | STATCAP | 9,800,000 | Malipo kwa ajili ya zoezi la kuhesabia watu. |
| 90/5 ya 23/5/22 | 002184 | Map Oil | 6,370,000 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta. |
| **Jumla** | | | **110,604,411** | |

### (b) Kukosekana kwa hati za malipo shilingi 361,288,701

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 361,288,701 zimetumika kwa ajili ya masuala mbali mbali ya Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali lakini hati za malipo hayo hazikuweza kupatikana ili kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.

Kukosekana kwa hati za malipo kunaweza kupelekea kutokuthibitika kwa malipo yaliyofanyika kupitia hati hizo jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 166(2)(f) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unaushauri ongozi wa Afisi ya Mtakwim Mkuu wa Serikali kuhakikisha malipo yote ya fedha yanayofanyika yanaambatanishwa na nyaraka za matumizi pamoja na kuhifadhiwa vizuri na hati za malipo kwa lengo la kuziwasilisha wakati wa ukaguzi ili kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 70: Hati za Malipo zilizokosekana kwa ukaguzi**

| Hati Nam. | Hundi Nam. | Alielipwa | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 13/8/21 | 001976 | STATCAP | 27,810,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13/8/21 | 001976 | STATCAP | 200,000 |
| 27/8/21 | 001987 | STATSCAP | 22,270,000 |
| 6/9/21 | 001996 | MAP OIL | 5,394,000 |
| 6/9/21 | 002001 | STATCAP | 1,200,000 |
| 9/9/21 | 002003 | STATCAP | 31,270,000 |
| 22/9/21 | 002018 | STATCAP | 25,450,000 |
| 22/9/21 | 002018 | STATCAP | 240,000 |
| 24/9/21 | T.T | OCGS Project A/C Pemba | 32,440,000 |
| 24/9/21 | 002022 | STATCAP | 11,360,000 |
| 27/9/21 | 002024 | ZANCOS TOURS | 3,600,000 |
| 4/10/21 | 002028 | STATCAP | 1,672,000 |
| 4/10/21 | 002029 | STATCAP | 4,680,000 |
| 5/10/21 | 002030 | STATCAP | 1,540,000 |
| 8/10/21 | 002040 | STATCAP | 1,080,000 |
| 12/10/21 | 002043 | STATCAP | 7,280,000 |
| 5/11/21 | 002057 | Map Oil | 4,500,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11/11/21 | T.T | ZANCOS | 240,000 |
| 11/11/21 | T.T | ZANCOS | 240,000 |
| 1/12/21 | 002075 | STATCAP | 26,170,000 |
| 8/12/21 | 002086 | Map Oil | 4,968,000 |
| 22/12/21 | 002099 | STATCAP | 1,240,000 |
| 30/12/21 | 002101 | Khamiar Enterprises | 911,400 |
| 30/12/21 | T.T | TRA | 18,600 |
| 7/1/22 | 002105 | Map Oil | 3,750,000 |
| 14/1/22 | 002107 | Statcap | 58,680,000 |
| 14/1/22 | 002107 | Statcap | 25,770,000 |
| 24/2/22 | 002129 | Statcap | 41,600,000 |
| 2/3/22 | 002136 | Adem Store | 505,974 |
| 2/3/22 | T.T | TRA | 10,326 |
| 3/3/22 | 002137 | Statcap | 15,000,000 |
| 31/5/22 | T.T | Bankcharges | 198,401 |
| **Jumla** | | | **361,288,701** |

Majibu ya Uongozi wa Afisi

a. Majibu ya hoja kutumia fedha kinyume na malengo yaliokusudiwa TZS 110,604,411

Ofisi ya Mtakwimu imetumia fedha zinazotoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na UNFPA kwa ajili ya kutekeleza shughuli ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu. Bajeti ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia kwa Zanzibar ilikuwa shilingi 860,000,000 ambapo kati ya Fedha hizo, UNFPA ilichasngia shilingi 156,436,553 sawa na asilimia 18 tu ya jumla ya mahitaji ya bajeti ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia, Asilimia 82 sawa na shilingi 703,563,447 ni fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kazi hiyo ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia ambapo isingeliweza kufanyika bila ya kutumia fedha kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b. Kukosekana kwa hati za malipo TZS 361,288,701

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (National Bureau of Statistics (NBS)). Kutokana na ukaribu huo hujitokeza baadhi ya wakati kuwepo kwa Tafiti ambazo hufanyika Tanzania Bara na Zanzibar kwa wakati mmoja na vile vile mfadhili wa tafiti hizo huwa mmoja.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia June 2022, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu ilipokea fedha kutoka UNFPA kupitia NBS kwa kazi ya Utengaji wa maeneo ya kuhesabia (Demarcation) na Sensa ya majaribio (Pilot Census) kazi ambayo ilifanyika Tanzania nzima. Mheshimiwa Mwenyekiti, Kukosekana kwa hati za malipo ya shilingi 361,288,701 ni kuwa, hati za malipo ziliwasilishwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi wa pamoja baina ya NBS na OCGS.

Hati hizo za malipo zilifanyiwa ukaguzi na Kampuni ya Arnest and Young Global Limited na Taarifa ya Ukaguzi ilitolewa na kuwasilishwa Ofisi ya Taifa na Takwimu na OCGS kupatiwa nakala ya taarifa hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

a) Kamati imegundua kuwa hakukuwa na fedha ambayo Afisi imeitumia kinyume na malengo yaliyokusudiwa kwa vile bajeti nzima ya ununuzi wa vifaa vya utafiti ni shilingi milioni 860 kwa ajili ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia. Kilichojitokeza, kulikuwa na fedha za Wahisani wa Maendeleo na nyengine zimetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

b) Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa hoja hii kwa vile kuna uzembe ulifanyika kwa baadhi ya Watendaji wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali hususan kwa kuruhusu mafaili (vielelezo) kuchukuliwa na Wakaguzi kutoka Tanzania Bara badala ya kufuata maadili ya uhifadhi wa nyaraka za Serikali ambapo Mkaguzi alitakiwa kuzifuata nyaraka sehemu zilipo na kuchukua nakala ikiwezekana.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhakikisha nyaraka zote zinazohitajika kwa ajili ya ukaguzi zinabaki ndani ya taasisi, isipokua kuwepo ombi maalum kwa maandishi kutoka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, au taasisi nyengine zenye mamlaka kisheria.

## Hoja nambari 7.4.4.6: Kukosekana utaratibu wa manunuzi wa kutumia ushindani wa bei shilingi 32,191,100

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Afisi ya Mtakwimu imefanya ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya ofisi kwa mujibu wa hati za malipo zenye jumla ya shilingi 32,191,100.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taratibu za ushindani wa bei jambo ambalo linaweza kusababisha kufanyika kwa manunuzi yenye thamani kubwa ukilinganisha na uhalisia wa bei ya dukani kutoka kwa washindani mbali mbali. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 5(2)(c) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2020.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhakikisha unatekeleza malengo iliyojipangia ikiwemo kufanya manunuzi kwa kuzingatia shindani wa bei kwa lengo la kupata bidhaa kwa bei nafuu na zenye ubora. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 71: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kuzingatia ushindani wa bei**

| Nam. | Hati ya Malipo | Alielipwa | Kiasi cha Fedha (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 13/9/2021 | Swisan Enterprises | 2,028,600 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 2. | 24/9/2021 | Shukuru Food and Beverage | 30,162,500 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji. |
| **Jumla** | | | **32,191,100** | |

### Majibu ya Uongozi wa Afisi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu ilinunua wino kwa ajili ya kuchapisha na kutoa nakala za madodoso yaliyotumika katika mafunzo kwa Wasimamizi pamoja na Makarani kutoka katika Kampuni ya Swisan Enterprises Limited baada ya kushindanishwa na Wazabuni wengine ambao ni Mamelodi Enterprises (shilingi 2,955,500) na Ocean Tech Computer Services (shilingi 2,714000). Swisan Enterprises Ltd. (shilingi 2,380,500). Swisan alipewa kazi hiyo baada ya kuonekana bei yake ipo chini ikilinganishwa na Wazabuni wengine.

Wakati wa Sensa ya majaribio Ofisi ilifanya mafunzo 19 Agosti, 2021 hadi 1 Septemba, 2021 kwa Wakufunzi, Makarani, Maafisa TEHAMA, Wanahabari pamoja na Washiriki wengine, ambao walitarajiwa kushiriki kwenye Sensa ya 23 Agosti, 2022. Pamoja na mahitaji mengine mafunzo hayo yalihitaji upatikanaji wa chakula na vinywaji hivyo Kampuni ya Shukuru Food and Beverage ilichaguliwa baada ya kushindanishwa Kampuni tatu zenye bei tofauti ambazo ni Zainiki Food and Beverage (shilingi 38,100,000) Zan Catering and Take Away (shilingi 35,560,000) na Shukuru Food and Beverage (shilingi 31,750,000). Kampuni ya Shukuru Food and Beverage ilishinda kwa kuwa na bei ya chini na kupewa Mkataba wa Kutoa huduma.

Hivyo, Ofisi ilifuata utaratibu wa ushidani, kwa kuandaa kampuni tatu zenye vigezo na kuchagua kampuni moja ya kutoa huduma husika.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kutafuta ukweli wa suala hili, Kamati ya PAC imegundua kwamba changamoto iliyojitokeza haikusababishwa na Afisi ya Mtakwimu isipokuwa ni utaratibu wa zabuni ambao unaelekeza kuzawadiwa zabuni Kampuni iliyokuwa na sifa bora ukilinganisha na wengine ambapo kigezo kimoja cha kutambua sifa hizo ni kulinganisha bei za Wazabuni husika. Kwa mnasaba huo, Afisi imetekeleza wajibu wake wa kumchagua Mzabuni mwenye bei ya chini (lowest bidder) na kumpatia kazi. Kamati imepitia vielelezo vyote ikiwemo na Mkataba wa Mzabuni na kuridhika navyo.

Kwa msingi huo, baada ya kupitia nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati, imeridhika na majibu yaliyowasilishwa na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na kuiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 7.4.4.7: Hati za malipo zilizokosekana kwa ajili ya ukaguzi shilingi 657,826,312

Ukaguzi umebaini Afisi ya Mtakwimu Mkuu imefanya malipo kwa kipindi cha mwezi wa Julai, Agosti na Septemba, 2021 ambapo jumla ya shilingi 480,417,012 zilitumika, kati ya

fedha hizo shilingi 440,417,012 ilikuwa ni Mishahara na shilingi 40,000,000 ikiwa ni matumizi mengineyo.

Aidha, ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 217,409,300 ziliidhinishwa kulipwa ZSSF ikiwa ni mikato kwa wafanyakazi kwa kipindi cha mwezi wa Februari, Machi na Aprili kwa mwaka wa fedha 2021/2022, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa hati za malipo hayo jambo ambalo ukaguzi haukuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.

Kukosekana kwa hati za malipo kunaweza kupelekea kutokuthibitika kwa malipo yaliyofanyika kupitia hati hizo jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 166(2)(f) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unaushauri ongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhakikisha malipo yote ya fedha yanayofanyika yanaambatanishwa na nyaraka za matumizi pamoja na kuhifadhiwa vizuri na hati za malipo kwa lengo la kuziwasilisha wakati wa ukaguzi ili kuthibitisha halali wa malipo yaliyofanyika.

**Majibu ya Uongozi wa Afisi**

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kukosekana kwa hati za malipo wakati wa ukaguzi. Hati hizo zinahusiana na mishahara ya miezi mitatu na baadhi ya malipo ya matumizi ya kawaida (OC). Kukosekana kwa hati hizo kunatokana na mafaili yenye hati hizo kwa bahati mbaya kusafirishwa pamoja na mafaili mengine ya fedha za miradi ya UNFPA ambayo yalirejeshwa Ofisi ya Taifa na Takwimu (NBS).

Uongozi umefuatilia mafaili hayo bila ya mafanikio. Hata hivyo, nakala za hati za malipo ya mishahara ya miezi mitatu zimeweza kupatikana na zipo tayari kwa ukaguzi.

Kuhusiana hoja ya fedha za Matumizi ya Mengineyo (OC) kati ya shilingi 40,000,000 zilizopokelewa kwa miezi mitatu ya Julai, Agosti na Septemba 2021, shilingi 6,000,000 zilipelekwa Pemba kwa matumizi ya Ofisi ya Mtakwimu Pemba ambapo matumizi ya fedha hizo pamoja na kumbukumbu za matumizi zinapatikana Pemba. Matumizi yaliobakia ya TZS 34,000,000 kwa bahati mbaya yalichanganyika na matumizi ya fedha za UNFPA zilizopelekwa Dodoma kama taarifa ya awali ilivyoelezwa.

Kuhusu malipo ya ZSSF ya TZS 217,409,300 ambazo zilikosekana kwa ukaguzi kuanzia mwezi wa Februari, hadi Juni 2022. Maelezo ya hoja hii ni kuwa kuanzia mwezi Februari, hadi Juni 2022 malipo ya mishahara pamoja na mikato yote ya mishahara yalilipwa na Tume ya Mipango. Kwa wakati huo Ofisi ya Mtakwimu Mkuu ilikuwa ikipata ruzuku kupitia Tume ya Mipango. Hivyo basi malipo ya mikato ya ZSSF kwa mwezi wa Februari,

hadi Juni 2022 yalilipwa na Tume ya Mipango.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kulikosekana mashirikiano ya karibu kati ya Mkaguzi na Mkaguliwa hususan katika upatikanaji wa vielelezo. Hili linajitokeza kutokana na Kamati kupatiwa baadhi ya nyaraka zilizokuwepo lakini Mkaguzi hakupatiwa. Kwa msingi huo, hoja hii na kiwango cha fedha kilichoainishwa kutumika bila ya kuwepo vielelezo isingejitokeza katika hali hii. Hata hivyo, Kamati ilihitaji kupatiwa vielelezo vya Pemba na kujibiwa kwamba Pemba wanafanyiwa nao ukaguzi lakini Kamati ilisisitiza kwamba ni busara nakala hizo zingekuwepo mbele ya Kamati ili kuweka sawa majibu kama ilivyoibuliwa na Mkaguzi.

Kwa upande wa nyaraka (files) ambazo zimepelekwa Tanzania Bara kwa ajili ya ukaguzi, Kamati imegundua kuwa uchukuaji wake ulifanyika kinyume na taratibu kwani hakukuwa na kielelezo chochote kinachothibitisha Afisi kutakiwa kupeleka nyaraka hizo. Aidha, utoaji wa nyaraka sehemu moja kwenda sehemu nyengine ni hatari kwa vile nyaraka za Serikali huwa na utaratibu wake wa kuzihamisha au kuchukuliwa.

kwa mnsaba huo, Kamati inaitaka Afisi ya Mtakwimu kufanya ufuatiliaji wa zilizochukuliwa Tanzania Bara hasa ukizingatia hizo ni nyaraka za Serikali ambazo zinahitajika kuhifadhiwa na Serikali. Hivyo, hoja hii inabakia ili Mkaguzi afuatilie utekelezaji wake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi wahakikishe wanafuatilia upatikanaji au urejeshwaji wa nyaraka za Afisi hiyo ziliopo Tanzania Bara.
2. Uongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali uweke utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ili zitakapohitajika ziweze kupatikana kwa urahisi.

## Hoja nambari 7.4.4.8: Matumizi ya fedha kwa njia ya fedha taslimu bila ya kufuata taratibu shilingi 18,223,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 18,223,000 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya Afisi ya Mtakwim Mkuu wa Serikali. Dosari zilizobainika na ukaguzi ni kufanya matumizi hayo kwa fedha taslim pasipo kufuata taratibu za sheria zinavyoelekeza.

Kufanya matumizi kwa njia ya fedha taslim ni kwenda kinyume na kanuni ya 58(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unaushauri ongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhakikisha matumizi yote ya fedha yanatumika kwa mujibu wa utaratibu na miongozo ya fedha iliyotolewa ili kuepusha kujitokeza kwa malipo hewa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

**Jadweli Nambari 72: Malipo ya fedha taslimu bila kufuata taratibu**

| Nam. | Hati Nam. | Alielipwa | Kiasi cha malipo (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 11/6/2022 | Business Census Account | 1,000,000 | Malipo kwa ajili ya posho mbali mbali. |
| 2. | 26/6/2022 | | 1,893,000 | |
| 3. | 27/6/2022 | | 180,000 | |
| 4. | 12/5/2022 | | 300,000 | |
| 5. | 2/6/2022 | | 4,770,000 | |
| 6. | 3/6/2022 | | 1,100,000 | |
| 7. | 4/6/2022 | | 1,400,000 | |
| 8. | 5/6/2022 | | 1,050,000 | |
| 9. | 6/6/2022 | | 210,000 | |
| 10. | 7/6/2022 | | 1,590,000 | |
| 11. | 8/6/2022 | | 2,650,000 | |
| 12. | 9/6/2022 | | 880,000 | |
| 13. | 10/6/2022 | | 1,200,000 | Malipo ya fedha za wastaafu |
| **Jumla** | | | **18,223,000** | |

### Majibu ya Uongozi wa Afisi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwa kuwepo kwa malipo yaliolipwa kwa fedha taslim. Aidha, tunakubalina na ushauri wa mkaguzi kuhakikisha malipo na matumizi yote ya fedha yanafanyika kwa mujibu wa utaratibu na miongozo ya fedha iliyotolewa ili kuepusha kujitokeza kwa malipo hewa.

Kwa sasa Ofisi inalipa malipo yote kwa njia ya Benki kama utaratibu wa na miongozo ya fedha inavyoelekeza. Hata hivyo, utekelezaji wa muongozo unatoa changamoto kwa wadau wa takwimu (mfano. masheha, watoa taarifa na wananchi wa kawaida).

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa hoja, imebaini kuwa ni kweli awali malipo hayo yalikuwa yakifanyika kwa njia ya kawaida lakini kwasasa Afisi imesharekebisha kasoro hiyo kwa vile watafiti hivi sasa wanalipwa kupitia hesabu (account) ya benki. Kamati

imeridhika na hatua zilizochukuliwa na Afisi na kuiondoa hoja hii.

## Hoja nambari 7.4.4.9: Kukosekana kwa mkataba wa nyongeza

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imebainika Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar ilisaini hati ya makubaliano ya mwaka mmoja kuanzia tarehe 1/10/2013 hadi 30/9/2014 na Benki Kuu ya Tanzania.

Katika makubaliano ya kazi za utafiti wa kupanda na kushuka kwa bei za vyakula ambapo kila robo mwaka jumla ya shilingi 8,000,000 zitalipwa ikiwa ni sawa na shilingi 32 milioni kwa mwaka. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa mkataba wa nyongeza au kufanya mapitio ya mkataba mpya baada ya mkataba wa awali kumalizika kwa muda wake.

Kuendelea kufanya kazi ya utafiti bila ya kuwepo kwa makubaliano mapya ya mkataba kunaweza kupelekea kujitokeza kwa mgogoro wa kimaslahi pale pande moja itakaposhindwa kutekeleza matakwa ya makubaliano ya awali.

Ukaguzi unaushauri ongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuchukuwa jitihada za makusudi kufanya mapitio na maboresho ya mkataba wa awali ili kuweza kutekeleza jukumu hilo kwa mujibu wa makubaliano mapya.

### Majibu ya Uongozi wa Afisi

Ni kweli Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imesaini hati ya makubaliano (MoU) na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kuanzia 1 Oktoba 2013 hadi 30 Septemba 2014 makubaliano ya mwaka mmoja kwa kazi ya kugharamia ukusanyaji na uchambuzi wa data za faharisi ya bei (Consumer Price Index (CPI)) ambapo kila robo mwaka BOT huingiza TZS 8,000,000 na kwa mwaka TZS 32,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na uandishi wa ripoti.

Pamoja na kuwa makubaliano hayo ni ya mwaka mmoja Ofisi ya Mtakwinu na Benki Kuu ya Tanzania wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu katika utekelezaji wa utafiti huo jambo ambalo limepelekea kudumu kwa makubalianao hayo kwa muda mrefu.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imegundua kuwa Mkataba ulikuwepo wakati Mkaguzi anakagua isipokuwa ulikuwa wa zamani. Hata hivyo, Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeshaanda Mkataba mpya na kuuwasilisha Afisi katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupatiwa ushauri wa kisheria na hatimae pande mbili hizo zitiliane saini kwa hatua ya

utekelezaji. Kwa mnasaba huo, hoja hii imeondolewa na Kamati.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ufuatilie ukamilishaji wa Mkataba huo ili hatua ya utekelezaji zianze.

## Hoja nambari 7.4.4.10: Malimbikizo ya deni la umeme shilingi 67,980,235.44

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa deni la shilingi 67,980,235.44 linalotokana na kupatiwa kwa huduma ya umeme inayotumika katika utekelezaji wa kazi za Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokulipwa kwa deni hilo kwa muda mrefu jambo ambalo linaweza kukwamisha juhudi za Shirika la Umeme kujiendesha kiufanisi.

Aidha ni kwenda kinyume r kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri ongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhakikisha unatenga bajeti ya kutosha kuweza kulipa deni hilo ili kunusuru kuongezeka kwa deni hilo na hatimae kushindwa kulilipa jambo ambalo linaweza kupelekea kukosekana kwa huduma ya umeme na kushindwa kutekeleza majukumu ya Afisi kwa mujibu wa utaratibu.

### Majibu ya Uongozi wa Afisi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, inakubaliana na hoja ya mkaguzi kuwa, wakati wa ukaguzi kulikuwepo kwa deni la umeme la shilingi 67,980,235.44. Malimbikizo ya deni hilo yanatokana na uchache wa fedha zilizokuwa zikipatipana kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC), Aidha, kutokutekelezwa kikamilifu kwa makubaliano ya kuchangia gharama za umeme kwa Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji Mali wa Serikali (ZPPDA) kumepelekea kuongezeka kwa deni hilo na kufikia kiasi hicho.

Hata hivyo, Ofisi imeweza kulilipa deni hilo na hadi kufikia tarehe 18 Disemba 2023 Ofisi imeshalipa deni lote la umeme la shilingi 67,980,235.44 na kwa sasa Ofisi inadaiwa matumizi ya deni la mwezi wa Disemba 2023 kiasi cha TZS 7,065,103.46 na deni hilo litalipwa mara tu baada ya kuingizwa kwa fedha za matumizi mengineyo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Mkaguzi kubaini kasoro za kutolipwa kwa deni la umeme na kufikia shilingi 7,065,103.46. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa asilimia 95 ya deni hilo limeshalipwa na kubakia deni la mwezi mmoja tu wa Disemba. Kwa mazingira hayo, Kamati imeridhika na utekelezaji wa hoja hiyo na kuamua kuiondoa.

### Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali uhakikishe unaandaa mpango mzuri utakaohakikia madeni ya umeme yanalipwa kwa wakati ili kuepusha kurundikana kwa madeni hayo na kupelekea ugumu katika kuyalipa.

## HITIMISHO

Kamati ya PAC kama Kamati inayosimamia masuala ya kifedha, hufanya kazi zake za uchunguzi kwa kupitia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuchunguza hoja mbali mbali zilizojitokeza katika Ripoti hizo pamoja na kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu Hesabu za Mawizara na Taasisi za Serikali kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2020.

Katika kutekeleza hayo, Kamati ya PAC ilieleza mambo ambayo imeyabaini kupitia majibu ya Watendaji na kutoa Mapendekezo kwa Wahusika kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Taasisi za Umma. Kwa mnasaba huo, Kamati hii inaliomba Baraza la Wawakilishi, kuipitia, kuijadili na hatimaye kuiridhia Ripoti hii kwa lengo la kufanyiwa kazi na Serikali.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya PAC inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Mawizara na Taasisi zake kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati hii.

Kwa umuhimu wa pekee, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza pamoja na Watendaji wote wa Afisi ya Baraza kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha katika muda wote ambao Kamati hii ilipokuwa ikiwajibika.

****Mwisho****